

MWONGOZO WA UMISHENARI WA TIBA

UMEKUSANYWA KUTOKA KWENYE MAANDISHI YA ELLEN G. WHITE

KITABU CHA KIADA NA MWONGOZO WA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA ULIOELEZEWA KATIKA ROHO YA UNABII.

HUDUMA YA ENENDENI KOTE MTANDAONI, JERSEY 2025, AUGUST.

TWAMSHUKURU BABA WA MBINGUNI KWA MWONGOZO HUU AMBAO NI MSAADA WA KUTIBU MAGONJWA MENGI KWA KUSHIRIKIANA NA MSHAURI WAKO WA AFYA

MKUSANYAJI WA NUKUU ZIHUSUZO KAZI YA UMISHENARI WA TIBA: Vance Ferrell-Harvest Time Books.

Altamont, Tennessee, United State of America.

Watafsiri, Waombezi, Wahariri, Washauri, Wataalamu wa

Teknolojia, na watia moyo wote

1. Grace Momadi-Masaka, Jersey, Marekani

2. Nhandi Emmanuel Masunga- Bariadi, Tanzania

3. **Isack Msusu-Kigoma, Tanzania**

4. **Watson Mwaibasa-Mbeya, Tanzania**

Kitabu Mwenzi wa hiki ni The Broken Blue Print (Mchoro au ramani iliyovunjika)

MAANA YA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA

Mlango wa Kuingia katika Makazi ya Watu— Kazi ya umishenari wa tiba ni kazi ya utangulizi kwa injili (piooner work), mlango ambao kupitia huo Ukweli kwa ajili ya wakati huu unapata mlango wa kuingia katika makazi mengi ya watu. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa wamishenari wa dhati/kweli wa tiba, kwani wanapaswa kujifunza kuyahudumia mahitaji ya roho na ya mwili. Ukarimu halisi kabisa unapaswa kuoneshwa na watendakazi wetu kwani, kwa maarifa na uzoefu unaopatikana kwa kazi ya vitendo, wanatoka kwenda kutoa tiba rahisi kwa

wagonjwa. Pale wanapokwenda nyumba kwa nyumba watapata njia ya kufikia mioyo mingi. Wengi watafikiwa ambao vinginevyo kamwe hawangesikia ujumbe wa injili. - The Review and Herald, Desemba 17, 1914. {WM 125.1}

Jambo kuu juu ya kazi ya umishenari wa tiba ni kuwaandaa watu kwa SIKU YA HUKUMU! Ni daraja au ngazi ya kuwasaidia watu Ili wapatikane TAYARI, ile SIKU YA HUKUMU! Soma Ufunuo 14:6-12. Injili ya milele, ikisema mche na MUNGU na kumtukuza maana saa ya hukumu imefika, Kuwa na ibada ya Kweli, na Binadamu wasipokuwa na ibada ya Kweli wanapewa onyo, na baadaye hukumu (adhabu au thawabu) Kazi ya Umishenari wa Tiba rahisi ni mlango, na daraja ambalo kuna jiwe la kuvukia mto, mlango wa kufikia nyumba nyingi katika miji. —

Umishenari wa kumsaidia mtu katika mahitaji yake ambayo yanamsibu, mahitaji ya kiroho, kijamii, kiuchumi, au kimwili, mfano anahitaji ushauri, anahitaji kusafishiwa mazingira yake, ana kidonda, anaumwa homa, mke wake amemkimbia, anahitaji ada, hana chakula, anahitaji mume au mke, anahitaji kusaidiwa masomo yake au kazi za nyumbani, anahitaji kukata nywele zake n.k (Soma zaidi Counsel on Health, 556).

Mkono wa kulia unatumika kufungua mlango ili mwili uweze kupata mpenyo au nafasi ya kupita. Hii ndio sehemu ya kazi ya umishonari wa matibabu/tiba MWT (Mmishenari wa Tiba) sio kazi ya kusomea masomo ya mitishamba (herbology) au Kanuni Nane za Afya, au unesi au udaktari au tiba rahisi tu, ILA ni Kuandaa watu kwa ajili ya hukumu ya MWISHO wa DUNIA hii kumlaki BWANA mawinguni wakiwa washindi na kuishi na MUNGU wetu MILELE NA MILELE NENO mmishenari wa tiba lilianza kutumiwa mnamo 1893 kwa neno “Upendo usiojifikiria au usio na uchoyo ukivutia kwake (disinterested BENEVOLENCE kwa Kingereza. KINDNESS (WEMA usio na Ubinafsi) NOT JUST I LOVE YOU, but ACTION.) UPENDO KWA VITENDO), Si kusema nakupenda tu, na vitendo hamna, bali kusiwepo kujisaidia na kujifikiria mwenyewe tu!

Watendakazi wa tiba na Injili "wamefungwa pamoja na uhusiano usioweza kufunjika au kuyeyuka"

KAZI YA UMISHENARI WA MATIBABU

Kazi ya umishenari wa tiba ni kazi ya mstari wa mbele kwa injili, Mlango wa awali wa kuingia kwenye nyumba na mioyo ya watu kwa wakati huu ikitumiwa itatuingiza kwenye nyumba nyingi. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa wamishenari wa kweli wa tiba; kwani wanapaswa kujifunza kuhudumia mahitaji ya roho na mwili. Upendo na kujali watu kusiko na ubinafsi kabisa kunapaswa

kuonyeshwa na watendakazi wetu. Kwa hayo maarifa na uzoefu uliopatikana kwa kazi ya vitendo, wanaenda kutoa matibabu kwa wagonjwa. Wanapoenda nyumba kwa nyumba watapata ufikiaji wa mioyo mingi. Wengi watafikiwa ambao isingekuwa hivyo kamwe wasingesikia ujumbe wa injili ya milele na kupata kuwepo mbinguni. Maonyesho ya kanuni za matengenezo ya afya hufanya mengi kuelekea kuondoa ubaguzi dhidi ya kazi yetu ya injili. Daktari Mkuu ni MUNGU Mwenyewe, Mwanzilishi wa kazi ya Umishenari wa Tiba, atawabariki wote ambao kwa hivyo wanatafuta kutoa Ukweli kwa wakati huu.

Uponyaji wa mwili umefungwa na utume wa injili. Wakati Kristo alipowatuma wanafunzi Wake katika safari yao ya kwanza ya umishenari, aliwaambia, "Mnapoenda, hubirini, mkisema, Ufalme wa mbinguni umekaribia. Ponyeni wagonjwa, toeni ukoma, toeni wafu, toeni pepo kwa hiari. Mmepokea, toeni bure. “Mt. 10: 7, 8. Na wakati wa mwisho wa huduma Yake ya kidunia aliwapa agizo lao, Akisema, "Ishara hizi zitafuata wale waaminio; Kwa Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; na wakinywa kitu cha mauti, hakitawaumiza; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Marko 16:17, 18.

MFANO WA KRISTO

Njia ya Kristo ya kuwasilisha Ukweli haiwezi kuboreshwa. Mwokozi aliwapa wanafunzi masomo ya vitendo, aliwafundisha jinsi ya kufanya kazi kwa njia ambayo itafurahisha roho kuingia katika Ukweli. Aliwahurumia waliochoka, wenye kulemewa, walioonewa. Aliwalisha wenye njaa na akawaponya wagonjwa. Daima Alizunguka-zunguka akitenda mema. Kwa mema aliyotimiza, kwa Maneno Yake ya upendo na matendo mema, Alifasiri na kufafanua injili kwa wanadamu. Kwa kifupi kama ilivyokuwa kipindi cha huduma Yake ya umma, katika hija Yake

ya miaka 33 1/2 hapa duniani Alitimiza kazi aliyokuja kuifanya. Kweli alizofundisha zilivutia sana! Jinsi kazi Yake ilivyokuwa, na jinsi maisha aliyoishi yalivyokuwa makamilifu! Ni chakula cha kiroho cha ajabu kiasi gani, alichotoa kila siku alipowasilisha mkate wa uzima kwa maelfu ya roho zenye njaa! Maisha Yake yalikuwa huduma hai ya Neno. Hakuahidi chochote ambacho hakufanya. Maneno ya maisha yaliwasilishwa kwa usahili kiasi kwamba mtoto angeweza kuyaelewa. Wanaume, wanawake, na watoto walivutiwa sana na njia Yake ya kuelezea Maandiko hivi kwamba wangeweza kuisikia sauti Yake, wakaweka Maneno yao sawa na Yake, na kuiga ishara Zake. Vijana waliambukizwa na roho Yake ya huduma, na wakatafuta kuiga njia Zake za neema kwa kutafuta kuwasaidia wale ambao waliona wanahitaji msaada.

Kama vile tunavyofuatilia njia ya kijito cha maji kwa kuangalia kijani kibichi kando yake, ndivyo Kristo angeweza kuonekana katika matendo ya rehema yaliyoashiria njia Yake kila hatua. Popote alipokwenda, afya iliboreshwa (afya na uzima ulikuwa hapo), na furaha ilifuata popote alipopita. Vipofu na viziwi walifurahi mbele Zake. Maneno Yake kwa wajinga yaliwafungulia chemchemi ya uzima. Alitoa baraka Zake kwa wingi na kwa mfululizo/mpigo. Alikuwa na hazina za umilele zilizokusanywa, na zilizotolewa kwa watu, yaani zawadi ya Bwana kwa mtu. Kazi ya Kristo kwa niaba ya mwanadamu haijakamilika. Inaendelea hata hivi leo. Vivyo hivyo mabalozi Wake wanapaswa kuhubiri injili na kufunua upendo Wake wa huruma kwa roho zilizopotea na zinazoangamia. Kwa shauku isiyo na ubinafsi kwa wale wanaohitaji msaada, Wamishenari wa Tiba wanapaswa kutoa onyesho la Ukweli wa injili. Kazi hii inahitaji zaidi ya mahubiri. Uinjilishaji wa ulimwengu ni kazi ambayo Mungu amewapa wote wanaokwenda kwa Jina Lake.

YALIYOMO

UTANGULIZI 9

SEHEMU YA 1 18

ASILI, KUSUDI, NA WAKATI UJAO 18

SURA YA 1 18

KWA NINI UMISHENARI WA TIBA NA UJUMBE WA AFYA ULITOLEWA KWA KANISA LA MASALIA? 18

SURA YA 2 31

UJUMBE WA ISAYA 58 KWA KANISA LA MASALIA 31

SURA YA 3 45

WAKATI UJAO WA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA 45

SEHEMU YA 2 58

MWONGOZO WA UINJILISTI 58

SURA YA 4 58

WALE WALIOITWA KUFANYA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA 58

SURA YA 5 71

SEHEMU NA JINSI WAMISHENARI WA TIBA WANAPASWA KUPOKEA MAFUNZO YAO. 71

SURA YA 6 87

JINSI VIKUNDI VIDOGO VYA WAMISHENARI WA TIBA VINAVYOPASWA KUFANYA 87

SURA YA 7 99

JINSI TAASISI ZA UMISHENARI WA TIBA ZINAVYOPASWA KUFANYA KAZI 99

SEHEMU YA 3 117

KANUNI NA VIWANGO 117

SURA YA 8 118

KANUNI ZA KAZI ZINAZOPASWA KUZINGATIWA 118

SURA YA 9 123

KANUNI ELEKEZI KATIKA UANZISHWAJI NA UENDESHAJI WA TAASISI ZA UMISHENARI WA TIBA 123
SURA YA 10 166
VIWANGO VYA KUFANYA KAZI AMBAVYO VINAPASWA KUZINGATIWA 166
SEHEMU YA 4 183
HUDUMA YA UPONYAJI 183
SURA YA 11 183
JINSI YESU ALIVYOENDELEA NA KAZI YAKE YA UMISHENARI WA TIBA 183
SURA YA 12 186
JINSI HUDUMA ILIYOWEKWA WAKFU INAVYOPASWA KUJIHUSISHA NA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA 186
SURA YA 13 197
MAENEO YA KAZI NA MAELEKEZO AMBAYO MMISHENARI WA TIBA ANAPASWA KUSHIRIKI 197
SURA YA 14 210
HATUA KUMI ZINAZOPASWA KUFUATWA KATIKA UREJESHAJI WA AFYA 210
SEHEMU YA 5 222
TIBA RAHISI 222
SURA YA 15 222
KWA NINI MUNGU AMEWAELEKEZA WATU WAKE KUTUMIA TIBA RAHISI BADALA YA KUTEGEMEA MAOMBI PEKEE KWA AJILI YA UPONYAJI? 222
SURA YA 16 230
KANUNI MAALUM AMBAZO KWAZO TUNAWEZA KUJUA NI TIBA ZIPI NDIYO "DAWA ZA FAMASIA " NA ZIPI ZIMEIDHINISHWA NA MUNGU. 230
SURA YA 17 256
JINSI MAJI YANAVYOWEZA KUSAIDIA KATIKA KUPONYA WAGONJWA 256

SURA YA 18 266
JINSI MITISHAMBA INAVYOWEZA KUSAIDIA KATIKA KUPONYA WAGONJWA 266
SEHEMU YA 6 278
KANUNI ZA AFYA 278
SURA YA 19 278
JE, TUNAPASWA KUHATARISHA KANUNI ZETU ZA AFYA ILI KUWASAIDIA WALE WALIO KARIBU NASI? 278
SURA YA 20 292
MAONI JUU YA MAFUA 292
SEHEMU YA 7 294
MUUNDO WA BIBLIA 294
SURA YA 21 294
UJUMBE WA AFYA KAMA UNAVYOPATIKANA KATIKA BIBLIA 294
SURA YA 22 302
KAZI YA UMISHENARI WA TIBA KAMA INAVYOPATIKANA KATIKA BIBLIA 302
SURA YA 23 318
VISA VYA UMISHENARI WA AFYA NA TIBA KATIKA BIBLIA 318
SURA YA 24 321
MAANDISHI YA UMISHENARI WA AFYA NA TIBA YALIYOPANGWA KULINGANA NA KITABU 321
SURA YA 25 336
UPONYAJI WA KIMUNGU KAMA UNAVYOPATIKANA KATIKA BIBLIA 336
NUKUU MUHIMU 342
BONASI YA JUMBE KUTOKA LOMA LINDA 353
UFUNDISHAJI NA UPONYAJI 365

UTANGULIZI

Katika majira ya joto ya mwaka 1960, Vance Ferrel alianza kufanya kazi ya kubuni njia na mbinu za kuendesha kazi ya umishenari ya afya na Umishenari wa tiba katika jiji kubwa la Pwani ya Magharibi—kazi ambayo ingetimiza mpango uliotolewa kwa watu wa Mungu katika Biblia na Roho ya Unabii. Kabla ya mwaka kwisha, alitambua kwamba uelewa ulio wazi zaidi ulihitajika wa kile kinachojumuisha "mpango au blueprint au mchoro" kuhusiana na kazi ya Umishenari wa Tiba. Kutojua upeo na uharaka wa kazi hiyo kulikuwa kukimzuia kufanya kazi hiyo ipasavyo, na jambo hili lilikuwa likiwazuia waumini wengine wa Marejeo ya Yesu kuanza kazi kama hiyo mahali pengine.

Ni nini kinachojumuishwa katika kazi ya Umishenari ya Tiba? Nani anapaswa kufanya hiyo kazi? Je, Umishenari wa tiba unapaswa kuendelezwa vipi? Ni taasisi gani zinapaswa kuendeshwa ndani ya miji? Ni zipi zinapaswa kuwa vijini pekee? Je, kazi kama hiyo ina umuhimu gani? Je, ni wataalamu au wanataaluma pekee ndiyo wanaohusika katika hilo? Je, ni tiba gani zinafaa kutumika? Ni tiba gani ambazo zitakuwa marufuku kutumiwa (mfano Hyonotism, magnetism, mesmerism, tafakari ya ubongo ukiwa tupu, waganga wa kienyeji, uchawi, Reiki, yoga nk)? Haya yote ni maswali yanayohitaji majibu.

Hii ilisababisha utafiti katika Biblia na Roho ya Unabii. Kukusanya, kupanga, na kuandika nukuu kuliendelea kwa mwaka mzima.

Huko nyuma katika siku hizo, Fahirisi ya Juzuula Tatu ilikuwa bado haijachapishwa. Hakukuwa konkodansi ya diski-laza kusaidia kupata vifungu. Bado-CD za Machapisho ya Roho ya Unabii zilikuwa mbali sana katika siku zijazo. Kwa hiyo, ili kufanya mkusanyo kuwa kamili kadiri iwezekanavyo, mkusanyaji alisoma kwa makini kila kitabu cha afya cha Roho ya Unabii na kuandika kila kitu ambacho kingeeleza uharaka, upeo, na mbinu ya kazi ya Umishenari wa Tiba mbao Mungu alikuwa ameamuru watu Wake wafanye katika siku hizi za mwisho. Utafiti huo ulijumuisha yote yaliyochapishwa na vitabu vya RYU, Roho ya unabii, pamoja na idadi ya machapisho ambayo hayakuchapishwa kwa muda mrefu, kama vile Loma Linda Messages.

Mradi huo ulipokamilika, mkusanyaji alisoma Biblia nzima kwa makini, ili kutayarisha sura tano za mwisho za kitabu ulicho nacho mkononi.

Kisha nyenzo zote zilizokusanywa zilipangwa chini ya mada zake za kimantiki, na kazi ya polepole ya kucharaza mimeograph stencils ilianza. Ikiwa umewahi kuandika kwa stencil ya mimeograph, utajua itakuwa kazi kubwa kiasi gani

kuandika kurasa mia mbili kwa kutumia njia hiyo. Maelfu ya nakala za sura kadhaa za kwanza zilinakiliwa, pamoja na nakala mia tatu za Mwongozo kamili. Ndani ya miezi michache, toleo hilo la kwanza liliuzwa na kumalizika kabisa, lakini hakuna pesa zilizopatikana kwa uchapishaji wa toleo la pili.

Akiamini kwamba mbegu ilikuwa imepandwa na kwamba wengi sasa wangeshika kazi ya umishenari ya Kweli wa Tiba, mwandishi alihamisha familia yake hadi Magharibi ya Kati yani Midwest ya Marekani, na huko aligundua mwito wa haraka katika Roho ya Unabii wa kusambaza kwa upana jumbe za kitabu hicho, cha Pambano Kuu. Kwa hivyo kazi ilianza ya kuweka kitabu cha Pambano Kuu katika sauti, ambayo ndani ya miaka miwili iliyofuata ingeingia katika majimbo kumi na sita.

Miaka ikaendelea kupita, na ikawa dhahiri kwamba Mwongozo wa Umishenari wa Tiba ulihitaji kuchapishwa tena. Zile Stencil zilikuwa haziwezi kutumika tena, na hapakuwa na pesa au wakati wa kuzichapa tena. Kwa bahati nzuri, nakala moja ya thamani ilikuwa imehifadhiwa. Usadikisho ulikuwa mzito hivi kwamba nyenzo hii ilikuwa lazima iwekwe katika maandishi yaliyo wazi zaidi na kuchapishwa tena. Hata hivyo, baada ya kufanya kazi siku nzima ili kutegemeza familia yake na kutumia muda mwingi wa jioni pamoja na familia yake, hakukuwa na wakati wa kufanya kazi hiyo. Siku moja Vance Ferrel alipiga magoti mbele za Mungu na kulia kwa sababu ya hali hiyo ngumu, kwamba alikuwa na usadikisho wa kuwasaidia watu na Ujuzi wa Umishenari wa Tiba, ila hali ilikuwa ngumu kwa yeye kusonga mbele..

Kisha, katika masika ya 1977, katika chumba kidogo cha dari hapo Kusini mwa Illinois, Vance Ferrel ayaliweka wakfu upya maisha yake yote ili kufanya kazi ya Mungu. Matangazo ya Pambano Kuu yalianza tena kwenye radio, na ndani ya mwaka mmoja yalikuwa yakirushwa kwa upana kwenye vituo vinne vya matangazo ya satilaiti (satellite reflected).

Lakini ufahamu uliokua wa miaka mingi ulikuwa umethibitika kuwa hakika: ukurasa uliochapishwa ungekuwa na nguvu na ufanisi zaidi, hadi mwisho wa wakati, kuliko Neno lililowekwa kwenye sauti au linalozungumzwa.

Kwa hiyo katika majira ya jotoya mwaka 1979, uwekaji chapa ulianza katika vijuzuu vya Sabato ya Kweli na trakti Kitabu cha Great Controversy au Pambano Kuu. Ilitarajiwa kwamba kazi ya Mwongozo wa Umishenari wa Tiba ingeanza hivi karibuni; lakini, katika majira ya baridi kali ya 1979-1980, Mikutano ya Maoni ya Glacier ilipokaribia, uharaka wa kuingia kwa nadharia mpya ya theol ogy katika madhehebu yetu ulidai uangalifu, na trakti zinazotetea nafasi zetu za kihistoria

zilianza kupangwa. Katika kiangazi cha 1980, trakti hizo zilianza kuchapishwa. Tayari trakti kumi na sita za Pambano Kuu, trakti ishirini za Sabato, na trakti thelathini zinazotetea imani za kihistoria zilikuwa zimepangwa (typeset) na zilikuwa tayari kuchapishwa. Hatimaye, trakti nyinginezo zilitokezwa, zilizozungumzia habari kama vile viwango kuhusuuvaaji wa pete za arusi, muziki, na Celebration Church au ibada ya Sherehe.

Kazi ya kupanga chapa ya huu Mwongozo wa Wamshenari wa Tiba ulipewa mtendakazi, na wiki zilipita huku ukichapwa katika programu mpya ya kompyuta. Takriban miezi miwili baadaye kazi hiyo ilikamilishwa na nyenzo zilihifadhiwa kwenye diski za floppy, zikiwa zimetayarishwa kufanyiwa kazi kupitia utaratibu wa kupanga chapa. Lakin iligunduliwa hitilafu na ikaonekana kuwa wamepoteza kitabu chote. Muda na kazi ilikuwa imepotea.

Mwaka ulipita na tena tulijaribu kuchapa Mwongozo huu. Ulipokamilika, tuligundua kwamba kazi mbaya katika kuchapa ilikuwa imefanywa, na masahihisho ya kina yalipaswa kufanywa. Hii ilichukua muda zaidi.

Hatimaye kitabu kilikuwa tayari kwa ajili ya uchapishaji, lakini pesa zilikosekana za kukichapisha katika karatasi za bei ya chini ili kuenezwa sana miongoni mwa watu wetu (paperback).

Sehemu za kitabu (sura za Isaya 58, utambulisho wa dawa za kulevya, n.k.) zilichapishwa katika muundo wa Vijuzuu. Lakini bado Mwongozo ulikuwa haujachapishwa tena.

Isipokuwa Pambano Kuu, hakuna kitabu ambacho tumejaribu kuchapisha ambacho tulikumbana na shida na matatizo mengi sana.

Tunaambiwa kwamba Shetani atashindana na kila jitihada ili kufanya kazi ifaayo katika siku hizi za mwisho. Je, wewe, rafiki mpendwa, unajaribu kufanya nini kwa ajili ya Mungu? Je, Umedhamiria kwa kiasi gani kwa uthabiti kutii urithi wako wa Biblia-Roho ya Unabii? Hebu uwe na hakika kwamba utakutana na magumu unapojaribu kutimiza mapenzi ya Mungu kwa maisha yako. Lakini pia ujue kwamba malaika watakatifu watakusaidia. Hawa wanaandika katika vitabu vya mbinguni kwamba wewe ni mwaminifu kwa Muumba wako wakati ambapo sehemu kubwa ya ulimwengu iko katika uasi. Katikati ya yote yanayotokea, tunaweza kumshukuru Mungu kwa pamoja kwa baraka Zake nyingi. Yeye peke Yake Ndiye awezaye kuandaa mbegu iliyovuviwa na Roho Mtakatifu na kuipanda katika mioyo ya watu, na kuleta mavuno. Yeye peke yake Ndiye anaweza kuongoza na kuwezesha, kwenda mbele, na kufuata baada yake.

Mungu daima atatunza, na kutetea, Biblia na Roho za Kweli za Unabii ambazo Amewapa wanadamu. Ikiwa watu wa Mungu watalisoma tu Neno Lake na kulitii, bila kuchanganya mawazo yao wenyewe ndani yake, basi watatiwa nguvu na kusaidiwa. Utii rahisi, kwa imani, kwa Neno la Mungu, katika katika kuwezeshwa na Kristo ndio unaohitajika leo.

Miaka kadhaa iliyopita, hatimaye tuliweza kuchapa kitabu hiki, lakini baadaye tuligundua kwamba kurasa mbili za kitabu cha asili (kutoka Sura ya 14) hazikuwa zimechapwa kwenye kitabu kilichochapishwa. Hili na matatizo mengine madogo yamerekebishwa, na sasa tunakuletea toleo bora zaidi la kitabu hiki ambacho ni muhimu sana. na toleo hili limeongezwa mambo mengine mazuri zaidi, na uchapishaji unaendelea na pia kipo mtandaoni bure kwa Kingereza angalia Harvestime.Org na Kwa Kiswahili, RohoYaUnabii.Org, au RohoYaUnabii.Net au MaarifaMtandaoni.Com

Kuhusiana na maarifa yaliyo humu, Mwongozo wa Umishenari wa tiba ni kitabu cha kipekee katika fasihi ya masalia. Kuna mikusanyiko inayohusu maisha yenye afya na tiba asilia, lakini haielezi manufaa ya kufanya kazi hiyo, kama inavyotolewa katika Biblia na Roho ya Unabii.

Wewe unachohitaji kufanya ni kusoma sura tatu za kwanza za Mwongozo huu ili kuona kwamba ni kitabu kinachohitajika na kila mwamini Anayemngoje Yesu arudi haraka.

Tunapoinua, huduma hii ya Umishenari wa Tiba wa Vitendo, na kushiriki kwa upana jumbe zinazotolewa katika Neno la Mungu Lililovuviwa na Roho Mtakatifu—Biblia na Roho ya Unabii, Mbingu itashirikiana na jitihada zetu. Wakati ujao unaweza kuingia giza upesi miongoni mwa watu wetu wa imani na katika ulimwengu unaotuzunguka, lakini njia mbele ya masalia itakuwa angavu—ilimradi wathamini, wasome, na kutii Neno Lake Lililoandikwa.

KAZI ILIYOFANIKIWA YA UMISHENARI WA TIBA INAPATIKANA KATIKA HUDUMA YA UPONYAJI, Uk. 126 hadi 128.

126:1—Wengi huvunja sheria za afya kwa kutojua, nao wanahitaji kufundishwa.

126:2—Zoezi ambalo linaweka msingi wa magonjwa mengi na maovu makubwa zaidi ni matumizi ya huru ya dawa zenye sumu (drugs au dawa za famasia).

126:3-4—Watu wanahitaji kufundishwa kwamba dawa hazitibu magonjwa. [MUHIMU: Aya hii inaelezea kile ambacho dawa hufanya mwilini.]

127:1—Tumaini pekee la mambo bora ni kufundishwa kwa kanuni zinazofaa. Wacha Matabibu wafundishe watu kwamba nguvu ya kurejesha afya haiko katika dawa, lakini katika asili. Ugonjwa ni juhudi ya asili ya kuuweka mfumo huru kutoka katika hali zinazotokana na ukiukaji wa sheria za afya. Katika kesi ya ugonjwa, sababu ya ugonjwa inapaswa kutafutwa, na kutambuliwa kabisa. Tabia zisizo za afya zinapaswa kubadilishwa, tabia mbaya zirekebishwe (mfano kula kwa kupindukia, kutokunywa maji, kutofanya mazoezi, kutopumzika katika Siku ambayo Bwana ameagiza nk). Kisha asili inapaswa kusaidiwa katika juhudi zake za kufagilia mbali uchafu na kuweka upya hali sahihi katika mfumo.

127:2—Hewa safi, nuru ya jua, kiasi kwa kutokula kabisa vitu vibaya kwa mwili (vilevi) na kula kwa kiasi vile vizuri (maharage), pumziko, mazoezi, chakula kinachofaa, chenye lishe bora, matumizi ya maji, kila mtu anapaswa kufahamu mawakala hawa wa asili na jinsi ya kuwatumia ili kuwa katika hali njema ya afya. Ni muhimu pia kuelewa kanuni zinazohusika katika tiba/matibabu ya wagonjwa na kuwa na mafunzo ya vitendo ambayo yatawezesha mtu kutumia ujuzi huu kwa njia ifaayo.

127:3-128:4 —Hatuwezi kukumbushwa mara nyingi sana kwamba afya haitegemei bahati nasibu. Bali ni matokeo ya utii wa sheria.

Soma kila neno kwenye kurasa hizi tatu kwa uangalifu, tena na tena—hadi yazame akilini. Hapa utapata kanuni za msingi za uponyaji.

Mwito kwa Mpendwa Msomaji

Jiunge na darasa la Uandishi, Ukalimani, Kutafsiri na Uhariri WhatsApp!

Hitaji letu kuu katika huduma hii ya Machapisho Uhamishoni ni Roho Mtakatifu, ushauri, na kisha Maombi yako msomaji. Kumbuka pia huduma zingine za machapisho kwa kila lugha, taifa na jamaa. Toka mtambo wa kuchapa ubuniwe kule Ujerumani mwaka 1456 na Johannes Gutenberg, Neno la Mungu limefikia mabilioni, ila bado kuna makundi 6000 hayajafikiwa, angalia Joshugaproject.org na habari za '1040 window' Sambaza Biblia popote ndiyo kauli mbiu ya muumini, Sambaza Neno la Mungu kote. Jiunge nasi katika kuandika vitabu vya kuboresha watu, kutafsiri, kuhakiki, na kuhariri. Ombi letu, ni unapochapa, usibadilishe chochote labda typos tu, tuwasilane kama kuna kosa la dhana au lugha!

Sasa umefika wakati wa kuandika vitabu ambavyo vinaendana na muktadha wa rasilimali, mazingira na utamaduni wetu, kwani ulimwengu wa Kikristo sasa umehamia Afrika na Amerika ya Kusini. Ila hapa Kwetu Afrika Mashariki, sisi tumekuwa wazito kuandika kuhusiana na Mada mbalimbali ambazo zinaendana na mazingira yetu kwenye mada za afya, lishe, mahusiano kati ya wazazi au ndoa, kilimo na mazao yake, kulea na kukuza watoto, aina za biashara zinazoendelea, hali ya kisiasa na muumini, utendaji wa kufikia watu na kujenga makanisa, nyimbo zetu na noti zake, haya yote tunayasoma na kuyaiga kwenye vitabu na mitandao ya magharibi na ni mema tu, ila kama ulimwengu wa Kikristo umehamia kwetu, tunabidishwa pia kuwa waandishi kwa sababu tunajua hali yetu katika kufikia wengine au kuboresha afya na jamii kuliko mtu mwingine. Kwa nini nyimbo zetu nzuri zenye ujumbe mzito zisichaguliwe kwa makini, nyimbo zilizoimbwa miaka 50 hivi na kuwekwa kwenye vitabu na kisha watu waimbe. Tenzi tunazoimba za magharibi ni nzuri, ila nasi hapa tuna nyimbo nzuri na zinaendana na utamaduni wetu, kwa nini tusijiongeze nasi, ili tuongeze kwenye maktaba yetu ya nyingine, vizuri vingine, tuna wataalamu wengi wa nyimbo sasa.

Na hata vitabu vya watoto, tunahitaji watu wanaopenda watoto kufanya kazi hii kwa kushirikiana. Pia umefika wakati wa 'Reverse Mission' Watu wa Amerika ya Kusini sasa ni wainjilisti kila mahali duniani, ikiwemo magharibi kama vile Ulaya, Marekani na hata, Asia, Australia, Mashariki ya kati na Afrika! Sisi Afrika tuna Wauminin wengi kuliko Amerika ya kusini, ila bado tunaona kwamba tupate waandishi kutoka nchi zenye Wakristo wachache kuliko sisi ambao hawaandiki kwa muktadha wa mazingira yetu na watoto wetu wanaona pengine wawe na vile vitu walivyo navyo nchi zingine au wawe na mwenendo kama ule, mfano mdogo

sana utakuwa, wanafikiri sisi ni lazima tule kimchi, taco, panzit, empanada, manicotti, tortellini, sushi, falafel, je viwanda vyetu vinatengeneza vitu hivi? Kila chakula duniani kinacholimwa hufanana tu, ila jinsi ya kukitengeneza hupishana, Mwafrika atatumia ngano kupika ugali, Mhindi chapati, Mchina Noodle, Mzungu mkate au makaroni, nk. Ni kweli Kiswahili ilikuwa lugha ya kuzungumzwa na siyo ya Maandishi, ila wakati umefika maandishi kuongezwa kwenye mambo mazuri! Naelewa kwamba si utamaduni wetu kuandika, ila si utamaduni wetu kufanya mambo mengi ambayo sasa tunayafanya! Nategemea tunaiga mazuri tu! Na si kila kitabu tunachoandika ni lazima kiuzwe, vingine ni vya kusaidia jamii, wewe hautaweza kuuza kila kitu katika dunia hii kama unataka kufanya uinjilisti au kubariki watu, vingine vitakudodea.

Watu husema utamaduni wa mtu mweusi ni kusaidia jamaa na ndugu zake wa damu tu na wala sio taasisi. Yawezekana ni kweli ila tuna la kujifunza kutoka kwa kila mwanadamu. Wenzetu wa Nigeria wameanza kuweka vitabu vyao vya kuboresha jamii mtandaoni ili watu wasome na kufaidika katika nyanja mbalimbali kama vile uchumba, maombi ya kuondoa laana kwenye familia nk. Joel Nanauka ni mfano mzuri katika Ulimwengu wa Kiswahili kwenye kuandika na kugawia watu ujuzi wake, tumevisoma vitabu vyake vizuri ambavyo ametubariki kwa mamilioni kwenye ujasiliamali nk. Ukiwa na chochote, hata ni kama senti mbili za Mjane, ujuzi, uwezeshaji wa aina fulani tafadhali usisite kutufikia na pia kama una ujuzi wa kuandika vitabu au kufundisha wengine kuandika vitabu, tuwasiliane, maana ulimwengu wa Kiswahili una umasikini wa Maandishi yaliyoandikwa kwa muktadha wa utamaduni, nyenzo, na maisha yetu ya kila siku, tunaomba mashauri pia kwa kutumia email

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo BWANA!

Waliofanikisha Kazi

(Watafsiri, Wahariri, Washauri, Wana maombi, Watu wa Teknolojia, na wengine wote waliofanikisha kazi hii). Watu elfu moja wote wataamini siku moja kwa ule ujumbe wa kimya! Sambaza kwa Marafiki, ndugu jamaa, jirani na kila mtu - Samaritan Laymen Ministries

Grace Momadi-Masaka—New Jersey,usa

Nhandi Masunga-Bariadi, Tanzania

Musa Budodi—Shinyanga, Tanzania

Sandra Barron—Kentucky, USA

Cindy Tustch—Washington, USA.

Mbusi Mpagalushu—Bariadi, Tanzania

Esther Shigela Masunga-Bariadi, Tanzania

David Masaka—Pennslyvania, Marekani

Judi Mmari Mugane—Siha, Tanzania

John Mugane—Nakuru, Kenya

Paul Momadi Masaka, Jersey, Marekani

Gerard Nyafanga—Shirati,

Paul Momadi Masaka- New Jersey,

Daniel Daniel Masaka—Kisii, Kenya

Tunamshukuru Mzee Vance na Seth Ferrel kutupa idhini ya kutafsiri vitabu vyao vyote vya Harvest Time Books, na hata kusema kwamba kama tupo tayari kutafsiri Encyclopedia for Natural Remedies (rangi ya pinki), basi tuwaite tu, na tuanze kazi, kama unaweza kutusaidia kujiunga nasi tutashukuru, hasa kama una utaalamu wa kuweka miti na mimea mbadala ambayo haipatikani hapa kwetu. Nimetamani kutafsiri kitabu hiki kwa zaidi ya miaka kumi ila sikufanikiwa mpaka nilipokutana na Mwinjilisti Masunga. Bwana atusaidie kuifanya kazi hii ya umishenari wa Tiba. Kama una kitabu chochote cha Harvest Time Books unachotaka kutafsiri, tuwasiliane. Kwa kujua vitabu vingine ambavyo Huduma ya HTB wanavyo angalia Harvestimebooks.com

Kwa nini kazi tulipewa Kazi ya Umishenari wa Tiba.

Kwa nini kazi ya Umishenari wa tiba ni muhimu.

Ni nani anapaswa kuifanya kazi ya Umishenari wa Tiba.

Je kazi ya Umishenari wa Tiba inapaswa ifanywaje

Je, kazi ya Umishenari wa Tiba inapaswa ifanywe wapi

Je, kazi ya Umishenari wa Tiba inapaswa kufanywa wakati gani

Wakati wa taabu na dhiki

Kazi binafsi na kazi kwa vikundi

Kanuni za kufanya kazi

Jinsi, ambavyo Yesu alivyofanya kazi ya Umishenari wa Tiba.

Hatua kumi za Uponyaji.

Utumiaji wa Tiba Sahili/Rahisi

Utumiaji wa Maji

Dawa za Magharibi au Dawa za vidonge za Hospitalini.

Yote yaliyoandikwa katika Biblia kuhusu Umishenari wa Tiba

SEHEMU YA 1

ASILI, KUSUDI, NA WAKATI UJAO

SURA YA 1

KWA NINI UMISHENARI WA TIBA NA UJUMBE WA AFYA ULITOLEWA KWA KANISA LA MASALIA?

Je, ni nini kinachofanya maisha na kazi ya watu wanaoshika amri za Mungu na imani ya Yesu kuwa yenye thamani kubwa kwa ulimwengu ulio kwenye ukingo wa uharibifu?

1. HAPA KUNA KAZI ILIYO MBELE YETU: ENENDENI ULIMWENGUNI MWOTE NA UJUMBE

"Sasa tunaishi katika matukio ya mwisho ya kufunga historia ya ulimwengu huu. Hebu wanadamu na watetemeke wakiwekea umakini wa jukumu walilo nalo la kuujua Ukweli. Miisho ya dunia imefika. Kuzingatia ipasavyo mambo haya kutawaongoza wanadamu wote kujitoa kikamilifu na pia kutoa vyote walivyo navyo na nafsi zao kwa Mungu wao. Wajibu mzito wa kuuonya ulimwengu juu ya adhabu inayokuja uko juu yetu. Kutoka kila upande, mbali na karibu, wito unatujia kusaidia au kutoa msaada."—Evangelism, 16.

"Tunapaswa kuhisi jukumu hili sasa, la kufanya kazi kwa bidii ili kuwapatia wengine Kweli ambazo Mungu amezitoa kwa wakati huu. Hatuwezi kuwa na bidii na unyofu kutosha……. Sasa ni wakati wa onyo la mwisho kutolewa. Kuna nguvu maalum katika uwasilishaji wa Ukweli kwa wakati huu; Lakini itaendelea kuwa hivi hadi lini? —Ni kwa muda mfupi tu. Ikiwa kuliwahi kuwa na shida au taharuki, ni sasa. Wote sasa wanaamua hatima yao ya milele. Wanadamu wanahitaji kuamshwa ili kutambua uzito wa wakati, ukaribu wa siku ambayo rehema juu ya mwanadamu itakakoma."— Evangelism, 16-17.

"Kama jitihada za bidii zingetolewa kwa kazi ya kuwajulisha watu Ukweli kwa wakati huu katika miji ambayo haijaonywa, watu wasingelibakia bila kutubu kama ilivyo sasa. Kutokana na nuru ambayo nimepewa, najua kwamba huenda leo maelfu ya watu wangelikuwa na furaha kubwa zaidi katika ile Kweli,

endapo kazi Ingeendelezwa mbele kama hali inavyodai, katika mistari yenye hoja nzito (aggressive line).”—Evangelism, 21.

“Hatuna wakati wa kupoteza. Mwisho uko karibu. Njia ya kutoka mahali hadi mahali ili kueneza Ukweli hivi karibuni itazungukwa na hatari upande wa kulia na wa kushoto. Kila kitu kitawekwa kwenye njia jambo ambalo litazuia njia ya wajumbe wa Bwana, ili wasiweze kufanya yale ambayo inawezekana kwao kuyafanya sasa. Ni lazima tuangalie kwa hekima na vyema kazi iliyo mbele ya nyuso zetu, na kisha tusonge mbele kwa haraka kwa kadri iwezekanavyo katika vita vikali.”—Evangelism, 30-31.

Wote sasa wanaamua hatima yao ya milele. Wanadamu wanahitaji kuamshwa ili kutambua uzito wa wakati, ukaribu wa siku ambapo rehema juu ya mwanadamu itakapokoma. Juhudi zilizoamuliwa zinapaswa kufanywa kwa ujumbe wa wakati huu kama kipaumbele dhahiri mbele ya watu. Malaika wa tatu anapaswa kutoka na kwenda kwa nguvu nyingi. Hebu mtu yeyote asiipuuze kazi hii au kuichukulia kama ile iliyo na umuhimu mdogo.”— Shuhuda kwa Kanisa 6: 16.

2. HAPA KUNA TATIZO LA KIMSINGI: JINSI YA KUWAFIKIA WATU NA KUPATA UJASIRI WAO, KWAMBA WATUAMINI.

“Kuwafikia watu, popote walipo, bila ya kujali nafasi au hali yao, na kuwasaidia kwa kila njia—hii ndiyo huduma ya Kweli.”—Ministry of Healing, 156.

"Kila mahali kuna mioyo ambayo inalilia kitu ambacho haina. Inatamani sana uwezo utakaowapa nguvu dhidi ya dhambi, nguvu ambayo itawakomboa kutoka katika utumwa wa uovu, nguvu ambayo itawapa afya na uzima na amani.”—Ministry of Healing, 143.

“Mpango wa Mungu kwanza, ni kuufikia moyo.”—Ministry of Healing, 157.

“Mafanikio yako hayatategemea sana maarifa na yale mafanikio uliyojipatia (accomplishment), kama vile uwezo wako wa kupata njia yako ya kuelekea moyoni.”—Evangelism, 437.

3. TATIZO HILI LA MSINGI LIMETATULIWA—KRISTO ALILITATUA

“Kwa njia Zake za pekee, Yeye alisaidia wote waliokuwa katika huzuni na dhiki.”—Ministry of Healing, 23.

“Kamwe hapakuwahi kuwepo na mwinjilisti kama Kristo. Yeye Alikuwa Mkuu wa Mbinguni, lakini alijinyenyekeza na kuchukua asili yetu ili apate kukutana na

watu pale walipokuwa….. Alikwenda kutoka jiji hadi jiji, kutoka mji hadi mji, akihubiri injili na kuponya wagonjwa.”— Ministry of Healing, 22.

4. KRISTO ALITATUAJE JAMBO HILI? - NI KWA KUKIDHI MAHITAJI YAO

“Bwana wetu Yesu Kristo alikuja katika ulimwengu huu kama mtumishi asiyechoka kwa ajili ya hitaji la muhimu la mwanadamu. Yeye ‘Aliuchukua udhaifu wetu na kubeba magonjwa yetu,’ ili aweze kuhudumia kila hitaji la ubinadamu. Mzigo wa ugonjwa na unyonge, uharibifu na dhambi, Yeye alikuja kuuondoa. Ilikuwa ni utume Wake kuwaletea wanadamu urejeshwaji kamili; Yeye Alikuja kuwapa afya na amani na ukamilifu wa tabia. Hali na mahitaji ya wale walioomba msaada Wake vilikuwa tofauti-tofauti, na hakuna aliyekuja Kwake na kisha akatoka bila msaada. Kutoka Kwake ulitiririka mkondo wa nguvu za uponyaji, na katika mwili na akili na roho wanadamu wakafanywa kuwa kamili.”—Ministry of Healing, 17.

“Wakati wa huduma Yake, Yesu alitoa muda Wake mwingi zaidi katika kuwaponya wagonjwa kuliko kuhubiri. Alikuwa kama mkondo muhimu, unaoeneza uhai na shangwe.”—Ministry of Healing, 19- 20.

“Maisha yake yalisongwa na shughuli nyingi kwa kiasi kikubwa …. . popote alipokwenda, alipeleka baraka.”—Ministry of Healing, 24.

“Mwokozi aliifanya kila kazi ya uponyaji kuwa tukio la kupandikiza kanuni za Kiungu katika akili na nafsi. Hili ndilo lilikuwa kusudi la kazi Yake. Alitoa baraka za kidunia, ili apate kuilekeza mioyo ya watu kupokea injili ya neema Yake.”— Ministry of Healing, 20.

“Kama vile tunavyofuata njia ya mkondo wa maji unaoonekana kwa njia ya kijani kibichi, vivyo hivyo Kristo alionekana katika matendo ya rehema yaliyoashiria njia Yake katika kila hatua. Popote alipoenda afya ilichipuka, na furaha ikafuata popote alipopita.”— Welfare Ministry, 57.

5. JE, TUNAPASWA KUTUMIA MBINU YAKE? NAAM, HII NDIYO NJIA PEKEE INAYOFANYA KAZI

“Ikiwa kuna wakati muhimu wa kuelewa na kufuata mbinu sahihi za kufundisha na kufuata mfano wa Kristo, basi ni sasa.”— Evangelism, 53.

“Mbinu ya Kristo pekee itatoa mafanikio ya kweli katika kuwafikia watu. Mwokozi alichangamana na watu kama mtu aliyewatakia mema. Alionyesha huruma Yake kwao, alihudumia mahitaji yao, Naye akaaminika kwao-. Kisha akawaambia, ‘Nifuateni.’ ”— Ministry of Healing, 143.

“Kama mnawaendea watu kwa njia inayokubalika, inyenyekezeni mioyo yenu mbele za Mungu, na kujifunza njia Zake. Tutapata maelekezo na mafunzo mengi kwa ajili ya kazi yetu kutokana na kujifunza mbinu za Kristo za kazi na njia Yake ya kukutana na watu.”—Evangelism, 53.

“Ifanye kazi ya Kristo kuwa mfano wako. Daima alienda Yete huku na huko akitenda mema—akiwalisha wenye njaa na kuponya wagonjwa. Hakuna mtu aliyekuja Kwake kwa ajili ya kuhurumiwa akakatishwa tamaa.”—Welfare Ministry, 53.

Kristo alipowaona makutano ya watu waliokusanyika kumzunguka, “Aliwahurumia, kwa sababu walikuwa wamechoka na kutawanyika kama kondoo wasio na mchungaji.” Kristo aliona ugonjwa, huzuni, hitaji na hali mbaya ya umati ule ambao ulisongamana katika hatua Zake. Kwake mahitaji na shida za wanadamu katika ulimwengu wote ziliwasilishwa. Miongoni mwa walio juu na walio chini, wanaoheshimiwa mno na wadhilifu kabisa, Aliona roho ambazo zilikuwa zikitamani baraka zile hasa ambazo alikuwa amekuja kuleta....Welfare Ministry, 54.

Je, ni mfano gani tunapaswa kuuweka mbele ya ulimwengu? Tunapaswa kufanya kazi ile ile ambayo mmishenari Mkuu wa tiba alichukua kwa niaba yetu. Tunapaswa kufuata njia ya kujitoa dhabihu iliyokanyagwa na Kristo.”— Welfare Ministry, 54.

“Kristo aliwaona wagonjwa wenye huzuni, wahitaji na makutano ya watu duni wakijaa mbele Yake. Leo pia wahitaji wapo. Ulimwengu unahitaji watendakazi ambao watafanya kazi kama Kristo alivyofanya kwa ajili ya watu wanaoteseka na wadhambi.”—Welfare Ministry, 54.

“Je, ndugu zangu na dada zangu, mnauliza: Je, tunaiga mfano gani? Sikuelekezi kwa watu wakuu na watu wema, bali kwa Mkombozi wa ulimwengu. Ikiwa tungekuwa na roho ya kweli ya umishenari, lazima tungejazwa na upendo wa Kristo; Ni lazima tumtazame Mwandishi na Mkamilishaji wa imani yetu, tujifunze tabia Yake, tukuze roho Yake ya upole na unyenyekevu, na kutembea katika nyayo Zake.”—Welfare Ministry, 55.

“Utume wa Kiungu hauhitaji marekebisho. Njia ya Kristo ya kuwasilisha Ukweli haiwezi kuboreshwa. Mwokozi aliwapa wanafunzi masomo ya vitendo, akiwafundisha jinsi ya kufanya kazi kwa njia ya kufanya nafsi kuwa na furaha katika Ukweli. Aliwahurumia waliochoka, wale waliolemewa na mizigo, na waliokandamizwa. Aliwalisha wenye njaa na kuwaponya wagonjwa. Mara kwa

mara alienda kufanya mema. Kwa mema aliyotimiza, kwa maneno Yake ya upendo na matendo Yake ya fadhili, alifasiri injili kwa wanadamu."—Welfare Ministry, 56.

"Muungano wa kazi inayofanana na Kristo kwa ajili ya mwili na kazi inayofanana na Kristo kwa ajili ya nafsi ndiyo tafsiri ya kweli ya injili."—Welfare Ministry, 33.

"Mungu huwaita maelfu wamfanyie kazi, si kwa kuwahubiria wale wanaoijua Kweli kwa wakati huu, bali kwa kuwaonya wale ambao hawajapata kamwe kusikia ujumbe wa mwisho wa rehema. Fanya kazi kwa moyo uliojaa hamu ya dhati ya roho za watu. Fanya kazi ya umishenari wa tiba/kitabibu. Ndivyo utapata ufikiaji wa mioyo ya watu, na njia itatayarishwa kwa ajili ya tangazo lililoamuliwa zaidi la Ukweli."—Welfare Ministry, 57-58.

"Kazi ya umishenari wa tiba ndiyo kazi ya uanzilishi wa injili, mlango ambao Ukweli wa wakati huu utaingia ndani ya nyumba nyingi. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa wamishenari wa Kweli wa tiba, kwa kuwa wanapaswa kujifunza kuhudumia mahitaji ya nafsi na mwili.

Kutokuwa na ubinafsi kabisa, kunapaswa kuonyeshwa na watendakazi wetu, kwa maarifa na uzoefu unaopatikana kwa kazi ya vitendo, wakitoka kwenda kutoa tiba kwa wagonjwa. Wanapoenda nyumba kwa nyumba watapata ufikiaji wa mioyo mingi. Wengi watafikiwa ambao vinginevyo hawangesikia ujumbe wa injili."— Welfare Ministry, 125.

"Kanuni inatolewa katika mfano huu (wa Msamaria Mwema) kwamba ingekuwa vyema kwa wafuasi wa Kristo kuifuata. Kwanza, ni kukidhi mahitaji ya muda mfupi ya wahitaji na kupunguza mahitaji na mateso yao ya kimwili, na kisha utapata njia iliyo wazi ya moyo, ambapo unaweza kupanda mbegu nzuri za wema na dini."—Welfare Ministry, 118.

6. LAKINI JE, YESU HAKUTUAGIZA KUHUBIRI INJILI TU? —HAPANA, ALITUAGIZA SISI KUWAHUDUMIA WAGONJWA NA WAHITAJI PIA

"Wakati Mwokozi aliposema, "Enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi," alisema pia kwamba, "Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Ahadi hiyo inafika mbali kama lilivyo agizo hilo la utume. Si kwamba karama zote hizo zinatolewa kwa kila aaminiye. Roho hugawa "kwa kila mtu kama apendavyo." 1 Wakorintho 12:11. Lakini vipawa vya Roho vimeahidiwa kwa kila mtu kulingana na mahitaji yake kwa ajili ya kazi

ya Bwana. Ahadi hiyo ni yenye nguvu na ya kuaminika sasa kama ilivyokuwa mnamo siku za mitume. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Huu ni upendeleo kwa watoto wa Mungu, na imani inapaswa kuyashikilia yote yanayowezekana kupatikana kama uidhinishaji wa imani.

"Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Ulimwengu wetu huu ni hospitali kubwa ya wagonjwa wenye maambukizo, lakini Kristo alikuja kuponya wagonjwa, kutangaza kuokolewa kutoka katika utumwa wa Shetani. Alikuwa na afya na nguvu ndani Yake Mwenyewe. Aliweka uzima Wake ndani ya wagonjwa, wenye shida, waliopagawa na mapepo. Yeye Hakumfukuza yeyote aliyekuja kupata nguvu Yake ya uponyaji. Alijua kwamba wale waliomwomba msaada walikuwa wamekuja na magonjwa; lakini Yeye hakukataa kuwaponya. Na pindi uweza wa Kristo ulipoingia ndani ya mioyo ya maskini hawa, walisadikishwa dhambi zao, na wengi waliponywa magonjwa yao ya kiroho, pamoja na maradhi ya mwili. Leo Injili bado ina nguvu ile ile, na kwa nini sisi leo tusishuhudie matokeo kama yale? Kristo anasikia maumivu ya kila mwenye shida aumiaye. Wakati roho wachafu wanapochana mwili wa mwanadamu, Kristo anahisi laana hiyo. Wakati homa inapokuwa ikiwaka katika mkondo wa maisha, Yeye anayasikia maumivu hayo. Naye Yuko tayari kuponya sasa kama wakati ule alipokuwa duniani katika mwili. Watumishi wa Kristo ndio wawakilishi Wake, mifereji ya kazi Zake. Yeye Anatamani kuonyesha uweza Wake wa kuponya kupitia hao. Namna Mwokozi alivyoponya magonjwa kuna fundisho kwa wanafunzi Wake. Katika tukio moja Yesu alipaka macho ya mtu kipofu kwa matope, na akamwambia, "Nenda kanawe katika birika ya Siloamu, . . . Basi akaenda na kunawa; akarudi anaona." Yohana 9:7. Uponyaji ule ungefanywa tu kwa uweza wa Mponyaji Mkuu yule, lakini Kristo alitumia njia nyepesi ya asili. Wakati hakuonekana akitumia tiba ya vidoge, aliruhusu matumizi ya tiba za asili nyepesi. Kwa wagonjwa wengi waliopokea uponyaji, Yesu alisema, "Usitende dhambi tena, lisije likakupata jambo lililo baya zaidi." Yohana 5:14. Hivyo alifundisha kwamba ugonjwa ni matokeo ya kukiuka sheria za Mungu, zote mbili, yaani, za asili na za kiroho. Maumivu makubwa duniani yasingekuwepo ikiwa watu wangedumu kuishi kulingana na mpango wa Mwumbaji. Desire of Ages 823-824

Mafundisho haya ni kwa ajili yetu. Kuna masharti ya kuzingatiwa na wote wanaotaka kuhifadhi afya. Lazima wote wajifunze masharti haya. Bwana hapendezwi na ujinga unaohusu sheria Zake, ziwe za asili au za kiroho. Tunapaswa tuwe watenda-kazi pamoja na Mungu kwa ajili ya kurejesha afya ya mwili na ya roho. Na tunapaswa tufundishe watu wengine namna ya kuhifadhi na

kurejesha afya. Kwa wagonjwa tunapaswa kutumia tiba ambayo Mungu ametoa katika vitu vya asili, na tunapaswa tuwaelekeze Kwake Yeye pekee awezaye kurejesha. Ni kazi yetu kuwapeleka wagonjwa na wenye mateso kwa Kristo katika mikono ya imani yetu. Tunapaswa tuwafundishe kumwamini Mponyaji Mkuu. Tunapaswa tushikilie ahadi Zake, na kuomba udhihirisho wa nguvu Zake. Kiini chenyewe cha injili ni urejeshaji, na Mwokozi anatutaka tuwafanye wagonjwa, wasio na tumaini, na wenye shida washikilie nguvu Zake. Nguvu ya upendo ilikuwa katika kuponya kote kwa Kristo, na ni katika kushiriki upendo ule tu, kwa imani, ndipo tunapoweza kuwa nyezo za kazi Yake. Ikiwa tunapuuza kujiunganisha na Kristo kwa mwunganiko wa kimbingu, mkondo wa nguvu iletayo uzima hauwezi kutiririka katika vijito vilivyojaa kutoka kwetu ili kwenda kwa watu. Kuna mahali ambapo hata Mwokozi hakuweza kutenda matendo mengi makuu kwa sababu ya kutokuamini kwao. Vivyo hivyo sasa. kutokuamini kunalitenganisha kanisa na Msaidizi Wake wa kimbingu. Kanisa lina udhaifu wa kushindwa kushikilia Ukweli wa milele. Kwa kanisa kukosa imani, Mungu anafadhaishwa, na kupokonywa utukufu Wake. Ni katika kufanya kazi ya Kristo kwamba kanisa linakuwa na ahadi ya uwepo wa Kristo. Yeye Alisema, ‘Enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi; "na, tazama, Mimi Niko pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Kujitia nira Yake ni moja kati ya masharti ya kwanza ya kupokea uwezo Wake.’ Desire of Ages, 824-825

7. JE, KAZI HII INAHUSISHA TU, UPONYAJI WA UGONJWA?

—INAHUSISHA PIA KAZI YA ELIMU NA KATIKA KUISHI MTINDO WA MAISHA WA UTIIFU

“Wengi wametarajia kwamba Mungu angewaepusha na magonjwa kwa sababu tu wamemwomba afanye hivyo. Lakini Mungu hakuzingatia maombi yao, kwa sababu imani yao haikukamilishwa kwa matendo. Mungu hatafanya muujiza wa kuwaepusha na magonjwa wale ambao hawajijali wao wenyewe, lakini wanaendelea kukiuka sheria za afya, na hawafanyi juhudi za kuzuia magonjwa. Tunapofanya yote tuwezayo kwa upande wetu ili kuwa na afya, basi na tutegemee kwamba matokeo yenye baraka yatafuata, na tunaweza kumwomba Mungu kwa imani abariki jitihada zetu, kwa ajili ya kuhifadhi afya. Kisha Yeye atajibu maombi yetu, ikiwa Jina Lake linaweza kutukuzwa kwa njia hiyo.”—Counsels on Diet and Food, 26.

“Hebu asiwepo mtu yoyote anayedai kuwa mtauwa, na huku anashugulika na afya yake ya mwili kwa uzembe na kutojali, huku akiendelea kujigamba na kujidanganya yeye mwenyewe kwamba kutokuwa na kiasi si dhambi, na kwamba

hakutaathiri hali yake ya kiroho. Kuna uhusiano wa hisia za huruma ya karibu sana kati ya mwili na asili ya maadili."— Counsels on Diet and Food, 43.

"Ili kufaa kwa ajili ya unyakuo au kwenda mbinguni, watu wa Mungu lazima wajitambue. Ni lazima wajielewe wenyewe na maumbile ya miili yao, ili kwamba waweze kuungana na mwandishi -Zaburi kwa kusema, 'Nitakushukuru Bwana, kwa kuwa nimeumbwa kwa jinsi ya kutisha ya ajabu.' Daima Wangepaswa kuithibiti hamu au uchu wa chakula, uchu wao wa chakula utiishwe na viungo vya maadili na akili. Mwili unapaswa kuwa mtumishi wa akili, na sio akili kuwa mtumwa wa mwili."— Counsels on Diet and Foods, 33.

"Wale ambao huchagua kuwa wenye majivuno na ujuvi, wakisema, "Bwana Ameniponya na sihitaji kujizuia katika lishe yangu; Naweza kula na kunywa kama nipendavyo," hivi karibuni tu, watahitaji nguvu ya Mungu irejezayo katika mwili na roho pia. Kwa sababu Bwana amekuponya kwa rehema Zake, wewe haupaswi kabisa kudhania kuwa unaweza kujifungamanisha mwenyewe na mazoea ya kuiendekeza nafsi kwa mazoea ya ulimwengu. Fanya kama Kristo Alivyokuamuru akiwepo hapa ulimwenguni baada ya kazi Yake ya uponyaji_" enenda zako, wala usitende dhambi tena." Yohana 8:11. Uchu wa chakula haupaswi kuwa mungu wako."—Counsels on Diet and Food, 25.

8. KWA KUWA TUNAISHI KARIBU SANA NA UJIO WA PILI WA KRISTO, JE, TUNA WAKATI WA KAZI HII? —NI LAZIMA TUFANYE HIVYO ILI KUJIANDAA KWA UJIO WAKE!

"Mungu ameonyesha kwamba matengenezo ya afya yanahusiana kwa karibu sana na ujumbe wa malaika wa tatu kama vile mkono ulivyo kwa mwili-mkono unavyohusiana na mwili. Hakuna mahali popote penye sababu kubwa sana ya kuzorota kimwili na kimaadili kama kupuuza somo hili muhimu. Wale wanaojifurahisha kwa uchu na tamaa mbaya, na kufumba macho yao kwa nuru kwa kuogopa kwamba wataziona anasa za dhambi wanazoziendekeza, na ambazo hawataki kuziacha, wana hatia mbele za Mungu."— Counsels on Diet and Foods, 71-72.

"Maarifa na ujuzi vinapaswa kuongezwa kuhusiana na jinsi tunavyokula, na kunywa, na kuvaa ili kuhifadhi afya. Ugonjwa husababishwa na kukiuka sheria za afya; Ni matokeo la kukiuka sheria ya asili."— Counsels on Diet and Foods, 21.

"Watu wa Mungu wanapaswa kujiweka katika mkao ambao, utawawezesha kukua katika neema, wakitakaswa, mwili, nafsi, na roho, kwa ile Kweli. Wanapojitenga na anasa zote zinazoendekezwa na ambazo zinaharibu afya, watakuwa na

mtazamo safi zaidi wa kile kinachojumuisha utauwa wa Kweli. Badiliko la ajabu litaonekana katika uzoefu wa kidini.”— Counsels on Diet and Foods, 34.

"Umejikwaa katika matengenezo ya afya. Inaonekana kwako kuwa kiambatisho kisicho na maana cha Ukweli. Si hivyo; Ni sehemu ya ile Kweli. Hapa kuna kazi iliyo mbele yako ambayo itakuja karibu na kukujaribu zaidi kuliko kitu chochote ambacho bado kimeletwa juu yako. Unajikwaa juu ya baraka zile zile ambazo mbingu imeweka katika njia yako ili kufanya maendeleo yao na kusonga mbele kwako kusiwe kugumu.”— Counsels on Diet and Foods, 39.

“Tunahitaji kujifunza kuwa uchu wa kula unaoendekezwa ndiyo kikwazo kikubwa zaidi, cha uboreshaji wa akili na utakaso wa nafsi.”— Counsels on Diet and Foods, 45.

“Chochote kinachopunguza nguvu za kimwili hudhoofisha akili, na kuifanya isiweze kutofautisha kati ya haki na makosa-kuchuja baya na jema. Tunakuwa na uwezo mdogo wa kuchagua mema, na kuwa na nguvu kidogo ya kufanya yale tunayojua kuwa ndiyo sahihi.”— Counsels on Diet and Foods, 48-49.

“Kwa vile wazazi wetu wa kwanza waliipoteza bustani ya Edeni kwa sababu ya tamaa ya kula, tumaini letu pekee la kuirejesha Edeni ni kupitia kukana kabisa nguvu ya uchu wa kula na shauku/tamaa.”— Counsels on Diet and Food, 59.

“Nguvu ya kudhibiti uchu wa kula itathibitisha uharibifu wa maelfu, wakati, kama wangeshinda katika kipengele hiki, wangekuwa na uwezo wa kimaadili kupata ushindi juu ya kila jaribu lingine la Shetani. Lakini wale ambao ni watumwa wa ulafi wa chakula, watashindwa katika kukamilisha tabia ya Kikristo.”— Counsels on Diet and Foods, 59.

“Mungu hudai kwamba hamu ya chakula lazima itakaswe, na kwamba kujikana nafsi kuzingatiwe kwa yale yote yasiyofaa. Hii ni kazi ambayo itabidi ifanywe kabla ya watu Wake Bwana kusimama mbele Zake wakiwa wakamilifu.”— Shuhuda kwa Kanisa, 9: 153-154.

“Ikiwa mwanadamu ataitunza nuru ambayo Mungu katika rehema humpa kuhusiana na matengenezo ya afya, mtu anaweza kutakaswa kwa njia ya ile Kweli, na kupewa stahiki kwa ajili ya kutokufa.”— Counsels on Diet and Foods, 70.

9. JE, KANUNI ZA MAISHA YENYE AFYA ZINAPASWA KUWA NA UHUSIANO GANI KATIKA UJUMBE WETU KWA ULIMWENGU? —ZINAPASWA KUWA KARIBU KAMA MKONO ULIVYO NA MWILI

"Nilionyeshwa kuwa Matengenezo ya afya, ni sehemu ya ujumbe wa malaika wa tatu, na ina uhusiano wa karibu nayo kama vile sehemu ya juu ya mkono ilivyo na mwili wa mwanadamu. Niliona kwamba sisi kama watu lazima tuchukue hatua ya mapema katika kazi hii kuu. Wachungaji na watu lazima waifanye kwa mapatano. Watu wa Mungu hawako tayari kwa kilio kikuu cha malaika wa tatu. Wana kazi ya kufanya ambayo hawapaswi kuiacha ili Mungu awafanyie. Yeye Amewaachia kazi hii wao. Ni kazi ya mtu binafsi; Mtu mmoja hawezi kuifanya kwa ajili ya mwingine."— Counsels on Diet and Foods, 74.

"Matengenezo ya afya yanapaswa kusimama kwa ukubwa na uwazi zaidi katika kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu …….. Katika umoja ulioboreshwa na kamili na huduma ya Injili, kazi ya matengenezo ya afya itafunua uwezo wake uliotolewa na Mungu. Chini ya ushawishi wa injili, matengenezo makubwa yatafanywa na kazi ya umishenari wa tiba. Lakini ukiitenganisha kazi ya umishenari wa tiba na Injili, kazi itaharibiwa/italemaa vibaya."— Counsels on Diet and Foods, 75.

"Kwa miaka mingi Bwana amekuwa akiitaa usikivu wa watu Wake kwenye matengenezo ya afya. Hili ni mojawapo ya matawi makuu ya kazi ya kutaandaa ujio wa Mwana wa Adamu."— Counsels on Diet and Foods, 70-71.

"Ninaweza kuona katika majaliwa ya Bwana kwamba kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kuwa daraja kubwa la kuvukia, ambalo kwalo roho iliyo na ugonjwa inaweza kufikiwa."— Counsels on Diet and Foods, 76.

"Somo kuu la matengenezo linapaswa kuchochewa/kutibuliwa, na akili ya umma inapaswa kuamshwa. Kiasi katika mambo yote kinapaswa kuunganishwa na ujumbe, kuwageuza watu wa Mungu kutoka katika ibada yao ya sanamu, ulafi wao, na ubaradhifu wao mkubwa katika mavazi na mambo mengine."— Counsels on Diet and Food, 71.

"Bwana hudisaini/hupanga kwamba somo kubwa la matengenezo ya afya litasisitizwa mawazoni mwa watu, na umma utapatwa na tashishwi ya kina kulichunguza; kwa maana haiwezekani kwa wanaume na wanawake, wenye tabia zao za dhambi, zenye kudhuru afya, na zenye kudhoofisha ubongo, kuweza kupambanua Ukweli mtakatifu, ambao kupitia huo wanapaswa kutakaswa, kusafishwa, kuinuliwa, na kufanywa wafae kwa jamii ya malaika wa mbinguni, katika ufalme wa utukufu…."— Counsels on Diet and Food, 70.

"Ni vizuri, katika kuwasilisha Ukweli kwa wasioamini, kwanza tuwasilishe baadhi ya mada ambazo watakubaliana nasi. Kanuni za afya na kiasi zitavutia maamuzi

na busara yao, na kutokana na masomo haya, tunaweza kuwaongoza kuelewa madai ya lazima ya Amri ya Nne."— Counsels on Health, 545.

"Matengenezo ya afya yanapofanywa ipasavyo, ni mpenyo wa kuingia, na hivyo kufanya njia ya zile Kweli zingine kuufikia moyo."— Counsels on Health 434.

10. JE, KUNA SABABU NYINGINE KWA NINI MATENGENEZO YA AFYA LAZIMA YAHUBIRIWE?
—NDIYO, NI SEHEMU YA SUALA LA MSINGI KATIKA PAMBANO KUU: UTII KWA SHERIA ZA MUNGU.

"Tangu mwanzo wa pambano hilo kuu kule mbinguni, limekuwa ni kusudi la Shetani kuivunjilia mbali Sheria ya Mungu [Amri Kumi – Kutoka 20:3-17; Yohana-8:44; Ufuuo 12:7 -9,12,17]. Ilikuwa ni kwa kusudi la kutekeleza jambo hilo yeye aliingia katika maasi yake dhidi ya Muumbaji wake, na ingawa alitupwa chini kutoka mbinguni, yeye ameendelea na vita ile ile juu ya dunia hii. Kuwadanganya wanadamu, na kwa njia hiyo kuwashawishi kuivunja Sheria ya Mungu [Amri Kumi], ni lengo ambalo adui amelifuatilia kwa uthabiti sana bila ya kutetereka."—Great Controversy, 582.

"Pambano kuu la mwisho kati ya Ukweli na uongo ni vita vya mwisho katika pambano la muda mrefu juu ya sheria ya Mungu. Sasa tunaingia sasa katika vita hii."— Great Controversy, 582.

"Yesu, akitazama chini hadi kizazi cha mwisho, aliona ulimwengu ukihusika katika udanganyifu sawa na ule uliosababisha uharibifu wa Yerusalemu. Dhambi kuu ya ulimwengu wa Kikristo ni kukataa kwao sheria ya Mungu, msingi wa serikali Yake mbinguni na duniani."—Great Controversy, 22.

"Uvunjaji wa sheria ya kimwili ni uvunjaji wa sheria ya Mungu. Muumba wetu ni Yesu Kristo. Yeye Ndiye Mwanzilishi wa miili yetu-Muumbaji. Yeye Ameumba mfumo wa mwanadamu. Yeye ndiye Mwanzilishi wa sheria za kimwili, kama vile alivyo Mwanzilishi wa sheria ya maadili. Na mwanadamu ambaye ni mzembe na asiyejali matokeo kama kichaaa katika mazoea na matendo yanayohusu maisha na afya yake ya kimwili, hutenda dhambi dhidi ya Mungu."— Counsels on Diet and Foods, 43.

"Wanaume na wanawake hawawezi kukiuka sheria ya asili kwa kuendekeza hamu mbaya na tamaa mbaya, bila ya kuvunja sheria ya Mungu. Kwa hivyo Yeye ameruhusu nuru ya matengenezo ya afya kutuangazia, ili tuweze kuona dhambi yetu katika kuvunja sheria alizoziweka katika maisha na uhai wetu. Furaha na Starehe zetu zote au mateso vyaweza kugunduliwa kwamba vimetokana na utii

au uvunjaji wa sheria ya asili. Baba yetu wa mbinguni Mwenye neema anaona hali ya kusikitisha ya watu ambayo inahitaji karipio, ambayo wengine kwa kujua lakini wengi kwa kutojua, wanaishi kwa kukiuka sheria ambazo Yeye ameweka. Na kwa upendo na huruma Yake, kwa jamii ya wanadamu, Yeye husababisha nuru kuangaza juu ya matengenezo ya afya. Yeye Anaandika sheria Yake na adhabu ambayo itafuata ukiukaji wa hiyo sheria, ili wote wapate kujifunza na kuwa waangalifu katika kuishi kwa amani na sheria ya asili. Anatangaza sheria Yake kwa kuibanisha wa kabisa na kuifanya iwe maarufu sana kiasi kwamba inakuwa kama mji uliowekwa juu ya kilima. Viumbe wote wenye uwajibikaji wanaweza kuielewa ikiwa watataka. Watu wenye utindio wa ubongo au wenye maradhi ya akili (idiots) ndiyo hawatawajibika. Kuiweka wazi sheria ya asili, na kuhimiza utii wake, ni kazi inayoambatana na ujumbe wa malaika wa tatu, kuandaa watu kwa kuja kwa Bwana."— Counsels on Diet and Foods, 69; 3 Shuhuda kwa Kanisa, 161.

"Hatuwezi kukumbushwa mara nyingi kiasi cha kutosha, kwamba afya haiji kwa bahati nasibu. Afya ni matokeo ya utii wa sheria."—Ministry of Healing, 128.

"Mafanikio ya matengenezo hutegemea uelewa ulio dhahiri wa zile Kweli za msingi alizoziweka Mungu…… Wakati, kwa upande mmoja, hatari hujificha katika falsafa na imani za kishupavu au kupitiliza, kwa upande mmoja, kuna hatari kubwa katika kuwa huru kiasi cha kutojali matengenezo ya afya. Msingi wa matengenezo yote endelevu, ni sheria ya Mungu. Twapaswa kuwasilisha kwa mistari iliyo wazi na bainishi, hitaji la kuitii sheria hii ya Mungu. Kanuni Zake hazina budi kuwekwa mbele ya watu."—Ministry of Healing, 129.

"Nilionyeshwa tena kwamba matengenezo ya afya ni tawi moja la kazi kubwa ambayo yapasa kuwaandaa watu kwa ajili ya ujio wa Bwana. Haya Yameunganishwa kwa uwazi na ujumbe wa malaika wa tatu kama vile mkono ulivyo kwa mwili. Sheria ya Amri Kumi imekuwa ikizingatiwa kwa udogo sana na mwanadamu; lakini Bwana hangekuja kuwaadhibu wakosaji wa sheria hiyo bila kwanza kuwatumia wanadamu ujumbe wa onyo. Malaika wa tatu anatangaza ujumbe huo. Kama wangekuwa waatiifu daima kwa sheria ya Amri Kumi, wakitekeleza katika maisha yao kanuni za maagizo hayo, laana ya maradhi ambayo sasa inafurika ulimwenguni isingekuwepo."— Counsels on Diet and Foods, 69.

"Ingawa matengenezo ya afya sio ujumbe wa malaika wa tatu, yameunganishwa kwa uhusiano wa karibu nayo. Wale wanaotangaza ujumbe wanapaswa kufundisha matengenezo ya afya pia. Hili ni somo ambalo ni lazima tulielewe, ili

tuwe tayari kwa matukio ambayo yanatukaribia, na linapaswa kuchukua kipaumbele. Shetani na mawakala wake wanatafuta kuzuia kazi hii ya matengenezo, na watafanya yote wawezayo kuwachanganya na kuwatatanisha watu na kuwabebesha mizigo wale wanaojihusisha nayo kwa moyo wote. lakini asiwepo hata mmoja anayepaswa kukatishwa tamaa na jambo hilo, au kusitisha jitihada zake kwa sababu hiyo."— Counsels on Diet and Foods, 77.

"Tunapigana vita halisi kila siku ambayo ndiyo itakayoamua matokeo yetu kwa umilele. Tunakutana na maadui wasioonekana. Malaika waovu wanajitahidi kumdhibiti kila mwanadamu. Chochote kinachodhuru afya, sio tu hupunguza nguvu za kimwili, lakini pia huelekea kwenye kudhoofisha nguvu za akili na maadili. Kuendekeza mazoea yoyote yasiyo ya afya hufanya iwe vigumu kwa mtu kutofautisha kati ya mema na mabaya, na hivyo kufanya mambo yawe magumu zaidi katika kuupinga uovu. Hali hii huongeza hatari ya kushindwa na kutofikia goli kwa kukata tamaa."— Ministry of Healing, 128.

"Hivyo kazi ya umishenari wa tiba wa dhati, inafungamanishwa na kushika amri za Mungu bila kutenganishwa, ambapo Sabato inatajwa kwa njia mahususi, kwa kuwa ndiyo kumbukukizi kuu, kwenye kazi ya uumbaji ya Mungu. Ushikaji/Utunzaji wake unafungamanishwa na kazi ya kurudisha sura ya kimaadili ya Mungu ndani ya mwanadamu. Hii ndiyo huduma ambayo watu wa Mungu wanapaswa kuendeleza wakati huu. Huduma hii ikifanywa ipasavyo, italeta baraka tele kwa kanisa."—Shuhuda kwa Kanisa, 6: 266.

SURA YA 2

UJUMBE WA ISAYA 58 KWA KANISA LA MASALIA

Mwongozo wa Kutayarisha Watu kwa ajili ya Kilio Kikuu na Kubadilishwa miili.

Ndani ya sura ya hamsini na nane ya Isaya unapatikana ujumbe maalum kwa ajili ya watu wetu. Hatungetambua umuhimu wake mkubwa kama uvuvio usingeufunua kwetu. Na Mungu kupitia Maandiko anapozungumza na wakati wetu, tunahitaji kuwa wasikivu sana kwa kile anachosema.

Hapa, ndani ya sura hii, yanapatikana matatizo manne mahususi katika kanisa letu leo. Nabii wa siku zetu anatoa maoni juu ya unabii wa wakati wetu ambao uliandikwa karne nyingi zilizopita.

Fikiria kwa uangalifu kanuni zifuatazo na matumizi yake, na kwa maombi uziweke moyoni katika maisha yako mwenyewe. Tuko hapa tukitazama msingi wa tatizo la Laodikia. Jambo la muhimu ni kwamba, kila moja ya mabadiliko haya manne yanayohitajika sana (ikiwa yatatiiwa jinsi yanavyopaswa kutiiwa) yanaweza baada ya muda kukuongoza kwenye mgogoro mkubwa na kanisa lako au serikali yako. Lakini hii inaonyesha wazi jinsi ambavyo hali imekuwa mbaya na tata sana.

Ni wakati wa kuomba na ni wakati wa kubadilisha maisha yetu- bila kujali ni gharama gani. Eliya alikuwa tayari kufanya kile kilichohitajika kufanywa katika siku zake, katika kila moja ya maeneo haya manne; isingekuwa kuingilia kati kwa Mungu, ingegharimu maisha yake.

Wakati wewe na mimi tumefika mahali ambapo tuko tayari kufa kwa ajili ya imani zetu—imani ambazo hatimaye zinageuka kuwa vitendo—basi kazi ya Mungu duniani itakamilika na Yesu atarudi.—Rafiki, hebu tuanze!

SURA YA PEKEE KWA AJILI YA WATU WA MUNGU LEO

“Sura nzima ya hamsini na nane ya Isaya inapaswa kuonwa kuwa ni ujumbe wa wakati huu, utolewe tena na tena.”— Special Testimonies, Series B, No. 2, Page 5.

“Sura nzima inatumika kwa wale wanaoishi katika kipindi hiki cha historia ya dunia. Fikiria sura hii kwa makini; kwa maana itatimizwa.”— Manuscript 36, 1897.

“Je, Bwana asema nini katika sura ya hamsini na nane ya Isaya? Sura nzima ina yenye umuhimu mkubwa zaidi.”— Shuhuda kwa Kanisa, 8: 159.

“Waadventista wengi wa Siku ya Saba wanashindwa kutambua jukumu ambalo liko juu yao ili kushirikiana na Mungu na Kristo kwa ajili ya kuokoa roho. Hawaionyeshi mbele ya ulimwengu hali ya kujali sana ambayo Mungu anayo kwa wenye dhambi. Hawatumii vyema fursa walizopewa. Ukoma wa ubinafsi umelishika kanisa. Bwana Yesu Kristo ataliponya kanisa kwa ugonjwa huu mbaya ikiwa litahitaji kuponywa. Dawa hiyo inapatikana katika sura ya hamsini na nane ya Isaya.”— Counsels on Stewardship, 85.

KWANZA, ONYESHA DHAMBI NA KUACHANA NAYO

—ACHA KUITAZAMA KWA UKIMYA

“Piga kelele, usiache, Paza sauti yako kama tarumbeta; Uwahubiri watu wangu kosa lao, Na nyumba ya Yakobo dhambi zao.”—Isaya 58:1.

“Kazi yetu ni kuwaamsha watu. Shetani pamoja na malaika zake wote ameshuka kwa nguvu nyingi, kufanya kazi kwa kila udanganyifu unaoweza kuwaziwa ili kukabiliana na kazi ya Mungu. Bwana ana ujumbe kwa watu Wake. Ujumbe huu utapelekwa, bila kujali ikiwa watu wataukubali au kuukataa.

Kama katika siku za Kristo, kutakuwa na njama za kina za nguvu za giza, lakini ujumbe haupaswi kufichwa kwa maneno laini au hotuba za kutaka haki, kilio cha amani, amani, wakati hakuna amani, kwa wale wanaomwacha Mungu. ‘Hakuna amani, asema Mungu wangu, kwa waovu.’ [Isaya 58:1-2, imenukuliwa].”— Manuscript 36, 1897.

PILI, WATENDEE WENGINE KWA HAKI.

ACHA KUWATENDEA VIBAYA NA KUWATUMIA KWA FAIDA YAKO MWENYEWE

“Walakini wanitafuta kila siku; hupenda kujua njia Zangu; kama vile taifa waliotenda haki, wasioacha sheria ya Mungu wao, hutaka Kwangu amri za haki; hufurahi kumkaribia Mungu. Husema, Mbona tumefunga, lakini huoni? Mbona tumejitaabisha nafsi zetu, lakini huangalii? Fahamuni, siku ya kufunga kwenu mnatafuta anasa zenu wenyewe, na kuwalemea wote watendao kazi kwenu.

“Tazama, ninyi mwafunga mpate kushindana na kugombana, na kupiga kwa ngumi ya uovu. Hamfungi siku hii ya leo hata kuisikizisha sauti yenu juu.

Je! Kufunga namna hii ni saumu niliyoichagua mimi? Je! Ni siku ya mtu kujitaabisha nafsi yake? Ni kuinama kichwa kama unyasi, na kutanda nguo za magunia na majivu chini yake? Je! Utasema ni siku ya kufunga, na ya kukubaliwa na BWANA?"— Isaya 58:2-5.

"Ndugu zangu, mnahitaji kujifunza kwa makini zaidi sura ya hamsini na nane ya Isaya (58). Sura hii inaashiria njia pekee ambayo tunaweza kufuata kwa ajili ya usalama.

"Piga kelele, usiache, Paza sauti yako kama tarumbeta; Uwahubiri watu Wangu kosa lao, Na nyumba ya Yakobo dhambi zao."—Waonyeshe mahali wanapofanya kosa. Waonyeshe hatari iliyo mbele yao. Waambie dhambi wanazofanya, wakati huo huo wanajivunia haki yao wenyewe. Wakidhani wanamtafuta Mungu, wanamsahau, wakisahau kwamba Yeye ni Mungu wa upendo na huruma, mvumilivu na mwema, anayeshughulikia rehema ya haki na upendo. Sera ya kidunia imewajia katika maisha yao ya kibiashara na kidini. Mioyo yao haijatakaswa kupitia Kweli. Mungu hutazama kaida/sherehe zao za nje za unyenyekevu kama dhihaka kuu. Anachukulia udanganyifu wowotete wa kidini kama tusi Kwake Mwenyewe.

"Watu ambao nabii aliwazungumzia walikuwa na madai makubwa ya uchaji Mungu, na waliashiria kufunga kwao na aina zingine za nje kama ushahidi wa uchaji Mungu wao. Lakini matendo yao yalikuwa yamechafuliwa na ugonjwa wa ubinafsi na tamaa. Hawakuwa na kitu chochote isipokuwa kile walichopokea kwanza kutoka kwa Mungu. Yeye Aliwapa fadhili Zake ili wawe mkono Wake wa msaada, wakifanya kile Kristo angefanya ikiwa angekuwa mahali pao, wakiwasilisha vyema kanuni za mbinguni."—Letter 76, 1902.

"Ishara za nje za kufunga na sala, bila roho iliyopondeka na yenye majuto, hazina thamani machoni pa Mungu. Kazi ya ndani ya neema inahitajika. Unyenyekevu wa roho ni muhimu. Mungu anaangalia hili. Atawapokea kwa neema wale watakaonyenyekeza mioyo yao mbele Yake. Atayasikia maombi yao na kuponya ukafiri wao au kurudi nyuma kwao. Wahudumu wa Mungu na watu wanahitaji kazi ya kutakaswa katika roho zao, ili hukumu za Mungu ziondolewe kwao. Mungu anasubiri—anasubiri unyenyekevu na toba. Yeye Atawapokea wote watakaomgeukia kwa mioyo yao yote."—Manuscript 33, 1903.

"Watu walioelezewa hapa wanatambua kwamba hawana kibali cha Mungu; lakini badala ya kutafuta kibali Chake kwa njia Yake Mwenyewe, wanaingia katika kutopatana na Mungu-mgogoro. Wanauliza kwa nini, kwa kuwa wanashika kaida/sherehe nyingi, Naye Bwana hawatambui kwa namna ya pekee. Mungu

anajibu malalamiko yao: “Fahamuni, siku ya kufunga kwenu mnatafuta anasa zenu wenyewe, na kuwalemea wote watendao kazi kwenu.”

Tazama, ninyi mwafunga mpate kushindana na kugombana, na kupiga kwa ngumi ya uovu. Hamfungi siku hii ya leo hata kuisikizisha sauti yenu juu.' Kufunga huku ni onyesho la nje tu, wanajifanya au ni maigizo tu, unyenyekevu wa dhihaka. Waabudu hawa, wakati wanaomboleza na kuangua vilio, ila wanahifadhi sifa zote za tabia zao zinazokera. Mioyo yao haijanyenyekezwa, wala haijatakaswa kutokana na uchafu wa kiroho. Hawajapokea mvua laini za neema ya Mungu. Wamefilisika Roho Mtakatifu, wanaishi bila utamu wa ushawishi wa mbinguni. Hawana toba, wala imani inayofanya kazi kwa upendo na kutakasa roho. Hawatendi haki na ni wenye ubinafsi katika mahusiano yao na wengine, wakiwanyanyasa bila huruma wale wanaowaona kuwa wako chini yao.

Bado wanamtuhumu Mungu kwa kupuuzia kuonyesha nguvu Yake kwao, na kujitukuza juu ya wengine kwa sababu ya uadilifu wao. Bwana anawatumia ujumbe wa onyo la moja kwa moja, akionyesha kwa nini hawakupata neema Yake."— Manuscript 48, 1900.

"[Isaya 58:1-4, imenukuliwa] …… Nyumba ya Yakobo, wakati onyo hili lilikuwa likitolewa kwa Isaya, ilionekana kuwa watu wenye usongo/bidii sana, wakimtafuta Mungu kila siku, na wakipenda kujua njia Zake; lakini kwa kweli walikuwa wamejaa kiburi cha kujitegemea wao wenyewe. Hawakutembea katika ile Kweli. Kutenda wema, rehema, na upendo havikutendwa. Wakati wangali wanaonyesha kuomboleza kwa dhambi zao, walikuwa wakipenda kiburi na tamaa ya fedha na vitu. Wakati huo huo wangali wakionyesha unyenyekevu wa nje, walikuwa wanamlazimisha mtu anayefanya kazi kwao kufanya kazi ngumu. Walikuwa na maoni ya juu kuhusiana na mema yote waliyoyafanya, lakini walidharau sana huduma za wengine. Walimdharau na kumnyanyasa maskini. Na kufunga kwao kuliwapa tu maoni ya juu zaidi ya wema wao binafsi.

"Kuna dhambi za aina hii kati yetu leo, na zinaleta laana ya Mungu juu ya kanisa Lake. Popote ambapo dhambi hizo zinapatikana, nyakati za kufunga na sala zinahitajika hakika; lakini lazima ziambatane na toba ya kweli na matengenezo yaliyoazimiwa. Bila unyenyekevu wa roho kama huo na moyo uliopondeka, nyakati hizi huongeza tu hatia ya mkosaji. Bwana ameelezea saumu aliyoichagua, ile atakayoikubali. Ni ile inayoleta matunda kwa utukufu Wake, katika toba, katika kujitolea, katika uchaji-Mungu wa kweli. [Isaya 58:6-7, imenukuliwa].

"Katika saumu ambayo Mungu ameichagua, rehema, upole, na huruma vitaonyeshwa. Uroho wa mali utaondolewa, na udanganyifu na uonevu

vitafanyiwa toba na kukataliwa. Mamlaka yote na ushawishi vitatumika kuwasaidia maskini na watu walioonewa."— Review, Oktoba 13, 1891.

“Je! Saumu niliyoichagua, siyo ya namna hii? Kufungua vifungo vya uovu, kuzilegeza kamba za nira, kuwaacha huru walioonewa, na kwamba mvunje kila nira?"—Isaya 58:6.

"Bwana hajampa mtu kazi ya kuweka nira shingoni mwa watu Wake, akiwafunga kwa njia ambayo hawana uhuru wa kumtazama Yeye na kuongozwa Naye. Si mpango wa Bwana kwamba watu Wake wathibitiwe na kuongozwa na mawazo ya wanadamu wenzao kirahisi, wakati ambapo wao wenyewe tegemeo lao ni Mungu tu."— Letter 76, 1902.

TATU, WAHUDUMIE MAHITAJI YAO KWA HURUMA NA REHEMA

"Je! Siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? Umwonapo mtu aliye uchi, umvike nguo; wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe?"—Isaya 58:7.

"Kwa yule anayetembea katika njia ya uzima wa milele, akitumia baraka zake kuwabariki wengine, nabii Isaya anasema:

“Naye BWANA atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui. Isaya 58: 11.”

"Baraka hizi tunazihitaji. Tunahitaji maji ya uzima yanayotiririka kutoka kwa Yesu Kristo, ambayo yatakuwa ndani yetu chemichemi ya maji inayotiririka uzima wa milele. 'Bwana atakuongoza daima.' Tunapoongozwa na Bwana, tutakuwa na utambuzi dhahiri. Hatutaita uadilifu kuwa uovu, wala hatutafikiri kwamba mambo ambayo Bwana ameyakataz ndiyo sahihi. Tutaelewa mahali Bwana anafanya kazi.

"Wengi hawajalijua hili. Kuna baadhi ya watu ambao najua wamepotoshwa na adui. Lakini Mungu anataka kukufanya wewe kuwa mshirika wa tabia ya Uungu-2Petro1:4. Yeye Hataki nira yoyote ya mamlaka ya mwanadamu iwe shingoni mwako, badala yake utamwangalia Yeye ambaye anaweza kumwokoa kabisa kila mtu amwendeaye katika uadilifu na Kweli. Hatuna muda wa kucheza na adui, kwa sababu tuko karibu sana na mwisho wa historia ya dunia hii."— Manuscript 43, 1908.

"Uchaji Mungu na maarifa ya kiroho yaliyokomaa na ukuaji wa kanisa huenda sambamba na bidii, uchaji Mungu, na akili ya umishenari ambayo imeletwa ndani

yake, na kupelekwa kuwa baraka kwa wale wanaohitaji msaada wetu zaidi. Nakuhimiza tena utafakari sura ya Isaya 58, ambayo inafungua shamba kubwa la mizabibu la kufanya kazi kulingana na mistari ambayo Bwana ameonyesha. Hii itakapokamilika kutakuwa na ongezeko la rasilimali za maadili na kanisa halitaendelea kubakia limesimama kamwe. Kutakuwa na baraka na nguvu zikiandamana na kazi yao. Watakuwa wameushinda ubinafsi na uchoyo ambao umefunga roho , na sasa nuru yao itatolewa na kuangaza ulimwengu kwa njia ya miale safi, na angavu ya imani hai na mfano wa Kiungu. Bwana anazo ahadi Zake kwa ajili wote watakaofanya matakwa/mahitaji Yake."— Manuscript 14a, 1897.

"Suala la kutunza ndugu zetu wazee na dada ambao hawana makazi linasisitizwa kila wakati. Nini kinaweza kufanywa kwa ajili yao? Nuru ambayo Bwana amenipa imekuwa ikirudiwa: Si vizuri kuanzisha taasisi za kutunza wazee……. Wala hawapaswi kupelekwa mbali na nyumbani ili waweze kutunzwa mahali fulani. Hebu wanachama wa kila familia wawahudumie ndugu zao wenyewe. Hili lisipowezekana, kazi hiyo ni ya kanisa, na inapaswa kukubaliwa kama wajibu na kama upendeleo/fursa….

“Mchungaji anapaswa kuelimisha familia mbalimbali na kuimarisha kanisa ili litunze wagonjwa na masikini wake lenyewe . . Hebu watu na wajinyime anasa na mapambo yasiyo ya lazima, ili waweze kuwafanyia wahitaji wenye kuteseka waweze kufarijika-kwa kupata mahitaji ya msingi. Katika kufanya hivyo watakuwa wamezingatia mafundisho yaliyotolewa katika sura ya hamsini na nane ya Isaya, na baraka iliyotangazwa hapo itakuwa yao.”—Shuhuda kwa Kanisa 6: 272.

“Tulihisi kwamba mafundisho ya Bwana katika Isaya 58 yalikuwa kwa ajili yetu, na kwamba baraka Zake zingekuja kwetu kwa njia ya kutii Neno Lake. Kila mtu anaweza kufanya kitu kwa ajili ya watoto wadogo walio wahitaji, kwa kuwasaidia kuwapatia makazi ambapo wanaweza kutunzwa.”—Welfare Ministry, 221.

“Nimeelekezwa kuwaelekeza watu wetu kwenye sura ya hamsini na nane ya Isaya. Soma sura hii kwa uangalifu/umakini sana, na uelewe aina ya huduma ambayo italeta uzima makanisani. Kazi ya injili inapaswa kubebwa kwa njia ya ukarimu wetu na pia kwa njia ya kazi zetu. Unapokutana na roho zinazohitaji msaada, zipe huo msada. Unapowapata wale walio na njaa, walishe. Katika kufanya hivyo utakuwa ukifanya kazi katika mistari ya huduma ya Kristo. Kazi takatifu ya Mwalimu ilikuwa kazi ya fadhili. Hebu watu wetu kila mahali wahimizwe kuwa na sehemu katika hilo.”— Manuscript 7, 1908.

“Sina hofu kuhusu watendakazi wanaoshiriki katika kazi iliyoonyeshwa katika sura ya hamsini na nane ya Isaya. Sura hii ipo wazi, na inatosha kumwangazia mtu yeyote anayetaka kufanya mapenzi ya Mungu. Kuna fursa tele kwa kila mtu kuwa baraka kwa wanadamu. Ujumbe wa malaika wa tatu hautapewa nafasi ya pili katika kazi hii, lakini unapasawa kuwa kitu kimoja na sura hii. Kunawezekana kuwa, na hakika kuna, hatari ya kuzika kanuni kubwa za Ukweli wakati wa kufanya kazi ambayo ni sahihi kufanya. Kazi hii inapaswa kuwa ujumbe kama ulivyo mkono kwa mwili. Mahitaji ya kiroho ya nafsi/roho yanapaswa kuwekwa wazi.”—Letter 24, 1898.

“Sura ya hamsini na nane ya Isaya ina Ukweli wa sasa kwa watu wa Mungu. Hapa tunaona jinsi kazi ya umishenari wa tiba na huduma ya injili zinavyopaswa kufungwa pamoja kama ujumbe unaotolewa kwa ulimwengu. Juu ya wale wanaoshika Sabato ya Bwana kuna jukumu la kufanya kazi ya rehema, ukarimu na fadhili. Kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kufungwa pamoja na ujumbe, na kugongwa muhuri kwa muhuri wa Mungu.”— Evangelism, 516-517.

“[Kristo alitangaza,] 'Imeandikwa, nyumba Yangu itaitwa nyumba ya sala, lakini nyinyi mmefanya kuwa pango la wezi.' Kisha Mrejeshaji alifanya kazi Yake ya umishenari wa tiba. Kipofu na kilema walikuja Kwake katika hekalu, Naye aliwaponya.' Maeneo ya soko, maduka ya bidhaa, huitaji utakaso. Mahakama za haki, ofisi ya wakili, taasisi za taaluma za tiba na vikundi vyenye kuipenda kazi hiyo, zinahitaji kutakaswa. Je, sisi tuanhitaji kusema kwamba kazi ya umishenari wa tiba inahitaji kusafishwa? Kristo, aliyekuja kwenye dunia yetu kuonyesha moyo wa Baba wa huruma, amebainisha mbinu ambayo Watunza Sabato wanapaswa kuifuata katika kazi zao. Hii imeelezwa kwa wazi katika sura ya hamsini na nane ya Isaya. Mungu hatakuwa mwanachama wa utendaji usio na uaminifu. Roho inayotunza Sabato imepigwa muhuri na ishara ya serikali ya Mungu, na mtu asiikosee heshima ishara hii. Kwa kujifunza Neno la Mungu kwa ukaribu, tutajua kama tuna alama ya Mfalme, kama tumechaguliwa na kutengwa kwa ajili ya kumheshimu Mungu.” – Medical Ministry, 123.

“Sura ya hamsini na nane ya Isaya ni maagizo ya tiba kwa magonjwa ya mwili na roho (Rx:Doctors prescriptions). Ikiwa tunatamani afya na furaha ya kweli ya maisha, ni lazima tuweke katika vitendo sheria zilizotolewa katika Andiko hili. Hapa Mungu anatuagiza juu ya utumishi unaokubalika Kwake, na baraka Zake ambazo huambatana nazo, Bwana asema: [MH 256.4]

“7 Je! Siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? Umwonapo mtu aliye uchi, umvike nguo; wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe?

8 Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara; na haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakufuata nyuma ukulinde.

9 Ndipo utaita, na Bwana ataitika; utalia, Naye atasema, Mimi hapa. Kama ukiiondoa nira; isiwepo kati yako, wala kunyosha kidole, wala kunena maovu;

10 na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri.

11 Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui.” [MH 256.5]

"Ikiwa wale wanaougua magonjwa wangejisahau wenyewe na kujali maslahi ya wengine; kama wangetekeleza agizo la Bwana la kuwahudumia wale walio wahitaji zaidi kuliko wao wenyewe, basi wangetambua Ukweli wa ahadi ya kinabii, “Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara.” Ministry of Healing, 256, 258 [MH 258.1]

“Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara; na haki yako itakutangulia; utukufu wa BWANA utakufuata nyuma ukulinde.

Ndipo utaita, na BWANA ataitika; utalia, Naye atasema, Mimi hapa. Kama ukiiondoa nira; isiwepo kati yako, wala kunyosha kidole, wala kunena maovu; na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri.

Naye BWANA atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui.” — Isaya 58:8-11.

“Hii ndiyo kazi maalumu iliyo mbele yetu sasa. Kuomba kwetu kote na kuacha kula au kujinyima, hakutasaidia chochote isipokuwa tutashikilia kwa uthabiti kazi hii. Wajibu mtakatifu uko juu yetu. Wajibu wetu umesemwa dhahiri. Bwana amesema nasi kupitia nabii Wake. Mawazo ya Bwana na njia Zake siyo yale watu wenye mwili unaokufa, vipofu, na wabinafsi wanavyoamini kuwa au wanavyotaka iwe. Bwana huangalia moyo. Ikiwa ubinafsi hukaa humo, Yeye Anajua. Tunaweza

kutafuta kuwaficha ndugu na dada zetu tabia zetu halisi, lakini Mungu anajua. Hakuna anachoweza kufichwa. Shuhuda kwa Kanisa 2: 34

“Mfungo ambao Mungu anaweza kuukubali umeelezwa. Ni kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa au kutelekezwa, ndani ya nyumba yako. Wewe usisubiri waje kwako. Kazi haiko juu yao kukutafuta/kukuwinda na kukusihi uwapatie mahali pa kukaa. Unapaswa kuwatafuta na kuwaleta katika nyumba yako. Lazima nafsi yako ivutwe kwao. Unao mkono mmoja wa kufikia juu na kwa imani shika mkono wenye uwezo/nguvu uletao wokovu, wakati kwa mkono mwingine wa upendo uwafikie walioonewa na kuwafariji.

"Ukishiriki katika kazi hii ya rehema na upendo, je, kazi hiyo itaonekana kuwa ngumu sana kwako? Je, utashindwa na kusetwa chini ya mzigo, na familia yako kunyimwa msaada na mvuto wako? Lo, hapana; Mungu ameondoa kwa uangalifu kabisa mashaka yote juu ya swali hili, kwa kuweka ahadi kwako kwa sharti la utii. Ahadi hii inajumuisha sana yote ambayo wenye shauku/kiu zaidi, wenye kusita zaidi, wanaweza kuyatamani. “Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara” Amini tu kwamba Yeye aliyeahidi ni Mwaminifu. Mungu anaweza kufanya upya nguvu za kimwili. Na zaidi, anasema atafanya. Na ahadi haikomei hapa. “Na haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakufuata nyuma ukulinde.” Mungu atajenga ngome kukuzunguka. Ahadi haishii hata hapa. “Ndipo utaita, na Bwana ataitika; utalia, Naye atasema, Mimi hapa.” Ikiwa utauacha uonevu na kuondoa maneno ya ubatili, ikiwa utamkunjulia nafsi yako mwenye njaa, “ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri. Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji au ukame, na kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui.'” —Shuhuda kwa Kanisa, 2: 33-35.

“Tunapaswa kuyaweka katika vitendo maagizo ya sheria, na hivyo kuwa na uadilifu/haki mbele yetu; thawabu itakuwa utukufu wa Mungu. Nuru ya haki ya Kristo itakuwa mlinzi wetu mbele, na utukufu wa Bwana utakuwa thawabu yetu. Hebu tumshukuru Bwana kwa uhakikisho huu. Hebu daima tusimame katika nafasi ambayo Bwana Mungu wa mbinguni anatupatia idhini.

Hebu tufikiri kwamba ni upendeleo mkuu kwetu, kuunganishwa na Mungu - kuwa mkono Wake wa msaada/kusaidia.” —Notebook Leaflets, Na. 23, ukurasa wa 1.

"Kumbuka ahadi iliyovuviwa ya nabii kwa wale ambao hufanya kwa nguvu zao kutuliza dhiki na msongo wa kimwili na kiroho [Isaya 58:8, imenukuliwa]. Kama

Wakristo tunapaswa kuwa na haki ambayo itaendelezwa na kuonekana haki inayowakilisha tabia ya Yesu Kristo alipokuwa katika ulimwengu wetu.” – Manuscript 43, 1908.

“Kwa wote wanaohudumia mahitaji ya wenye njaa na wanaoteswa au kuteseka, ahadi ni, 'Ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani.' Wengi wapo katika giza. Wamepoteza dira yao. Hawajui njia gani ya kufuata. Hebu walio na wasiwasi au tashwishwi watafute wengine walio katika wasiwasi au tashwishwi, na kuwaambia maneno ya matumaini na kutia moyo na faraja. Watakapoanza kufanya kazi hii, nuru ya mbinguni itawaonyesha njia wanayopaswa kuifuata. Kwa maneno yao ya faraja kwa watu watesekao, wao wenyewe watafarijiwa. Kwa kusaidia wengine, wao wenyewe watasaidiwa watoke katika matatizo yao.” — Manuscript 116, 1902.

“Kama waumini katika Kristo tunahitaji imani kubwa zaidi.

Tunahitaji kuwa na bidii zaidi katika maombi. Wengi wanashangaa kwa nini maombi yao hayana uhai yaani yamekufa, imani yao ni dhaifu sana na yenye kuyumba-yumba, uzoefu wao wa Kikristo wenye giza na usio na uhakika. Je! sisi si hatukufunga wanasema, na "kutembea kwa kuomboleza mbele ya Bwana wa majeshi?" Katika sura ya hamsini na nane ya Isaya (58) Kristo ameonyesha jinsi hali hii ya mambo inaweza kubadilishwa.

Yeye Anasema: "Je! hii si ndiyo saumu niliyoichagua? Kufungua vifungo vya uovu, na kulegeza Kamba za ubaya, na kuwaacha huru walioonewa, na kuvunja kila nira? Je! mwenye njaa, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako, umwonapo mtu aliye uchi, umfunike; wala usijifiche kutoka kwa ndugu/jamaa zako? Mistari ya 6, 7. Haya ndiyo maagizo ya utayarishaji ambayo Kristo ameyaagiza kwa ajili ya nafsi iliyokata tamaa, yenye mashaka, na inayotetemeka. Hebu wenye huzuni, waendao kwa kuomboleza mbele za Bwana, wainuke na kumsaidia mtu yule anayehitaji msaada. Shuhuda kwa Kanisa 6: 266.

“Kwa wale ambao wamejishughulisha na kazi hii ningesema: Endelea kufanya kazi kwa busara na uwezo. Wahimize washirika wako kufanya kazi chini ya jina fulani ambapo wanaweza kupangwa kushirikiana katika utendaji wenye upatanifu. Wafanye vijana wa kiume na wa kike makanisani wafanye kazi. Unganisha kazi ya umishonari ya matibabu na tangazo la ujumbe wa malaika watatu. Fanya juhudi za mara kwa mara, zilizopangwa ili kuwainua washiriki wa kanisa kutoka katika ngazi (hatua/hali) iliyokufa ambayo wamekuwa humo kwa miaka mingi. … Watu wa Mungu lazima watambue hitaji lao kuu na hatari, na kuchukua kazi iliyo karibu nao. Shuhuda kwa Kanisa 6: 266

“Kwa wale wamejishugulisha na kazi hii, wakizungumza maneno katika majira yake na pia nje ya majira/msimu, wakiwasaidia wenye uhitaji, wakiwaambia juu ya upendo wa ajabu wa Kristo kwao, Mwokozi daima Yupo kugusa mioyo ya maskini na wenye huzuni na wanyonge. Kanisa linapokubali kazi yake iliyopewa na Mungu, ahadi ni hii: “Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara; na haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakufuata nyuma." Kristo Ndiye haki yetu; Yeye Anatutangulia katika kazi hii, na utukufu wa Bwana unafuata. Shuhuda kwa Kanisa 2: 267

“Yote yaliyopo mbinguni yanangoja mwitikio na mipango inayohitaji kukamilishwa kwa kila nafsi itakayofanya kazi katika mistari ya Kristo. Washiriki wa makanisa yetu mmoja mmoja wanapochukua kazi waliyoteuliwa kuifanya, watakuwa wamezungukwa na anga hewa tofauti kabisa. Baraka na nguvu zitahudhuria kazi zao. Watapata maendeleo na utamaduni wa juu wa akili na moyo. Ubinafsi ambao umezifunga nafsi zao utashindwa. Imani yao itakuwa kanuni hai. Maombi yao yatakuwa ya dhati zaidi. Ushawishi wa kuhuisha na utakaso wa Roho Mtakatifu utamiminwa juu yao, nao wataletwa karibu na ufalme wa mbinguni.” —Shuhuda kwa Kanisa, 6: 266-268.

NNE, TOA UJUMBE WA MWISHO AMBAO ULIMWENGU UNAUHITAJI ZAIDI

“Na watu wako watapajenga mahali palipokuwa ukiwa; utaiinua misingi ya vizazi vingi; nawe utaitwa, Mwenye kutengeneza mahali palipobomoka; na, Mwenye kurejeza njia za kukalia. Kama ukigeuza mguu wako usihalifu Sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu Wangu; ukiita Sabato siku ya furaha, na siku takatifu ya BWANA yenye heshima; ukiitukuza, kwa kutokuzifanya njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe; ndipo utakapojifurahisha katika BWANA; Nami nitakupandisha mahali pa nchi palipoinuka; nitakulisha urithi wa Yakobo baba yako; kwa maana kinywa cha BWANA kimenena hayo.” —Isaya 58:12- 14.

"Hapa zimetolewa sifa ya watu watakao kuwa wana matengenezo, watakaobeba bendera ya ujumbe wa malaika wa tatu, wale watu wenye kushika amri za Mungu, wanaomheshimu Mungu na kwa uaminifu wanajihusisha, katika mwonekano wote wa sayari zote katika kujenga mahali pa zamani palipokuwa ukiwa. Ni nani anayewaita, Mwenye kutengeneza palipobomoka; na, Mwenye kurejeza njia za kukalia? Ni Mungu. Majina yao yameandikishwa mbinguni kama wanamatengenezo, warejeshaji, kwa kuwa wanainua misingi ya vizazi vingi.” — Review, Oktoba 13, 1891.

“Kadiri mwisho unavyokaribia, shuhuda za watumishi wa Mungu zitakuwa zenye kuazimiwa zaidi na zaidi na kwa nguvu zaidi, zikiangaza mwanga wa Ukweli juu ya mifumo ya makosa na ukandamizaji ambayo imeshikilia hatamu kwa muda mrefu. Bwana ametuma ujumbe kwa wakati huu, kuanzisha Ukristo juu ya msingi wa umilele; na wote wanaoamini Ukweli wa sasa lazima wasimame, si katika hekima yao bali katika Mungu, na kuinua msingi wa vizazi vingi. Hawa watasajiliwa katika vitabu vya mbinguni kama wenye kutengeneza palipobomoka, warejeshaji ya njia za kukalia. Tunapaswa kudumisha Kweli kwa sababu tu hiyo ni Kweli, katika uso wa upinzani mkali na mchungu zaidi. Mungu Yuko kazini juu ya akili za binadamu; si mtu pekee afanyae kazi. Nguvu kubwa inayotia nuru hutoka kwa Kristo; mfano Wake ung’aao unapaswa kupokelewa mbele ya watu.” —Letter 1f, 1890.

“Kazi iliyoanishwa katika maneno haya [Isaya 58] ni kazi ambayo Mungu Mwenyewe amewapa watu Wake waifanye. Ni kazi ya uteule wa Mungu Mwenyewe. Pamoja na kazi ya kutetea amri za Mungu na kutengeneza palipobomoka katika sheria ya Mungu, tunapaswa kuchanganya huruma kwa mateso ya kibinadamu. Tunapaswa kuonyesha upendo mkuu na usiogawanyika kwa Mungu; tuinue ukumbusho Wake ambao umekanyagwa chini na miguu isiyo mitakatifu: na kwa hii tunadhihirisha upole, wema, na huruma inayohitajika zaidi kwa jamii ilyoanguka. 'Nawe mpende jirani yako kama nafsi yako.' Kama watu tunapaswa kushikilia hii kazi. Upendo ulioonyeshwa kwa binadamu aliye kwenye mateso hutoa umuhimu na nguvu wa Kweli.” —Special Testimonies, Series A, Na. 10, ukurasa wa 3- 4.

“Siwezi kuwasisitiza na kusihi kwa uzito wa kutosha washiriki wote wa kanisa letu kuliko hivi, wale wote ambao ni wamishenari wa Kweli, wote wanaoamini ujumbe wa malaika wa Tatu, wote wanaoigeuza miguu yao kutoka kwenye Sabato, wanapaswa kuzingatia ujumbe wa sura ya hamsini na nane ya Isaya. Kazi ya rehema iliyoamriwa katika sura hii ni kazi ambayo Mungu anahitaji watu Wake waifanye kwa wakati huu. Ni kazi aliyoiweka Yeye Mwenyewe. Nasi hatujaachwa katika shaka juu ya mahali ambapo ujumbe huo unahusu au kuingia, na wakati wa utimizo wake uliowekwa alama, kwa kuwa twasoma hivi: “Nao wa kwako watapajenga mahali pa kale palipoharibiwa na penye ukiwa; utaitwa, mwenye kutengeneza mahali palipobomoka, Mwenye kurejeza njia za kukalia." Mstari wa 12. Kumbukizi/kumbukumbu ya Mungu, Sabato ya siku ya saba, ishara ya kazi Yake katika kuumba ulimwengu, imehamishwa mahali pasipokuwa pake na mtu wa dhambi. Watu wa Mungu wana kazi maalum ya kufanya katika kutengeneza mbomoko/mvunjiko ambao umefanywa katika sheria Yake; na kadiri

tunavyokaribia mwisho, ndivyo kazi hii inavyokuwa ya dharura na nyeti zaidi. Wote wanaompenda Mungu wataonyesha kwamba wanabeba ishara Yake kwa kushika amri Zake. Hao ndio warejeshaji wa njia za kukaa ndani. Bwana asema hivi: “Kama ukigeuza mguu wako usiiache Sabato, usifanye anasa yako katika siku Yangu takatifu, na kuiita Sabato siku ya furaha; . . . ndipo utakapojifurahisha katika Bwana; Nami nitakupandisha mahali palipoinuka duniani.” Mistari 13, 14. Hivyo kazi ya umishenari wa Kweli wa tiba inafungamanishwa na kushika amri za Mungu bila kutenganishwa, ambapo Sabato inatajwa kwa njia mahususi, kwa kuwa ndiyo iliyo kuu. ukumbusho wa kazi ya uumbaji ya Mungu. Utunzaji Wake unafungamanishwa na kazi ya kurudisha sura ya kimaadili ya Mungu ndani ya mwanadamu. Hii ndiyo huduma ambayo watu wa Mungu wanapaswa kuendeleza wakati huu. Huduma hii ikifanywa kwa usahihi upasao, italeta baraka tele kwa kanisa.” –Shuhuda kwa Kanisa, 6: 265-266.

“Katika sura ya hamsini na nane ya Isaya imeainishwa kazi ambayo watu wa Mungu wanapaswa kufanya. Wanapaswa kukuza sheria na kufanya iwe ya kuheshimika, kwa kujenga mahali pa palipochakaa na penye ukiwa, na kuinua misingi ya vizazi vingi. Wote wafanyao kazi hii, Mungu asema [Isaya 58:12-14, iliyonukuliwa]

“Suala la Sabato litakuwa hoja mtambuka au chanzo katika pambano kuu la mwisho ambalo ulimwengu wote utatenda sehemu. Wanadamu wameheshimu kanuni za Shetani kuliko kanuni zinazotawala mbinguni. Wameikubali sabato ya uwongo, ambayo Shetani ameitukuza kama ishara ya mamlaka yake. Lakini Mungu ameweka muhuri Wake juu ya matakwa/mahitaji Yake ya kifalme. Kila taasisi ya Sabato inabeba jina la mwandishi Wake, alama isiyofutika ambayo inaonyesha mamlaka ya kila taasisi. Ni kazi yetu kuwaongoza watu kulielewa hili. Tunapaswa kuwaonyesha kwamba ni matokeo muhimu kama wana alama ya ufalme wa Mungu au alama ya ufalme wa uasi, kwa kuwa wanajikubali kuwa raia wa ufalme ambao alama yao wanayo. Mungu ametuita sisi kuinua kiwango cha Sabato Yake iliyokandamizwa. Ni muhimu jinsi gani, basi, kwamba mfano wetu katika kushika Sabato uwe sahihi." —Shuhuda kwa Kanisa, 6: 352-353.

“Wengi kanisani wanawasilishwa kwangu kama watu wanaoonekana kama miti inayotembea. Wanapaswa kuwa na mwingine na uzoefu wa kina zaidi kabla ya kutambua mitego iliyotandazwa katika nyavu za yule mdanganyifu. Hakupaswi kuwepo na nusu ya kazi iliyofanywa kwa sasa. Bwana anawaita wanawume na wanawake walioongoka imara, wenye kuwajibika, waadilifu wenye kuazimia, kusimama kwenye pengo, na kutengeneza wigo [Isaya 58:12-14, iliyonukuliwa].

“Kuna ushuhuda ulioazimiwa unaotakiwa kubebwa na wahudumu wote katika makanisa yetu yote. Mungu ameruhusu ukengeufu kutokea ili kuonyesha jinsi tegemeo letu kwa mwanadamu linavyoweza kuwekwa kwa udogo. Tunapaswa kumwangalia Mungu siku zote; kazi Yake haipaswi kuwa sivyo ndio na la, bali NDIO na AMINA.” —Notebook Leaflets, Na. 19, ukurasa wa 2-3.

“Muungano unaopaswa kuwepo kati ya kazi ya umishenari wa tiba na huduma umewekwa wazi katika sura ya hamsini na ya Isaya. Kuna hekima na baraka kwa wote watakaoshiriki katika kazi iliyowasilishwa. Hii sura iko wazi, na ndani yake kunatosha kuangaza kwa yeyote anaetaka kufanya mapenzi ya Mungu. Inatoa fursa tele kutoa huduma kwa binadamu anayeteseka na wakati huo huo kuwa chombo katika mikono ya Mungu cha kuleta nuru ya Kweli mbele ya dunia inayoangamia. Kama kazi ya ujumbe wa malaika wa tatu ikibebwa katika namna iliyo sahihi, huduma haitapewa nafasi iliyo dhaifu wala maskini na wagonjwa hawatapuuzwa. Katika Neno Lake, Mungu ameiunganisha mistari miwili ya kazi, na hapana mtu atakayevitenganisha hivi viwili.” - Counsels on Health, 514-515.

“Je, ni wapi tunapata watu wanaotakiwa? Ni nani atakayejenga mahali pa zamani palipokuwa ukiwa, na kuinua misingi ya vizazi vingi? Wapi kuna watu wenye nuru kutoka mbinguni kuona uvunjaji umefanyika katika sheria ya Mungu?

“Katika Ufunuo, Yohana anasema, 'hekalu la Mungu lililoko mbinguni likafunguliwa, na Sanduku la Agano likaonekana ndani ya hekalu Lake (Ufunuo. 11:19). Yohana aliona katika maono watu wa Bwana wakingojea kwa hamu kuja Kwake Bwana na kutafuta Ukweli. Hekalu la Mungu lilipofunguliwa kwa watu Wake, nuru ya sheria ya Mungu, ambayo ilikuwa katika Sanduku la Agano, iling'aa. Wale wanaoipokea nuru hii wanapewa nuru ya kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu.

“Malaika huyu alionekana akipaa katikati ya mbingu, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake..... Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu.

“Hawa ni watu wafanyao matengenezo ya uvunjaji wa sheria ya Mungu. Wanaona kwamba Sabato ya amri ya nne imewekewa mbadala wa sabato bandia, siku ambayo haina utakaso katika Neno la Mungu. Katikati ya upinzani mkubwa wanakuwa waaminifu kwa Mungu wao, na kuchukua nafasi chini ya bendera ya malaika wa tatu.” — Manuscript 48, 1900.

“Sura ya hamsini na nane ya Isaya ina kweli ya sasa kwa watu wa Mungu. Hapa tunaona jinsi kazi ya umishenari wa tiba na huduma ya injili zimefungwa pamoja kama ujumbe uliotolewa kwa Dunia. Juu ya hao waitunzao Sabato ya Bwana limewekwa jukumu la kufanya kazi ya rehema na wema. Kazi ya umishenari wa tiba inapaswa ifungamanishwe na ujumbe, na kugongwa muhuri kwa mhuri wa Mungu.” — Evangelism, 516-517.

SURA YA 3

WAKATI UJAO WA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA

MWONGOZO KWA AJILI YA KUIMALIZA KAZI

1. MUNGU ANAISUBIRI IINULIWE JUU

HAKUNA MABADILIKO KATIKA UJUMBE—“Hakuna mabadiliko katika ujumbe ambao Mungu alituma awali. Kazi katika miji ni kazi muhimu kwa wakati huu. Kama miji ingefanyiwa kazi kama Mungu apendavyo, matokeo yatakuwa operesheni yenye utendaji wenye harakati kubwa ambalo hatujalishuhudia bado.” – Medical Ministry, 304.

KILA MATENGENEZO YA KWELI YANA NAFASI YAKE —“Kila matengenezo ya kweli yana nafasi yake katika kazi ya ujumbe wa malaika wa tatu. Haswa haya Matengenezo ya kiasi, huhitaji umakini na msaada wetu." -Counsels on Health, 433.

KUTAZAMIA MAREJEO YAKE BWANA HIVI KARIBUNI—“Watunza Sabato wanaotazamia marejeo ya Mwokozi wao yaliyo karibu wanapaswa wasiwe watu wa mwisho kuwa na shauku katika kazi hii kubwa ya matengenezo. Ni lazima wanaume na wanawake waelekezwe, na wachungaji na washiriki wahisi kuwa uzito wa kazi upo juu yao kuchochea jambo hili na kulipeleka katika nyumba za wengine.” – Shuhuda kwa Kanisa, 1: 489.

KAZI ILIYOPUUZWA MUDA MREFU: WITO WA MWISHO KWENYE KARAMU—Tena na tena Bwana ameonesha kazi ambayo kanisa huko Battle Creek na mengine

yote yaliopo kote Marekani yanapaswa kufanya. Watu wanapaswa kufikia kiwango cha juu zaidi katika maendeleo ya kiroho kuliko vile walivyofikia. Wanapaswa kuamka kutoka kwenye usingizi na kwenda nje ya kambi, wakifanya kazi kwa ajili ya roho zilizo karibu kuangamia. Watendakazi wa umishenari wa tiba wanafanya kazi ambayo imepuuzwa kwa muda mrefu ambayo Mungu alitoa kwa kanisa" —Shuhuda kwa Kanisa 8: 70-71.

KAZI PEKEE AMBAYO PUNDE ITAFANYIKA (UPESI)—"Moyo wangu unahuzunika ninapotazama makanisa yetu, ambayo yanapaswa kushikamana katika moyo na nafsi na kufanyia mazoezi kazi ya umishenari wa tiba. Ningependa kukuambia kwamba hivi karibuni hakutakuwa na kazi itakayofanywa katika nyanja za huduma isipokuwa kazi ya umishenari wa tiba." - Counsels on Health, 533.

KWA NINI BADO IPO KATIKA UCHANGA WAKE—"Kazi ya umishenari wa tiba bado iko katika uchanga wake. Maana ya kweli ya kazi ya umishenari wa tiba inajulikana na wachache tu. Kwa nini?— Kwa sababu mpango wa Mwokozi wa kazi haujafuatwa. Pesa ya Mungu imetumika vibaya." – A Call to Medical Evangelism 10.

ALAMA MPYA INAYOHITAJIKA—"Kipengele kipya kinahitajika kuletwa katika kazi. Watu wa Mungu lazima wapokea onyo, na kutumika kwa ajiliya roho roho mahali sahihi walipo . . Kama Yeye (Kristo) alivyokwenda kutoka mahali hata mahali, akibariki na kufariji wenye mateso na kuwaponya wagonjwa. Sababu ambayo Bwana hajaamua kuonyesha nguvu Yake zaidi ni kwa sababu kuna hali ya chini ya kiroho miongoni mwa wale wanaodai kuamini Kweli." – Medical Ministry, 319.

KAZI YA KUFANYA—"Kuna kazi ya kufanywa kwa makanisa yetu ambayo ni wachache tu wanaitambua au kuifikiria. 'Mimi nilikuwa na njaa,' Kristo anasema, kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi mkanivika, nalikuwa mgonjwa mkaja kuniona……. Mathayo 25:35... Kuna kazi ambayo bado haijaguswa ambayo lazima ifanyike. Utume wa Kristo ulikuwa ni "kumponya mgonjwa, kumtia moyo asiye na matumaini, kuponya, kufariji, na kurejesha watu waliovunjika moyo." Hii kazi ya urejeshaji inapaswa kuendelezwa mbele." – A Call to Medical Evangelism, 22-23.

WENGI WATAKUWA WAKISUBIRI — "Nilioneshwa watu wa Mungu wakisubiri mabadiliko yatokee - nguvu zinazoleta umakini ziwawashikilie. Lakini watakatishwa tamaa, kwani wamekosea. Lazima wachukue hatua, lazima washike kazi hiyo wenyewe kwa dhati na Wamlilie Mungu kwa bidii ili kupata maarifa ya Kweli juu yao. Matukio ambayo yanapita mbele yetu yana ukubwa wa

kutosha kutusababisha kuamka na kusisitiza Ukweli nyumbani mwa mioyo ya wote watakaosikiliza. Mavuno ya dunia yamekaribia kuiva." —Shuhuda kwa Kanisa 1: 261.

MTU MMOJA LAZIMA ATIMIZE UTUME—"Kwa nini haijaeleweka kutoka katika Neno la Mungu kwamba kazi inayofanyika kupitia nyanja za umishenari wa tiba ni utimilifu wa Maandiko. [Luke 14:21-23, Yule mtumwa akaenda, akampa bwana wake habari ya mambo hayo. Basi, yule mwenye nyumba akakasirika, akamwambia mtumwa wake, Toka upesi, uende katika njia kuu na vichochoro vya mji, ukawalete hapa maskini, na vilema, na vipofu, na viwete. Mtumwa akasema, Bwana, hayo uliyoagiza yamekwisha tendeka, na hata sasa ingaliko nafasi. Bwana akamwambia mtumwa, Toka nje uende barabarani na mipakani, ukawashurutishe kuingia ndani, nyumba yangu ipate kujaa. Hii ni kazi ambayo makanisa katika kila eneo, kaskazini na kusini na mashariki na magharibi, yanapaswa kufanya. Makanisa yamepewa fursa ya kujibu kazi hii. Je, ni kwa nini hawajafanya? Mtu fulani anapaswa kutimiza huu utume." - Review and Herald, Mei 25, 1897.

SASA NI MUDA WAKE KUFANYIKA — "Tumefika wakati ambapo kila mshiriki wa kanisa anapaswa kuchukua kazi ya umishenari wa tiba. Ulimwengu ni nyumba ya wakoma wa dhambi iliyojaa waathirika wa magonjwa ya kimwili na ya kiroho (Lazer House). Kila mahali watu wanaangamia kwa kukosa maarifa ya Ukweli ambayo tumepewa. Washiriki wa kanisa wanahitaji kuwa na mwamko, ili waweze kutambua jukumu lao la kutoa Ukweli huu." -Shuhuda kwa Kanisa 7: 62.

ITAFANYIKA — "Tunapaswa kuyahisi mambo haya kwa kina, kwa kuwa ni ya kweli. Tunapaswa kuwa na makadirio ya juu ya Ukweli na pia thamani ya roho. Muda ni mfupi, na kuna kazi kubwa ya kufanywa. Ikiwa hujisikii shauku kwa ajili ya kazi inayoendelea mbele, ikiwa hutaunga mkono kazi ya umishenari wa tiba katika makanisa, basi kazi hii itafanywa bila kibali chako; kwani ni kazi ya Mungu, na ni lazima ifanyike. Ndugu na dada zangu, chukueni msimamo wenu upande wa Bwana na muwe wafanyakazi wenye ari, wenye bidii, watenda kazi wenza jasiri pamoja na Kristo, mkifanya kazi pamoja Naye kutafuta na kuwaokoa watu waliopotea." -Shuhuda kwa Kanisa 8: 75.

MAWAKALA NA TAASISI ZITAINULIWA JUU—"Hivyo anasema Bwana: 'Majengo yataonyesha maudhui kwa kazi Yangu pekee pale tu wanaoyajenga watafuata maelekezo Yangu katika kuanzishwa kwa taasisi. Endapo wote waliozitunza na kuendeleza kazi siku za nyuma wangedhibitiwa kwa usafi, kanuni zisizo na ubinafsi, kamwe kusingelikuwa na watu wajikusanyiao hisa kubwa za mali kwa

ubinafsi katika eneo moja au mawili. Taasisi zingelisimamishwa mahali nyingi zingine. Mbegu za Kweli, zilizopandwa katika mashamba mengi, zingekuwa zimechipuka juu na kubeba matunda kwa utukufu Wangu. Maeneo yaliyopuuzwa sasa yanapaswa kupokea umakini. Watu Wangu kufanya kazi kwa kasi na haraka. Wale wote walio na dhamira safi wakijiweka wakfu kikamilifu Kwangu, mwili, nafsi, na roho zitafanya kazi katika njia Yangu na Jina Langu. Kila mtu atasimama katika kura yake, akiniangalia Mimi, kiongozi, na Mwongozo wake na Mshauri. Nitawafundisha wajinga, na kuwapaka dawa ya macho ya mbinguni wengi ambao sasa wako katika giza la kiroho. Nitawasimamisha mawakala ambao watabeba mapenzi Yangu kuwaandaa watu kusimama mbele Yangu wakati wa mwisho. Katika maeneo mengi ambapo hayapata bado vituo vya afya (sanitariums) na shule, nitasimamisha taasisi Zangu, na taasisi hizi zitakuwa vituo vya mafunzo ili kufundisha watendakazi.” —Counsels on Health, 226-227.

KUJENGA TABIA - "Hebu asiwepo yeyote mwenye kufikiri kwamba aweza kufanya kama atakavyo katika suala la lishe. Lakini kabla ya wote wanaoketi mezani pamoja nawe, hebu ionekane kwamba unafuata kanuni katika suala la ulaji, kama ilivyo katika mambo mengine yote, ili utukufu wa Mungu uweze kudhihirishwa. Huwezi ukamudu kufanya vingenevyo; kwani una tabia ya kujenga kwa ajili ya maisha milele.” -Counsels on Diet and Foods, 34.

KARIBU NA KUJARIBU ZAIDI—“Malaika alisema “Ziepukeni tamaa za mwili zipinganazo na roho.” Umejikwaa kwenye matengenezo ya afya. Inaonekana kwako kuwa kiambatanisho kisicho na maana kwenye Ukweli. Si hivyo; ni sehemu ya Ukweli. Hapa kuna kazi mbele yako ambayo itakuja kwa karibu sana na kuwa yenye kujaribu zaidi ya chochote ambacho kimewahi kuletwa kwako ukibebe. Wakati usitapo na kurudi nyuma, ukishindwa kushikilia mibaraka ambayo ni haki yako kuupokea, utateseka kwa hasara. Unajikwaa juu ya mbaraka ambao mbingu imeuweka katika njia yako ili kufanya maendeleo yawe yasiwe na ugumu sana.” -Counsels on Diet and Foods, 39.

HAWEZI KUWATEGEMEZA WATUMISHI WAKE KATIKA DHAMBI—“Bwana ametoa ujumbe kwa watu Wake kuhusu matengenezo ya afya. Nuru hii imekuwa ikimulika katika njia yao kwa miaka thelathini; na Bwana hawezi kuendelea kuwategemeza watumishi Wake katika njia ambayo inapingana au kuzuia. Yeye Yeye huchukizwa wakati watumishi Wake wanapotenda kinyume na ujumbe juu ya kipengele hiki, ambacho amewapatia kukitoa kwa wengine. Je, Yeye anaweza kupendezwa pale ambapo ni nusu tu ya watendakazi wanaofanya kazi mahali fulani, wanafundisha kwamba kanuni za afya zimeunganishwa kwa ukaribu sana

na ujumbe wa Malaika yule wa tatu kama vile mkono ulivyounganishwa na mwili, wakati watendakazi wenzao, kwa matendo yao, wanafundisha kanuni zilizo kinyume kabisa? Hii inachukuliwa kama dhambi machoni pa Mungu…" -Counsels on Diet and Foods, 38.

KUTOKUWA NA STAHIKI KUMALIZA KAZI—"Utumiaji mbaya wa nguvu zetu za mwili hupunguza kipindi cha muda katika maisha yetu ambacho kingeweza kutumika katika kumtukuza Mungu. Na hutufanya tusifae kufanikisha kazi ambayo Mungu ametupatia kuifanya. -Christ Object Lessons, 346, 1900. CD 49.1." -Councils on Diet and Foods, 49.

HAITAWEZEKANA KUMTUKUZA MUNGU—"Haiwezekani kumtukuza Mungu huku tukiishi katika uvunjaji wa sheria za uzima. Moyo hauwezi kudumisha utakaso kwa Mungu endapo uchu wa tamaa ya kula unaendekezwa." -Counsels on Diet and Foods, 44.

UTAKASO NA UKAMILIFU HAVIWEZEKANI—"Mwili uliosheheni magonjwa pamoja na akili iliyovurugika, kwa sababu ya kuendelea kuendekeza tamaa zenye kuumiza, hufanya utakaso wa mwili na roho ushindikane. Mtume alielewa umuhimu wa masharti ya afya ya kimwili kwa ajili ya kufanikisha ukamilifu wa tabia ya Kikristo." -Counsels on Diet and Foods, 44.

2. ITATIKISA NA KU TAKASA KANISA KWA WOKOVU WETU NA WOKOVU WA ULIMWENGU

"Nuru ambayo Mungu aameitoa juu ya matengenezo ya afya ni kwa ajili ya wokovu wetu na wokovu wa dunia. Wanaume na wanawake wanapaswa kujulishwa kuhusiana na makao yetu ya kibinadamu-(miili yetu), yaliyowekwa na Muumba wetu kama makao Yake, na ambayo Yeye anatamani tuwe mawakili waaminifu kwayo. 'Kwa maana sisi tu hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema, ya kwamba Nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, Nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa Watu Wangu." —Welfare Ministry, 130-131.

KUPUNGUZA MATESO NA KUTAKASA WATU WAKE —"Tumepewa kazi ya kuendeleza matengenezo ya afya. Bwana anatamani watu Wake wapatane miongoni mwao wenyewe. Kama unavyopaswa kujua, hatutaacha nafasi ambazo, kwa miaka thelathini na mitano iliyopita, Bwana amekuwa akituamuru kusimama. Jihadhari na jinsi unavyojiweka katika upinzani dhidi ya kazi ya matengenezo ya afya. Kazi hii itasonga mbele; kwa maana ni njia ya Bwana kupunguza mateso katika dunia yetu, na ya kuwatakasa watu Wake." – Medical Ministry, 279.

KUPUNGUZA MATESO NA KUTAKASA KANISA LAKE –“Kazi ya matengenezo ya afya ni njia ya Bwana kupunguza mateso katika ulimwengu wetu na kulitakasa kanisa Lake. Wafundishe watu kwamba wanaweza kutenda kama mkono wa wa Mungu wa kusaidia kwa kushirikiana na Mwalimu mkuu katika kurejesha afya ya kimwili na kiroho.” —Shuhuda kwa Kanisa, 9: 112-113.

KURUDI NYUMA KUMELETA UKOSEFU MKUBWA -“Kushindwa kufuata kanuni sahihi kumeharibu historia ya watu wa Mungu. Kumekuweko na kurudi nyuma kwa mfululizo katika matengenezo ya afya, na matokeo yake, Mungu ameaibishwa kwa ukosefu mkubwa wa nguvu za kiroho. Vizuizi vimewekwa ambavyo visingeonekana kamwe, endapo watu wa Mungu wangetembea katika nuru.” -Counsels on Diet and Foods, 33.

KUREJESHA EDENI – "Kama wazazi wetu wa kwanza walivyopoteza Edeni kupitia uendekezaji wa uchu wa cjali;a, tumaini letu pekee la kurejesha Edeni ni kupitia ukanaji thabiti wa ulafi na tamaa." -Counsels on Diet and Foods, 59.

KAMA WAMESHINDA KATIKA HATUA HII –"Nguvu ya ulafi wa chakula inayotawala italeta uharibifu kwa maelfu ya watu, wakati ambapo, kama wangelipata ushindi katika hili, wangelipata nguvu ya kimaadili ambayo ingeliwafanya kuwa washindi katika kila jaribu la Shetani. Lakini wale ambao ni watumwa wa hamu ya chakula watashindwa kuwa wakamilifu katika kuwa na tabia ya Kikristo. Uasi endelevu wa mwanadamu kwa miaka elfu sita umeleta ugonjwa, maumivu, na kifo kama matunda yake. Na kwa kadiri tunavyokaribia mwisho wa wakati, jaribu la Shetani la kuendekeza uchu wa chakula, litakuwa na nguvu kubwa zaidi na gumu zaidi kulishinda." 3T 491.3 -Counsels on Diet and Foods, 59.

HAIWEZEKANI — “Haiwezekani kwa kwa wale wanaojitoa kuongozwa na uchu kufikia ukamilifu ya Ukristo.” -Counsels on Diet and Foods, 236.

ILI KUFAA KWA AJILI YA KUBADILISHWA—“Ili kufaa kwa ajili ya kunyakuliwa kwenda mbinguni, watu wa Mungu ni lazima wajitambue wenyewe. Ni lazima wajielewe katika muonekano wa maumbo yao ili waweze kushangilia pamoja na mtunga Zaburi “Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa kwa jinsi ya ajabu ya kutisha.” Wanapaswa kuwa na matamanio ya kutiisha maadili na viungo vya akili. Mwili wapaswa kutawaliwa na akili na siyo akili kutawaliwa na mwili.” -Counsels on Diet and Foods, 33.

KUFAA KWA AJILI YA KUTOKUFA—“Basi wanadamu, wanaweza kuifanya miili yao kutokuwa mitakatifu kwa kuendekeza dhambi. Kama si watakatifu, hawafai kuwa waabudu wa kiroho, wala hawana thamani yoyote kwa mbingu. Kama

mwanadamu atathamini nuru ambayo Mungu Amempatia kwa rehema juu ya matengenezo ya afya, anaweza kutakaswa kupitia Ukweli, na kufanywa kufaa kwa ajili ya kutokufa." -Counsels on Diet and Foods, 70.

KUSAFISHWA AU KUTAKASWA: STAHIKI KUHUSIKA KATIKA KILIO KIKUU—"Mungu anawataka watu Wake kujitakasa na uchafu wote wa mwili na roho, wakikamilisha utakatifu katika kumcha Bwana. Wale wote ambao hawajali na wanajiondoa katika kazi hii, wakimngojea Bwana awafanyie yale ambayo Yeye anataka wayafanye wao wenyewe, watakutwa wamepungua. Burudiko au nguvu ya Mungu huja tu kwa wale ambao wamejiandaa kwa ajili yake kwa kufanya kazi ambayo Mungu anawaamuru, ambayo ni, kujitakasa na uchafu wote wa mwili na roho, wakikamilisha utakatifu katika kumcha Mungu." -Counsels on Diet and Foods, 33.

MAANDALIZI KWA AJILI YA KILIO KIKUU—"Nilionyeshwa kwamba kazi ya matengenezo ya afya ni kana kwamba haijaanza hata kutekelezwa bado. Wakati baadhi wakihisi kwa kina, na kuiweka kwenye vitendo imani yao, wengine hubaki kutojali na kwa uchache sana wamechukua hatua ya kwanza kwenye matengenezo. Ndani yao kuna kutokuamini, na kadiri matengenezo haya yanavyozidi kupinga tamaa mbaya ya ulaji, wengi hurudi nyuma. Wana miungu mingine badala ya Bwana. Ladha na ulafi wao ni mungu wao. . [Watu wa Mungu] Wanayo kazi ya kufanya kwa ajili yao wenyewe ambayo hiyo hawapaswi kuiacha kwa kudhani kuwa Mungu afanye kwa ajili yao. Ameiacha kazi hii ili wao waifanye. Ni kazi ya mtu binafsi; mtu hawezi kufanya kwa ajili ya mwingine." -Counsels on Health, 453.

JARIBIO KUBWA LA MWISHO—"Ukweli wa wakati huu, ujumbe wa Malaika wa tatu, utatangazwa kwa kilio kikuu, tunapokaribia jaribio kubwa la mwisho. Jaribio hili lazima lije kwa makanisa kuhusiana na kazi ya ya Kweli ya umishenari wa tiba, kazi ambayo ndani yake kuna Tabibu Mkuu Mwenye kuamua na kuongoza katika yote inayohusisha." -Manuscript dated 1900; Loma Linda Messages, 62.

UDANGANYIFU WA MWISHO WA SHETANI - "Mwisho unapokaribia na kazi ya kutoa onyo la mwisho kwa ulimwengu inapoenea, inakuwa muhimu zaidi kwa wale wanaoukubali Ukweli wa sasa kuwa na ufahamu wazi wa asili/maudhui na ushawishi wa Shuhuda, ambazo Mungu katika majaliwa Yake ameziunganisha na kazi ya ujumbe wa malaika wa tatu tangu kutokea zilipoanza." – Shuhuda kwa Kanisa 5: 654.

"Mkipoteza usadikisho/imani katika Shuhuda mtakengeuka kutoka kwenye Ukweli wa Biblia. Nimekuwa na hofu kwamba wengi wangechukua msimamo wa maswali

au hoja moyoni, na kuwa wenye mashaka, na katika taabu yangu kwa ajili ya nafsi zenu ningewaonya. Ni wangapi watatii onyo hilo? Sasa mnapozishikilia Shuhuda mikononi mwenu, Je, pale shauri moja la shuhuda linakatiza njia zako, likisahihisha makosa yako binafsi, je, ungejisikia kuwa na uhuru kamili wa kukubali au kukataa sehemu yoyote ya Shuhuda au Shuhuda yote nzima? Kile ambacho utakuwa na mwelekeo mdogo kukipokea ndicho sehemu inayohitajika zaidi katika maisha yako" – Shuhuda kwa Kanisa 5: 98.

"Shetani ni . . daima hushinikiza kilicho bandia au udanganyifu kuongoza watu mbali na Ukweli. Udanganyifu wa mwisho kabisa wa Shetani utakuwa kufanya Shuhuda za Roho wa Mungu zisilete matokeo au zisiwe na athari. 'Pasipo maono, watu huacha kujizuia (huangamia)…. (Mithali 29:18). Shetani atafanya kazi kwa akili, katika njia tofauti na kupitia mawakala tofauti, ili kuyumbisha imani ya masalia wa Mungu katika Shuhuda wa Kweli." —2 Selected Messages, 78.

WEKA MLANGO WAZI KWA AJILI YA ULIMWENGU, UFUNGE KWA WALE WOTE AMBAO HAWATAKI KUINGIA—"Ah! Laiti watu wangelijua majira ya kujiliwa kwao! Kuna wengi ambao bado hawajaisikia ile Kweli ipimayo kwa wakati huu. Kuna wengi ambao Roho wa Mungu anashindana nao. Wakati wa hukumu za Mungu za uharibifu ni wakati wa rehema kwa wale ambao hawakuwa na nafasi ya kujifunza ni nini iliyo Kweli. Bwana atawatazama kwa upendo na upole. Moyo Wake wa rehema umeguswa; Mkono Wake bado umenyooshwa ili kuokoa, wakati mlango ukiwa umefungwa kwa wale ambao hawakutaka kuingia. " -Shuhuda kwa Kanisa 9: 97.

MLANGO UTAFUNGWA —"Ndugu zangu, muwe waangalifu, waangalifu sana. Kuna kazi inayofanywa na wamishenari wa tiba ambayo inaitikia mwito wa maelezo yaliyotolewa katika aya ya Mathayo24:48-51. Bwana anafanya kazi kuwafikia wale ambao wameharibika maadili kabisa kwa uovu. Wengi watajua nini maana ya kuvutwa na Kristo, lakini hawatakuwa na ujasiri wa kimaadili wa kupambana dhidi ya uchu wa chakula na tamaa (passion). Lakini wafanyakazi hawapaswi kuvunjika moyo kwa sababu ya hili; kwa maana imeandikwa, "Nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani." 1 Timotheo 4: 1.

Je! ni wale tu waliookolewa kutoka katika vina vya chini kabisa ndio wanaorudi nyuma? Wapo wale katika huduma ambao wamepata nuru na maarifa ya Ukweli, ambao hawatakuwa washindi. Hawazuii hamu yao ya chakula na tamaa au kujikana kwa ajili ya Kristo. Watu wengi waliotengwa na walio masikini kwa unyonge, watoza ushuru na wenye dhambi, watalishikilia tumaini lililowekwa

mbele yao katika injili na wataingia katika ufalme wa Mbinguni mbele ya wale ambao wamepata fursa kubwa na nuru kuu, lakini wametembea gizani. Katika siku ile kuu ya mwisho wengi watasema: "Bwana, Bwana, tufungulie." Lakini mlango utafungwa, na kubisha kwao kutakuwa bure.” - Shuhuda kwa Kanisa 8: 75.

KUFUNGWA NA SHERIA NA SABATO—“Hivyo kazi ya Kweli ya umishenari wa tiba inafungamanishwa na kushika amri za Mungu bila kutenganishwa, ambapo Sabato inabainishwa kwa njia mahususi, kwa kuwa ndiyo kumbukizi kuu katika kazi ya uumbaji ya Mungu. Utunzaji wa Sabato unafungamanishwa na kazi ya kurudisha sura ya kimaadili ya Mungu ndani ya mwanadamu. Hii ndiyo huduma ambayo watu wa Mungu wanapaswa kuendeleza wakati huu. Huduma hii ikifanywa ipasavyo, italeta baraka iliyosheheni kwa kanisa.”—Shuhuda kwa Kanisa, 6: 266.

ISHARA YA WALE WAMPENDAO MUNGU NA KUTII SHERIA YAKE—"Huruma ya kweli kati ya mwanadamu na wanadamu wenzake ndiyo itakuwa ishara ya kuwatofautisha wale wanaompenda na kumcha Mungu na wale ambao hawaijali sheria Yake. Ni huruma iliyoje ambayo Kristo alionyesha katika kuja katika ulimwengu huu na kutoa maisha Yake dhabihu kwa ajili ya ulimwengu unaokufa! Dini Yake iliongoza kwenye kazi ya Kweli ya umishenari wa tiba.” —Medical Ministry, 251

KUJIBU MASHITAKA YA SHETANI: UWASILISHAJI WETU MBELE YA ULIMWENGU—"Bwana anapenda, kujibu mashitaka ya Shetani kupitia watu Wake, kwa kuonesha matokeo ya utiifu kwa kanuni za haki. Yeye Anapenda taasisi zetu za afya zisimame kama mashadidi wa ile Kweli. Zinapaswa kutoa/kuonyesha tabia kupitia kazi ambayo lazima iendelezwe katika siku hizi za mwisho katika kumrejesha mwanadamu kupitia matengenezo ya mazoea, hamu ya chakula, na tamaa. Waadventista Wasabato wanapaswa kutambuliwa katika dunia kwa kanuni za kiwango cha juu za matengenezo ya afya ambazo Mungu ametupatia.” —Manuscript, God’s Design in Establishing Sanitariums,” Desemba 22, 1899.

IMEFUNGWA NA KUTIWA MUHURI WA MUNGU—“Sura ya Hamsini na nane ya Isaya ina Ukweli wa sasa kwa watu wa Mungu. Hapa tunaona jinsi kazi ya umishenari wa tiba na huduma ya injili zinavyopaswa kuunganishwa pamoja wakati ujumbe unaotolewa kwa dunia. Wajibu wa kufanya kazi ya rehema na wema umewekwa juu ya wote wanaotunza Sabato ya Bwana umewekwa. Kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kufungwa pamoja na ujumbe wa injili, na kugongwa muhuri kwa muhuri wa Mungu.” – Welfare Ministry, 121.

3. ITAINUA UJUMBE WA MALAIKA WA TATU HADI KILIO KIKUU

UTAMBUZI DHAHIRI, BADILIKO LA AJABU —“Mungu humuita kila mshiriki wa kanisa kutoa maisha yake kikamilifu, bila ya kujibakiza, kwa ajili ya huduma ya Bwana. Yeye anatoa mwito wa watu kufanya matengenezo ya dhati yaliyoamuliwa. Viumbe vyote vinaugua chini ya laana. Watu wa Mungu wangejiweka wenyewe mahali ambapo watakuwa katika neema, wakitakaswa, mwili, nafsi, na roho kwa ile Kweli. Wakati wajitengapo na uendekezaji wote unaoharibu afya, watakuwa na utambuzi wazi wa kile kinachojumuisha utauwa wa kweli. Badiliko la ajabu litaonekana katika uzoefu wa kidini.”-Councils on Diet and Foods, 34.

KAMA WATENDAKAZI WATANYENYEKEZA MIOYO YAO: UAMSHO WA AJABU UTAKUJA—“Kama watenda kazi watanyenyekeza mioyo yao mbele ya Mungu, baraka itakuja. Watakuwa wote kwa wakati huo wakipokea mawazo mapya yenye kuburudisha, na kutakuwa na uamsho wa ajabu wa kazi ya injili ya umishenari wa tiba.” – Medical Ministry, 257.

VUGUVUGU KUBWA LA MATENGENEZO—"Katika maono ya Usiku, wasilisho lilipita mbele yangu la vuguvugu kubwa la matengenezo miongoni mwa watu wa Mungu. Wengi walikuwa wakimsifu Mungu. Wagonjwa waliponywa na miujiza mingine ilikuwa imetendeka. Roho ya maombezi, yaani kuombea wengine ilionekana, kama ilivyodhihirishwa kabla ya ile siku kuu ya Pentekoste. Mamia na maelfu walionekana wakitembelea familia, na kufungua mbele yao Neno la Mungu. Mioyo ilichomwa kwa nguvu ya Roho mtakatifu, na roho ya uongofu wa kweli ikawa imedhihirika. Milango ilikuwa imefunguliwa wazi kila upande kwa ajili ya kutangaza Ukweli. Dunia ilionekana kuangazwa na mvuto wa mbinguni. Baraka kubwa zilipokelewa na watu wa Mungu wa wanyofu na wanyenyekevu. Nilisikia sauti ya kushukuru na sifa, na hapo kulionekana kuwa ni matengenezo kama yale tuliyoyashuhudia katika mwaka 1844. Hata hivyo, baadhi ya watu walikataa kuongoka. Hawakuwa tayari kutembea katika njia ya Mungu, na ili kazi ya Mungu iweze kuendelea mbele, wito ulitolewa kwa ajili ya kutoa sadaka za hiari, wengine waling'ang'ania ubinafsi kwa mali zao za kidunia. Hawa watu wenye tamaa wakawa wamejitenga na ushirika wa waumini.” -Counsels on Health, 580.

MSUKUMO WA KIDINI UNAOSHAMBULIA WENGINE UNAKANDAMIZA UHURU: UWANJA WA KAZI —“Msukumo wa kidini wenye fujo au unaoshambulia, hukandamiza uhuru wa taifa letu, wale ambao wangesimamia uhuru wa dhamiri watawekwa katika nyadhifa zisizofaa au zinazoumiza. Kwa ajili ya faida yao, na kutokana na fursa waliyonayo wangepaswa kuwa wenye akili kwa kujielimisha

kuhusiana na ugonjwa, sababu zake, kinga na tiba. Na wale wanaofanya hivi watapata uwanja wa kazi popote pale. Daima watakuwepo watu ambao wanateseka, wengi tu, ambao watahitaji msaada, na sio tu kwa wale ambao ni wa imani sawa, ila hata miongoni mwa wale ambao hawaijui ile Kweli. Ufupi wa muda unadai muda na nishati ambayo haijaamshwa miongoni mwa wale wanaodai kuamini Ukweli wa leo" -Counsels on Health, 506.

FALSAFA YENYE HEKIMA NA UZOEFU WA KWELI KUAMSHA AKILI YA UMMA — "Wote wamefungwa kwa wajibu mtakatifu mno kwa Mungu, kuweka umakini kwenye falsafa zenye hekima na uzoefu wa dhatii ambao sasa Yeye anawapatia kwa kurejelea matengenezo ya afya. Yeye hupangilia kwamba somo kuu la matengenezo ya afya litazinduliwa/litatibuliwa, na akili ya umma ingeamshwa kwa kina kuichunguza mada hiyo; kwa maana haiwezekani kwa wanaume na wanawake, wakiwa na tabia zao za dhambi, zenye kudhuru afya, zenye kudhoofisha ubongo, kuweza kupambanua Ukweli mtakatifu, ambao kupitia huo wanapaswa kutakaswa, kusafishwa, kuinuliwa, na kufanywa wafae kwa jamii ya malaika wa mbinguni, katika ufalme wa utukufu." -Counsels on Diet and Food, 70.

KULITIBUA SOMO — "Somo kubwa la matengenezo ya afya linapswa litibuliwe, na nia na akili ya umma inapaswa kukorogwa/kuamshwa. Kiasi katika mambo yote kinapaswa kuunganishwa na ujumbe, kuwageuza watu wa Mungu kutoka katika kuabudu sanamu, ulafi wao wa chakula, na matumizi ya pesa kwa ubaradhifu katika mavazi pamoja na vitu vingine." - Counsels on Diet and Food, 71.

MPENYO WA KUUFIKIA MOYO—"Wakati inapoendeshwa kwa usahihi, kazi ya afya ni mpenyo wa kuingilia, ikitengeneza njia ya zile Kweli zingine kufikia moyo. Wakati ujumbe wa Malaika wa tatu upokelewapo katika ukamilifu wake, matengenezo ya afya yatapewa sehemu yake ndani ya mabaraza ya mikutano, ndani ya kazi ya kanisa, kazi ya nyumbani, na mezani, na ndani ya mipangilio yote ya kaya. Ndipo mkono wa kulia utaokoa na kulinda mwili." - Counsels on Diet and Food, 73.

MKONO WA KUUME WA KUFUNGUA MILANGO—"Kazi ya umishenari wa tiba ni mkono wa kuume wa injili. Ni muhimu katika kuendeleza kazi ya Mungu. Kila mji unapaswa kuingiwa na watendakazi waliofunzwa kufanya kazi ya umishenari wa tiba. Kama mkono wa kulia wa ujumbe wa malaika wa tatu, njia za Mungu za kutibu magonjwa zitafungua milango ya kuingiza Ukweli wa sasa." - Shuhuda kwa Kanisa, 7: 59.

HUPOKELEWA NA WOTE WANAOTAKA NURU—"Mivuto inayohusishwa na matengenezo ya afya itapendekezwa kwenye maamuzi ya wote wanaotaka nuru, na watasonga mbele hatua kwa hatua ili kupokea Kweli maalum za wakati huu." - Shuhuda kwa Kanisa 6: 379.

TANGU SASA - "Tangu sasa kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kuendelezwa kwa bidii ambayo haikuwahi kuhusishwa kabla. Kazi hii ni mlango ambao Ukweli hupata kuingia katika miji mikubwa." — Shuhuda kwa Kanisa 9: 167.

MPAKA DUNIA NZIMA ITAFUNIKWA—"Tutaona kazi ya umishenari wa tiba ikipanuka na kuongezeka katika kila hatua ya maendeleo yake, kwa sababu ya kutiririka kwa mamia na maelfu ya maelfu ya vijito, mpaka dunia nzima itafunikwa kama maji ya bahari." – Medical Ministry, 317.

4. ITAKUWA MSINGI WA VITENDO KWENYE HUKUMU KATIKA SIKU KUU YA MUNGU

TABAKA MBILI— "Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu Wake, na malaika watakatifu wote pamoja Naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu Wake; na mataifa yote watakusanyika mbele Zake; Naye atawabagua." Hiyo ndiyo picha ambayo Kristo aliionyesha alipokuwa katika Mlima wa Mizeituni, aliwapa wanafunzi Wake picha ya tukio la siku kuu ya hukumu. Na alionyesha kwamba uamuzi wa hukumu unageukia kwenye jambo moja. Wakati mataifa yote yatakapokuwa yamekusanywa mbele Zake, kutakuwa na makundi mawili tu, na hatima yao ya milele itaamuliwa na kile ambacho wamemfanyia Yeye au ambacho wamepuuza kumfanyia Yeye alipokuwa katika nafsi za maskini na wenye shida.

Katika siku hii Yesu hawaonyeshi watu kazi kuu aliyowafanyia ya kuutoa uhai Wake kwa ajili ya ukombozi wao. Yeye Anaonyesha kazi ya uaminifu waliyofanya kwa ajili Yake Yeye. Atawaambia wale atakaowaweka mkono Wake wa kuume kwamba, "Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu; kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia." Lakini hawa watu wanaopongezwa na Kristo hawajui kwamba walikuwa wanamhudumia Yeye. Anajibu maulizo yao ya mshangao kwamba, "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi." —The Desire of Ages, 637.

MAKUNDI MAWILI—"Katika siku za mwisho kutakuwa na makundi mawili tu, kundi moja ni lile lililo mkono wa kulia na jingine, lile la mkono wa kushoto. Na Kristo anasema kwa lile kundi la kulia, Njoni ninyi mliobarikiwa na Baba Yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu; kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia. Ndipo wenye haki watakapomjibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona una njaa, tukakulisha, au una kiu tukakunywesha? Tena ni lini tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha, au u uchi, tukakuvika? Ni lini tena tulipokuona u mgonjwa, au kifungoni, tukakujia? Na Mfalme atajibu, akiwaambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea Mimi. Kisha atawaambia na wale walioko mkono Wake wa kushoto, Ondokeni Kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake .. . . Matthew 25:34-41

"Hakika sasa tunataka kumleta Kristo katika maisha yetu ya kila siku. Wale ambao hawakuwalisha wenye njaa, au kuwavisha wenye uchi, au hawakuwatembelea wagonjwa hawakujua hilo, na kwa nini? Kwa sababu wamejifundisha na kujielimisha katika shule ya kujifurahisha wenyewe na kujiendekeza, na matokeo yake ni kwamba, waliipoteza mbingu na raha ya umilele ambayo wangekuwa nayo, kama tu wangezitoa nguvu zao wakfu kwa Mungu" —Medical Ministry, 133-134.

SIFA NA SHUKRANI, KWA MAANA ROHO ZIMEOKOLEWA—"Kutakuwa na pongezi iliyobarikiwa, baraka takatifu, kwa washindi waaminifu waliozileta roho kwa Bwana. Wataungana na wale wanaoshangilia mbinguni, watu wanaopiga kelele wanaporudi nyumbani na mavuno.

Furaha itakuwaje wakati waliokombolewa na Bwana wote watakapokutana,-wakikusanyika katika makao yaliyoandaliwa kwa ajili yao! Lo! Ni furaha iliyoje kwa wote ambao wamekuwa watendakazi wasio na ubaguzi au upendeleo, na wasio na ubinafsi wakiwa pamoja na Mungu katika kuendeleza kazi Yake duniani! Moyo wa kila mvunaji utaridhika wakati sauti iliyo wazi ya Yesu itakaposikika, ikisema "Njoni, mliobarikiwa na Baba Yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu; "Mkombozi anatukuzwa kwa sababu hakufa bure. Wakiwa na mioyo iliyochangamka na yenye furaha, wale ambao wamekuwa watendakazi pamoja na Mungu wanaona taabu ya nafsi zao kwa ajili ya watu wanaoangamia, wadhambi wanaokufa, na kisha wanaridhika. Masaa ya fadhaa na wasiwasi waliyotumia, hali zenye kutatanisha ambazo wamelazimika kukutana

nazo, huzuni ya moyo kwa sababu ya wengine waliokataa kuona na kupokea vitu vinavyoleta amani yao, hatimaye vinasahaulika. Kujinyima kwao walikopitia ili kusaidia kazi hiyo hakutakumbukwa tena. Wanapozitazama roho walizozitafuta ili zimwamini Yesu, na kuziona zikiokolewa, yaani zikiokolewa milele,- Minara ya kumbukizi inayotokana na rehema za Mungu na upendo wa Mwokozi,- ndipo kutarindima katika matao ya mbinguni vifijo vya sifa na shukurani. " —Medical Ministry, 134-135.

“Kuna njia nyingi za kufanya kazi ya stadi/sanaa ya uponyaji, lakini kuna njia moja tu ambayo Mbingu inaikubali. Tiba za Mungu ni mawakala rahisi wa asili, ambazo hazitaundikia mwili au kuudhoofisha mfumo kupitia sifa zake za nguvu." - Counsels on Health, 323

SEHEMU YA 2

MWONGOZO WA UINJILISTI

SURA YA 4

WALE WALIOITWA KUFANYA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA

AGIZO LA UNISHENARI TIBA

1. KILA MSHIRIKI WA KANISA ANAITWA KUFANYA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA

“Tumefika wakati ambao kila mshiriki wa kanisa anapaswa kushikilia kazi ya umishenari wa tiba. Ulimwengu ni nyumba ya wakoma iliyojaa wagonjwa wenye maambukizo ya kimwili na kiroho (Lazar House). Kila mahali watu wanaangamia kwa kukosa maarifa ya Zile Kweli zilizotolewa kwetu. Washiriki wa kanisa wanahitaji uamsho, ili kusudi watambue wajibu wao wa kutoa UIkweli huu. Wale ambao wameangazwa na Ukweli wanapaswa kuwa wabeba nuru kwa ulimwengu. Kuificha nuru yetu kwa wakati huu ni kufanya makosa ya kutisha. Ujumbe kwa watu wa Mungu leo ni, “Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja, Na utukufu wa Bwana umekuzukia.” Isaya 60:1.

Kila upande tunaona wale ambao wamekuwa na nuru na maarifa mengi wakichagua kwa makusudi uovu badala ya wema. Hawathubutu kufanya matengenezo, wanazidi kuwa katika hali mbaya na mbaya zaidi. Lakini watu wa Mungu hawapaswi kutembea katika giza. Wanapaswa kutembea katika nuru, kwa kuwa wao ni wanamatengenezo. “Mbele ya mwanamatengenezo wa kweli kazi ya umisihenari wa tiba itafungua milango mingi. Asiwepo anayesubiri hadi aitwe kwenye eneo fulani la mbali kabla ya kuwasaidia wengine. Popote ulipo unaweza kuanza kuwasaidia wengine mara moja. Fursa ziko kwenye ufikiaji wa kila mtu. Ifanye kazi ambayo unawajibika kuifanya- kazi inayopaswa kufanywa nyumbani na katika ujirani wako. Usisubiri mpaka watu wengine wakusihi uchukue hatua za utendaji. Kwa njia ya hofu ya Mungu songa mbele bila kukawia, ukitambua wajibu wako binafsi kwa Yule aliyetoa Maisha Yake kwa ajili yako. Tenda kana kwamba umemsikia Kristo akikuita wewe binafsi kufanya yote uwezavyo katika huduma Yake. Usiangalie ili kuona ni nani mwingine ambaye yuko tayari. Ukiwa umejitoa wakfu kwelikweli, Mungu, kupitia utendaji wako, atawaleta katika Kweli wengine ambao anaweza kuwatumia kama njia za kufikisha nuru kwa wengi wanaopapasa gizani.

Wote wanaweza kufanya kitu. Katika jitihada za kujitetea au kutoa udhuru, wengine husema, majukumu yangu ya nyumbani, watoto wangu, wanatumia wakati wangu na fedha zangu. Wazazi, watoto wako wanapaswa kuwa mkono wako wa msaada, wakiongeza uwezo wako na uwezo wa kufanya kazi kwa ajili ya Bwana.

“Hebu watu wetu waonyeshe kwamba wanapendezwa na kazi ya umishenari wa tiba. Hebu wajiandae ili kuwa watu wenye manufaa kwa kusoma vitabu ambavyo vimeandikwa kwa mafundisho yetu katika Nyanja hizi.” – Counsels on Health, 425-426.

“Kazi Yake Masihi ilikuwa umishenari wa tiba ambao anawaomba watu Wake waifanye leo . . Hakuna yule aliyekuja Kwake kwa ajili ya msaada na akatoka bila kuponywa. Hakuna hata uzi wa ubinafsi uliofumwa katika muundo ambao amewaachia watoto Wake wafuate. Aliishi maisha ambayo alitamani wote wanaomwamini wayaishii.” —Welfare Ministry, 116.

“Kwa miaka mitatu wanafunzi walikuwa na Kielelezo cha ajabu cha Kristo mbele yao. Siku baada ya siku walitembea na kuzungumza Naye, wakisikia maneno Yake ya kuchangamsha na kuwatia moyo wale waliochoka na wenye mizigo mizito na kuona udhihirisho wa nguvu Zake kwa niaba ya wagonjwa na wanaoteseka. Wakati ulipofika wa kuwaacha, aliwapa uwezo wa kufanya kazi kama Yeye alivyofanya kazi. Aliwapa neema Yake, akisema, ‘Mmepata bure, toeni bure.’ Walipaswa kwenda ulimwenguni ili kusambaza nuru ya injili Yake ya upendo na uponyaji. Kazi aliyoifanya walipaswa kuifanya. Na hii ndiyo kazi ambayo sisi pia tunapaswa kuifanya duniani.” – Welfare Ministry, 117.

"Tunapaswa kutenda sehemu yetu, tukisimama karibu na upande wa Kristo kama watendakazi pamoja Naye. Yeye Ndiye kichwa; Sisi ni mkono Wake wa kusaidia. Anapanga kwamba sisi, kwa kufanya kazi ya umishenari wa tiba, tutaondoa mizigo mizito na kuwaacha wanyonge walioonewa wawe huru. Tusifunge macho yetu kwa taabu inayotuzunguka, au masikio yetu kwa kilio cha dhiki kinachoendelea kupaa.”— Welfare Ministry, 118.

“Tutazikuta nyayo Zake kando ya kitanda cha mgonjwa, katika vibanda vya maskini, na popote pale walipo wenye dhiki wanaohitaji faraja. Kwa kufanya kama Yesu alivyofanya alipokuwa hapa duniani, tutakuwa tunafuata nyayo Zake.” – Desire of Ages, 640.

“Kazi ya umishenari wa tiba huleta kwa ubinadamu injili ya kuachiliwa kutoka kwa mateso. Ni kazi ya inayoitangulia injili. Ni Injili kwa vitendo, huruma ya Kristo inayofunuliwa wazi. Kazi hii ndilo hitaji kubwa na ulimwengu uko wazi kwa ajili ya hii kazi. Mungu anatoa uwezeshaji iil kwamba umuhimu wa kazi ya umishenari wa tiba utaeleweka na ndivyo maeneo mapya yatafikiwa mara moja.” – Welfare Ministry, 119.

“Kazi ya umishonari ya matibabu lazima ifanyike, kama njia ya kushinda chukina ubaguzi wa watu na kupata ufikiaji wa akili, si katika sehemu moja au mbili tu, bali katika sehemu nyingi ambako ile Kweli bado haijatangazwa. Tunapaswa kufanya kazi kama wamishenari wa tiba wa injili.” - Shuhuda kwa Kanisa 9: 211.

“Bwana alinipa nuru kubwa juu ya matengenezo ya afya. Kuhusiana na mume wangu, nilipaswa kuwa mtendakazi wa umishenari wa tiba. Nilipaswa kuwa mfano kwa kanisa kwa kuwapeleka wagonjwa nyumbani kwangu na kuwatunza. Nimefanya kazi hi, nimewapa wanawake na watoto tiba ya nguvu.”- A Call to Medical Evangelism, 9.

“Alipokuwa akienda mahali hadi mahali, aliwabariki na kuwafariji wanaoteseka na kuwaponya wagonjwa. Hii ndiyo kazi yetu sisi.” Medical Ministry, 319.

“Msukumo wa kidini ulio mkali unapokandamiza uhuru wa taifa letu, wale ambao wangesimamia uhuru wa dhamiri watawekwa katika nafasi ngumu au tata. Kwa ajili yao wenyewe, pale walipo na fursa wanapaswa wawe na akili kuhusiana na magonjwa, na sababu yake, kinga, na tiba. Wale wote wanaofanya hivi watapata uwanja wa kazi popote pale ulimwenguni. Kutakuwa na wanaoteseka, wengi tu, ambao watahitaji msaada.” -Counsels on Health, 506.

“Watumishi wa Kristo wanapaswa kufuata mfano Wake. Alipokuwa akienda kutoka mahali hadi mahali, aliwafariji wenye mateso na kuwaponya wagonjwa. Kisha akaweka mbele yao zile Kweli kuu kuhusiana na ufalme |Wake. Na hii ndiyo kazi ya wafuasi Wake. -Christ’s Object Lessons, 233.

“Anza kufanya kazi ya umishenari wa tiba kwa nafasi uliyo nayo. Utaona kwamba kwa njia hiyo, milango itafunguliwa kwako kwa ajili ya usomaji wa Biblia. Baba wa Mbinguni atakuweka wewe katika mahusiano na wale wanaohitaji kujua jinsi ya kuwatendea wagonjwa wao. Weka katika vitendo kile unachojua kuhusu matibabu ya ugonjwa. Hivyo mateso yataondolewa, na utakuwa na nafasi ya kumega mkate wa uzima kwa roho zenye njaa.” -A Call to Medical Evangelism, 26.

“Kwa ndugu zangu wahudumu ningesema, Ifanye kazi hii kwa busara na uwezo. Panga kazi kwa vijana wa kiume na wa kike katika makanisa yetu. Unganisha kazi ya umishenari wa tiba na kutangazwa kwa ujumbe wa malaika wa tatu. Fanya juhudi za mara kwa mara, zenye mikakati iliyopangiliwa ili kuinua makanisa kutoka kwa kiwango cha kuwa wafu/mfu ambamo wameanguka, na wamebakia hivo kwa miaka. Tuma kwenye makanisa watendakazi ambao wataweka kanuni za matengenezo ya afya katika uhusiano wao na ujumbe wa malaika wa tatu mbele ya kila familia na mtu binafsi. Wahamasishe wote kushiriki katika kazi kwa ajili ya wanadamu wenzao, na utajionea mwenyewe kama pumzi ya uhai haitarudi haraka katika makanisa haya” -Welfare Ministry, 124.

“Kwa nini haijaeleweka kutoka kwa Neno la Mungu kwamba kazi inayofanywa katika nyanja za umishenari wa tiba ni utimilifu wa Maandiko (Luka 14:21-23, imenukuliwa)? Hii ndiyo kazi ambayo makanisa katika kila eneo, kaskazini na kusini na mashariki na magharibi, yanapaswa kuifanya. Makanisa yamepewa nafasi ya kujibu kazi hii. Kwa nini basi hayajafanya hivyo? Mtu fulani lazima atimize agizo hizi la utume." –Welfare Ministry, 121-122.

“Kazi ambayo ilipaswa kufanywa imeachwa bila kutekelezwa. Wale ambao wamekuwa wakijishughulisha na kazi ya umishenari wa tiba wamekuwa wakifanya sehemu ile ya kazi ambayo Bwana angefanya.” –Welfare Ministry, 122.

“Mfanyie kazi Bwana, sio kwa kuwahubiria wale ambao tayari wanaijua ile Kweli ya wakati huu, bali kwa kuwaonya wale ambao hawajawahi kusikia ujumbe wa mwisho wa rehema. Fanya kazi kwa moyo uliojaa hamu ya dhati kwa roho za watu. Fanya kazi ya umishenari wa tiba Ndivyo utapata ufikiaji wa mioyo ya watu, na njia itakuwa imeandaliwa tayari kwa ajili kutanganza/kuhubiri Ukweli kwa njia iliyoamuliwa zaidii.” -Welfare Ministry, 57- 58.

“Kazi ya umishenari wa tiba ndiyo kazi inayoitangulia injili, mlango ambao Ukweli kwa wakati huu utapata mpenyo kuingia nyumba nyingi. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa wamishenari wa Kweli wa tiba, kwa kuwa wanapaswa kujifunza kuhudumia mahitaji ya nafsi na mwili. Kutokuwa na ubinafsi au uchoyo kutoka moyoni kabisa, kunapaswa kuonyeshwa na watendakazi wetu kwani, kwa ujuzi na uzoefu unaopatikana kwa kazi ya vitendo, wanatoka kwenda kutoa tiba kwa wagonjwa. Wanapoenda nyumba kwa nyumba watapata ufikiaji wa mioyo mingi.” -Welfare Ministry, 125.

“Hakuna kitu kinachoweza, au kitakachowahi kusaidia katika kutoa tabia kwa kaziya uwasilishaji wa Ukweli, ili kuwasaidia watu mahali walipo, kwa ubora zaidi kama kufanya kazi ya Msamaria mwema . . Mpangilio tofauti wa mambo unahitaji kuanzishwa miongoni mwetu kama watu, na kadiri sehemu hii ya kazi inavyofanywa, kutaundwa angahewa tofauti kabisa linalozunguka nafsi za watendakazi.” -Welfare Ministry, 132.

“Watu wa Mungu wanapaswa kuwa wamishenari wa dhati wa tiba. Wanapaswa kujifunza kuhudumia mahitaji ya nafsi na mwili. Wanapaswa kujua jinsi ya kutoa tiba rahisi ambazo hufanya mengi ili kupunguza maumivu na kuondoa magonjwa. Wanapaswa kufahamu kanuni za matengenezo ya afya, ili waweze kuwaonyesha wengine jinsi mazoea sahihi katika kula, kunywa, na kuvaa, magonjwa yanaweza kuzuiwa na afya kurejeshwa. Onyesho la thamani la kanuni za matengenezo ya afya litafanya mengi katika kuondoa chuki na ubaguzi dhidi ya kazi yetu ya

kiinjilisti. Tabibu mkuu, Mwanzilishi wa kazi ya umishenari wa tiba, atambariki kila mtu ambaye atasonga mbele kwa unyenyekevu na kwa kumtegemea Bawna, akitafuta kueneza Ukweli wa wakati huu. –Welfare Ministry, 127.

“Watendakazi - wamishenari wa injili ya tiba - wanahitajika sasa. Hamwezi kumudu kuendelea kutumia miaka mingi katika maandalizi. Hivi karibuni milango iliyofunguliwa kwa kushiriki Ukweli itafungwa milele. Pelekeni ujumbe sasa. Msikawie, na kumruhusu adui kumiliki mashamba yaliyofunguliwa sasa mbele yenu. Hebu makundi madogo yaende kufanya kazi ambayo Kristo aliwapa wanafunzi Wake. Hebu na wafanye kazi kama wainjilisti, wakitawanya machapisho yetu na kuzungumza juu ya ile Kweli kwa wale wanaokutana nao. Hebu wawaombee wagonjwa, wakiwahudumia mahitaji yao, si kwa kutumia dawa za famasia, bali kwa tiba za asili, na kuwafundisha jinsi ya kuirejesha afya na kuepuka magonjwa.” -Shuhuda kwa Kanisa 9 : 172.

2. KILA MAMA ANAITWA KUFANYA KAZI YA UMISHENARI wA TIBA

“Zipo njia nyingi ambazo maji yaweza kutumika kutuliza maumivu na kuzuia ugonjwa. Watu wote wapaswa kuwa na utambuzi katika maarifa ya matumizi ya tiba rahisi majumbani mwao. Hasa akina mama, wanapaswa kujua jinsi ya kutunza familia zao wakati wa afya na maradhi.” -Ministry of Healing, 237.

(Ministry of Healing, 237; 2 Testimonies, 370, 536-537; Fundamentals of Christian Education, 139, 141, 143, 152-154; Counsels on Health, 39, 114-115, 144, 608; Counsels to Parents, Teachers, and Students, 125)

3. KILA MTOTO ANAITWA KUFANYA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA

"Tumia muda kuwasomea watoto wako vitabu vya afya, vile vile kutoka kwenye vitabu vinavyohusu masuala ya kidini…

“Bwana ameteua vijana kuwa mkono Wake wa kusaidia. Ikiwa katika kila kanisa watu wangejiweka wakfu wenyewe kwa Mungu, ikiwa wangetenda kwa kujikana nafsi nyumbani, wakampa ahueni mama yao aliyetindikiwa na shuguli, mama angeweza kupata wakati wa kuwatembelea majirani, wakati nafasi inapojitokeza, wangeweza wao wenyewe kutoa msaada kwa kufanya vishuguli vidogo vidogo vya rehema na upendo. Vitabu na majarida yanayoshughulikia mada ya afya na kiasi vinaweza kuwekwa katika nyumba nyingi. Mgawanyo wa machapisho haya ni jambo muhimu; kwani maarifa ya thamani yanaweza kutolewa kuhusu matibabu ya magonjwa.” -Shuhuda kwa Kanisa, 7 : 64-65

(7 Testimonies, 64-65; Counsels to Parents, Teachers, and Students, 176-177; Counsels on Health, 426-428, 430, 486)

4. KILA MHUDUMU ANAITWA KWENYE KAZI YA UMISHENARI WA TIBA

“Hebu wachungaji wetu ambao wamepata uzoefu wa kuhubiri Neno, wajifunze jinsi ya kutoa tiba rahisi, na kisha wafanye kazi kwa akili kama wainjilisti wamishenari wa tiba.” -Counsels on Health, 397.

“Moyo wangu unahuzunika ninapotazama makanisa yetu, ambayo yanapaswa kuunganishwa moyoni na nafsini na kufanya kwa vitendo kazi ya umishenari wa tiba . . “Ningependa kukuambia kwamba hivi karibuni hakutakuwa na kazi yoyote itakayofanywa katika nyanja za huduma bali kazi ya umishenari wa tiba. Kazi ya mchungaji ni kuhudumu. Wahudumu wetu wanapaswa kufanyia kazi mpango wa injili wa kuhudumu.

“Hamtawahi kuwa wahudumu wa Agizo la Injili hadi muazimie kuonyesha kuwa mnapendezwa na kazi ya umishenari wa tiba, injili ya uponyaji na baraka na kuimarishwa. Njoni kumsaidia Bwana….. . dhidi ya nguvu kuu za giza, ili isisemwe juu yako “Ulaaniwe Merozi, alisema malaika wa Bwana, Walaanini kwa uchungu wenyeji wake; Kwa maana hawakuja kumsaidia Bwana, Kumsaidia Bwana juu ya hao wenye nguvu. Waamuzi 5:23 ……

“Ni kwa sababu ya maagizo ambayo nimeyapokea kutoka kwa Bwana kwamba nina ujasiri wa kusimama kati yenu na kuzungumza kama ninavyofanya, bila kujali jinsi ninyi mnavyoweza kuitazama kazi ya umishenari wa tiba. Ningependa kusema kwamba kazi ya umishenari wa tiba ni kazi ya Mungu. Bwana anataka kila mmoja wa wahudumu Wake aingie kwenye mstari wa kazi hii. Shikilia kazi ya umishenari wa tiba, na itakuwezesha kuwafikia watu. Mioyo yao itaguswa unapohudumia mahitaji yao. Unapopunguza mateso yao, utapata fursa ya kuzungumza nao kuhusu upendo wa Yesu.” -Counsels on Health, 533.

Wengine wanashindwa kabisa kutambua umuhimu wa wamishenari kuwa pia ni wamishenari wa tiba. Mhudumu wa Injili atafanikiwa maradufu katika kazi yake ikiwa anaelewa jinsi ya kutibu magonjwa. Nuru inayozidi kuongezeka imetolewa kwangu juu ya mada hii.” Medical Missionary, 245.

(6 Testimonies, 240-241, 288-289, 300-301, 377,378; 7 Testimonies, 111-112; 8 Testimonies, 77, 163; 9 Testimonies, 169-170; Counsels on Health 331, 394, 397, 513-518, 524, 533; Counsels on Diet and Foods, 74; Welfare Ministry 123-124; Ministry of Healing, 149)

5. KILA DAKTARI ANAITWA KWA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA

“Kristo ametupa mfano. Alifundisha kutoka katika Maandiko zile Kweli za injili, na pia aliwaponya wale walioteseka na waliokuja Kwake ili kupata nafuu. . na ndivyo madaktari wetu wanavyopaswa kufanya kazi. Wanafanya kazi ya Bwana wanapofanya kazi kama wainjilisti, wakitoa maagizo ya jinsi nafsi inavyoweza kuponywa na Bwana Yesu. Kila daktari anapaswa kujua jinsi ya kuomba kwa imani kwa ajili ya wagonjwa, na pia kusimamia matibabu kwa usahihi. Wakati huohuo anapaswa kufanya kazi kama mmoja wa wahudumu wa Mungu, kufundisha toba na uongofu, na wokovu wa nafsi na mwili. -Counsels on Health, 389.

(Ministry of Healing 119-121; 6 Testimonies 229234, 246; Gospel Workers 360-362; Counsels on Health 503-504)

6. KILA MTENDAKAZI WA BIBLIA ANAITWA KUFANYA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA

“Watendakazi wote wa injili wanapaswa kujua jinsi ya kutoa tiba rahisi ambayo hufanya mengi ili kupunguza maumivu na kuondoa magonjwa. -Counsels on Health, 389.

"Sauti ya ujumbe wa malaika wa tatu inapaswa kusikika kwa nguvu. Hebu mafundisho ya matengenezo ya afya yaletwe katika kila jitihada inayofanywa ili kuwaangazia awtu nuru ya Ukweli mbele za watu.” —Evangelism 533 (Medical Ministry, 304).

“Kazi ya umishenari wa tiba ndiyo kazi ya inayoitangulia injili, mlango ambao Ukweli kwa wakati huu ni utapata mpenyo kwenye nyumba nyingi. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa wamishenari wa Kweli wa tiba, kwa kuwa wanapaswa kujifunza kuhudumia mahitaji ya nafsi na mwili. Kutokuwa na ubinafsi mtupu kunapaswa kuonyeshwa na watendakazi wetu kwani, kwa ujuzi na uzoefu unaopatikana kwa kazi ya vitendo, wanatoka kwenda kutoa matibabu kwa wagonjwa. Wanapoenda nyumba kwa nyumba watapata uwezekano wa kuifikia mioyo mingi. — Welfare Ministry, 125.

(Christian Service, 132-140; Evangelism, 513, 551; Gospel Workers, 360-363).

7. KILA MUUGUZI ANAITWA KWA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA

“Wauguzi wamishenari wanaowatunza wagonjwa na kuwaondolea dhiki wanadamu maskini, watapata fursa nyingi za kuomba pamoja nao, kuwasomea Neno la Mungu, na kuzungumza juu ya Mwokozi. Wanaweza kuomba pamoja na

wale wasiojiweza ambao hawana nguvu ya kudhibiti uchu wa chakula ambayo shauku imeshusha…….. Ufunuo wa upendo usio na ubinafsi, unaodhihirishwa katika matendo ya fadhili zisizo na upendeleo/maslahi, utafanya iwe rahisi kwa watuwanaoteseka kuamini katika upendo wa Kristo. -Counsels on Health, 388

(Counsels on Health, 388-389; 9 Testimonies, 171; Welfare Ministry, 126; Counsels on Health, 396)

8. KILA MWINJILISTI WA VITABU ANAITWA KWA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA

"Mwinjilisti wa vitabu anapoenda kutoka mahali hadi mahali, atakutana na wengi ambao ni wagonjwa. Anapaswa kuwa na ujuzi wa kivitendo, kwa kujua sababu za ugonjwa kuwepo, na anapaswa kuelewa jinsi ya kutoa tiba rahisi, ili aweze kuhudumia wanaoteseka. Zaidi ya hayo, anapaswa kuomba kwa imani na unyenyekevu kwa ajili ya wagonjwa, akiwaelekeza kwa Tabibu Mkuu. Anapotembea na kufanya kazi hivyo na Mungu, malaika wanaohudumu wako karibu naye, wakimpa uwezo wa kuifikia mioyo. Ni uwanja mpana kama nini wa juhudi za umishenari ulio mbele ya waumini waaminifu, waliowekwa wakfu; Ni baraka iliyoje atakayokuwa nayo katika utendaji wa bidii na uadilifu wa kazi yake. -Counsels on Health, 463-464.

(9 Testimonies, 34, 172; 6 Testimonies, 323-4; Counsels on Health 397, 435, 462-464, 466; 7 Testimonies, 59)

Ni muhimu tuelewe kwamba mtu hawi mmishenari wa tiba hadi aunganishe pande zote mbili za muundo/pateni. Mmishenari wa tiba kwa magonjwa ya roho na mwili. Mhudumu au mtendakazi wa injili hawezi kuitwa hivyo isipokuwa yeye pia anahudumia mahitaji ya kimwili; Tabibu au muuguzi hawezi kuitwa hivyo isipokuwa yeye pia anahudumia mahitaji ya kiroho. Ni mpaka tunapounganisha haya mawili ndipo tunapofuata katika muundo ambao Yesu alitupa na kuwa wamishenari wa tiba.

(Soma pia 6 Testimonies, 240-241, 288-293; 7 Testimonies, 59,111; 8 Testimonies, 46, 168, 148,162; 9 Testimonies, 169-170, 222; Gospel Workers, 360; Counsels on Health, 212, 219, 288, 508, 513,518, 519-523, 528, 534, 536, 557-558; Counsels to Parents, Teachers, and Students, 468).

9. KILA MFUASI WA YESU ANAITWA KWA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA

“Akawaita wanafunzi Wake kumi na wawili, akawapa amri juu ya pepo wachafu, wawatoe, na kupoza magonjwa yote na udhaifu wa kila aina. Na katika kuenenda

kwenu, hubirini, mkisema, Ufalme wa mbinguni umekaribia. Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure. Mathayo 10:1,7-8

Upana wa kazi ya umishenari wa injili haueleweki. Kazi ya umishenari wa tiba inayotakiwa sasa imeainishwa katika agizo ambalo Kristo aliwapa wanafunzi Wake kabla tu ya kupaa Kwake. 'Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.' Alisema, 'Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote…na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.' Mathayo 28:18-20. Maneno haya yanaonyesha shamba/eneo leetu na kazi yetu. Shamba letu ni ulimwengu; Kazi yetu ni kutangaza Kweli ambazo Kristo alikuja kwenye ulimwengu wetu ili kuzitangaza.—Counsels on Health, 509

"Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. 18 watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya. 20 Nao wale wakatoka, wakahubiri kotekote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo." Marko 16:15, 18, 20 15

"Utume wa Kiungu/Bwana hauhitaji marekebisho. Njia ya Kristo ya kuwasilisha Ukweli haiwezi kuboreshwa. Mwokozi aliwapa wanafunzi masomo ya vitendo, akiwafundisha jinsi ya kufanya kazi kwa njia ya kufanya nafsi kuwa na furaha katika Ukweli. Aliwahurumia watu waliochoka, wale waliolemewa na mizigo, na waliokandamizwa. Aliwalisha wenye njaa na kuwaponya wagonjwa. Daima alienda akitenda mema. Kwa mema aliyotimiza, kwa maneno Yake ya upendo na matendo Yake ya fadhili, alifasiri injili kwa wanadamu." -Welfare Ministry, 56.

"Bwana wetu anafundisha kwamba lengo la kweli la maisha ni huduma. -Christ's Object Lessons, 326.

"Ifanye kazi ya Kristo kuwa mfano wako. Mara kwa mara Masihi alienda huku na huko akitenda mema—akiwalisha wenye njaa na kuponya wagonjwa. -Welfare Ministry, 53.

Yeye asemaye ya kuwa anakaa ndani yake, imempasa kuenenda mwenyewe vile vile kama yeye alivyoenenda. 1 Yohana 2:6

"Yafanye maisha ya Kristo kuwa somo lako endelevu, na fanya kazi kama Bwana alivyofanya, kwa kufuata mfano Wake." -Welfare Ministry, 128.

Mbinu ya Kristo pekee ndiyo itatoa mafanikio ya kweli katika kuwafikia watu. Mwokozi alichangamana na wanadamu kama mtu aliyewatakia mema. Alionyesha huruma Yake kwao, akahudumia mahitaji yao, Naye akaaminika kwao, kwa kupata ujasiri wao. Kisha akawaambia, “Nifuateni.” Kuna haja ya kuja karibu na watu kwa juhudi binafsi. Kama muda kidogo ungetengwa kwa ajili ya mahubiri, na muda mwingi zaidi ungetumiwa katika huduma binafsi kwa watu, matokeo makubwa zaidi yangeonekana. Maskini hawana budi kuponywa, wagonjwa wauguzwe, walio na huzuni na waliofiwa wafarijiwe, wasio na maarifa waelekezwe, wasio na uzoefu washauriwe. -Ministry of Healing, 143.

Mkombozi wa ulimwengu alikuwa mmishenari Mkuu wa kuigwa Mfano/modeli. Shuhuda kwa Kanisa 5: 385.

“Kristo anasimama mbele yetu kama kielelezo, mmishenari mkuu wa tiba, kielelezo kwa wale wote ambao wangemfuata.” - Welfare Ministry, 53.

“Naye alikuwa akizunguka katika Galilaya yote, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri Habari Njema ya ufalme, na kuponya ugonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu. Na habari Zake zikaenea katika Syria yote; wakamletea wote waliokuwa hawawezi, walioshikwa na maradhi mbalimbali na mateso, wenye pepo, na wenye kifafa, na wenye kupooza; akawaponya. Na makutano mengi wakamfuata, kutoka Galilaya, na Dekapoli, na Yerusalemu, na Uyahudi, na ng'ambo ya Yordani.” Mathayo 4: 23-25

Wengi wanahisi kwamba ungekuwa upendeleo mkubwa kutembelea sehemu za makumbusho ya matukio ya maisha ya Kristo duniani, kukanyaga mahali Yeye alipokanyaga, kulitazama ziwa lile ambalo alipenda kufundisha kando yake, na vilima na mabonde ambavyo mara kwa mara macho yake yalitazama. Lakini kumbe hatuhitaji kwenda Nazareti, Kapernaumu, au Bethania, kwamba ili watembee katika nyayo za Yesu. Tutakutana na nyayo Zake kando ya kitanda cha mgonjwa, katika vijumba vya kimaskini, katika mitaa yenye msongamano mkubwa katika miji mikubwa, na kila mahali ambapo kuna mioyo ya wanadamu inayohitaji faraja. Katika kufanya vile Yesu alivyofanya akiwa duniani, hakika tutakuwa tunatembea katika nyayo Zake. Desire of Ages, 640.

“Kwa sababu ndio mlioitiwa; maana Kristo Naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuate nyayo Zake.” 1 Petro 2:21

Je! Ndugu na dada zangu, mnajiuliza kwamba: Tuige mfano gani au modeli gani? Siwaelekezi kwa watu wakubwa na wazuri, bali kwa Mkombozi wa ulimwengu. Ikiwa tunahitaji kuwa na roho ya Kweli ya umishenari lazima tujazwe na upendo

wa Kristo; lazima tumwangalie Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yetu, na kisha tujifunze tabia Yake, tukuze Roho Yake ya upole na unyenyekevu, na kutembea katika nyayo Zake. Shuhuda kwa Kanisa 5: 385

Naye Yesu alikuwa akizunguka katika miji yote na vijiji, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri habari njema ya ufalme, na kuponya magonjwa yote na udhaifu wa kila aina. Na alipowaona makutano, aliwahurumia, kwa sababu walikuwa wamechoka na kutawanyika kama kondoo wasio na mchungaji. Ndipo alipowaambia wanafunzi Wake, Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache. Basi mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke watenda kazi katika mavuno Yake. -Mathayo 9:35-38

“Wanafunzi walikuwa wanaenda kuwa na nguvu sawa na ile aliyokuwa nayo Yesu, na hivyo kuponya namna yote ya magonjwa na namna zote za maradhi’ miongoni mwa watu.’ Kwa kuponya kwa Jina Lake magonjwa ya mwili, wangeshuhudia nguvu Yake ya kuponya roho za watu…….Hivyo ndivyo Kristo alivyowapatia wanafunzi Wake kazi ya utume…… Alitoa kwa ukamilifu nyenzo/mahitaji kwa ajili ya kutenda kazi hiyo, na alibeba Mwenyewe wajibu unaohusisha mafanikio ya kazi hiyo. Kwa kadiri ambavyo wangetii Neno Lake, na kufanya kazi kwa kuunganika Naye, wasingeshindwa. Enendeni kwa mataifa yote, aliwaambia. Enendeni sehemu za mbali zinazokaliwa na watu duniani, lakini mjue kwamba uwepo Wangu uko kule. Fanyeni kazi kwa imani na ujasiri, maana hautakuja kamwe muda ambao nitawatelekeza. Agizo la Mwokozi kwa wanafunzi wale liliwajumuisha waamini wote. Linahusisha wote wanaomwamini Kristo mpaka mwisho wa wakati. Desire of Ages, 821-822.

Mungu atawatumia watu walio tayari kutumiwa. Sio watu walio na akili mahiri zaidi au wenye vipaji vikubwa zaidi ndio ambao kazi yao huleta matokeo makubwa na yenye kudumu zaidi. Waume na wake wote ambao wameusikia ujumbe kutoka mbinguni wanahitajika. Watendakazi wenye ufanisi zaidi ni wale wanaoitikia mwaliko, “Jitieni nira Yangu, mjifunze Kwangu.” Mathayo 11:29. Ministry of Healing, 150.

“Bwana lazima apewe nafasi ya kuwaonyesha watu wajibu wao, na kufanya kazi juu ya akili zao. Hakuna mtu anayepaswa kujifungamanisha kutumika kwa muda wa miaka kadhaa, chini ya uongozi wa kundi moja la watu au katika tawi moja maalum la kazi ya Bwana; Kwa maana Bwana Mwenyewe atawaita watu, kama ilivyokuwa zamani, Alipowaita wavuvi wanyenyekevu, na Yeye Mwenyewe atawapa maagizo kuhusu shamba lao la kazi na mbinu wanazopaswa kufuata. Atawaita watu wanaokokota jembe, kwenye nyanja za kilimo na kutoka kwa kazi

zingine, kutoa maelezo ya mwisho ya onyo kwa roho zinazoangamia. Kuna njia nyingi za kufanya kazi kwa Bwana, na Mwalimu mkuu atafungua ufahamu wa watendakazi hawa, na kuwawezesha kuona mambo ya ajabu katika Neno Lake. - Counsels on Health, 395.

Yeye Yuko tayari kuponya sasa kama wakati ule alipokuwa duniani katika mwili. Watumishi wa Kristo ndio wawakilishi Wake, mifereji ya kazi Zake. Yeye Anatamani kuonyesha uweza Wake wa kuponya kupitia hao. Namna Mwokozi alivyoponya magonjwa kuna masomo kwa wanafunzi Wake. Katika tukio moja alipaka macho ya mtu kipofu kwa matope, na akamwambia, "Nenda kanawe katika birika ya Siloamu, . . . Basi akaenda na kunawa; akarudi anaona." Yohana 9:7. Uponyaji ule ungefanywa tu kwa uweza wa Mponyaji Mkuu Yule, lakini Kristo alitumia njia nyepesi ya asili. Wakati hakuonekana akitumia tiba ya vidonge vya famasia, alijikita kwenye matumizi ya tiba za asili nyepesi.

Kwa wagonjwa wengi walioteseka waliopokea uponyaji, Yesu alisema, "Usitende dhambi tena, lisije likakupata jambo lililo baya zaidi." Yohana 5:14. Hivyo alifundisha kwamba ugonjwa ni matokeo ya kukiuka sheria za Mungu, zote mbili, yaani, sheria za asili na sheria za kiroho. Maumivu na huzuni kubwa duniani visingekuwepo ikiwa watu wangedumu kuishi kulingana na mpango wa Mwumbaji……Tunapaswa kuwa watendakazi wenza pamoja na Mungu kwa ajili ya urejeshaji wa afya ya mwili na roho.

Kristo alikuwa mwongozi na mwalimu wa Israeli ya kale, na aliwafundisha kwamba afya ni zawadi ya kutii sheria za Mungu. Tabibu Mkuu huyu aliyeponya wagonjwa kule Palestina alikuwa amenena na watu kutokea katika nguzo ya wingu, akiwaambia wanachopaswa kufanya, na kile ambacho Mungu angewafanyia. Alisema, "Kwamba utaisikiza kwa bidii sauti ya Bwana, Mungu wako, na kuyafanya yaliyoelekea mbele zake, na kutega masikio usikie maagizo yake, na kuzishika amri zake, mimi sitatia juu yako maradhi yoyote niliyowatia Wamisri; kwa kuwa Mimi ndimi Bwana nikuponyaye." Kutoka 15:26. Kristo aliwapatia Waisraeli maelekezo bayana kuhusu mwenendo wao wa maisha, na aliwahakikishia kwamba, "Bwana atakuondolea ugonjwa wote." Kumbukumbu 7:15. Walipotekeleza masharti hayo, ahadi hiyo ilithibitika kwao. "Katika kabila zao asiwepo mwenye kukwaa." Zaburi 105:37. Mafundisho haya ni kwa ajili yetu. Kuna masharti ya kuzingatiwa na wote wanaotaka kuhifadhi afya. Lazima wote wajifunze masharti haya. Bwana hapendezwi na ujinga unaohusu sheria zake, ziwe za asili au za kiroho. Tunapaswa tuwe watenda-kazi pamoja na Mungu kwa ajili ya kurejesha afya ya mwili na ya roho. Na tunapaswa tufundishe wengine

namna ya kuhifadhi na kurejesha afya. Kwa wagonjwa tunapaswa kutumia tiba ambayo Mungu ametoa katika vitu vya asili, na tunapaswa tuwaelekeze kwake Yeye pekee awezaye kurejesha. Ni kazi yetu kuwapeleka wagonjwa na wenye mateso kwa Kristo katika mikono ya imani yetu.

“Tunapaswa tuwafundishe kumwamini Mponyaji Mkuu. Tunapaswa tushikilie ahadi zake, na kuomba udhihirisho wa nguvu zake. Kiini chenyewe cha injili ni urejeshaji, na Mwokozi anatutaka tuwafanye wagonjwa, wasio na tumaini, na wenye shida washikilie nguvu Zake. Nguvu ya upendo ilikuwa katika kuponya kote kwa Kristo, na ni katika kushiriki upendo ule tu, kwa imani, ndipo tunapoweza kuwa nyenzo za kazi Yake. Ikiwa tunapuuza kujiunganisha na Kristo kwa mwunganiko wa kimbingu, mkondo wa nguvu iletayo uzima hauwezi kutiririka katika vijito vilivyojaa kutoka kwetu kwenda kwa watu. Kuna mahali ambapo hata Mwokozi hakuweza matendo mengi makuu kwa sababu ya kutokuamini kwao. Vivyo hivyo sasa kutokuamini kunalitenganisha kanisa na Msaidizi Wake wa kimbingu. Lina udhaifu wa kushindwa kushikilia Ukweli wa milele. Kwa kanisa kukosa imani, Mungu anafadhaishwa, na kupokonywa utukufu Wake. “Ni katika kufanya kazi ya Kristo kwamba kanisa linakuwa na ahadi ya uwepo wa Kristo. Alisema, Enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi; "na, tazama, Mimi Niko pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Kujitia nira Yake ni moja kati ya masharti ya kwanza ya kupokea uwezo Wake. Maisha yenyewe ya kanisa hutegemea uaminifu wake katika kutimiza agizo la Bwana la utume.” Desire of Ages, 823-825.

SURA YA 5

SEHEMU NA JINSI WAMISHENARI WA TIBA WANAPASWA KUPOKEA MAFUNZO YAO.

MWONGOZO WA SHULE ZA UMISHENARI WA TIBA

1. TUMEFIKA WAKATI AMBAPO KILA MSHIRIKI WA KANISA ANAPASWA KUSHIKILIA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA.

“Tumefika wakati ambapo kila mshiriki wa kanisa anapaswa kushikilia kazi ya umishenari wa tiba. Ulimwengu ni nyumba ya wagonjwa wa ukoma iliyojaa waathiriwa wa maambukizo ya kimwili na ya kiroho. Kila mahali watu wanaangamia kwa kukosa ujuzi wa Ukweli ambao umetolewa kwetu. Washiriki wa kanisa wanahitaji uamsho, ili waweze kutambua wajibu wao wa kuzitoa kwa watu Kweli hizi. -Counsels on Health, 425.

“Watu wa Mungu wanapaswa kuwa wamishenari wa tiba walio dhati. Wanapaswa kujifunza kuhudumia mahitaji ya nafsi na mwili. Wanapaswa kujua jinsi ya kutoa tiba sahili ambayo hufanya mengi ili kupunguza maumivu na kuondoa magonjwa. Wanapaswa kufahamu kanuni za matengenezo ya afya, ili waweze kuwaonyesha wengine kwamba kwa mazoea sahihi ya kula, kunywa, na kuvaa, magonjwa yanaweza kuzuiwa na afya kurejeshwa. Onyesho la thamani la kanuni za matengenezo ya afya litafanya mengi katika kuondoa chuki dhidi ya kazi yetu ya kiinjilisti. Tabibu mkuu, Mwanzilishi wa kazi ya umishenari wa tiba, atambariki kila mtu ambaye atasonga mbele kwa unyenyekevu na mategemeo, akitafuta kutoa Ukweli kwa wakati huu.” -Welfare Ministry, 127.

2. USISAHAU KAMWE KWAMBA MUNGU NDIYE MWALIMU PEKEE NA KWAMBA YEYE PEKE YAKE NDIYE ANAYEFUNDISHA

“Ghala kubwa la Kweli ni Neno la Mungu—Neno lililoandikwa, Kitabu cha Asili, na Kitabu cha Uzoefu katika kushughulika kwa Mungu na maisha ya mwanadamu. Hapa kuna hazina ambazo watenda kazi wa Kristo wanapaswa kuchota. Katika kutafuta Ukweli wanapaswa kumtegemea Mungu, na sio akili za wanadamu, watu wakuu ambao hekima yao ni upumbavu tu kwa Mungu. Kupitia njia Zake Mwenyewe alizowekwa, Bwana atatoa ujuzi Wake Mwenyewe kwa kila mtafutaji.

“Ikiwa mfuasi wa Kristo ataamini Neno Lake na kulitenda, hakuna sayansi katika ulimwengu wa asili ambayo hataweza kufahamu na kuifurahia. hakuna chochote isipokuwa kile kitakachomletea njia na nyenzo ili aweze kutoa kwa wengine ile Kweli. - Christ’s Object Lesson, 125.

Watu wa kawaida wanapaswa kuchukua nafasi zao kama watendakazi. Kwa kushiriki huzuni za wanadamu wenzao kama Mwokozi alivyoshiriki huzuni za wanadamu, kwa imani watamuona Mwokozi akifanya kazi nao. —Shuhuda kwa Kanisa 7: 272.

Mungu atawachukua watu ambao hawaonekani kuwa wamekirimiwa kwa talanta nyingi sana, watu wasio na kujiamini wenyewe sana, Naye atawafanya watu hawa dhaifu kuwa na nguvu, kwa sababu wao wamemtumaini Yeye kuwafanyia yale ambayo hawawezi kuyafanya wenyewe. Mungu atakubali utumishi/huduma inayofanywa kwa moyo wote, na Yeye Mwenyewe atafidia mapungufu.

Mara nyingi Bwana amewachagua watu ambao wamepata fursa ndogo ya elimu ya darasani kuwa watenda kazi pamoja Naye. Watu hawa wametumia uwezo wao kwa uaminifu zaidi, na Bwana amewatunukia thawabu kwa uadilifu wao katika kazi Yake, bidii yao katika kazi, na kiu yao ya kutafuta maarifa. Yeye ameshuhudia machozi yao na kusikia maombi yao. Kama vile ambavyo baraka Zake ziliwajia mateka katika ikulu ya Babeli, hali kadhalika Yeye huwapatia watenda kazi Wake hekima na maarifa leo.

Watu wenye upungufu wa elimu ya darasani/shuleni, wale walio wa hadhi ya chini katika nafasi za kijamii, kupitia neema ya Kristo, nyakati zingine wamefanikiwa kwa namna ya kushangaza katika kuzileta roho kwa Bwana. Siri ya mafanikio yao ilikuwa imani yao kwa Mungu. Watu hawa walijifunza kila siku kutoka Kwake, Yeye ambaye Ndiye Mshauri wa ajabu na Mweza yote. Watendakazi wa namna hii wanapaswa kutiwa moyo. Bwana huwaunganisha na wale walio na uwezo bora zaidi ili kujaza mapengo ambayo wengine huyaacha. Ministry of Healing, 150- 151.

(Akizungumzia kuhusu wale elfu tano) Majaliwa ya Mungu yalikuwa yamemweka Yesu mahali alipokuwa, Naye alimtegemea Baba Yake wa mbinguni kwa mbinu, njia na uwezo kutatua hitaji hilo. Tunapoletwa katika maeneo yenye shida, twapaswa kumtegemea Mungu. Katika kila dharura twapaswa kutafuta msaada kutoka Kwake,Yeye ambaye ana rasilimali zisizo na ukomo chini ya amri Yake. Ministry of Healing, 48-49.

“Ikiwa unasonga karibu na upande wa Kristo, umevaa nira Yake, kila siku utajifunza juu Yake, jinsi ya kubeba ujumbe wa amani na faraja kwa wenye huzuni na waliokatishwa tamaa, wenye kusononeka na waliovunjika moyo. Unaweza kuwaelekeza waliokata tamaa kwa Neno la Mungu na kuwapeleka wagonjwa kwa Bwana katika maombi.” -Colporteur Ministry, 41.

Kristo anawakaribisha kwa uhakikisho wenye matumaini wanaume na wanawake wote wanaotusababishia kukatishwa tamaa. Ndani yao Anaona sifa ambazo zitawawezesha kuchukua nafasi katika shamba Lake la mizabibu. Ikiwa wataendelea kuwa wanafunzi daima, kupitia uongozi Wake, Yeye atawafanya

kuwa wanaume na wanawake wanaofaa kufanya kazi ambayo haiko nje ya uwezo wao; kupitia kujazwa kwa Roho Mtakatifu, Atawapa nguvu ya kuzungumza.

“Sehemu nyingi zenye ukame, ambazo hazijafanyiwa kazi lazima zifanyiwe kazi na watu wapya ambao hawajazoea kazi. Mwangaza wa mtazamo wa Mwokozi juu ya ulimwengu utachochea ujasiri kwa wafanyakazi wengi, ambao, ikiwa wataanza kwa unyenyekevu, na kuweka mioyo yao katika kazi hiyo, watakuwa watu sahihi kwa wakati na mahali sahihi. Kristo anaona taabu zote na kukata tamaa kwa ulimwengu, hali ambayo inaweza kuwaweka chini watendakazi wetu wenye uwezo mkubwa kwa uzito wa kukatishwa tamaa kukubwa sana hata wasijue jinsi ya kuanza kazi ya kuongoza wanaume na wanawake katika mzunguko wa kwanza wa ngazi 2 Pet 5:1-4. Njia zao sahihi na za kinagaubaga zina thamani ndogo. Watu kama hawa watasimama tu juu kidogo ya mzunguko wa chini ya ngazi, wakisema: "Njooni hapa tulipo."

Yeye husahihisha uchaji-Mungu wetu uliopotoka, akiwapa mzigo wa kazi kwa ajili ya masikini na wahitaji katika maeneo magumu kwa wanaume na wanawake walio na mioyo inayoweza kuhisi kwa ajili ya wajinga/wasiojua na kwa ajili ya wale walio nje ya njia. Bwana anawafundisha wafanyakazi hawa jinsi ya kukutana na wale anaowataka wasaidiwe. Watatiwa moyo waonapo milango inafunguliwa kwa ajili ya wao kuingia mahali ambapo wanaweza kufanya kazi ya umishenari wa tiba/kitabibu. Wakiwa na ujasiri mdogo wao wenyewe binafsi kwa udogo, wanampa Mungu utukufu wote kwa kutojitumainia nafsi zao. Mikono yao inaweza kuwa rafu na sugu na isiyo na ujuzi, lakini mioyo yao ni miepesi kuwaonea huruma awtu; wamejazwa na hamu ya dhati ya kufanya kitu ili kupunguza huzuni nyingi sana; na Kristo Yupo kwa ajili ya kuwasaidia. —Shuhuda kwa Kanisa 7: 271-272.

Kristo Ndiye Mwalimu Mkuu (6 Testimonies, 86, 152-153, 331; 9 Testimonies, 170; Fundamentals of Christian Education, 184, 224, 383, 450-451), the Greatest Educator— (Desire of Ages, 809: 5 Testimonies, 588; Fundamentals of Christian Education, 48).

3. KUMBUKA DAIMA KWAMBA MUNGU NDIYE TABIBU MKUU

Bwana angetaka watu Wake waje Kwake kwa ajili ya nguvu yao ya uponyaji. Yeye Atawabatiza kwa Roho Wake Mtakatifu na kuwafanya kufaa kwa huduma ambayo itakuwa baraka katika kurejesha afya ya kiroho na kimwili ya wale wanaohitaji uponyaji. — Shuhuda kwa Kanisa 9: 178.

“Mungu Ndiye ambaye ameweka riziki na majaliwa kwamba asili itende kazi ya kurejesha nguvu zilizochoka. Nguvu ni ya Mungu. Yeye Ndiye Mganga Mkuu.” -Medical Ministry, 11-12.

“Hatuwezi kuponya. Hatuwezi kubadilisha hali ya ugonjwa wa mwili. Lakini ni sehemu yetu, kama wamishenari wa tiba, kama watendakazi pamoja na Mungu, kutumia nyenzo ambazo Yeye ametoa. Kisha tunapaswa kuomba kwamba Mungu abariki mbinu hizi. Tunamwamini Mungu; Tunaamini katika Mungu anayesikia na kujibu maombi. Alisema, Mathayo 7:7 Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa; -Medical Ministry, 13.

Kristo Ndiye Mponyaji Mkuu (Ministry of Healing, 22, 233, 244; Gospel Workers, 44; Counsels on Health, 30); the Great Medical Missionary (Ministry of Healing, 267; 8 Testimonies, 201-202, 206; 9 Testimonies, 170); Anatamani kuitumia nguvu Yake ya uponyaji kupitia watumishi Wake watiifu (Desire of Ages 823- 824; Counsels on Health 30; 9 Testimonies 178).

4. JIANDIKISHE KATIKA MOJA AU ZAIDI, YA SHULE ZIFUATAZO ZA UMISHENARI WA TIBA

[1] – NENO LA MUNGU

SOMO LA BIBLIA“Kuna kazi ya thamani sana inayopaswa kufanywa kuhusiana na matamanio ya kituo cha afya (Sanitarium) na Shule ya Loma Linda; Na hii itafanywa wakati wote watafanya kazi hadi mwisho huo. Neno la Mungu linapaswa kuwa kitabu chetu cha kujifunzia-kitabu cha Kiada. - Medical Ministry, 59.

Kutoka kwenye somo la Neno la uzima, wanafunzi wanaweza kuja na akili zilizotanuka, zilizoinuliwa, na zilizoboreshwa. Ikiwa wao ni kama Danieli, yaani wasikilizaji na watendaji wa Neno la Mungu, wanaweza kusonga mbele kama yeye alivyofanya katika matawi yote ya elimu au mafunzo. Wakiwa na nia safi, watakuwa na akili yenye nguvu na nia thabiti. Kila kitivo cha kiakili kitahuishwa. Wanaweza kujielimisha na kujinidhamisha kiasi kwamba wote walio ndani ya uwanja wa ushawishi wao, nao wataona jinsi mwanadamu anavyoweza kuwa, na kile anachoweza kufanya, akiunganishwa na Mungu Mwenye hekima na nguvu zisizo na ukomo.—Ministry of Healing, 466.

SOMO LA MAISHA YA YESU— “Yafanye maisha ya Kristo kuwa funzo lako la kudumu-endelevu, na fanya kazi kama alivyofanya Masihi, ukifuata mfano Wake.” -Welfare Ministry, 128.

Je! Ndugu na dada zangu, mnajiuliza kwamba: Tuige mfano gani? Siwaelekezi kwa watu wakubwa na wazuri, bali kwa Mkombozi wa ulimwengu. Ikiwa tunahitaji kuwa na roho ya Kweli ya umishenari lazima tujazwe na upendo wa Kristo; lazima tumwangalie Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yetu, tujifunze tabia Yake, tukuze Roho Yake ya upole na unyenyekevu, na kutembea katika nyayo Zake. Shuhuda kwa Kanisa 5: 385.

[2] – SOMO LA HEKIMA YA YESU YA TIBA/KITABIBU

Kitabu Huduma ya Uponyaji (Ministry of Healing) kinaweza kufanya kazi ileile kwenye huduma zetu za Sanitariamu na taasisi za afya ambayo 'Vielelezo vya maisha ya Kristo' (Christ's Object Lesson) kimefanya kwa shule zetu. Kitabu hiki kimejumuisha hekima za Tabibu Mkuu. Shuhuda kwa Kanisa 9: 71

[3] – SHULE YA NYUMBANI

"Wengi wanaotamani kupata ujuzi katika njia za umishenari wa tiba wana kazi za nyumbani ambazo nyakati fulani huwazuia kukutana na wengine kwa ajili ya kujifunza. Hawa wanaweza kujifunza mengi katika nyumba zao wenyewe kuhusiana na mapenzi ya Mungu ya wazi kuhusu nyanja hizi za kazi ya umishenari, hivyo kuongeza uwezo wao wa kuwasaidia wengine. Akina baba na akina mama, pateni msaada wote uwezao kutokana na masomo ya vitabu na machapisho yetu. Chukua muda wa kuwasomea watoto wako kutoka kwenye vitabu vya afya, na pia kutoka kwenye vitabu vinavyoshughulikia zaidi masomo ya kidini/kiroho. Wafundishe umuhimu wa kutunza mwili, ambao ndiyo nyumba wanayoishi. Unda mduara wa kusoma nyumbani, ambamo kila mwanafamilia ataweka kando mahangaiko yenye shughuli nyingi ya siku hiyo na kuungana katika masomo, naam mafunzo. Akina baba, akina mama, kaka, dada, beba kazi hii kwa moyo wote, na kujionea wenyewe kama kanisa la nyumbani halitaboreshwa sana." - Counsels on Health, 427.

"Tangu mwanzo wa akili, akili ya mwanadamu inapaswa kuwa na akili mahiri kuhusiana na muundo/mfumo wa kimwili. -Medical Ministry, 221.

"Wazazi wanapaswa kutafuta kuwavutia watoto wao katika masomo ya fiziolojia (Seli, tishu na ogani za mwili na zinavyohusiana katika kufanya kazi zake). Kuna wachache tu kati ya vijana ambao wana ujuzi wowote wa mafumbo na siri za maisha, uzima au uhai. Utafiti wa kiumbe cha ajabu kiitwacho mwanadamu, uhusiano na kutegemeana kwa sehemu zake ngumu kwa kinagaubaga, ni moja ya yale ambayo wazazi wengi wanaweka shauku ndogo sana. - Counsels on Health, 428.

“Hebu watu wetu waonyeshe kwamba wanapenda kazi ya umishenari wa tiba. Hebu wajiandae kuwa watu wa manufaa kwa kusoma vitabu ambavyo vimeandikwa kwa mafundisho yetu katika kazi hii na nyanja hii ya umishenari wa tiba.” -Counsels on Health, 426.

"Soma machapisho ya waandishi bora zaidi juu ya mada hizi, na utii kwa uadilifu, kwa uendelevu na bidii kile ambacho busara na akili yako inakuambia ni Ukweli." - Counsels on Health, 566.

"Jifunze kutafakari na pia kusoma, ili akili zako ziweze kupanuka, kuimarika, na kukua." - Counsels on Health, 405.

Zipo njia nyingi ambazo maji yaweza kutumika kutuliza maumivu na kuzuia ugonjwa. Watu wote wapaswa kuwa na utambuzi katika maarifa ya matumizi ya tiba rahisi majumbani mwao. Hasa akina mama, wanapaswa kujua jinsi ya kutunza familia zao katika hali za afya na maradhi. Ministry of Healing, 237.

“Baba na mama, mnatambua umuhimu wa majukumu yaliyo juu yenu? Je, unatambua umuhimu wa kuwalinda watoto wako dhidi ya tabia kuvunja moyo, zenye kukatisha tamaa? Ruhusu watoto wako kujumuika tu na makundi ambayo yatakuwa na ushawishi unaofaa kwa ajili ya tabia zao. Usiwaruhusu kuwa nje jioni isipokuwa unajua walipo na wanafanya nini. Waelekeze kwenye kanuni za usafi wa kimaadili.

Ikiwa umepuuza kuwafundisha mstari juu ya mstari, kanuni juu ya kanuni, hapa kidogo na pale kidogo, anza mara moja kufanya wajibu wako. Chukua majukumu yako, na ufanye kazi kwa ajili ya sasa na umilele. Usiruhusu siku ipite bila kutubia upuuziaji wako kwa watoto wako. Waambie kwamba umeamua sasa kufanya kazi yako uliyowekewa na Mungu. Waambie washikamane nawe katika matengenezo. Fanya juhudi za dhati kuukomboa wakati uliopita . .

“Unapofanya wajibu wako kwa uaminifu nyumbani, Baba akiwa kuhani wa nyumbani, Mama kama mmishonari wa nyumbani, unaongeza mawakala kwa ajili ya kufanya mema nje ya nyumba.”— -Counsels on Health, 429-430.

"Kazi ya mama huanza na mtoto mchanga mikononi mwake. Mara nyingi nimemwona mtoto mdogo akijitupa, na kujigaragaza na kupiga kelele, kwa kuwa mapenzi au chaguzi zake zimekatazwa au wazazi wamekatiza njia yake kwa namna yoyote. Huu ni wakati wa kukemea roho mchafu. Adui atajaribu kudhibiti akili za watoto wetu, lakini je, tutamruhusu kuwafinyanga kulingana na mapenzi yake?” -Fundamentals of Healings, 334-335.

Kuna kazi kwa akina mama ya kuwasaidia watoto wao kujenga tabia sahihi na kuwa na ladha iliyotakaswa. Elimisha hamu ya kula (appetite); wafundishe watoto kuchukia vichocheo (pombe zote, mfano -mbege, chai nyeusi ya china, kahawa, pilipili, na vyakula vilivyokolezwa viungo sana). Wakuze watoto wako ili wawe na uimara wa kimaadili kwamba waweze kupinga uovu unaowazunguka. Wafundishe kutoshawishiwa au kupindishwa na watu wengine, kwamba wasikubali kuathiriwa na mvuto wenye nguvu, bali wawashawishi watu wengine kwa wema. Ministry of Healing, 334-335.

“Pepo la kutokuwa na kiasi lina nguvu kubwa, na si rahisi lishindwe. Lakini ikiwa wazazi wataanza kupambana dhidi yake kwenye maeneo ya sebule zao wakati wanakota moto wakati wa baridi katika familia zao wenyewe, katika kanuni wanazowafundisha watoto wao tangu wakiwa wachanga sana, basi wanaweza kutumaini mafanikio. Itawapa faida, akina mama, kutumia saa za thamani ambazo mmepewa na Mungu katika kujenga tabia za watoto wenu, na kuwafundisha kuzingatia kikamilifu au kwa ukali kanuni za kiasi katika kula na kunywa. -Fundamentals of Healings, 143.

"Lishe huathiri afya ya mwili na maadili. Basi, ni kwa uangalifu kiasi gani, wakina mama wanapaswa kujifunza, jinsi ya kuandaa chakula rahisi zaidi, na chenye afya, ili viungo vya usagaji wa chakula visiwe dhaifu, mishipa ya fahamu au neva iwe timamu au na msawaziko mzuri, au maagizo wanayowapa watoto wao yasipunguzwe nguvu yake au kuhafifishwa. Fundamentals of Healings, 143.

Usipuuze kufundisha watoto wako jinsi ya kupika (Yakobo na Esau walipika!). Kwa kufanya hivyo, unawapa kanuni ambazo lazima wawe nazo katika elimu yao ya kidini au kiroho. Katika kuwapa watoto wako masomo katika fiziolojia, na kuwafundisha kupika kwa urahisi na bado kwa ustadi, unaweka msingi wa matawi muhimu zaidi ya elimu. Shuhuda kwa Kanisa 2: 537.

Wana heri (furaha) wazazi ambao maisha yao yanaakisi tabia halisi ya Mwenyezi Mungu, ili ahadi na amri za Mungu ziamshe katika mtoto shukrani na kicho; wazazi ambao huruma, ulaini, haki na uadilifu na ustahimilivu hutafsiri kwa mtoto upendo na haki na uvumilivu wa Mungu, basi ni hakika kwa kumfundisha mtoto kuwatii wao, wazazi humfundisha mtoto kumpenda, kumwamini na kumtii Baba yake wa mbinguni. Wazazi wanaompa mtoto zawadi kama hiyo wanakuwa wamemkrimia hazina yenye thamani zaidi kuliko utajiri wa zama zote—hazina inayodumu milele zote. Ministry of Healing, 375-376

(Soma haswa: 7 Testimonies, 62-67, Counsels on Health, 425-430; Child Guidance, 339-470; Adventist Home, 251-263; Ministry of Healing, 349-408.)

[4] - SHULE ZA UMISHENARI WA TIBA ZA KANISA MAHALIA

"Kazi ya Umishenari Wa Tiba Inapaswa Kuwa Sehemu Ya Kazi Ya kila kanisa katika nchi yetu." -Counsels on Health, 514.

“Wachungaji na walimu wanapaswa kufanya kazi kwa akili mahiri katika nyanja zao, wakiwaelekeza washiriki wa kanisa jinsi ya kufanya kazi katika nyanja za umishenari za tiba. Wakati wale wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo wanapokuwa na Mwokozi anayekaa ndani yao, watapatikana wakifanya kama Kristo alivyofanya. Hawatakuwa na nafasi ya Kula kutu kwa uzembe wa kukaa kivivu bila ya kuchangamkia kazi.” -Welfare Ministry, 123.

“Kwa ndugu zangu wahudumu/wachungaji ningesema, Fanya kazi hii kwa busara na uwezo. Wapangieni kazi vijana wa kiume na wa kike katika makanisa yetu. Unganisha kazi ya umishenari wa tiba na hubiri/tangazo la ujumbe wa malaika wa tatu. Fanya juhudi za kimkakati mara kwa mara, ili kuyainua makanisa yaliyoangukia kifoni, ili yatoke kwenye shimo hilo la mfu, na wamekaa humo shimoni kwa miaka. Tuma kwenye makanisa watendakazi wa kanisa ambao wataweka kanuni za matengenezo ya afya wakiyaunganisha na ujumbe wa malaika wa tatu mbele ya kila familia na watu binafsi. Wahamasishe watu wote kushiriki katika kazi kwa ajili ya wanadamu wenzao, na kujionea mwenyewe kama pumzi ya uhai haitarudi haraka kwenye makanisa haya. -Welfare Ministry, 124.

Kila kanisa linapaswa kuwa shule ya mafunzo kwa watenda kazi Wakristo. Washiriki wake wanapaswa kufundishwa jinsi ya kuwasilisha masomo ya Biblia-(Kusoma Biblia-Bible readings), jinsi ya kuongoza na kufundisha madarasa ya shule ya Sabato, namna bora ya kuwasaidia watu maskini, na kuwahudumia wagonjwa, na jinsi ya kushughulika na wale ambao bado hawajaongoka. Hatuna budi kuwa na shule za afya, shule za mapishi, na madarasa katika safu mbalimbali za kazi saidizi ya Kikristo. Hatupaswi kuwa na ufundishaji tu, bali pia kazi halisi inapaswa ifanyike chini ya waalimu wenye uzoefu. Walimu na waongoze njia katika kufanya kazi miongoni mwa watu, na wengine kwa kuungana nao, watajifunza kutokana na kielelezo chao. Kielelezo kimoja kina thamani zaidi kuliko maelekezo mengi. Ministry of Healing, 149 (Welfare Ministry, 105-112).

[5] - SHULE ZA UMISHENARI WA TIBA KWENYE MKUTANO WA KAMBI NA MIKUSANYIKO MINGINE MIKUBWA

"Katika mikusanyiko yetu mikubwa, maelekezo yanapaswa kutolewa juu ya afya na kiasi. Kusudia kuamsha akili na dhamiri. Waamuru kuwa vipaji vyote viletwe kwenye huduma, na kufuatilia masomo ya kazi ya machapisho. 'Elimisha, elimisha, elimisha,' ndio ujumbe ambao umesisitizwa juu ya moyo wangu. -Counsels on Health, 449.

"Katika mkutano wa kambi, maagizo juu ya mada za afya yanapaswa kutolewa kwa watu. Katika mikutano yetu huko Australia, mihadhara juu ya masomo ya afya ilitolewa kila siku, na shauku kubwa iliamshwa. -Counsels on Health, 467.

Lakini kwenye hafla kama za mikutano yetu ya makambi ya kila mwaka hatupaswi kamwe kupoteza fursa ya kuwafundisha waumini jinsi ya kufanya kazi ya umishenari kwa vitendo mahali watakapoweza kuishi. Katika hali nyingi itakuwa vizuri kuwatenga watu fulani kubeba mzigo wa kazi za aina mbalimbali za elimu katika hii mikutano. Hebu wengine wawasaidie watu kujifunza jinsi ya kusoma Biblia na kuendesha mikutano ya nyumba kwa nyumba. Hebu wengine waubebe mzigo wa kuwafundisha watu jinsi ya kutekeleza kanuni za afya na kiasi, na jinsi ya kutoa tiba rahisi kwa wagonjwa. Bado wengine wanaweza kufanya kazi kwa masilahi yetu ya kazi ya machapisho na kazi ya vitabu. Shuhuda kwa Kanisa 9: 82-83.

[6] - SHULE ZA KUFUNDISHA UINJILISTI WA KUHUBIRI

Mikutano ya awali ya kambi ilikuwa, kwa kweli, juhudi za uinjilisti. (Tazama Evangelism, 21, Footnote.) Walihamishwa kutoka mahali hadi mahali, na kwa kiasi kikubwa ilihudhuriwa na wasio washiriki. Kwa hivyo mashauri yaliyonukuliwa hapo juu yangetumika pia kwa shule za mafunzo ya Efoti za kiinjilisti. (Soma Evangelism, 107-110, kwa zaidi juu ya maeneo haya.)

[7] - VITUO VYA AFYA (SANITARIUMS) VYA NCHI: SHULE ZA UMISHENARI WA TIBA ZILIZOUNGANISHWA

"Bwana ameniagiza kuwaonya wale ambao katika siku zijazo wataanzisha vituo vya afya katika sehemu mpya, waanze kazi yao kwa unyenyekevu, wakiweka wakfu uwezo wao kwa utumishi Wake. Majengo au miundo mbinu wanayoiweka haipaswi kuwa mikubwa au ghali. Vituo vya afya (Sanitarium) mahalia vinapaswa kuanzishwa kwa kuunganishwa na shule zetu za mafunzo. Katika vituo hivi vya afya vijana wa kiume na wa kike wenye uwezo na kujitoa wakfu wanapaswa kukusanywa—wale watakaojiendesha kwa mwenendo wa upendo na hofu ya Mungu, wale ambao, wakiwa wamejitayarisha kwa ajili ya kuhitimu, hawatahisi kwamba wanajua yote wanayohitaji kujua, lakini watajifunza kwa bidii na

kufanyia mazoezi kwa uangalifu masomo yaliyotolewa na Kristo. Haki ya Kristo itawatangulia watu kama hao, na utukufu wa Mungu utawafuata.” -Counsels on Health, 220.

“Bwana anatoa wito kwa vijana wetu kuingia katika shule zetu na kujipatia stahiki kwa ajili ya huduma. Katika sehemu mbalimbali, nje ya miji, shule zinapaswa kuanzishwa, ambapo vijana wetu wanaweza kupata elimu ambayo itawatayarisha kwenda kufanya kazi za kiinjilisti na kazi ya umishenari wa tiba.- Counsels on Health, 395.

"Ninashukuru ninapofikiria faida zinazofurahiwa na shule ambazo zimeanzishwa karibu na vituo vyetu vya afya, ili kazi ya taasisi hizo mbili za elimu iweze kuunganishwa. Wanafunzi katika shule hizi, huku wakipata elimu katika ujuzi wa Ukweli uliopo, wanaweza pia kujifunza jinsi ya kuwa wahudumu wa uponyaji kwa wale wanaotoka kwenda kutumikia wanadamu. -Counsels on Health, 542.

"Kutoka kwenye vituo vyetu vya afya watendakazi waliofunzwa wanapaswa kwenda mahali ambapo Ukweli haujawahi kutangazwa, na kufanya kazi ya umishenari kwa ajili Bwana." - Medical Ministry, 323.

“Bwana asema hivi: ‘Majengo yatatoa tabia kwa kazi Yangu pale tu wale wanaoyasimamisha watafuata maagizo Yangu kuhusiana na kuanzishwa kwa taasisi. Kama wale ambao wamesimamia na kudumisha kazi hiyo hapo awali daima wangedhibitiwa na kanuni safi, zisizo na ubinafsi, kamwe kusingekuwa na kujikusanyia kwa ubinafsi sehemu kubwa ya mali Zangu katika sehemu moja au mbili. Taasisi zingeanzishwa katika maeneo mengi mahalia. Mbegu za kweli, zilizopandwa katika mashamba mengi zaidi, zingechipuka na kuzaa matunda kwa utukufu Wangu.....

Nitainua mawakala ambao watatekeleza mapenzi Yangu ya kuandaa watu ili kusimama mbele Yangu wakati wa mwisho.

Katika maeneo mengi ambayo kabla ya haya yalipaswa kuwa yametolewa kwa ajili ya vituo vya afya na shule. Nitaanzisha na kuziimarisha taasisi Zangu, na taasisi hizi zitakuwa vituo vya elimu kwa ajili ya mafunzo ya watendakazi. - Counsels on Health, 226-227.

[8] - SHULE NJE YA JIJI

“Haki ya Kristo itawatangulia watu hao, na utukufu wa Mungu utawafuata.” - Counsels on Health, 220

“Bwana anatoa wito kwa vijana wetu kuingia katika shule zetu na kujipatia stahaki kwa kadri ifaavyo kwa ajili ya huduma. Katika sehemu mbalimbali, nje ya miji, shule zinapaswa kuanzishwa na kuimarishwa, mahali ambapo vijana wetu wanaweza kupata elimu ambayo itawatayarisha kwenda kufanya kazi za kiinjilisti na kazi ya umishenari wa tiba-Counsels on Health, 395.

[9] – SHULE ZA MAFUNZO YA UTUME/MISHENI YA JIJI

Utume wetu unapaswa kuunganishwa na shule za mafunzo kwa wale ambao wanakaribia kuingia shambani mwa Bwana kama watendakazi. Watu wanapaswa kuhisi uhitaji wa lazima wa kuwa wanafunzi walio chini ya mtu mwenye ujuzi ili kujifunza kazi ya kufanya yaani kazi kwa ajili ya kuongoa roho (mentors/washauri na wanagenzi/apprentices)." -Evangelism, 107.

“Katika taasisi zetu zote za afya, maelekezo kuhusu sheria za afya yanapaswa kutolewa na kufanywa kuwa kipengele maalum cha kazi. Kanuni za matengenezo ya afya zinapaswa kuwekwa kwa uangalifu na kwa kina mbele ya wote, wagonjwa na pia wasaidizi. -Counsels on Health, 452.

Wakati utume wa miji unapaswa kuanzishwa mahali ambapo wainjilisti wa vitabu, wafanyakazi wa Biblia, na wamishenari wa tiba wanaweza kufundishwa kuyafikia matabaka fulani, lazima pia, katika miji yetu, tuwe na wainjilisti waliowekwa wakfu ambao kupitia kwao ujumbe unapaswa kutolewa kwa uthabiti na kuazimia ili kuwashtua wasikilizaji. Shuhuda kwa Kanisa 9: 137.

[10]- BASI ANZA KAZI YAKO KATIKA SHULE YENYE UZOEFU

Hebu mtu asiziachilie fursa ndogo-ndogo zimpite, eti kwa sababu anatafuta fursa kubwa zaidi. Unaweza kufanya kazi ndogo kwa ufanisi mkubwa, lakini ukashindwa kabisa hata kule kuifanya kazi iliyo kubwa, na kuanguka kwenye mvunjiko wa moyo. Ni kwa kufanya kwa uwezo wako wote kile ambacho mkono wako unapata kukifanya, ndipo unakuza umahiri wa kufanya kazi kubwa zaidi. Ni kwa kudharau fursa za kila siku, kwa kupuuzia mambo madogo yaliyopo karibu nawe, ndivyo watu wengi wanakosa kuzaa matunda na kunyauka. Usitegemee msaada wa mwanadamu. Angalia ng’ambo ya wanadamu mpaka kwa Yule aliyeteuliwa na Mungu ili kubeba majonzi na huzuni zetu, na kututimizia mahitaji yetu. Huku ukimwamini Mungu kama alivyosema katika Neno Lake, kuwa na mwanzo mpya popote pale unapopata kazi ya kufanya, na kisha songa mbele kwa imani isiyoyumba-yumba. Ni imani katika uwepo wa Kristo ndiyo inayotia nguvu na uthabiti. Tenda kazi isiyo na maslahi ya kukunufaisha wewe tu, nawe uifanye kwa juhudi madhubuti, na kwa nguvu yenye ustahimilivu. Katika maeneo ambayo

hali ni zenye kuchukiza na zenye ukinzani, na kukatisha tamaa sana kiasi kwamba wengi wanayaepuka, yaani hawako radhi kwenda huko, mabadiliko makubwa yametokea kutokana na jitihada za watendakazi wenye kujidhabihu nafsi zao. Kwa subira na ustahimilivu wametenda kazi, bila kutegemea nguvu za kibinadamu, bali Mungu, na neema Yake iliwategemeza. Kiasi cha mafanikio mema yaliyotimizwa kwa namna hiyo kamwe hakitajulikana katika ulimwengu huu, lakini matokeo yenye baraka yataonekana baada ya maisha haya kule mbinguni. —Ministry of Healing, 153-154.

"Kote karibu nasi ipo milango wazi kwa huduma. Tunapaswa kufahamiana na jirani zetu, na kutafuta kuwavuta kwa Kristo. Tunapofanya hivyo, Kristo ataidhinisha huduma yetu na kushirikiana nasi."— Counsels on Health, 396.

"Mbele ya mwanamatengenezo wa kweli, kazi ya umishenari wa tiba itafungua milango mingi. Asiwepo mtu anayehitaji kusubiri hadi aitwe kwenye eneo fulani la mbali kabla ya kuanza kuwasaidia wengine (kama vile nchi za nje). Popote pale ulipo, unaweza kuanza kazi mara moja. Fursa ziko ndani ya kila mtu. Chukua kazi ambayo unawajibika kwayo—kazi inayopaswa kufanywa nyumbani kwako na katika ujirani wako. Usisubiri wengine wakusihi uchukue hatua na kuwa mtendaji. Katika kumcha Mungu songa mbele bila ucheleweshe, ukizingatia wajibu wako binafsi kwa Yule aliyetoa maisha Yake kwa ajili yako. Tenda kana kwamba umemsikia Kristo akikuita wewe binafsi kufanya uwezavyo katika huduma Yake. Usiangalie kuona kwamba ni nani mwingine aliye tayari. Ikiwa umewekwa wakfu kamili, Bwana kwa njia ya utendaji wako, atawaleta katika ile Kweli watu wengine ambao anaweza kuwatumia kama njia za kuwaletea wengi nuru wanaopapasa gizani." -Counsels on Health, 425-426.

"Kilio cha mtu wa Makedonia kinakuja na kusikika katika kila kona. Je watu watakwenda katika kazi za kawaida ili kuona kama wataruhusiwa kufanya kazi, au kama wataenda na kufanya kazi kwa ubora kwa kadiri wawezavyo, kulingana na uwezo wao wenyewe na kwa msaada wa Mungu, wakianza kwa unyenyekevu na kuhamasisha shauku ya watu katika Ukweli kwenye maeneo ambayo hakuna kitu ambacho kimefanywa kutoa ujumbe wa onyo? -Medical Ministry, 321.

Mungu anatoa wito kwa kuwaita watendakazi. Kazi inahitaji watu ambao wamekuwa na jitihada binafsi za kuinuka katika kufanikisha mambo, ambao wakijiweka mikononi mwa Bwana kama wanafunzi wanyenyekevu, wamejidhihirisha kuwa watendakazi pamoja Naye. Hawa ndio watu wanaohitajika katika huduma na katika kazi ya shule. Hebu wale ambao wamejionesha kuwa watu mashujuaa waondoke na kufanya kile wawezacho

katika utumishi wa Bwana. Hebu waingie kwenye jeshi la watendakazi na kwa subira na bidii endelevu wathibitishe kustahili kwao. Huwa tunajifunza kuogelea ndani ya maji na wala sio nchi kavu au kwenye ardhi. Shuhuda kwa Kanisa 7: 280-281.

[11] - TUNAONYWA TUSITUMIE MIAKA MINGI KUJIANDAA KWA KAZI YA MUNGU

Miongoni mwetu wapo vijana wengi wa kiume na wa kike ambao, kama wangepewa vivutio, wangechukua mwelekeo wa kawaida kusoma kwa miaka kadhaa masomo yatakayowaandaa kustahili kufanya kazi ya utumishi. Lakini Je, hii italipa? Muda ni mfupi. Watenda kazi kwa ajili ya Kristo wanahitajika kila mahali. Kunapaswa kuwa na watenda kazi dhati, waaminifu na wenye bidii mia moja nyumbani na kwenye maeneo ya utume ugenini ambako sasa yupo mmoja tu. Njia kuu na njia ndogo bado hazijafanyiwa kazi. Vivutio vya haraka vinapaswa kutolewa kwa wale ambao sasa wanapaswa kushiriki katika kazi ya Bwana. Shuhuda kwa Kanisa 8: 229.

Vijana wanapaswa kutiwa moyo kuhudhuria shule zetu za mafunzo kwa ajili ya watendakazi wa Kikristo, ambazo zinapaswa kufanana zaidi na zaidi na shule za manabii. Taasisi hizi zimeanzishwa na Bwana, na zikiendeshwa kwa kupatana na kusudi Lake, vijana waliopelekwa hapo watatayarishwa haraka kushiriki katika mielekeo mbalimbali ya kazi ya umishenari. Wengine watafunzwa kuingia shambani kama wauguzi wamishenari, wengine kama wainjililisti wa vitabu nyumba kwa nyumba, na wengine kama wachungaji au wahudumu wa injili. Shuhuda kwa Kanisa 8: 230.

“Vijana wa kiume na wa kike, jikusanyieni maarifa mengi. Usisubiri hadi uchunguzi wa kibinadamu utamke kwamba wewe una uwezo wa kufanya kazi, lakini nenda kwenye barabara kuu na njia panda, na uanze kufanya kazi kwa ajili ya Mungu. Tumia kwa busara maarifa uliyonayo. Tumia uwezo wako kwa uadilifu, ukitoa nuru ambayo Mungu amekupatia kwa ukarimu. Fahamu jinsi bora ya kuwapatia wengine amani, nuru, Ukweli na baraka zingine nyingi za mbinguni. Piga hatua daima, songa mbele kwa kujiboresha. Endelea kufikia juu na juu zaidi. Ni uwezo wa kuweka katika uwajibikaji nguvu za kiakili na kimwili daima, ukizingatia uhalisia milele katika fikra, hilo ndilo lenye thamani sasa. Mtafute Bwana kwa bidii zaidi, ili uweze kutakaswa zaidi na zaidi, na kuboreshwa kielimu/kiutamaduni zaidi. Ndipo utakuwa na cheti cha shahada yenye sifa na ubora sana kuzidi ile mtu ye yote anayoweza kuwa nayo—uthibitisho wa Mungu. Shuhuda kwa Kanisa 7: 281.

“Huhitaji kwenda miisho ya dunia kwa ajili ya hekima, kwa maana Mungu Yuko karibu. Sio uwezo ulio nao sasa au utakaokuwa nao baadaye, ndio ambao utakupa mafanikio. Ni yale tu ambayo Bwana anaweza kukufanyia. Tunahitaji kuwa na imani ndogo sana katika kile ambacho mwanadamu anaweza kufanya na kuwa na imani na ujasiri zaidi katika kile ambacho Mungu anaweza kufanya kwa kila nafsi inayoamini. Bwana Anatamani umfikie Yeye kwa imani. Anatamani kuwa na wewe na kutarajia mambo makubwa kutoka Kwake. Bwana Anatamani kukupa wewe ufahamu katika mambo ya kimwili na ya kiroho pia. Yeye anaweza kunoa ubongo- Anaweza kuimarisha akili. Anaweza kutoa busara, mbinu na ujuzi. Weka talanta zako katika kazi, mwombe Mungu hekima, nawe utapewa. -Christ’s Object Lessons, 146.

Kazi hii inahitaji kujitoa/kujidhabihu. Wakati wengi wakingoja kila kizuizi kiondolewe, kazi ambayo wangeweza kuifanya inaachwa bila kutimizwa, na umati mkubwa wa watu unakufa bila tumaini na bila Mungu. —Ministry of Healing, 156

“Mazoea ya kuwapa watu wachache kila fursa ili kukamilisha elimu yao katika nyanja nyingi sana ambazo hawawezi kuzitumia zote, ni jeraha badala ya kuwa na faida kwa yule ambaye ana fursa nyingi, hivyo kuwanyima wengine fursa wanazohitaji sana. Badala ya kuwa na maandalizi ya muda mrefu, ibada isiyo ya kipekee sana ya kusoma tu, kungekuwa na fursa zaidi ya kuongezeka kwa imani ya mwanafunzi katika Mungu. Yeye ambaye kwa muda mrefu hutumia nguvu zake zote kwa masomo yake peke yake, na anavutiwa kupita kawaida, - kwa kweli hushinda katika vitabu vyake, na kupoteza lengo ambalo alianza nalo wakati alipokuja shuleni. Imeonyeshwa kwangu kwamba baadhi ya wanafunzi wanapoteza hali yao ya kiroho, kwamba imani yao inazidi kuwa dhaifu, na kwamba hawana ushirika endelevu na Mungu. Wanatumia karibu muda wao wote katika usomaji au uchunguzi wa vitabu; Wanaonekana kutojua kitu kingine chochote zaidi ya hivyo vitabu. Lakini maandalizi haya yote yatakuwa na faida gani kwao? Je, watapata faida gani kwa muda na pesa zote zinazotumika? Nakuambia, faida itakuwa mbaya zaidi kuliko kupoteza. Lazima wasitegemee sana katika kazi ya hivi, badala yake imani zaidi katika nguvu za Mungu. Watu wanaopenda amri ya Mungu wanapaswa kushuhudia ulimwengu kwa imani yao kwa matendo yao.” -Fundamentals of Christian Education, 336-337.

“Katika kazi hii ya mwisho ya kuhitimisha Injili, kuna uwanja mkubwa wa kushughulikiwa; Na, zaidi ya hapo awali, kazi inapaswa kuwa na wasaidizi kutoka katika watu wa kawaida. Vijana na wale wale waliokuwa watu wazima, wataitwa kutoka shambani, kutoka shamba la mizabibu, na kutoka kwenye karakana, na kutumwa na Bwana ili kutoa ujumbe Wake. Wengi wa hawa wanaweza kuwa na nafasi ndogo ya elimu, lakini Kristo anaona ndani yao sifa ambazo zitawawezesha kutimiza kusudi Lake. Ikiwa wataweka mioyo yao katika kazi na kuendelea kuwa

wanafunzi, Yeye atawastahilisha kufanya kazi kwa ajili Yake. -Welfare Ministry, 108- 109.

“Watendakazi—wamishenari wa tiba wa injili—wanahitajika sasa. Huwezi kumudu kutumia miaka katika maandalizi. Hivi karibuni milango iliyofunguliwa kwa ajili ya ile Kweli itafungwa milele. Beba ujumbe sasa. Usisubiri, kuruhusu adui kumiliki mashamba yaliyo wazi kwa sasa mbele yako. Hebu vikosi vidogo viende kufanya kazi ambayo Kristo aliwateua wanafunzi Wake. Hebu wafanye kazi kama wainjilisti, kutawanya machapisho yetu, na kuzungumza juu ya Ukweli kwa wale wanaokutana nao. Hebu na waombee wagonjwa, wakihudumia mahitaji yao, si kwa njia ya madawa ya famasia, bali kwa njia ya dawa za asili, na kuwafundisha jinsi ya kurejesha afya na kuepuka magonjwa.” - Counsels on Health, 397.

“Hebu na wanuie kuwatibu wagonjwa, kwa kuwa wana nafasi, wakitekeleza kwa vitendo nadharia waliyojipatia kutokana na kusoma vitabu. Nimeagizwa kwamba katika hali nyingi ujuzi zaidi wa vitendo unaweza kupatikana kwa njia hii kuliko kwa kozi ndefu ya masomo katika shule ya tiba/udaktari. - Medical Ministry, 84.

(For additional study: Fundamentals of Christian Education, 334-367, “Speedy Preparation for the Work”; 3 Testimonies, 323-324; 5 Testimonies, 22; Counsels on Health, 395; Counsels to Parents, Teachers, and Students, 404-419)

SURA YA 6

JINSI VIKUNDI VIDOGO VYA WAMISHENARI WA TIBA VINAVYOPASWA KUFANYA

Mwongozo wa Uinjilisti wa Timu ya Wamishenari wa tiba

1. BAADHI YA MAMBO HALISI YA KUFIKIRIA

"Wakati unaoishi sasa una mambo ya kustaajabisha kwa kina, kwa wote wanaoishi ulimwenguni. Watawala na viongozi wa serikali, wanaume wanaoshika nyadhifa za uaminifu na mamlaka, wanaume na wanawake wenye akili mahiri wa tabaka zote, wamefuatilia matukio yanayotuhusu. Wanatazama mahusiano yenye migogoro, yasiyotulia na yaliyopo miongoni mwa mataifa. Wanaona kiwango ambacho kinachukua nafasi ya kila kipengele cha kidunia, na wanatambua kwamba jambo kubwa na la kuamua linakaribia kutokea, —kwamba ulimwengu uko kwenye ya mgogoro wa ajabu. -Education, 179.

“Malaika kwa sasa wanazuia pepo za migogoro mikali, ili zisivume mpaka ulimwengu uonywe juu ya maangamizi yake yanayokuja; Lakini dhoruba inakusanyika, tayari kupasuka juu ya nchi; Na Mungu atakapowaamuru malaika Wake kuziachia huru pepo, kutakuwa na tukio la hatari ambalo hakuna kalamu inayoweza kuliandika.”— Education, 179-180.

“Kazi ambayo ingepaswa kuwa katika utendaji, kazi wa kuvutia roho kwa Kristo haijafanywa kwa muda mrefu. Wakaaji wa majiji yasiyomcha Mungu ambayo yatatembelewa hivi karibuni na misiba wamepuuzwa kikatili. Wakati umekaribia ambapo miji mikubwa itafagiliwa mbali, na wote wanapaswa kuonywa kuhusu hukumu hizi zinazokuja. Lakini ni nani anayetoa onyo kwa ajili ya utimilifu wa kazi hii kwa utumishi unaohusisha moyo wote, jambo ambalo Mungu anahitaji?” - Welfare Ministry, 135.

Mataifa yote watakusanyika mbele Zake; Naye atawabagua." Hivyo ndivyo ambavyo Kristo alipokuwa kwenye Mlima wa Mizeituni aliwaonyesha wanafunzi Wake picha ya tukio la siku kuu ya hukumu. Na alionyesha kwamba uamuzi wa hukumu unageukia kwenye jambo moja tu. Wakati mataifa yote yatakapokuwa yamekusanywa mbele zake, kutakuwa na makundi mawili tu, na hatima yao ya

milele itaamuliwa na kile ambacho wamemfanyia au ambacho wamepuuza kumfanyia alipokuwa katika nafsi za maskini na wenye shida. Katika siku hii Yesu hawaonyeshi watu kazi kuu aliyowafanyia ya kuutoa uhai Wake kwa ajili ya ukombozi wao. Anaonyesha kazi ya uaminifu waliyofanya kwa ajili Yake. Atawaambia wale atakaowaweka mkono Wake wa kuume kwamba, "Njoni, mliobarikiwa na Baba Yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu; kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika." — Desire of Ages, 637.

2. KIKOSI CHA NYUMBANI

"Lazima tufanye mipango ya busara ya kuionya miji, na wakati huo-huo kuishi ambapo tunaweza kuwalinda Watoto wetu na sisi wenyewe dhidi ya ushawishi wa kuchafua na kukatisha tamaa ulioenea sana katika maeneo haya." -Evangelism, 76-77.

"Hebu Watu wenye busara/uamuzi mzuri wateuliwe, sio kwa kutangaza nia zao, bali kutumia viwango hivyo katika maeneo ya vijijini, kwa urahisi wa kupata miji, inayofaa kwa shule ndogo za mafunzo kwa watendakazi, na ambapo vifaa vinaweza pia kutolewa kwa ajili ya kutibu wagonjwa na watu waliochoka ambao hawajui Ukweli. Tafuta maeneo kama haya kutoka kwenye miji mikubwa. - Evangelism, 77.

"Biashara ya kwanza maishani mwako inapaswa kuwa mmishenari nyumbani."- Shuhuda kwa Kanisa 4: 138.

Ni lazima kaya zetu ziwe na utaratibu/mipango, na jitihada za bidii lazima zifanyike ili kuvutia kila mshiriki wa familia katika shughuli za umishenari. Ni lazima tutafute kuhusisha huruma za watoto wetu katika kazi ya dhati na bidii kwa ajili ya wale ambao hawajaokolewa, ili wafanye yote wawezayo nyakati zote na mahali pote kumwakilisha Kristo. Christian Service, 207.

Mbele ya mwanamatengenezo wa kweli, kazi ya umishenari wa tiba itafungua milango mingi. Asiwepo mtu anayehitaji kusubiri hadi aitwe kwenye eneo fulani la mbali kabla ya kuanza kuwasaidia wengine. Popote ulipo, unaweza kuanza mara moja. Fursa ziko ndani ya kila mtu. Chukua kazi ambayo unawajibika kwayo—kazi inayopaswa kufanywa nyumbani kwako na katika ujirani wako. Usisubiri wengine wakusihi uchukue hatua ya utendaji. Katika kumcha Mungu songa mbele bila kukawia, ukizingatia wajibu wako binafsi kwa Yule aliyetoa maisha Yake kwa ajili yako. - Counsels on Health, 425-426.

"Wote wanaweza kufanya kitu. Katika jitihada za kujitetea au kutoa udhuru, wengine husema, ‘Kazi zangu za nyumbani, watoto wangu, hudai wakati wangu na uwezo wangu.’ Wazazi, watoto wako wanapaswa kuwa mkono wako wa kusaidia, wakiongeza uwezo wako na uwezo wako wa kufanya kazi kwa ajili ya Bwana. Watoto ni washiriki wadogo wa familia ya Bwana. Wanapaswa kuongozwa kujiweka wakfu kwa Mungu, ambaye aliwaumba na kuwakomboa. Wanapaswa kufundishwa kwamba nguvu zao zote za mwili, akili, na nafsi ni Zake Bwana. Wanapaswa kufundishwa kusaidia katika nyanja mbalimbali ya huduma isiyo na ubinafsi. Usiruhusu watoto wako kuwa vizuizi. Pamoja na wewe watoto wanapaswa kushiriki mizigo ya kiroho na ya kimwili. Kwa kuwasaidia wengine wanaongeza furaha na utendaji wao wenyewe.”— Counsels on Health, 426.

“Kama katika kila kanisa watu wangejiweka wakfu Kwake Bwana, kama wangejizoeza kujikana nafsi nyumbani, wakimsaidia mama yao aliyetindikiwa na kazi, basi mama angeweza kupata wakati wa kufanya ziara za ujirani-mwema, na, fursa inapotolewa, wangeweza kutoa msaada wenyewe kwa kufanya kazi ndogo za rehema. na upendo. Vitabu na machapisho yanayoshughulikia suala la afya na kiasi vinaweza kuwekwa katika nyumba nyingi. Usambazaji wa maandishi haya ni jambo muhimu; Kwa maana hiyo ujuzi wa thamani unaweza kutolewa kuhusiana na jinsi ya kutibu magonjwa—maarifa ambayo yangekuwa baraka kubwa kwa wale ambao hawana uwezo wa kulipa fedha za kumwona daktari. -Counsels on Health, 428.

“Nenda kwa majirani zako mmoja baada ya mwingine, na uwe karibu nao mpaka mioyo yao ichangamke kwa kupendezwa na upendo wako usio na ubinafsi. Wahurumie, waombee, tazama fursa za kuwatendea mema, na kadri uwezavyo, wakusanya wachache kwa pamoja na ufungue Neno la Mungu kwa akili zao zenye giza. -Welfare Ministry, 87.

Ndugu na dada zangu, watembeleeni wale wanaoishi karibu nanyi, na kwa huruma na wema tafuta kufikia mioyo yao. Hakikisha unafanya kazi kwa namna ambayo itaondoa chuki badala ya kuitengeneza ubaguzi. — Shuhuda kwa Kanisa 9: 34-35.

"Kwa wote wanaofanya kazi na Kristo ningesema, popote unapoweza kupata watu karibu na nyumba, boresha fursa yako. Chukua Biblia yako, na ufungue mbele yao kweli Zake kuu. Mafanikio yako hayatategemea sana maarifa na mafanikio yako, kama vile uwezo wako wa kutafuta njia yako ya kuelekea moyoni mwa watu.” -Gospel Workers, 193.

"Kuna uwanja mpana wa huduma kwa wanawake na wanaume. Mpishi mwenye ufanisi, mshonaji, muuguzi—msaada wa watu wote unahitajika. Hebu wanafamilia maskini wafundishwe jinsi ya kupika, kutengeneza na kukarabati mavazi yao wenyewe, jinsi ya kuuguza wagonjwa, jinsi ya kutunza nyumba ipasavyo. Hata watoto wanapaswa kufundishwa kufanya kazi fulani ndogo ya upendo na rehema kwa wale wasiobahatika kama wao au walio wahitaji kuliko wao."— Welfare Ministry, 75.

Wakati mioyo ya wanadamu inapohurumia mioyo iliyolemewa na kukatishwa tamaa kwa huzuni, wakati mkono unanyooshwa ili kusaidia wahitaji, wakati walio uchi wanavikwa, na mgeni anakaribishwa kwenye kiti sebuleni mwako na anapewa nafasi moyoni mwako, malaika wanasogea karibu zaidi, na kila ombi lililoelekezwa mbinguni hujibiwa. Kila tendo la haki, huruma, na ukarimu huleta nyimbo mbinguni. — Shuhuda kwa Kanisa 2: 25.

"Kazi ya umishenari wa tiba ndiyo kazi inayotangulia injili, mlango ambao Ukweli kwa wakati huu utapata upenyo kwenye nyumba nyingi. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa wamishenari wa kweli wa tiba, kwa kuwa wanapaswa kujifunza kuhudumia mahitaji ya nafsi na mwili. Kutokuwa na ubinafsi kwa moyo wa dhati kunapaswa kuonyeshwa na watendakazi wetu kwani, kwa ujuzi na uzoefu unaopatikana kwa kazi ya vitendo, wanatoka kwenda kutoa tiba kwa wagonjwa. Wanapoenda nyumba kwa nyumba wataifikia mioyo mingi. Wengi watafikiwa ambao vinginevyo, kamwe hawangesikia ujumbe wa injili. Welfare Ministry, 125.

"Bwana alinipa nuru kubwa juu ya matengenezo ya afya. Kuhusiana na mume wangu nilipaswa kuwa mtendakazi wa umishenari wa tiba. Nilipaswa kuwa mfano kwa kanisa kwa kuwapeleka wagonjwa nyumbani kwangu na kuwatunza. Hili nimefanya, kwa kuwapa wanawake na watoto tiba ya nguvu. -A Call to Medical Evangelism, 9.

"Mara nyingi unafuu wa mahitaji yao ya kimwili ndiyo njia pekee ambayo wanaweza kufikiwa. Welfare Ministry, 126.

"Mwasilishe Yesu kwa sababu unamjua Yeye kama Mwokozi wako binafsi. Acha upendo Wake unaoyeyusha, neema Yake tele, itiririke katika midomo ya mwanadamu. Huhitaji kuwasilisha hoja za mafundisho makuu ya imani, isipokuwa kama umeulizwa. Lakini lichukue Neno, na kwa upendo mwororo, wenye shauku kwa roho, waonyeshe haki ya thamani ya Kristo, ambaye wewe na wao lazima waje kuokolewa." - Welfare Ministry, 92

3. VIKOSI VYA INJILI

“Hebu katika kila kanisa viwepo vikosi vya watendakazi vilivyopangwa vizuri ili kufanya kazi kwa maeneo yaliyo karibu na kanisa hilo. Acha ubinafsi, na umruhusu Kristo akuongoze kama uzima wako na nguvu. Hebu tuingie katika kazi hii bila kukawia, na Kweli itakuwa kama chachu duniani. Wakati vile vikosi vinapopangwa ili kufanya kazi katika makanisa yetu yote, kutakuwa na ukarabati, matengenezo, nguvu ya kutia shime katika makanisa, kwa sababu washiriki wanafanya kazi ile ile ambayo Mungu amewapa kufanya.” – Welfare Ministry, 107.

“Katika kila mji mkubwa kunapaswa kuwa na vikosi vya watendakazi waliopangwa, wenye nidhamu; sio kikosi kimoja au viwili tu, bali vikosi kadhaa kwa ujumla vinapaswa kuwekwa kufanya kazi. .

“Kila kikosi cha watendakazi kinapaswa kuwa chini ya kiongozi mwenye uwezo, na izingatiwe daima kwamba wao wanapaswa kuwa wamishenari kwa maana ya juu kabisa ya Neno hilo. Kazi hiyo yenye utaratibu, iliyofanywa kwa busara, ingeleta matokeo yenye baraka.” – Medical Ministry, 300-301.

Kwa wale ambao wamejishughulisha na kazi hii ningesema: Endelea kufanya kazi kwa busara na uwezo. Wahamasishe washiriki wako kufanya kazi chini ya jina fulani ambapo wanaweza kupangwa kushirikiana katika utendaji wenye maelewano. Wafanye vijana wa kiume na wa kike makanisani wafanye kazi. Unganisha kazi ya umishenari wa tiba na tangazo la ujumbe wa malaika wa tatu. Fanya juhudi za mara kwa mara, zilizopangwa ili kuwainua washiriki wa kanisa kutoka katika kiwango cha wafu ambacho wamekuwa miaka mingi. Tuma watendakazi makanisani ambao wataziishi kanuni za matengenezo ya afya. Na watumwe wale wanaoweza kuona umuhimu wa kujinyima chakula, au watakuwa mtego kwa kanisa. Angalia kama pumzi ya uhai haitaingia katika makanisa yetu. Kipengele kipya kinahitajika kuletwa kwenye kazi. Watu wa Mungu lazima watambue hitaji lao kuu na hatari, na kuchukua kazi iliyo karibu nao.” - Shuhuda kwa Kanisa 6:267.

“Ndugu na Dada Haskell wamekodisha nyumba katika mojawapo ya sehemu bora zaidi ya jiji, na wamekusanyika pamoja na wanafamilia wanaosaidia kazi za nyumbani, ambao siku baada ya siku wanatoka na kwenda kwa ajili ya usomaji wa Biblia, kuuza karatasi zetu, na kufanya kazi ya umishenari wa tiba. Wakati wa saa ya ibada watendakazi wanasimulia uzoefu wao. Masomo ya Biblia hufanywa mara kwa mara nyumbani, na vijana wa kiume na wa kike waliohusishwa kwenye utume hupokea mafunzo ya vitendo, kupitia mafunzo ya kina ya usomaji wa Biblia na kuuza machapisho yetu…

“Kazi kama hiyo inapaswa kufanywa katika miji mingi. Vijana wanaoenda kufanya kazi katika miji hii wanapaswa kuwa chini ya uongozi wa viongozi wenye uzoefu, waliowekwa wakfu. Hebu watendakazi wapewe nyumba nzuri, ambamo wanaweza kupata mafunzo ya kina.” —Evangelism, 108-109.

“Kwa nini waumini hawana kule kujali kwa kina zaidi na kwa dhati kwa ajili ya wale walio nje ya Kristo? Kwa nini watu wawili au watatu hawakutani pamoja na kumsihi Mungu kwa ajili ya wokovu wa mtu mmoja maalum, na kisha kwa ajili ya mwingine? Katika makanisa yetu hebu makundi yaundwe kwa ajili ya huduma. Hebu watu tofauti waungane katika kazi kama wavuvi wa watu. Hebu watafute kukusanya roho kutoka katika uharibifu wa ulimwengu kwenda kwenye usafi wa kuokoa wa upendo wa Kristo.

“Uundaji wa makundi madogo madogo kama msingi wa juhudi za Kikristo umewasilishwa kwangu na Yule ambaye hawezi kukosea kamwe. Ikiwa kuna idadi kubwa ya watu kanisani, hebu washiriki wapangwe katika makundi madogo-madogo, na kufanya kazi sio tu kwa ajili ya washiriki wa kanisa, bali kwa ajili ya watu wasioamini. Ikiwa katika sehemu moja wapo wawili tu au watatu ambao wanaujua Ukweli, hebu wajiunge katika kikundi cha watendakazi. Hebu waweke kifungo chao cha muungano kutokuvunjika, wakijibidisha pamoja katika upendo na umoja, wakitiana moyo kusonga mbele, kila mmoja akiambukizwa ujasiri na nguvu kutokana na msaada wa wengine. Shuhuda kwa Kanisa, 7: 21- 22.

4. TIMU ZA UINJILISTI ZA WAMISHENARI TIBA

“Kutokana na maagizo ambayo Bwana amenipa mara kwa mara, najua kwamba kunapaswa kuwa na watendakazi wanaofanya ziara za uinjilisti wa tiba kati ya miji na vijiji. Wale wanaofanya kazi hii watakusanya mavuno mengi ya roho, kutoka kwa tabaka za juu na za chini. Njia ya kazi hii inatayarishwa vyema zaidi kwa juhudi za mtangazaji mwaminifu.” - Counsels on Health, 397.

“Wajumbe wanapaswa kuteuliwa ambao wanaweza kuwasilisha Neno la Mungu kutoka mji hadi mji juu ya somo la kiasi.” - A Call to Medical Missionary, 37.

“Somo la Kiasi cha Kikristo linapaswa kupata nafasi katika mahubiri yetu katika kila mji tunakofanyia kazi." - A Call to Medical Missionary, 38.

"Katika kila juhudi kama unayofanya sasa, mema zaidi yangetokana na kazi yako, ikiwa tu mngekuwa na jambo linalofaa kusoma na lililo tayari kwa kusambazwa. Vipeperushi vinavyohusu mambo muhimu ya Ukweli kwa wakati huu vinapaswa kutolewa bure kwa wote ambao watavikubali, bila pesa na bila gharama kubwa, hali ambayo ingeweza hatimaye kusababisha kurudi mara mia kwenye hazina kile

ambacho kimetoka. Mnapaswa kupanda kando ya maji yote.” – Counsels on Health, 465.

“Maelekezo yanapaswa kutolewa juu ya afya na kiasi.....na kufuatilia kazi ya machapisho kuhusu masuala haya.” —Counsels on Health, 449 (Tazama ukurasa wa 465-466).

“Wengine wanaweza kufikiria suala la lishe ni muhimu vya kutosha kujumuishwa katika suala la dini.” - Evangelism, 265.

5. WAMISHENARI WA TIBA WANAOUZA VITABU

“Lazima kuwe na juhudi za dhati zinazofanywa kuwaelimisha watu juu ya somo la matengenezo ya afya.” -Counsels on Health, 466.

“Njia ya kazi hii (ya wainjilisti wa tiba) inatayarishwa vyema zaidi kwa juhudi za mtangazaji mwaminifu.” -The Counsels on Health, 397.

"Wainjilisti wa vitabu wanapaswa kuvuta umakini wa wale wanaowatembelea kuhusiana na machapisho yetu ya afya, wakiwaambia kuhusu maagizo muhimu yaliyo kwenye majarida haya kuhusu utunzaji wa wagonjwa na tiba ya magonjwa.” -Counsels on Health, 462.

“Kadiri nafasi inavyotolewa, hebu huyo mwinjilisti wa vitabu azungumzie juu ya thamani ya lishe bora. Hapaswi kamwe kuona aibu kusema ‘Hapana, asante; mimi sili nyama. Ikiwa chai itatolewa na wenyeji, hebu na aikatae.”-The Counsels on Health, 463.

Mwinjilisti anayeuza vitabu anapotoka sehemu moja hadi nyingine anapaswa kuwa na ujuzi wa kivitendo wa sababu za ugonjwa, na anapaswa kuelewa jinsi ya kutoa tiba rahisi….akiwaelekeza kwa Tabibu Mkuu.” The Counsels on Health, 463- 464.

“Tangazo la onyo dhidi ya uovu mkubwa wa kutokuwa na kiasi linapaswa kusikika; na ili hili lifanyike, kila mshika Sabato anapaswa kusoma na kufanyia mazoezi maelekezo yaliyomo katika majarida yetu ya afya na vitabu vyetu vya afya. Na wanapaswa kufanya zaidi ya hili: wanapaswa kufanya juhudi za dhati kusambaza machapisho haya miongoni mwa majirani zao. “Uuzaji wa maandishi yetu ya afya hautazuia uuzaji wa machapisho yanayohusu sehemu zingine za ujumbe wa Malaika wa tatu. Yote haya yanapaswa kuandaa njia kwa ajili ya kuja kwa Bwana.njia ya kuja kwa Bwana.” -Counsels on Health, 462.

6. MKUTANO WA MAKAMBI

(Inapaswa kuzingatiwa hapa kwamba mikutano ya awali ya makambi ilikuwa Efoti zilizofanyika kwenye hema za uinjilisti. Hizi zilihudhuriwa zaidi na watu wasio washiriki na mikutano hii ya hema hizi ilihamishwa kutoka jiji hadi jiji).

“Mikutano ya hadhara inapaswa kufanyika, ili kuwasilisha mada, na shule za mafunzo zinapaswa kuendeshwa.” - Evangelism, 534.

“Hebu (watendakazi) wachukue kanuni hai za matengenezo ya afya kwenda katika jamii ambazo kwa kiasi kikubwa hazijui kanuni hizi. Hebu madarasa yaanzishwe, na maagizo yatolewe kuhusu tiba ya magonjwa." – Shuhuda kwa Kanisa 8, uk. 148.

"Mianzo [ya taasisi za afya] inaweza kufanywa katika kila sehemu maarufu ambapo mikutano ya makambi inafanyika." -Counsels on Health, p. 468.

"Katika mkutano wa makambi, maelekezo juu ya mada za afya yanapaswa kutolewa kwa watu. Katika mikutano yetu nchini Australia, mihadhara kuhusu masomo ya afya ilitolewa kila siku, na shauku kubwa iliamshwa .... Maelfu ya watu walihudhuria mihadhara hiyo, na mwisho wa mkutano wa makambi watu hawakuridhika kuangusha jambo hilo kwa yale ambayo tayari walikuwa wamejifunza. Katika miji kadhaa ambako mikutano ya makambi ilikuwa imefanyika, baadhi ya wananchi wakuu walihimiza kwamba matawi ya vituo vya kutibu magonjwa kwa usahili, magonjwa ya mtindo wa maisha (Sanitarium) vianzishwe na hivyo kuahidi ushirikiano wao. Katika miji kadhaa kazi imeanzishwa kwa mafanikio mazuri.” - Counsels on Health, pp. 467-468.

7. TIMU ZA WAMISHENARI WA NJE

“Upana wa kazi ya injili ya umishenari wa tiba bado haujaeleweka [Mathayo 28:18-20 huonyesha agizo ambalo Kristo amempa kila mmoja wetu].” -The Counsels on Health, 509.

“Kuna hitaji kubwa katika sehemu zote za dunia kwa ajili ya walimu wa Kikristo na wamishenari wa tiba. Katika sehemu zote za maeneo ndani na nje ya nchi, kuna milango wazi kwa wale wanaoweza kufanya mema kwa ajili ya mwili na roho, wakiwasilisha nuru ya thamani ya Kweli. Upuuziaji wa siku za nyuma katika mwelekeo huu haupaswi kuendekezwa. Nuru kubwa imeangaza kwenye njia yetu katika mielekeo fulani, kuliko mingine, lakini licha ya kuwa na nuru hii kubwa katika nyanja hii, bado tumetembea nyuma ukilinganisha na nuru tuliyopewa na Bwana” - Fundamentals of Christian Education, 231-232.

“Wale ambao wamefunzwa kwa ajili ya kazi ya umishenari wa tiba katika nchi za ughaibuni wanapaswa kuhimizwa kwenda bila kuchelewa kule ambako wanatarajia kutenda kazi, na kuanza kazi miongoni mwa watu, wakijifunza lugha za kule wanapofanya kazi, na huku wakiendelea na kazi. Na haitachukua muda kwao kuweza kuzifundisha zile Kweli rahisi za Neno la Mungu.” -Huduma ya Uponyaji, 155. [MH 155.1]

“Ulimwenguni kote, wajumbe wa rehema wanahitajika. Kuna mwito kwa familia za Kikristo kwenda katika jamii mbalimbali zilizo gizani na zenye mafundisho yenye makosa, kwenda katika maeneo ya ughaibuni, ili kufahamu mahitaji ya wanadamu wenzao, na kufanya kazi kwa ajili ya utume wa Bwana. Endapo familia kama hizo zingetulia katika maeneo yenye giza duniani, mahali ambapo watu wamefunikwa na utusitusi wa kiroho, na kuruhusu nuru ya maisha ya Kristo ing’ae kupitia kwao, ni kazi nzuri kama nini ingeweza kutekelezwa huko.” — Huduma ya Uponyaji, 155-156. [MH 155.2]

8. INAPOWEZEKANA ENENDENI WAWILI WAWILI

“Akiwaita Kwake wale kumi na wawili, Yesu aliwataka waondoke wawili wawili katika miji na vijiji. Hakuna aliyetumwa akiwa peke yake, ndugu alienda na ndugu, rafiki alienda na rafiki. Kwa njia hiyo wangeweza kusaidiana na kutiana moyo, wakishauriana na kuomba pamoja, nguvu za mmoja zikijazia mapungufu ya mwingine. Kwa namna ile ile Masihi aliwatuma wale sabini baadaye. Kusudi la Mwokozi lilikuwa ni kwamba wajumbe wa injili wajumuike namna hii. Katika wakati wetu kazi ya uinjilisti ingefanikiwa kwa mbali sana ikiwa kielelezo hiki kingefuatwa.” - Desire of Ages, 350.

“Kwa nini tumeacha njia ya kazi ambayo ilianzishwa na mwalimu Mkuu? Kwa nini watendakazi katika kazi Yake leo hawajatumwa kwenda wakiwa wawili-wawili? Oh, unasema, hatuna watendakazi wa kutosha kufanya kazi shambani. Kama hakuna watendakazi wa kutosha, anza kazi katika sehemu ndogo. Tuma watendakazi katika sehemu ambazo njia inaonekana kufunguka, na wafundishe Ukweli wa thamani wa wakati huu. Je, sisi hatujaona bado hekima ya watendakazi kwenda wawili kwa wawili?” -Evangelism, 74.

(vikosi vya Injili vinapaswa kujigawanya katika timu ya watu wawili-wawili, wakati wanapotoka kwenda kila siku nyumba kwa nyumba.)

9. PALE KAZI INAPOASISIWA KATIKA SEHEMU MOJA NA WATENDAKAZI WALIOFUNZWA, ANZA KAZI MPYA MAHALA PENGINE.

“Katika kila mji unaofikiwa, msingi thabiti unapaswa kuwekwa kwa kazi ya kudumu.” - Evangelism, 462.

“Kila kanisa linapaswa kuwa shule ya mafunzo kwa watenda kazi Wakristo. Washiriki wake wanapaswa kufundishwa jinsi ya kuwasilisha masomo ya Biblia, jinsi ya kuongoza na kufundisha madarasa ya shule ya Sabato, namna bora ya kuwasaidia watu maskini, na kuwahudumia wagonjwa, na jinsi ya kushughulika na wale ambao bado hawajaongoka. Hatuna budi kuwa na shule za afya, shule za mapishi, na madarasa katika safu mbalimbali za kazi saidizi ya Kikristo. Hatupaswi kuwa na ufundishaji tu, bali pia kazi halisi inapaswa ifanyike chini ya waalimu wenye uzoefu.” -Ministry of Healing, 149. [MH 149.2]

“Kazi ya Mwokozi haikuzuiliwa na mipaka ya muda au mahali. Huruma Yake haikujua kikomo. Kwa kiwango kikubwa sana Yeye aliendesha kazi Yake ya kuponya na kufundisha kwa mtindo huu, nao watu wakajazana kiasi kwamba hapakuwa na jengo lolote katika Palestina lililokuwa kubwa kiasi cha kutosha kupokea umati wa watu waliosongamana karibu Yake. Juu ya miteremko ya milima ya kijani kibichi ya Galilaya, katika njia za kusafiri, kando ya bahari, katika masinagogi, na kila mahali ambapo wagonjwa wangeweza kuletwa Kwake, kulikuwa na hospitali Yake hapo. Katika kila jiji, kila mji, kila kijiji, alikopita, aliweka mikono Yake juu ya wale waliokuwa wakiteseka, Naye akawaponya. Popote palipokuwa na mioyo iliyo tayari kupokea ujumbe Wake, aliwafariji hao kwa hakikisho la pendo la Baba yao wa mbinguni.” -Ministry of Healing, 17-18. [MH 17.3] (zaidi juu ya hiki tazama Evangelism, 353-354; 381-383.)

10. UHAKIKISHO WA MWONGOZI WA KIUNGU NA BARAKA

Kila siku unapotoka kwenda kufanya kazi yako, weka mbele ya akili yako Ukweli wa ajabu kwamba ikiwa umejisalimisha, mnyenyekevu, na mtiifu mbingu yote inasubiri kukusaidia na kukuongoza katika kazi hii.

"Ikiwa walimu wa Neno Lake Bwana wako tayari, Bwana atawaongoza katika uhusiano wa karibu na watu. Atawaongoza katika nyumba za wale wanaohitaji na kutamani Ukweli, akiwaleta katika hali zinazofaa zaidi kwa talanta zao." - Welfare Ministry, 101.

“Kristo anaita kila mwanamume na mwanamke kuvaa silaha za haki Yake na kuanza kufanya kazi. “Niko mkono wako wa kuume ili kukusaidia,” Yeye Atangaza. Mwambie Mungu wako majaribu na fadhaa zako zote. Yeye Hatasaliti imani yako kamwe. Hakuna kitu chenye thamani sana kwa Kristo kama mali Yake aliyoinunua, kanisa Lake, watenda kazi wanaokwenda kutawanya mbegu za

Ukweli.... Fikiri juu ya Yesu. Yeye sasa Yuko katika Patakatifu Pake, si katika hali ya upweke, bali amezungukwa na elfu kumi mara elfu kumi ya malaika wa mbinguni wanaongoja kufanya agizo Lake. Naye wote anawaamuru waende wakamfanyie kazi yule mtakatifu aliye dhaifu zaidi anayeweka tumaini lake kwa Mungu. Watu wakubwa na watu wa chini, matajiri na maskini, wana msaada uleule unaotolewa na Bwana.” – Christian Service, 261.

“Katika kazi hii malaika wote wa mbinguni wako tayari kushirikiana. Rasilimali zote za mbinguni ziko kwa ajili ya amri itakayotolewa na wale wanaotafuta kuokoa waliopotea. Malaika watakusaidia kufikia wale wasiojali na walio wagumu kabisa. Na mtu anaporudishwa kwa Mungu, mbingu zote hufurahi; maserafi na makerubi hushika vinubi vyao vya dhahabu, na kuimba sifa kwa Mungu na Mwana-Kondoo kwa ajili ya rehema na fadhili zao zenye upendo kwa wana wa wanadamu.” —Christ’s Object Lessons, 197.

"Katika kufanya kazi kwa ajili ya roho zinazoangamia, wewe unakuwa na ushirika wa malaika." – Shuhuda kwa Kanisa 9:129.

“Na malaika wa Mungu, wenye nguvu zaidi, hutumwa na Mungu ili kuwahudumia watendakazi Wake wa kianadamu ambao wanausema Ukweli kwa wale wasioujua..” - Shuhuda kwa Kanisa 8:17.

“Malaika wa Mungu wanangojea kushirikiana na wote watakaopanga mipango ambayo kwayo roho ambazo Kristo alizifia zitapata kusikia habari njema za wokovu.” - Shuhuda kwa Kanisa 6 :433.

“Malaika wa mbinguni kwa muda mrefu wamekuwa wakingojea mawakala wa kibinadamu - washiriki wa kanisa - kushirikiana nao katika kazi kubwa inayopaswa kufanywa..” — Shuhuda kwa Kanisa 9 :46-47.

“Malaika wote wa mbinguni wako katika mkao wa huduma ya watu wanyenyekevu, watu wanaomwamini Mungu.” – The Acts of the Apostles, 154.

“Mpinzani wetu hataturuhusu kupumzika. Ikiwa kweli sisi ni watoto wa Mungu tutasumbuliwa na kuteswa sana, na hatuhitaji kutarajia kwamba Shetani au wale walio chini ya ushawishi wake watatutendea mema/vizuri. Lakini kuna malaika ambao wana nguvu zai, nao watakuwa pamoja nasi katika mizozo yetu yote ikiwa tu tutakuwa waaminifu.” —Shuhuda kwa Kanisa 3: 526.

“Kufanya kazi ya umishenari wa tiba huleta miale ya mng’ao wa mbinguni kwa roho zilizochoka, zilizochanganyikiwa, zinazoteseka..... Katika kila kazi ya

rehema, kila kazi ya upendo, Malaika wa Mungu wapo hapo.” -A call to Medical Evangelesm, 27.

“Kwa kuwa atakuagizia malaika Zake Wakulinde katika njia zako zote..” — Zaburi 91:11. “Tazama, Mimi namtuma malaika aende mbele yako, ili akulinde njiani na kukupeleka mpaka mahali pale nilipokutengezea." — Kutoka 23:20.

“Si nguvu inayotoka kwa wanadamu inayofanikisha kazi, ni nguvu ya mawakala wa mbinguni inayofanya kazi na wakala wa kianadamu, ndiyo ambayo huleta kazi kwenye ukamilifu.” – Christian Service, 260.

“Njia ya Mungu ya kutusaidia tunaweza tusiijue au kuitambua, lakini jambo moja tuna uhakika nalo ni kuwa: Yeye kamwe hawaanngushi wale wote wanaomtumaini Yeye. Kama Wkristo wangeweza kutambua ni mara ngapi Bwana ameelekeza njia yao, ili makusudi ya adui dhidi yao yasitimizwe, wasingeingia katika jaribu la kulalamika. Imani yao ingebaki kwa Mungu, na hakuna jaribu lingekuwa na nguvu ya kuwasukuma (Kwa watoto Wake, Bwana anatangaza; “mkafanye kazi, kwa kuwa Mimi ni pamoja nanyi. Mkristo daima ana msaidizi mwenye nguvu katika Bwana).” – Prophets and Kings, 576.

“Tunapojitoa kikamilifu kwa Mungu, na katika kazi yetu kufuata maagizo Yake Bwana, Yeye Mwenyewe Ndiye anawajibika katika kuleta utimilifu wa hiyo kazi. Yeye Asingetaka tufikirie kwamba kufaulu kwa kazi, kumetokana na juhudi zetu za uadilifu. Hatupaswi kufikiria hata mara moja kuhusu kushindwa. Tunapaswa kushirikiana na Yule asiyejua kushindwa.” —Christ’s Object Lessons, 363.

SURA YA 7

JINSI TAASISI ZA UMISHENARI WA TIBA ZINAVYOPASWA KUFANYA KAZI

Mwongozo Kwa Ajili Ya Kituo Cha Uinjilisti Cha Umishenari Wa Tiba

1. VITENGO VYA MSTARI WA MBELE VYA UMISHENARI WA TIBA – VITUO VIDOGO VYA MJI

[1]- WATENDAKAZI WETU WANAPASWA KWENDA VYA MIJINI

“Tangu sasa kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kuendelezwa kwa bidii ambayo haijawahi kuonyeshwa kabla. Kazi hii ni mlango ambao Kweli itaifikia miji mikubwa” -Counsels on Health, 392.

“Hebu kazi ya Bwana na isonge mbele. Hebu kazi ya umishenari wa tiba na kazi ya elimu zisonge mbele. Nina uhakika kwamba huu ni upungufu wetu mkubwa---- watendakazi wenye bidii, waliojitoa wakfu, wenye akili mahiri na uwezo. Katika kila mji mkubwa kunapaswa kuwa na uwakilishi wa kazi ya ile Kweli ya umishenari wa tiba. Hebu watu wengi na wajiulize sasa, Je, Bwana utaniruhusu nifanye nini? Ni kusudi la Bwana kwamba njia Yake ya uponyaji bila madawa ya famasia/drugs italetwa katika njia itakayoifanya ijulikane au kuwa mashuhuri katika kila mji mkubwa kupitia taasisi zetu za tiba.” —Counsels on Health, 393-394.

“Hakuna mabadiliko katika jumbe ambazo Mungu amezituma hapo awali. Kazi katika miji ni kazi ya muhimu kwa wakati huu. Miji inapofanyiwa kazi ambavyo

Mungu angetaka ifanyike, matokeo yake yatakuwa ni mazingira ya operesheni kubwa ambayo bado hatujashuhudia.”— Medical Ministry, 304.

[2]- LAKINI MAONYO YAMEKWISHATOLEWA DHIDI YA KUISHI AU KUTENGENEZA VITUO VIKUBWA KATIKA MIJI

“Vyama vya kibiashara na mashirika ya ulimwengu ni mitego (trade unions). Jieupushe nayo… kwa sababu ya vyama hivi na mashirika, hivi karibuni itakuwa ni vigumu sana kwa taasisi zetu kuendeleza kazi yake mijini. Waelimishe watu wetu ili watoke mjini na kwenda mashambani, ambapo wanaweza kupata kipande kidogo cha ardhi, na kujitengenezea makazi yao na Watoto wao.

“Migahawa yetu lazima iwe mijini; kwa maana vinginevyo wafanyakazi katika migahawa hii hawataweza kuwafikia watu na kuwafundisha kanuni sahihi za kuishi. Na kwa sasa itabidi tujipatie nyumba za kukutania katika miji. Lakini hata hivyo kutakuwa na malumbano na machafuko katika miji, kiasi kwamba wale wanaotaka kuondoka hawataweza. Ni lazima tujiandae kwa masuala haya. Hii ndiyo nuru niliyopewa.” – Country Living, 10-11. (Soma kijitabu kizima.)

[3]- VITUO VINGI VIDOGO VYA UMISHENARI WA TIBA VIANZISHWE MIJINI

“Lazima tufanye kuliko tulivyofanya ili kuwafikia watu wa miji yetu. Hatupaswi kusimamisha majengo makubwa, lakini tena na tena nuru imetolewa kwangu kwamba tunapaswa kuanzisha katika miji yetu yote vituo au miundo-mbinu midogo ambayo itakuwa ni vituo vya mvuto.” – Counsels on Health, 481.

VYUMBA VYA TIBA—"Katika kila mji ambamo tuna kanisa, kuna haja ya kuwa na sehemu ambapo tiba rahisi inaweza kutolewa (hydrotherapia, kazi ndogondogo nk). Miongoni mwa nyumba za washiriki wa kanisa letu kuna wachache wanaomudu kupata nafasi ya chumba kimoja kwenye makazi yao ambayo ni fursa kwa ajili ya kumhudumia vizuri mgonjwa.

Sehemu (eneo) inapaswa itolewe ambapo matibabu yanaweza kutolewa kwa magonjwa yanayowapata watu mara kwa mara. Jengo hilo linaweza kuwa lisilovutia na hata rafu au lisiloonekana maridadi, lakini linapaswa kuwa na vifaa vya kutoa matibabu rahisi. Yote yaliyozungumzwa yakijumuishwa pamoja kwa ustadi, yatathibitisha baraka, si kwa watu wetu tu, bali kwa majirani zao, na huenda ikawa njia ya kuwavutia wengi kwenye kanuni za afya." -Counsels on Health, 468.

“Nimepewa nuru kwamba katika miji mingi ni vyema kwamba migahawa yetu ya afya iunganishwe na vyumba vya tiba-Sanitarium. Hizi nyanja mbili, zinaweza kushirikiana katika kushikilia kanuni sahihi.

Kwa kuhusiana na haya wakati mwingine inashauriwa kuwa na vyumba ambavyo vitatumika kama vyumba vya wageni, ili wagonjwa wanaokuja walale humu wakiwa wanaendelea na tiba. Taasisi hizi zitatumika katika kuinua kanuni sahihi kwa ajili ya vituo vya tiba rahisi (Sanitariums) vilivyopo nchini na ingekuwa bora viendeshwe katika majengo ya kukodi. Hatupaswi kusimamisha katika miji majengo makubwa ambayo tutawatunza wagonjwa, kwa sababu Mungu ameonesha wazi kuwa wagonjwa wanaweza kutunzwa vizuri zaidi nje ya miji.” -Shuhuda kwa Kanisa 7: 60.

KUMBI ZA HADHIRA—“Kama watu tumepewa kazi ya kuzifundisha kanuni za matengenezo ya afya… Kuhusiana na utume wetu mijini kunapaswa kuwa na vyumba vinavyofaa ambapo wale ambao wanavutiwa wanaweza kukusanywa kwa ajili ya mafundisho.” -Counsels on Health, 443.

“Mipango inapaswa kupangwa ili kufanya mikutano ihusuyo migahawa yetu. Wakati wowote inapowezekana, hebu chumba kitengwe ambapo wadau/patrons wanaweza kualikwa kwenye mihadhara juu ya sayansi ya afya na kiasi cha Kikristo, ambapo walezi wanaweza kupokea maelekezo juu ya utayarishaji wa chakula bora, kisichokobolewa au kusindikwa na juu ya masomo mengine muhimu. Katika mikutano hii kunapaswa kuwa na maombi na kuimba na mazungumzo, si tu juu ya mada za afya na kiasi, bali pia juu ya masomo mengine ya Biblia yanayofaa. Watu wanapofundishwa jinsi ya kutunza afya ya kimwili, fursa nyingi zitapatikana za kupanda mbegu za injili ya ufalme.” -Counsels on Health, 481.

“Kazi ya uinjilisti yenye mafanikio inaweza kufanywa kuhusiana na kazi ya umishenari wa tiba. Ni kadri mistari hii ya kazi inavyounganishwa ndipo tunaweza kutarajia kukusanya tunda la thamani zaidi kwa Bwana.” —Ministry of Healing, 26-27.

“Kanuni za matengenezo ya afya zinapaswa kuhamasishwa na kutangazwa kama sehemu ya kazi katika miji hii. Sauti ya ujumbe wa malaika wa tatu inapaswa kusikika kwa nguvu. Hebu mafundisho ya matengenezo ya afya yapelekwe kwa kila jitihada inayofanywa ili kuangaza nuru ya Kweli mbele ya watu.” -Evangelism, 533.

“Watendakazi wa Injili wanapaswa pia kutoa mafundisho katika kanuni za mitindo ya maisha yenye afya. Kuna magonjwa kila mahali, na mengi ya hayo yanaweza kuzuiwa kwa kuzingatia sheria za afya. Watu wanahitaji kuona umuhimu wa kanuni za afya katika ustawi wao, kwenye maisha haya na maisha yajayo. Wanahitaji kuamshwa kwenye wajibu wao kwa ajili ya miili yao iliyoumbwa na Muumba wao kama makao Yake, ambayo Yeye huwataka wawe mawakili waaminifu kwa hayo makao (miili). Wanahitaji kuvutiwa na ile kweli itolewayo katika Maandiko Matakatifu: [MH 146.1]

“Ninyi ni hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema, Nitakaa ndani yao, na ndani yao nitatembea; Nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu Wangu.” 2 Wakorintho 6:16. [MH 146.2]

Maelfu wanahitaji mafundisho, na hawa wangeyapokea kwa furaha maagizo yahusuyo njia rahisi za kutibu wagonjwa— njia mbadala zinazochukua nafasi ya matumizi ya dawa zenye sumu (drugs).” -Ministry of Healing, 146.

“Mazungumzo ya afya yatatolewa, machapisho yataongezwa. Kanuni za matengenezo ya afya zitapokelewa kwa kuidhinishwa vyema, na wengi wataangazwa. Mivuto inayohusishwa na matengenezo ya afya itapendekezwa kwenye maamuzi ya wote wanaotaka nuru, na watu watasonga mbele hatua kwa hatua ili kupokea zile Kweli maalum kwa wakati huu." - Shuhuda kwa Kanisa 6: 379.

(Kwa zaidi habari juu kumbi za hadhara, Angalia Counsels on Health hapo MaarifaMtandaoni.Com, 37-40, 422, 452, 449, 469, 481; Medical Ministry, 26-27, 147; 190.)

MIGAHAWA ya AFYA NA USAFI (Hyegenic restaurants)—“Nikiwa New York katika majira ya baridi kali ya 1901, nilipata nuru kuhusu kazi katika jiji hilo kuu. Usiku baada ya usiku kazi ambayo ndugu zetu wanapaswa kuibeba ilipita mbele yangu. New York Kuu, ujumbe unapaswa usonge mbele kama taa inayowaka. Mungu atawainua watendakazi kwa ajili ya kazi hii na malaika Zake watatangulia mbele yao… Iliwasilishwa mbele zangu kwamba hatupaswi kupumzika kwa sababu tuna migahawa/hoteli za mbogamboga huko Brooklyn (vegeterian restaurants), badala yake migahawa mingine inapaswa kuanzishwa katika sehemu zingine za jiji. Watu wanaoishi sehemu moja ya jiji kuu la New York huwa hawajui kinachoendelea katika sehemu zingine za jiji hilo kuu. Wanawake na wanaume wanaokula kwenye migahawa hii iliyoanzishwa katika maeneo tofauti dhamiri zao zitasukumwa kuelekea kwenye boreshaji wa afya. Watakapoaminishwa, watakuwa tayari zaidi kukubali ujumbe wa pekee wa Mungu wa Kweli.

Popote Kazi ya umishenari wa tiba inapofanywa katika miji yetu mikubwa, shule za upishi zinapaswa kuanzishwa; na popote ambapo kazi thabiti na ya nguvu ya umishenarikwa njia ya Elimu inaendelea, mgahawa wa usafi na Afya wa aina fulani unapaswa kuanzishwa, na ambao utatoa kielelezo cha vitendo cha uteuzi sahihi na utayarishaji mzuri wa vyakula (mambo mane katika chakula-Je, kina afya, Je, gharama ni nzuri, Je, kinapendeza macho, Je, kinapatikana karibu)." - Counsels on Health, 487-488.

"Nimeagizwa kwamba moja ya sababu kuu kwa nini migahawa ya usafi na afya na vyumba vya tiba vinapaswa kuanzishwa katika vituo vya miji mikubwa ni kwamba kwa njia hii usikivu ya viongozi utavutwa kwenye ujumbe wa Malaika wa tatu. Kwa kutambua kuwa migahawa hii inaendeshwa kwa njia tofauti kabisa na jinsi migahawa ya kawaida inavyoendeshwa, watu wenye akili mahiri wataanza sababu tofauti katika mbinu za biashara, na watachunguza kanuni zinazotuongoza kutoa chakula bora. Hivyo wataongozwa kwenye ujuzi wa ujumbe wa wakati huu." Counsels on Health, 491. (Angalia pia kurasa 408-411, 443, 449-451, 471-496; Medical Ministry, 265-281.)

SHULE ZA UPISHI—Kuhusiana na utume wetu mijini kunapaswa kuwa na vyumba vinavyofaa ambapo wale ambao wanavutiwa na kuguswa, wanaweza kukusanywa kwa ajili ya mafundisho. Shule za upishi lazima zianzishwe. Watu wanapaswa kufundishwa jinsi ya kuandaa chakula kizuri. Wanapaswa kuonyeshwa hitaji la kutupilia mbali vyakula visivyo na afya. Lakini hatupaswi kamwe kutetea lishe ya njaa. Inawezekana kuwa na lishe bora, yenye lishe bila kutumia chai, kahawa, na chakula cha nyama. Kazi ya kufundisha watu jinsi ya kuandaa lishe ambayo haichukui muda huwa ya afya na ya kupendeza kwa ladha, ni ya muhimu sana. Kazi ya matengenezo ya afya ni njia ya Bwana ya kupunguza mateso katika ulimwengu wetu na kutakasa Kanisa Lake. Wafundishe watu kwamba wanaweza kutenda kama mkono wa kusaidia wa Mungu..... Kazi hii ina muhuri wa mbinguni, na itafungua milango ya kuingia kwa zile Kweli zingine za thamani. Kuna nafasi kwa wote kufanya kazi ambao watachukua kazi hii kwa akili mahiri."—Counsels on Health, 443-444.

"Popote Ukweli unapobebwa, watu wanapaswa kupewa maelekezo kuhusu utayarishaji wa chakula chenye afya. Mungu anatamani kwamba watu wafundishwe kila mahali watu na walimu stadi waonyeshe watu jinsi ya kutumia kwa hekima bidhaa za chakula ambazo wanaweza kupata kwa urahisi katika sehemu yao ya nchi. Kwa hivyo maskini, pamoja na wale walio katika hali bora zaidi, wanaweza kufundishwa kuishi kwa afya. .

Hatupaswi kupuuza kazi hii kwa sababu ya athari ambayo tunaweza kuogopa itakuwa nayo katika uuzaji wa bidhaa za chakula zinazotengenezwa katika viwanda vyetu vya chakula cha afya. Hili sio jambo muhimu zaidi. Kazi yetu ni kuwaonyesha watu jinsi wanavyoweza kupata na kuandaa chakula chenye afya, jinsi wanavyoweza kushirikiana na Mungu katika kujirudishia mfano Wake."—A Call to Medical Evangelism, 31. (Zaidi tazama Health, 443; 471-496, Medical Ministry, 256-281)

MADUKA YA VITABU VYA AFYA NA DINI NA MAKTABA ZA KUAZIMA WATU— Vyombo vya habari, kama vile media, magazeti na mitambo ya kuchapa vitabu ni njia yenye nguvu ya kusogeza akili na mioyo ya watu. Unapaswa kuwa dhati na bidii zaidi kwa kujipatia machapisho ya kusoma yenye tabia ya kuinua na kuokoa mbele ya watu.

Kunapaswa kuwa na juhudi za dhati zaidi kufanywa ili kuwaelimisha watu juu ya somo kuu la matengenezo ya afya. Vipeperushi vya kurasa nne, nane, kumi na mbili, kumi na sita, na zaidi zenye makala zilizonyoka, za moja kwa moja, zilizoandikwa vizuri juu ya swali hili kuu, zinapaswa kutawanywa kama majani ya msimu wa kupukutisha majina."— Counsels on Health, 465-466.

"Wale wanaokuja kwenye migahawa yetu wanapaswa kupewa vitu vya kusoma. Usikivu wao unapaswa kuvutiwa kwenye maandishi yetu juu ya kiasi na matengenezo ya mfumo wa lishe, na vipeperushi vinavyoshughulikia masomo ya Kristo pia vinapaswa kutolewa kwao. Counsels on Health, 482.

"Shikilia kanuni za matengenezo ya afya, na Bwana awaongoze wanyoofu moyoni.Wasilisha kanuni za kiasi katika namna yake ya kuvutia zaidi. Sambaza vitabu vinavyotoa maelekezo kuhusu maisha yenye afya." —Counsels on Health, 479.

"Maelekezo yanapaswa kutolewa juu ya afya na kiasi. Tafuta kuamsha akili na dhamiri. Leta katika huduma vipaji vyote walivyo navyo watu, na fuatilia kazi kwa machapisho juu ya somo. 'Elimisha, elimisha, elimisha' ndio ujumbe ambao umesisitizwa juu yangu."—Counsels on Health, 449.

"Vitabu vyenye ujumbe maalumu wa kwenda ulimwenguni wakati huu wa sasa--vinapaswa kusambazwa ke. "Kwa nini," aliuliza, "watu wetu hawathamini na kusambaza kwa upana zaidi vitabu vilivyo na sifa za mbinguni? Kwa nini si umaalumu hatubainishu juu ya vitabu vyenye maonyo kuhusu kazi ya Shetani? Kwa nini hatutoi juhudi kubwa katika kusambaza vitabu vinavyoonyesha mipango

ya Shetani ya kupingana na kazi ya Mungu, ambavyo vinafichua mipango na kuweka wazi udanganyifu wake?” – Shuhuda kwa Kanisa 9: 67.

“Mengi zaidi yalipaswa kukamiliswa katika uuzwaji wa vitabu vyetu kuliko tunayoona yametimizwa sasa.” - Shuhuda kwa Kanisa 9: 70.

“Kwa sababu vitabu vilikuwa vikiuzwa kwa bei ya chini, vingine vikipunguzwa bei hasa kwa ajili ya tukio fulani, vingi vilinunuliwa, na vingine na watu wasio wa imani yetu. Wakasema: “Lazima itakuwa vitabu hivi vina ujumbe kwa ajili yetu. Watu hawa wako tayari kujitolea ili tuwe navyo, na tutavihifadhi kwa ajili yetu na marafiki zetu." {9T 72.1} Lakini kutoridhika kulionyeshwa na baadhi ya watu wetu wenyewe. Mmoja alisema: "Lazima zuio liwekwe kwa hii kazi, la sivyo biashara yetu itaharibika.” Ndugu mmoja alipokuwa akibeba vitabu vingi, mwinjilisti wa vitabu akaweka mkono wake juu ya mkono wa huyo mtu asiyekuwa mshiriki na kusema: "Ndugu yangu, unafanya nini na hivi vitabu vingi?" Kisha nilisikia sauti ya Mshauri wetu ikisema: “Msiwakataze. Hii ndiyo kazi inayopaswa kufanywa. Mwisho uko karibu. Tayari muda mwingi umekwishapotea, ambao vitabu hivi vilipaswa kuwa katika kutawanywa.Viuzeni mbali na karibu. Vitawanyeni kama majani ya wakati wa vuli. Kazi hii ni ya kuendelea bila kutoa makatazo kwaa mtu yeyote. Roho zinaangamia nje ya Kristo. Hebu watu na waonywe juu ya kutokea Kwake upesi katika mawingu ya mbinguni.” — Shuhuda kwa Kanisa, 9: 72.

“Waazime majirani zako baadhi ya vitabu vyetu vidogo. Ikiwa shauku yao imeamshwa, chukua baadhi ya vitabu vikubwa zaidi." - Shuhuda kwa Kanisa 9: 35.

“Kwa kuazimisha au kuuza vitabu, kwa kusambaza vijizuu, na kwa kuifungua Biblia na kusoma na watu kama darasa, washiriki wetu wanaweza kufanya kazi kwa kiwango kikubwa sana kwa majirani zao wenyewe.” - Shuhuda kwa Kanisa 9: 35.

MADUKA YA CHAKULA CHA AFYA—Hebu vituo vya mvuto vianzishwe katika miji mingi ya kusini ya nchi yetu kwa kufunguliwa kwa maduka ya vyakula na migahawa ya mboga-mboga (Vegeterian Restaurants). Hebu pia kuwe na vifaa na miundo-mbinu kwa ajili ya utengenezaji wa vyakula sahili, vya afya kwa bei nafuu. Lakini pasiwepo ubinafsi, na sera ya kidunia isiingizwe kazini, kwa maana Mungu anakataza hili. Watu wasio na ubinafsi na waishike kazi hii kwa kumcha Mungu, na kwa upendo kwa wanadamu wenzao.”—Counsels on Health, 493-494.

“Watu wenye uwezo na hekima ya uchumi wanapaswa kuchaguliwa ili kufanya kazi inayohusiana na chakula; kwa maana, ili kazi iwe na mafanikio, hekima kuu na uchumi lazima vitekelezwe.”— Counsels on Health, 494.

[4] - Vituo Hivi Vidogo Vya Jiji Vinapaswa Kuendeshwa vikihusiana Na Kila kimoja

Mihadhara ya dini na afya na shule za upishi inapaswa kuunganishwa na tiba rahisi. (Counsels on Health, 469-470).

Kazi ya usambazaji wa vitabu na vijuzuu ikiunganishwa pamoja na migahawa ya afya na usafi (Counsels on Health, 482)

Vyumba vya mihadhara na shule za mapishi vinapaswa kuunganishwa na misheni za jiji. (Counsels on Health, 443).

Kazi ya umishenari wa tiba mara zote iunganishwe na shule za upishi, na kazi ya elimu na migahawa ya afya na usafi (Counsels on Health, 487).

Migahawa ya Afya na usafi na Vyumba vya Tiba (Counsels on Health, 488).

Vituo vya mvuto kupitia maduka ya chakula na migahawa ya mboga-mbonga (Vegeterian food stores), Zenye nyenzo na miundo mbinu ya utengenezaji wa vyakula rahisi vya afya vya bei nafuu. (Counsels on Health 493); 495-496 inaonyesha kuwa mpango bora wa kiwanda cha chakula cha afya kuwa karibu na shule ya nchi.

MAHALI PA VITUO VYA MIJI—Vituo vingi vidogo vinapaswa kutawanywa kila jiji (Counsel on Health, 485, 487; Shuhuda kwa Kanisa 7: 55).

MFANO UNAOTIA MOYO: KANISA LILILOTII MWONGOZO—“Sabato asubuhi, Novemba 10, 1900, tuliingia katika Kanisa la San Francisco, California na tukakuta limejashonana kwa watu wengi. Niliposimama mbele ya watu niliowafikiria juu ya ndoto hiyo na maagizo ambayo nilipewa miaka mingi iliyopita, na nilitiwa moyo sana. Nikiwatazama watu waliokusanyika, na hakika nilihisi kwamba ningeweza kusema ‘Bwana ametimiza Neno Lake.’

"Miaka michache iliyopita imekuwa kipindi cha shughuli nyingi kama za mzinga wa nyuki-beehive activity- (Mafunuo yaliyotolea mnamo 1876 wakati shughuli za makanisa mawili mapya ya wakati huo huko San Francisco na Oakland yaliwakilishwa kama mikusanyiko mawili ya shughuli nyingi (mizinga miwili ya nyuki) Kwa kweli kumekuwa na shughuli nyingi huko San Francisco. Juhudi nyingi za Kikristo katika nyanja mbali mbali zimeendelezwa na ndugu na dada zetu huko. Hii inajumuisha kuwatembelea wagonjwa na maskini, kuwatafutia makazi

watoto yatima na kushugulika na watu waliokosa ajira au kazi, kuwatunza wagonjwa, kufundisha Ukweli kutoka nyumba hadi nyumba, kusambaza machapisho, na kuendesha madarasa kuhusiana na mtindo wa maisha yenye afya na utunzaji wa wagonjwa. Shule ya watoto imeendeshwa katika ghorofa ya chini ya nyumba ya kukutania hapo Laguna. Kwa muda fulani bweni wanaume wenye vibarua iliwekwa wa utume wa tiba uliendelea kutekelezwa. Kwenye mtaa wa Market, karibu na Jumba la Jiji, kulikuwa na vyumba vya matibabu, vilivyoendeshwa kama tawi la Sanitarium ya St. Helena. Katika eneo hilo hilo kulikuwa na kituo cha duka la chakula cha afya. Karibu na katikati ya jiji, si mbali na jengo la mawasiliano ambapo watu huja kuhudumiwa, uliwekwa mgahawa wa mboga-mboga (Vegeterian food), ambao ulikuwa wazi siku sita katika juma na kufungwa kabisa siku ya Sabato. Kando ya ukingo wa maji, kazi ya misheni kwenye meli iliendelea. Nyakati mbalimbali wahudumu wetu walifanya mikutano katika kumbi kubwa jijini. Kwa hivyo ujumbe wa onyo ulitolewa na wengi."— Welfare Ministry, 112. 2

2. NYUMA YA YALE YANAYOENDELEA: VITUO VYA UMISHENARI WA TIBA NA VITUO VIDOGO HUKO MASHAMBANI (OUTPOST CENTERS)

[1]- VITUO VIDOGO VINGI VYA WAMISHENARI WA TIBA VINAPASWA KUANZISHWA MASHAMBANI AU NJE YA MJI

1- SANITARIUM (Vituo vya kusaidia wagonjwa kwa tiba rahisi)— "Utangazaji wa ile Kweli katika sehemu zote za ulimwengu unahitaji kuwepo kwa vituo vidogo vya sanitarium ili kutibu magonjwa katika sehemu nyingi, si katikati ya majiji, bali mahali ambapo mvuto wa jiji utahisiwa kwa udogo kwa kadri iwezekanavyo."— Medical Ministry, 159.

"Sanitarium nyingi ndogo zinapaswa kuanzishwa ili kutibu magonjwa kwenye sehemu zilizo nje ya mji.

Katika vituo hivi wawepo wanaume na wanawake wenye uwezo na waliojitoa wakfu, ambao watafanya kazi kwa upendo na hofu ya Mungu. Taasisi hizi zinapaswa kuwa shule za mafunzo."— Medical Ministry, 156.

"Vituo vidogo, vinapaswa kuanzishwa Mungu anapanga kwamba vituo vya matibabu vitakuwa njia ya kuwafikia watu wa hali ya juu na chini, tajiri na maskini. Vituo hivi vinapaswa kuendesha kazi kwa kuelekeza usikivu wa watu kwenye ujumbe ambao Mungu ametuma kwa ulimwengu."— Counsels on Health, 501.

“Kuhusiana na utumiaji wa dawa za famasia (drugs) katika taasisi zetu, hii ni kinyume na nuru ambayo Bwana amependezwa kuitoa. Biashara ya kuwapa watu madawa ya famasia (drugs) imeleta madhara zaidi katika ulimwengu wetu na kuua watu wengi zaidi ya kusaidia au kuponya. Nuru ilitolewa kwanza kwangu kwamba ni kwa nini taasisi hizi za Sanitarium zinapaswa kuanzishwa, vituo vya Sanitarium vinapaswa kurekebisha utendaji wa tiba wa madaktari-kufanya matengenezo katika taaluma ya utabibu.” (Reform the medical practice of physicians)—Medical Ministry, 27.

“Vituo vyetu vya Sanitarium vinapaswa kuanzishwa kwa lengo moja—kuendeleza Ukweli wa sasa.”— Counsels on Health, 272.

"Madhumuni ya taasisi zetu za afya hayapaswi kufanana kwa ukaribu mara zote kama yale ya hospitali. Taasisi za afya zinazohusiana na kazi ya mwisho ya injili duniani zinasimamia kanuni kuu za injili katika utimilifu wake. Ikiwa jengo la kituo cha Sanitarium, lililounganishwa na ujumbe huu wa mwisho linashindwa kumwinua Kristo na kanuni za injili kama zilivyowekwa katika ujumbe wa malaika wa tatu, litakuwa limeshindwa katika kipengele chake cha maana zaidi, na kupingana na lengo hasa la uwepo wake.”—Medical Ministry, 27 -28.

VITUO VYA TIBA SAHILI YAANI SANITARIUM VINAPASWA KUWA VIDOGO NA NDANI YA ENEO/NCHI—“Wale wanaohusika na sehemu za vituo vya tiba wanapaswa kujifunza kwa maombi tabia na lengo la kazi ya matibabu.”— Counsels on Health, 265.

“Tumepoteza mambo mengi mazuri kwa kushindwa kufanya hivyo. Tambua hitaji la mabadiliko katika mipango yetu kuhusiana na eneo la kituo cha Sanitarium. Ni mapenzi ya Bwana kwamba taasisi hizi zianzishwe nje ya jiji.”— Counsels on Health, 265.

“Sanitarium zinapaswa kusimikwa mashambani, nje ya mji, katikati ya mazingira yenye kuvutia kadri iwezekanavyo.”— Counsels on Health, 265.

“Wagonjwa wanapaswa kutunzwa mbali na misukosuko na pilikapilika za miji.”— Counsels on Health, 265.

“Wakati wa mapumuziko/faragha nje na miji, wagonjwa wataathiriwa kwa njia chanya kwa urahisi zaidi na Roho wa Mungu.”—Counsels on Health, 266.

“Sanitarium zinapaswa kuanzishwa katikati ya mazingira ya kupendeza zaidi, katika sehemu zisizosumbuliwa na msukosuko wa jiji.”— Counsels on Health, 266.

“Sanitarium zinapaswa kuzungukwa na mambo mazuri ya asili,na yenye kupendeza macho; waweke wagonjwa sehemu ambapo mioyo itarindima kwa wimbo.”—Counsels on Health, 268.

Sanitarium hazipaswi kuzungukwa na nyumba za kifahari au za matajiri (Counsels on Health, 270).

Msijenge Sanitarium kubwa na za gharama kubwa, lakini taasisi sawa na nyumbani katika maeneo ya kupendeza (miundo mbinu isiwe mikubwa kama mammoth/tembo) (Counsels on Health, 211).

Kituo cha tiba cha Sanitarium kisiwekwe Los Angeles (Counsels on Health, 166; 231; 7 Testimonies, 85).

“Sio mapenzi ya Bwana kwa watu Wake kujenga kituo cha Sanitarium kikubwa mahali popote pale (no Mammoth sanitariums). Vituo vingi vya Sanitarium vinapaswa kuanzishwa. Havipaswi kuwa kubwa sana, lakini zijitosheleze kwakufanya kazi nzuri na yenye mafanikio.”— Counsels on Health 225.

“Kituo cha tiba cha Battle Creek Sanitarium ni kikubwa mno. Wafanyakazi wengi sana watahitajika kuwahudumia wagonjwa wanaokuja. Asilimia 10% tu ya wagonjwa waliopo hapo sasa ndiyo wangeweza kuhudumiwa kwa ubora na hivyo kupata matokeo bora katika kituo kimoja cha umishenari wa tiba.” - Shuhuda kwa Kanisa 8:205.

(Kwenye Mkutano Mkuu GC uliofanyika Oakland, California, 1903, Daktari J.H. Kellogg alitoa tamko kuhusu jengo ambalo Shuhuda hii ilirejelea. Alisema, "Katika kusimamisha jengo letu tulijenga jengo linaloweza kuchukua wagonjwa 296. Moja ya kumi ya hawa wagonjwa ni 29. Kwa hiyo tunaweza kuhitimisha kwamba "vyumba vya wagonjwa 29 au 30 tu ndivyo vingekuwa kikomo cha kituo chochote kikubwa zaidi cha sanitarium,” ili kiweze kushughulikia ipasavyo mahitaji ya kimwili na kiroho ya wagonjwa, watendakazi, na wanafunzi.)

(Tahadhari kali sana zimetolewa kuhusiana na usahili mkali na uchumi badala ya kuonekana kwa maonyesho yasiyo ya lazima. Tazama Counsels on Health, 214 227, 239, 274-279, 300, 242, 319, 468; Ministry of Healing, 154-168. Hizi zinapaswa kusomwa kwa uangalifu na mtu yeyote anayezingatia kazi hii)

VITUO VYA TIBA HAVIPASWI KUKARIBIANA SANA— “Sio sahihi au haki kuanzisha kazi ya kituo cha Sanitarium mahali ambapo tayari kuna kituo kingine kimeanzishwa.”— Medical Ministry, 154.

“Si mpango Wake Bwana kwa taasisi kuwa karibu sana na nyingine inayofanya kazi ya aina hiyo hiyo.”—Medical Ministry, 151.

“Taasisi zetu, kwa ajili ya nchi yoyote, hazipaswi kusongamana pamoja katika eneo moja. Mungu hakupanga kamwe kwamba nuru ya ya ile Kweli izuiliwe hivyo.”— Counsels on Health, 216

“Miundo-mbinu ya vituo inapaswa kuanzishwa katika maeneo mbalimbali duniani kote… Jitihada zinapaswa kufanywa popote pale ambapo uhitaji ni mkubwa zaidi.”—Counsels on Health, 214.

“Swali la kwanza kutatuliwa katika huduma hii ya kuwa na vituo vya tiba sahili (sanitariums) ni ‘Je, kuwe na kituo cha sanitarium katika eneo hili?’Na Iwapo ni vyema kuwepo, njia ya wajibu ni wazi.”— Medical Ministry, 153.

2- SHULE ZA MAFUNZO—“Sanitarium zitakazoanzishwa kwa ajili ya siku zijazo hazipaswi kuwa na majengo makubwa na ya gharama kubwa. Vituo mahalia vidogo vya tiba vinapaswa kuanzishwa pamoja na shule zetu.”— Medical Ministry, 156. (Tazama pia Counsels on Health, 200.

"Ni vyema kwamba shule zetu za mafunzo kwa watendakazi wa Kikristo zinapaswa kuanzishwa karibu na taasisi zetu za afya, ili wanafunzi waweze kuelimishwa katika kanuni za maisha yenye afya-mtindo wa maisha wenye afya. Taasisi zinazopeleka watendakazi ambao wanaweza kutetea imani yao, na ambao wana imani inayofanya kazi kwa upendo na kuitakasa nafsi, ni za thamani kubwa. Nina maagizo ya wazi kwamba, kwa kadri inavyowezekana, shule zinapaswa kuanzishwa karibu na vituo vyetu vya Sanitarium, ili kila taasisi iwe msaada na nguvu kwa nyingine…… Bwana Ameelekeza katika kuanzishwa kwa vituo vyetu vya Sanitarium, na katika ujenzi wa shule zetu karibu na vituo vyetu vya sanitarium, ili ziwe njia bora katika kuwafunza wanaume na wanawake kwa ajili ya kazi ya kuhudumia wanadamu wanaoteseka.”—Counsels on Health, 301.

“Tahadhari zimetolewa mbele yangu kuhusu kazi ya kuwafunza wauguzi na wainjilisti wamishenari wa tiba. Hatupaswi kuweka kazi hii katika sehemu moja. Katika kila kituo cha tiba kilichoanzishwa, vijana wa kiume na wa kike wanapaswa kufunzwa kuwa wamishenari wa tiba. Bwana atafungua njia mbele yao wanapoenda kufanya kazi kwa ajili Yake.”— Counsels on Health, 225.

“Kila kituo cha Sanitarium kilichoanzishwa na Waadventista Wasabato kinapaswa kufanywa kwa njia za elimu.”— Medical Ministry, 175 (Counsels on Health. 393; 395-396).

"Kazi ya elimu inapaswa kuendelezwa pamoja na vituo vyetu vya Sanitarium au vituo vya tiba sahili. Kuna uhusiano wa karibu kati ya kazi ya shule zetu na vituo vyetu vya tiba; Na, popote inapowezekana, kuna faida zilizoamuliwa katika kuwa na shule katika uhusiano wa karibu na kituo cha Sanitarium. Kungekuwa na mpango ulioamuliwa wenye faida katika mistari yote miwili ya kazi."— Counsels on Health, 242-243.

SHULE ZA KILIMO—"Katika sehemu mbalimbali ardhi na majengo yanapaswa kununuliwa ili yatumike kwa madhumuni ya vituo vya Sanitarium. Watu wetu wanapaswa kutafuta fursa za kununua sehemu ardhi na miundo-mbinu mbali na miji, ambapo tayari majengo yamejengwa na bustani za matunda ambayo tayari yameanza kutoa matunda. Ardhi ni mali yenye thamani."— Counsels on Health, 227.

"Ilikuwa ni mpango Wake Bwana kwamba badala ya kujenga upya kile kituo kimoja kikubwa cha sanitarium, watu wetu wanapaswa kuwekeza vituo vya sanitarium katika sehemu kadhaa. Vituo hivi vidogo vilipaswa kuanzishwa ambapo ardhi inaweza kulindwa kwa madhumuni ya kilimo. Ni mpango wa Mungu kwamba kilimo kitaunganishwa na kazi ya kituo cha tiba na shule zetu. Vijana wetu wanahitaji elimu inayopatikana kutokana na mistari hii ya kazi. Ni vizuri, na zaidi ya hayo, ni muhimu kwamba jitihada zifanywe kutekeleza mpango wa Bwana katika jambo hili."— Counsels on Health, 223.

"Wanafunzi hawapaswi kuruhusiwa kuchukua masomo mengi sana hivi kwamba hawatakuwa na wakati wa mazoezi ya kimwili. Afya haiwezi kuhifadhiwa isipokuwa sehemu fulani ya kila siku imetolewa kushugulisha nguvu ya misuli kwenye hewa ya wazi. Saa zilizotengwa zinapaswa kutolewa kwa kazi ya mikono."—Medical Ministry, 77.

"Mwanafunzi aliyepauka ngozi (pale), na dhaifu ni tusi/aibu ya daima kwa matengenezo ya afya. Ingekuwa bora zaidi kwa wanafunzi kwenda nje na kufanya kazi kwenye udongo. Mazoezi ni mazuri kwa mwili. Mungu anapanga kwamba sehemu zote za mfumo wa mwili wa mwanadamu ushugulishwe kwa kazi na kutumika. Kunapaswa kuwa na saa zilizotengwa kila siku ili kufanya kazi."— Medical Ministry, 79.

"Katika taasisi zetu zote elimu, kazi ya kimwili na kiakili inapaswa kuunganishwa. Kupitia mazoezi ya nguvu ya kimwili, masuala ya tamaa za kinyama huepukwa na kuwekwa katika mipaka sahihi (animal passion). Mazoezi ya afya katika hewa safi nje ya jengo yataimarisha misuli, yatachochea mzunguko sahihi wa damu, husaidia kulinda mwili dhidi ya ugonjwa, na itakuwa msaada mkubwa katika hali

ya kiroho. Kwa miaka mingi imewasilishwa kwangu kwamba walimu na wanafunzi wanapaswa kuungana katika kazi hii. Hili lilifanyika zamani katika shule za manabii."—Medical Ministry, 81.

3- VIWANDA VYA CHAKULA CHA AFYA — "Biashara na mradi wa chakula cha afya inapaswa kuunganishwa na shule yetu, na tunapaswa kuitayarisha. Tunajenga majengo kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa, na chakula kitahitajika kwa wagonjwa. Popote ambapo maslahi yanaamshwa, watu wanapaswa kufundishwa kanuni za matengenezo ya afya. Ikiwa aina hii ya kazi itafanywa, itakuwa ni mpenyo kwa ajili ya kazi ya kuwasilisha ile Kweli. Kazi ya chakula cha afya inapaswa kuanzishwa hapa. Inapaswa kuwa moja ya tasnia iliyounganishwa na shule. Mungu ameniagiza kwamba wazazi wanaweza kupata kazi katika tasnia/industry hii na kuwapeleka watoto wao shule. Lakini kila kitu kinachofanywa kinapaswa kufanywa kwa unyenyekevu na usahili mkubwa zaidi. Hakupaswi kuwa na ubadhirifu katika jambo lolote. Kazi thabiti inapaswa kufanywa……. Mara tu wasaidizi katika safu hii ya kazi wanapotawaliwa na Roho Mtakatifu, Bwana atawapa watu busara na akili mahiri katika utengenezaji wa vyakula, kama vile alivyowapa watendakazi juu ya ufahamu, ujuzi na uwezo katika hema la kukutania."— Counsels on Health, 495-496.

(Kwa zaidi kuhusu tasnia ya chakula cha afya, soma Counsels on Health, 471-496.)

4- TASNIA ZA WANAFUNZI (Student Industries)— "Katika kila mahali ambapo shule zimeanzishwa tunapaswa kusoma ni tasnia gani zinaweza kuanzishwa ambazo zitawapa wanafunzi ajira."—Medical Ministry, 323.

5- WAFANYAKAZI, WATENDAKAZI, NA NYUMBA ZA WANAFUNZI—"Kwa kuunganishwa na vituo vyetu vya tiba kunapaswa kuwa na ardhi, sehemu ndogo ambayo inaweza kutumika kwa ajili ya nyumba za wasaidizi na wengine ambao wanapokea mafunzo ya kazi ya umishenari wa tiba —Counsels on Health, 227."

6- KUMBI ZA MIHADHARA—"Nuru ilipokuja kwamba tuanze kazi ya vituo vya tiba sahili yaani sanitarium, sababu zilitolewa kwa uwazi. Kulikuwa na wengi ambao walihitaji kuelimishwa kuhusu maisha yenye afya…….. Kama sehemu ya tiba, mihadhara ilipaswa kutolewa juu ya tabia sahihi za kula na kunywa na kuvaa. Maelekezo yalipaswa kutolewa kuhusu uchaguzi na utayarishaji wa chakula, kuonyesha kwamba chakula kinaweza kutayarishwa ili kiwe chenye afya, kisichokobolewa wala kusindikwa na chenye lishe, na wakati huohuo kiwe na ladha na cha kupendeza."—Counsels on Health, 469.

“Katika taasisi zetu zote za afya, inapaswa kufanywa kuwa kipengele cha kipekee kwa ajili ya kutoa maelekezo kuhusiana na sheria za afya. Kanuni za matengenezo ya afya zinapaswa kuwekwa kwa uangalifu na kwa kinagaubaga mbele ya wote, wagonjwa na wasaidizi. Kazi hii inahitaji ujasiri wa kimaadili.”—Counsels on Health, 452.

7- SHULE ZA UPISHI—“Vituo vya tiba pamoja na shule zetu zinapaswa kuunganishwa na shule za upishi, ambapo mafundisho yanatolewa kuhusu utayarishaji sahihi wa chakula. Katika shule zetu zote kuwe na wale wanaofaa kuelimisha wanafunzi, wanaume na wanawake, katika sanaa ya upishi. Wanawake haswa, wanapaswa kujifunza jinsi ya kupika.”—Medical Ministry, 270 (Counsels on Health 469).

[1] - VITUO HIVI VYA NCHI VINAPASWA KUENDESHWA VIKIHUSIANA NA KINGINE.

Vituo vya tiba vinapaswa kuunganishwa na mihadhara ya afya na shule za upishi (Counsels on Health, 469-470).

Sanitarium zinapaswa kwa kuunganishwa pamoja na shule zetu, ili kuwafunza watu wetu wote—vijana kwa wazee—kama wamishenari wa tiba (Medical Ministry, 156; Counsels on Health, 211, 225, 227, 243 -244, 301; Medical Ministry, 323).

Sanitarium za zinapaswa kuunganishwa na shule za kilimo (Mashauri ya Afya 223).

Sanitarium zinapaswa kuunganishwa na mashamba shule za kilimo (Counsels on Health, 223; Medical Ministry, 79).

Shule zinapaswa kuunganishwa na tasnia za wanafunzi (Medical Ministry, 323).

Sanitarium na shule zinapaswa kuunganishwa na shule za upishi (Medical Ministry, 270).

Sanitarium zinapaswa kuwa na vyumba vya mihadhara (Counsels on Health, 469).

[2] - VITUO VYA JIJI VINAPASWA KUWA SEHEMU YA KUPATA WATEJA KWA AJILI YA VITUO VYA MASHAMBANI/VIJIJINI

"Nimepewa nuru kwamba, inashauriwa katika miji mingi, migahawa iunganishwe na vyumba vya tiba…… Majengo haya yatatumika kama mahali pa kupata wateja/walengwa wa kusaidiwa kiafa katika sanitarium zilizopo vijijini.”—Counsels on Health, 488.

“Kuanzia sasa kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kuendelezwa kwa dhati na bidii zaidi. Misheni za tiba zinapaswa kufunguliwa kama mashirika ya anzilishi

kwa ajili ya kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu……. Kazi maalum inapaswa kufanywa mahali ambapo watu wanakuja na kuondoka kila wakati. Kristo alifanya kazi huko Kapernaumu muda mwingi kwa sababu hapa palikuwa mahali pa njia panda, ambapo wasafiri walikuwa wakipita mara kwa mara na ambapo wengi mara nyingi walikawia kuondoka. Kristo aliwatafuta watu pale walipokuwa, na kuweka mbele yao zile Kweli kuu kuhusiana na ufalme Wake. Alipokuwa akienda kutoka mahali hadi mahali, alibariki na kuwafariji walioteseka na kuwaponya wagonjwa. Hii ndiyo kazi yetu."— Counsels on Health, 500-501.

(Kwa zaidi juu ya hili, soma shuhuda 9, 121-122; Counsels on Health, 318; Ministry of Healing, 22, 29 30; Luka 4:28-41; 5:17-19).

"Mwalimu mkuu aliweka mipango kwa ajili ya kazi Yake. Jifunze mikakati hii. Tunampata akisafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine, akisindikizwa na umati wa wasikilizaji wenye shauku. Alipoweza, angewaongoza mbali na miji iliyojaa watu, hadi kwenye utulivu wa mashambani. Hapa angeomba pamoja nao, na kuzungumza nao juu ya zile Kweli za milele."—Medical Ministry, 299. [Soma ukurasa mzima.]

(Kwa zaidi juu ya hili: Huduma ya Uponyaji, 52-54; Christ's Object Lesson, 24-27; Huduma ya Uponyaji, 261-268; Mathayo 5:1; 13:1-2; 14:13-14; 15:29-30).

3 - KIWANGO CHA VITUO VYA WAMISHENARI WA TIBA

1 - NDANI YA MIJI YA AMERIKA—"Hebu wengi sasa waulize, 'Bwana, utaniruhusu nifanye nini?' Ni kusudi la Bwana kwamba njia Yake ya uponyaji bila dawa italetwa katika umashuhuri, katika kila jiji kubwa kupitia taasisi zetu za tiba. Mungu huwekeza kwa heshima takatifu wale wanaotoka kwa uwezo Wake kuponya wagonjwa. Hebu nuru iangaze zaidi na tena mbali zaidi, katika kila mahali ambapo inawezekana kupata mlango wa kuingia. Shetani atafanya kazi iwe ngumu kadri iwezekanavyo, lakini nguvu za Bwana zitakuwa juu ya watendakazi wote wenye mioyo ya kweli. Tukiongozwa na mkono wa Baba yetu wa Mbinguni, na tusonge mbele, tukiboresha kila fursa ya kupanua kazi ya Mungu."—Medical Ministry, 325.

"Misheni ni muhimu kama msingi wa jitihada za umishenari katika miji yetu."— Injili Workers, 365.

"Katika kila jiji ambalo tuna kanisa, kuna uhitaji wa mahali ambapo matibabu yanaweza kutolewa."— Counsels on Health, 468.

“Kutokuwa na kiasi kumeujaza ulimwengu wetu, na misheni ya tiba (utume wa tiba) inapaswa kuanzishwa katika kila jiji. Kwa hili simaanishi kwamba taasisi kubwa zinapaswa kuanzishwa, na kuhitaji fedha nyingi zitumike katika kuendesha.”—Medical Ministry, 322.

"Mianzo inaweza kufanywa katika kila sehemu maarufu ambapo mikutano ya kambi hufanyika. (wakati huo, juhudi za uinjilisti kama efoti, au mahubiri ya hadhara, zilifanywa kwenye mahema, zikihama kutoka sehemu moja mpaka nyingine). Fanya mwanzo mdogo, na upanue kadri hali inavyoweza kuruhusu. — Counsels on Health, 468.

Vituo vinapaswa kusimikwa katika majiji yote ambayo hayajui kazi kubwa ambayo Bwana angefanya ili kuuonya ulimwengu kwamba mwisho wa mambo yote umekaribia.”— Counsels Health, 214.

Boston na miji mingine ya kaskazini mashariki ya Marekani ijulikanayo kama New England cities: Counsels on Health, 554-555 / New York: 7 Testimonies, 37 / San Francisco: 7 Testimonies, 110-111 / Los Angeles: 7 Testimonies, 55 / San Diego: 7 Testimonies, 55 / Southern California: 7 Testimonies,112 / The South: 7 Testimonies, 57, 227; Counsels on Health, 494/ Prominent thoroughfares: Counsels on Health, 500-501 / Tourist Resorts: 7 Testimonies, 55 / Inland and seaside resorts: Counsels on Health, 488

2 - KATIKA MAENEO YA KIGENI—Katika nchi za nje shughuli nyingi za kuendeleza ujumbe huu ni lazima zianzishwe na kupelekwa mbele. Kufunguliwa kwa migahawa ya Afya na usafi (Hyegenic Restaurants) na vyumba vya tiba, na kuanzishwa kwa Sanitarium kwa ajili ya huduma ya wagonjwa na wanaoteseka na wenye dhiki, ni muhimu huko Ulaya kama tu ilivyo Amerika. — Shuhuda kwa Kanisa 7: 51.

“Bwana anafanya kazi bila upendeleo kwenye kila sehemu ya shamba Lake la mizabibu……. Katika nchi za kigeni mashirika mengi ya umishenari wa tiba yanapaswa kuanzishwa na kuendelezwa mbele hadi kupata mafanikio.”— Counsels on Health, 224.

Katika nchi nyingi misheni za tiba zinapaswa kuanzishwa ili kutumika kama mkono wa Mungu wa msaada katika kuwahudumia waliotaabika. — Shuhuda kwa Kanisa 7: 51.

3 - KUENENDA KATIKA ULIMWENGU WOTE—“Kristo aliukumbatia ulimwengu katika kazi Yake ya umishenari, na Bwana amenionyesha kwa ufunuo kwamba si mpango Wake kwamba vituo vikubwa visimikwe, taasisi kubwa kuanzishwa, na

fedha za watu wetu katika sehemu zote za dunia kutindikiwa na kuisha katika kutegemeza hizi taasisi chache kubwa, wakati kipaumbele au umuhimu katika nyakati hizi hutaka jambo fulani lifanyike wakati majaliwa ya Bwana yanafungua njia, katika sehemu nyingi. Miundo mbinu na vituo vinapaswa kuanzishwa katika maeneo mbalimbali duniani kote. Kwanza tuanze na kituo ki kwendamoja, na kisha sehemu nyingine ya shamba la mizabibu, hadi mashamba yote ya mizabibu yamelimwa. Juhudi zinapaswa kufanywa popote ambapo hitaji ni kubwa zaidi. Lakini hatuwezi kuendeleza vita hivyo vikali, na wakati huohuo kufanya kuwa wabaradhifu kwa kutokuwa wachumi wazuri na kupitiliza katika kuwekeza kwenye sehemu chache tu."— Counsels on Health, 214.

"Kuanzia sasa kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kuendelezwa kwa dhati na bidii zaidi. Misheni za tiba zinapaswa kufunguliwa kama mawakala waanzilishi katika kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu. Ni kubwa kiasi gani, hitaji la nyenzo za kufanya kazi hii! Misheni za tiba za injili haziwezi kuanzishwa bila msaada wa kifedha. Kila mradi kama huo unahitaji huruma yetu na fedha zetu, majengo au miundo-mbinu hiyo na vifaa hivyo vinaweza kutolewa ili kufanikisha kazi hiyo."— Counsels on Health, 500.

Mungu amewastahilisha watu Wake kuangazia nuru ulimwengu. Yeye Amewapatia uwezo/stadi ambazo kwazo watu wanapaswa kupanua kazi Yake mpaka itakapoizunguka dunia yoe. Katika sehemu zote za dunia waamini wanapaswa kuanzisha Sanitarium, shule, nyumba za uchapishaji, na vituo vya ukarimu na udugu, kwa ajili ya kufanikisha kazi Yake. Shuhuda kwa Kanisa 7:51.

"Kuna hitaji kubwa katika sehemu zote za dunia kwa walimu wa Kikristo na wamishenari wa tiba. Katika sehemu zote za ndani ya nchi na nje ya nchi, milango ipo wazi kwa wale wanaoweza kufanya mema kwa mwili na roho, wakiwasilisha nuru ya thamani ya Ukweli. Kupuuza siku za nyuma katika mwelekeo huu lazima kusiendelezwe. Nuru kubwa imeonyesha kwenye njia yetu katika njia zingine zaidi ya zile zingine, na bado maendeleo yetu kwenye kazi hii yamekuwa nyuma sana ya nuru ambayo tumekuwa nayo. —Fundamentals of Christian Education, 231-232.

"Ni kusudi la Bwana kwamba katika kila sehemu ya taasisi zetu za afya duniani zitaanzishwa kama tawi la kazi ya injili. Taasisi hizi zinapaswa kuwa wakala Wake Bwana kwa ajili ya kufikia daraja la watu ambalo hakuna kitu kingine kitakachoweza kuwafikia. Taasisi hizi hazihitaji kuwa na majengo makubwa, lakini zinapaswa kupangiliwa hivyo ili kazi yenye matokeo ifanyike."— Counsels on Health, 468.

“Hakuna mabadiliko katika jumbe ambazo Mungu ametoa hapo awali. Kazi katika miji ni kazi muhimu kwa wakati huu. Miji inapofanyiwa kazi kama vile Mungu atakavyo ifanywe, matokeo yatakuwa ni operesheni ya harakati kubwa ambayo bado hatujawahi kuishuhudia.”—Medical Ministry, 304.

"Tutaona kazi ya umishenari wa tiba ikipanuka na kuongezeka katika kila hatua ya maendeleo yake, kwa sababu ya kuingia kwa mamia na maelfu ya vijito, hadi dunia yote ifunikwe kama maji yanavyofunika bahari." —Medical Ministry, 317

Tumaini pekee la mambo yaliyo bora ni katika kuwaelimisha watu kanuni sahihi. Madaktari wawafundishe watu kwamba nguvu za urejeshwaji hazipo katika madawa ya famasia, bali katika asili. — Ministry of Healing, 127

SEHEMU YA 3

KANUNI NA VIWANGO

SURA YA 8

KANUNI ZA KAZI ZINAZOPASWA KUZINGATIWA

(Marejeleo tu, sura ifuatayo itaweka nukuu zilizotolewa hapa)

1- Kumtegemea Mungu pekee kwa kila hitaji la mwanadamu: Yohana 3:27; 15:5; 2 Nyakati. 20:12; Yer. 10:23; 2 Kor. 3:5; Kut. 20:3: Mit. 3:5; 6 Shuhuda, 359-364; Ministry of Healing, 48-49.

2- Uaminifu katika kushika mafundisho ya Biblia na Roho ya Unabii: Isa. 8:20; Kumb. 8:1-3; Mt. 4:4; Zaburi 119:11; 1 Kor. 10:11; Testimonies for the Ministers, 105-111.

3- Simama kwenye kanuni katika kila uamuzi unaofanywa: Isa. 8:20; Ayubu 1:8; Matendo 5:29; Mt. 7:24; Wafalme na Manabii 483; Medical Ministry, 71-73: Counsels on Health, 287-296; Medical Ministry, 124; Ministry of Healing, 25.

4- Kwa unyenyekevu na usahili, si kwa kujionyesha katika Taasisi, majengo, vyombo na kazi: Zaburi 116:6; Marko 10:5; 2 Kor. 1:12; 11:3; Mt. 23:5; Counsels on Health, 274-279, 300, 319; Evangelism,136-139; Medical Ministry, 160; Ministry of Healing, 47.

5- Uaminifu thabiti katika masuala yote: Kum. 25:15; Warumi. 12:17; Medical Ministry, 71-72.

6 - Unadhifu na utaratibu katika kila jambo linalofanyika: Medical Ministry, 212.

7- Uaminifu katika mambo madogo: Mhu. 9:10; Luka 16:10; Yohana 6:12; Counsels on Health, 404, 428; Ministry of Healing, 40; Patriarchs and Prophets, 573-574.

8- Usimamizi mzuri wa Uchumi katika Maeneo Yote: Mt. 10:8- 10; Yohana 6:12; Counsels on Health, 280, 281, 299, 300; Ministry of Healing, 48.

9- Pesa taslimu pekee—epuka deni wewe binafsi- na wengine: Rum 13:8; Mithali. 22:7; Luka 6:35; Zaburi 37:21. Kamwe usiwe na madeni ya mwingine: Mit. 6:1-2; 11:15;17:18; 22:26; 3 Shuhuda 173, 175; 6 Shuhuda, 206-207, 210-213, 216, 217, 469,

470; 7 Shuhuda, 206-209, 235, 236, 284; Counsels on Health, 262, 263, 304, 305; 8 Shuhuda, 89; 9 Shuhuda, 71; 9 Shuhuda, 271-272.

10. Pasiwe na mikataba isiyoweza kubatilishwa—Usisaini mikataba, makubaliano au ukodishaji/uazimaji ambao, kwa kweli utakufunga pale ulipo kwa muda mrefu. Counsels on Health 238; 9 Shuhuda 170-171. Hii, bila shaka, itajumuisha kusainiwa kwa ukodishaji na jiji: Country Living, 32; 9 Testimonies, 92-93; Evangelism, 29; Country Living, 8-11, 13, 29, 30.

11-Malipo ya haki au kutotozwa ada ya tiba—Njia mbili zimetolewa katika Roho ya Unabii. Tumeagizwa kutoza ada za matibabu za uaminifu, na za haki (Medical Ministry, 121- 122, 125, 128). Lakini njia ya juu zaidi—mbinu ya Bwana Mwenyewe—inatolewa waziwazi (Mt. 10:1, 7-10; Lk. 6:38; 22:35; Mt. 6:25-34; Zaburi 37:3; Isa. 65:13; Medical Ministry, 123, 125, 126, Life Sketches of Ellen White 302. Medical Ministry 131-133 Prophets and Kings, 65 Medical Ministry, 152, 154, 155, 156, 159, 181, Mount of Blessing, 144, 145, 147, 148 Desire of Ages, 273; Ministry of Healing 480-482). Kila mmoja anapaswa kuwa huru kujitafutia ushauri wa Bwana kuhusu njia anayopaswa kufuata. Wengine hutumia viwango vya mpango wa kutotoza na wengine hawatumii. Soma na uombe mwongozo.

12- Mshahara sahili na unaolingana na kazi —Isipokuwa kwa wale wanaotoa sehemu au wakati wao wote na huduma: Matendo 2:44, 45; 4:32; Counsels on Health, 302-307, 314-318, 311.

13- Mpango wa ushirikiano/ubia, mashirika yasiyo ya huduma, ambayo hayatengenezi fedha: Kila kitu kinachozidi mapato kiandae kujenga vituo mahali pengine kinachofanana na hiki (Kum. 8:18; Mithali 3:27, 28; Mat 6:19, 20; Counsels of Health,308-310, 220, 224, 225; Medical Ministry, 165).

14- Mali Chache—Fikiria kwa makini kila ununuzi unaoufanya, Usinunue zaidi ya mahitaji yako na kumiliki zaidi ya vile unavyohitaji au visivyo muhimu (Mt. 10:7-10; 19:21; 8:19-20; Ufu. 3:17; Luka 12:33; Mt.13:44; Met. 13:17; Marko 4:19; 1 Tim. 6:7; Mt. 16:24-26; 8 Shuhuda, 52-53).

15- Kukagua Ukuaji—Baada ya kufikia ukubwa uliokusududiwa, ujenzi unapaswa ukome hapo na taasisi nyingine ianzishwe mahali pengine (Counsels on Health, 308-310, 220, 224, 225, 275, 217; Medi cal Ministry, 164, 322; 21 Testimonies, 7 Testimonies; 212, 214-227, 239).

16- Endelea Kusonga—Wakati wafanyakazi wamefunzwa na kazi imesimikwa mahali pamoja, anza kituo kingine cha mvuto mahali pengine (Mt. 9:35, 10:11, 23; 28:19; Mdo. 1:8 Ministry of Healing, 17. Counsels on Health, 430; 396; Evangelism, 458 Testimonies, 148: 9 Testimonies, 171 Counsels on Health, 517, 518, 542).

17- Fuata mwongozo mzima—Ishi kila mara na familia yako mashambani, au vijijini—fanya kazi mijini, lakini usiishi humo. Soma Country Living, kitabu kizima. Daima changanya afya, ustawi wa jamii, uinjilisti, na elimu (Mt. 4:23-24; 9:35, 36; 28; 18-20; Mk 16:15-17; Luka 4:16-21; Isa. 58:1-14). Afya na Ustawi (Welfare Ministry, 117- 133; Ministry of Healing, 139-208). Health and Evangelism (Evangelism, 513-547; Counsels on Health, 497-558; Medical Ministry, 237-257). Afya na Elimu (Counsels on Health, 425-470; Fundamentals of Christian Education, 145-148, Ministry of Healing, 125-160. Welfare and Evangelism: Welfare Ministry, 295-319). Ustawi na Elimu (Ministry of Healing, 183-200, Welfare Minis try, 194-202). Evangelism na Education (Counsels for Parents, Teachers, and Students, 493-545; Fundamentals of Christian Education, 201-211).

18- Walete Wagonjwa kwa Yesu—Fuata kielelezo alichotoa Yeye katika kazi ya Umishenari wa Tiba (Ministry of Healing, 95-107; Welfare Ministry, 53-59, 117-124).

A - Walete kwa Tabibu Mkuu—Mungu pekee Ndiye anayeweza kuponya (Zaburi 103:2-5; Kut. 15:26; 23:25; Yohana 10: L0; Ministry of Healing; 112-113, 130-131; Medical Ministry, 7-30, 120; Counsels on Health, 29, 346).

B - Mwombe Mungu akuponye, lakini mwambie "mapenzi Yako yatimizwe" (Yakobo 5:14-16; Luka 22:42; Warumi 8:26; Zaburi 37:5, 7; Ministry of Healing, 225-233, Counsels on Health, 247, 373-376).

C - Badilisha mazoea mabaya; Tii sheria za afya (Kutoka 15:26; Yohana 5:14; 8:11; 1 Kor. 3:16-17; 6:19-20; Kut. 23:25; Luka 9:23; 1 Kor. 10:31; Flp 4:13 Ministry of Healing,126-129; 234-268; 271 346; Counsels on Health, 37-303; Medical Ministry, 221-236. Counsels on Diet and Food, kitabu kizima).

D - Kusafisha mwili (Ministry of Healing, 127; Zaburi 51:7; Isa. 1:16; 2 Selected Message, 289, 446, 460; Counsels on Health, 61, 63. Kufunga/saumu: Zaburi 107:17-21; Mt. 17:19-21; 6:16-18, 4:1-2; Medical Ministry, 281-282; 2 Selected Message, 305-450; Counsels on Health, 477, 148; Ministryb of Healing, 283; Counsels on Diet and Food, 185-191).

E - Tumia tiba rahisi ya maji (Zaburi 51:1, 7; 2 Wafalme 5:10, 14; Waamuzi 9:6-7; Law. 11-15; Ministry of Healing, 127, 237, 276; Counsels on Health, 323, 55, 56, 61, 62 103, 104, 168,169, 247; Medical Ministry, 227, 228, 230, 233, 281, 282; Shuhuda 5, 195, 443; 2 Selected message 281, 266, 287, 288,

289, 290, 291, 294, 297, 304, 446, 450, 451, 453, 456, 458, 460, 463).

F- tumia chakula cha mimea sahili ya shambani (Eze. 47:12; Ufu. 22:2; Zaburi 104:14; MedicalMinistry, 230-231; 2 Selected Messages, 279, 287-291; 293- 302. Pia soma matumizi ya mitishamba, kijitabu kizima).

G- Mshukuru Bwana kwa kupona (1 The. 5:18; Luka 17:12-19; 19:37; Huduma ya uponyaji, 251 256, 100, 101, 233; mashauri juu ya afya, 348). Kwa Vitabu vya Kiswahili angalia RohoYaUnabii.Org, au MaarifaMtandaoni.Com au EllenWhite estate.

H – endelea kumwamini Bwana na kutii sheria Zake (Yohana 5:14; Kutoka 15:26; Kum. 28; Ministry of Healing, 233).

19- Kamwe usitoe kwa watu sumu iliyo katika mfumo wowote (Kut. 20:13; 1 Kor. 3:16-17; Kum. 27:24-25; Mithali 6:16-17; Mwa. 9:5; Kum. 29:18-20; Hes. 35:16-18; Hab. 2:10; Eze 22:8-9. Ministry of Healing, 126-127, 146, 233; mashauri juu ya afya, 261, 212, 323, 389, 393,394, 452, 469, 501; Medical Ministry, 27, 29, 57, 75, 85, 125, 221-229, 231; 2 Selected messages, 279-284, 287-291, 293-295, 305;441-454, 456, 460).

20- Kazi ya pamoja (teamwork) na kutiana moyo, kamwe usiwe mtu wa kukosoa-kosoa (Mt. 7:1- 5; Rum. 14:4-13; Luka 22:32; 1 Kor. 4:5; Kut. 17:12; Mt. 18:19;Counsels on Health, 242-244, 296-298, Medical Ministry, 137, 138, 164).

21 – Shauriana pamoja na ndugu: Fikiria kwa makini mashauri yote ambayo hayapingani na kanuni za Bwana (Mit. 11:15; 15:22; 24:6; Flp. 2:2-3; cf: Isa. 30:1; Rum. 11:34; Testimonies for Ministers, 252; Counsels on Health, 296).

22- Hakuna watawala/mabosi - wakati hakuna kanuni zilizo hatarini, kila mmoja yuko huru kutafuta mwongozo wa moja kwa moja kutoka kwa Bwana katika kutekeleza kazi yake. Wakati hakuna kanuni inayokiukwa, hakuna anayepaswa kutafuta dhamiri ya mtu mwingine ili kumwelekeza namna hususani ambayo watu wa Mungu wataendeleza kazi hiyo (Mt. 23:8-11; Gal. 2:4; Kut. 20:3; Zaburi 23:8-11; 119:45; Medical Ministry, 203; Testimonies to Ministers, 347-359, 374-386).

23- Onyesha dhambi—kanuni zinapokiukwa, hakikisha ni zipi; Kisha kwa unyenyekevu wa kina wa roho, na baada ya kujipeleleza moyoni kwa dhati na bidii, shauri kwa upole na mhusika wa jambo hili. Warudishe wana-kondoo kwa Yesu kwa uangalifu, ukikumbuka ni mara ngapi wewe mwenyewe umepotea (Yakobo 5:19-20; Yuda 23; Zaburi 51:12; Isa. 58:1; Yoshua 7:11-12; Isa. 59:2, 64:7; Ministry of Healing, 113-115; Shuhuda 3, 293-304, 252-293; 1 Selected Message, 195-197).

24- Usitoe siri au Usisaliti imani au ujasiri watu walionao kwako: Linda masilahi ya mgonjwa na kazi (Isa. 39:1-6; Mhu. 3:7; Mit. 17:27; 11:13; 25:9; 13:3; 21:23; Medical Ministry, 212-213).

25- Kutojihusisha na vyama vya kidunia au vyama vya siri (secret society). (Ufu. 18:1-4, 2 Kor 6:14-18, Efe 5:6-7,11; Mwanzo 19:15.

Kutoka 20:3; Kut. 23:2, 32-33; 33:15-16; 34:12-15; Hesabu 16:26; 25:1-5; Yoshua 23:6-13; Kum. 7:24; 12:30; 13:6-8; 1 Wafalme 11:2; 2 Wafalme 1:3; 17:15; 2 Nya. 16:12; 19:2; Ezra 4:3; 6:21; 9:12, 14; 10:11; Neh. 9:2; 10:30; 13:13; Zaburi 1:1; 6:8; 26:4, 5, 9; 28:3; 31:6; 50:18; 84:10; 101:4, 7; 106:34-35; 119:115; 120; 139:19, 21-22; 141:4; Mit. 1:10, 11, 14, 15; 4:14, 15; 9:6; 13:20; 14:7; 20:19, 22:10; 24:1; 29:16, 24; Mhubiri 9:18; Isa. 1:23; 8:11-12; 52:11; Yer. 15:17; 51:6; Hos. 4:17; 7:5, 8, 9; Amosi 3:3; Mika 6:6; Yohana 18:18, 25; 1 Kor. 10:21, 31; 15:33, 1 Tim. 6:5; 2Tim. 3:4, 5; Ufu. 2:2; 2 Petro 2:18, 19; 3:17; 1 Yohana 1:5-7; 2:15; Counsels on Health, 226, 237-239, 274, 291, 300, 401, 456-459, 520, 521, 522, 525, Medical Ministry, 123, 125, 206, 207, 24-25, 62-63, 71-72, 75, 84-85, 127, 132, 160, 161, 164, 329; Shuhuda 8, 45; Shuhuda 9, 175; Country Living, 10-12; Soma kitabu kizima).

26 – Jitahidini kupata umoja miongoni mwa watenda kazi na katika Kanisa, bila kukana kanuni za imani (Yohana 17:21; Rum. 12:5; 1 Kor. 1:10; 2 Kor. 13:11; Efe. 4:3; 1 Petro 3:8; Isa. 52:8; 2 Selected Message, 158-161; Gospel Workers, 483-490; 5 Shuhuda 571-573)

27. Uaminifu kwa Uadventista wa Sabato—bila ya kuvunja kanuni zile za msingi zilizoansishwa katika Matendo 23:5, Kutoka, 22:28, Mathayo 22:21, Matendo 5:27-29, Testimonises for the Ministers, 15-23, 32, 61; 2 Selected Messages 63, 71, 387-479; Great Controversy, 39-46; Testimonies for the Ministers, 53).

SURA YA 9

KANUNI ELEKEZI KATIKA UANZISHWAJI NA UENDESHAJI WA TAASISI ZA UMISHENARI WA TIBA

Ingawa nukuu nyingi katika sura hii zinanarejelea Vituo vya afya, kanuni zinazohusika zinaweza kutumika kwa taasisi zingine pia.

1- LENGO

UTUKUFU WA MUNGU NA WOKOVU WA WANADAMU

“Sanitarium ambazo zimeanzishwa zinapaswa kuunganishwa kwa karibu na bila kutenganishwa na injili. Bwana ametoa maagizo kwamba Injili iendelezwe mbele; Na injili inajumuisha matengenezo ya afya katika hatua zake zote. Kazi yetu ni kuuangazia ulimwengu; kwa maana ni mpofu kwa harakati zinazofanyika, ikitayarisha njia kwa ajili ya mapigo ambayo Mungu ataruhusu yaufikie ulimwengu.”—Medical Ministry, 159- 160.

"Madhumuni ya taasisi zetu za afya, sio kama yale ya hospitali mara zote. Taasisi za afya zilizounganishwa na kazi ya kufunga injili duniani zinasimamia kanuni kuu za injili katika utimilifu wake wote. Kristo Ndiye atayepaswa kufunuliwa katika taasisi zote zinazohusiana na kazi ya kufunga kazi ya Bwana, lakini hakuna hata moja kati ya hizo inayoweza kuifanya kwa ukamilifu kama vile taasisi za afya ambapo wagonjwa na mateso huupata nafuu ili kupata msaada na ukombozi dhidi ya maradhi ya kimwili na kiroho. Wengi wa hawa, kama wale watu waliopooza zamani katika Maandiko, wanahitaji msamaha wa dhambi kwanza, na kisha watahitaji kujifunza jinsi ya ‘kuenenda, na wasitende dhambi tena.’ ”—Medical Ministry, 27- 28.

“Ikiwa kituo cha sanitarium kilichounganishwa na ujumbe huu wa kufunga kazi, kinashindwa kumwinua Kristo na kanuni za injili kama zilivyoandikwa katika ujumbe wa malaika wa tatu, basi kinashindwa katika kipengele chake muhimu zaidi, na kinapingana na lengo hasa la kuwepo kwake.”—Medical Ministry, 28.

“Mara nyingi katika utunzaji wa wale wanaoteseka, umakini zaidi unatolewa kwa mambo madogo-madogo, wakati hitaji la wagonjwa la zile Kweli kuu zote za kuokoa za injili, ambazo zingehudumia roho na mwili, husahauliwa. Unapopuuza kutoa ombi kwa ajili ya wagonjwa, unawanyima baraka kubwa; Kwa maana malaika wa Mungu wanangoja kuhudumia nafsi hizi kwa kujibu maombi yako.”—Medical Ministry, 195.

“Japokuwa tunakutana na gharama kubwa katika kuanzisha Sanitarium, inabidi jambo hili lifanyike, kwa vile kusudi letu kubwa ni kuongoa roho, na pia kuponya miili ya wanaume na wanawake. Mungu anapanga kwamba kwa njia ya mawakala hawa wa upandaji Wake mwenyewe, matajiri na maskini, walio juu na wa chini, watapata mkate wa mbinguni na maji ya uzima. Yeye Anapanga kwamba wataelimishwa katika mazoea sahihi ya mtindo wa maisha wenye afya, kiroho na kimwili. Wokovu wa roho nyingi uko hatarini.”— Mashauri kuhusu Afya, 470.

“Nimeagizwa kwamba tusichelewe kufanya kazi inayohitaji kufanywa katika maeneo ya matengenezo ya afya. Kupitia kazi hii tunapaswa kufikia roho katika barabara kuu na barabara za vichochoroni. Nimepewa nuru maalum kwamba katika vituo vyetu vya Sanitarium. . Wanawake wanapaswa kufundishwa jinsi ya kutunza miili yao wenyewe, na wakati huo huo jinsi ya kusimikwa vyema katika imani.”— Counsels on Health, 393.

““Hebu kazi ya Bwana na isonge mbele. Hebu kazi ya umishenari wa tiba na kazi ya elimu zisonge mbele. Nina hakika kwamba huu ndiyo upungufu wetu mkubwa----watendakazi dhati na wenye bidii, waliojitoa, wenye akili mahiri na uwezo. Katika kila mji mkubwa kunapaswa kuwa na uwakilishi wa kazi ya ile Kweli ya umishenari wa tiba. Hebu sasa wengi na wajiulize, Bwana, Je, unataka nifanye nini? Ni kusudi la Bwana kwamba njia Yake ya uponyaji bila madawa ya famasia, italetwa katika umashuhuri katika kila mji mkubwa kupitia taasisi zetu za tiba.” Mungu huwekeza kwa heshima takatifu wale wanaoenda mbali zaidi na tena mbali zaidi, katika kila mahali ambapo inawezekana kupata nafasi ya kuingia. Shetani atafanya kazi iwe ngumu kadri iwezekanavyo, lakini nguvu za Bwana zitakuwa juu ya watendakazi wote wenye mioyo ya kweli. Tukiongozwa na mkono wa Baba yetu wa Mbinguni, na tusonge mbele, tukiboresha kila nafasi ya kupanua kazi ya Mungu.”—Counsels on Health, 393-394.

Taasisi ya afya, inayoendeshwa ipasavyo, inatoa sifa kwa kazi yetu katika nyanja mpya.”— Medical Ministry 25.

“Uongofu wa roho sasa unapaswa kuwa lengo letu moja.”—Medical Ministry, 328.

Tunapaswa kukumbuka daima kwamba ufanisi wa kazi ya umishenari wa tiba ni katika kuwaelekeza wanaume na wanawake wadhambi kwa Mtu wa Kalvari, aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Kwa kumtazama watabadilishwa kuwa mfano Wake. Lengo letu katika kuanzisha vituo vyetu vya injili ni kuwatia moyo wagonjwa na watu wanaoteseka kumtazama Yesu na kuishi.”—Counsels on Health, 528. “

Kuanzishwa kwa vituo vya Sanitarium ni mpango wa Mungu, ambapo watu kutoka makanisa yote wanapaswa kufikiwa na kueleweshwa Ukweli kwa wakati huu."—Counsels on Health 470.

"Saa za wasiwasi ambazo wametumia, hali zenye kutatanisha ambazo wamelazimika kukutana nazo, huzuni ya moyo kwa sababu wengine walikataa kuona na kupokea vitu vinavyoleta amani yao, vimesahauliwa. Kujikana nafsi kwao walikokufanya ili kusaidia kazi hiyo hakukumbukwi tena. Wanapozitazama roho walizotaka zije kwa Yesu, na kuziona zikiokolewa, zikiokolewa milele,—Kumbukumbu kubwa za rehema ya Mungu na upendo wa Mkombozi,—Zitasikika zikirindima katika matao ya mbinguni, vifijo vya sifa na shukrani."—Medical Ministry, 135.

"Hebu tukumbuke kwamba wakala mmoja muhimu zaidi ni kazi yetu ya umishenari wa tiba. Hatupaswi kamwe kupoteza mtazamo wa lengo kuu la kuanzisha sanitarium zetu— kusonga mbele kwa kazi ya Mungu inayofunga."—Counsels on Health, 233.

2- MAHALI

[1] – ISIWE KARIBU SANA NA VITUO VINGINE VYA TIBA

"Kuanzisha kituo cha Sanitarium mahali ambapo tayari kuna kituo kingine cha afya kilichoanzishwa, ni kukosa hekima ya utumiaji wa fedha au na kutotenda haki,."—Medical Ministry, 154.

"Sio mpango Wake Bwana kwa taasisi kuwa karibu sana na taasisi nyingine inayofanya kazi ya aina hiyo hiyo; Kwa vile taasisi yoyote popote pale ilipo, lazima iwe na miundo-mbinu na vifaa vizuri na watoa huduma (wasaidizi) wenye uzoefu."—Medical Ministry, 151.

"Taasisi zetu, kwa kwenye nchi yoyote, hazipaswi kukusanywa pamoja katika eneo moja. Mungu hakupanga kamwe kwamba nuru ya ile Kweli iwekwe hivyo."—Counsels on Health, 216.

Kuna madaktari ambao, kwa sababu ya uhusiano wao wa zamani na vituo vyetu vya sanitarium, wanaona ni faida kuwa karibu na taasisi hizi; nao hufumba macho yao kwenye shamba kubwa la Bwana ambalo halijafanyiwa kazi, vilivyopuuzwa na havifanyiwi kazi, ambamo kazi isiyo na ubinafsi ingekuwa baraka kwa wengi."— Counsels on Health, 394.

Swali la kwanza kuwekwa sawa na kutatuliwa ni; Je, kunapaswa kuwa na sanitarium katika eneo hili, au Je, ni kweli sanitarium inahitajika mahali hapa? Kama kunapaswa kuwa, basi njia ya wajibu ni wazi."—Medical Ministry, 153.

[2] – AMBAPO KUNA HAJA/UHITAJI

"Miundo-mbinu ya taasisi, au viuto vinapaswa kupandwa katika maeneo mbalimbali duniani kote. Kwanza eneo moja, na kisha sehemu nyingine ya shamba la mizabibu liingizwe, hadi maeneo yote yamelimwa. Juhudi zinapaswa kufanywa popote pale ambapo hitaji ni kubwa zaidi. Lakini hatuwezi kuendeleza vita hivyo vikali na wakati huohuo kuwa na matumizi yenye ubaradhifu au ya kupitiliza kiasi katika sehemu chache." —Counsels on Health, 214.

"Tunapaswa kuanzisha vituo vingi, kwa kujenga miundo-mbinu na kuweka vifaa katika majiji ya Marekani, na hasa katika majiji ya kusini mwa nchi, ambako bado ni sehemu ndogo tu iliyokwisha kufanyiwa kazi."— Counsels on Health, 224.

"Vituo vinapaswa kuanzishwa katika majiji yote ambayo hayajui kazi kubwa ambayo Bwana angefanya ili kuuonya ulimwengu kwamba mwisho wa mambo yote umekaribia."— Counsels on Health, 214.

"Mwanzo unaweza kufanywa katika kila sehemu maarufu ambapo mikutano ya kambi hufanyika. Anza kwa hatua ya mianzo midogo na kisha upanue kadri hali zinavyoweza kuhitaji."— Counsels on Health, 468.

[3] – NJE YA MIJI AU MASHAMBANI PEKE YAKE

"Wale ambao wanahusika na kuchagua mahali pa kupanda vituo vyetu vya sanitarium wanapaswa kusoma kwa maombi tabia na lengo la kazi ya kituo cha afya. Wanapaswa kukumbuka daima kwamba wanafanya kazi ili kurejesha sura ya Mungu ndani ya mwanadamu." — Counsels on Health, 265.

"Ubinafsi usiwepo, wala matamanio binafsi ya ukuu, hakika haya hayapaswi kuruhusiwa kuingia katika kazi ya kuchagua maeneo kwa ajili ya vituo vyetu vya Sanitarium…..Hebu tujifunze kutoka Kwake Bwana kutochagua vituo vyetu vya afya kwa kufuata matamanio yetu au ladha zetu zinazotupendeza, lakini sehemu zile zinazofaa zaidi kwa kazi yetu." —Counsels on Health, 265.

"Nimepewa nuru kwamba katika kazi ya umishenari wa tiba tumepoteza faida kubwa kwa kushindwa kutambua hitaji la kufanya mabadiliko katika mipango yetu kuhusu eneo la sanitarium. Ni mapenzi ya Bwana kwamba taasisi hizi zianzishwe nje ya jiji. Zinapaswa kuwa mashambani, katikati ya mazingira yenye kuvutia kwa kadri iwezekanavyo." ——Counsels on Health, 265. (Sanitariums in

the country: Counsels on Health, 265-268; the only exception to this that is given: Counsels on Health, 488; Medical Ministry, 323).-

[4] - KISIZUNGUKWE NA NYUMBA ZA KIFAHARI

"Inaweza kuonekana kwetu kuwa itakuwa bora kuchagua maeneo yetu ya kituo cha afya miongoni mwa watu matajiri, kwamba hii ingetoa tabia kwa kazi yetu na tutapata wafadhili, na ulinzi salama kwa ajili ya taasisi zetu. Lakini katika hili hakuna asubuhi (nuru). 1 Samweli 16:7 Bwana haangalii kama binadamu aangaliavyo; maana wanadamu huitazama sura ya nje, bali Bwana huutazama moyo. Kadri ambavyo tunakuwa na majengo machache yaliyo makubwa yanayozunguka taasisi zetu kwa ukaribu, ndivyo tutakavyopata masumbufu na fadhaa kwa udogo zaidi."— Counsels on Health, 269.

[5] – DAIMA ZIUNGANISHWE NA SHULE ZETU

"Bwana ameniagiza kuwaonya wale ambao katika siku zijazo wataanzisha vituo vya afya katika sehemu mpya, kwamba waanze kazi yao kwa unyenyekevu, wakiweka wakfu uwezo wao kwa utumishi Wake. Majengo yanayojengwa hayapaswi kuwa makubwa au ghali. Vituo vya afya vidogo katika sehemu mahalia, vinapaswa kuanzishwa kuhusiana na shule zetu za mafunzo. Katika vituo hivi vijana wa kiume na wa kike wenye uwezo na waliowekwa wakfu wanapaswa kukusanywa."— Counsels on Health, 220.

"Katika maeneo yetu ya vituo vya afya, watendakazi waliofunzwa wanapaswa kwenda mahali ambapo Ukweli haujawahi kutangazwa, na kufanya kazi ya umishenari kwa ajili ya Bwana-Mwenyewe, wakidai ahadi hiyo, Tazama, Niko pamoja nanyi hadi ukamilifu wa dahari. —Counsels on Health, 211.

"Nina maagizo yaliyo wazi kwamba, popote inapowezekana, shule zinapaswa kuanzishwa karibu na vituo vyetu vya afya, ili kila taasisi iwe msaada na nguvu kwa nyingine." —Counsels on Health, 301.

"Tahadhari zimetolewa kwangu kwa kurejelea kazi ya kuwafunza wauguzi na wainjilisti wamishenari wa tiba. Hatupaswi kuweka kazi hii katika sehemu moja. Katika kuanzisha kila kituo cha sanitarium, vijana wa kiume na wa kike wanapaswa kufunzwa kuwa wamishenari wa tiba. Bwana atafungua njia mbele yao wanapotoka kwenda kumfanyia kazi.—Counsels on Health, 225 (see Counsels on Health 227, 242, 243, 493, 542).

“Kila kituo cha afya kinapoanzishwa na Waadventista Wasabato kinapaswa kuendeshwa kwa kwa misingi na mistari ya elimu.” —Medical Ministry 175. (See also Counsels on Health 393, 395-396.)

[6] – AMBAPO ARDHI INAPATIKANA KWA MADHUMUNI YA KILIMO

“Ilikuwa ni mpango Wake Bwana, kwamba badala ya kujenga upya kile kituo kimoja kikubwa cha Sanitarium, watu wetu wanapaswa kupanda vituo vingine katika sehemu kadhaa. Vituo hivi vidogo vya Sanitarium vilipaswa kuanzishwa mahali ambapo ardhi kuna ardhi kwa madhumuni ya kilimo. Ni mpango wa Mungu kwamba kilimo kitaunganishwa na kazi ya kituo chetu cha tiba na shule zetu. Vijana wetu wanahitaji kupata elimu kutoka kwenye kazi hii. Ni vizuri, na zaidi ya hayo, ni muhimu kwamba jitihada zifanywe kutekeleza mpango wa Bwana katika jambo hili.”— Counsels on Health, 223.

“Bwana atafanya kazi juu ya akili za wanadamu katika sehemu zisizotarajiwa. Wengine ambao wanaonekana kuwa ni maadui wa Ukweli, katika majaliwa ya Mungu, watawekeza mali zao ili kuendeleza ardhi na kuweka miundo-mbinu kwa kusimamisha majengo. Baada ya muda, mali au miundo-mbinu hii itauzwa kwa bei iliyo chini sana ukilinganisha na gharama yake ya kujengea (for sale). Watu wetu watatambua mkono wa Mungu uliotoa majaliwa katika ofa za watu hawa na watanunua mali hizi zenye thamani kwa matumizi ya kazi za elimu-kuelimisha/shule. Watapanga na kusimamia kwa unyenyekevu, kujinyima, kujikana na kujitolea. Hivyo watu wenye uwezo, bila wao wenyewe kujua wanatoa msaada wa ziadi, na kuunga mkono kazi hii ya Mungu na jambo hili litawawezesha watu wa Bwana kuendeleza kazi Yake upesi.” ——Counsels on Health, 227.

“Katika maono ya usiku Bwana alinionyesha mali, ambayo ilikuwa ni majengo yasiyo na watu ndani yake, huko mashambani, mali hii ilifaa kwa madhumuni ya kituo cha Sanitarium, na iliuzwa kwa bei iliyo chini sana ukilinganisha na gharama ya ujenzi wake hapo awali (offer for sale).”— Counsels on Health, 231-232.

“Muda ulipita kabla hatujapata maeneo haya.” — Counsels on Health, 232. (Jinsi Walimu na Wanafunzi Wanavyopaswa Kufanya Kazi Pamoja Mashambani: Medical Ministry, 81, 77, 79)

3- UJENZI WA AWALI

[1] – ONYESHO NA MWONEKANO

“Kazi ya Mungu inapaswa kuendelezwa bila maonyesho ya nje.” — Counsels on Health, 300.

"Kwa hali yoyote ile, pesa zisiwekezwe kwa maonyesho ya ufahari-kujionyesha. Kazi ya umishenari wa injili inapaswa kuendelezwa kwa usahili na unyenyekevu, kama ilivyokuwa kazi ya Mkuu wa Mbinguni, ambaye kwa kuona mahitaji ya ulimwengu uliopotea, mwenye dhambi, aliweka kando vazi Lake la kifalme na taji yake ya kifalme na kuvika Uungu Wake na ubinadamu, ili aweze kusimama mbele ya mwanadamu/ubinadamu. Ndivyo Yeye alivyoendesha kazi Yake ya umishenari ili kuacha mfano kamili kwa wanadamu kufuata. Mathayo 16:24 Wakati huo Yesu aliwaambia wanafunzi Wake, Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate. Kila mmishenari wa kweli wa tiba atatii maneno haya. Hatanyumbulisha kila mshipa wa fahamu ili kufuata desturi za kidunia na kufanya maonyesho mbele za watu, bali atawaza juu kuongoa roho kwa ajili ya Mwokozi. HAPANA, HAPANA. Ikiwa Mkuu wa Mbinguni angeweza kuondoka katika nyumba Yake tukufu ili kuja kwenye ulimwengu uliokaangwa na kuharibiwa na laana, ili kuanzisha mbinu sahihi za kufanya kazi ya umishenari wa tiba, sisi ambao ni wafuasi Wake tunapaswa kufanya vivyo hivyo kwa kujikana nafsi na kujitoa. —Counsels on Health, 319.

Kwa wale wanaojishughulisha na kazi ya umishenari wa tiba, jaribu la kujiinua litakuja, kujionyesha wazi kwa ajili ya vile watu watakavyoshangazwa au kuona. Kata kila kitu cha tabia hii kutoka kwenye kazi yako. Hebu mzigo wote wa roho za, uwe wa kile ambacho Kristo alikuwa akifanya katika kazi Yake. Tunapaswa kusimama juu ya jukwaa la Ukweli wa milele—Ukweli safi, usioghoshiwa. Katika hili tunaweza kuchukuliwa kuwa wa pekee, lakini hili ndiyo fungu la wote wanaomfanya Kristo kuwa sehemu yao. Kila mtendakazi katika safu za umishenari wa tiba anapaswa kufanya kazi hiyo kuwa ya mafanikio kwa kuishi akiwa ameunganishwa na mtendakazi Mkuu. —Medical Ministry, 161.

“Wale ambao mapenzi yao yamewekwa kwa Mungu watafanikiwa. Watakuwa vipofu kwa ubinafsi kwa ajili ya Kristo, na vivutio vya kidunia havitakuwa na uwezo wa kuwavuta kutoka kwenye utii wao kwa Bwana. Watatambua kwamba maonyesho ya nje tu, wala hayampi mtu nguvu. Sio kujigamba, au onyesho la nje, ndio ambavyo hutoa uwakilishi sahihi wa kazi ambao sisi, kama watu waliochaguliwa na Mungu, tunapaswa kufanya. Wale ambao wameunganishwa na kazi yetu ya sanitarium, wanapaswa kupambwa kwa neema ya Kristo. Hii itawapa ushawishi mkubwa zaidi kwa wema.

“Bwana Yuko dhati, makini na mwenye ari kwangu. Ahadi Zake zimetolewa kwa sharti kwamba tufanye mapenzi Yake kwa uaminifu; Kwa hiyo, katika ujenzi wa vituo vya Sanitarium Bwana anapaswa kufanywa kuwa wa kwanza na wa mwisho na bora katika kila kitu.

“Hebu wote waliounganishwa na utumishi wa Mungu walindwe, ili wasije wakawa na tamaa ya kujionyesha na kuwaongoza wengine katika Kujifurahisha nafsi na kujitukuza wenyewe. Mungu hataki yeyote watumishi Wake waingie katika shughuli zilizo na gharama isiyo ya lazima, na kutumia fedha nyingi ambazo huwaletea watu mizigo mizito ya deni.”—Counsels on Health, 274-275.

"Kamwe mwonekano haupaswi kutegemewa kama njia ya mafanikio. Huu ni udanganyifu. Tamaa ya kuwapa watu mwonekano ambao haufai kwa kila njia katika kazi ambayo Mungu ametupa tuifanye, mwonekano ambao ungeweza kudumishwa tu kwa kutumia kiasi kikubwa cha pesa, ni jeuri asiye na huruma. Ni kama donda-ndugu ambalo huwa linakula sehemu muhimu za mwili. —Counsels on Health, 277.

“Wazo la kwamba maonyesho ya nje humletea mtu ushawishi kwa mtu au cheo chake ni mojawapo ya uongo wa Shetani.” —Medical Ministry, 160

[2] - UKUBWA

“Katika kuanzisha taasisi, hatupaswi kamwe kushindana na taasisi za ulimwengu kwa ukubwa au fahari.”—Counsels on Health, 300.

“Tunaamini kwamba Bwana atakuja hivi karibuni, na Je, imani yetu haipaswi kuwakilishwa katika majengo tunayojenga? Je, tutaingia katika gharama kubwa, na kuwa na matumizi makubwa ya pesa kwenye jengo ambalo hivi karibuni litateketea katika moto huo mkubwa? —Counsels on Health, 276.

“Basi tufunge kwa kamba matamanio yetu kabambe ya ukuu; Hebu na tujilinde dhidi ya ubadhirifu au kuwa wana uchumi wabaya kwa kupuuzia siku za mbeleni.”— Counsels on Health, 276.

"Pesa nyingi zaidi kuliko ilivyohitajika zimetumika katika taasisi zetu za zamani. Wale ambao wamefanya hivi wamedhani kwamba matumizi haya ya fedha yaliyopitiliza, yangetoa tabia kwa kazi. Lakini wazo kama hili sio kisingizio cha matumizi yasiyo ya lazima.”— Counsels on Health, 276.

“Tabia hudhihirika katika kazi, si kwa kuwekeza fedha katika majengo makubwa, bali kwa kudumisha kiwango cha Kweli cha kanuni za kidini, pamoja na tabia zetu kufanana na tabia bora ya Kristo.”—Counsels on Health, 276.

"Sanitarium zilizoanzishwa kwa ajili siku zijazo hazipaswi kuwa majengo makubwa na yenye gharama kubwa. Saniarium mahalia, zinapaswa kuanzishwa kwa kuunganishwa na shule zetu.” —Medical Ministry, 156.

“Ni zile nafsi zenye kiu tu, ndiyo zinaweza kuongozwa kwenye maji ya uzima ambayo tunasihi kwa ajili ya sanitarium—Na sio Sanitarium ghali, zenye majumba makubwa ya kifahari, bali taasisi zinazofanana na nyumba au makazi ya watu katika maeneo ya kupendeza.”— Counsels on Health, 211.

"Kituo cha afya cha Battle Creek ni kikubwa mno. Watendakazi wengi sana watahitajika kuwahudumia wagonjwa wanaokuja. Sehemu ya kumi ya idadi ya wagonjwa wanaokuja sasa hivi katika taasisi hiyo ndiyo idadi inayofaa kuhudumiwa ili kupata matokeo bora zaidi katika kituo kimoja cha wamishenari wa tiba (idadi iwe ndogo).”— Counsels on Health, 214.

“Kunyonya kiasi kikubwa cha fedha katika sehemu chache tu, ni kinyume na kanuni za Kikristo. Kila jengo linapaswa kujengwa kwa kurejelea uhitaji wa majengo yanayofanana na hayo katika maeneo mengine.”— Counsels on Health, 217.

Sio mapenzi ya Bwana kwa watu Wake kusimamisha kituo kikubwa cha Sanitarium popote pale. Sanitarium nyingi zinapaswa kuanzishwa. Hazipaswi kuwa vikubwa, lakini ziwe zimekamilika vya kutosha kufanya kazi nzuri na yenye mafanikio.”— Counsels on Health, 225.

“Nimeonyeshwa tena na tena kuwa sio jambo la busara kusimamisha taasisi kubwa. Sio kwa ukubwa wa taasisi kwamba kazi kubwa zaidi ya roho inaweza kutimizwa. Mzinga wa kituo cha afya unahitaji wafanyakazi wengi. Na mahali ambapo wengi huletwa pamoja na hivyo kujikusanya, ni vigumu sana kudumisha kiwango cha juu cha kiroho.” ——Counsels on Health, 239.

"Ukweli kwamba wagonjwa wengi wanakuja kwenye kituo cha sanitarium kipya huko haupaswi kusomwa kama ishara kwamba ile mipango ya kazi mikubwa huko, ilikuwa bora zaidi. Katika taasisi kubwa kama hii, watakuja wanaume na wanawake wengi ambao sio wagonjwa kabisa. Wafanyakazi watahitajika kuwasubiri na kuwatumika; Wauguzi wetu watakuwa watumishi wa wanaume na wanawake wa kidunia ambao hawana mwelekeo wa uchamungu au dini. Lakini hii sio kazi ambayo Mungu amewapa wamishenari Wake wa tiba.” — Medical Ministry, 159.

[3] - IDADI YA WAGONJWA

“Wagonjwa wanapaswa kufikiwa, sio kwa majengo makubwa, bali kwa kuanzishwa vituo vingi vidogo vya Sanitarium, ambavyo vinapaswa kuwa kama taa zinazoangaza mahali penye giza.”— Counsels on Health, 211.

“Kristo aliukumbatia ulimwengu katika kazi Yake ya umishenari, na Bwana amenionyesha kwa njia ya mafunuo kwamba si mpango Wake wa vituo vikubwa kusimikwa, taasisi kubwa kuanzishwa, na fedha za watu wetu katika sehemu zote za dunia kutindikiwa kwa kusaidia kuzibeba taasisi chache tu kubwa, wakati mahitaji ya nyakati, yanataka jambo fulani lifanyike wakati majaliwa yanafungua njia, katika sehemu nyingi. Vituo vinapaswa kuanzishwa katika maeneo mbalimbali duniani kote. Kwanza kianze kituo kimoja sehemu fulani, na kisha sehemu nyingine ya shamba la mizabibu la Bwana iingizwe kwenye mkakati, hadi mashamba yote yamelimwa. Juhudi zinapaswa kufanywa popote pale ambapo hitaji ni kubwa zaidi. Lakini hatuwezi kuendeleza vita hivyo vikali, na wakati huohuo kuwa na ubaradhifu wa matumizi ya pesa na kuwa na roho ya kujionyesha kupita kiasi katika sehemu chache.”— Counsels on Health, 214.

“Vituo vinapaswa kusimikwa katika miji yote ambayo haijaifahamu kazi kubwa ambayo Bwana angeifanya ili kuuonya ulimwengu kwamba mwisho wa mambo yote umekaribia.‘ Kuna vituo vingi sana,’ akasema Mwalimu Mkuu, ‘mahali pamoja.’ ” — Counsels on Health, 214.

“Vivunje vituo vikubwa, ndilo limekuwa Neno la Bwana. ‘Peleka nuru sehemu nyingi.’ Wale wanaotamani kupata mafunzo ya kazi ya umishenari yenye ufanisi wanapaswa kuelewa kwamba vituo vikubwa vya sanitarium vitaendeshwa kwa kufanana kwa karibu na taasisi za ulimwengu kiasi kwamba wanafunzi wanaofanya kazi katika sanitarium hizo vya afya hawawezi kupata mafunzo yenye ulinganifu kwa ajili ya kazi ya umishenari ya Kikristo.” —Medical Ministry, 158-159

“Wengine watavutiwa na hatua moja ya Injili, na wengine na kwa hatua nyingine. Tumeagizwa na Bwana wetu kufanya kazi kwa njia ambayo makundi/madaraja yote yatafikiwa. Ujumbe lazima uende kwenye ulimwengu wote. Sanitarium zetu zinapaswa kusaidia kupata idadi ya watu wa Mungu. Hatupaswi kuanzisha taasisi chache kubwa-kubwa; Kwani hivyo isingewezekana kuwapa wagonjwa jumbe ambazo zitaleta afya kwa nafsi. Sanitarium ndogo vidogo zinapaswa kuanzishwa katika sehemu nyingi.”— Medical Ministry, 327.

"Kamwe, kamwe usijenge taasisi kubwa (kama tembo-mammoth institutions). Hebu taasisi hizi na ziwe ndogo, na ziwe nyingi zaidi, ili kazi ya kuleta roho kwa Kristo itimie.” —Medical Ministry, 323. 159.

“Kutangazwa kwa Ukweli katika sehemu zote za ulimwengu kunahitaji sanitarium ndogo katika sehemu nyingi.”— Medical Ministry, 159.

[4] - GHARAMA ZA UJENZI

“Wakati kazi ya ujenzi inasonga mbele, hebu watu wakumbuke kwamba, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu na Musa, Mungu alipanga mchoro wa kila sehemu ya safina na Patakatifu (Kutoka 25:8); Ndivyo ilivyo katika ujenzi wa taasisi Zake leo, Yeye mwenyewe anaangalia kazi iliyofanywa. Wakumbuke kwamba mjenzi Mkuu, kwa Neno Lake, kwa Roho Yake, na kwa uangalizi Wake, anapanga kuelekeza Mwenyewe kazi Yake. Wanapaswa kuchukua muda kumwomba ushauri.” —Counsels on Health, 278-279.

"Majengo ya matofali na mawe sio mazuri sana katika kujengea sanitarium, kwa kuwa kwa ujumla huleta ubaridi na unyevu. Inaweza kusemwa kuwa jengo la matofali linaonyesha mwonekano wa kuvutia zaidi, na kwamba jengo hilo linapaswa kuvutia. Lakini tunahitaji majengo yenye vyumba vikubwa; Na ikiwa matofali ni ya gharama kubwa sana, lazima tujenge kwa mbao.Hekima ya kiuchumi, ni lazima liwe somo letu. Hili ni jambo la lazima, kwa sababu ya ukuu wa kazi ambayo lazima ifanywe katika maeneo mengi katika shamba la maadili la Mungu.

"Imependekezwa kuwa wagonjwa hawatajisikia kuwa salama kutokana na moto katika muundo wa mbao. Lakini ikiwa tuko mashambani (pembeni), na sio katika miji ambayo majengo yamejaa pamoja, moto unaweza kulipuka kutoka ndani, ila chanzo chake hakiweza kutoka nje, kwenye majengo mengi; Kwa hivyo matofali hayangekuwa ulinzi. Inapaswa kuwasilishwa kwa wagonjwa kwamba kwa ajili ya afya jengo la mbao ni bora kuliko lile la matofali.”— Counsels on Health, 279.

"Wale wanaoongoza katika uanzishwaji wa taasisi za tiba lazima wawe mfano sahihi. Hata kama pesa ipo, hawapaswi kutumia zaidi ya vile inavyohitajika kabisa. Kazi ya Bwana inapaswa kufanywa kwa kurejelea mahitaji ya kila sehemu ya shamba Lake la mizabibu.”— Counsels on Health, 275.

[5] - SAMANI/FANICHA NA MAKAZI-MALAZI

"Katika kazi zetu zote za mapema lazima tuzingatie umuhimu wa uchumi. Lazima kusiwe na gharama zisizo na sababu. Bwana anakuja hivi karibuni, na gharama zetu katika majengo zinapaswa kupatana na imani yetu. Fedha zetu zinapaswa kutumiwa katika kuandaa vyumba vinavyoleta uchangamfu- furaha, mazingira yenye afya, na chakula chenye afya, kisichokobolewa au kusindikwa.” —Counsels on Health, 277.

"Wanaume wenye busara wanathamini faraja, na mahali pasipo na usumbufu zaidi ya uzuri na maonyesho ya nje. Ni makosa kudhani kwamba kwa kuweka mwonekano wa furaha, tutapata wagonjwa wengi zaidi, na kwa hivyo fedha nyingi zaidi zitapatikana. Lakini hata kama njia hii ingeleta wafadhili wengi, hatuwezi kukubali kwamba vituo vyetu vya afya vipambwe na samani kwa mawazo ya anasa ya kipindi hiki. Ushawishi wa Kikristo ni wa thamani sana kutolewa dhabihu kwa njia hii. Mazingira yote, ndani na nje ya taasisi zetu, lazima yapatane na mafundisho ya Kristo na usemi wa imani yetu. Kazi yetu katika idara zake zote inapaswa kuwa kielelezo, si cha maonyesho na ubadhirifu au ufujaji wa pesa, bali ya maamuzi yaliyotakaswa."— Counsels on Health, 277.

"Sio majengo makubwa ya gharama kubwa, sio samani za kitajiri, sio meza zilizosheheni mapochopocho ya kupendeza,ndiyo ambazo zitatupa ushawishi na mafanikio ya kazi yetu. Ni imani inayofanya kazi kwa upendo na kuitakasa nafsi; Ni mazingira ya neema ambayo inamzunguka muumini. Ni Roho Mtakatifu anayefanya kazi juu ya akili na moyo humfanya mwanadamu kuwa na harufu ya uzima na kumwezesha Mungu kubariki kazi yake."— Counsels on Health, 278.

"Vyumba vilivyo na samani za bei nafuu kuliko unavyotamani vitaendana na kazi ambayo Mungu ametupa tuifanye katika siku hizi za mwisho. Mawazo yako hayajafinyangwa na kutengenezwa na wazo la kweli la vitendo la maana ya kutembea kwa unyenyekevu na Mungu. Wewe unatazama mwonekano kama njia kuu ya kukuinua wewe hadi kwenye mafanikio. Huu ni udanganyifu. Unatafuta kufanya mwonekano ambao haufai kwa njia yoyote katika kazi ambayo Mungu amekupa uifanye, mwonekano ambao ungehitaji kiasi kikubwa cha pesa ili kuviendeleza kuwa kama vilivyo bila kuharibika au kuchakaa. Hatuwezi kukubali kuwa na vyumba vya sanitarium vilivyopambwa kwa samani ambazo ni mfano wa ibada ya sanamu ya kipindi hiki (zama), hata kama hii italeta wafadhili wengi. Ushawishi wa Kikristo una thamani zaidi kuliko hili." —Medical Ministry, 167.

"Wanapaswa kuhesabu gharama ya kila hatua inayochukuliwa. Hawapaswi kuanza kazi bila kujua ni kiasi gani cha pesa wanachopaswa kuwekeza." —Medical Ministry, 153.

"Ikiwa wangetegemea msaada wa Mungu, wakiweka tumaini lao Kwake Yeye tu, na kujionyesha kuwa tayari kuanza kwa udogo, na kuruhusu sifa ya kazi yao ijizungumzie yenyewe, kama wangekuwa na nia iliyotakaswa, na kama wangefanya azimio lao kuwa na ushawishi wa kuokoa katika ulimwengu, wangebarikiwa katika kazi zao, na vituo vingi zaidi vya afya vingeanzishwa kuwa wawakilishi wa Ukweli." —Medical Ministry, 156.

"Anza kwa mianzo midogo na upanue kazi kadri hali inavyoweza kuhitaji. Hesabu gharama ya kila kinachofanywa, ili uweze kuwa na uhakika wa kumaliza. Chukua kidogo kwa kadri iwezekanavyo kutoka kwenye hazina. Watu wenye imani na uwezo wa kifedha wanahitajika ili kujipanga kiuchumi. Vituo vyetu vya sanitarium lazima visimamishwe kwa matumizi ya fedha yaliyo na mipaka. Majengo ambayo mara nyingi hutumika katika kuanzia kazi yanaweza kupatikana kwa gharama nafuu."— Counsels on Health, 468.

"Kabla ya kuweka mikakati na mbinu zinazohitaji matumizi makubwa ya fedha, tunapaswa kuzingatia ikiwa mipango hii inadhinishwa na Bwana."— Counsels on Health, 518.

[6] - VIFAA

"Kwa wasimamizi wa vituo vyetu vya afya wote, ningesema, usiruhusu deni kubwa liundwe. Usifanye hatua yoyote isiyo ya lazima. Weka kando tamaa yako ya kujipatia vifaa au nyenzo kwa mara moja. Hebu matumizi bora zaidi yafanywe kwa vifaa vichache, badala ya kuongeza deni. Yote ambayo yanahitajika yanaweza kupatikana kwa wakati, lakini vyombo vyote, samani na vifaa havihitaji kununuliwa kwa mara moja. Hebu kucheua mambo, mawazo tulivu, na hesabu za busara iwe kanuni ya utekelezaji. Ikiwa mafanikio yatazifikia taasisi zetu zilizoanzishwa kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa, itakuwa ni kwa sababu wasimamizi wamependelea kupatana na mambo muhimu zaidi, badala ya kulimbikizia madeni." —Medical Ministry, 166.

"Daktari hapaswi kujifunza jinsi ya kukidhi matakwa ya ulimwengu. Hapaswi kuiga ulimwengu katika mwonekano au vifaa, akijikomba mwenyewe kuwa hii ndiyo njia ya kukutana na tabaka za juu. Injili inakataza kuthamini mawazo ya kidunia."— Medical Ministry, 160.

"Anza kufanya kazi ya umishenari wa tiba kwa mambo yaliyokuwa kwenye uwezo wake, yale yasiyoleta usumbufu wowote."—A Call to Medical Evangelism and Health Education, 26 (speaking especially of personal work).

4- GHARAMA ZA UENDESHAJI

[1] - UCHUMI

"Watu walio katika nafasi zenye nyadhifa za kutumainiwa wanapaswa kuzingatia fedha wanazoshughulikia kama mapato ya Mungu, na kuzitumia kwa njia ya kiuchumi. Wakati kuna vingi katika hazina, hawapaswi kuwekeza katika kuongeza jengo juu ya jengo kwenye ujenzi katika sehemu ambazo tayari zimepewa

kumbukizi za Mungu. Mamia ya maeneo mengine yanahitaji pesa hizo, ili wao pia wawe na kitu fulani kilichosimikwa ili kuwakilisha ile Kweli.” —Medical Ministry, 165.

"Sanitarium nyingi zinapaswa kuanzishwa. Hazipaswi kuwa kubwa, lakini ziwe zimekamilika vya kutosha kufanya kazi nzuri na yenye mafanikio.”— Counsels on Health, 225.

“Mtu ambaye ndiye mhasibu, anayesimamia malipo ya fedha anapaswa kujifunza ni kiasi gani anaweza kutunza fedha, badala ya kiasi gani anaweza kutumia. Gharama zote zisizohitajika zinapaswa kupunguzwa. Hebu wasaidizi waelewe kwamba matumizi hayapaswi kuzidi uzalishaji. Kupoteza katika kituo sanitarium ni jambo kubwa. Kuna watu wengi ambao wanahusika katika mistari tofauti ya kazi, na ni muhimu zaidi kuelewa hitaji la uchumi. Uchumi ni sayansi yenye thamani sana. Wengi hupoteza pesa nyingi kwa kushindwa kuokoa matumizi ya mambo au vitu vidogo-vidogo visivyokuwa na maana.” —Medical Ministry, 176.

"Kiongozi wangu aliyekuwa akiniongoza aliponichukua katika idara tofauti, ukosefu wa hekima ya uchumi ulikuwa kila mahali na uligusa moyo wangu kwa huzuni, kwa kuwa nilifahamu kwa uhakika juu ya deni lililokuwa juu ya taasisi hiyo. Ukosefu wa uaminifu wa kijinga na wa mambo madogomadogo, kupuuza wajibu kwa ubinafsi, viliandikwa na malaika aliyekuwa anarekodi. Ubaradhifu ulioruhusiwa hapa na pale katika kipindi cha mwaka ni kiasi kikubwa.

Ubaradhifu wa fedha hizi nyingi hapa na pale ungeweza kuokolewa na wasaidizi; Lakini kila mmoja alisema, ‘Si mali yangu kuichunga au mambo hayo hayanihusu.’ Je, wangepita bila kujali hivi ikiwa hasara hiyo wangeibeba wao binafsi? Hapana, wangejua nini cha kufanya hasa na jinsi ya kufanya; Lakini inaleta tofauti kubwa, kwamba sasa mali hiyo ni ya taasisi. Hili ni tunda la ubinafsi na limeandikishwa dhidi yao kwa jina la ukosefu wa uaminifu.”— Counsels on Health, 420.

"Kuitwa kwako daktari kwa hali yoyote hakukuondolei wajibu wako wa kufanya mazoezi ya kuwa mwanauchumi mwenye busara. Kuna sehemu mpya za kuingia na injili, na ili kuingia katika maeneo haya ambayo hayafikiwa kunahitajika uchumi wa karibu zaidi. Je, utaingia katika mashamba haya ya kazi ya Bwana kama ulivyoingia , ukiwa umeridhika kuwaachia watu wengine tu kutekeleza roho ya kujikana nafsi na kujinyima na kuinua msalaba huku wewe ukiendekeza matamanio yako, ukitumia pesa nyingi kwa lakshari/luxury kwa kujionyesha tu?” —Medical Ministry, 130.

"Chunga pesa ndogo zinazotumiwa vibaya. Usiruhusu hata uvujaji mdogo. Ni hasara ndogo-ndogo ndizo ambazo huzungumza mwishoni. Kusanya vipande vya masazo; Usiruhusu chochote kipotee. Usipoteze dakika katika kuzungumza; dakika zilizopotea huharibu masaa. Bidii ya uaminifu ya kudumu, ikifanya kazi katika imani, daima itavikwa taji la mafanikio."— Counsels on Health, 304-305

"Wengine wanafikiri ni chini ya wadhifa wao, kutunza vitu vidogo-vidogo. Wanafikiri ni ushahidi wa akili finyu na roho ya ubahili. Lakini uvujaji mdogo-mdogo tu, kwenye mashimo mengi, umezamisha meli nyingi. Hakuna kitu ambacho kingetimiza kusudi la yeyote kinachopaswa kuruhusiwa kupotea. Ukosefu wa elimu ya uchumi hakika utaleta deni kwa taasisi zetu. Ingawa pesa nyingi zinaweza kupokelewa, zitapotea katika upotevu mdogo-mdogo wa kila tawi la kazi. Uchumi si ubahili." —Counsels on Health, 305.

"Wengine wanaonekana kutokuwa na wazo la sayansi ya kushughulikia pesa. Wanaruhusu mamia ya dola kupita mikononi mwao bila kuzalisha au kutoa chochote kwa Mungu." — Medical Ministry, 130.

"Mungu anakuita ili unyooke, na kunyosha mambo. Kuwa mwanaume-uwe hodari. Weka mbali ubadhirifu wako. Mawazo yanayopitiliza katika utumiaji wa pesa lazima yasiingizwe chini ya jina la kazi ya umishenari wa tiba. Ni wakati muafaka kwamba tuwe Wakristo moyoni. Uadilifu, kujinyima, na unyenyekevu vinapaswa kuwa sifa ya maisha yetu." —Medical Ministry, 131.

"Wote ambao wameunganishwa na taasisi zetu wanapaswa kuwa na uangalizi wenye wivu kwamba hakuna kitu kinachopotea, hata kama jambo hilo haliingii chini ya sehemu ya kazi waliyopewa. Kila mtu anaweza kufanya kitu kuhusu uchumi. Wote wanapaswa kufanya kazi yao, sio kwa ajili ya kupata sifa kwa wanadamu, bali kwa namna ambayo inaweza kupita mtihani wa uchunguzi wa Mungu." —Counsels on Health, 281.

[2] – MATUMIZI

"Uwezo wa kutumia na kutoa pesa za Bwana haupaswi kuachwa katika maamuzi ya mtu yeyote. hesabu lazima itolewe kwa kila dola inayotumiwa."—Medical Ministry 165. (Compare with Medical Ministry under Equipment.)

"Ili kusonga mbele kwenye kazi zetu zote, lazima tuzingatie umuhimu wa uchumi. Lazima kusiwe na matumizi yasiyohitajika."— Counsels on Health, 277.

"Kunapaswa kuwe na saa maalumu katika kufanya kazi, saa zilizobainisha kwa ajili ya kula, bila kuanza kushughulikia kwa kinagaubaga tena gharama halisi ya

kila bidhaa ya chakula na kupata aina ya bidhaa za bei nafuu zaidi. Nunua vyakula hivyo ambavyo ndiyo bora zaidi katika kutengeneza nishati ili kuendesha utendaji hai wa mwili. Hakuna ubadhirifu unaponunua vyakula ambavyo mwili unaweza kuvichukua na kumeng'enya vizuri zaidi, na kuvipeleka katika kila sehemu ya seli hai ya mwili wetu ili sehemu zote za mwili zipate lishe." —Medical Ministry, 79- 80.

"Uzuiaji wa kutofaulu una thamani kubwa zaidi kuliko inavyoweza kukadiriwa. Hebu vijana ambao wamepewa jukumu la kufanya kazi fulani wasiwe na kusita, wasiwasi,kukosa utulivu, na kukosa ujasiri. Hebu wajifunze hekima kutokana na kushindwa kwa wengine." —Medical Ministry, 153.

"Wale ambao wanasimamia vituo vyetu vya sanitarium, wanapaswa kusonga kwa tahadhari/uangalifu zaidi. Kuna wakati wataona ongezeko kidogo. Hebu watende kwa hekima na busara na kujua kuendana na hali na kurekebisha mambo. Hebu wajifunze na kutekeleza maagizo ambayo Kristo alitoa kuhusu kujenga mnara. Mawazo yanayocheuliwa vyema kuhusu siku za mbeleni kabla mambo hayajatokea, yana thamani kubwa zaidi kuliko mawazo ya baadaye baada ya mambo kutokea." —Medical Ministry, 157

"Wengine wanapuuza kufanya matendo ya rehema kwa ajili ya wahitaji, na kutumia pesa kidogo ya posho iliyotunzwa kwa njia hii. Wengi hutenda tendo moja baada ya tendo jingine la kumuibia Mungu kwa njia ngumu, katika nafsi ya watakatifu Wake."—Medical Ministry, 158.

[3] - DENI

"Mungu hataki kazi Yake iendelee kuaibishwa na deni. Panapoonekana hitaji la kuongeza miundo-mbinu au vifaa vingine vya taasisi, jihadhari na kusonga mbele kupita uwezo wako. Afadhali kuahirisha maboresho hayo hadi Mungu atakapofungua njia ya kufanywa bila kujiingiza katika madeni makubwa na kulazimika kulipa riba. —Counsels on Health, 304.

"Wanadamu ambao wangefanya vyema kama wangejiweka wakfu kwa Mungu, kama wangekuwa tayari kufanya kazi kwa unyenyekevu, wakikuza biashara zao polepole, na kukataa kuingia kwenye madeni, wameshindwa kwa sababu hawajafanya kazi katika mistari inayofaa. Baada ya kupata shida, wamejiuza, kama watu wasio na uwezo wa kusimamia. Wanatamani ahueni kutokana na shinikizo la kifedha, na hawakuacha kufikiria matokeo ya baada ya hapo.

"Wale wanaowasaidia watu kama hao kutoka kwenye shida, wanashawishika kuwafunga kwa kamba zenye nguvu katika umbo la ahadi ambazo huwa wanahisi

kwamba wao ni watumwa ambao wamefungwa. Mara chache sana watu kama hao huachana na sifa mbaya za usimamizi mbovu na kushindwa.

"Kwa wale ambao wanahusika katika deni, ninaagizwa kusema: Usikate tamaa ikiwa unasonga katika mistari sahihi. Fanya kazi kwa uwezo wako wote ili kuleta afueni katika hali hiyo mwenyewe. Usiitupe taasisi ambayo tayari imekwishajipatia aibu kwenye chama kingine ambacho tayari kimelemewa na madeni. Ni bora kwa kila sanitarium kusimama kwa kuwajibika kuhusiana na mzigo wake yenyewe." ——Medical Ministry, 157

Mahudhurio makubwa ya wagonjwa, yasiwe ni jambo la kushangilia kama ndiyo kuwekwa huru kutoka kwa madeni. — Shuhuda kwa Kanisa 6: 211.

Epukeni kuingia katika madeni kama vile ambavyo mngeweza kuepuka ugonjwa.— Shuhuda kwa Kanisa 6: 211.

Tunapaswa kuepuka deni kama vile tunavyopaswa kuepuka ukoma. — Shuhuda kwa Kanisa 6: 217.

Hebu watu wajilinde wenyewe kama vile kwa uzio wa waya ulio na miiba dhidi ya mwelekeo wa kuingia kwenye deni. — Shuhuda kwa Kanisa 7: 235-236.

“Mazoea ya kuchukua pesa kutoka kwenye hazina kabla ya kujipatia hizo pesa ni mtego.” ——Colporteur Ministry, 93-94.

“Mtu anapojihusisha kwa hiari na deni, anajiingiza katika moja ya nyavu za Shetani anazoweka kwa ajili ya roho za watu.” —Counsels on Stewarship, 94.

Epuka doa na kivuli cheusi cha deni kwenye taasisi kwa kukataa kujenga majengo makubwa na ya gharama kubwa. (3 Testimonies, 175; 7 Testimonies, 206-209, 235-236; Counsels on Health, 263, 304-305: 9 Testimonies, 71. Haiko katika mpango wa injili: 6 Testimonies, 206-207, 211; 9 Testimonies, 71. Taasisi ziko hatarini kwa sababu ya madeni: 6 Testimonies, 469. 6 Testimonies 216-inaeleza namna ya kuepuka. Inasababishwa na ukosefu wa uchumi na kwa kufanya kazi kwa njia mbaya (6 Testimonies, 216; 7 Testimonies, 207, 284). Taasisi ya Afya (3 Testimonies, 175; Counsels on Health, 262), Nyumba za uchapishaji (Counsels on Health, 304-305; 7 Testimonies, 235- 236), Jumuiya ya watu (Counsels on Health, 66) ni mifano ya matatizo makubwa yanayopatikana kwa sababu ya madeni. Ikiwa deni litakuja, ni wajibu wetu kuliondoa (6 Testimonies, 207), Kwa kuwa amri ya nane inatuhitaji tulipe (Patriarchs and Prophets, 309). Tunapaswa kulipa madeni tuliyatengeneza.

Mbinu za kuondoa deni ni pamoja na: [1] Fanya kazi zote zinazoweza kufanywa; [2] Jizoeze kujikana nafsi inapobidi; [3] Mweke Bwana kwanza, na kila juma weka kando kitu/pesa kwa ajili ya hili katika sanduku la kujinyima au kujikana nafsi (6 Testimonies, 103); [4] Tumia Mpango wa Kitabu cha kuleta ahueni: uza Vitabu vya Roho ya Unabii na Wainjilisti wa vitabu, na mapato ya hivi vitabu viwili yaende kwa kusudi hili (Christ's Object Lesson, kwa ajili ya kusaidia Shule; Huduma ya Uponyaji, kwa ajili ya kusaidia Taasisi za tiba; 6 Testimonies, 468-471; 9 Shuhuda, 70-71); [5] Zawadi na matoleo kutoka kwa marafiki (Shuhuda 6, 103-04). [6] Unapokiri dhambi inapofanywa, basi Bwana atasamehe na fedha itakuja kufuta madeni (8 Testimonies, 89).

Ushauri wa Taasisi ya Afya: [1] Kujitoa dhabihu kwa binafsi kwa upande wa wafanyakazi wote [2] Toa fedha mwenyewe ili kuweka mfano kwa wengine; [3] Hamasisha hekika katika kutumia fedha (uchumi) na tasnia; [4] Ombea baraka za Mungu juu ya taasisi, ili watu waguswe moyo kwa ujasiri wa kutoa pesa (Counsels on Health, 263); [5] Fanya Kazi kwa dhati na bidii; [6] Hamasisha wote wafanye kazi kwa bidii kwa malipo madogo hadi taasisi itakaposimikwa; [7] Sikiliza ushuhuda ulio wazi dhidi ya ubinafsi; [8] Kushauri na kukemea makosa. Hatua hizi zikichukuliwa, watakuwa na imani katika taasisi na fedha zitapokelewa/zitakuja. Wafanyakazi lazima waweke mambo sawa na Mungu; Wote lazima wawe wanyenyekevu, na wote lazima watii amri za Mungu (Counsels on Health 292-293). Mipango mingine ya kuondoa deni (Shuhuda 9 75; Fundamentals of Christian Education, 520, 532; shuhuda 6, 473, 478; 9 shuhuda 71, 79, 80, 88).

[4] - KUMILIKI, AU KUKODISHA?

(Kumiliki mali kwa ajili ya Kituo cha mashambani, kunapendekezwa. Tazama nukuu chini ya “Mahali.”) “Kuna sababu kwa nini tusijenge kituo katika miji. Katika miji hiyo, hukumu za Mungu zinakaribia kuanguka.”— Country Living, 8.

"Vituo hivi vitatumika kupata wateja wa sanitarium zilizo mashambani na ingekuwa vyema kama vingeendeshwa kwenye majengo ya kukodi. Hatupaswi kusimamisha katika miji majengo makubwa ya kuwatunza wagonjwa, kwa sababu Mungu ameonyesha wazi kwamba wagonjwa wanaweza kutunzwa vizuri zaidi nje ya miji.” —Counsels on Health, 488. (Hii inazungumza juu ya vyumba vya tiba vikihusianishwa na migahawa).

Je, tunapaswa kukodisha majengo? Kwa ufahamu wa mkusanyaji habari, hakuna taarifa ya moja kwa moja inayotolewa juu ya hili. Maeneo ya jiji la kibiashara, yaliyopangwa ipasavyo yanapatikana mara nyingi kwa misingi ya

kukodisha tu, hasa katika jumuiya kubwa zaidi. Mikataba kama hiyo ya ukodishaji mara kwa mara hujumuisha malipo ya awali ya kodi ya mwezi wa kwanza wa kukodi jumba hilo na mwezi wa mwisho, na kunyang'anywa pesa ya hiyo ya mwisho kama penalti au adhabu, ikiwa mkataba wa ukodishaji umevunjwa [umekatishwa mapema]. Lakini mara nyingi mikataba kama hii ya ukodishaji inahusisha mkataba uliovishwa chuma (iron-clad contract), ambao ni mkataba mkali na mkodishaji analazimika kufanya malipo ya kila mwezi kama inavyotakiwa, kwa muda wa kuanzia mwaka mmoja hadi mitano angalau. Je, tuko salama kweli katika kutia sahihi mkataba wa namna hiyo, tukijikamua kulipa kiasi kikubwa cha pesa, jambo ambalo litatufunga kuhudumu katika eneo fulani kwa idadi ya miaka fulani—katika miji ambayo itaharibiwa hivi karibuni? Nukuu zifuatazo ziko wazi kabisa:

“Bwana anawajaribu watu Wake ili kuona ni nani atakayekuwa mwaminifu kwa kanuni za Ukweli Wake. Kazi yetu ni kutangaza kwa ulimwengu ujumbe wa malaika wa kwanza, wa pili na wa tatu. Katika kutekeleza majukumu yetu hatupaswi kudharau wala kuwaogopa maadui zetu. Kujifunga wenyewe kwa mikataba na wale wasio wa imani yetu haipo kwenye utaratibu wa Mungu. Tunapaswa kuwatendea kwa fadhili na adabu wale wanaokataa kuwa waaminifu kwa Mungu, lakini hatupaswi kamwe kuungana nao katika shauri lao kuhusu masilahi muhimu ya kazi Yake Bwana.” Counsels on Health, 238

Bwana lazima apewe nafasi ya kuwaonyesha wanadamu wajibu wao na kufanya kazi katika nia na akili zao. Hakuna mtu anayepaswa kujifunga ili kutumika kwa muda wa miaka kadhaa chini ya uongozi wa kundi moja la watu au katika tawi moja bainishi la kazi ya Mwalimu mkuu; kwa maana Bwana Mwenyewe atawaita wanadamu, kama zamani alivyowaita wavuvi wanyenyekevu, na Yeye Mwenyewe atawapa maelekezo kuhusuiana na eneo lao la kazi na mbinu wanazopaswa kufuata. Yeye Atawaita watu kutoka kwenye jembe la kukokotwa na kutoka kwenye kazi zingine ili kutoa sauti ya mwisho ya onyo kwa roho zinazopotea. Kuna njia nyingi za kufanya kazi kwa Bwana, na Mwalimu Mkuu atafungua ufahamu wa watendakazi hawa, na kuwawezesha kuona mambo ya ajabu katika Neno Lake. —Shuhuda Kwa Kanisa 9: 170.

Huu sio wakati wa watu wa Mungu kuweka upendo wao katika hazina zao ulimwenguni. Sio muda mrefu, kama ilivyokuwa kwa wanafunzi wa awali, nasi tutalazimika kutafuta kimbilio katika sehemu zenye ukiwa na zenye faragha. Kama ilivyokuwa ishara wakati wa kuzingirwa kwa Yerusalemu na majeshi ya Kirumi kwa Wakristo wa Uyahudi kukimbia, ndivyo basi kwa upande wa kanisa

letu Amri ya kutekeleza sabato ya kipapa itakavyokuwa ilani kwetu. Huu utakuwa ni wakati wa kuondoka katika miji mikubwa, na kuishi katika sehemu na nyumba zilizotengwa katikati ya milima. Na sasa, badala ya kutafuta majumba/makao ya gharama kubwa hapa ulimwenguni, tunapaswa kujiandaa kuhamia katika ile nchi iliyo bora, ile ya mbinguni.— Shuhuda kwa Kanisa 5: 464-465.

Wakati wa maono ya usiku, nilisimama na kuona tukio, ambalo niliweza kuziona nyumba zikitikiswa kama mwanzi katika upepo. Majengo, makubwa na madogo, yalikuwa yakianguka chini. Sehemu za anasa na starehe, kumbi za michezo/sinema, hoteli, na nyumba za matajiri zilitikiswa na kusambaratishwa. Maisha mengi yalifutiliwa na yasiwepo, na anga likajazwa kelele/mayowe/kugumia za watu waliojeruhiwa na waliojawa na hofu.

Malaika wa Mungu wa kuangamiza walikuwa kazini. Mguso mmoja tu, na majengo, yaliyojengwa kwa uangalifu sana, ambayo watu waliyaona kuwa salama dhidi ya kila hatari, upesi yakawa lundo la takataka. Hakukuwa na uhakikisho wa usalama mahali popote. — Shuhuda kwa Kanisa 9:93.

“Wakati umekaribia ambapo miji mikubwa itafagiliwa mbali.” —Evangelism, 29.

“Bwana ametutumia onyo na mashauri ili tutoke mijini. Basi tusifanye uwekezaji zaidi katika miji.”— Country Living, 12-13.

"Mungu ametuma onyo baada, baada ya onyo kwamba shule zetu na nyumba za uchapishaji na sanitarium zinapaswa kuanzishwa nje ya jiji, mahali ambapo vijana wanaweza kufundishwa kwa ufanisi zaidi kile ambacho ni Ukweli. Mtu yeyote asijaribu kutumia shuhuda hizo kuthibitisha uanzishwaji wa maslahi makubwa ya biashara katika miji. Usifanye Shuhuda kutokuwa na athari yoyote ambayo imetolewa juu ya somo hili.

“Watu watainuka wakinena mambo potovu, ili kukabiliana na mienendo ileile ambayo Bwana anawaongoza watumishi Wake kufanya. Lakini ni wakati ambapo wanaume na wanawake walijadiliana kuanzia sababu hadi matokeo. Tumechelewa sana, tumechelewa sana, kuanzisha makampuni makubwa ya biashara mijini—tumechelewa sana kuwaita vijana wa kiume na wa kike kutoka mashambani hadi mjini. Hali zinatokea katika miji ambazo zitafanya iwe vigumu sana kwa wale wa imani yetu kubaki ndani yake. Kwa hiyo lingekuwa kosa kubwa kuwekeza pesa katika kuanzisha masilahi ya biashara mijini.”— Country Living, 29.

“Kazi ya watu wa Mungu ni kujiandaa kwa ajili ya matukio ya wakati ujao, ambayo hivi karibuni yatawajia kwa nguvu yenye upofu. Katika ulimwengu huu, ukiritimba mkubwa utaundwa. Wanadamu watajifunga pamoja katika miungano (Unions(ambayo itawafunga kwenye vifungo vya adui.” —Country Living, 10.

"Lakini muda si mrefu, kutakuwa na ugomvi na machafuko ya kutisha katika miji, kiasi kwamba wale wanaotaka kuondoka hawataweza. Ni lazima tujiandae kwa masuala haya. Hii ndiyo nuru niliyopewa.”— Country Living, 11.

Mtu anaweza kuuliza kama tunapaswa kuingia katika majukumu kwenye miji ambayo tunatarajia kuikimbia hivi karibuni, kwa kuzingatia taarifa tulizopewa kuhusu madeni tuliyoyalimbikiza na jinsi ambavyo hayapaswi kuachwa, lakini yalipwe kwa uaminifu.

5- ADA ZA TIBA

[1] – KUTOKUWA NA UBINAFSI NA REHEMA

—SIO WIZI AU UDHALIMU

"Bwana angetaka wahusika wa taaluma ya tiba waachane na mazoea yote yanayohusisha ubinafsi, ubadhirifu, ubahili, ukosefu wa haki. Yeye Ametoa hekima na ustadi kwa madaktari, Naye anapanga kusiwepo na kitu chochote chenye ladha ya unyang'anyi, hila na ukosefu wa haki kitakachofanywa na wale wanaoifanya sheria na kanuni ya Yehova kuwa kiongozi wa maisha yao.” — Medical Ministry, 121

[2] - ADA ZA KIDUNIA SIO KIWANGO CHETU watu wa Mungu

“Gharama zinazotozwa na madaktari wengine wanaohusika na taaluma ya tiba hazipaswi kuwa kigezo/kiwango chake daktari Mkristo.” —Medical Ministry, 121.

“Mara nyingi kiasi kikubwa sana cha fedha hutozwa hata kwa ajili ya huduma ndogo na madaktari, kwa sababu madaktari hawa wanajiongoza kwa kufuata malipo sawa na yale ya madaktari wa kidunia.” —Medical Ministry, 125.

“Gharama au malipo ya juu watozayo madaktari, ndio jambo linaoendelea sasa duniani; Lakini kanuni sahihi zinapaswa kuletwa katika kazi yetu.”—Medical Ministry, 126.

[3] - ADA ZA UAMINIFU (honest fees)

Kila daktari anapaswa kuwa mkweli na mwaminifu. Ikiwa atafanya upasuaji/opereshini rahisi, basi atoze bei sahili -nafuu (simple surgery simple fees).”—Medical Ministry, 121.

Malipo yanayotolewa yanapaswa kuwiana na kazi iliyofanywa.”—Medical Ministry, 126.

“Lakini watu maskini mara nyingi hutozwa kwa ajili ya huduma ambazo hawakupata kamwe.” —Medical Ministry, 122.

“Tunapaswa kutekeleza kanuni kali za rehema na haki.” —Medical Ministry, 125.

"Kutoza kiasi kikubwa cha fedha kwa kazi ya dakika chache tu, sio haki. Madaktari walio chini ya kazi ya Tabibu Mkuu zaidi kuwahi kujulikana ulimwenguni lazima waache kanuni za injili zidhibiti kila ada. Rehema na upendo wa Mungu viandikwe kila shilingi au dola inayopokelewa.” —Medical Ministry, 125-126.

“Kamwe usiwe na wazo kwamba daktari mwaminifu na mkweli hawezi kufaulu. Hisia kama hiyo inamvunjia heshima Mungu wa ukweli na haki. Anaweza kufanikiwa; kwa maana ana Mungu na mbingu ziko upande wake.”— Medical Ministry, 128-129.

[4] – MUUNDO WA INJILI WA KUJITOA MHANGA: TOA BILA MALIPO - BILA MALIPO

Akawaita wanafunzi Wake kumi na wawili, akawapa amri juu ya pepo wachafu, wawatoe, na kupoza magonjwa yote na udhaifu wa kila aina. Hao Thenashara Yesu aliwatuma, akawaagiza, akisema, Katika njia ya Mataifa msiende, wala katika mji wo wote wa Wasamaria msiingie. Na katika kuenenda kwenu, hubirini, mkisema, Ufalme wa mbinguni umekaribia. Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure. Msichukue dhahabu, wala fedha, wala shaba mishipini mwenu” Mathayo 10:1, 5, 7-9

[5] - MBINU ZA KRISTO ZINAPASWA KUWA ZETU SISI

“Yeye anayefanya kazi hii ya Bwana ya umishenari wa tiba, lazima aiweke ndani ya moyo wake wote; Kwani ni kazi inayohitaji mtu ajitoe kabisa. Yeye anayeifanya kama kazi inayofanywa kwa ajili ya ujira, atashindwa kabisa.”— Medical Ministry, 181.

Usianzishe kituo cha sanitarium binafsi kwa faida binafsi au kwa kutengeneza pesa (Medical Ministry, 152, 154-155).

Wafanyabiashara na wabadilisha fedha walikuwa wakitoza bei kubwa. Kristo aliwafukuza watu nje ya hekalu. “Kisha Mrejeshaji akafanya kazi Yake ya umishenari wa tiba. ‘Vipofu na vilema wakamjia hekaluni; Naye akawaponya.’ ”—Medical Ministry 123 (Zingatia muktadha)

“Kristo, ambaye alikuja katika ulimwengu wetu kufunua moyo wa Baba wa huruma nyororo, Yeye ametuonyesha njia ambazo watunza-Sabato wanapaswa kufuata wafanapofanya kazi yao. Haya yamebainishwa waziwazi katika sura ya hamsini na nane ya Isaya (58).” —Medical Ministry, 123.

“Sanitarium ambazo zimeanzishwa zinapaswa kuunganishwa kwa ukaribu, na bila kutenganishwa na injili.” —Medical Ministry, 159.

“Sanitarium nyingi zinapaswa kuanzishwa katika maeneo ya nje ya miji ……..Taasisi hizi zinapaswa kuwa shule za mafunzo. Wale wanaoshiriki katika sehemu hii ya kazi hawapaswi kujiona kuwa sasa ndiyo wamehitimu, kwamba wanajua yote wanayohitaji kujua. Wanapaswa kujifunza kwa uadilifu na bidii na kuishi kwa vitendo taaluma na huduma ya tiba uangalifu masomo ambayo Kristo ametoa.” —Medical Ministry, 156.

[6] - KANUNI ZA KUDUMISHA KATIKA KUFUATA MFANO WA KRISTO

Mungu Ndiye aliyetoa nyenzo na hekima kwa ajili ya kuponya wagonjwa (Medical Ministry, 121).

“Sanitarium zetu zinapoendeshwa jinsi zinavyopaswa, kazi kubwa ya umishenari wa tiba itafanyika.” — Medical Ministry, 126.

“Hebu kila mmoja afanye kazi kwa kanuni za kujitolea. Fanya kazi kungali mchana; Kwa maana usiku unakuja, ambao hakuna mtu awezaye kufanya kazi. Watu wa Mungu wanapofanya kazi kwa bidii, kwa unyenyekevu, kwa kujitolea, watapata thawabu nyingi ambazo Ayubu anazungumza juu yake: Ayubu 29:11-13 Maana sikio liliponisikia, ndipo likanibarikia; Na jicho liliponiona, likanishuhudia. Kwa sababu nalimwokoa maskini aliyenililia; Yatima naye, na yule asiyekuwa na mtu wa kumsaidia. Baraka yake yeye aliyekuwa karibu na kupotea ilinijia; Nikaufanya moyo wa mjane kuimba kwa furaha. — Medical Ministry, 129.

Matokeo ya kufanya kazi hivyo, yatakuwa katika Dunia Mpya (Medical Ministry, 129).

“Watendakazi wa umishenari wa tiba wanatambuliwa na Kristo, sio kwa sababu wamebeba jina la hiyo kazi tu, bali kwa sababu wako chini ya uangalizi na

uongozi wa mmishenari Mkuu, ambaye alitoka mbinguni ili kutoa maisha Yake kwa ajili ya maisha ya ulimwengu.”—Medical Ministry, 129.

“Kisha, kama mashahidi wa Mungu, onyesha uthibitisho kwamba uko wewe chini ya nidhamu ya taaluma na mafunzo ya mmishenari Mkuu wa tiba; kwamba umejiweka mikononi Mwake, ili kudhihirisha Roho Wake, kuuonyesha ulimwengu tabia takatifu ya kazi Yake kuu, na kuwafunulia watu wasioamini faida ya kuwa chini ya ulinzi Wake.”—Medical Ministry, 130.

“Hawapaswi kuthamini hata kanuni moja ambayo ina doa la ubinafsi. Wanapaswa kusimama mbele ya ulimwengu kama wafuasi wa Kristo, wakishiriki kujikana Kwake na kufedheheshwa, na kutangaza kuja Kwake.”— Medical Ministry, 130.

“Saa za wasiwasi ambazo wametumia, hali zenye kutatanisha ambazo wamelazimika kukutana nazo, huzuni ya moyo kwa sababu wengine walikataa kuona na kupokea vitu vinavyoleta amani yao, vimesahauliwa. Kujinyima kwao ili kusaidia kazi hiyo hakukumbukwi tena. Wanapozitazama roho walizotaka zimwamini Yesu, na kuziona zikiokolewa, zikiokolewa milele,— maandiko ya rehema ya Mungu na upendo wa Mkombozi,—ndipo zitakaporindima katika matao ya mbinguni kwa vifijo vya sifa na shukrani.”—Medical Ministry, 135.

“Hatupaswi kufunika rehema kwa ubinafsi na kisha kuiita kazi hiyo, umishenari ya tiba.”—Medical Ministry, 131.

“Kazi yoyote tunayofanya, tunapaswa kuifanya kwa Kristo. Kuna aina nyingi za kazi za muda zinazopaswa kufanywa kwa ajili ya Mungu. Kafiri/asiyeamini angefanya kazi hii kwa nguvu zake bila moyo ndani yake, kwa ajili ya kutimiza wajibu tu au kufuata ratiba, na kwa ujira aliopokea. Hajui furaha ya ushirikiano na Mtendakazi Mkuu. Hakuna ukiroho katika kazi ya Yeye anayejitumikia mwenyewe (kwa ajili ya nafsi yake au ubinafsi)

Nia au malengo ya kawaida, matarajio ya kawaida, msukumo wa kawaida, shauku ya kuonekana mjanja na watu, hutawala katika maisha yake. Mtu kama huyo anaweza kupokea sifa kutoka kwa wanadamu, lakini sio kutoka kwa Mungu. Wale ambao wameunganishwa kikweli na Kristo hawafanyi kazi kwa ajili ya ujira wanaopokea. Wanafanya kazi pamoja na Mungu, hawatafuti kujiinua.

"Katika siku kuu ya mwisho, maamuzi yatafanywa ambayo yatakuwa ya kushangaza kwa wengi. Maamuzi au hukumu ya mwanadamu haitakuwa na nafasi katika maamuzi yaliyotolewa.” —Medical Ministry, 133.

“Usiache kamwe kiwango cha Kweli, hata ingawa kung’ang’ania hicho kiwango kunakufanya uwe ombaomba.”—Medical Ministry, 132.

“Watu watakaojitolea kwa kazi kubwa ya kufundisha ile Kweli si watu watakaohongwa mali/utajiri au kuogopa umaskini.”—Life Sketches of Ellen G. White, 302.

Somo muhimu sana kutoka katika utawala wa Sulemani (Prophets and Kings, 61-65).

Sio kwa sababu ya mishahara tunayopokea ndio tunapaswa kufanya kazi. Nia inayotusukuma kumfanyia Mungu kazi haipaswi kuwa na kitu ndani yake kinachofanana na kujitumikia nafsi. Mioyo isiyo na ubinafsi na roho ya kujitoa imekuwa daima na daima itakuwa ndio hitaji la kwanza la huduma inayohitajika. Bwana wetu na Mwalimu anakusudia kwamba hakuna uzi hata mmoja wa ubinafsi utakaofumwa katika kazi Yake.

Katika juhudi zetu tunapaswa kuleta busara na ustadi, usahihi na hekima, ambavyo Mungu wa ukamilifu alivitaka kutoka kwa wajenzi wa hema ya kukutania ya duniani Patakatifu; lakini bado katika kazi zetu zote tunapaswa kukumbuka kuwa vipaji vikubwa kabisa au huduma bora zinakubalika pale tu nafsi inapowekwa juu ya madhabahu, kuwa dhabihu hai, ya kuteketezwa. - Prophets and Kings, 65.

“Sheria ya Mungu ni sheria ya upendo. Yeye Amekuzunguka kwa uzuri wa kukufundisha kwamba haujawekwa duniani ili tu kujichimbia chini mwenyewe, kujitafutia vitu, kuchimba na kujenga, kuhangaika, kuhenyeka na kusokota, bali kufanya maisha kuwa angavu na yenye furaha na uzuri kwa upendo wa Kristo,—kama vile maua, ili kuyapa furaha maisha mengine kwa huduma ya upendo.”—Thoughts from The Mount of Blessing, 97.

“Wakati Yesu alipokuwa akiwafungulia hazina za mbinguni, swali la kipaumbele kabisa katika akili nyingi lilikuwa, jinsi gani uhusiano Naye utaendeleza matazamio yetu katika ulimwengu? Yesu anaonyesha kwamba katika kuyafanya mambo ya ulimwengu kuwa mahangaiko yao makuu, walikuwa kama mataifa ya kipagani yaliyowazunguka, wakiishi kana kwamba hakuna Mungu, ambaye uangalizi Wake mwororo uko juu ya viumbe Vyake.

Haya yote Yesu alisema Luka 12:30-31 kwa maana, hayo yote ndiyo watafutayo mataifa ya duniani, lakini Baba yenu anajua ya kuwa mna haja na hayo. Bali utafuteni ufalme wa Mungu, na hayo mtazidishiwa. Mathayo 6:33 Bali utafuteni kwanza ufalme Wake, na haki Yake; na hayo yote mtazidishiwa. Nimekuja

kuwafungulia ninyi ufalme wa upend na haki na amani. Fungueni mioyo yenu ili kupokea ufalme huu, na mfanye huduma Yake kuwa ya kuvutia zaidi. Ingawa ni ufalme wa kiroho, usiogope kwamba mahitaji yako kwa maisha haya hayatatunzwa. Ukijitoa kwa utumishi wa Mungu, Yeye aliye na uwezo wote mbinguni na duniani atakupa mahitaji yako."— Thoughts from the Mount of Blessing, 98-99.

"Mbingu zote zinatazama kwa shauku kubwa kuona ni muhuri gani wa kazi ya umishenari wa tiba utawekwa katika usimamizi wa wanadamu. Je, watu wataufanyia biashara mpango wa Mungu uliowekwa wakfu kwa ajili ya kuzifikia sehemu zilizo gizani kwa udhihirisho wa baraka Zake? —Medical Ministry, 131.

"Nawauliza wale wanaoishi katika ubatili wa kujifurahisha wenyewe na ubinafsi, je, mtaendelea kutenda kana kwamba hauna jukumu kujizoeza kujikana nafsi? Je, wewe unaishi kwa madhumuni gani? Je, unatimiza mema gani? Je, unaweza kumudu kuishi kwa ajili yako mwenyewe? Je, wewe unaweza kweli kupata uzima wa milele unapoishi hivyo?" —Medical Ministry, 133.

"Lakini badiliko limekuja ambalo limezuia kazi ambayo Mungu alipanga ili isonge mbele bila chembe ya ubinafsi. Mbingu yote inatazama kwa wasiwasi mkubwa kuona nini kitakuwa matokeo ya kazi ambayo ni kubwa na muhimu sana. Mungu anatazama, ulimwengu wa mbinguni unatazama; Na roho zinaangamia. Je, mradi wa rehema, ambao kwa huo katika siku za nyuma Mungu amedhihirisha neema Yake katika kuokoa na kurejesha, kuwa suala la bidhaa za ubinafsi? Je, chombo kilichotolewa kwa majaliwa na Mbingu kuleta mema kwa mwanadamu na utukufu kwa Mungu kitapotea au kuharibiwa kupitia matumizi yasiyofaa? Je, chombo cha Mungu cha baraka kitatumiwa na wale wanaodai kuamini Ukweli katika kununua na kuuza na kupata faida?

"Uzoefu wa siku za mitume utatujia sisi, ikiwa wanadamu watapokea Roho Mtakatifu afanye kazi ndani yao. Bwana ataondoa baraka Yake pale ambapo masilahi ya ubinafsi yanaendekezwa, lakini Yeye atawaweka watu Wake katika milki ya mema kote ulimwenguni ikiwa watatumia hii kwa ajili ya kuuinua ubinadamu. Kazi Yake inapaswa kuwa ishara ya ukarimu Wake, alama/ishara ambayo itauvuta ulimwengu umwamini Yeye, na kuleta rasilimali kwa ajili ya maendeleo ya ufalme Wake.

"Mungu ataujaribu unyofu wa wanadamu. Wale ambao watajikana nafsi zao, kuchukua msalaba, na kumfuata Kristo

watakuwa na kazi endelevu ya kufanya katika kazi ya kurejesha utaratibu wa kianadamu ulioanguka. Wale wanaojitolea kwa ajili ya Ukweli huvutia sana ulimwengu. Mfano wao ni wa kuambukiza na wa kushawishi. Watu huwa wanaona kwamba ndani ya Kanisa kuna imani inayofanya kazi kwa upendo na kuitakasa nafsi.” —Medical Ministry, 131-132.

6- VIWANGO VYA KITAASISI

[1] - USAWA

“Katika huduma zetu za vituo vyetu vya sanitarium mahitaji na huduma lazima vitolewe kwa madaraja yote.”—Medical Ministry, 169.

“Bwana hatoi mwito kwa watu wetu waanzishe taasisi ambapo wote wanaokuja wanaweza kupokea chakula na mahali pa kulala bila malipo, na ambapo mambo ya pekee ya imani yetu hayapaswi kuletwa. Bwana hajaweka kazi hii juu ya Muadventista yeyote wa Siku ya Sabato. Kufanya hivyo kungekuwa matumizi mabaya ya wakati na mali.”—Medical Ministry, 169-170.

"Malazi na matibabu lazima yawe ya kufaa watu kiasi kwamba wagonjwa wa tabaka la juu watavutiwa. Vyumba lazima viwekwe kwa matumizi ya wale ambao wako tayari kulipa bei huria-ya ukarimu. Lakini madaktari hawapaswi kuweka makadirio ya juu sana kwa wagonjwa matajiri ambao wanaweza kumudu kulipa bei ya juu; Wala pasiwepo matumizi ya kupita kiasi au ubaradhifu kwa nia ya kupata upendeleo.

Gharama za matibabu na malazi lazima zisiwe za juu sana hivi kwamba kutakuwa na kusita kuweka chakula rahisi na kizuri ambacho ni muhimu kwa afya. Uliza bei nzuri kwa matibabu uliyopewa. Kazi hii itajionyesha yenyewe kwa nia zote. — Medical Ministry, 170.

“Matengenezo yanahitajika kuhusiana na usimamizi wa taasisi hizi. Taasisi hizi hazipaswi kuendeshwa kama ambavyo ulimwengu ungeziendesha. Ingawa wengi ambao hawana uwezo wa kulipa wanatibiwa bila malipo, wengine hutozwa bei kubwa kwa shughuli ambazo huchukua muda mfupi tu. Utozaji ada wa madaktari wa kidunia haupaswi kutawala katika taasisi zetu.”——Medical Ministry, 170.

[2] - BORA KUPATA HASARA ZA KIFEDHA KULIKO KUWA MAMLUKI KWA TAMAA YA PESA NA KUWA NA HISIA ZA HASIRA

"Unapaswa kujiweka kila wakati katika nafasi ya yule unayeshughulika naye na kuona jinsi ungehisi chini ya hali kama hiyo; Kisha tenda kama vile ambavyo ungetaka wengine wakutendee, ili kivuli kisipate sababu ya kutupwa katika

thamani ya Ukweli. Ukweli haupaswi kulaumiwa kwa ajili ya kupata dola au senti chache. Usiruhusu tukio litolewe kwa mtu yeyote kusema kwamba Waadventista Wasabato daima hufanya vitendo vibaya vya hiana. Tutavuna dharau. Hebu shughuli zetu zote za kibiashara zisimame katika nuru safi, isiyochafuliwa mbele ya ulimwengu na kwa wale wa imani yetu. Usiruhusu njia yako ya kutenda iwe ya tabia hiyo kwamba inahitaji maelezo ili kuifanya ionekane kuwa njia inayofaa au inayostahili kibali." — Medical Ministry, 171.

7- MSHAHARA NA SAA

[1] - HAKI

Wafanyakazi wanaopaswa kuajiriwa ni wale wazalishaji (Counsels on Health, 319).

Wafanyakazi wanapaswa kulipwa kulingana na saa za kazi ya uaminifu (Counsels on Health, 315).

Kila mtu anapaswa kupokea mishahara ya haki (Counsels on Health, 303, 305-306).

Ingekuwa bora zaidi kutumia fedha kidogo kwenye majengo na zaidi kwa mishahara ya haki (Counsels on Health, 312).

"Wakati fulani umewatia moyo watendakazi kwamba mishahara yao ingeongezwa, halafu umeshindwa kutimiza ahadi iliyoifanya. Je, hii ni kuruhusu nuru yako iangaze katika matendo mema? Je, huduma hiyo inakubalika kwa Bwana? Je, aina hii ya kazi itaendelea katika taasisi za Mungu, ambazo zilianzishwa ili kufanya kazi kwa ajili ya kuongoa roho za wale waliounganishwa nazo? Unapaswa kuweka mambo sawa kwa kurejesha kisicho halali kwa kadri iwezekanavyo. Je, hukujua wakati unazuia mishahara kuwa usingepaswa kufanya hivi, na pia usingetaka watu wakufanyie hivyo? —Medical Ministry, 183

[2] - USAWA

Kusiwe na mishahara ya juu kwa vikundi maalum au watu wenye talanta zaidi(Counsels on Health, 299, 302-303, 307, 316- 318, 320). Isipokuwa: Msimamizi Mkuu (Counsels on Health, 305), Tabibu Mkuu (Counsels on Health, 311). Mfano wa Huram na talanta zake maalum kwenye hekalu la Sulemani akidai mishahara mikubwa na athari za kufanya hili kwa wafanyakazi wenzake. (Prophets and Kings, 64). "Mshahara wa mwanamke unapaswa kuendana na huduma zake."—Counsels on Health, 365.

[3] - KUSHIRIKI KWA USAWA KATIKA HASARA NA USTAWI

Wakati pesa inapokuwa ngumu-hebu wote wakubali kwa usawa kupunguziwa kwa mishahara (Counsels on Health, 304).

Kunapokuwa na mafanikio zaidi—wote wanapokea mishahara ya juu (Counsels on Health, 311).

Hakuna anayepaswa kufanyishwa kazi masaa mengi kupita kiasi (Counsels on Health, 311).

“Usiwaruhusu wasaidizi kufanya kazi kupita kiasi. Hebu wagonjwa waone wauguzi walio na moyo mkunjufu, waangavu na waangalifu, sio wauguzi ambao, kwa sababu wana kazi nyingi, wamekatishwa tamaa na kuvunjwa moyo. Ni kinyume kabisa na kanuni ambazo huduma zetu za vituo vya sanitarium zimeanzishwa pale wauguzi wanapovunjika miili au afya, katika kazi zao.” — Medical Ministry, 212.

"Wafanyakazi katika vituo vyetu vya sanitarium wanapaswa kupewa mafunzo kwa kazi ambayo wanaendana nayo vyema. Lakini wakati dharura inapotokea, na msaada unapohitajika, wafanyakazi hawapaswi kusema, hiyo si kazi yangu. Msaidizi ambaye ana wazo kwamba anapaswa kufanya kazi aliyopewa tu, na si zaidi, ambaye hajisikii jukumu la kusaidia popote na wakati wowote msaada unapohitajika, anapaswa kufuta wazo hili mara moja akilini mwake. Hapaswi kamwe kuhisi kwamba kosa limefanywa kwake ikiwa katika dharura ataombwa kufanya kazi kwa muda wa ziada. Msaada wa ziada unapohitajika, hebu wafanyakazi wasaidie kwa hiari, katika upole wa Kikristo, nao watapata baraka.”—Medical Ministry, 176-177.

Kufanya kazi kupita kiasi, kula kupita kiasi, ukosefu wa mazoezi, na afya ya mfanyakazi (Medical Ministry, 291-297).

Madaktari hawapaswi kufanya kazi kupita kiasi—pata usaidizi/msaada zaidi ikibidi— kuchukua likizo ni muhimu hapa na pale (Counsels on Health, 354).

Uwe na wafanyakazi wa kutosha wa kumsaidia daktari ipasavyo (Counsels on Health, 360).

Kati ya watu wote, madaktari wanapaswa kuwa na saa za zilizotengwa kwa ajili ya kupumzika (Counsels on Health, 361).

8 - KIKOMO CHA UKUAJI

"Ikiwa wewe unayesimamia taasisi unaona taasisi zingine zikijitahidi kwa ushujaa ili kusimama, na kufanya kazi sawa na kazi ya taasisi ambazo umeunganishwa nazo, usiwe na wivu." — Counsels on Health, 308.

"Afadhali punguza baadhi ya mipango yako mikubwa na uwasaidie wale wanaotatizika. Kuwasaidia katika kutekeleza baadhi ya mipango yao ya kuongeza vituo vyao. Usitumie kila dola katika kupanua vituo vyako na kuongeza majukumu yako. Hifadhi sehemu ya fedha zako kwa kuanzisha katika maeneo mengine taasisi za afya na shule."—Counsels on Health, 308.

"Kila mtu anapaswa kulenga kuendeleza kazi yenye mafanikio kwa kazi iliyowekwa mikononi mwake. Taasisi zetu zote zinapaswa kukumbuka hili na kujitahidi kupata mafanikio: lakini wakati huo huo wakumbuke kwamba mafanikio yao yataongezeka kwa uwiano kadri wanavyoishi na kutenda kwa ukarimu usio na ubinafsi, wakishiriki wingi wao na taasisi ambazo zinajitahidi kupata nafasi ya ufanisi. Taasisi zetu zilizofanikiwa zinapaswa kusaidia zile taasisi ambazo Mungu amesema zinapaswa kuwa hai na kufanikiwa, lakini ambazo bado zinatatizika kuishi. Kati yetu kuna kiasi kidogo sana cha upendo wa kweli, usio na ubinafsi."—Counsels on Health, 309.

"Michango ilitolewa kwa ajili kituo chetu cha sanitarium cha Battle Creek katika historia yake ya awali, na je, kituo hiki cha sanitarium hakipaswi kuzingatia kwa umakini kile ambacho kinaweza kufanya ili kusaidia taasisi-pacha kwenye Pwani ya Pasifiki? Ndugu zangu katika Battle Creek, je, haionekani kuwa kwa mujibu wa amri ya Mungu kuacha matakwa yenu, kupunguza shughuli zenu za ujenzi, na kuacha kupanua taasisi zetu katika kituo hicho? Kwa nini msihisi kwamba ni fursa na wajibu wenu kuwasaidia wale wanaohitaji msaada?"—Counsels on Health, 309-310.

"Ni ubinafsi tu ndio unaowazuia wanadamu kutuma msaada mahali ambapo kazi ya Mungu haifanikiwi ukilinganisha na taasisi ambayo wanaisimamia."— Counsels on Health, 310.

"Zuia matamanio yako ya ukuu katika kupanua taasisi na kukusanya majukumu. Hebu baadhi ya fedha zinazoingia kwenye vituo vya afya zipewe kwa taasisi zinazohitaji msaada. Hakika hii ndiyo sawa. Ni kwa mujibu wa mapenzi na njia ya Mungu, na italeta baraka za Mungu juu ya kituo cha sanitarium.—Counsels on Health, 312.

"Kutokana na nuru niliyopewa, wasimamizi wa taasisi zetu zote, na hasa vituo vya sanitarium vipya vilivyoanzishwa, wanapaswa kuwa waangalifu ili kutumia

vizuri mali, ili waweze kuwa katika nafasi ya kusaidia taasisi kama hizo ambazo zinapaswa kuanzishwa katika sehemu nyingine za dunia.”—Counsels on Health, 224- 225.

"Hatupaswi kunyonya fedha kwa ajili ya maeneo machache pesa zote za hazina, lakini lazima tufanye kazi ili kujenga kazi katika maeneo mengi. Eneo jipya linapaswa kuongezwa kwa Ufalme wa Bwana. Sehemu zingine za shamba Lake la mizabibu zinapaswa kuwekewa vituo ambavyo vitatoa sifa kwa kazi hiyo. Bwana anatukataza kutumia njama za ubinafsi katika utumishi Wake. Yeye Anatukataza kuchukua mipango ambayo itamnyang'anya jirani yetu vituo ambavyo vitafanya asiweze kutenda sehemu yake katika kuwakilisha Ukweli. Tunapaswa kuwapenda jirani zetu kama nafsi zetu.”— Counsels on Health, 275.

“Watu walio katika nyadhifa za uaminifu wanapaswa kuzingatia njia wanazoshughulikia kama mapato ya Mungu, na kuzitumia kwa njia ya kiuchumi. Wakati kuna wingi katika hazina, hawapaswi kuwekeza katika kuongeza jengo hata jengo katika sehemu ambazo tayari zimepewa kumbukizi za Mungu. Mamia ya maeneo mengine yanahitaji pesa hizi, ili wao pia, wawe na kitu kilichothibitishwa kuwakilisha Ukweli.”— Medical Ministry, 165.

"Bwana hakika anatufungulia njia kama watu kugawanya na kugawanya tena makundi ambayo yamekua kwa kiwango kikubwa kufanya kazi pamoja kwa faida kubwa. Na mgawanyiko huu unapaswa kufanywa, sio tu kwamba wanafunzi wanaweza kuwa na faida kubwa zaidi, lakini kwamba walimu wanaweza kufaidika, na maisha na afya kuokolewa. Kuanzisha shule nyingine itakuwa bora kuliko upanuzi zaidi wa shule katika . Hebu eneo lingine lipate faida kutokana na moja ya taasisi zetu za elimu. —Medical Ministry, 322

“Bwana atazipa sanitarium zetu ambazo tayari zimeanza kazi fursa ya kushirikiana Naye katika kusaidia taasisi mpya zilizoanzishwa. Kila taasisi mpya inapaswa kuzingatiwa kama msaidizi-mwenza katika kazi kuu ya kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu. Mungu amezipa vituo vyetu vya afya fursa ya kuanzisha kazi ambayo itakuwa kama jiwe lenye uzima, linalokua kadiri linavyoviringishwa kwa mkono usioonekana.Hebu jiwe hili la ajabu lisaidiwe kubiringika/kujongea.”—Counsels on Health, 220.

9- KUTOHUSISHWA NA VIKUNDI VYA KILIMWENGU AU MASHIRIKA

Taarifa kuhusu hili zitapatikana zikiwa zimekusanywa pamoja katika sehemu yenye kichwa “Viwango vya Kufanya Kazi.”

10 - PANGA KWA HATUA ZINAZOPATANA

“Hebu kikundi kiundwe kwa utaratibu wa Jumuiya ya Kikristo ya Juhudi, na tuone kile kinachoweza kufanywa na kila wakala wa kianadamu anayewajibika katika kutazama na kuboresha fursa za kufanya kazi kwa Bwana. Bwana Ana shamba la mizabibu ambalo kila mtu anaweza kufanya kazi nzuri. Wanadamu wanaoteseka wanahitaji msaada kila mahali.”—Counsels on Health, 537.

11 - USIMAMIZI

[1] - HAUPASWI KUSUKUMA MAWAZO, BILA KUJALI USHAURI

“Hakuna mtu anayepaswa kujiweka kama mtawala, kama bwana juu ya wanadamu wenzake, ili kutekeleza misukumo yake ya asili. Hakuna sauti na ushawishi wa mtu mmoja unapaswa kuruhusiwa kuwa nguvu ya kudhibiti. Wale wanaowadhulumu wafanyakazi wenzao katika taasisi zetu, na wanaokataa kubadili namna yao ya kuwatendea wasaidizi chini ya usimamizi wao, wanapaswa kuondolewa. Kama waangalizi, walipaswa kuwa na ushawishi wa hali ya juu, unaosafisha kwa ajili ya haki. Uwekezaji wao kwa nguvu unaifanya iwe muhimu zaidi kwao kuwa vielelezo vya Ukristo wa Kweli.”—Medical Ministry, 165.

“Nimeagizwa na Bwana kusema kwamba nafasi hiyo haimpi mtu neema au kumfanya kuwa mwadilifu. ‘Kumcha Bwana ni mwanzo wa hekima.’ Baadhi ya watu waliokabidhiwa nafasi za uwajibikaji hupenda kudhania kwamba nafasi ya uongozi ni kwa ajili ya kujitukuza. Usiruhusu meneja afikirie kwamba akili zote lazima ziwe chini ya akili yake, kwamba matakwa yote lazima yawe chini ya matakwa yake, na kwamba mbinu zote lazima ziwekwe kando ya mbinu zake. Hakuna jeraha kubwa zaidi kwa taasisi yoyote kuliko hili la kumruhusu mtu kama huyo kubaki katika nafasi yake, baada ya kuwa kwenye kipimo sahihi. Ni dhambi dhidi ya Mungu kuruhusu wasimamizi wasio waaminifu kubaki katika nafasi za uaminifu; Kwa maana watu wa Bwana wanaweza kupotoshwa kwa ukosefu wao wa uaminifu.” —— Medical Ministry, 165.

[2] - LAZIMA AWE MWANAFUNZI, YUKO TAYARI KUPOKEA USHAURI

“Asiwepo mtu katika taasisi, hata msimamizi, anayepaswa kuchukua msimamo kwamba yuko huru kufuata maamuzi yake katika mambo yote. Mtu yeyote asifikiri kwamba anajua mengi sana na kwamba hahitaji tena kujifunza. Tusipojifunza juu ya Kristo kila wakati, na tusipokuwa tayari kuchukua maelekezo na ushauri kutoka kwa ndugu zetu, tutashindwa katika kazi yetu; Kwa maana tutakuwa watu waliojitosheleza wenyewe, na kwa wale wanaojitegemea wenyewe na kujitosheleza, Mungu hawezi kufanya kazi nao”—Medical Ministry, 166.

[3] - LAZIMA AJIDHIBITI-AWEZE KUTAWALA NAFSI

“Mtu aliye mkuu wa kazi yoyote katika kazi ya Mungu anapaswa kuwa mtu mwenye akili mahiri, mtu mwenye uwezo wa kusimamia masilahi makubwa kwa mafanikio, asiye na hasira, mwenye uvumilivu, asiye na hasira kama wa Kristo, na kujitawala nafsi. Ni yule tu ambaye moyo wake unabadilishwa kwa neema ya Kristo Ndiye anayeweza kuwa kiongozi anayefaa.” ——Medical Ministry, 164.

[4] - LAZIMA ASIMAME BILA WOGA KWA AJILI YA HAKI

"Mtu anayechukua nafasi ya msimamizi lazima awe jasiri na wa kweli, awe tayari kusimama bila woga kwa kile anachojua kuwa sawa. Ni lazima awe mtu ambaye ni mwepesi wa kupambanua na kubagua, mtu anayeweza kusahihisha jambo baya kuwa sahihi kwa msuguano mdogo kwa kadri iwezekanavyo. Ukosefu wa utambuzi, kushindwa kufikiri sababu na matokeo, mara nyingi huleta katika taasisi zetu hali ya mambo ambayo yanamchukiza kabisa Mungu.” —Medical Ministry, 166.

[5] -HAPASWI KUKUBALI MAOMBI YA KIDUNIA

Si kukidhi matakwa ya raha au starehe; Hakuna burudani za kidunia na matumbuizo au za maonyesho (Counsels on Health, 293, 271-274; Medical Ministry, 205).

Sio kukidhi ladha na mazoea ya watu wasiowekwa wakfu kwa kuleta ubunifu (Medical Ministry, 163).

[6] - ANAPASWA KUWA KAMA KRISTO

“Wale wanaosimamia kazi hii wanapaswa kwanza wawe kama Kristo. Kila siku wanapaswa kujifunza katika shule ya Kristo. Ndipo watakuwa na hekima ya kujua jinsi ya kukabiliana na akili za wanadamu. Watajua jinsi ya kuchukua mambo kutoka hatua hadi hatua ya ujuzi wa Kweli, kwa wale wanaokuja kwenye taasisi ili kujitayarisha kwa manufaa katika utumishi wa Mungu.”— Medical Ministry, 175.

[7] - WANAPASWA KUONGOZWA NA KUSIMAMIWA NA BWANA

"Anapaswa kuwa na hadhi na maarifa, yaliyochanganyika na hisia wazi ya jinsi ya kutumia mamlaka yake. Kristo lazima afunuliwe katika maisha yake. Ni lazima awe mtu anayeweza kutoa mafundisho ya kidini/kiroho na kuwa na ushawishi wa kiroho. Ni lazima ajue jinsi ya kushughulika na akili, na lazima aruhusu akili yake mwenyewe kutawaliwa na Roho. Hekima itatoka midomoni mwake kwa maneno ya kutia moyo kwa wote ambao ameunganishwa nao. Lazima ajue jinsi ya

kutambua na kurekebisha makosa. Ni lazima awe mtu ambaye atapatana na wafanyakazi wenzake, mtu ambaye ana uwezo wa kubadilika na kuendana na hali. Anapaswa kuwa na uwezo wa kuzungumza juu ya mambo mbalimbali ya imani yetu, kulingana na muktadha. Maneno na matendo yake yanapaswa kudhihirisha haki, hukumu, na upendo wa Mungu."—Medical Ministry, 169.

[8] - LAZIMA AWE MPOLE NA MUELEWA

"Wale walio katika nafasi za kuwajibika watalazimika kushughulika na wale ambao maisha yao si rahisi. Taabu na ufukara, bila matumaini ya hali bora katika siku zijazo hufanya mzigo wao kuwa mzito sana. Na wakati maumivu na ugonjwa yanapongezeka, ndiyo mzigo huwa mzito zaidi kuliko nguvu za kuubeba. Wasimamizi wa Mungu wasiweke ukali katika shughuli zao na watu kama hao. Huu utakuwa ukatili wenyewe. Hebu wajivike kwa adabu kama kwa vazi. Hebu wawe wenye uungwana, kujistahi, adabu, fadhili na wapatanishi katika kushughulika na wale walio chini kabisa na maskini zaidi. Mungu ataona na kuwapa thamani kwa shughuli hizo."—Medical Ministry, 172.

[9] - LAZIMA AWAFUNZE KWA UANGALIFU WAFANYAKAZI WENZAKE

"Wale wanaochukua nyadhifa za jukumu katika vituo vya sanitarium, ama kama meneja au matroni, wanapaswa kuhisi umuhimu wa jukumu lililo juu yao kuwafunza na kuwazoeza wale walio chini ya uwezo wao kufanya kazi yao kikamilifu na haraka."—Medical Ministry, 175.

[10]- UNAPASWA KUPENDA NA KUSHUGHULIKA KWA UPOLE NA WATU WANAOKOSEA, KUKUMBUKA JINSI KRISTO ANAVYOSHUGHULIKA NAWE

"Kristo anasema, Kondoo Wangu husikia sauti Yangu, nao wananifuata, wakitoka mbali na njia za dhambi. Kama Kristo alivyofanya kazi, ndivyo wewe unavyopaswa kufanya kazi. Katika huruma nyororo na upendo hutafuta kuwaongoza wanaokosea kwenye njia sahihi. Hii itahitaji uvumilivu mkubwa na ustahimilivu, na udhihirisho wa mara kwa mara wa upendo wa kusamehe wa Kristo. Kila siku huruma ya Mwokozi lazima ifunuliwe. Mfano aliouacha lazima ufuatwe. Alichukua asili yetu ya dhambi iwe juu ya asili Yake isiyo na dhambi, ili apate kujua jinsi ya kuwasaidia wale wanaojaribiwa."—Medical Ministry, 181.

"Sio lazima kuleta kila kitu kinachohitaji kusahihishwa mbele ya meneja/msimamizi. Unapomwona mfanyakazi katika makosa, nenda kwake, na uzungumze naye kwa upole na utulivu, ukionyesha nia ya dhati ya ustawi wake. Katika visa tisa kati ya kumi, juhudi zako zitafanikiwa. Utaokoa nafsi na kifo, na kuficha wingi wa dhambi."—Medical Ministry, 181-182.

"Ingawa wanafunzi lazima wawe tayari kuanza na majukumu yaliyo madogo na kutoa ushahidi kwamba wanaweza kuaminiwa, yeye [mkufunzi] anapaswa kuhisi upendo mwororo wa dhati zaidi juu yao. Hapaswi kukatishwa tamaa na ujinga wao, bali awape sifa kwa mambo yote mazuri anayoyaona ndani yao. Katika kujielimisha katika mwelekeo huu, anapata uzoefu wa thamani, - uzoefu ambao anahitaji ili kuwa Mkristo wa vitendo.

“Wanafunzi wakifanya makosa, asifikirie kuwa hawastahili kujaribiwa tena, kana kwamba wamefanya dhambi ambazo haziwezi kusamehewa. Anapaswa kuonyesha makosa yao kwa fadhili; Na wao, kwa upande wake, wanapaswa kushukuru kwa rafiki mwaminifu kiasi cha kuwaambia makosa yao na jinsi ya kuyarekebisha. Kuwatupilia mbali waliokosea, kuwatendea kwa ukali, haingekuwa kama Kristo anavyomtendea. Sisi sote tunakosea, na tunahitaji huruma na kufikiriwa na wengine na hata msamaha wa mtu mwingine. Msimamizi hawezi kupata ukamilifu popote pale, na asitarajie hilo, lakini lazima avumilie upotovu wa wanadamu, na kujaribu kuwafundisha.” —Medical Ministry, 211.

12 – WAFANYAKAZI

[1] – UNADHIFU, UANGALIFU, NA USAHIHI

Hebu kila kitu ndani na karibu na vituo vya sanitarium viwe na utaratibu na unadhifu (Counsels on Health, 242).

Mavazi ya kujistahi, kiasi na nadhifu ya wafanyakazi, lakini mwenendo ni muhimu zaidi (Counsels on Health, 292)

"Jenga kwa ajili ya umilele. Masomo ya Kristo yako mbele yetu. Tunapaswa kufanya kwa uangalifu, kwa uzuri, kwa unadhifu, na kwa usahihi chochote kitakachofanywa.”—Medical Ministry, 204.

"Kila kitu kinachohusiana na kituo cha sanitarium kinapaswa kuwa safi, nadhifu, chenye utaratibu. Unadhifu na utaratibu mara nyingi utakuwa na ushawishi zaidi kuliko maneno tu.”—Medical Ministry, 212.

Sio busara kuwa na wanafunzi wengi wasio na uzoefu kama wafanyakazi, na wachache sana wenye uzoefu na ufanisi (Counsels on Health, 292; Medical Ministry, 173 174).

[2] - USHAURI NA UKIMYA DHIDI YA UKOSOAJI NA MAZUNGUMZO YASIYO NA MAWAZO

Unapoona ni wapi mabadiliko yanaweza kufanywa na kuwa na suluhisho linalowezekana, nenda kwa mkuu wa taasisi na ushauriane naye. Usizungumze au kusikiliza kuhusu kukata tamaa. Nyamaza kimya au fanya kazi ya kusahihisha uovu (Counsels on Health, 243- 244). Hakuna ukosoaji (Medical Ministry, 137-138).

“Ikiwa tungeyalinda maneno yetu, ili midomo yetu isitoe chochote kutoka humo isipokuwa tu fadhili, tutatoa uthibitisho kwamba tunajitayarisha kuwa washiriki wa familia ya mbinguni. Kwa maneno na matendo tutaonyesha sifa za yule aliyetuita kutoka gizani na kuingia katika nuru Yake ya ajabu. Lo, ni ushawishi ulioje wa matengenezo ungetokea ikiwa sisi kama watu tungethamini kile chenye kustahili kwa kweli ya kipaji cha usemi na ushawishi wake juu ya nafsi za wanadamu!”—Medical Ministry, 213.

"Mazungumzo niliyosikia katika vyumba vya wasaidizi hayakuwa ya tabia ya kuinua na kuimarisha akili au maadili. Mazungumzo ya kipuuzi, mzaha wa kipumbavu, kicheko kisicho na maana, kilianguka kwa uchungu juu ya sikio langu….

“Nilistaajabu nilipoona wivu ukiendekezwa na kusikiliza maneno ya wivu, mazungumzo ya kizembe, ambayo yaliwafanya malaika wa Mungu kuaibishwa.”—Counsels on Health, 412

“Hebu wasaidizi, katika idara yoyote wanayofanya kazi, wawe waangalifu na wenye hekima. Wakirudia yote wanayosikia na kuyazungumza yote wanayoyaona, watakuwa laana kwa taasisi. Kuna wale wanaopata furaha katika kuwaambia watu mambo ili kuchochea mihemko. Hili ni jambo la kukatisha tamaa kwa taasisi, na halipaswi kupata kibali hata kidogo.”—Counsels on Health, 212.

“Usiruhusu futuhi na mizaha katika uzoefu wako, bali uwe mchangamfu; Kwa maana hii ni neema iliyo bora kabisa.”— Medical Ministry, 214.

Mazungumzo ya kipuuzi, mzaha wa kipumbavu, vicheko visivyo na maana, maneno yanayozungumzwa bila kuchukua tahadhari na husuda, maongezi ya kizembe, utani wa matusi, mazungumzo ya ubatili, mzaha juu ya mambo matakatifu (Counsels on Health, 412-413).

[3] - UMOJA

“Umoja wa utendaji katika kazi tofauti-tofauti lazima udumishwe.”—Counsels on Health, 203.

"Ni muhimu sana kwamba maelewano yawepo katika taasisi zetu. Afadhali kazi hiyo kuwa na ulema kuliko watendakazi ambao hawajajitolea kikamilifu

kuajiriwa. Ni watu wasiowekwa wakfu, wasioongoka ndio ambao wamekuwa wakiharibu kazi ya Mungu. Bwana hawezi kuwatumia kwa namna yoyote watu ambao hawajajiweka wakfu kabisa kwa utumishi Wake."—Medical Ministry, 207.

[4] - UAMINIFU KWA TAASISI

Uaminifu kwa taasisi zetu: kwa kupata mafunzo kutoka katika hizi taasisi, hatupaswi kutoka na kuziacha kwa ajili ya kazi mahali pengine. Hatupaswi kushawishi watu kuja kufanya kazi kwenye taasisi kwa kuwapa mishahara ya juu. (Counsels on Health, 282, 284; Medical Ministry, 201).

"Bwana lazima apewe fursa ya kuwaonyesha watu wajibu wao na kufanyia kazi akili zao. Hakuna mtu anayepaswa kujifunga ili kutumikia kwa muda wa miaka kadhaa chini ya uongozi wa kundi moja la watu au katika tawi moja maalum la kazi ya Bwana, kwa maana Bwana Mwenyewe atawaita watu, kama alivyowaita wavuvi wanyenyekevu zamani, na yeye Mwenyewe atawapa maagizo kuhusu shamba lao la kazi na mbinu wanazopaswa kufuata. Atawaita watu kutoka kwenye jembe la plau na kutoka kwa kazi zingine, kutoa maelezo ya mwisho ya onyo kwa roho zinazoangamia. Kuna njia nyingi za kufanya kazi kwa Bwana, na Mwalimu Mkuu atafungua ufahamu wa wafanyakazi hawa, na kuwawezesha kuona mambo ya ajabu katika neno Lake."— Counsels on Health, 395.

[5] - WAFANYAKAZI WA KIKRISTO

Vituo vyetu vya sanitarium havipaswi kuwa na wafanyakazi ambao hawako chini ya utawala wa Roho wa Mungu, na ambao hawatii maagizo ya Kristo—ambao wanaudhika kirahisi, wasumbufu, wanaokosa adabu, wasio waungwana, wasiojistahi, wanaogombeza wengine, wasio na tabia za kupendeza na wasio na nidhamu. (Medical Ministry, 173).

"Ingekuwa bora zaidi kulipa mishahara ya juu zaidi na kupata wasaidizi wazuri, wenye busara katika taasisi zetu kuliko kuwakubali wale ambao huwezi kuwanidhamisha na kuwafundisha."—Medical Ministry, 173.

"Hebu wale walioajiriwa katika taasisi zetu wawe wale ambao wataacha nuru ya Ukweli iangaze kwa maneno na matendo yao ya kila siku. Ni kwa kuwa hivyo tu, ndiyo kwamba Kristo anaweza kuwakubali kuwa watenda kazi pamoja Naye."— Medical Ministry, 173.

"Juhudi kipekee zinapaswa kufanywa ili kupata huduma za watenda kazi Wakristo waangalifu. Ni kusudi la Mungu kwamba taasisi ya afya ziandaliwe kwa kupangwa na kudhibitiwa kwa upekee na Waadventista Wasabato, na pale

wasioamini wanapoletwa kuchukua nafasi za kuwajibika, ushawishi unatawala hapo hapo utaonyesha uzito mkubwa dhidi ya kituo hicho cha sanitarium"—Counsels on Health, 401.

[6] – UAMINIFU KATIKA MAMBO MADOGO

"Ni muhimu usitawishe uaminifu katika mambo madogo, na kwa kufanya hivyo utapata mazoea ya uadilifu katika majukumu makubwa zaidi. Matukio madogo ya maisha ya kila siku mara nyingi hupita bila taarifa yetu, lakini ni mambo haya, ndiyo ambayo yanaunda tabia. Kila tukio la maisha ni kubwa kwa wema au kwa ubaya. Akili inahitaji kuzoezwa kwa majaribio na matendo ya kila siku, ili ipate nguvu ya kusimama katika hali yoyote ngumu."—Counsels on Health, 404.

[7] – WIZI

"Wasaidizi katika kituo cha sanitarium hawapaswi kuhisi uhuru wa kuchukua vyakula vinavyotolewa kwa ajili ya wagonjwa, kwa matumizi yao wenyewe."—Counsels on Health, 408.

[8] – MUONEKANO BINAFSI

"Wengi huvaa kama ulimwengu, ili kuwa na ushawishi juu ya wasioamini; Lakini hapa wanafanya makosa ya kusikitisha. Kama wangekuwa na ushawishi wa kweli na wa kuokoa, hebu waishi kwa kudhihirisha taaluma yao, waonyeshe imani yao kwa matendo yao ya haki, na waonyeshe tofauti kuwa wazi kati ya Mkristo na walimwengu. Maneno, mavazi, matendo, huzungumza kwa niaba ya Mungu."—Counsels on Health, 598.

"Wakristo ni nuru ya ulimwengu, chumvi ya dunia. Mavazi yao yanapaswa kuwa safi na ya kujistahi, mazungumzo yao yanapaswa kuwa safi na ya kimbingu, na mwenendo wao usiwe na lawama."—Counsels on Health, 604 (Evangelism, 672-673; Welfare Ministry, 61).

[9] – UCHANGAMFU

"Katika vituo vya afya vya sanitarium na hospitali, mahali ambapo wauguzi huhusishwa mara kwa mara na idadi kubwa ya wagonjwa, inahitajika jitihada iliyoamuliwa ili hali iwe ya kupendeza na uchangamfu sikuzote na kuonyesha hekima ya kufikiria wengine kwa uangalifu katika kila neno na tendo."— Counsels on Health, 406.

[10]- UTULIVU

“Wauguzi, na wote wanaohusika na chumba cha wagonjwa, wanapaswa kuwa wachangamfu, watulivu, na wajimiliki wenyewe. Hali yoyote ile ya kukurupuka au haraka-haraka, msisimko, au kuchanganyikiwa kunapaswa kuepukwa. Milango inapaswa kufunguliwa na kufungwa kwa uangalifu na nyumba nzima iwe kimya.”— Counsels on Health, 407.

[11]- IBADA BINAFSI NA MAOMBI

"Hatuwezi kupiga magoti kila wakati katika maombi, lakini njia ya kiti cha rehema huwa wazi kila wakati. Tunapojishughulisha na kazi hai, tunaweza kuomba msaada; Na tunaahidiwa na Yule ambaye hatatudanganya, "MTAPOKEA".... Mkristo anaweza na atapata muda wa kuomba...Wote wanaotamani sana wanaweza kupata mahali pa ushirika na Mungu, ambapo hakuna sikio linaloweza kusikia ila lile la Bwana, lililo wazi kwa kilio cha wasiojiweza, walio na huzuni, na wahitaji—kwa, naam Yule anayeona hata kuanguka kwa shomoro mdogo.”—Counsels on Health, 423-424.

“Ikiwa mihangaiko ya kazi itaruhusiwa kutuondoa kwenye kusudi letu la kumtafuta Bwana kila siku, tutafanya makosa makubwa zaidi; Tutapata hasara, kwa maana Bwana hatakuwa pamoja nasi; kwa kuwa tumefunga mlango ili asiweze kufikia roho zetu. Lakini ikiwa tunaomba huku mikono yetu inatumika, sikio la Mwokozi liko wazi kusikiliza maombi yetu. Ikiwa tumedhamiria kutotenganishwa na Chanzo cha nguvu zetu, Yesu atakuwa amedhamiria vile vile kuwa katika mkono wetu wa kuume ili kutusaidia, ili tusijipatie aibu mbele ya adui zetu. Neema ya Kristo inaweza kutimiza kwa ajili yetu yale ambayo juhudi zetu zote zitashindwa kufanya.”—Counsels on Health, 424.

[12]- IBADA YA HADHARA

“Hakuna nafsi inayoweza kufanikiwa bila muda wa kuomba, kuyachunguza Maandiko; na wote wanapaswa, kadiri inavyowezekana, wawe na nafasi la kuhudhuria ibada ya hadhara.”— Counsels on Health, 422.

“Mungu anakutunza mahali ambapo ni wajibu wako kuwa. Lakini hakikisha, kwa kadri iwezekanavyo, kwenda mahali ambapo sala inazoeleka kufanywa.”— Counsels on Health, 424.

[13]- UTUNZAJI YA SABATO

Jihadharini kuifanya Sabato kuwa ya kawaida katika maeneo ya vituo vya sanitarium na taasisi (Counsels on Health, 236 237).

Utunzaji wa Sabato katika Taasisi (Counsels on Health, 368, 422, 489, 491; Medical Ministry, 164, 214).

Ada/Fedha (malipo) zinazotokana na kazi iliyofanywa Sabato zinapaswa kuwekwa kwenye hazina ili kuwasaidia maskini (Medical Ministry, 216).

Wagonjwa hawapaswi kupuuzwa siku ya Sabato (Counsels on Health, 236).

“Mwokozi ametuonyesha kwa mfano Wake kwamba ni sahihi kutua mizigo ya mateso/maumivu siku hii; Lakini madaktari na wauguzi hawapaswi kufanya kazi zisizo za lazima. Matibabu ya kawaida, na upasuaji unaoweza kusubiri, unapaswa kuahirishwa hadi siku inayofuata.”—Medical Ministry 214.

Mlo siku ya Sabato (Counsels on Health, 489 491).

“Wale ambao, kwa sababu yoyote ile, wanalazimika kufanya kazi siku ya Sabato, daima wako hatarini; Wanahisi hasara, na kutokana na kufanya kazi za lazima, wanaanguka katika mazoea ya kufanya mambo siku ya Sabato ambayo si ya lazima. Hisia ya utakatifu Wake imepotea, na Amri Takatifu haina matokeo yoyote.”—Medical Ministry, 215.

[14]- WATENDEE WAGONJWA WOTE SAWA

Kamwe usiwaheshimu matajiri, na kuwadharau au kuwapuuza maskini (Counsels on Health, 228-230).

Alika madhehebu na makundi/madaraja yote kushiriki manufaa ya taasisi zetu za tiba. (Counsels on Health, 246).

"Wale ambao kwa kweli ndiyo hawahitaji msaada sana,ndio wana uwezekano mkubwa wa kupokea usikivu wetu zaidi. Lakini tunahitaji kuonyesha hekima ya pekee katika kushughulika na wale wanaoonekana wasumbufu, wanaoleta wengine maumivu kwa kutofikiria na kutojali.”—Medical Ministry, 209.

[15]- Juhudi za kuleta roho kwa Bwana

“Kuanzia kwa meneja hadi kwa mtendakazi mnyenyekevu zaidi, wote wanapaswa kuhisi kuwajibika kwa wale wasioongoka kati ya idadi yao wenyewe.”—Medical Ministry, 182.

Kunapaswa kuwa na juhudi za kila siku za wafanyakazi katika kuleta roho (Medical Ministry, 190-192, 194-197; Counsels on Health, 540).

Uwe taratibu kuhusu kuendeleza mafundisho mapya, tofauti, ya daraja la juu au magumu, na pengine yenye kuchukiza kwa wagonjwa (Counsels on Health, 245-246; Medical Ministry, 189).

13 – MADAKTARI

[1] – MADAKTARI WA KIUME NA WA KIKE

Madaktari wa kiume wanapaswa kufanya kazi na wagonjwa wa kiume, na madaktari wa kike wanapaswa kufanya kazi na wagonjwa wa kike (Counsels on Health, 363-365).

Kamwe daktari wa kiume hapaswi kuwa peke yake na mgonjwa wa kike (Counsels on Health, 364).

Katika kila taasisi ya tiba, wanawake wenye uzoefu, waliokomaa wanapaswa kutoa tiba kwa wanawake (Counsels on Health, 364).

Madaktari wanawake wanapaswa kushughulikia magonjwa ya uzazi-gynecology and obstetrics (ukunga na magonjwa ya kike) na magonjwa ya wanawake (Counsels on Health 365-366; Medical Ministry, 61).

Katika shule ya tiba, wanawake wanapaswa kufundishwa na wanawake (Counsels on Health, 366).

Wanawake kama madaktari wanapaswa kufanya kazi pamoja na wanandoa wanahitaji kushauriana pamoja kuhusu yale mambo magumu (Medical Ministry, 140).

[2] – UHARAKA KATIKA MIADI

Usikose miadi (ukiweka appointment itunze na uwahi) na usichelewe. Ikiwa huwezi kuwa huko, tuma daktari mwenza ambaye anapaswa kuelezea sababu ya kutokuwepo (Medical Ministry, 192-194; Counsels on Health, 363).

[3] - VIWANGO VYA TABIA NA MAADILI

"Daktari anapaswa kutawaliwa na hisia kali za viwango vya maadili, wakati wote na kila wakati. Ninazungumza kwa uwazi, kwa sababu najua kwamba ni wajibu wangu kufanya hivi. Huwezi kuwa mwenye maadili mazuri sana katika maneno yako au mwenye kujistahi na muungwana sana wakati unafanya uchunguzi wako kwa wagonjwa. Ukali, kuwa rafu/jeuri, kukosa uangalifu katika mambo nyeti, au kutochukua tahadhari na kukosa utulivu katika chumba cha upasuaji, au kando ya kitanda cha mwenye mtu mwenye tatizo, ni dhambi mbele ya Mungu; na

itasomeka kwa nguvu akilini mwa wagonjwa kuhusu daktari. Pasipo daktari kupenda kuhusiana na mgonjwa kwa usahihi wa maadili, na miiko inayofuatwa na Biblia na jumuiya, bila shaka atawashtua hata bila kujua, wagonjwa wanaochukulia mambo kwa unyeti zaidi, na wale wanaojistahi na wenye utamaduni uliosafishwa zaidi”—Medical Ministry, 149.

"Haipaswi hata kidogo kwa tabibu kuhusiana na mgonjwa au kumwendea kwa mazoea au kama jambo la kawaida (commonness). Matendo ya daktari yanagusa hisia zao na kuweka wazo; Toni za sauti yake, mwonekano wa uso wake, maneno anayozungumza, hupimwa na mgonjwa. Kila jambo au mjongeo wake huchunguzwa kikamilifu.”—Medical Ministry, 149.

[4] - MWAMBIE MGONJWA HALI YAKE

"Huna haki ya kujifungia ndani yako mwenyewe, na kutosema chochote kwa wagonjwa. Haupaswi kuwaweka wagonjwa kusubiri uamuzi wako katika kesi yao. Si sawa kuwasababishia mateso ya akili kwa kuchelewa kusiko lazima. Kila kesi inapaswa kupokea uangalizi wa haraka kwa zamu yake na kulingana na umuhimu wake..

“Nimeonyeshwa kwamba kasoro hii katika tabia yako imewafanya wanaume na wanawake kukulaani mioyoni mwao, na karibu kumtukana Mungu. Sasa kama nilifikiri hili halingeweza kusahihishwa, nisingeandika kama ninavyofanya. Ni wajibu wako kama daktari Mkristo kuelimisha mazoea na adabu na tabia zako uwapo chumbani mwa wagonjwa, kuwa mchangamfu na mwenye urafiki, kudhihirisha huruma ya upole, kuzungumza kwa uhuru juu ya mambo muhimu kwa wagonjwa wako, na ambayo yanakuja ndani ya nyanja ya utendaji wako wa kitaaluma. Unaweza kufikia kiwango cha juu katika utaalamu kwenye nyanja yako.”—Medical Ministry, 148.

Mfunulie mgonjwa Ukweli kulingana na hali—lakini sikuzote ikiwa kuna hatari ya kifo (Medical Ministry, 38).

Ukweli hauwezi kuambiwa kabisa kwa mgonjwa kila wakati, lakini usijaribu kupindisha (Medical Ministry, 38).

"Sihalalishi kwa mtu yeyote katika kufanya udanganyifu kwa mtu aliye kifoni. Kwa upole iwezekanavyo waambie ukweli kuhusiana na kesi yao (kama ninavyoamini), na kisha uwaelekeze kwa Yesu kama tumaini lao pekee.”—Medical Ministry, 148.

[5] - LAZIMA AWE MHUDUMU WA DHATI, ANAYEFANYA KAZI KAMA KRISTO ALIVYOFANYA

“Daktari Mkristo ni mhudumu wa hali ya juu. Yeye ni mmishenari. Wale ambao kwa ustadi wao na uaminifu wao, juhudi za dhati, kwa hekima kutoka kwa Mungu, wanaweza kupunguza maumivu ya mwili, hawa wanajiweka katika uhusiano kama huo kwa wagonjwa wao hivi kwamba wanaweza kuwaelekeza kwa Mponyaji wa nafsi, anayeweza kusema, dhambi zako zimesamehewa. ”—Medical Ministry, 147

“Wagonjwa hawapaswi kulazimishwa kusubiri wanapohitaji ushauri na kujipatia ahueni. Kamwe daktari hapaswi kupuuza wagonjwa wake. Anapaswa kuwa na uamuzi wa haraka, wa kupenya, na anapaswa kuweka mazingira rafiki ndani ya chumba cha wagonjwa. Hapaswi kuwa na ubaridi, anayeonyesha mawazo yake kwa watu kirahisi, au kusitasita, bali anapaswa kusitawisha sifa hizo ambazo huwa na ushawishi wa kutuliza kwa wanaoteseka. Wagonjwa wanataka zaidi ya sura nzuri; Wanataka maneno mazuri, yenye matumaini. Daktari anapaswa kuwa tayari kuwapa maneno ya kutia moyo kwa furaha, maneno yaliyosemwa kutoka moyoni kwa hekima, kuonyesha kwamba anaelewa kesi za wale walio chini ya uangalizi wake. Hilo litahamasisha utulivu na ujasiri, hata katika mahojiano ya kwanza.”— Medical Ministry, 193.

“Muda ambao umetumika katika kuwasiliana na Mungu, katika kutafuta msaada Wake kabla ya kufanya kazi ya kuwaokoa wale waliokuwa katika hali mbaya, umewaleta malaika upande wa daktari na wasaidizi wake. Umefanikiwa kulingana na vile ulivyomtumaini Mungu. Yeye Amekuwa kando yako kwa hakika kama Kristo alivyokuwa kando ya wale waliokuwa wakiteseka alipowatembelea hapa duniani.”—Medical Ministry, 34.

"Ikiwa mgonjwa ataondolewa maumivu, na kurejeshewa afya, yaani kutoka kifo hadi uzima, ana mwelekeo wa kumwabudu yule ambaye, anadhani, ameokoa maisha yake. Mara chache anafikiria kuwa ni Mungu Ndiye ambaye amefanya kazi hii kupitia mawakala Wake wa kibinadamu. Huu ndio wakati mwafaka kwa Shetani kuingia na kumwongoza tabibu kujiinua badala ya Kristo. Lakini ujue Yesu anasema, ‘Bila Mimi hamwezi kufanya lolote.’

“Unapaswa kumwongoza mgonjwa kumwona Yesu kama Tabibu wa mwili na roho. Ikiwa tabibu ana upendo wa Kristo moyoni mwake, atatumia ushawishi wake kumweka mganga Mkuu mbele ya yule anayeteseka. Anaweza kuelekeza mawazo, shukrani, na sifa, zimwendee Yule aliye Chanzo cha nguvu zote, rehema, na wema.”—Medical Ministry, 149-150.

SURA YA 10

VIWANGO VYA KUFANYA KAZI AMBAVYO VINAPASWA KUZINGATIWA

Mwongozo wa sifa na viwango vya "kitaaluma" vya umishenari wa tiba

1 - SIFA INAYOHITAJIKA ILI KUWA MMISHENARI WA TIBA INAWEZA TU KUTOKA KWA DAKTARI MKUU: YESU

"Ukweli wa wakati huu, ujumbe wa Malaika wa tatu, utatangazwa kwa kilio kikuu, tunapokaribia jaribio kubwa la mwisho. Jaribio hili lazima lije kwa makanisa kuhusiana na kazi ya ya Kweli ya umishenari wa tiba, kazi ambayo ndani yake kuna Tabibu Mkuu Mwenye kuweka chini mipango (Rx) na kuongoza katika yote inayotenda." -Manuscript dated 1900; Loma Linda Messages, 62.

2- YESU ANAWASTAHILISHA WANAFUNZI WAKE AMBAO WATAISHI NA KUFUNDISHA UTII WA SHERIA YAKE

Magonjwa, mateso, na kifo ni kazi ya nguvu pinzani. Shetani ndiye mharibifu; Mungu ni mrejeshaji. Maneno yaliyosemwa kwa Israeli ni Ukweli kwa leo kwa wale wanaorejeshewa afya ya kimwili au afya ya kiroho: Mimi Ndimi BWANA nikuponyaye."— Medical Ministry, 11.

"Nguvu hiyo hiyo inayoshikilia asili inafanya kazi pia ndani ya mwanadamu. Sheria kuu zile zile zinazoongoza sawa, nyota na atomi hudhibiti mkondo wa maisha ya mwanadamu0. Sheria zinazotawala hatua ya moyo, zinazodhibiti mtiririko wa mkondo wa uzima wa mwili, ni sheria za akili kuu ambazo zina mamlaka ya maamuzi ya roho. Kutoka Kwake, kila chenye uhai hutokea huko. Ni kwa njia ya mapatano na Yeye ndipo kunapatikana duru ya utendaji wa kweli. Kwa vitu vyote vya uumbaji Wake sharti ni moja,— maisha yanategemezwa kwa kupokea uzima kutoka kwa Mungu, uzima unaoendana na mapenzi ya Muumba. Kuvunja sheria Yake, ya kimwili, kiakili, au kiadili, ni kuweka nafsi yako nje ya mapatano na ulimwengu, kuanzisha mifarakano, machafuko, na uharibifu."—Medical Ministry, 10.

"Ni Mungu Ndiye ambaye ameweka utoaji/riziki na kwamba asili itende kazi ya kurejesha nguvu zilizochoka. Nguvu ni ya Mungu. Yeye Ndiye Daktari Mkuu." - Medical Ministry, 11-12.

"Wagonjwa wanapaswa kuponywa kupitia jitihada za pamoja za mwanadamu na Mungu. Kila karama, kila nguvu, ambayo Kristo aliwaahidi wanafunzi Wake, huwapa wale ambao watamtumikia kwa uaminifu."— Medical Ministry, 12.

Majaliwa ya Mungu yalikuwa yamemweka Yesu mahali alipokuwa, Naye alimtegemea Baba Yake wa mbinguni kwa mbinu na uwezo kutatua hitaji hilo. Tunapoletwa katika maeneo yenye shida na utata, twapaswa kumtegemea Mungu. Katika kila dharura twapaswa kutafuta msaada kutoka Kwake, ambaye ana rasilimali zisizo na ukomo chini ya amri Yake. —Ministry of Healing, 48-49.

"Hatuwezi kuponya. Hatuwezi kubadilisha hali ya ugonjwa wa mwili. Lakini ni sehemu yetu, kama wamishenari wa tiba, kama watendakazi pamoja na Mungu, kutumia fedha na njia ambazo ametoa. Kisha tunapaswa kuomba kwamba Mungu atabariki mawakala haya. —Medical Ministry, 13.

3- DIPLOMA YETU: UIDHINISHAJI WA MUNGU

Vijana wa kiume na wa kike, jikusanyieni maarifa mengi. Usisubiri hadi uchunguzi wa kibinadamu utamke kuwa wewe una uwezo wa kufanya kazi, lakini nenda kwenye barabara kuu na vichochoroni, na uanze kufanya kazi kwa ajili ya Mungu. Tumia kwa busara maarifa uliyonayo. Tumia uwezo wako kwa uaminifu,

ukitoa nuru ambayo Mungu amekupatia kwa ukarimu. Jifunze ubora wa kuwapatia wengine amani, nuru, Ukweli na baraka zingine nyingi za mbinguni. Piga hatua daima. Endelea kufikia juu na juu zaidi. Ni uwezo wa kuweka katika uwajibikaji nguvu za kiakili na kimwili, daima ukizingatia uhalisia milele katika fikra, hilo ndilo jambo lenye thamani sasa. Mtafute Bwana kwa bidii zaidi, ili uweze kutakaswa zaidi na zaidi, na kusafishwa na mtu mwenye utamaduni wa kiroho zaidi. Basi utakuwa na shahada yenye sifa ya ubora, kuzidi ile mtu yeyote anayoweza kuwa nayo—uthibitisho wa Mungu. — Shuhuda kwa Kanisa 7: 281.

4- SIFA ZETU: KUFUATA MFANO AMBAO YESU ALITUPA

“Kristo anayatambulisha maslahi Yake na yale ya ubinadamu. Kazi inayobeba sifa za Kiungu ni ile inayodhihirisha roho ya Yesu, ambayo inafunua upendo Wake, uangalifu Wake, huruma Yake katika kushughulika na akili za wanadamu. — Testimonies to Ministers, 184.

“Kuna kazi ya kufanywa katika miji yetu yote, na wale ambao bado wanafanya kazi na kutembea kwa unyenyekevu na Mungu, wakijitahidi kila siku kuwa washindi, watapata ushindi wa thamani siku baada ya siku. Kazi inayofanywa kwa unyenyekevu itabeba sifa za Bwana/Kiungu. Hebu tukimbilie na kujificha kwa Mungu. — Counsels on Health, 544.

Mungu anaweza kumtumia kila mtu kwa kadiri tu anavyoweza kuweka Roho Wake katika hekalu la roho. Kazi ile ambayo Yeye ataikubali ni ile kazi inayoakisi sura Yake. Wafuasi Wake wanapaswa kuibeba, kama vitambulisho vyao kwa ulimwengu, sifa zisizoweza kufutika au kusahulika, za kanuni Zake za kutokufa.— Ministry of Healing, 37.

Mwokozi aliishi katika dunia hii maisha ambayo upendo kwa Mungu utambidisha kila muumini wa kweli katika Kristo kuishi. Kwa kufuata mfano Wake katika kazi yetu ya umishenari wa tiba, tutaufunulia ulimwengu kwamba sifa zetu zinatoka juu; Kwamba kama wawakilishi wa ufalme wa mbinguni, tunatimiza Maneno ya Sala ya Bwana, ‘Ufalme wako uje' Tukiwa tumeunganishwa na Kristo katika Mungu, tutaufunulia ulimwengu kwamba kama vile Mungu alivyomchagua Mwanawe kuwa mwakilishi Wake duniani, ndivyo Kristo alivyotuchagua kuwakilisha tabia Yake.”—Medical Ministry, 23.

Inafurahisha kuona kwamba kazi ya umishenari wa tiba, iliyofanywa ipasavyo, ilitoa sifa za kazi ya Yesu akiwa hapa duniani. Ilitoa uthibitisho kwamba Yeye alikuwa Masihi, na ushahidi wa Uungu Wake. (Matt. 11:2-6; Ministry of Healing, 34-37).

5- HATI YETU YA KUFANYA KAZI: UTUME WA KRISTO

“Utume wa Injili ni Hati Kuu ya Umishenari ya Ufalme wa Kristo (Missionary charter).”—Acts of the Apostles, 28.

“Utume wa Kiungu hauhitaji marekebisho. Njia ya Kristo ya kuwasilisha Ukweli haiwezi kuboreshwa. Mwokozi aliwapa wanafunzi masomo ya vitendo, akiwafundisha jinsi ya kufanya kazi kwa njia ya kufanya nafsi kuwa na furaha katika ukweli. Yeye Aliwahurumia waliochoka, wale waliolemewa na mizigo, waliokandamizwa. Aliwalisha wenye njaa na kuwaponya wagonjwa. Daima alienda akitenda mema. — Welfare Ministry, 56.

“Tumefika wakati ambao kila mshiriki wa kanisa anapaswa kushikilia kazi ya umishenari ya tiba. Ulimwengu ni nyumba ya wakoma iliyojaa wagonjwa wa ugonjwa wa kimwili na kiroho. Kila mahali wanaangamia kwa kukosa maarifa ya Kweli yaliyowekezwa kwetu. Washiriki wa kanisa wanahitaji uamsho, ili kusudi watambue wajibu wao wa kutoa ukweli huu. Wale ambao wameangazwa na Ukweli wanapaswa kuwa wabeba nuru kwa ulimwengu. Kuificha nuru yetu kwa wakati huu ni kufanya makosa mabaya. Ujumbe kwa watu wa Mungu leo ni, “Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja, Na utukufu wa Bwana umekuzukia.” — Counsels on Health, 425.

“Watu wa Mungu wanapaswa kuwa wamishenari wa Kweli wa tiba. Wanapaswa kujifunza kuhudumia mahitaji ya nafsi na mwili. Wanapaswa kujua jinsi ya kutoa tiba rahisi ambazo hufanya mengi ili kupunguza maumivu na kuondoa magonjwa. Wanapaswa kufahamu kanuni za matengenezo ya afya, ili waweze kuwaonyesha wengine jinsi ya kutenda, kwa mazoea sahihi ya kula, kunywa, na kuvaa, magonjwa yanaweza kuzuiwa na afya kurejeshwa. Onyesho la thamani la kanuni za matengenezo ya afya litafanya mengi katika kuondoa chuki na ubaguzi dhidi ya kazi yetu ya kiinjilisti. Tabibu mkuu, mwanzilishi wa kazi ya umishenari wa tiba, atambariki kila mtu ambaye atasonga mbele kwa unyenyekevu na uaminifu, akitafuta kueneza Ukweli wa wakati huu. –Welfare Ministry, 127.

Upana wa kazi ya injili kwa umishenari wa tiba haueleweki. Kazi ya umishenari wa tiba inayotakiwa sasa ni ile iliyoainishwa katika agizo ambalo Kristo aliwapa wanafunzi Wake kabla tu ya kupaa Kwake. “Nimepewa mamlaka yote Mbinguni na duniani,” alisema Masihi. "Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi. siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” Mathayo 28:18-20 Maneno haya yanaonesha shamba letu na kazi yetu. Shamba letu ni ulimwengu; kazi yetu ni

utangazaji wa zile Kweli ambazo Kristo alikuja katika ulimwengu wetu kuzitangaza. — Shuhuda kwa Kanisa 8: 204; Counsels on Health, 509.

6- NGUVU NA MAMLAKA AMBAYO KWAYO TUNAFANYA KAZI: JINA LAKE MATENDO YA MITUME 3:6, 12, 16

Lakini Petro akasema, Mimi sina fedha, wala dhahabu, lakini nilicho nacho ndicho nikupacho. Kwa Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama uende. Hata Petro alipoyaona haya akawajibu wale watu, Enyi Waisraeli, mbona mnastaajabia haya, au mbona mnatukazia macho sisi, kana kwamba tumemfanya huyu aende kwa nguvu zetu sisi, au kwa utauwa wetu sisi? Na kwa imani katika Jina Lake, Jina Lake limemtia nguvu mtu huyu mnayemwona na kumjua; na imani ile iliyo Kwake Yeye imempatia huyu uzima huu mkamilifu mbele yenu ninyi nyote.

“Wanafunzi walipaswa kuendeleza kazi yao katika Jina la Kristo.”—Acts of the Apostles, 28.

“Wale wanaoenenda katika Jina la Bwana ni wajumbe Wake wa kuwapa watu wengi walio gizani na kwenye makosa habari njema ya wokovu kupitia Kristo katika kutii sheria ya Mungu.”— Colporteur Evangelism, 10-11.

“Siyo tu kwamba Ukweli unapaswa kuwasilishwa katika mikusanyiko ya hadhara; Kazi ya nyumba kwa nyumba inapaswa kufanywa. Hebu kazi hii iende mbele kwa Jina la Bwana. Wale wanaojihusisha nayo wana malaika wa mbinguni kama wasaidizi na wenzi wao.”— Evangelism, 490.

7- WENGINE WATATAMANI MAANDALIZI MAALUM YA KAZI HII

Kila mshiriki wa kanisa anapaswa kuwa mmishenari wa tiba, akifuata mfano wa huduma iliyotolewa na Yesu (Welfare Ministry, 56-81, 128, 116-118, 120-125, 125-127, 142; 7 Testimonies, 62, 63, 272; 5 Testimonies, 385-386; 6 Testimonies, 267, 289, 290-301; 8 Testimonies, 71-75, 168-169;

9 Testimonies, 82-83, 167-168; Counsels on Health, 425-426, 548; Desire of Ages, 640; Christ’s Object Lessons, 233-234; A Call to Medical Evangelism, 26-27. Soma sura, “Utume wa umishenari wa tiba,” kwa habari zaidi kuhusu hili. Kuna taarifa mbili ambazo zinatuambia kwamba baadhi "watahisi kuwa ni wajibu wao" (Medical Ministry, 69) kupata "maandalizi maalum" (Medical Ministry, 57) katika kazi ya kutoa tiba ili kufaulu mitihani inayohitajiki kwa kawaida, kuwapa haki/ruhusa ya kufanya mazoezi kama madaktari kitaaluma wa mara zote. Kuhusu jinsi maandalizi haya yatatolewa, tunaagizwa:

“Ikiwa kuna mahitaji ya kisheria yanayofanya iwe muhimu kwamba wanafunzi wa tiba wachukue kozi fulani ya maandalizi ya masomo, basi vyuo vyetu vifundishe masomo ya ziada yanayohitajika kwa njia inayolingana na elimu ya Kikristo . .

Wanapaswa kupanga kuwabeba wanafunzi wao hadi kufikia hatua ya mafunzo ya kifasihi na kisayansi ambayo ni muhimu.”— Loma Linda Messages, 172 (toleo lisilofupishwa, 775).

8- JIFUNZE KOZI YA MSINGI YA MASOMO

Kazi yetu kuu ni kuendeleza shule na madarasa mengi madogo ya wamishenari wa tiba ili kumsaidia kila mshiriki katika kujifunza mafundisho ya msingi katika mbinu rahisi za huduma ambazo Yesu ametuagiza tuzitumie badala ya kuendeleza vituo vichache vikubwa vya matibabu, kuzalisha vilivyo na sifa za kitaaluma. (Soma sura, “"Shule za Wamishenari wa tiba," kwa maelezo juu ya hili.)

Katika kazi ya shule dumisheni usahili (simplicity). Hakuna hoja yenye nguvu kama mafanikio yale yanavyoanzishwa katika usahili. Mnaweza kupata mafanikio katika elimu ya wanafunzi kama wamishenari wa tiba bila ya kuwa na shule ya utabibu inayoweza kuhitimisha waganga/matabibu wanaoweza kushindana na madaktari wa ulimwengu. Hebu wanafunzi wapewe elimu ya vitendo. Kadiri msivyozidi kutegemea mbinu za kielimu za kidunia ndivyo wanafunzi watakavyokuwa bora zaidi. Maelekezo maalum yanapaswa kutolewa katika sanaa ya kutibu wagonjwa bila kutumia dawa zenye sumu na kupatana na nuru ambayo Mungu ameitoa. Katika matibabu ya wagonjwa, dawa zenye sumu hazihitajiki kutumiwa. Wanafunzi wanapaswa kumaliza shule bila kuachana na kanuni za matengenezo ya afya au upendo wao kwa Mungu na uadilifu. — Shuhuda kwa Kanisa 9: 175.

“Vijana wetu hawapaswi kutegemea kabisa shule ambazo wanaambiwa, ‘Ikiwa ungependa kukamilisha kozi yako ya mafundisho, ni lazima uchukue somo hili, au somo lingine,’— masomo ambayo labda hayangekuwa na manufaa yoyote kwa wale ambao shauku yao pekee ni kuupa ulimwengu ujumbe wa Mungu wa afya na amani (hata masomo mengine ya tiba ya dunia, yana vipengele ambavyo hupingana na Biblia-mfano mesmerism, ayuverdic, yoga, hyponitsm, uaguzi nk). —Medical Ministry, 75.

Elimu inayokidhi viwango vya ulimwengu inapaswa kuthaminiwa kwa udogo zaidi na zaidi na wale wanaotafuta kwa ufanisi katika kuifanya kazi ya kimishenari wa tiba ikipatana na kazi ya ujumbe wa malaika wa tatu. Wanapaswa kuelimishwa

kutoka katika mtazamo wa dhamiri, na, kwa uangalifu na kwa uaminifu wafuate njia sahihi katika matibabu yao ya wagonjwa, njia hizi zitakuja kupendwa kuliko njia ambazo wengi wamezizoea, ambazo zinadai matumizi ya dawa zenye sumu. — Shuhuda kwa Kanisa 9: 175.

9- HATUPASWI KUSHUSHA VIWANGO TULIVYOPEWA - ILI KUKIDHI MAHITAJI YA ELIMU YA ULIMWENGU

“Je, tuwakilishe mbele ya ulimwengu kwamba ni lazima madaktari wetu wafuate mfano wa ulimwengu kabla ya kuwa na sifa za kuwa madaktari wenye mafanikio? Hili ndilo swali ambalo sasa linajaribu imani ya baadhi ya ndugu zetu. Yeyote miongoni mwa ndugu zetu asimkosee Bwana kwa kutetea mbele ya makusanyiko ya walimwengu wazo ya kwamba tunahitaji kupata elimu ya juu kutoka kwa wasioamini kuliko ile iliyotajwa na Bwana. “Uwakilishi wa Mwalimu Mkuu unachukuliwa kuwa ufunuo wa kutosha. Wale walio katika safu zetu wanaohitimu kuwa madaktari wanapaswa kupokea tu elimu kama hiyo ambayo inapatana na Kweli hizi za Bwana/Kiungu….

"Sina neno la kusema katika kuunga mkono maoni ya ulimwengu ya elimu ya juu katika shule yoyote ambayo tutapanga kwa mafunzo ya madaktari." —Medical Ministry, 62.

“Kuna wale ambao watakupendekezea kwamba ili kufanikiwa katika taaluma yako lazima uwe mtu wa sera . . Kanuni ya sera ni ile ambayo hakika itasababisha matatizo. Yule anayeona kibali cha wanadamu kuwa bora zaidi kuliko kibali cha Mungu ataanguka chini ya jaribu la kuziangusha kanuni kwa ajili ya kupata faida au kutambuliwa na ulimwengu. Hivyo uaminifu kwa Mungu unaangushwa au kutolewa dhabihu kila mara. Ukweli, Ukweli wa Mungu, lazima utunzwe na kuthaminiwa katika nafsi na kushikiliwa kwa nguvu za mbinguni, la sivyo nguvu za Shetani zitaipokonya kutoka kwako.”— Medical Ministry 71.

"Usiache kamwe kiwango cha kweli, ingawa kung'ang'ania kwake kutakufanya kuwa ombaomba. Mungu ameweka kiwango cha juu cha haki. Yeye Amefanya tofauti iliyo wazi kati ya hekima ya kibinadamu na ya Kiungu. Wote wanaofanya kazi kwa upande wa Kristo lazima wafanye kazi ili kuokoa, na sio kuharibu. Sera ya kidunia haipaswi kuwa sera ya watumishi wa Mungu. Mamlaka ya Kiungu yanapaswa kutambuliwa. Kanisa duniani linapaswa kuwa mwakilishi wa kanuni za mbinguni. Katikati ya muungano wa kutisha wa dhuluma, udanganyifu, wizi/ujambazi, na uhalifu linapaswa kuangaza kwa nuru kutoka juu. Katika haki ya Kristo litasimama dhidi ya uasi uliopo.” ——Medical Ministry 132, 133.

“Lazima tuwe na wakufunzi wa tiba ambao watafundisha sayansi ya uponyaji bila kutumia dawa zenye sumu . . Tunapaswa kuandaa kundi la watendakazi ambao watafuata mbinu za Kristo.”—Medical Ministry, 75.

"Nimeagizwa kusema kwamba katika kazi yetu ya elimu pasiwe na maelewano ili kufikia viwango vya ulimwengu. Watu wanaoshika amri ya Mungu hawapaswi kuungana na ulimwengu, kubeba kazi mbalimbali kulingana na mipango na hekima ya kidunia.

“Watu wetu sasa wanajaribiwa kama watapata hekima yao kutoka kwa mwalimu Mkuu zaidi ambaye ulimwengu uliwahi kumjua, au kumtafuta mungu wa Ekroni. Hebu tuamue kwamba hatutafungwa kwa kiasi kikubwa kama uzi unavyojifungafunga, kwenye sera za elimu za wale wasioitambua sauti ya Mungu, na ambao hawatasikiliza amri Zake.”—Medical Ministry 61-62.

“Si salama kuwaamini madaktari ambao hawana hofu ya Mungu mbele yao. Bila ushawishi wa neema ya Mwenyezi Mungu, mioyo ya wanadamu ‘ni ya udanganyifu juu ya vitu vyote, na ni waovu sana.’ Kujitukuza-nafsi ni lengo lao. Chini ya taaluma ya udaktari, ni maovu gani yametendwa, ni udanganyifu gani uliotegemezwa!”— Counsels on Health, 456.

“Zaidi ya hayo, mafundisho ya madaktari hao yanaendelea kuongoza mbali na kanuni ambazo Mungu ametupa kuhusu afya, hasa kuhusu suala la lishe. Wanasema hatuishi kama tunavyopaswa, na kuagiza (Rx) mabadiliko ambayo ni kinyume na nuru ambayo Mungu ametuma. Ndugu zangu, Bwana awezaje kufanya baraka Zake zitulie tunapokuwa tunaenda moja kwa moja kwenye ardhi ya adui.”—Counsels on Health, 456-457.

“Mungu amewapa watu hawa nuru kuu, ila hatujawekwa nje ya uwezo wa majaribu. Ni nani kati yetu anayetafuta msaada kutoka kwa miungu ya Ekroni?”—Counsels on Health, 457.

“Kuna hatari katika kuondoka hata kidogo katika maagizo ya Bwana. Tunapokengeuka kutoka kwenye njia iliyo wazi ya wajibu, msururu wa hali utatokea ambao unaonekana kutozuilika kutuvuta mbali zaidi na zaidi kutoka kwenye Ukweli/haki na kile kilicho sahihi. Mahusiano ya karibu, na yasiyo ya lazima na wale ambao hawamheshimu Mungu yatatushawishi kufanya makosa tunayoyajua. Hofu ya kuwaudhi marafiki wa kidunia itatuzuia kutoa shukrani zetu kwa Mungu, au kukiri utegemezi wetu Kwake.

“Lazima tuwe karibu na Neno la Mungu. Tunahitaji maonyo ya Neno na kutiwa moyo, vitisho na ahadi zake. Tunahitaji mfano kamili unaotolewa tu katika

maisha na tabia ya Mwokozi wetu. Malaika wa Mungu watawahifadhi watu Wake, pale wanapotembea katika njia ya wajibu; Lakini hakuna hakikisho la ulinzi kama huo kwa wale wanaojitosa kwa makusudi juu ya ardhi ya Shetani. Wakala wa mdanganyifu mkuu atasema na kufanya lolote ili kupata kitu chake." ——Counsels on Health, 458-459.

"Adui ametumia mnyororo wa utegemezi kuwavuta watu pamoja. Wameungana kuharibu sura ya Mungu ndani ya mwanadamu, ili kuipinga na kuipotosha injili kwa kupotosha kanuni Zake. Wanawakilishwa katika Neno la Mungu kuwa wamefungwa katika matita ili kuchomwa moto. Shetani anaunganisha majeshi yake kwa ajili ya uasi na uovu."— Counsels on Health, 525.

"Hebu mzigo wote wa nafsi na uwe vile Kristo alivyokuwa katika kazi Yake. Hatupaswi kufanya maelewano na mazoea na utendaji wa ulimwengu. Tunapaswa kusimama juu ya jukwaa la Ukweli wa milele, ukweli safi, usioghoshiwa. Katika hili tunaweza kuchukuliwa kuwa wa kipekee, lakini hii ndiyo kura ya wote wanaomfanya Kristo kuwa sehemu yao. Kila mtendakazi katika safu za umishenari wa tiba anapaswa kufanya kazi hiyo kuwa ya mafanikio kwa kuishi katika uhusiano na mtendakazi Mkuu."— Medical Ministry, 161.

"Tangu sasa na kuendelea tunapaswa kusimama kama watu tofauti kabisa na wa kipekee, wasio na sera zote za kidunia, wala muungano wa pamoja na wale ambao hawana hekima ya kutambua madai ya Mungu, yaliyowekwa wazi katika sheria Yake."—Medical Ministry, 329.

"Hakuna mstari hata mmoja katika imani yetu ambao unapaswa kutufanya tulivyo, unaopaswa kudhoofishwa. Tuna alama za zamani za Ukweli, uzoefu, na wajibu; Na tunapaswa kusimama imara katika kutetea kanuni zetu, katika mtazamo kamili wa ulimwengu. Tukiwa na mioyo iliyojaa shauku, kujali na utii, tunapaswa kutoa mwaliko kwa wale walio katika barabara kuu na vinjia vidogo kupita. Kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kufanywa."— Counsels on Health, 521-522.

"Hakupaswi kuwa na mabadiliko katika sifa za jumla za kazi ya Mungu. Hizi zinapaswa kujitokeza wazi na dhahiri kama vile unabii ulivyofanya. Hatupaswi kuingia katika muungano wowote na ulimwengu, tukidhani kwamba kwa kufanya hivyo tungeweza kutimiza mengi zaidi."— Counsels on Health, 521.

"Baadhi ya maswali yameulizwa kuhusu uhusiano wetu na sheria za madaktari. Tunahitaji kusonga kwa uelewa, kwa kuwa adui angefurahi kuweka kazi yetu ili madaktari wetu wawe na ushawishi mdogo tu. Baadhi ya watu hawatendi kwa

kumcha Mungu, na wanaweza kutafuta kutuingiza kwenye matatizo kwa kutuwekea shingoni mwetu nira ambazo hatutaweza kukubali kuzibeba. Hatuwezi kujisalimisha kwa masharti yatakayokukiuka ya kanuni; Kwa maana hii ingehatarisha wokovu wa nafsi. — Medical Ministry, 84.

“Ungana na wale wanaomheshimu Mungu kwa kushika amri Zake. Ikiwa pendekezo litatoka kwa watu wetu kwamba watenda-kazi wetu watafute mafanikio kwa kukiri kuwa elimu ambayo ulimwengu hutoa ni muhimu, kwa hakika hili ni kunasema kwamba ushawishi ambao ulimwengu hutoa ni bora kuliko ule ambao Mungu hutoa. Mungu atavunjiwa heshima kwa njia hiyo. Mungu ana ujuzi kamili wa imani na tumaini na ujasiri ambao watu Wake wanaodai kuwa nao katika usimamizi Wake.”—Medical Ministry, 84-85.

"Kuna hatari ya endelevu miongoni mwa watu wetu kwamba wale wanaojishughulisha na kazi katika shule zetu na vituo vyetu vya afya wataendekeza wazo kwamba lazima wapatane na ulimwengu, wasome mambo ambayo ulimwengu unasoma, na kufahamu mambo ambayo ulimwengu unayafahamu. Hii ni moja ya makosa makubwa ambayo yanaweza kufanywa. Tutafanya makosa makubwa isipokuwa pale tu, tutakapozingatia sana kuchunguza Neno.” —Fundamentals of Christian Education, 534.

“Hatutaki hata moja ya aina hiyo ya ‘elimu ya juu’ ambayo itatuweka katika hali ambayo sifa haitakuwa kwa Bwana Mungu wa Israeli, bali kwa Mungu wa Ekroni. Bwana anapanga kwamba tusimame kama watu tofauti, hivyo tuliounganishwa Naye kabisa, ili Yeye aweze kufanya kazi nasi. Hebu madaktari wetu watambue kwamba wanapaswa kumtegemea kabisa Mungu wa Kweli.” —Loma Linda Messages, 173.

“Katika kitabu cha Kellog, ‘Hekalu Hai,’ kunaonyeshwa alfa ya uzushi wa kuogofya na kufisha. Omega itafuata, na itapokelewa na wale ambao hawako tayari kutii onyo ambalo Mungu ametoa.

“Madaktari wetu, walio na majukumu muhimu, wanapaswa kuwa na utambuzi thabiti wa kiroho. Wanapaswa kusimama daima katika kituo chao cha ulinzi. Hatari ambazo hatuzitambui sasa hivi karibuni zitatpasukia, na ninatamani sana kwamba wasidanganyike. Nina hamu kubwa ya kuwaona wakisimama huru katika Bwana. Ninaomba kwamba wawe na moyo wa ujasiri katika kusimama imara kwa ajili ya Ukweli kama ulivyo ndani ya Yesu, wakishikilia thabiti mwanzo wa ujasiri wao hadi mwisho.”—Series B, No 2, 50.

“Jifunze Biblia zaidi, na nadharia za udugu wa kitiba hupungua (vyama vya medical fratenity), na utakuwa na afya bora zaidi ya kiroho. Akili yako itakuwa safi na yenye nguvu zaidi. Mengi ambayo yanakubaliwa katika kozi ya tiba sio lazima kabisa. Wale wanaochukua mafunzo ya tiba hutumia muda mwingi katika kujifunza kile ambacho ni takataka tu. Nadharia nyingi wanazojifunza zinaweza kulinganishwa kwa thamani na mapokeo, semi na kanuni zinazofundishwa na Waandishi na Mafarisayo. Mengi ya mambo tata ambayo wanapaswa kuyajua, ni jeraha akilini mwao.””—Loma Linda Messages, 190.

“Hakuna hata moja ya shule za udaktari zinazosifiwa sana ulimwenguni huu, iliyoidhinishwa katika mahakama za juu, wala hizo hazijabeba maandishi na uidhinishaji wa mbinguni. Huna haki ya kuitetea au kuiuza shule moja juu ya nyingine, kana kwamba ndiyo pekee inayostahili kuheshimiwa. Wale wanaopendekeza shule moja ya dawa na kulaani kwa uchungu nyingine wanachochewa na usongo ambao hauendani na maarifa. Kwa fahari na kiburi cha Kifarisayo baadhi ya watu huwadharau wengine ambao hawajapata shahada ya elimu kutoka kwa kile kinachoitwa shule yenye viwango vya juu. Haya yote yanathibitisha kwamba hawawezi kujinyenyekeza kwenye msalaba wa Kalvari. Roho hii haitakubaliwa kamwe mbinguni; Wala watu wanaoithamini hawatasikia ‘vyema mtumishi mwema, umekuwa mwaminifu kwa madogo…….’ Nimezungumza waziwazi kuhusiana na hisia zako kuhusu mbinu za utendaji taaluma ya tiba. Baadhi yenu mmekuwa na bidii katika kuinua kile ambacho shule yenu ilitetea kana kwamba Bwana alikuwa ametaja njia hiyohiyo na ndiyo pekee aliyoruhusiwa. Utumiaji wa dawa zenye sumu umesababisha madhara zaidi kuliko yale mazuri (dawa za famasia), na endapo madaktari wetu wanaodai kuamini Ukweli wataacha kabisa karibia dawa zote zenye sumu na kufanya mazoezi ya uaminifu katika njia za usafi, kwa kutumia tiba za asili, mafanikio makubwa zaidi yangehudhuria juhudi zao. Hakuna haja kwa namna yoyote ile kusifia na kuzitukuza njia ambazo dawa (drugs) zinavyotumiwa na kupewa kwa wagonjwa. Najua ninazungumza nini. Ndugu katika taaluma ya udaktari, nawasihi mfikirie kwa uwazi na kuweka mbali mambo ya kitoto. Bwana hafurahishwi na mtazamo wako kwa wale ambao wamehitimu katika kile wewe unachokiita shule duni. Yeye Hakubaliani na roho iliyokuchochea. Mungu atatuhukumu sisi kwa jinsi tulivyopaswa kuwa, kile tulichopaswa kufanya kama tungekuwa watoto watiifu. Hatuwezi kuepuka matokeo ya dhambi za kutotenda au kutenda (ommission/commission) na makosa yetu ingawa hatuwezi kuyaona au kukadiria matokeo yake.”—Taken from the Paulson Collection of Testimonies, titled “Extracts on Medical Work,” pages 3, 6, 8, 10, 16, 19, 21, 23.

“Bwana ametuonyesha uovu wa kutegemea nguvu za mashirika ya kidunia. Ametuagiza kwamba utume wa umishenari wa tiba, umepokelewa na mamlaka ya juu kabisa; Yeye Anatutaka tuelewe kwamba ni kosa kuchukulia elimu inayotolewa na madaktari wanaokataa mamlaka ya Kristo kuwa ndiyo ya muhimu na ya juu zaidi, kuliko ile ya Tabibu mkuu zaidi aliyewahi kuishi duniani. Hatupaswi kukubali na kufuata maoni ya watu wanaokataa kumtambua Mungu kama Mwalimu wao, lakini wanaojifunza juu ya wanadamu, na wanaongozwa na sheria na masharti yaliyowekwa na mwanadamu.

“Wakati wa usiku wa Aprili 26 (1910) mambo mengi yalifunguliwa mbele yangu. Nilionyeshwa kwamba sasa kwa maana ya pekee sisi kama watu tunapaswa kuongozwa na mafundisho ya Mwenyezi Mungu. Wale wanaotaka kujipatia stahiki kwa ajili ya kazi ya umishenari wa tiba wanapaswa kuogopa kujiweka chini ya usimamizi/mwongozo wa madaktari wa kidunia, kuzinywa hisia zao na chuki za kipekee, na kujifunza kueleza mawazo na maoni ya hao madaktari wa kidunia. Hawapaswi kutegemea ushawishi wa walimu wa kidunia. Wanapaswa ‘kumtazama Yesu, Mwanzilishi na mkamilishaji wa imani yetu.’

"Sio lazima kwamba wamishenari wetu wa tiba wafuate njia bainishi iliyowekwa na madaktari wa ulimwengu kwa kinagaubaga. Hawana haja ya kutoa madawa ya famasia (drugs) kwa wagonjwa. Hawana haja ya kuyafuata madawa ya famasia (drugs) katika kutibu ili kuwa na ushawishi katika kazi zao. ……. Wakiwa wameunganishwa na Mwalimu wa Kiungu/mbinguni, wataelewa kwamba utegemezi wao uko juu ya Mungu, na si juu ya watu wanaojiita, wenye hekima wa ulimwengu. “Baadhi ya wamishenari wetu wa tiba wamefikiri kwamba mafunzo ya tiba kulingana na mipango ya shule za kidunia ni muhimu kwa mafanikio yao. Kwa wale ambao wamefikiri kwamba njia pekee ya mafanikio ni kwa kufundishwa na watu wa kidunia, na kwa kufuata njia ambayo imeidhinishwa na watu wa kidunia, naweza kusema, weka mbali mawazo hayo. Hili ni kosa ambalo linapaswa kusahihishwa. Ni jambo la hatari kuleta katika kazi ya Mungu, roho ambayo Neno la Mungu haliwezi kuidhinisha. Kuna haja kwa madaktari na kwa walimu kuwa na mawazo mapya, uelewa mpya wa kanuni ambazo lazima zitaratibu kazi ya tiba. Elimu inapaswa kutolewa ambayo inapatana kabisa na mafundisho ya Neno la Mungu.

“Kuna ukosefu wa imani katika uwezo wa Mungu unaowaongoza madaktari wetu kuegemea sana kwenye mkono wa sheria, na kuamini kwa kutegemea mno, ushawishi wa nguvu za kidunia . . Kristo alikuwa Tabibu Mkuu zaidi ambaye ulimwengu umewahi kumjua; Moyo Wake daima uliguswa na kilio cha binadamu.

Yeye Anahitaji kufanya kazi kwa wale ambao hawataweka utegemezi wao juu ya nguvu za kidunia.

“Mmishenari wa kweli wa tiba atakuwa na hekima katika kutoa tiba kwa wagonjwa, akitumia dawa ambazo asili hutoa. Na kisha atamtazama Kristo kama mponyaji wa kweli wa magonjwa. Kanuni za matengenezo ya afya zinazoletwa katika maisha ya mgonjwa, matumizi ya tiba za asili, na ushirikiano wa mawakala wa Bwama juu ya mateso, zitaleta mafanikio. .

“Wakati utakuja ambapo wamishenari wa tiba wa madhehebu mengine watakuwa na husuda na wivu kwa ushawishi unaotolewa na Waadventista Wasabato wanaofanya kazi katika mistari hii.”—Loma Linda Messages, 545.

10 - HATUPASWI KUHATARISHA VIWANGO TULIVYOPEWA - ILI KUPATA KIBALI AU USHAWISHI (MVUTO)

“Hatupaswi kupotosha kile tunachokiri kuamini ili kupata kibali.”—Medical Ministry, 127.

“Mwanzoni kabisa mwa kipindi cha injili, Masihi alifundisha kanisa Lake kutotegemea cheo na fahari ya kilimwengu, bali juu ya nguvu za imani na utii. Kibali cha Mungu kina thamani kubwa kuliko dhahabu na fedha. Nguvu ya Roho Wake ina thamani isiyokadirika.” — Counsels on Health, 226.

“Kama watu waliochaguliwa na Mungu, hatuwezi kuiga mazoea, desturi, kaida, mila, mapokeo au mitindo ya ulimwengu. Hatujaachwa gizani, kwa mfano wa mifano ya kidunia, na kutegemea sura ya nje kwa mafanikio. Bwana ametuambia nguvu zetu zinatoka wapi. Zakaria 4:6 Hili ndilo Neno la BWANA kwa Zerubabeli, kusema, Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa Roho Yangu, asema BWANA wa majeshi. —Counsels on Health, 274.

"Madaktari katika vituo vyetu vya afya hawana kina, na akili mahiri katika utendaji wao, wanafanya mambo kwa juu juu tu wakati ambao wanapaswa kuwa na kina katika utendaji wa taaluma yao. Wanaamua kutumia dawa za famasia (drugs) wakati ujuzi na stadi ya taaluma yao ingepasa kuwafundisha njia bora zaidi. Je, ninyi madaktari hamjui kwamba maisha yamepotea ambayo yangeokolewa ikiwa dawa hizo za famasia hazingetumiwa? Kama sheria, dawa zinapokuwa hazitumiki mara kwa mara ndivyo mgonjwa atafanikiwa na kunawiri zaidi. Nilifikiri suala la kutumia dawa za famasia (drugs) lilikuwa limetatuliwa kwa ajili yetu miaka iliyopita kwa ushuhuda wa Roho wa Mungu, lakini onyo la Bwana halijazingatiwa. Naona hata aibu na kusikitishwa na jambo hili, na ninawaambia kwamba matengenezo yaliyoamuliwa lazima yafanyike. Madaktari

katika vituo vya afya wanaiacha mbali nuru ambayo Bwana ametoa kuhusu matumizi ya dawa za famasia (drugs).

“Ulimwengu unaonekana kupendezwa na hata kuidhinisha katika baadhi ya mbinu na mawazo yetu; Lakini hatupaswi kuruhusu mfano wa ulimwengu utughilibu. Hatupaswi kutegemea kibali cha kibinadamu au matamanio ya mafanikio. Kama Bwana Mwenye hekima alivyopanga, Ukweli huu umetutoa nje ya machimbo ya ulimwengu kuwa watu wa kipekee wa Mungu, na hatuwezi kumudu kujifananisha na ulimwengu. Hatuwezi kuafikiana kudondosha kanuni zetu za Ukweli hata sentimenta moja, ili tu kupata kibali na ufadhili wa ulimwengu.”— Extracts on Medical Work, 3, 6, 8, 10, 16, 19, 21, 23.

11- HATUPASWI KUSHIRIKIANA NA, KUUNGANA, AU KUJIUNGA NA SHIRIKA LOLOTE LA KIDUNIA, CHAMA, AU MUUNGANO WA KIKAZI.

Sasa tunapaswa kutumia uwezo wetu wote tuliokabidhiwa ili kutoa ujumbe wa mwisho wa onyo kwa ulimwengu. Katika kazi hii tunapaswa kuhifadhi upekee wetu na utambulisho wetu. Hatupaswi kuungana na vyama vya siri au na vyama vya wafanyikazi (secret societies or trade unions). Tunapaswa kusimama huru kwa Mungu, tukimtazama Kristo kila mara kwa maelekezo. Harakati zetu zote zinapaswa kufanywa kwa utambuzi wa umuhimu wa kazi inayopaswa kutimizwa kwa ajili ya Mungu. — Shuhuda kwa Kanisa 7: 84.

“Hatupaswi kuingia katika muungano au ubia wowote na wale wasiompenda au kumcha Mungu.”— Counsels on Health, 300.

“Bwana anawajaribu watu Wake ili kuona ni nani atakayekuwa mwaminifu kwa kanuni za Ukweli Wake. Kazi yetu ni kutangaza kwa ulimwengu ujumbe wa malaika wa kwanza, wa pili na wa tatu. Katika kutekeleza majukumu yetu hatupaswi kudharau wala kuwaogopa maadui zetu. Kujifunga wenyewe kwa mikataba na wale wasio wa imani yetu haipo kwenye utaratibu wa Mungu. Tunapaswa kuwatendea kwa fadhili na adabu wale wanaokataa kuwa waaminifu kwa Mungu, lakini hatupaswi kamwe kuungana nao katika ushauri kuhusu masilahi muhimu ya kazi Yake Bwana. Kamwe, kamwe hatupaswi kuungana na dunia katika ushauri wake kuhusu masuala nyeti na muhimu ya kazi ya Mungu. Tunapaswa kumtegemea Mungu kikamilifu na kujongea kwa uthabiti, tukielekea mbele. Tukifanya kazi Yake bila ubinafsi au uchoyo, tukimtegemea Yeye kwa unyenyekevu, na kuendana na majaliwa Yake, na yote yale yanayohusu maisha yetu ya sasa na ya mbeleni, tukiushikilia ujasiri wetu kwa uthabiti mpaka mwisho, na tukikumbuka kwamba tunapokea baraka za mbinguni, siyo kwa sababu ya kustahili kwetu, bali kwa sababu ya kustahili na sifa za Kristo, na kwamba

kumkubali Yeye kwa njia ya imani katika Yeye na neema ya Mungu iliyosheheni, ndiyo jambo lililo bora kabisa kwa kila mwanadamu." Counsels on Health, 238

Watu wameungana ili kumpinga Bwana wa majeshi. Mashirikisho haya yataendelea hadi Kristo atakapoondoka katika mahali Pake pa maombezi kwa ajili ya watu Wake mbele ya kiti cha rehema na kuvaa mavazi ya kisasi. Mawakala wa kishetani wako katika kila mji, wanashughulika na kuwaandaa watu katika makundi wale ambao wako kinyume na sheria ya Mungu. Watu waliokiri kuwa watakatifu na wale wanaokiri kutokuamini wanachukua wanachagua kwenda upande wa makundi haya. Huu sio wakati wa watu wa Mungu kuwa wanyonge. Hatutathubutu kuacha mkao wa tahadhari hata kwa wakati mmoja. — Shuhuda kwa Kanisa 8: 42.

"Vyama vya wafanyakazi vitakuwa mojawapo ya mawakala ambayo yataleta juu ya dunia hii wakati wa taabu kuu ambayo haijawahi kutokea tangu ulimwengu uanze."— Country Living, 10.

"Kazi ya watu wa Mungu ni kujiandaa kwa ajili ya matukio ya wakati ujao, ambayo hivi karibuni yatawajia kwa nguvu ya upofu. Katika ulimwengu, ukiritimba mkubwa utaundwa. Wanadamu watajifunga pamoja katika miungano ambayo itawafunga kwenye vifungo vya adui." Watu wachache wataungana ili kujitwalia fedha zote zinazopatikana katika maeneo fulani ya biashara. Vyama vya wafanyakazi vitaundwa, na wale wanaokataa kujiunga na vyama hivi watakuwa watu waliowekewa alama."—Country Living, 10.

"Vyama vya kibiashara na mashirika ya ulimwenguni ni mtego. Jieupushe navyo, na kaa mbali navyo, ndugu, usiwe na mahusiano yoyote na hivi. Kwa sababu ya vyama hivi vya kibiashara na mashirika, hivi karibuni itakuwa vigumu sana kwa taasisi zetu kuendeleza kazi zao mijini." -Country Living, 10.

Watu wanatafuta kuwaleta wale wanaojihusisha katika biashara tofauti chini ya utumwa wa vyama fulani vya wafanyakazi. Huu sio mpango wa Mungu, bali mpango wa mamlaka ambayo hatupaswi kuukubali. Neno la Mungu linatimizwa; waovu wanajifunga mafungu-mafungu tayari kwa kuchomwa moto. — Shuhuda kwa Kanisa 7: 84.

"Wale wanaodai kuwa ni watoto wa Mungu kwa vyovyote vile hawatafungamana na vyama vya wafanyakazi ambavyo vimeundwa au vitaundwa. Hii Bwana anakataza. Je, wale wanaosoma unabii hawawezi kuona na kuelewa yaliyo mbele yetu?"— Country Living, 12.

“Ni wakati wa watu wa Mungu, wale wanaovaa ishara ya ufalme Wake, na ambao mamlaka yao yanatokana na ‘Imeandikwa,’ kufanya kazi. Ulimwengu ni uwanja wa kazi yetu, na tunapaswa kujitahidi kutoa ujumbe wa mwisho wa rehema kwa ulimwengu. Kila tendo letu linatazamwa kwa macho ya wivu [na wale wasio wa imani yetu]. Jihadharini kama matabibu. Unaweza kumtumikia Bwana katika nafasi yako kwa kufanya kazi na mbinu mpya na kutupa dawa. Kama wanamatengenezo tunapaswa kurekebisha mazoea ya tiba, kwa kutoa elimu inayoelekeza kwenye nuru. Kazi yetu inapaswa kufanywa huku tukimtambua Mungu kwa ukamilifu.”— Medical Ministry, 125.

“Bwana ametuonyesha uovu wa kutegemea nguvu za mashirika ya kidunia. Yeye Ametuagiza kwamba utume wa umishenari wa tiba umetoka kwa mamlaka ya juu kabisa na upokelewe hivyo; Yeye Anatutaka tuelewe kwamba ni kosa kuchukulia kuwa elimu inayotolewa na madaktari wa dunia wanaokataa mamlaka ya Kristo ndiyo muhimu zaidi, kuliko na Yule Tabibu mkuu zaidi aliyewahi kuishi duniani. —Medical Ministry, 206-207.

“Sasa ni lazima tutumie uwezo wetu tuliokabidhiwa katika kutoa ujumbe wa mwisho wa kuuonya ulimwengu. Katika kazi hii tunapaswa kutunza utambulisho wetu na upekee wetu. Hatupaswi kuungana na mashirika ya siri au jumuiya za kibiashara. Hatuna budi kusimama tukiwa huru katika Mungu, daima tukimwangalia Kristo kutuelekeza. Hatua zetu zote hazina budi kufanywa kwa utambuzi wa umuhimu wa kazi inayopaswa kukamilishwa kwa ajili ya Mungu.” Counsels on Health, 273.

“Kisha wazo hilo likapata kibali kwamba kazi ya umishenari wa tiba ingekuwa ya juu sana ikiwa taasisi zetu zote za tiba na masilahi mengine ya umishenari wa tiba yangefungwa chini ya udhibiti wa chama cha tiba huko Battle Creek.

"Niliambiwa lazima ninyanyue sauti yangu kwa kuonya dhidi ya hili. Hatukupaswa kuwa chini ya udhibiti wa watu. Hatukupaswa kuongozwa na watu wanaotaka neno lao liwe nguvu ya kutawala. Ukuzaji wa hamu ya kudhibiti umewekwa alama sana, na Mungu alituma onyo baada ya onyo, na kukataza uimarishaji. Yeye Alituonya dhidi ya kujifunga wenyewe ili kutimiza makubaliano fulani ambayo yangewasilishwa na watu wanaofanya kazi ili kudhibiti mienendo ya ndugu zao.

“Nuru imetolewa kwangu kwamba kuna karatasi ambazo zimebuniwa na kuandikwa na wanasheria ambazo zinapofusha macho ya watu wa kawaida wa Mungu. Tunapaswa kujilinda dhidi ya kukubalika kwa hati zilizoandaliwa kwa lugha ambayo inachanganya akili. Hatuna haja ya nyaraka kama hizo. Hizi ni

mtego, na watu wetu waonywe kuwa makini nazo. Maneno ya Bwana yalinijia, ‘Waambie watu Wangu, Usiweke tumaini lako katika maandishi yaliyobuniwa na kuandikwa na wanasheria, yaliyojaa ufundi na masharti na vikwazo, vinavyopofusha akili za wale wanaohusika nazo. Mungu anataka wale wanaoamini Ukweli kuchukua msimamo wao dhidi ya kila kitu cha aina hiyo.” —Manuscript 114, October 5,1903— (8 Testimonies, 217)

"Kuna wengi wanaodhani kuwa ni fursa yao kudhibiti kwa kiwango fulani matendo ya watendakazi wenzao. Wanafikiri kwamba wafanyakazi wengine, ambao Bwana anawatumia, wanapaswa kwanza kupata kibali chao kabla ya kufanya kazi fulani, na kwamba wanapaswa kufanya kazi kulingana na maelekezo yao. Hebu nira/kongwa zote za aina hiyo zivunjwe. Kazi inapaswa kwenda mbele kwa maelekezo Yake Bwana.

“Mungu hajampa mwanadamu yoyote kibarua cha kuwa mnyapara wa urithi Wake. Wakati nira ambazo sasa zimewekwa kwenye shingo za baadhi ya watu wa Mungu zinapovunjwa, kazi itasonga mbele kwa njia ambayo itatushangaza. Lakini, kwa upande mwingine, pasipo wahudumu na madaktari na wale walio katika ofisi husika kumpa Bwana njia sahihi, kuwatumia wafuasi Wake anavyoona inafaa, Yeye atakemea kwa hukumu….. .

“Ni roho ya mtu binafsi kujiona kwamba ndiye muhimu, ndiyo inayowaongoza watu kuweka sheria zinazozuia kazi za wenzao. Nimeagizwa kusema, vunja kila nira. Je, tukatae kutii Chanzo cha nguvu zote, na kusubiri ruhusa za wanadamu kabla ya kufanya kazi ambayo Mungu anatuamuru tuifanye? . .

“Kuna kazi kubwa ya kufanywa duniani kabla ya kusudi la milele la Mungu kutimizwa kikamilifu. Badala ya kuzuia njia ya yeyote kati ya watendakazi wetu, ni lazima tuwape njia sahihi ambayo Mungu amepanga wawe nayo, na kumwacha Yeye afanye kazi katika akili za wanadamu. Kila jitihada iwezekanayo lazima sasa ifanywe ili kuwasilisha Ukweli kama ulivyo ndani ya Yesu.”— Letter, October 10, 1899; Manuscript, 147-148.

“Pasipo wale wanaoweza kusaidia katika kuamshwa kuhusu wajibu wao, hawataitambua kazi ya Mungu wakati kilio kikuu cha Malaika wa Tatu kitakaposikika. Nuru inapoiangazia dunia, badala ya kutafuta msaada wa Bwana, watataka kuifunga kazi Yake ili kuendana na mawazo yao finyu. Acha nikuambie kwamba Bwana atafanya kazi katika kazi hii ya mwisho kwa namna nyingi sana nje ya utaratibu wa kawaida wa mambo, na kwa njia ambayo itakuwa kinyume na mipango yoyote ya kibinadamu.

Kutakuwa na wale miongoni mwetu ambao daima watataka kudhibiti kazi ya Mungu, kuamuru hata kuwa madikteta kwamba harakati na mijongeo gani ifanywe wakati kazi inakwenda mbele, chini ya uongozi wa malaika anayejiunga na malaika wa tatu katika ujumbe utakaotolewa kwa ulimwengu. Mungu atatumia njia na fedha ambazo kwazo itaonekana kwamba anashika hatamu mikononi mwake mwenyewe. Watendakazi watashangazwa kwa njia rahisi ambazo atatumia kuleta na kukamilisha kazi Yake ya haki."— Testimonies to Ministers, 300.

"Upana wa kazi ya umishenari ya injili haueleweki. Kazi ya umishenari wa tiba inayotakiwa sasa ni ile iliyoainishwa katika utume ambao Kristo aliwapa wanafunzi Wake kabla ya kupaa Kwake. Mathayo 28:18-20 "Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Maneno haya yanaonyesha eneo letu na kazi yetu. Eneo letu ni ulimwengu; Kazi yetu ni kutangaza zile Kweli ambazo Kristo alikuja katika ulimwengu wetu kutangaza." —Counsels on Health, 509

SEHEMU YA 4

HUDUMA YA UPONYAJI

SURA YA 11

JINSI YESU ALIVYOENDELEA NA KAZI YAKE YA UMISHENARI WA TIBA

Mwongozo wa mazoezi ya tiba ya daktari mkuu.

KIELELEZO CHA YESU KATIKA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA

Tunapaswa kufuata mfano wa Kiungu wa kazi ya umishenari ambayo Yesu alitupa wakati wa maisha Yake ya kidunia: Mt. 11:29; 16:24; Yohana 13:15; Warumi 15:5; 2 Kor. 10:1: Filipi. 2:5; Kol. 3:13; 1 Petro 2:21; Waebrania 12:2; Gospel Workers, 13-19, 41-50; Welfare Ministry, 53 58, 117-124.

KIELELEZO CHA MUNGU KATIKA KAZI YA UMISHENARI: MFANO WA YESU

1- Neno la Mungu lilikuwa msingi wa kila kitu alichofanya na kusema: Mt. 4:4; Ministry of Healing, 21.

2- Aliziinua amri za Mungu juu ya amri za wanadamu: Mt. 15:1- 9, 23.

3- Alichanganya kazi ya tiba, ustawi, uinjilisti, na elimu: Mt. 4:23-24; 9:35-36; Luka 4:17-21; Ministry of Healing, 139-160.

4– Sifa za Yesu zilikuwa aina ya kazi aliyoifanya—kazi ya umishenari wa tiba: Mt. 11:2-6; Ministry of Healing, 34-37.

5– Yeye Alifanya kazi kwa ajili ya matajiri: Marko 14:3; Luka 19:2-9; 18:23; Huduma ya Uponyaji, 24-25; Kwa watoto: Mt. 19:13-15; Ministry of Healing, 38-44; Lakini hasa kwa maskini na wahitaji na wale waliojiona kuwa hivyo: Mt. 11:5; Luka 4:17-21; 2 Kor. 8:9; Mt. 5:3; 19:21; Welfare Ministry, 169-177.

6- Yeye Alikuwa mzingatiaji mzuri sana wa uchumi wa kile alichokuwa nacho, (hakuwa mfujaji au bahili-he was economical): Mt. 10:8- 10: Yohana 6:12; Desire of Ages, 368; Ministry of Healing, 47-48, 207- 208; Counsels on Health, 281.

7– Alikuwa maskini—alikuwa na pesa kidogo, nafasi chache, na hakuwa na makazi ya kudumu: Mt. 8:20; 10:9-11; Luka 12:33; 2 Kor. 8:9; Ministry of Healing, 197-198.

8- Hakutafuta maonyesho au utangazaji kwa umma: Mt. 9:30; 12:16; 16:20; 17:9; Marko 3:12; 5:42; 9:30; Luka 5:14; Huduma ya Uponyaji, 31-32.

9- Alikuwa mwangalifu na kuchukua tahadhari: Mt. 9:30; 10:16.

10- Alitambua kwamba anaweza kukutana na mateso yanayoweza kutokea na pengine hata kifo: Mt. 10:17-40; Desire of Ages, 541.

11 - Hakuogopa mtu: Mt. 10:26, 28.

12- Kazi Yake iliitwa "ya shetani" -na wanadamu fulani: Mt. 10:24-25; 12:24.

13- Alifundisha na kuponya katika miji: Mt. 4:23-24; 9:35-36; Ministry of Healing, 29, 38, n.k.

14 – Alifundisha na kuponya makanisani: Mt.4:23-24; 9:35; 13:54; Katika nyumba na kutoka mlango hadi mlango: Mt. 8:6-8, 14; 9:23-25; Ministry of Healing, 24-25; na katika mitaa na mashambani: Mt. 8-9; Luka 6:1-4; Ministry of Healing, 38.

15 - Mara nyingi alikuwa na makao tulivu kama kituo cha jiji kwa kazi Yake: Luka 4:38-41; 5:17-19; Ministry of Healing, 29-30.

16 - Mara nyingi alifanya kazi Yake katika vituo vya miji mikubwa: Yohana 4:45; 5:1; 9 Shuhuda, 121; Counsels on Health, 500-501.

17– Aliwaleta watu mashambani kwa ajili ya mafundisho na uponyaji zaidi: Mt. 5:1; 13:1-2; 14:13-14; 15:29-30; Ministry of Healing, 54; Medical Ministry, 299; Christ's Object Lesson, 24-27.

18- Alisafiri kutoka jiji hadi jiji: Mt. 4:23-24; 9:35-36; 11:1; 14:34; Ministry of Healing, 22, 30, 31; Counsels on Health, 318, 501.

19 – Alipokataliwa mahali pamoja, alienda mahali pengine: Mt. 10:14, 23; 8:32-34; Ministry of Healing, 97.

20 - Aliwaita watendakazi wenzake wamishenari ili waje kufanya kazi ya tiba (recruited): Mt. 4:18-22; 8:22; 9:9, 37-38; 10:1; Wizara ya Uponyaji, 95-103.

21 - Mara nyingi alichagua wanafunzi wenye elimu ndogo ya mitaala ya kidunia (secular education) na kuwafundisha, kwa mafundisho Yake binafsi na kazi halisi ya kivitendo (practical) wakiwa pamoja Naye, akiwaonyesha jinsi ya kufundisha na kuponya: Mt. 4:18-24; 10:1-42; Ministry of Healing, 95-103.

22 - Watendakazi wa sehemu moja walipokuwa tayari kuendelea peke yao kazi baada ya kozi fupi ya masomo, aliwaacha na kwenda mahali pengine: Ministry of Healing, 95-99; Mt. 8:28-34.

23 - Au, angewapanga katika makundi ya injili ili kwenda pamoja na kufanya kazi ya umishenari wa tiba (Waligawanyika katika vikundi vya watu wawili walipokuwa wakitembea nyumba hadi nyumba): Mt. 10; Luka 10; Ministry of Healing, 139, 142.

24 – Alitumia tiba au dawa sahili za asili (simple remedies): Yohana 9:6-7; Ministry of Healing, 126- 127, 231-233.

25 - Aliwafundisha wale aliowaponya kutii sheria za Mungu, wasije wakawa wagonjwa tena: Yohana 5:14; Ministry of Healing, 73, 91, 113.

26 – Hakuomba malipo yoyote kutoka kwa wale aliowaponya: Mt. 10:8; Luka 6:38; 12:33; Medical Ministry, 122-123.

27 – Aliagiza kila mfuasi afanye kazi ile ile aliyoifanya awali: Marko 16:15-17; Mt. 28:18-20; 10:1, 7-8; Ministry of Healing, 104, 139-169, 226; Welfare Ministry, 52-58.

SURA YA 12

JINSI HUDUMA ILIYOWEKWA WAKFU INAVYOPASWA KUJIHUSISHA NA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA

Mwongozo wa uinjilisti wa wamishenari wa tiba -

1 – KAZI YA UMISHENARI WA TIBA NA HUDUMA

[1] - MCHUNGAJI AU HUDUMU WA INJILI KAMA MFANO WA MMISHENARI WA TIBA

Wachungaji wetu wanapaswa kuwa akili mahiri na ujuzi juu ya matengenezo ya afya. Wanahitaji kuwa na ufahamu wa fiziolojia (sehemu za mwili na kazi zake) na usafi; wanapaswa kufahamu sheria zinazoongoza uzima wa mwili, na athari zake juu ya afya ya akili na roho.

Maelfu kwa maelfu wanajua kidogo tu juu ya mwili huu wa ajabu ambao Mungu ametupa au utunzaji ambao mwili unapaswa kupokea; na wanafikiri kuwa ni muhimu zaidi kusoma masomo yasiyoleta hata matokeo kubwa katika maisha yao.

Wachungaji wana kazi ya kufanya hapa. Wanapochukua msimamo sahihi juu ya somo hili, mengi yatapatikana. Katika maisha yao na nyumba zao wanapaswa kutii sheria za uzima, wakitenda kanuni sahihi na kuishiki afya. Hapo wataweza kuzungumza kwa usahihi juu ya mada hii,wakiwaongoza watu juu zaidi na zaidi katika kazi ya matengenezo. Kuishi katika nuru wao wenyewe, wanaweza kutoa ujumbe wa thamani kubwa kwa wale ambao wanahitaji kubeba ushuhuda kama huo.

Kuna baraka za thamani na uzoefu wa thamani unaoweza kupatikana kama wachungaji watajumuisha uwasilishaji wa suala la afya pamoja na kazi zao zote katika makanisa. Watu lazima wawe na nuru juu ya matengenezo ya afya. Kazi hii imepuuzwa, na wengi wako tayari kuingia kifoni kwa sababu tu wanahitaji nuru ambayo walipaswa kuwa nayo na lazima wawe nayo kabla kuacha kuendekeza ubinafsi……. Viongozi au wenyeviti wa konferensi wanahitaji kujua kuwa ni wakati muafaka wa kujiweka wao wenyewe upande sahihi wa suala hili. Watendakazi na walimu wanapaswa kuwapa wengine nuru waliyopokea. Kazi yao katika kila safu inahitajika. Mungu atawasaidia; Atawaimarisha watumishi Wake ambao husimama imara, na hawatayumbishwa kutoka kwenye ukweli na haki ili kumudu kuendekeza nafsi.

Kazi ya kuelimisha katika vipengele vya umishenari wa tiba ni hatua bora na ya juu, na yenye umuhimu mkubwa katika kumuamsha mwanadamu katika majukumu yake ya maadili. Kama wachungaji wangeshikilia kazi hii katika idara zake mbalimbali kulingana na nuru ambayo Mungu ametoa, kungekuwa na matengenezo yaliyoazimiwa wazi zaidi katika ulaji, unywaji, na uvaaji. Lakini wengine wamesimama moja kwa moja ili kuzinga njia ya maendeleo ya matengenezo ya afya. Wamewarudisha watu nyuma kwa kutojali kwao, upinzani au malaumu, au kuwabeza kwa utani. Wao wenyewe na idadi kubwa ya wengine wamekuwa wagonjwa na hata kufa, lakini wote bado hawajajifunza hekima……..Kila hatua ambayo imekuwa ikifanyika imefanikiwa ila kwa vita vikali sana. Watu hawako tayari kujikana nafsi, hawako tayari kutoa akili na nia

kwenye matakwa ya Mungu; na katika mateso yao wenyewe,na katika mvuto wao kwa wengine, wamegundua matokeo ya hakika ya mwenendo huo.

Kanisa linaandika historia. Kila siku ni vita na kupiga gwaride ili kusonga mbele (battle and a march). Kila upande tumezungukwa na maadui wasioonekana, nasi tunashinda kupitia neema tuliyopewa na Mungu au tunashindwa. Ninawasihi wale ambao hawachukui msimamo wa upande wowote kuhusu matengenezo ya afya waongoke. Nuru hii ni ya thamani, na Bwana hunipa ujumbe wa kusisitiza kwamba wote wanaobeba majukumu katika safu yoyote katika kazi ya Mungu wazingatie kuwa Ukweli una nguvu katika moyo na maisha. Ni kwa njia hii tu yeyote anaweza kukabiliana na majaribu na watakuwa na uhakika wa kushinda katika ulimwengu.

Kwa nini baadhi ya ndugu zetu wanaohudumu wanaonyesha matamanio madogo sana kwenye matengenezo ya afya? Ni kwa sababu mafundisho juu ya kiasi katika mambo yote yanapingana na mazoea yao ya kuendekeza nafsi-kutojikana nafsi. Katika maeneo mengine hili limekuwa kikwazo kikubwa katika njia yetu ya kuwafanya watu kuchunguza, kufanyia kazi na kufundisha matengenezo ya afya. Hakuna mtu anayepaswa kutengwa kama mwalimu wa watu wakati mafundisho yake mwenyewe au mfano wake unapingana na ushuhuda ambao Mungu amewapa watumishi Wake kutoa kuhusu lishe, kwani hili litaleta mkanganyiko. Kupuuza kwake matengenezo ya afya humfanya asifae kusimama kama mjumbe wa Bwana. Nuru ambayo Bwana ametoa juu ya somo hili katika Neno Lake iko wazi, na watu watapimwa na kujaribiwa kwa njia nyingi ili kuona kama wataitii. Kila kanisa, kila familia, inahitaji kufundishwa juu ya kiasi cha Kikristo. Wote wanapaswa kujua jinsi ya kula na kunywa ili kutunza afya. Tuko katikati ya matukio ya kufunga historia ya ulimwengu huu; na kunapaswa kuwepo na hatua zenye kulingana katika kundi la watunza Sabato. Wale ambao wanasimama mbali na kazi kubwa ya kuwafundisha watu juu ya suala hili, hawafuati ambako Tabibu Mkuu anaongoza njia. "Mtu yeyote akitaka kunifuata,"Kristo alisema, "na ajikane mwenyewe, na ajitwike msalaba wake, anifuate."Mathayo16:24. --—Counsels on Diet and Foods, 452-454.

“Wachungaji wanapaswa kuwa na kiasi kwa ukali/uthabiti (strict) katika kula na kunywa, wasije wakatengeneza njia zilizopotoka kwa miguu yao, na kuwageuza walemavu—wale walio dhaifu nje ya njia ya safari ya imani— watoke njiani. Ikiwa, huku wakitangaza ujumbe mzito na muhimu zaidi ambao Mungu amewahi kutoa, wanadamu wanapigana dhidi ya Ukweli kwa kuendekeza mazoea mabaya ya kula

na kunywa, wanaondoa nguvu yote ya ujumbe walio nao."— Counsels on Health, 575.

"Wahudumu wa Kristo, wanaodai kuwa wawakilishi Wake, wanapaswa kufuata mfano Wake, na zaidi ya wengine wote wanapaswa kuunda mazoea ya kiasi kwa ukubwa/makini zaidi. Wanapaswa kuishi maisha na mfano wa Kristo mbele ya watu kwa maisha yao wenyewe kupitia kujikana nafsi, kujitolea na ukarimu wa vitendo. Kristo alishinda uchu wa kula kwa niaba ya mwanadamu; na badala yake wanapaswa kuwaonyesha/kuwawekea wengine mfano unaostahili kuigwa……

"Wanadamu wanaojishughulisha na kutoa ujumbe wa mwisho wa onyo kwa ulimwengu, ujumbe ambao ni wa kuamua hatima ya nafsi, wanapaswa kuweka katika matendo maishani mwao wenyewe kuhusu kweli wanazohubiri kwa wengine. Wanapaswa kuwa mifano kwa watu katika ulaji wao, katika unywaji wao, na katika mazungumzo yao safi na mwenendo wao."— Counsels on Health, 572-573.

[2] - MHUDUMU ANAPASWA KUWA MTENDAKAZI WA UMISHeNARI WA TIBA

"Hebu wachungaji wetu ambao wamepata uzoefu wa kuhubiri Neno, wajifunze jinsi ya kutoa tiba rahisi, kisha wafanye kazi kwa akili mahiri kama wainjilisti wamishenari wa tiba." -Counsels on Health, 397.

"Ningependa kukuambia kwamba hivi karibuni hakutakuwa na kazi yoyote itakayofanywa katika mistari ya huduma bali kazi ya umishenari wa tiba. Kazi ya mhudumu ni kuhudumu. Wahudumu wetu wanapaswa kufanyia kazi mpango wa injili wa kuhudumu…….

"Hamtawahi kuwa wahudumu wa Agizo la Injili hadi muonyeshe kupendezwa kwa kuazimia na kazi ya umishenari wa tiba, injili ya uponyaji na baraka na kuimarishwa. Njoo kwenye msaada wa Bwana…... dhidi ya nguvu kuu za giza, ili isisemwe juu yako Ulaanini Merozi, alisema malaika wa Bwana, Walaanini kwa uchungu wenyeji wake; Kwa maana hawakuja kumsaidia Bwana, Kumsaidia

Bwana juu ya hao wenye nguvu. Waamuzi 5:23 ……

"Ni kwa sababu ya maagizo ambayo nimepokea kutoka kwa Bwana kwamba nina ujasiri wa kusimama kati yenu na kusema jinsi ninavyofanya, haijalishi jinsi unavyoweza kutazama kazi ya umishenari wa tiba. Ningependa kusema kwamba kazi ya umishenari wa tiba ni kazi ya Mungu. Bwana anataka kila mmoja wa wahudumu Wake aingie kwenye mstari. Shikilia kazi ya umishenari wa tiba, na

itakupa uwezekano wa kuwafikia watu. Mioyo yao itaguswa unapohudumia mahitaji yao. Unatoa afueni kwenye kuteseka kwao, utapata fursa ya kuzungumza nao kuhusu upendo wa Yesu.” -Counsels on Health, 533.

[3]- MHUDUMU/MHUDUMU ANAPASWA KUWA MWALIMU WA UMISHENARI WA TIBA

Kuna baraka za thamani na uzoefu mwingi unaoweza kupatikana kama wahudumu watajumuisha uwasilishaji wa suala la afya pamoja na kazi zao zote katika makanisa. Watu lazima wawe na nuru juu ya matengenezo ya afya. — Counsels on Health, 431.

“Wachungaji na walimu wanapaswa kufanya kazi kwa akili mahiri katika mistari yao, wakiwaelekeza washiriki wa kanisa jinsi ya kufanya kazi katika nyanja za umishenari za tiba. Wakati wale wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo wanapokuwa na Mwokozi anayekaa ndani yao, watapatikana wakifanya kama Kristo alivyofanya. Hawatakuwa na nafasi ya kula kutu kwa uvivu kwa kutochukua hatua. Watakuwa wamejitosheleza juu ya kufanya kazi” -Welfare Ministry, 123.

“Kwa ndugu zangu wahudumu ningesema, Ifanye kazi hii kwa busara na uwezo. Panga kazi kwa vijana wa kiume na wa kike katika makanisa yetu. Unganisha kazi ya umishenari wa tiba na kutangazwa kwa ujumbe wa malaika wa tatu. Fanya juhudi za mara kwa mara, zilizopangwa ili kuinua makanisa kutoka kwa kiwango cha wafu ambamo wameanguka, na wamebakia humo miaka nenda rudi. Tuma kwenye makanisa watendakazi ambao wataweka kanuni za matengenezo ya afya vikifungamanishwa na ujumbe wa malaika wa tatu mbele ya kila familia na mtu binafsi. Watie moyo wote kushiriki katika kazi kwa ajili ya wanadamu wenzao, na kuona kama pumzi ya uhai haitarejeshwa kwa haraka katika makanisa haya” -Welfare Ministry, 124.

Kila kanisa linapaswa kuwa shule ya mafunzo kwa watenda kazi Wakristo. Washiriki wake wanapaswa kufundishwa jinsi ya kuwasilisha masomo ya Biblia, jinsi ya kuongoza na kufundisha madarasa ya shule ya Sabato, namna bora ya kuwasaidia watu maskini, na kuwahudumia wagonjwa, na jinsi ya kushughulika na wale ambao bado hawajaongoka. Hatuna budi kuwa na shule za afya, shule za mapishi, na madarasa katika safu mbalimbali za kazi saidizi ya Kikristo. (Ministry of Healing, 148-149).

"Katika mikusanyiko yetu mikubwa, maelekezo yanapaswa kutolewa juu ya afya na kiasi. Kusudia kuamsha akili na dhamiri. Leta kwenye huduma vipaji vyote, na

kufuatilia masomo ya kazi ya machapisho. ‘Elimisha, elimisha, elimisha,’ ndio ujumbe ambao umesisitizwa juu yangu. - Counsels on Health, 449.

“Tunapokaribia mwisho wa wakati lazima tuinuke juu zaidi na zaidi juu ya suala la matengenezo ya afya na kiasi cha Kikristo, tukiliwasilisha kwa njia chanya na iliyoamuliwa zaidi. Ni lazima tujitahidi daima kuwaelimisha watu, si kwa maneno yetu tu, bali kwa matendo yetu. Maagizo ya nadharia na matendo halisi kwa pamoja yana ushawishi wa kusema." Shuhuda kwa kanisa 6:112

"Katika mkutano wa makambi, maelekezo juu ya mada za afya yanapaswa kutolewa kwa watu. Katika mikutano yetu nchini Australia, mihadhara kuhusu masomo ya afya ilitolewa kila siku, na shauku kubwa iliamshwa. —Counsels on Health, 467.

2 - UHUSIANO WA VIONGOZI/WENYEVITI WA KONFERENSI NA VIONGOZI WENGINE KWA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA

“Kupitia wanafunzi wa kwanza karama ya Mwenyezi Mungu ilitolewa kwa Israeli; Mwinjilisti mwaminifu leo atafanya kazi kama hiyo katika kila jiji ambalo wamishenari wetu huingia. Ni kazi ambayo kwa kiasi fulani tumejaribu kuifanya kuhusiana na baadhi ya vituo vyetu vya sanitarium, lakini uzoefu mpana zaidi katika mistari hii unaweza kupatikana

“Je, viongozi/wenyeviti wetu wa makonferensi hawawezi kufungua njia kwa wanafunzi katika shule zetu kushiriki katika eneo hili ya kazi? Tena na tena imewasilishwa kwangu kwamba ‘kunapaswa kuwa na makundi yaliyopangwa na kuelimishwa kwa kina zaidi, ili kufanya kazi kama wauguzi, kama wainjilisti, kama wahudumu, kama waombaji, kama wanafunzi wa injili, kukamilisha tabia ya ule mfano wa Kiungu.’ — Counsels on Health, 541-542.

Wenyeviti wa makoferensi yetu wanapaswa kutambua kuwa ni wakati muafaka wa wao kujiweka kwenye haki upande wa hoja/swali hili. watumishi na walimu wanapaswa kuwapa wengine mwanga ambao wameupokea. Kazi yao katika kila mstari inahitajika. Mungu atawasaidia; Atawatia nguvu waja Wake wanaosimama kidete na hawatayumbishwa na Ukweli na uadilifu ili wasikite akili zao katika kuendekeza tamaa za mwili. — Shuhuda kwa Kanisa 6: 376-377.

Injili ya afya ina watetezi hodari, lakini kazi yao imefanywa kuwa ngumu sana kwa sababu wachungaji wengi, wenyeviti wa makonferensi, na wengine wenye nyadhifa za ushawishi wameshindwa kutoa umakini na kipaumbele cha matengenezo ya afya ipasavyo. Hawajaitambua katika uhusiano wake na kazi ya ujumbe kama mkono wa kuume wa mwili. Wakati heshima ndogo sana

imeonyeshwa kwa idara hii na watu wengi, na kwa baadhi ya wachungaji, Bwana ameonyesha kuijali kwa kuipa mafanikio tele. Kazi ya afya inapofanywa ifaavyo, kazi ya afya inakuwa daraja la kuvukia, linalotengeneza njia ili Kweli nyingine zifikie moyo. Wakati ujumbe wa malaika watatu unapopokelewa kwa utimilifu wake, matengenezo ya afya yatapewa nafasi yake katika mabaraza ya konferensi, katika kazi ya kanisa, nyumbani, mezani, na katika mipango yote ya nyumbani. Kisha mkono wa kulia utatumika katika kulinda mwili. — Shuhuda kwa Kanisa 6:327.

Imewasilishwa kwangu kwamba katika safu nyingi za kazi tunafanya lakini sehemu ndogo ya kile kinachopaswa kufanywa. Imani, bidii, na nguvu hazionyeshwi jinsi inavyopaswa kuwa, katika kazi ya huduma, Jitihada za wengi ni dhaifu na zisizo roho na za kuvunja moyo. Ni dhahiri kwamba nuru tuliyopewa na Mungu kuhusu wajibu na mapendeleo yetu haya jafanyiwa kazi. Wanadamu wameweka mipango yao wenyewe badala ya mipango ya Mungu. Nimeagizwa kusema kwamba ustawi wa kazi ya umishenari wa tiba uko katika utaratibu wa Mungu. Kazi hii lazima ifanyike; Ukweli lazima upelekwe kwenye barabara kuu na njia ndogo. Na wachungaji/wahudumu na washiriki wa kanisa wanapaswa kuamka na kuona umuhimu wa kushirikiana katika kazi hii. Shuhuda kwa Kanisa 6: 299.

Kwa bidii, na nguvu zisizochoka wale ambao wamehisi mzigo wa kazi ya usaidizi wa Kikristo wameshuhudia kwa kazi zao kwamba hawaridhiki kuwa waumini wa kinadharia tu. Wamejaribu kutembea katika nuru. Wameweka imani yao katika vitendo. Wameunganisha imani na matendo. Wamefanya kazi ile ile ambayo Bwana amebainisha ifanywe, na nafsi nyingi zimepewa nuru, na kusadikishwa, na kusaidiwa. — Shuhuda kwa Kanisa 6: 299.

Kutojali miongoni mwa wachungaji wetu kuhusiana na matengenezo ya afya na kazi ya umishenari wa tiba inashangaza. Hata wale ambao siyo Wakristo hushugulika na mada hii kwa heshima zaidi kuliko baadhi ya watu wetu wenyewe, na hao wanatutangulia mbele yetu, wakisonga mbele. — Shuhuda kwa Kanisa 6:299.

Kwa nini, nauliza, baadhi ya ndugu zetu wachungaji wako nyuma sana katika kutangaza mada iliyotukuka sana ya kiasi? Ndugu zangu, neno mlilopewa ni hili: "Shikeni kazi ya matengenezo ya afya; songa mbele." Ikiwa unafikiri kwamba kazi ya umishenari wa tiba inachukua sifa kubwa isiyo na uwiano, chukua watu ambao wamekuwa wakifanya kazi katika nyanja hii pamoja nawe kwenye nyanja zako za kazi, wawili hapa na wawili pale. Pokea wamishenari hawa wa tiba jinsi

ungempokea Kristo, na uone ni kazi gani wanaweza kufanya. Huwezi kuwaona kama mbilikimo katika uzoefu wao wa kiroho/kidini. Angalia kama kwa njia hii huwezi kuleta mengi ya mkondo muhimu wa mbinguni katika makanisa……Angalia kama hakuna watu watakaopata maarifa/elimu wanayohitaji sana, na utoe ushuhuda huu: “Mungu, ambaye ni mwingi wa rehema, kwa upendo Wake mkuu aliotupenda, hata tulipokuwa wafu kwa sababu ya dhambi, alituhuisha. pamoja na Kristo (mmeokolewa kwa neema;) akatufufua pamoja Naye, akatuketisha pamoja Naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu." Waefeso 2:4-6. Hitaji letu kuu ni umoja, umoja kamili katika kazi ya Mungu.

Wale ambao hawawezi kuona umuhimu na utendaji kazi wa umishenari wa tiba hawapaswi kuhisi wamepewa mamlaka kujitahidi kudhibiti awamu yake yoyote. Watu hawa wanahitaji ujuzi ulioongezeka katika kila mstari wa matengenezo ya afya. Wanahitaji kutakaswa, kusafishwa, kuboreshwa na kukuzwa. Wanahitaji kufinyangwa na kutengenezwa kwa mfano wa Mungu. Kisha wataona kwamba kazi ya umishenari wa matibabu ni sehemu ya kazi ya Mungu. Sababu ya washiriki wengi wa kanisa kutoelewa tawi hili la kazi, ni kwamba hawamfuati Kiongozi wao hatua kwa hatua katika kujinyima na kujitoa dhabihu. Kazi ya umishenari wa tiba ni kazi ya Mungu na ina saini/muhuri Wake, na ingawa fedha hazipaswi kuingizwa katika mstari huu mmoja ili kuzuia au kulemaza kazi ambayo inapaswa kufanywa katika maeneno mapya, haipaswi kuchukuliwa kuwa isiyo muhimu. — Shuhuda kwa Kanisa 6: 299- 300.

“Mkono wa kuume unatumiwa kufungua milango ambayo inasaidia mwili uweze kuingia ndani. Hii ndiyo sehemu ambayo kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kutenda. Kazi hii inapaswa kuandaa watu kupokea ili Ukweli wa wakati huu. Mwili usio na mikono hauna uwezo. Ili kuupa mwili heshima, heshima lazima pia itolewe kwa mikono inayomsaidia mtu, ambayo ni mawakala wa muhimu hivi kwamba bila ya hii, mwili hauwezi kufanya kitu chochote. Hivyo, mwili unaoutendea mkono wa kuume isivyo vyema, na ukikataa msaada, hauna uwezo wa kufanya jambo lolote……

“Katika nchi hii yote ni lazima kazi ifanyike ambayo bado haijafanywa. Kazi ya umishenari wa tiba lazima itambuliwe. Wale wanaoenda kushiriki katika kazi ya huduma lazima wawe na Akili mahiri juu ya suala la matengenezo ya afya. Watu hao ambao baada ya kuwa na uzoefu wa miaka mingi lakini hawaithamini kazi ya umishenari wa tiba, hawapaswi kuteuliwa kuongoza makanisa yetu. Hawatembei katika nuru ya Ukweli uliopo kwa wakati huu. Wale wanaouishi Ukweli na kuthamini suala la kiasi katika nyanja zake zote hawapaswi kuwekwa chini ya

uongozi (kuongozwa na) wa mhudumu ambaye hajazingatia nuru ambayo Mungu ameitoa juu ya matengenezo ya afya. Je, mtu anaweza kuwa msaada gani kwa kanisa ikiwa hatembei katika nuru?"— Medical Ministry, 238.

Watendakazi wa umishenari wa tiba wanafanya kazi iliyotelekezwa kwa muda mrefu ambayo Mungu alitoa kwa kanisa la Battle Creek—wanatoa mwito wa mwisho kwa karamu ambayo Bwana Ameitayarisha. — Shuhuda kwa Kanisa 8:71.

Ili kuendelea mbele sawa, kazi ya umishenari wa tiba inahitaji talanta. Inahitaji mikono yenye nguvu, iliyo tayari, na usimamizi wa busara na wenye upembuzi. Lakini je, hii inaweza kutokea wakati wale walio katika sehemu zenye kuwajibika— wenyeviti/viongozi wa konferensi na wakurugenzi—wakizuia njia? Bwana asema kwa Viongozi/Wenyeviti wa konferensi na ndugu wengine wenye ushawishi: "Ondoa mawe ya yanayokwaza, ambayo yamewekwa mbele ya watu."— Shuhuda kwa Kanisa 8: 71.

Watu wetu katika Battle Creek hawajatumia talanta zao katika kupanga na kubuni jinsi ya kupanda kiwango cha Ukweli katika maeneo ambayo ujumbe haujatangazwa na ambapo jitihada za makusudi zinapaswa kufanywa; na Bwana emeweka msukumo kwa Dk. Kellogg na washirika wake kufanya kazi ambayo ni ya kanisa na ambayo ilitolewa kwao, lakini ambayo hawakuchagua kuikubali. Wengine katika Battle Creek, badala ya kuchukua kazi waliyopewa na Mungu, kwa kufuata njia yao ya ubinafsi, wamepofusha macho yao ya kiroho na macho ya kiroho ya wengine; na Mungu ameweka kazi yake ya thamani katika mikono ya wale ambao wataichukua na kuipeleka mbele.

Mungu yu katika Patakatifu Pake, Naye anakaa pamoja naye aliye na roho iliyonyenyekea na iliyotubu, na kupondeka ili kuzifufua roho za wanyenyekevu, na kuifufua mioyo yao wenye majuto. Wale wanaofanya kazi ya umishenari wa tiba wanapaswa kupata kibali kamili na ushirikiano wa kanisa. Ikiwa hawana hii, wanazuiwa. Hata hivyo, wataendelea mbele.

Sio mpango wa Mungu kwamba kutakuwa na makanisa mawili hapo Battle Creek kwa sababu tu ya ukosefu wa ushirikiano. Ni bora zaidi kutafuta umoja wa vitendo. Ikiwa wahudumu wa umishenari wa tiba, watabeba mstari huu wa juhudi katika makanisa kila mahali, ikiwa watafanya kazi kwa hofu ya Mungu, watapata milango mingi ikiwa imefunguliwa mbele yao, na malaika watafanya kazi pamoja nao. Tafadhali soma mwaliko wa karamuni, na mwito wa mwisho upaswao kufanywa. Jifunze kile kinachofanywa ili kutimiza agizo la Yesu. Sielewi kwa nini kutojali namna hii kunadhihirishwa, kwa nini usimame mbali na kukosoa na kusogea mbali. Wavu wa injili unapaswa kutupwa baharini, nao unavuta

mema na mabaya. Lakini kwa sababu jambo hili liko hivyo, je, wanaume na wanawake watapuuza jitihada zinazofanywa ili kuokoa wale ambao wataamini na ambao wataungana katika kufikia tabaka hilo ambalo Kristo alisema juu yake katika kemeo Lake kwa Mafarisayo? Kuhusu watu wenye dhambi na makahaba, Yeye alisema, “Watawatangulia katika ufalme wa Mungu.” Je huoni hata kanisani wapo watu wasio na muunganiko na Mungu? Lakini Kristo anasema: Acheni ngano na magugu vikue pamoja hata wakati wa mavuno; na wakati wa mavuno nitawaambia wavunao, Yakusanyeni kwanza magugu, myafunge matita-matita, kisha mkayachome; bali ngano ikusanyeni ghalani mwangu..”

Wakati Bwana aletapo msukumo juu ya makanisa, akiwaamuru watu kufanya kazi fulani, na wanakataa kufanya kazi hiyo; na wakati baadhi, jitihada zao za kibinadamu zilizounganishwa na za Kiungu, zinapofanya bidii ili kufikia kina kirefu cha ole na taabu za mwanadamu, baraka za Mungu zitakuwa juu yao kwa wingi. Ingawa ni wachache tu wanaokubali neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, kazi yao haitakuwa bure; kwa maana nafsi moja ni ya thamani, na ya thamani sana, mbele za macho ya Mungu. Kristo angekufa kwa ajili ya nafsi hiyo moja ili mtu apate kuishi katika zama za milele.

Hebu tujifunze sura ya kumi na nane ya Mathayo. Sura hii inapaswa kuangaza macho yetu. “Angalieni,” Kristo asema: “Angalieni msidharau mmojawapo wadogo hawa; kwa maana nawaambia ya kwamba malaika wao mbinguni siku zote huutazama uso wa Baba Yangu aliye mbinguni. Kwa maana Mwana wa Adamu alikuja kukiokoa kilichopotea. Kwa maana Mwana wa Adamu alikuja kuokoa kile kilichopotea. Mwaonaje? Mtu akiwa na kondoo mia, na kisha mmoja akampotea, Je! Hawaachi wale tisa na tisini, akaenda milimani, na kumtafuta yule aliyepotea? Hata akipata kumwona, amin, nawaambia, amfurahia huyo zaidi, kuliko wale 99 wasiopotea. Vivyo hivyo haipendezi mbele za Baba yenu aliye mbinguni kwamba mmoja wa wadogo hawa apotee…….” Mathayo 18:10- 14.

Nafsi nyingi zinazookolewa, zinanyofolewa kutoka kutoka kwenye mkono wa Shetani, na wafanyakazi waaminifu. Lazima Mtu awe na mzigo wa roho ili kupata wale ambao wamepotea kwa Kristo. Kuokolewa kwa nafsi moja ambayo Shetani ameshinda juu yake kunaleta furaha miongoni mwa malaika wa mbinguni. Kuna wale ambao wameharibu ndani yao sura ya maadili ya Mungu. Wavu wa injili lazima ukusanyike katika maskini hawa waliofukuzwa. Malaika wa Mungu watashirikiana na wale wanaojishughulisha na kazi hii, wanaofanya kila juhudi kuokoa roho zinazoangamia, kuwapa fursa ambazo wengi hawajawahi kuzipata. Hakuna njia nyingine ya kuwafikia watu ila kwa njia ya Kristo. Daima Alifanya

kazi ili kuondoa mateso na kufundisha haki. Ni kwa njia hii tu kwamba wadhambi wanaweza kuinuliwa kutoka katika kina cha udhalilishaji……Wafanyakazi lazima wafanye kazi kwa upendo, kuwalisha, kuwasafisha na kuwavisha wale wanaohitaji msaada wao. Kwa njia hii hawa waliosahaulika wanatayarishwa kujua kwamba kuna mtu anayejali nafsi zao. Bwana amenionyesha kwamba wengi wa hawa maskini waliotengwa na jamii, kupitia huduma ya mashirika wa kibinadamu, watashirikiana na nguvu za Mungu na kutafuta kurejesha sura ya maadili ya Mungu ndani ya wengine ambao Kristo amelipa bei ya damu Yake Mwenyewe. Wataitwa wateule wa Mungu, wa thamani, na watasimama kando ya kiti cha enzi cha Mungu. “Ndipo itakapoonekana ishara Yake Mwana wa Adamu mbinguni; ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza, nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi. Naye atawatuma malaika Zake pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule wake toka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu.” “Kesheni basi; kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu. Lakini fahamuni neno hili; kama mwenye nyumba angaliijua ile zamu mwivi atakayokuja, angalikesha, wala asingaliiacha nyumba yake kuvunjwa. Kwa sababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari; kwa kuwa katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu Yuaja. Ni nani basi yule mtumwa mwaminifu mwenye akili, ambaye bwana wake alimweka juu ya nyumba yake, awape watu chakula kwa wakati wake? Heri mtumwa yule, ambaye bwana wake ajapo atamkuta akifanya hivyo. Amin, nawaambieni, atamweka juu ya vitu vyake vyote. Lakini mtumwa yule mbaya akisema moyoni mwake, Bwana wangu anakawia; akaanza kuwapiga wajoli wake, na kula na kunywa pamoja na walevi; bwana wake mtumwa huyo atakuja siku asiyodhani, na saa asiyojua, atamkata vipande viwili, na kumwekea fungu lake pamoja na wanafiki; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno..” Mathayo 24: 30,31, 42-51

Ndugu, kuwa makini, makini sana. Kuna kazi inayofanywa na matabibu wa kimishenari ambayo inajibu maelezo yaliyotolewa katika Mistari 48-51. Bwana anafanya kazi ili kuwafikia ale waliopotoka zaidi. Wengi watajua maana ya kuinuliwa kumwelekea Kristo, lakini hawatakuwa na ujasiri wa kimaadili kupigana na hamu ya kula na tamaa. Lakini wafanyakazi wasivunjike moyo kwa hili; kwa maana imeandikwa: " Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani." 1 Timotheo 4:1. Je, ni wale tu waliookolewa kutoka kwenye vilindi vya chini kabisa ndio wanaorudi nyuma? Kuna wale katika huduma ambao wamekuwa na nuru na ujuzi wa Ukweli, ambao hawatakuwa washindi.

Hawadhibiti uchu wa chakula na tamaa zao au kujikana wenyewe kwa ajili ya Kristo. Maskini wengi waliotengwa nje, hata watoza ushuru na wenye dhambi, watashika tumaini lililowekwa mbele yao katika injili na wataingia katika ufalme wa mbinguni mbele ya wale ambao wamepata fursa nyingi na nuru kuu, lakini ambao wametembea gizani. Katika siku kuu ya mwisho wengi watasema: “Bwana, Bwana, utufungulie.” Lakini mlango utafungwa, na kubisha kwao kutakuwa bure.

Tunapaswa kupata hisia za kina juu ya mambo haya, kwa kuwa ni ya kweli. Tunapaswa kuwa na makadirio ya juu ya Ukweli na thamani ya roho. Muda ni mchache, na kuna kazi kubwa ya kufanywa. Ikiwa huna matamanio katika kazi inayoendelea, ikiwa hutawatia moyo watenda-kazi ya umishenari wa tiba katika makanisa, basi itafanywa bila idhini yako; kwa maana ni kazi ya Mungu, na ni lazima ifanywe. Ndugu na dada zangu, chukueni nafasi zenu upande wa Bwana na muwe watenda kazi wenye bidii, thabiti, na wajasiri pamoja na Kristo, mkifanya kazi pamoja Naye katika kutafuta na kuokoa waliopotea. Shuhuda kwa Kanisa 8:71-75

SURA YA 13

MAENEO YA KAZI NA MAELEKEZO AMBAYO MMISHENARI WA TIBA ANAPASWA KUSHIRIKI

1 - WIGO WA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA NA MAFUNZO AMBAYO ANAPASWA KUHUSIKA NAYO.

Watenda kazi wote wa injili wanapaswa kujua jinsi ya kutoa tiba rahisi zinazoleta afueni kwa maumivu, na hata kuondoa magonjwa (hydrotherapia, mimea na chakula n.k).

Watendakazi wote wa Injili wanapaswa pia kutoa mafundisho katika kanuni za maisha zenye afya. Kuna magonjwa kila mahali, na mengi ya hayo yanaweza kuzuiwa kwa kuzingatia sheria za afya. Watu wanahitaji kuona umuhimu wa kanuni za afya katika ustawi wao kwenye maisha haya na maisha yajayo. Wanahitaji kuamshwa kwenye wajibu wao kwa ajili ya miili yao iliyoumbwa na Muumba wao kama makao Yake, ambayo Yeye huwataka wawe mawakili waaminifu kwa hayo makao (miili).

“Maelfu wanahitaji na wangepokea kwa furaha maagizo kuhusu mbinu rahisi za kuwatibu wagonjwa—mbinu zinazochukua mahali pa kutumia dawa zenye sumu (poisonous drugs). Kuna haja kubwa ya mafundisho kuhusiana na matengenezo ya lishe. Tabia mbaya za kula na matumizi ya vyakula visivyo na afya vinachangia sio kwa kiwango kidogo hali kutokuwa na kiasi na uhalifu na ukosefu wa furaha unaolaani ulimwengu.

“Katika kufundisha kanuni za afya, weka akilini lengo kuu la matengenezo—kwamba kusudi lake ni kupata maendeleo ya juu zaidi ya kimwili na kiakili na kiroho. Onyesha kwamba sheria za asili, zikiwa ni sheria za Mungu, zimeundwa kwa manufaa yetu; Kuzitii sheria hizi kunakuza furaha katika maisha haya, na husaidia katika maandalizi ya maisha yajayo huko mbinguni.

“Watie moyo watu kuchunguza kiumbe hicho cha ajabu, mfumo wa mwanadamu, na sheria zinazomtawala. Wale wanaoona uthibitisho wa upendo wa Mungu, wanaoelewa angalau mambo fulani ya hekima na wema wa sheria Zake, na matokeo ya utii, watazingatia wajibu na majukumu yao kwa mtazamo tofauti kabisa. Badala ya kutazama uzingatiaji wa sheria za afya kama suala la kujitoa mhanga au kujikana nafsi, wataiona kama ilivyo hakika na yenye baraka na isiyo na kifani.

“Kila mtendakazi wa injili anapaswa kuhisi kwamba kufundisha kanuni za maisha yenye afya ni sehemu ya kazi yake aliyochaguliwa kuifanya. Katika kazi hii kuna uhitaji mkubwa, na ulimwengu uko wazi kwa ajili yake.” ——Counsels on Health, 389-390.

[1] - TOA TIBA RAHISI AMBAZO HUFANYA MENGI ILI KUPUNGUZA MATESO NA KUONDOA MAGONJWA

“Wanafunzi hawa walikuwa wawe na uweza ule ule ambao Yesu alikuwa nao wa kuponya "ugonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu." Kwa kuponya magonjwa ya mwili katika Jina Lake Bwana, wangethibitisha nguvu Zake kwa ajili ya kuponya roho. Mathayo 4:23; 9:6.. .

Hivyo ndivyo Kristo alivyowapatia wanafunzi Wake kazi ya utume. Alitoa kwa ukamilifu mahitaji/majaliwa kwa ajili ya kutenda kazi hiyo, na alibeba mwenyewe wajibu kwa ajili ya mafanikio ya kazi hiyo. Alimradi walitii Neno Lake, na kufanya kazi kwa kuunganika Naye, wasingeshindwa. Enendeni kwa mataifa yote, aliwaambia. Enendeni sehemu za mbali zinazokaliwa na watu duniani, lakini mjue kwamba uwepo Wangu uko kule. Fanyeni kazi kwa imani na ujasiri, maana hautakuja kamwe muda ambao nitawaacha.

Agizo la Mwokozi kwa wanafunzi wale liliwajumuisha waamini wote. Linahusisha wote wanaomwamini Kristo mpaka mwisho wa wakati.

“Naye Yuko tayari kuponya sasa kama wakati ule alipokuwa duniani katika mwili. Watumishi wa Kristo ndio wawakilishi Wake, mifereji ya kazi Zake. Yeye Anatamani kuonyesha uweza Wake wa kuponya kupitia hao.

“Namna Mwokozi alivyoponya magonjwa mna fundisho kwa wanafunzi Wake. Katika tukio moja alipaka macho ya mtu kipofu kwa matope, na akamwambia, "Nenda kanawe katika birika ya Siloamu, . . . Basi akaenda na kunawa; akarudi anaona." Yohana 9:7. Uponyaji ule ungefanywa tu kwa uweza wa Mponyaji Mkuu yule, lakini Kristo alitumia njia nyepesi za mawakala wa asili. Wakati hakuonekana akitumia tiba ya vidoge vya famasia, aliruhusu matumizi ya tiba za asili nyepesi.

“Kwa wagonjwa wengi waliopokea uponyaji, Yesu alisema, "Usitende dhambi tena, lisije likakupata jambo lililo baya zaidi." Yohana 5:14. Hivyo alifundisha kwamba ugonjwa ni matokeo ya kukiuka sheria za Mungu, sheria zote mbili, yaani, za asili na za kiroho. Maumivu makubwa duniani yasingekuwepo ikiwa watu wangedumu kuishi kwa mapatano na mpango wa Mwumbaji...

“Tunapaswa tuwe watenda-kazi pamoja na Mungu kwa ajili ya kurejesha afya ya mwili na ya roho.

“Na tunapaswa tufundishe wengine namna ya kuhifadhi na kurejesha afya. Kwa wagonjwa tunapaswa kutumia tiba ambayo Mungu ametoa katika vitu vya asili,

na tunapaswa tuwaelekeze kwake Yeye pekee awezaye kurejesha. Ni kazi yetu kuwapeleka wagonjwa na watu wenye mateso kwa Kristo katika mikono ya imani yetu. Tunapaswa tuwafundishe kumwamini Mponyaji Mkuu. Tunapaswa kushikilia ahadi Zake, na kuomba udhihirisho wa nguvu Zake. Kiini chenyewe cha injili ni urejeshwaaji, na Mwokozi anatutaka tuwafanye wagonjwa, wasio na tumaini, na wenye shida washikilie nguvu Zake." -Desire of Ages, 821-825.

"Watu wetu wanapaswa kuwa wenye akili mahiri kuhusu matibabu ya magonjwa kwa kutokutumia dawa za sumu. Wengi wanapaswa kutafuta kupata elimu ambayo itawawezesha kukabiliana na magonjwa kwa njia mbalimbali kwa njia rahisi zaidi. Maelfu wameingia makaburini kwa sababu ya dawa za sumu, hawa wangerejeshewa afya kama njia sahili za tiba zingetumika. Tiba ya maji, kwa busara na ustadi, inaweza kuwa njia ya kuokoa maisha ya watu wengi. Hebu utafiti wa bidii ufanyike sawasawa na matibabu makini. Hebu maombi ya imani yatolewe kando ya kitanda cha wagonjwa. Hebu wagonjwa watiwe moyo kudai ahadi za Mungu kwa ajili yao wenyewe."—Medical Ministry, 227.

Watendakazi - wamishenari wa injili ya tiba - wanahitajika sasa. Hamwezi kuendelea kutumia miaka mingi katika maandalizi. Hivi karibuni milango iliyofunguliwa kwa ajili ya Ukweli itafungwa milele. Pelekeni ujumbe sasa. Msikawie, mkamruhusu adui kumiliki mashamba yaliyofunguliwa sasa mbele yenu. Hebu makundi madogo yaende mbele kufanya kazi ambayo Kristo aliwapa wanafunzi Wake. Hebu wafanye kazi kama wainjilisti, wakitawanya machapisho yetu na kuzungumza juu ya ile Kweli kwa wale wanaokutana nao. Hebu wawaombee wagonjwa, wakiwahudumia mahitaji yao, si kwa kutumia dawa za famasia (drugs(, lakini kwa tiba za asili, na kuwafundisha jinsi ya kuirejesha afya na kuepuka magonjwa."— Shuhuda kwa Kanisa 9: 172

Watendakazi wa Injili wote wanapaswa pia kutoa mafundisho katika kanuni za maisha yenye afya. Kuna magonjwa kila mahali, na mengi ya hayo yanaweza kuzuiwa kwa kuzingatia sheria za afya.—Ministry of Healing, 146.

Zipo njia nyingi ambazo maji yaweza kutumika kutuliza maumivu na kuzuia ugonjwa. Watu wote wapaswa kuwa na utambuzi mahiri katika maarifa ya matumizi ya tiba rahisi majumbani mwao. Hasa akina mama, wanapaswa kujua jinsi ya kutunza familia zao katika suala la afya na maradhi. —Ministry of Healing, 237.

"Pale msukumo mkali wa kidini utakapoharibu na kupindua uhuru wa taifa letu, wale ambao wangesimamia uhuru wa dhamiri watawekwa katika nyadhifa na nafasi ngumu. Kwa ajili ya faida yao, na kutokana na fursa waliyonayo

wangepaswa kuwa wenye akili kuhusiana na ugonjwa, sababu zake, kinga na tiba. Na wale wanaofanya hivi watapata uwanja wa kufanya kazi popote pale." -Counsels on Health, 506.

"Bwana ametoa njia sahili za kupiku magonjwa katika mitishamba (antidote), na hizi zinaweza kutumiwa kwa imani, bila kukana imani; Kwani kwa kutumia baraka zinazotolewa na Mungu kwa manufaa yetu tunashirikiana Naye. Anaweza kutumia maji na jua na mimea ambayo ameruhusu ikue, katika uponyaji wa magonjwa yanayoletwa na uzembe au ajali. Hatuonyeshi ukosefu wa imani tunapomwomba Mungu abariki tiba Zake. Imani ya kweli itamshukuru Mungu kwa ujuzi wa jinsi ya kutumia baraka hizi za thamani kwa njia ambayo itarejesha nguvu za kiakili na kimwili."—2 Selected Messages, 289.

"Kila mahali wagonjwa wanaweza kupatikana. Na wale wanaotoka kama watenda kazi kwa ajili ya Kristo wanapaswa kuwa wanamatengenezo wa kweli wa afya, walio tayari kuwapa wale walio wagonjwa tiba rahisi ambazo zitawapa nafuu, na kisha kuomba pamoja nao. Hivyo watafungua mlango wa kuingia kwa Ukweli. Kufanya kazi hii kutafuatiwa na matokeo mazuri. Familia zetu zinazotunza Sabato zinapaswa kuweka akili zao zikiwa zimejazwa na kanuni muhimu za matengenezo ya afya na njia nyinginezo za Ukweli, ili ziwe msaada kwa jirani zao. Mnapaswa kuwa wamishenari wenye kusaidia uhalisia wa maisha ya kila siku katika utendaji wenu. Kusanya maarifa yote yanayowezekana ambayo yatasaidia kukabiliana na magonjwa. Hilo laweza kufanywa na wale ambao ni wanafunzi wenye uadilifu na bidii"—Medical Ministry, 320.

"Hebu wachungaji wetu ambao wamepata uzoefu wa kuhubiri Neno, wajifunze jinsi ya kutoa tiba rahisi, kisha wafanye kazi kwa akili kama wainjilisti wamishenari wa tiba." -Counsels on Health, 397.

Wengine wanashindwa kabisa kutambua umuhimu wa wamishenari, wakiwemo pia wamishenari wa tiba. Mhudumu wa Injili atafanikiwa maradufu katika kazi yake ikiwa anaelewa jinsi ya kutibu magonjwa. Nuru inayozidi kuongezeka imetolewa kwangu juu ya mada hii." Medical Missionary, 245.

"Mwinjilisti wa vitabu anapoenda kutoka mahali hadi mahali, atakutana na wengi ambao ni wagonjwa. Anapaswa kuwa na ujuzi wa kivitendo ili kujua sababu za ugonjwa, na anapaswa kuelewa jinsi ya kutoa matibabu rahisi, ili aweze kuhudumia wanaoteseka na kuwapa nafuu. Zaidi ya hayo, anapaswa kuomba kwa imani na usahili kwa ajili ya wagonjwa, akiwaelekeza kwa Tabibu Mkuu. Anapotembea hivyo na kufanya kazi na Mungu, malaika wanaohudumu wako karibu naye, wakimpa uwezo wa kuifikia mioyo. —Counsels on Health, 463-464.

Nguvu ya Kristo ya kuponya ugonjwa bado haijabadilika (Desire of Ages, 465-466). Wazazi wanahitaji kuelewa tiba rahisi ya ugonjwa (Ministry of Healing, 237, 385). Kazi ya umishenari katika kutunza wagonjwa (Counsels on Health, 33). Kazi kwa ajili ya wagonjwa na maskini haiwezi kufanywa na wengine/wakala (lazima sisi tufanye) (Counsels on Health, 390). Wanafunzi kujifunza tiba ya wagonjwa (Education, 218; Testimonies 9, 178; Counsels on Health, 301). Kristo anatamani kuponya kupitia watumishi Wake (Desire of Ages, 823-824; Counsels on Health, 30)

Uponyaji wa kimwili unafungamana na injili (Ministry of Healing, 115, 141; Counsels on Health, 29, 497). Uponyaji na mafundisho ya imani visitenganishwe (Ministry of Healing, 141; 9 Testimonies, 171; Counsels on Health, 396). Wote wanapaswa kujielimisha katika matumizi ya tiba rahisi (2 Selected Messages, 290).

[2] - TOA MAELEKEZO KATIKA KANUNI ZA MAISHA YENYE AFYA

Washiriki wa kanisa wahudumu na kufundisha kanuni za afya (Shuhuda 9, 112-113; Counsels on Health, 443-446, 452). Watendakazi wa injili wanapaswa kuwa na uwezo wa kufundisha kanuni za afya (Ministry of Healing, 146-147; Gospel Workers, 233; Counsels on Health, 40, 389). Wajibu wa Wahudumu kuelewa, kutangaza na kufundisha kanuni za afya (Gospel Workers, 231). Utangazaji wa kanuni za afya zinazohitajika katika kujitayarisha kwa ajili ya kuja kwa Kristo (Shuhuda 6, 224; Counsels on Health, 206). Kanuni za afya zinazopaswa kufundishwa kwa mfano (Shuhuda 6, 112-113; Counsels on Health, 451, 463, 467).

Kwa matamko zaidi kuhusu hili, angalia Sehemu ya 8 kuhusu somo hili

[3] - TOA MAELEKEZO KUHUSU NJIA RAHISI ZA KUTIBU WAGONJWA

Watendakazi wa injili wanapaswa kujua jinsi ya kutoa tiba rahisi ili kuleta afueni kwa maumivu, na kuondoa magonjwa…….

“Maelfu wanahitaji kufundishwa na watakuwa na furaha kupata maelekezo kuhusu mbinu sahili za kutibu wagonjwa-mbinu ambazo zitakuwa mbadala wa dawa zenye sumu.”

Watendakazi wa Injili wanapaswa pia kutoa mafundisho katika kanuni za maisha yenye afya. Kuna magonjwa kila mahali, na mengi ya hayo yanaweza kuzuiwa kwa kuzingatia sheria za afya. Watu wanahitaji kuona umuhimu wa kanuni za afya katika ustawi wao kwenye maisha haya na maisha yajayo. Wanahitaji kuamshwa kwenye wajibu wao kwa ajili ya miili yao iliyoumbwa na Muumba wao

kama makao Yake, ambayo Yeye huwataka wawe mawakili waaminifu kwa hayo makao (miili). Wanahitaji kuvutiwa na ile Kweli itolewayo katika Maandiko Matakatifu: — Ministry of Healing, 146.

“Anza kufanya kazi ya umishenari wa tiba kwa vitu ulivyo navyo kwanza, ili usipate usumbufu. Utangundua kwamba hapo ndipo njia itafunguliwa kwako kufanya usomaji wa Biblia. Baba wa Mbinguni atakuunganisha wewe katika uhusiano na wale wanaohitaji kujua jinsi ya kuwatendea wagonjwa wao. Weka katika vitendo kile unachojua kuhusu tiba ya ugonjwa. Hivyo mateso yatatulizwa, na utapata nafasi ya kuumega mkate wa uzima kwa roho zenye njaa kali.” —A Call to Medical Evangelism, 26.

(Orodha ya tiba ya maji na maandalizi ya miti-shamba (herbs) kwa matatizo mbalimbali imetolewa: “Kuna tiba nyingi rahisi zaidi ambazo zitafanya mengi ili kurejesha hatua za kiafya kwa mwili. Maandalizi haya yote rahisi ambayo Bwana anatarajia tuyatumie sisi wenyewe, lakini pale mwanadamu anapoishiwa uwezo, ndio nafasi ya Mungu inaanzia. Ikiwa tutapuuza kufanya kile ambacho kipo ndani (kinaweza kufikiwa) ya kila familia, na kumwomba Bwana aondoe maumivu wakati sisi ni wavivu pia kutumia dawa hizi ndani ya uwezo wetu, hii inamaanisha ni ujuvi, yaani dhana tu isiyo na mantiki au hata pengine ni kiburi (presumption). 2 Selected Messages, 297.

“Bwana ametoa baadhi ya mitishamba rahisi ya shambani ambayo nyakati fulani huwa na manufaa; Na ikiwa kila familia ingeelimishwa jinsi ya kutumia mimea hii wakati wa ugonjwa, mateso mengi yanaweza kuzuiwa, na hakuna daktari atakayehitajika kuitwa. Mimea hii ya kizamani, sahili, ingetumiwa kwa akili, ingeweza kuponya wagonjwa wengi ambao wamekufa kwa kutumia dawa zenye sumu.”—Letter 82, 1897

“Kiasi kikubwa cha wema kinaweza kufanywa kwa kuwaelimisha wote ambao tunaweza kufikiwa, na kwa njia bora zaidi, si tu za kuponya wagonjwa, bali pia kuzuia magonjwa na mateso.” —Counsels on Health, 451.

“Na kazi hiyo ilipoendelea, tuliagizwa kwamba mahali tutapata majaliwa kwa kupata mahali panapofaa, ambapo tungeweza kuwaleta wagonjwa na wanaoteseka ambao hawakujua lolote kuhusu watu wetu na mambo kidogo tu yahusuyo Biblia, na hivyo kuwafundisha jinsi ya kurejesha afya kwa mbinu za tiba zenye busara bila ya kutumia dawa zenye sumu, na wakati huo huo tukiwahudimia kwa mambo ya kiroho yenye kuinua.”—Counsels on Health, 469.

Kusanya wafanyakazi ambao wana bidii ya kweli ya kimishenari, na waruhusu wasonge mbele ili kueneza nuru na maarifa mbali na karibu. Hebu wachukue kanuni hai za matengenezo ya afya na kwenda katika jamii ambazo kwa kiasi kikubwa hazijui kanuni hizi. Hebu madarasa yaanzishwe, na maagizo yatolewe kuhusu matibabu ya magonjwa. — Shuhuda kwa Kanisa 8: 148.

Ugonjwa unaopasa kueleweka (Counsels on Health, 366). Wafunze wanafunzi katika mbinu za kuponya wagonjwa (Counsels on Health, 301). Watendakazi wote wa Injili wanapaswa kujua jinsi ya kutoa na kufundisha tiba rahisi (Counsels on Health, 389).

[4] -ELEKEZA KUHUSU MATENGENEZO YA LISHE

Maskini wanapaswa kufundishwa kula chakula chenye lishe zaidi (9Testimonies, 163; Counsels on Health, 137). Lengo la maelekezo katika matengenezo ya lishe (Ministry of Healing, 146; 7Shuhuda, 116; Counsels on Health, 389, 482). Maelekezo ya matengenezo ya lishe yatatolewa nyumbani na shuleni (Education, 202-206).

[5] - WEKA AKILINI LENGO KUU LA MATENGENEZO

Madhumuni ya matengenezo ya afya ni kupunguza mateso na magonjwa (2Testimonies, 45; Counsels on Health, 531). Madhumuni ya matengenezo ya afya ni kuwaokoa wengi kutokana na kuzorota kimwili, kiakili na kimaadili (6Testimonies, 378). Madhumuni ya mageuzi ya afya ni kuleta afya ya kimwili na kiroho (1Testimonies, 546). Kusudi la matengenezo ni kuandaa akili kwa ajili ya kupokea Ukweli (Counsels on Health, 22). Madhumuni ya matengenezo ya afya ni maendeleo ya juu zaidi ya mwili, akili, na roho (Ministry of Healing, 146) Matengenezo ya afya yanatolewa ili kusaidia katika maandalizi ya kuja kwa Kristo (Shuhuda 1, 486-488, 559; shuhuda 3, 161-165; Counsels on Health, 20-21).

[6] - ONYESHA KWAMBA SHERIA ZA MUNGU ZIMEUNDWA KWA MANUFAA YETU

Sheria za afya zimejumuishwa katika sheria za Mungu (3Shuhuda, 165; Counsels on Health, 25). Dini ya kweli inaendana na sheria za afya (4Shuhuda, 554; 7Shuhuda, 137; Counsels on Health, 445, 480). Afya ni thawabu ya utii kwa sheria za asili (Ministry of Healing, 127). Kuzingatia sheria za afya ni baraka isiyokadirika (Ministry of Healing, 147; Education, 201; Counsels on Health, 40). Sheria za kimwili ni sheria za Mungu (6 Shuhuda 373). Sheria za nafsi zetu ziko katika kiwango sawa na Amri Kumi—ni dhambi kubwa kuvunja moja kama kuvunja nyingine (2Shuhuda, 70; 3Shuhuda, 161; Counsels for Parents, Teachers, and Students, 295; Counsels on Health, 40). Utiifu kwa sheria za maisha

huhakikisha afya (Counsels on Health, 49). Sheria za asili ni sheria za Mungu (Ministry of Healing, 113, 146; Education, 99, 196; 5Shuhuda, 445; 6Shuhuda, 369; Counsels on Health 325, 389, 390). Kuweka wazi sheria za asili huambatana na ujumbe wa malaika wa tatu (3 Shuhuda, 161).

Utiifu kwa sheria za asili hutuzwa na— Afya ya Kimwili na Akili (Ministry of Healing, 127). Inakuza furaha katika maisha haya (Ministry of Healing, 146; Education, 103; Counsels on Health, 286, 390). Hutuzwa na asili kwa nguvu na uzuri (Prophets na Kings, 485). Kufurahia kwetu kote maisha kunafuatiliwa hadi kwenye utii wetu au uvunjaji wa sheria ya asili (3Testimonies, 161). Sheria za afya hukuza umbo la mwanadamu kwa uzuri (Ministry of Healing, 292). Hutengeneza angahewa la uzima kuhusu nafsi (6Testimonies, 371). Husaidia katika Maandalizi ya Maisha ya Baadaye (Ministry of Healing, 146: Counsels on Health, 386, 390). Njia ya utii kwa sheria za asili ni njia ya moja kwa moja kwenda mbinguni (Counsels on Health, 222).

[7] - KUHIMIZA WATU KUSOMA KIUMBE HICHO CHA AJABU, MFUMO WA MWANADAMU, NA SHERIA AMBAZO ZINAUONGOZA

Sheria ya kimwili ya Mungu imeandikwa kwa kidole chake mwenyewe juu ya kila neva, msuli, na kitivo cha mwili au uwezo wowote ule wa mwanadamu (Education, 196- 197; Counsels on Diet and Food, 17). Ujinga wa fiziolojia umewaleta wengi kaburini (Fundamentals of Christian Education, 321). Watoto wanapaswa kuelewa fiziolojia (Ministry of Healing, 402; Education, 196; 7 Testimonies, 65). Elimu yetu inapaswa kujumuisha maarifa kamili ya fiziolojia kadri iwezekanavyo (Education, 195-201; Counsels for Parents, Teachers and Students, 295). Utafiti wa fiziolojia unapaswa kuwatia moyo wanafunzi kumcha Mungu (Education, 201).

[8] - WAONYESHE USHAHIDI WA UPENDO WA MUNGU, HEKIMA NA WEMA WA SHERIA ZAKE, NA MATOKEO YA UTII.

Tunapaswa kufuata njia ya Yesu. Kwanza, alihudumia mahitaji ya kimwili ya watu (alilisha, aliwavisha, na aliwaponya); Kisha, imani na upendo wao vilivutwa Kwake. Alihudumia mahitaji yao ya kiroho (akawaletea msamaha wa dhambi, na kuwafungulia zile Kweli kuu za Biblia).

“Kazi ya umishenari wa tiba ndiyo kazi inayotangulia injili, mlango ambao Ukweli kwa wakati huu utapata upenyo wa nyumba nyingi. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa wamishenari wa wa tiba wa dhati, kwa kuwa wanapaswa kujifunza kuhudumia mahitaji ya nafsi na mwili. Kutokuwa na ubinafsi bila hila na unyofu

wa moyo, kunapaswa kuonyeshwa na watendakazi wetu kwani, kwa ujuzi na uzoefu unaopatikana kwa kazi ya vitendo, wanatoka kwenda kutoa matibabu kwa wagonjwa. Pale wanapoenda nyumba kwa nyumba wataifikia mioyo mingi. Wengi watafikiwa ambao vinginevyo hawangesikia ujumbe wa injili. Welfare Ministry, 125.

“Watu wa Mungu wanapaswa kuwa wamishenari wa kweli/dhati wa tiba. Wanapaswa kujifunza kuhudumia mahitaji ya nafsi na mwili. Wanapaswa kujua jinsi ya kutoa matibabu rahisi ambayo hufanya mengi ili kupunguza maumivu na kuondoa magonjwa……. Wanapaswa kufahamu kanuni za matengenezo ya afya, ili waweze kuwaonyesha wengine jinsi ya kuenenda, kwa mazoea sahihi ya kula, kunywa, na kuvaa, magonjwa yanaweza kujizuia na afya kurejeshwa. Onyesho la thamani la kanuni za matengenezo ya afya litafanya mengi katika kuondoa chuki dhidi ya kazi yetu ya Kiinjilisti. Tabibu mkuu, mwanzilishi wa kazi ya umishenari wa tiba, atambariki kila mtu ambaye atasonga mbele kwa unyenyekevu na uaminifu, akitafuta kueneza Ukweli wa wakati huu. –Welfare Ministry, 127.

“Sura ya hamsini na nane ya Isaya (58) ina Ukweli wa sasa kwa watu wa Mungu. Hapa tunaona jinsi kazi ya umishenari wa tiba na huduma ya injili zinavyopaswa kufungwa pamoja kama ujumbe unaotolewa kwa ulimwengu. Juu ya wale wanaoshika Sabato ya Bwana kuna jukumu la kufanya kazi ya rehema na fadhili. Kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kufungwa pamoja na ujumbe, na kugongwa muhuri kwa muhuri wa Mungu.”— Welfare Ministry, 121.

"Mkono wa kuume hutumika kufungua milango ambayo mwili unaweza kupata pa kuingilia. Hii ndiyo sehemu ambayo kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kutenda. Kwa kiasi kikubwa ni kuandaa njia ya kupokea Ukweli kwa wakati huu. Mwili usio na mikono hauna maana.” —Welfare Ministry, 122-123.

2 - MANENO KWENYE PICHA HUONYESHA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA

Ni onyesho la kazi ya vitendo ya injili (Ministry of Healing, 144; 6Shuhuda , 240-241, 289; 8Shuhuda, 77, 168). Ni upenyo kwa ajili ya ukweli (Ministry of Healing, 144-145; Shuhuda 6, 293; 7Shuhuda , 59, 272: 9Shuhuda, 167; Counsels on Health, 27, 499-500). Tafsiri ya Injili (Counsels on Health, 498). Inafungua milango ya Ukweli (7 Testimonies, 62; Counsels on Health, 425). Inashinda ubaguzi (9Shuhuda9, 34, 211; Counsels on Health, 430,497, 532).

Ni mkono wa kuume wa ujumbe (Shuhuda 6, 241, 288-293; 7Shuhuda, 59; 9Shuhuda, 220; Counsels on Health, 288, 293; 7 Shuhuda, 59). Inapaswa kufanywa kama sehemu ya Injili (6 Testimonies, 292). Ni Injili inayotekelezwa

kwa vitendo (8Shuhuda, 168). Ni Injili katika kielelezo (6Shuhuda, 241). Imefungwa na Kristo kwa Injili (8Shuhuda, 46, 168). Ni nakala kamili ya muundo wa huduma tuliyopewa na Yesu tukiwa hapa duniani (Welfare Ministry, 116-124). Imeainishwa katika Agizo la Kristo kwa wanafunzi Wake (8 Testimonies, 203-204; Counsels on Health, 509).

3 – MATIBABU YA WAGONJWA: MUHTASARI WA SOMO LA KITABU CHA HUDUMA YA UPONYAJI 126-128

[1] - WAFUNDISHE WATU KWAMBA DAWA ZENYE SUMU HAZITIBU, LAKINI HUBADILISHA TU MUUNDO AU ENEO LA UGONJWA

Watu wanatakiwa kufundishwa kuwa dawa hazitibu au kuponya magonjwa. Ni kweli kwamba nyakati fulani zinaleta nafuu ya muda mfupi, na mgonjwa huonekana kupata nafuu kama matokeo ya dawa hizo; hii ni kwa sababu maumbile ya asili yana nguvu hai ya kutosha kupambana na kuondoa sumu na kisha kurekebisha hali zilizosababisha ugonjwa huo. Afya inarejeshwa licha ya kutokuwa na dawa. Lakini katika kesi nyingi mengi ya kuugua, dawa hubadilisha tu sura na eneo la ugonjwa huo. Mara nyingi athari ya sumu itokanayo na madawa kwa muda huonekana kama haipo, lakini matokeo hubakia kwenye mfumo na hufanya madhara makubwa katika kipindi fulani cha baadaye. Kwa kutumia dawa zenye sumu, wengi hujiletea wenyewe magonjwa ya kudumu maishani mwao, na watu wengi wamepoteza maisha yao, ambao wangeweza kuokolewa kwa kutumia njia za asili za uponyaji. Sumu zilizomo katika dawa nyingi ziitwazo tiba huunda tabia na hamu ya kula ambayo inamaanisha uharibifu kwa roho na mwili. Nyingi ya dawa hizi maarufu za nostrum, zinazoitwa dawa za kaunta ambazo hazihitaji maagizo au maelekezo ya tiba toka kwa daktari unapotaka kununua (non-Prescription drugs-Rx) na hata baadhi ya dawa zinazotolewa na waganga (za famasia zinazoitwa dawa za magharibi au za wazungu), hushiriki katika kuweka msingi wa tabia ya uraibu wa vileo, wa bangi, uraibu wa mofini, ambazo ni laana mbaya sana kwa jamii (dawa nyingi za maumivu zitumiwapo baada ya muda hujenga uraibu maana ni vileo- narcotic). — Ministry of Healing, 126-127.

[2] - WAFUNDISHE WATU KWAMBA UPONYAJI WA KWELI UNATOKANA NA KUONDOLEWA KWA UCHAFU NA KWA UTIIFU KWA SHERIA ZA ASILI.

Tumaini pekee la mambo yaliyo bora ni katika kuwaelimisha watu kanuni sahihi. Hebu waganga wawafundishe watu kwamba nguvu za urejeshwaji hazipo katika madawa, bali katika asili. Ugonjwa ni juhudi ya maumbile ya asili ya kuuweka mfumo huru kutoka kwenye hali iliyosababishwa na ukiukaji wa sheria za afya.

Pale mtu anapopatwa na ugonjwa, sababu ya kuja kwa huo ugonjwa inapaswa kutambuliwa-kueleweka. Tabia mbaya yafaa zibadilishwe. Mazoea mabaya yarekebishwe. Kisha asili inapaswa kusaidiwa katika juhudi zake za kuondoa uchafu mwili na kuweka upya hali sahihi katika mfumo. —Ministry of Healing, 127.

[3] - WAFUNDISHE WATU SHERIA NANE ZA TIBA ASILI NA JINSI YA KUZITUMIA- (Eight remedies, eight doctors-NEWSTART).

Hewa safi, mwanga wa jua, kuwa na kiasi, pumziko, kufanya mazoezi, chakula kinachofaa, matumizi ya maji, kumtumaini Mungu na uweza Wake—hizi ndizo tiba za kweli. Kila mtu apaswa kuwa na maarifa ya vitu vya asili viletavyo uponyaji na jinsi ya kuyatumia maarifa hayo (azifahamu tiba nane rahisi na kuzitumia, ikiwemo usafi, usafi, roho ya shukrani, kilimo, roho ya shukrani, mtazamo wa maisha, na kuhudumia watu). Ni muhimu pia kuelewa kanuni zinazohusika katika tiba ya wagonjwa na kuwa na uzoefu wa vitendo utakaomwezesha mtu kutumia ujuzi huo kwa njia ifaayo.

Matumizi ya tiba za asili yanahitaji kiasi kikubwa cha uangalifu na jitihada, mambo ambayo wengi hawako tayari kuyafanyia kazi. Mchakato wa asili wa uponyaji na kuujenga mwili tena pale ulipoharibika ni wa taratibu ila una uhakika, na kwa wale wasio na subira, huona mambo yanaenda polepole sana kwao. Kusalimisha vile vitu vinavyoendekezwa au kujifurahisha navyo kunahitaji kujitoa kafara. Lakini mwishowe itagunduliwa kwamba asili, isipozuiwa, hufanya kazi yake kwa busara na kwa ubora. Wale wanaodumu katika kuzitii sheria zake watavuna thawabu katika afya ya mwili na akili —Ministry of Healing, 127.

[4] - WAFUNDISHE WATU JINSI YA KUEPUKA MAGONJWA KWA KUTII SHERIA ZA UZIMA ZINAZOONGOZA MWILI WA MWANADAMU

Kwa ujumla, watu hutoa umakini mdogo sana katika kuzingatia suala la afya. Ni bora kuzuia ugonjwa kuliko kujua jinsi ya kuutibu wakati umeupata (Kinga ni bora kuliko tiba au kuzuia ni bora kuliko kuponya).

Ni jukumu la kila mtu, kwa ajili yake mwenyewe, na kwa ajili ya jamii ya ubinadamu, kujielimisha mwenyewe kuhusu sheria za afya na kudhamiria kuzitii. Kila mtu anahitaji kuelewa ule mwili ushangazao kuliko miili ya viumbe vyote, yaani mwili wa binadamu. Watu wanapaswa kuelewa kazi za viungo mbalimbali vya mwili na jinsi vinavyotegemeana, kiungo kimoja kinategemea kiungo kingine kwa ajili ya utendaji kazi mzuri wa viungo vyote. Wanapaswa kujifunza ushawishi wa akili juu ya mwili, na wa mwili juu ya akili, na sheria ambazo zinaendesha na kusimamia mwili na akili ya mwanadamu.—Ministry of Healing, 128.

[5] - WAFUNDISHE WATU KWAMBA UTII WAO KWA SHERIA HIZI ZA KIMWILI UTAAMUA KWA KIASI KIKUBWA HATIMA YAO YA MILELE.

Hatuwezi kukumbushwa mara nyingi kwamba afya haiji kwa bahati nasibu. Afya ni matokeo ya utii wa sheria. Jambo hili linatambuliwa na wanamichezo wanaoshindana katika riadha na mashindano mengine ya michezo ya nguvu (mieleka, masumbwi, kuogelea, kusketi kwenye theluji n.k). Watu hawa hufanya maandalizi makini. Hujisalimisha kwenye mafunzo ya kina na nidhamu ya hali ya juu. Kila mazoea ya mwili hudhibitiwa kwa uangalifu. Wanajua kwamba kupuuzia, kutokuwa na kiasi kwa kufanya vitu kupita kiasi, au uzembe na kutegea, hudhoofisha au kulemaza kiungo cha mwili au utendaji wa mwili, na hali hii ingeleta kushindwa katika shindano. Je, ni muhimu jinsi gani basi kuwa na uangalifu kama huo ili kuhakikisha tunapata mafanikio katika makabiliano ya maisha. Sisi hatuko katika maigizo (hatuko kwenye drama au movie). Twapigana vita halisi kila siku ambayo ndiyo itakayoamua matokeo yetu kwa umilele. Twakutana na maadui wasioonekana. Malaika waovu wanajitahidi kumdhibiti kila mwanadamu. Chochote kinachodhuru afya, sio tu hupunguza nguvu za kimwili, lakini pia huelekea kwenye kudhoofisha nguvu za akili na maadili. Kuendekeza mazoea yoyote yasiyo ya afya hufanya iwe vigumu kwa mtu kutofautisha kati ya mema na mabaya, na hivyo kufanya mambo yawe magumu zaidi katika kuupinga uovu. Hali hii huongeza hatari ya kushindwa na kufeli. —Ministry of Healing, 128.

SURA YA 14

HATUA KUMI ZINAZOPASWA KUFUATWA KATIKA UREJESHAJI WA AFYA

Mwongozo wa uponyaji wa kiungu

HATUA KUMI KATIKA UPONYAJI WA KIUNGU

Dhambi na magonjwa zimetokana na uvunjaji wa sheria za Mungu. Kama unataka afya ya kimwili lazima utii sheria nane za Mungu za afya. Kama unataka afya ya kiroho, lazima utii sheria kumi za maadili za Mungu.

Mungu hatawarudishia afya wale wanaotamani tu ili tu waendelee kutenda dhambi na kumvunjia heshima Muumba wao. Kupenda utii ni kupenda afya na uzima. Kupenda dhambi ni kupenda kuzorota, kuhaharibikiwa na kifo. Mungu hatatuepusha na kile tunachotafuta.

Huu ndio uamuzi mkubwa basi, ambao lazima uufanyie kazi, Je, uko tayari kujikana nafsi na kutii sheria zote za Mungu? Ikiwa ndivyo, basi hatua kumi zifuatazo za afya ni kwa ajili yako.

1- NENDA KWA TABIBU MKUU - KWA MAANA NI MUNGU PEKEE —NDIYE ANAYEWEZA KUPONYA

“Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana. Naam, vyote vilivyo ndani yangu Vilihimidi Jina Lake takatifu. Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana, Wala usizisahau fadhili Zake zote. Akusamehe maovu yako yote, Akuponya magonjwa yako yote, Aukomboa uhai wako na kaburi, Akutia taji ya fadhili na rehema, Aushibisha mema uzee wako, Ujana wako ukarejezwa kama tai.” Zaburi 103:1-5

“Nanyi mtamtumikia Bwana, Mungu wenu, Naye atakibarikia chakula chako, na maji yako; nami nitakuondolea ugonjwa kati yako.” Kutoka 23:25

“Ugonjwa, mateso, na kifo ni kazi ya nguvu pinzani. Shetani ni mharibifu; Mungu ni Mrejeshaji.”—Medical Ministry, 11.

“Yesu Kristo Ndiye mponyaji Mkuu, lakini anatamani kwamba kwa kuishi kulingana na sheria Zake, tunaweza kushirikiana Naye katika uponyaji na kudumisha afya…..

“Hatuwezi kuponya. Hatuwezi kubadilisha hali ya ugonjwa wa mwili. Lakini ni sehemu yetu, kama wamishenari wa tiba, kama watendakazi pamoja na Mungu,

kutumia njia ambazo Yeye ametoa. Kisha tunapaswa kuomba kwamba Mungu atabariki njia (mawakala) hizi. Tunamwamini Mungu; Tunaamini katika Mungu anayesikia na kujibu maombi."—Medical Ministry, 13.

"Nguvu za Mungu za uponyaji zipo kwenye asili yote. Mfano mwanadamu anapokata nyama yake au kuvunja mfupa, asili mara moja huanza kuponya jeraha, na hivyo kurejesha afya na uzima wa mtu. Lakini mwanadamu anaweza kujiweka katika nafasi ambayo asili inazuiwa na isiweze kufanya kazi yake. . . Ikiwa mtu atatumia tumbaku . . Nguvu ya uponyaji ya asili itakuwa imedhoofishwa kwa kiwango kikubwa au kidogo. Wakati kileo kinapotumiwa, mfumo huo hauwezi kustahimili magonjwa katika uwezo wake wa asili uliopewa na Mungu, aliye mponyaji. Ni Mungu, Ndiye ambaye hitaji hilo kwamba asili ifanye kazi kurejesha nguvu zilizochoka. Nguvu ni ya Mungu. Yeye Ndiye Mponyaji Mkuu."—Medical Ministry, 11-12.

2- MWOMBE AKUPONYE, IKIWA NI MAPENZI YAKE

"Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Bwana atamwinua; hata ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa. Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii." Yakobo 5:15-16

"Akisema, Ee Baba, ikiwa ni mapenzi Yako, uniondolee kikombe hiki; walakini si mapenzi yangu, bali Yako yatendeke." Luka 22:42

"Niliona sababu ya Mungu kutosikia maombi ya watumishi Wake kwa ajili ya wagonjwa waliopo miongoni mwetu kikamilifu zaidi ni kwamba Yeye hangeweza kutukuzwa kwa kufanya hivyo wakati walikuwa wakikiuka sheria za afya. Na pia niliona kwamba alipanga kuwepo kwa Matengenezo ya Afya na Taasisi ya Afya ili kuandaa njia ya maombi ya imani kujibiwa kikamilifu. Imani na matendo mema yanapaswa kwenda sambamba katika kuwaokoa walioteswa walio miongoni mwetu, na katika kuwafanya wafae katika kumtukuza Mungu hapa duniani, na kuokolewa wakati wa kuja kwa Kristo……..

"Mtu yeyote asidhani kwamba Taasisi ni mahali pao kuja kuinuliwa kwa maombi ya imani. Hapa ni mahali pa kupata nafuu kutokana na magonjwa kwa njia ya tiba, na kanuni/mazoea sahihi za kuishi, na kujifunza jinsi ya kuepuka magonjwa. ……

Wale wanaowatibu wagonjwa wanapaswa kusonga mbele katika kazi yao muhimu kwa kumtegemea Mungu kwa nguvu kwa ajili ya baraka Zake ili kuzifikia njia ambazo Yeye ametoa kwa neema, na ambazo kwa rehema anatutaka tuonyeshe

usikivu wetu kama vile, hewa safi, usafi, lishe bora, muda unaofaa kufanya kazi na pumziko na matumizi ya maji." —Counsels on Health, 274.

Ni kazi bure, naam kazi iliyopotea, kuwafundisha watu kumtazama Mungu kama mponyaji wa udhaifu wao, mpaka wafundishwe kuacha mazoea yasiyofaa. Ili kupokea baraka Zake katika jibu la maombi, ni sharti waache kutenda maovu na kujifunza kutenda mema. Mazingira yao lazima yawe masafi, mienendo yao maishani iwe sahihi. Ni sharti waishi kwa kupatana na sheria ya Mungu, ya asili na ya kiroho. Kwa wale wanaotamani maombi kwa ajili ya kurejeshewa afya, inapaswa wafahamishwe wazi kwamba uvunjaji wa sheria ya Mungu, iwe ya asili au ya kiroho, ni dhambi, na kwamba ili wao wapate baraka Zake, dhambi lazima iungamwe na kuachwa. —Ministry of Healing, 227-228.

Katika kuwaombea wagonjwa ikumbukwe kwamba "Sisi hatujui kuomba jinsi itupasavyo." Warumi 8:26. Sisi Hatujui ikiwa mbaraka tunayotamani itatufaa au la, itakuwa bora au la. Hivyo maombi yetu yanapaswa kujumuisha wazo hili: "Bwana, Wewe wajua kila siri ya nafsi. Unawafahamu watu hawa. Yesu, Wewe uliye Mtetezi wao, ulitoa maisha Yako kwa ajili yao. Upendo Wako kwao ni mkuu kuliko wetu unavyoweza kuwa. Kwa hivyo, hivyo kwa ajili ya utukufu wako na nia njema ya watesekao, twaomba, katika Jina la Yesu, ili waweze kurejeshwa kwenye afya njema. Ikiwa si mapenzi Yako warejeshwe, twaomba neema Yako iwafariji na uwepo Wako uwe nao katika kuteseka kwao." — Ministry of Healing, 229-230.

3- AMINI KWAMBA YEYE ATAKUPONYA IKIWA ANAONA KUWA NI BORA ZAIDI

"Yesu akageuka, akamwona, akamwambia, Jipe moyo mkuu, binti yangu; imani yako imekuponya. Yule mwanamke akapona tangu saa ile." Mathayo 9:22

"Umkabidhi Bwana njia yako, Pia umtumaini, Naye atafanya." Zaburi 37:5

"Ikiwa watachukua msimamo kwamba katika kuomba kwa ajili ya uponyaji hawapaswi kutumia tiba rahisi zinazotolewa na Mungu ili kupunguza maumivu na kusaidia mwili katika kazi yake, wakidhani kuwa hicho ni kitendo ni kuikana imani, wanachukua msimamo usio wa hekima. Kufanya hivi sio kuikana imani; Inapatana kabisa na mipango ya Mungu. Hezekia alipokuwa mgonjwa, nabii wa Mungu alimletea ujumbe kwamba atakufa. Alimlilia Bwana, na Bwana akamsikia mtumishi Wake, na kufanya muujiza kwa niaba yake, akimtumia ujumbe kwamba aongezewe miaka kumi na tano ya kuishi kwake. Sasa Neno moja kutoka kwa Mungu, mguso mmoja wa kidole cha Bwana, ungemponya Hezekia papo hapo, lakini maagizo ya pekee yalitolewa kuchukua mtini na kuuweka juu ya sehemu

iliyoathiriwa, na Hezekia akawa mzima. Katika kila kitu tunapaswa kwenda kutokana na majaliw aa Mungu” —Counsels on Health, 380-382.

Orodha ya tiba ya maji na maandalizi ya mitishamba kwa matatizo mbalimbali imetolewa: “Kuna tiba nyingi rahisi zaidi ambazo zitafanya mengi katika kurejesha hatua za kiafya kwa mwili. Maandalizi haya yote rahisi ni yale ambayo Bwana anatarajia tuyatumie sisi wenyewe, lakini pale mwanadamu anapoishia ndio nafasi ya Mungu inaanzia. Ikiwa tutapuuza kufanya kile ambacho kipo ndani ya uwezo wetu kufikiwa katika kila familia, na kumwomba Bwana aondoe maumivu wakati sisi ni wavivu pia kutumia dawa hizi ndani ya uwezo wetu, hii inamaanisha ni ujuvi tu au dhana tu isiyo na mantiki (presumption). 2 Selected Messages, 297.

“Tumeungana katika maombi ya dhati kuzunguka kitanda cha wagonjwa wanaume, wanawake, na watoto, na tumehisi kwamba walirudishwa kwetu kutoka kwa wafu kama jibu la maombi yetu ya dhati. Katika maombi haya tulifikiri tulipaswa kuwa chanya, na tukitumia imani, hivyo ilitupasa kuomba mgojwa aishi, yaani uzima tu, na sio kitu chochote isipokuwa uzima. Hatukuthubutu kusema, ‘Ikiwa itamtukuza Mungu,’ tukihofia ni kuonyesha kwamba tunatilia mashaka. Tumewatazama kwa fadhaa wale ambao wamerudishwa kwetu kutoka kwenye ugonjwa, kana kwamba wametoka kwa wafu. Tumeona baadhi ya hawa, hasa vijana, wakinyanyuliwa toka vitandani, na kupatiwa afya, na wamemsahau Mungu, wengine wenye maadili machafu katika maisha, na kusababisha huzuni na uchungu kwa wazazi na marafiki, na wamekuwa aibu kwa wale walioogopa kuomba. Hawakuishi kwa kumheshimu na kumtukuza Mungu, bali kumlaani kwa maisha yao maovu.

“Hatupaswi kuwekaa chini mipango yetu, wala tusitafute kumleta Bwana kwenye kile tunachotaka sisi. Kama maisha ya wagonjwa yanaweza kumtukuza, tunaomba ya kwamba waishi, hata hivyo, si kama tutakavyo bali atakavyo Yeye. Imani yetu inaweza kuwa thabiti, na yenye kutegemeka zaidi, kwa kukabidhi kila mategemeo yetu kwa Mungu mwenye hekima yote na, na bila wasiwasi, kwa ujasiri kamili wa kumtumainia yote. Tuna ahadi. Tunajua ya kuwa anatusikia tukiomba kulingana na mapenzi Yake.”— Counsels on Health, 378-379.

4 - BADILISHA MAZOEA MABAYA, NA KUTII SHERIA ZA MUNGU

Kutoka 15:26 akawaambia, Kwamba utaisikiza kwa bidii sauti ya Bwana, Mungu wako, na kuyafanya yaliyoelekea mbele zake, na kutega masikio usikie maagizo yake, na kuzishika amri zake, mimi sitatia juu yako maradhi yo yote niliyowatia Wamisri; kwa kuwa Mimi ndimi Bwana nikuponyaye.

“Nanyi mtamtumikia Bwana, Mungu wenu, Naye atakibarikia chakula chako, na maji yako; Nami nitakuondolea ugonjwa kati yako.” Kutoka 23:25

Afya haiji kwa bahati nasibu. Afya ni matokeo ya utii wa sheria.—Ministry of Healing, 128.

Kushindwa kutunza mashine hai ni tusi kwa Muumbaji. Kuna sheria za kimbingu zilizowekwa ambazo kama zikitunzwa zitawakinga wanadamu na magonjwa na vifo vya mapema. —Counsels on Diet and Foods, 16.

Mungu kwa kweli Ndiye Mwandishi wa sheria za mwili sawa kama alivyo mwandishi wa sheria za maadili. Sheria Yake imeendikwa kwa chanda Chake Mwenyewe katika kila mshipa wa fahamu, katika kila msuli na katika kila uwezo wa akili na mwili, ambavyo vimekabidhiwa kwa mwanadamu.

Muumbaji wa mwanadamu amepangilia mashine hai ya miili yetu. Kila kazi imefanywa kwa jinsi ya ajabu na kwa hekima. Na Mungu aliahidi Mwenyewe kuitunza mashine hii ya mwanadamu katika hali ya utendaji wa kiafya endapo wakala wa kibinadamu atatii sheria Zake na kushirikiana na Mungu. Kila sheria iongozayo mfumo wa utendaji kazi wa mwanadamu inapaswa izingatiwe kabisa kwamba ni ya Kiungu hasa katika asili katika tabia na katika umuhimu kama Neno la Mungu lilivyo. Kila uzembe au kutokuwa makini, kila tendo la unyanyasaji wa mwili na utendaji wowote mbaya unaofanywa juu ya mashine hii ya ajabu kwa kutojali sheria Zake maalumu katika makazi (au mwili) ya mwanadamu, ni uvunjaji wa sheria ya Mungu. Tunaweza kutazama na kupendezwa na kazi ya Mungu katika ulimwengu wa asili, lakini makazi (au mwili) ya mwanadamu ni ya ajabu zaidi. [Dhambi ya kufuata njia ambayo hutumia nguvu au kutia giza ubongo pasipo uhitaji Kwa hakika ni dhambi kuvunja sheria za miili yetu kama ilivyo kuvunja amri kumi. Kufanya hivyo ni kuvunja sheria za Mungu. Wale wanaoasi sheria ya Mungu katika miili yao, watakuwa wamejiweka katika uvunjaji wa sheria ya Mungu iliyotangazwa kutoka mlima Sinai.—Counsels on Diet and Foods, 16-17.

“Kuna njia nyingi za kushugulika na sanaa ya uponyaji, lakini ipo njia moja tu ambayo mbingu inaikubali. Dawa zipatikanazo kutoka kwa Mungu ni mawakala wa asili na ambazo hazitaundikia au kudhoofisha mfumo wa mwili kwa sababu ya sifa zake kuu. Hewa safi, maji, usafi, lishe sahihi, mazoezi, mapumzika, maisha safi, na imani thabiti kwa Mungu ni tiba kwa mahitaji mengi ambayo maelfu wanakufa kwa kuzikosa; lakini dawa hizi watu huziona ni zamani na wakati kwa sababu utumiaji na uandaaji wake unahitaji ujuzi/ustadi maalum ambao watu hawauchangamkii. Hewa safi, mazoezi, maji safi, na mahali safi pa kuishi

vinaweza kufikiwa na watu wote kwa gharama ndogo, lakini dawa za hospitali ulimwenguni ni ghali, gharama yake ni kubwa madukani na hata kwa athari inayozalishwa kwenye mifumo yetu ni kubwa pia. -—Counsels on Health, 323.

Tumaini pekee la mambo yaliyo bora ni katika kuwaelimisha watu kanuni sahihi. Waganga wawafundishe watu kwamba nguvu za urejeshwaji hazipo katika madawa, bali katika asili. Ugonjwa ni juhudi ya maumbile ya asili kuuweka mfumo huru kutoka kwenye hali iliyosababishwa na ukiukaji wa sheria za afya. Pale mtu anapopatwa na ugonjwa, sababu ya kuja kwa huo ugonjwa inapaswa kutambuliwa-kueleweka. Tabia mbaya yafaa zibadilishwe. Mazoea mabaya yarekebishwe. Kisha asili inapaswa kusaidiwa katika juhudi zake za kuondoa uchafu mwili na kuweka upya hali sahihi katika mfumo. Hewa safi, mwanga wa jua, kuwa na kiasi, pumziko, kufanya mazoezi, chakula kinachofaa, matumizi ya maji, kumtumaini Mungu na uweza Wake—hizi ndizo tiba za kweli. Kila mtu apaswa kuwa na maarifa ya maumbile ya asili yaletayo uponyaji na jinsi ya kuyatumia (azifahamu tiba nane rahisi na kuzitumia, ikiwemo usafi, roho ya shukrani, mtazamo wa maisha, na kuhudumia watu). Ni muhimu pia kuelewa kanuni zinazohusika katika tiba ya wagonjwa na kuwa na uzoefu wa vitendo utakaomwezesha mtu kutumia ujuzi huo kwa njia ifaayo.

Matumizi ya tiba za asili yanahitaji utunzaji, uangalifu na jitihada kubwa, mambo ambayo wengi watu hawako tayari kuyafanyia kazi. Mchakato wa asili wa uponyaji na kuujenga mwili tena pale ulipoharibika ni wa taratibu ila una uhakika, na kwa wale wasio na subira, huona mambo yanaenda polepole sana kwao. Kusalimisha vile vitu vinavyoendekezwa au kujifurahisha navyo kunahitaji kujitoa kafara. Lakini mwishowe itagunduliwa kwamba asili, isipozuiwa, hufanya kazi yake kwa busara na kwa ubora. Wale wanaodumu katika kuzitii sheria zake watavuna thawabu katika afya zao za mwili na akili. —Ministry of Healing, 127.

5 - KUSAFISHA MWILI

“Unisafishe kwa hisopo nami nitakuwa safi, Unioshe, nami nitakuwa mweupe kuliko theluji” Zaburi 51:7

“Jiosheni, jitakaseni; ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho Yangu; acheni kutenda mabaya” Isaya 1:16

Pale mtu anapopatwa na ugonjwa, sababu ya kuja kwa huo ugonjwa inapaswa kutambuliwa-kueleweka. Tabia mbaya yafaa zibadilishwe. Mazoea mabaya yarekebishwe. Kisha asili inapaswa kusaidiwa katika juhudi zake za kuondoa uchafu mwili na kuweka upya hali sahihi katika mfumo. —Ministry of Healing, 127.

“Maji ni kimiminika bora zaidi kinachoweza kusafisha tishu.”—Healthful Living 90.

"Uchafu wa mwili, ikiwa hautatolewa, hurudishwa ndani ya damu, na kulazimishwa kwenye viungo vya ndani. Mwili, ili utoe uchafu wa hiyo sumu, hufanya jitihada za kuukomboa mfumo. Jitihada hii hupelekea kuwepo kuwa na homa, na ndiyo kile kinachoitwa ugonjwa. Lakini hata hivyo, ikiwa wale wanaoteseka wangeusaidia mwili katika jitihada zake, kwa kutumia maji safi na laini, mateso mengi yangezuiwa. Lakini wengi, badala ya kufanya hivyo, na kutafuta kuondoa sumu kutoka kwenye mfumo, huchukua sumu iliyo ya hatari zaidi kwenye mfumo, ili kuondoa sumu ambayo tayari iko.”— 2 Selected Messages, 460.

"Tiba za Kristo husafisha mfumo. Lakini Shetani amemjaribu mwanadamu kuingiza katika mfumo, tiba inayodhoofisha utendaji wa mfumo wa kibinadamu, kuziba na kuharibu mipango safi na mizuri ya Mungu. Dawa zinazotolewa kwa wagonjwa hazileti uzima, lakini zinaharibu. Dawa za famasia haziponyi. Badala yake, huleta katika mfumo mbegu ambazo huzaa mavuno machungu sana.”—2 Selected Messages, 289.

6 - TUMIA TIBA RAHISI YA MAJI Zaburi 51:1, 7

Ee Mungu, unirehemu, Sawasawa na fadhili Zako. Kiasi cha wingi wa rehema Zako, Uyafute makosa yangu. Unisafishe kwa hisopo nami nitakuwa safi, Unioshe, nami nitakuwa mweupe kuliko theluji

"Kufanya majaribio na dawa za famasia (drugs) ni shughuli ya gharama kubwa sana. Kupooza kwa ubongo na ulimi mara nyingi ni matokeo, na wahasiriwa hufa kifo kisicho cha kawaida, wakati, kama wangetendewa kwa uvumilivu, kwa bidii isiyochoka, isiyo na ulegevu na maji ya moto na baridi, vitambaa vya moto vya kukanda mwili au hydrotherapia, vitambaa au mataulo yenye maji ya moto-moto (packs), na mashuka yenye kudondosha maji, wangekuwa hai leo.”—Medical Ministry, 228.

Katika afya njema na katika kuugua, maji safi ni mojawapo ya baraka bora na za pekee kabisa za mbingu. Matumizi yake sahihi huimarisha afya. Ni kinywaji ambacho Mungu alitupatia ili kutuliza kiu kwa wanyama na mwanadamu. Yakinywewa kwa uhuru kwa jinsi ipasavyo, husaidia kusafirisha mahitaji ya mfumo wa mwili, na kusaidia mwili kukabiliana na magonjwa. Matumizi ya maji kwa nje ya mwili ni mojawapo ya njia rahisi na toshelevu katika kurekebisha mzunguko wa damu (haidrotherapia; maji huosha mwili ndani na nje). Kuoga na maji baridi yaliyotulia kunasaidia mwili uwe mchangamfu. Kuogea maji ya moto

husaidia kufungua matundu ya vinyweleo vya ngozi na hivyo husaidia uondoaji wa uchafu mwilini (takamwili). Kuogea maji ya moto, na maji vuguvugu huzipoza neva na husawazisha mzunguko wa damu. Lakini wengi hawajawahi kujifunza kupitia uzoefu binafsi kuhusu matokeo yenye manufaa ya matumizi sahihi ya maji, na huogopa jambo hili. Tiba ya maji haithaminiwi jinsi inavyopaswa, na ili kuyatumia maji kwa ustadi kuna hitaji la kufanya kazi yenye juhudi, ambayo wengi hawataki kuifanya. Lakini hakuna anayepaswa kuhisi kuwa na kisingizio kwa sababu tu ya ujinga wake au uzembe kuhusiana na jambo hili. Zipo njia nyingi ambazo maji yaweza kutumika ili kutuliza maumivu na kuzuia ugonjwa. Watu wote wapaswa kuwa na utambuzi katika maarifa ya matumizi ya tiba rahisi majumbani mwao. Hasa akina mama, wanapaswa kujua jinsi ya kutunza familia zao katika suala la afya na maradhi. —Ministry of Healing 237.

Tiba ya maji, kwa busara na ustadi, inaweza kuwa njia ya kuokoa maisha ya watu wengi. —Medical Ministry, 227.

“Bwana ametufundisha kwamba ufanisi mkubwa wa uponyaji upo katika matumizi sahihi ya maji. Matibabu haya yanapaswa kutolewa kwa ustadi. Tumeagizwa kuwa katika matibabu yetu kwa wagonjwa tutupilie mbali matumizi ya dawa za famasia. Kuna mitishamba rahisi ambayo inaweza kutumika kwa ajili ya kuponya wagonjwa, ambayo athari yake juu ya mfumo ni tofauti sana na ile ya dawa hizo zinazotia sumu kwenye damu na kuhatarisha maisha.”—2 Selected Messages, 288.

Vitu vya asili ni baraka za Mungu, zinazotolewa ili kuleta afya kwa mwili, akili, na nafsi. Hutolewa ili zilete uzima kwenye uzima, na kwa wagonjwa ili kuwaponya. Vitu hivi vikitumika kwa pamoja na matibabu ya maji, vinafaa zaidi katika kurejesha afya kuliko dawa zote za famasia za hapa duniani.”— Counsels on Health, 169.

7- TUMIA MIMEA RAHISI YA SHAMBA

“Na matunda yake yatakuwa ni chakula; na majani yake yatakuwa ni dawa.” Ezekieli 47:12

“na majani ya mti huo ni ya kuwaponya mataifa.” Ufunuo wa Yohana 22:2

“Huyakuza majani kwa makundi, Na maboga kwa matumizi ya mwanadamu; Ili atoe chakula katika nchi.” Zaburi 104:14

“Bwana ametoa dawa za magonjwa katika mitishamba sahili, na hizi zinaweza kutumiwa kwa imani, bila kukana imani; Kwani kwa kutumia baraka

zinazotolewa na Mungu kwa manufaa yetu tunashirikiana Naye. Yeye Anaweza kutumia maji na jua na mimea ambayo ameruhusu ikue, katika uponyaji wa magonjwa yanayoletwa na uzembe au ajali. Hatuonyeshi ukosefu wa imani tunapomwomba Mungu abariki tiba Zake. Imani ya kweli itamshukuru Mungu kwa ujuzi wa jinsi ya kutumia baraka hizi za thamani kwa njia ambayo itarejesha nguvu za kiakili na kimwili."—2 Selected Messages, 289.

Mungu amewezesha ukuaji wa mimea kutoka ardhini kwa matumizi ya mwanadamu, na ikiwa tunaelewa asili ya mizizi na mimea hii- na kuitumia ipasavyo - hakutakuwa na ulazima wa kukimbilia kwa daktari mara kwa mara, na watu wangekuwa na afya bora zaidi kuliko ilivyo leo. Ninaamini katika kumwita Daktari Mkuu pale tunapokuwa tumeshatumia tiba niliyoitaja. 2 Selected Messages, 297-298.

"Nuru ilitolewa kwamba kuna afya katika harufu ya mtidhari/mpaini (pine), mierezi, na mberoshi. na kuna aina nyingine kadhaa za miti ambayo ina sifa za dawa ambayo inakuza afya. Miti kama hiyo isikatwe ovyo-ovyo."— 2 Messages Selected, 301.

8- MSHUKURU MUNGU KWA REHEMA NA NEEMA YAKE, VYOVYOTE MATOKEO YATAKAVYOKUWA

"Shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu." 1 Wathesalonike 5:18 (Zaburi 103: 1-5, Luka 19: 37, 17: 12-19)

Wakati mtu anapokuuliza Je, unajisikiaje, usijaribu kuchekecha ubongo wako kwa kufikiria ni jambo gani unaweza kumwambia, ambalo ni la kuhuzunisha ili upate huruma yake. Usizungumze juu ya ukosefu wako wa imani, na huzuni na mateso yako. Mjaribu hufurahia kusikia maneno kama hayo. Unapopenda kuzungumzia juu ya mada za kusikitisha, wewe unamtukuza adui. Hatupaswi kupiga kambi kwenye kuelezea nguvu kubwa za Shetani ambazo zitatushinda. Mara nyingi tunajiangusha wenyewe mikononi mwake kwa kuzungumza juu ya uwezo wake. Hebu badala yake sisi tuzungumzie kuhusu uweza mkuu wa Mungu kuyafunga maslahi yetu yote pamoja na maslahi Yake Mwenyewe. Elezea juu ya uwezo wa Kristo usio na kikomo, na kisha uongee juu ya utukufu Wake.—Ministry of Healing, 253.

Fungua mlango wa moyo wako kwa upendo Wake, na uruhusu utiririke kwa wengine. Kumbuka kwamba wanadamu wote wana mitihani ambayo ni migumu kuibeba, yaani majaribu ambayo ni magumu kuyapinga, na wewe unaweza kufanya jambo fulani ili kupunguza mizigo hii. Onyesha shukrani kwa baraka ulizo

nazo; onyesha kuthamini umakini unaopokea kutoka kwa watu. Sheheni moyo wako kwa ahadi za thamani za Mungu, ili uweze kutoa kutoka kwenye hazina hii maneno ambayo yatakuwa faraja na nguvu kwa wengine. Hii itakufanya uzungukwe kwa hali ambayo itakuwa ya msaada na ya kuinua kwako.—Ministry of Healing, 257.

Hakuna ulimi unaoweza kuelezea, hakuna akili yenye ukomo inayoweza kufikiria baraka inayotokana na kuthamini wema na upendo wa Mungu. Hata humu-humu duniani, twaweza kuwa na furaha kama chemchemi yenye utajiri, isiyopungua kamwe, kwa sababu inalishwa maji na vijito vinavyotiririka kutoka kwenye kiti cha enzi cha Mungu. Basi na tuelimishe mioyo na midomo yetu kunena sifa za Mungu kwa upendo Wake usio na kifani.

Hebu na tuelimishe roho zetu kuwa na matumaini na kukaa katika nuru inayoangaza kutoka kwenye msalaba wa Kalvari. Kamwe tusisahau kwamba sisi ni watoto wa Mfalme wa mbinguni, wana na binti za Bwana wa majeshi. Ni fursa yetu kuwa na utulivu endelevu katika Mungu. —Ministry of Healing, 253

9- ENDELEA KUMWAMINI NA KUTII Sheria Zake Yohana 5:8, 14

Yesu akamwambia, Simama, jitwike godoro lako, uende. Baada ya hayo Yesu akamkuta ndani ya hekalu, akamwambia, Angalia, umekuwa mzima; usitende dhambi tena, lisije likakupata jambo lililo baya zaidi. (Kutoka 15:26)

Tujapoomba uponyaji kwa mgonjwa, haijalishi hatima ya hali ya mgonjwa itakuwaje, hebu tusipoteze imani kwa Mungu. Ikiwa tunaitwa kukutana na msiba, tupokee kikombe hiki kichungu, tukikumbuka kwamba mkono wa Baba yetu ndiyo hukishikilia midomoni mwetu. Lakini tujapopona na kurudishiwa afya, isisahaulike kwamba mpokeaji wa rehema ya uponyaji anawekwa chini ya wajibu uliofanywa upya kwa Muumba —Ministry of Healing, 233.

Mungu huwataka watu Wake wawe na maendeleo endelevu. Tunahitaji kujifunza kuwa uchu ulioendekezwa ni kizuizi kikubwa sana cha uboresahaji wa akili na utakaso roho. Pamoja na madai yetu yote kuhusu matengenezo afya wengi wetu wanakula isivyo sahihi. Uendekezaji wa uchu ni chanzo kikuu cha udhaifu wa kimwili na kiakili, na kwa kiasi kikubwa huweka msingi wa udhaifu na vifo vya mapema. Hebu kila mmoja ambaye anatafuta kumiliki usafi wa roho akumbuke akilini kwamba katika Kristo kuna nguvu za kutawala uchu. —Counsels on Diet and Foods, 127.

10 - WASAIDIE WENGINE KUREJESHA AFYA YA MWILI NA ROHO KUPITIA UTII WA SHERIA ZA MUNGU. MUNGU ANAAHIDI AFYA TELE KWA WOTE WANAOFANYA HIVI.

“Je! Siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? Umwonapo mtu aliye uchi, umvike nguo; wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe? Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara; na haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakufuata nyuma ukulinde.” Isaya 58:7-8

“Akawaita wanafunzi Wake kumi na wawili, akawapa amri juu ya pepo wachafu, wawatoe, na kupoza magonjwa yote na udhaifu wa kila aina. Hao Thenashara Yesu aliwatuma, akawaagiza, akisema, Katika njia ya Mataifa msiende, wala katika mji wowote wa Wasamaria msiingie. Na katika kuenenda kwenu, hubirini, mkisema, Ufalme wa mbinguni umekaribia. Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure.” Mathayo 10:1, 5, 7-8

Sura ya 58 ya Isaya ni maagizo ya tiba kwa magonjwa ya mwili na roho (Rx:Doctors prescriptions). Ikiwa tunatamani afya na furaha ya kweli ya maisha, ni lazima tuweke katika vitendo sheria zilizotolewa katika Andiko hili. —Ministry of Healing, 256.

Matendo mema yana baraka mara mbili, yanamnufaisha mtoaji na mpokeaji ule wema. Ufahamu wa kutenda haki ni mojawapo ya dawa bora kwa miili na akili zilizo na magonjwa. Wakati akili inapokuwa huru na yenye furaha kutokana na hisia ya wajibu uliyofanywa vyema na moyo ulioridhika unaotokana na kuwapa watu wengine furaha, ushawishi ushangiliao na wenye kuinua huleta maisha mapya kwenye nafsi nzima. —Ministry of Healing, 257.

Kukiri kwetu kuhusu uaminifu Wake, ni njia teule ya Mbingu kwa ajili ya kumdhihirisha Kristo ulimwenguni. Ni kweli kwamba twapaswa kukiri neema Yake kama ilivyodhihirishwa kupitia watakatifu wa kale; lakini kile ambacho kitakuwa na matokeo chanya zaidi, ni ushuhuda wa uzoefu wetu binafsi. Sisi ni mashahidi wa Mungu tunapofunua ndani yetu utendaji wa nguvu ambao ni wa Bwana. —Ministry of Healing, 100.

"Huruma ya kweli kati ya mwanadamu na wanadamu wenzake inapaswa kuwa ni ishara ya kuwatofautisha wale wanaompenda na kumcha Mungu na wale ambao hawajali sheria Yake. Ni huruma iliyoje ambayo Kristo alionyesha katika kuja katika ulimwengu huu kutoa maisha Yake dhabihu kwa ajili ya ulimwengu

unaokufa! Dini Yake iliongoza kwenye kazi ya Kweli ya umishenari wa tiba. Alikuwa nguvu ya uponyaji. ‘Nataka rehema, wala si sadaka,’ akasema. Hili ndilo jaribu ambalo Mwandishi Mkuu wa Ukweli alitumia kutofautisha kati ya dini ya kweli na uongo. Mungu anataka wamishenari Wake wa tiba watende kwa upole na huruma nyororo ambayo Kristo angeonyesha kama angekuwa katika ulimwengu wetu leo.”—Medical Ministry, 251.

Hewa safi, mwanga wa jua, kuwa na kiasi, pumziko, kufanya mazoezi, chakula kinachofaa, matumizi ya maji, kumtumaini Mungu na uweza Wake—hizi ndizo tiba za Kweli. Kila mtu apaswa kuwa na maarifa ya maumbile ya asili yaletayo uponyaji na jinsi ya kuyatumia (azifahamu tiba nane rahisi na kuzitumia, ikiwemo usafi, roho ya shukrani, mtazamo wa maisha, na kuhudumia watu).

Ni muhimu pia kuelewa kanuni zinazohusika katika tiba ya wagonjwa na kuwa na uzoefu wa vitendo utakaomwezesha mtu kutumia ujuzi huo kwa njia ifaayo.

Matumizi ya tiba za asili yanahitaji kiasi kikubwa cha uangalifu na jitihada, mambo ambayo wengi hawako tayari kuyafanyia kazi. Mchakato wa asili wa uponyaji na kuujenga mwili tena pale ulipoharibika ni wa taratibu ila una uhakika, na kwa wale wasio na subira, huona mambo yanaenda polepole sana kwao. Kusalimisha vile vitu vinavyoendekezwa au kujifurahisha navyo kunahitaji kujitoa kafara. Lakini mwishowe itagunduliwa kwamba asili, isipozuiwa, hufanya kazi yake kwa busara na kwa ubora. Wale wanaodumu katika kuzitii sheria zake watavuna thawabu katika afya zao za mwili na akili. —Ministry of Healing, 127

SEHEMU YA 5

TIBA RAHISI

SURA YA 15

KWA NINI MUNGU AMEWAELEKEZA WATU WAKE KUTUMIA TIBA RAHISI BADALA YA KUTEGEMEA MAOMBI PEKEE KWA AJILI YA UPONYAJI?

Mwongozo wa kufundisha utii wa sheria za mungu na kujilinda kutokana na udanganyifu wa kimiujiza wa shetani—kwa kutumia tiba rahisi.

SABABU SABA KWA NINI MUNGU AMETUELEKEZA TUTUMIE TIBA RAHISI

Je, Mungu hataki kwamba tutegemee tu maombi na imani katika huduma ya uponyaji wa Bwana? Kwa nini tutumie tiba rahisi ikiwa tumeomba uponyaji na kuwa na imani ya kuamini kwamba, ikiwa ni mapenzi Yake, Yeye atajibu maombi yetu?

1- KWA SABABU TUMEAGIZWA KUWA ITAKUWA NI UJUVI/KIBURI KUMWOMBA MUNGU APONYE BILA KUTUMIA DAWA ANAZOTUPA.

Tunapaswa kushirikiana na Mungu katika kumrejesha mgonjwa na mateso ya afya.

“Wale watafutao uponyaji kwa maombi wasipuuze kutumia tiba ambazo zimo katika uwezo wao kuzifikia. Kutumia tiba zifaazo sio kuikana imani kwa maana Mungu amezitoa ili kupunguza maumivu na kuisaidia asili katika utendaji wake wa uponyaji.

Kushirikiana na Mungu kwa kujiweka katika mkao mwafaka zaidi katika safari ya kupona siyo kuikana imani (pamoja na maombi, lakini pia utumiaji wa dawa si kukosa imani katika nyakati fulani za dharura- acute sickness). Mungu ameweka karibu yetu maarifa ya kanuni za uzima. Ujuzi huu umewekwa ndani ya uwezo wetu ili tuweze kuutumia. Twapaswa kutumia kila njia kwa ajili ya urejeshaji wa afya, tukichukua kila kinachonufaisha kwa kadiri iwezekanavyo, tukitenda kazi kwa kupatana na sheria za asili. Tujapoomba uponyaji wa mgonjwa, twaweza kufanya kazi kwa nguvu zetu zote, tukimshukuru Mungu kwamba tunao upendeleo wa kushirikiana Naye, na kuomba baraka Zake kwa njia ambazo Yeye Mwenyewe ametupatia. [MH 231.3]

Tuna idhini yaNneno la Mungu kutumia tiba rahisi kuleta uponyaji.

Wakati mmoja Kristo aliyapaka macho ya kipofu kwa udongo na kumwambia, “Nenda ukanawe katika bwawa la Siloamu Basi akaenda, akanawa, akaja akiona.” Yohana 9:7. Tiba hiyo ingeweza kufanywa tu kwa uweza wa Mponyaji Mkuu, lakini Kristo alitumia njia rahisi ya asili. Ingawa hakupendezwa na dawa zile tunazozijua za hospitalini, Aliidhinisha matumizi ya tiba rahisi na za asilia. [MH 233.1]

“Katika kuwaombea wagonjwa, ni muhimu kuwa na imani; Kwa maana ni inaendana na Neno la Mungu. Yakobo 5:16 Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii. Kwa hiyo hatuwezi kuacha kuwaombea wagonjwa, na tunapaswa kuhuzunika sana ikiwa hatungeweza kuwa na nafasi ya kumkaribia Mungu, na kuweka mbele zake udhaifu wetu wote na udhaifu wetu, kumwambia Mwokozi Mwenye huruma yote kuhusu mambo haya, tukiamini kwamba Yeye husikia maombi yetu. Wakati mwingine majibu ya maombi yetu huja mara moja; Wakati fulani inatubidi tusubiri kwa subira na kuendelea kwa bidii kuomba mambo tunayohitaji..

“Kungoja huku hakumaanishi kwamba kwa sababu tunamwomba Bwana alete uponyaji basi hatuna jambo la kufanya. Kinyume chake, tunapaswa kutumia vizuri zaidi njia ambayo Bwana katika wema Wake ametupatia katika mahitaji yetu.

“Nimeona mambo mengi sana ya kufanya mambo kwa kupitiliza au ushabiki, katika kuwaombea wagonjwa, ambayo nimehisi kwamba sehemu hii ya uzoefu wetu inahitaji mawazo thabiti, yaliyotakaswa, ili tusije tukafanya harakati ambazo tutazipa jina la imani, lakini ambazo kwa kweli ni mawazo ya ujuvi (dhana) tu yasiyo na mantiki. Watu waliochoshwa na mateso wanahitaji kushauriwa kwa busara, ili waenende kwa busara; Na wanapojiweka mbele za

Mungu ili waombewe ili wapate kuponywa, hawapaswi kuchukua msimamo wa kwamba, njia za kurejesha afya kwa mujibu wa sheria za asili zinapaswa kupuuzwa. “Ikiwa watachukua msimamo kwamba katika kuomba kwa ajili ya uponyaji hawapaswi kutumia tiba rahisi zinazotolewa na Mungu ili kupunguza maumivu na kusaidia mwili katika kazi yake, wakidhani kuwa hicho kitendo ni kuikana imani, wanachukua msimamo usio wa hekima. Kufanya hivi sio kuikana imani; Inapatana kabisa na mipango ya Mungu. Hezekia alipokuwa mgonjwa, nabii wa Mungu alimletea ujumbe kwamba afe. Mfalme alimlilia Bwana, na Bwana akamsikia mtumishi Wake, akafanya muujiza kwa niaba yake, akimtumia ujumbe kwamba aongezewe miaka kumi na tano ya kuishi kwake. Sasa neno moja kutoka kwa Mungu, mguso mmoja wa kidole cha Bwana, kingemponya Hezekia papo hapo, lakini maagizo ya pekee yalitolewa kuchukua tunda la mkuyu/mtini na kuuweka juu ya sehemu iliyoathiriwa, na Hezekia akawa mzima.” —Counsels on Health, 380-382.

Orodha ya tiba ya maji na maandalizi ya miti-shamba kwa matatizo mbalimbali yametolewa: “Kuna tiba nyingi rahisi zaidi ambazo zitafanya mengi kurejesha hatua za kiafya kwa mwili. Maandalizi haya yote rahisi ambayo Bwana anatarajia tuyatumie sisi wenyewe, lakini pale mwanadamu anapoishia na anashindwa kufanya jambo lolote ndio nafasi ya Mungu inaanzia. Ikiwa tutapuuza kufanya kile ambacho kipo ndani (kinaweza kufikiwa) ya kila familia, na kumwomba Bwana aondoe maumivu wakati sisi ni wavivu pia kutumia dawa hizi ndani ya uwezo wetu, hii inamaanisha ni dhana tu isiyo na mantiki. 2 Selected Messages, 297.

2- KWA SABABU WATU LAZIMA WAPEWE FURSA NA WAKATI WA KUJIFUNZA KUHUSU SHERIA ZA KIMAUMBILE ZINAZOTAWALA UTU WAO

“Niliona kwamba sababu ya Mungu kutosikia maombi ya watumishi Wake kwa ajili ya wagonjwa waliopo miongoni mwetu kikamilifu zaidi ni kwamba hangeweza kutukuzwa kwa kufanya hivyo kwa kuwa walikuwa wakikiuka sheria za afya. Na pia niliona kwamba alipanga kuwepo kwa Matengenezo ya Afya na Taasisi ya Afya ili kuandaa njia ya maombi ya imani kujibiwa kikamilifu. Imani na matendo mema vinapaswa kwenda bega kwa bega katika kuwaokoa walioteswa walio miongoni mwetu, na katika kuwafanya watu wafae katika kumtukuza Mungu hapa mtu, na kuokolewa wakati wa kuja kwa Kristo...

“Mtu yeyote asidhani kwamba Taasisi ni mahali pao pa nakuinuliwa kwa maombi ya imani. Hapa ni mahali pa kupata nafuu kutokana na magonjwa kwa njia ya matibabu, na kujipatia kanuni/mazoea sahihi za kuishi, na kujifunza jinsi ya

kuepuka magonjwa. Lakini ikiwa kuna sehemu moja chini ya mbingu zaidi ya mahali pengine ambapo ombi la kutuliza, lenye huruma linapopaswa kutolewa na wanaume na wanawake wacha Mungu na wenye imani, naam, ni katika taasisi kama hiyo. Wale wanaowatibu wagonjwa wanapaswa kusonga mbele katika kazi yao muhimu kwa kumtegemea Mungu kwa nguvu kwa ajili ya baraka Zake ili kuzifikia njia ambazo ametoa kwa neema, na ambazo kwa rehema anatutaka tuonyeshe usikivu wetu, kama vile hewa safi, usafi, lishe bora, muda unaofaa kufanya kazi na pumziko na matumizi ya maji." —Counsels on Health, 247.

3- KWA SABABU WATU LAZIMA WAPEWE NAFASI NA WAKATI WA KUJIFUNZA NI NINI KILICHOWAFANYA WAWE WAGONJWA-

LAZIMA WAFUNDISHWE NI SHERIA GANI WALIKIUKA.

Ni kazi bure kuwafundisha watu kumtazama Mungu kama mponyaji wa udhaifu wao, mpaka wafundishwe kuacha mazoea yasiyofaa. Ili kupokea baraka Zake katika jibu la maombi, ni sharti waache kutenda maovu na kujifunza kutenda mema. Mazingira yao lazima yawe masafi, mienendo yao maishani iwe sahihi. Ni sharti waishi kwa kupatana na sheria ya Mungu, ya asili na ya kiroho. [MH 227.4; HU Aya ya 11]

Kwa wale wanaotamani maombi kwa ajili ya kurejeshewa afya, inapaswa wafahamishwe wazi kwamba uvunjaji wa sheria ya Mungu, iwe ya asili au ya kiroho, ni dhambi, na kwamba ili wao wapate baraka Zake, dhambi lazima iungamwe na kuachwa. - Ministry of Healing, 227-228 [MH 228.1; HU Aya ya 12]

4- KWA SABABU WATU LAZIMA WAPEWE FURSA NA WAKATI WA KUJIFUNZA JINSI YA KUREJESHA AFYA

Ni lazima wafundishwe umuhimu wa tiba rahisi inayotolewa na Mungu ili kusafisha mfumo na kusawazisha mzunguko wa damu

"Kazi hiyo ilipoendelea, tuliagizwa kwamba mahali panapofaa patafutwe, ambapo tungeweza kuwaleta wagonjwa na wanaoteseka ambao hawakujua lolote kuhusu watu wetu na Maandiko ya Biblia, na hivyo kuwafundisha jinsi ya kurejesha afya kwa njia za busara za matibabu bila kutumia dawa zenye sumu, na wakati huo huo tukiwahudimia kwa kuwazunguka na mambo ya kiroho yenye kuinua."—Counsels on Health, 469.

"Anza kufanya kazi ya umishenari wa tiba kwa manufaa uliyo nayo. Utangundua kwamba hapo ndipo njia itafunguliwa kwako kufanya usomaji wa Biblia. Baba wa Mbinguni atakuweka katika uhusiano na wale wanaohitaji kujua jinsi ya

kuwatendea wagonjwa wao. Weka katika vitendo kile unachojua kuhusu matibabu ya ugonjwa. Hivyo mateso yatatulizwa, nawe utapata nafasi ya kuumega mkate wa uzima kwa roho zenye njaa.” —A Call to Medical Evangelism, 26.

“Bwana ametoa baadhi ya miti-shamba (herbs) sahili ya shambani ambayo nyakati fulani huwa na manufaa; Na ikiwa kila familia ingeelimishwa jinsi ya kutumia mimea hii ikiwa ni ugonjwa, mateso mengi yangeweza kuzuiwa, na hakuna daktari anayehitaji kuitwa. Mimea hii ya kizamani,na rahisi, ingetumiwa kwa akili, ingeweza kuponya wagonjwa wengi ambao wamekufa kwa kutumia dawa za famasia.”—Letter 82, 1897 (written February 10, 1897).

“Watendakazi wa Injili wanapaswa pia kutoa mafundisho katika kanuni za maisha yenye afya. Maelfu wanahitaji mafundisho, na hawa wangeyapokea kwa furaha maagizo yahusuyo njia rahisi za kuwatibu wagonjwa—njia mbadala zinazochukua nafasi ya matumizi ya dawa zenye sumu.” -Ministry of Healing, 146. [MH 146.1; HU Aya ya 22]

“Kiasi kikubwa cha wema kinaweza kufanywa kwa kuwaelimisha wote ambao tunaweza kuwafikia, na kwa njia bora zaidi, si tu katika kuponya wagonjwa, bali pia kuzuia magonjwa na mateso.” —Counsels on Health, 451.

5- KWA SABABU WATU LAZIMA WAPEWE FURSA NA WAKATI WA KUJIFUNZA JINSI YA KUDUMISHA AFYA

Ni lazima wafundishwe mbinu rahisi za kuishi na kula kwa afya: jinsi ya kutumia kanuni za sheria za kimwili za Mungu, kwa mahitaji na matatizo yao ya kila siku.

“Nuru ilipokuja kwamba tuanze kazi ya vituo vya tiba, sababu zilitolewa kwa uwazi. Kulikuwa na wengi ambao walihitaji kuelimishwa kuhusu maisha yenye afya. . Kama sehemu ya matibabu, mihadhara ilipaswa kutolewa juu ya tabia sahihi za kula na kunywa na kuvaa. Maelekezo yalipaswa kutolewa kuhusu uchaguzi na utayarishaji wa chakula, kuonyesha kwamba chakula kinaweza kutayarishwa ili kiwe chenye afya na chenye lishe, na wakati huohuo kiwe na ladha na cha kupendeza.”—Counsels on Health, 469.

“Katika taasisi zetu zote za afya, inapaswa kufanywa kuwa kipengele cha kipekee kwa ajili ya kutoa maelekezo kuhusiana na sheria za afya. Kanuni za matengenezo ya afya zinapaswa kuwekwa kwa uangalifu na kwa kina mbele ya wote, wagonjwa na wasaidizi. Kazi hii inahitaji ujasiri wa kimaadili.”—Counsels on Health, 452.

6 - KWA SABABU SHETANI ATAJARIBU KUGHUSHI UPONYAJI WA IMANI YA - (mambo ya Kiroho)

ATAFANYA HIVYO ILI KUVUTA USIKIVU KUPITIA NJIA RAHISI ZA MUNGU ZA KUONDOA UGONJWA

“Wachawi wa Misri hawakuweza kufanya miujiza hiyo yote ambayo Mungu aliifanya kupitia kwa Musa. Ni miujiza michache tu kati ya hiyo, ndiyo ambayo wangeweza kuiigiza. Fimbo za waganga wa kichawi zikawa nyoka, lakini fimbo ya Haruni ikawameza…

"Waganga wa Misri walionekana kana kwamba wanafanya mambo kadhaa kwa uchawi wao sawa na yale ambayo Mungu aliyafanya kwa mkono wa Musa na Haruni. Kwa kweli hawakufanya fimbo zao kuwa nyoka, bali kwa uchawi, wakisaidiwa na yule mdanganyifu mkuu, walifanya nyoka hao waonekane kama nyoka; kuighushi kazi ya Mungu…

“Wachawi hawakufanya kazi kwa sayansi yao peke yao, bali kwa uwezo wa mungu wao, Ibilisi, ambaye kwa werevu alitekeleza kazi yake ya udanganyifu ya kughushi kazi ya Mungu. Musa, kwa uwezo wa Mungu, alikuwa amebadilisha fimbo kuwa nyoka aliye hai. Shetani, kupitia kwa wachawi, aliiga muujiza huu. Asingeweza kutokeza nyoka walio hai, kwa kuwa hana uwezo wa kuumba au kutoa uhai. Nguvu hii ni Mungu tu peke yake, Ndiye aliyo nayo. Lakini yote ambayo Shetani angeweza kufanya ni kazi bandia—alitoa vitu bandia. Kwa uwezo huo, akifanya kazi kupitia kwa waganga, alisababisha fimbo kuchukua sura ya nyoka.Shuhuda kwa Kanisa 5: 696-697

Ilikuwa ni kwa onesho la uwezo usio wa kawaida (muujiza), katika kumfanya nyoka kuwa chombo chake, ndipo Shetani aliposababisha anguko la Adamu na Hawa katika Edeni. Kabla ya mwisho wa wakati atafanya maajabu makubwa zaidi. Kadiri uwezo wake unavyoenea, atafanya miujiza halisi. Maandiko yanasema: "Yeye ... huwadanganya wakaao juu ya nchi kwa miujiza ile aliyopewa kuifanya," na siyo tu ile miujiza anayojifanya kuitenda. Kitu zaidi ya upotovu tu kinaoneshwa katika hili. Lakini kuna kikomo ambacho Shetani hawezi kupita, na hapa hutumia udanganyifu kama msaada wake na kuigiza kazi ambayo yeye hana uwezo wa kuifanya.” —Shuhuda kwa Kanisa 5:698.

"Tunapaswa kuwa macho dhidi ya michezo/sanaa za udanganyifu ya Shetani. Ataimiliki miili ya binadamu, na kuwafanya wanaume na wanawake kuwa wagonjwa. Kisha atakoma ghafla kutumia nguvu zake mbaya, na itatangazwa kuwa muujiza umefanywa (mtu atapona). Tunahitaji sasa kuwa na ufahamu wa

kweli wa uwezo wa Yesu Kristo ili kuwaokoa wote wanaomjia."—Medical Ministry, 110.

"Matukio ya kuogofya, yanayopita akili za kibinadamu, kwa vile ni ya kimiujiza (supernatural) yataanza kuonekana mbinguni, siyo baada ya muda mrefu, kama ishara ya nguvu ya utendaji kazi wa kimiujiza wa mashetani. Roho za mashetani zitawaendea wafalme wa dunia na ulimwengu wote, kuwafungia katika uongo, na kuwasihi wajiunge na Shetani katika pambano lake la mwisho dhidi ya serikali ya mbinguni. Kwa njia ya mawakala hawa, watawala na watawaliwa kwa pamoja watadanganywa. Watu watainuka wakijifanya kuwa Kristo Mwenyewe, na wakidai kuwa na cheo na hadhi ya kuabudiwa ambavyo inamstahili Mkombozi wa ulimwengu tu. Watatenda miujiza ya ajabu ya uponyaji na watadai kuwa na mafunuo kutoka mbinguni yanayopingana na ushuhuda wa Maandiko.

Kama tendo la juu kabisa katika sakata kuu la uongo, Shetani mwenyewe atajifanya kuwa Kristo…… Sasa mdanganyaji mkuu atafanya ionekane kana kwamba Kristo amekuja. Sauti yake ni laini na tulivu, lakini ikiwa tamu. Kwa sauti ya upole na huruma anasema baadhi ya mambo ya neema ile ile ya zile Kweli za mbinguni ambazo Kristo alizisema; anaponya magonjwa ya watu, na ndipo, katika kujifanya kwake Kristo, anadai aliibadili Sabato na kuifanya Jumapili, na anawaamrisha watu wote kuiadhimisha siku yeye Shetani ameibariki." -The Great Controversy, 624.

"Wengine watajaribiwa kupokea maajabu haya kana kwamba yanatoka kwa Mungu. Wagonjwa wataponywa mbele yetu. Miujiza itatendwa mbele yetu. Je! Tumejiandaa kwa hali ya kujaribiwa inayotungojea wakati maajabu ya uongo ya Shetani yatakapodhihirishwa kikamilifu? Je! Roho nyingi hazitanaswa na kuchukuliwa? Kwa kujitenga na maagizo wazi na amri za Mungu, na kuzingatia mafundisho ya hekaya, akili za wengi zinajiandaa kupokea maajabu haya ya uongo. Lazima wote tujihami na kujiweka tayari kwa pambano ambalo lazima tushiriki hivi karibuni. Imani katika Neno la Mungu, linalosomwa kwa maombi na kutumika kwa vitendo, itakuwa ndiyo ngao yetu dhidi ya nguvu za Shetani nayo itatupatia ushindi, kwa damu ya Kristo."—Shuhuda kwa Kanisa 1:302.

7- KWA SABABU SHETANI ATATAFUTA KUFAIDIKA NA VIPENGELE VYA KUVUTIA VYA "MATENDO YAKE YA KIMUUJIZA YA UPONYAJI"

Atafanya hivyo ili kuuongoza ulimwengu kukataa ahadi na amri za Mungu

"Mungu Ndiye anayekinga viumbe Vyake, na kuwalinda kwa kuwazingira, dhidi ya uwezo wa mharibifu. Lakini ulimwengu wa Kikristo umeonyesha kudharau sheria

ya Yehova; Na Bwana atafanya tu, yale aliyotangaza kwamba atafanya—ataondoa baraka Zake duniani, na kuondoa ulinzi Wake wa kulinda kwa wale wanaoasi sheria Yake, na kuwafundisha na kuwalazimisha wengine kufanya kama wao wafanyavyo. Shetani anawatawala wote ambao Mungu hana ulinzi juu yao. Atawapendelea na kuwafanikisha wengine, ili kuendeleza mipango yake mwenyewe; Naye atawaletea wengine taabu, na kuwaongoza watu kuamini kwamba ni Mungu anayewatesa.

“Wakati akiwatokea wanadamu kama tabibu mkuu anayeweza kuponya magonjwa yao yote, ataleta magonjwa na maafa, mpaka miji yenye watu wengi, itapungua idadi na kuwa uharibifu ukiwa. Hata sasa yuko kazini. Anafanya kazi kwa kuleta ajali na misiba ya baharini na nchi kavu, moto mkubwa, vimbunga vikali na mvua ya mawe kali, tufani, mafuriko, tsunami, mawimbi ya maji, na matetemeko ya ardhi—katika kila mahali na Shetani anatumia uwezo wake kwa njia elfu. Matukio haya yatawazuru wanadamumara kwa mara na mabaya zaidi. Uharibifu utakuwa juu ya mwanadamu na mnyama.”— Counsels on Health, 460-461.

“Kupitia umizimu, Shetani anaonekana kama mfadhili wa jamii, akiponya magonjwa ya watu, na akikiri kuwasilisha mfumo mpya na uliotukuka zaidi wa imani ya kidini; lakini wakati huohuo anafanya kazi ya kuangamiza.”— Counsels on Health, 460.

“Shetani ni mwanafunzi wa Biblia mwenye bidii. Anajua kuwa wakati wake ni mfupi, na anatafuta kila namna kuipinga/kuipiku kazi ya Bwana juu ya dunia hii. Haiwezekani kutoa wazo lolote la uzoefu wa watu wa Mungu ambao watakuwa hai duniani wakati utukufu wa mbinguni na kurudiwa kwa mateso ya zamani vitakapochanganywa. Watatembea katika nuru itokayo kwenye kiti cha enzi cha Mungu. Kwa njia za malaika kutakuwa na mawasiliano ya kila wakati kati ya mbingu na dunia. Na Shetani, akiwa amezungukwa na malaika waovu, na akidai kuwa ni Mungu, atafanya miujiza ya kila aina, ili kudanganya, yumkini, walio wateule.

Watu wa Mungu hawatapata usalama wao katika kutenda miujiza, kwa maana Shetani ataigiza miujiza ile watayoitenda, kwa kazi zake bandia. Watu wa Mungu waliothibitishwa na kuimarishwa watapata nguvu zao katika ishara iliyozungumziwa katika Kutoka 31: 12-18. Wanapaswa kuweka msimamo wao juu ya neno lililo hai: "Imeandikwa." Huu pekee ndio msingi ambao kwake wanaweza kuwa salama. Wale waliovunja Agano lao na Mungu katika siku hiyo watakuwa bila Mungu na bila matumaini.” {9T 16.1}.

SURA YA 16

KANUNI MAALUM AMBAZO KWAZO TUNAWEZA KUJUA NI TIBA ZIPI NDIYO "DAWA ZA FAMASIA " NA ZIPI ZIMEIDHINISHWA NA MUNGU.

FAFANUZI THEMANINI NA TANO ZA "DAWA"

Ni nini, kulingana na roho ya unabii, ni "dawa za kulevya au dawa zenye sumu ziitwazo drugs kwa Kiingereza"? Tuko hapa kushughulika na mada ambayo ilikuwa imemletea fadhaa kubwa Ellen White wakati wa uhai wake. Hili linapaswa kuwa jambo la kuzingatia sana kwa mtu yeyote wa Mungu anayetaka kufanya kazi ya dhati/kweli ya umishenari wa tiba. Alipokea njozi nyingi kuhusiana na hii mada. Katika baadhi ya mambo, kuondolewa kwa tatizo hili ndiyo sababu Waadventista Wasabato waliitwa kuanzisha vituo vya sanitarium na shule za tiba na kuendelea na kazi ya tiba. Inafaa kwamba wakati ambapo ni machache sana yanayosemwa au kuandikwa juu ya mada hii, kwamba utafiti huu wa kina usio wa kawaida unapaswa kuchapishwa.Inajumuisha taarifa kutoka kwenye vitabu vinavyopatikana kwa sasa, na pia kutoka vitabu vya Healthful living (Maisha yenye Afya) na How to live (Jinsi ya Kuishi). Lakini haijumuishi kiasi kikubwa cha makala nyingi zilizoandikwa kwa njia ya barua binafsi na kwa sasa zinapatikana tu katika miswada (mimeograph studies) yaliyochapishwa au kuzalishwa kwa njia ya mitambo kama vile Loma Linda Messages (Ujumbe wa Loma Linda).

Ikiwa utasoma somo hili kwa umakini na kulicheua vizuri, hutabaki vile vile. Habari zilizomo humu, ikitekelezwa, inaweza kurefusha maisha yako—na maisha ya wapendwa wako. Na, kwa kuongeza, inaweza kusaidia vijana kufanya chaguzi bora, kwa kuzingatia kazi ya maisha.

1- DAWA ZA FAMASIA (DRUGS) SIO NJIA SAHIILI YA TIBA

"Watu wetu wanapaswa kuwa wenye akili mahiri kuhusiana matibabu ya magonjwa kwa kutokutumia dawa za sumu. Wengi wanapaswa kuitafuta elimu ambayo itawawezesha kukabiliana na magonjwa kwa njia mbalimbali kwa njia rahisi zaidi. Tiba ya maji, kwa busara na ustadi, inaweza kuwa njia ya kuokoa maisha ya watu wengi. Hebu utafiti adilifu, na wenye bidii uungwaniswe na tiba makini. Hebu maombi ya imani yatolewe kando ya kitanda cha wagonjwa. Hebu wale wanaougua watiwe moyo kudai ahadi za Mungu kwa ajili yao wenyewe."— Medical Ministry, 227.

2- DAWA ZENYE SUMU NI NJIA RAHISI

"Swali ni Je, watatunza kanuni za afya na usafi [utakaso wa kimwili] au watatumia njia rahisi ya kutumia dawa, kuchukua nafasi ya kutibu magonjwa bila kuridhia kutumia dawa zenye sumu?"— Manuscript 22, 1887.

3- DAWA NI NJIA YA DHARURA

Matumizi ya tiba za asili yanahitaji kiasi kikubwa cha uangalifu na jitihada ambayo wengi hawako tayari kuifanyia kazi. Mchakato wa asili wa uponyaji na kuujenga mwili tena pale ulipoharibika ni wa taratibu ila una uhakika, na kwa wale wasio na subira, huona mambo yanaenda polepole sana kwao. Kusalimisha vile vitu vinavyoendekezwa au kujifurahisha navyo kunahitaji kujitoa kafara. Lakini mwishowe itagunduliwa kwamba asili, isipozuiwa, hufanya kazi yake kwa busara na kwa ubora. Wale wanaodumu katika kuzitii sheria zake watavuna thawabu katika afya zao za mwili na akili. —Ministry of Healing, 127.

4- DAWA HUCHUKUA KAZI KIDOGO

“Tumia dawa (remedies) ambazo Mungu amezitoa. Hewa safi, mwanga wa jua, na matumizi mazuri ya maji ni mawakala wanaosaidia katika kurejesha afya. Lakini matumizi ya maji yanachukuliwa kuwa jambo linalochosha/gumu sana. (Kwa kusema) Ni rahisi kutumia dawa za famasia kuliko kutumia dawa za asili.” — Healthful Living, 247.

5- DAWA ZENYE SUMU NI NJIA YA UVIVU

“Kazi ya kwanza ya daktari lazima iwe kuwaelimisha wagonjwa na wanaoteseka hususani namna wanayopaswa kufuata ili kuzuia magonjwa. Jambo jema kubwa zaidi linaweza kutendeka kwa kujaribu kwetu kuwapa nuru akilini mwao wale wote tunaoweza kukutana nao, kama njia bora zaidi kwao ya kuzuia magonjwa na mateso, na kanuni zilizovunjwa, na kifo cha mapema. Lakini wale ambao hawajali kuhusu kazi inayolemea/kuchosha nguvu zao za kimwili na kiakili watakuwa tayari kuagiza dawa za sumu, ambazo humletea binadamu tatizo kubwa mara mbili kuliko lile wanalodai kuwa wameondoa. Tabibu ambaye ana ujasiri wa kweli ili kuhatarisha sifa yake katika kuelimisha ufahamu kuhusu ukweli ulio wazi, katika kuonyesha asili ya ugonjwa na jinsi ya kuuzuia, na mazoezi hatari ya kutumia dawa zenye sumu, atakuwa na shughuli iliyo ngumu, lakini ataishi na kuendelea kuishi…… Yeye, ikiwa ni mwanamatengenezo, atazungumza waziwazi.”—Medical Ministry, 221-222.

6- DAWA SIO NJIA YA ASILI YA TIBA

“Katika kuwatibu wagonjwa, tabibu atamtafuta Mungu kwa ajili ya hekima; Kisha, badala ya kuweka utegemezi wake juu ya dawa na kutarajia kwamba dawa italeta afya kwa wagonjwa wake, atatumia urejeshaji wa asili, na kutumia njia za asili ambapo wagonjwa wanaweza kusaidiwa kupona. Bwana atasikia na kujibu maombi ya tabibu Mkristo.”—Healthful Living, 247-248.

7- DAWA ZENYE SUMU NI NJIA ISIYO NA IMANI

"Oh ni kwa jinsi gani uwezekano ulivyo mkubwa wa namna ambayo ameweka ili atufikie! Anasema, ‘Chochote mtakachomwomba Baba kwa Jina Langu, atawapa ninyi.’ Anaahidi kuja kwetu kama mfariji, ili atubariki. Kwa nini hatuamini ahadi hizi? Kile tunachokosa katika imani tunafidia kwa kutumia dawa zenye sumu. Hebu tuache dawa hizo, tukiamini kwamba Yesu hapendi tukiwa wagonjwa, na kwamba ikiwa tunaishi kulingana na kanuni za matengenezo ya afya, atatuweka salama.” -Manuscript 169, 1902.

8- DAWA ZA FAMASIA NI SUMU

“Watu wetu wanapaswa kuwa na akili katika kutibu magonjwa bila msaada wa dawa zenye sumu.” —Medical Ministry, 56-57.

"Maelekezo maalum yanapaswa kutolewa katika sanaa ya kutibu wagonjwa bila kutumia dawa zenye sumu na kupatana na nuru ambayo Mungu ameitoa. Katika matibabu ya wagonjwa, dawa zenye sumu hazihitajiki kutumiwa.”- Shuhuda kwa Kanisa 9: 175.

9- DAWA ZENYE SUMU NI DAWA ZENYE ZENYE SUMU

Pale utumiaji vibaya wa afya unapopitiliza kiasi cha mwili kuugua, mara nyingi mwathirika anaweza kujifanyia mambo ambayo hakuna mtu mwingine anaweza kumfanyia. Jambo la kwanza kufanya ni kudadisi chanzo halisi cha huo ugonjwa na kisha kwenda kuufanyia kazi kwa akili (yaani kuutibu) ili kuondoa sababu zilizouleta. Ikiwa utendaji kazi linganifu wa mfumo wa mwili umekuwa haupatani kwa sababu ya kufanya kazi kupita kiasi, kula kupita kiasi, au makosa mengine, usijaribu kutibu shida hizo kwa kuongeza mzigo wa dawa zenye sumu mwilini mwako (Msisitizo: Mfano mzuri ni kama unakula chakula kingi kupita unavyopaswa kula, au chenye tindikali nyingi, au pilipili, au baking soda na kisha ukawa na mazoea ya kutumia dawa za kupunguza tindikali au antacids/magnesium bila ya kutumia njia za asili, na kuacha kula kwa ulafi au kuacha pilipili n.k basi unakuwa haujasahihisha tatizo la urari au balansi ya mwili, hivyo dawa za famasia zitaleta shida kubwa zaidi ya uliyonayo kwenye mfumo, kama vile kuharibu figo, ini, kuharisha, na kuharibu mmeng'enyo wa chakula). — Ministry of Healing, 235. [MH 235.1]

10 - DAWA ZA FAMASIA NI SUMU YA KUFISHA

"Mama ambaye anakuwa hajiwezi, na ambaye angeweza kupata tu nafuu kwa njia ya kujiepusha (kanuni) na chakula kwa muda mfupi, na kuacha kazi, na kuwa na utulivu na kupumzika, badala ya kufanya hivyo, hujikuta amepelekwa kwa daktari. Na yeye, ambaye angepaswa kuwa tayari kutoa maelekezo machache rahisi na kanuni za kuepuka katika chakula, na kumweka kwenye njia sahihi, huyo naye hukutwa hana uelewa (ni mjinga) kuhusu kufanya hivyo, au anakuwa na shauku kubwa ya kupata malipo. Anaifanya kesi hiyo ya ugonjwa ionekane kuwa baya na ya kutishaa, na anatoa dawa zake zenye sumu ambazo, kama yeye mwenyewe angekuwa mgonjwa, hangethubutu kuzichukua. Mgonjwa anazidi kuwa na hali mbaya, na dawa za sumu hutolewa kwa uhuru zaidi (bila kizuizi) mpaka asili inazidiwa nguvu kutokana na jitihada za hizo dawa, na kukaa chini, hata kusababisha migogoro, na kisha mama huyo hufa. Alitiwa dawa za sumu hadi kufa. Mfumo wake unakuwa na sumu zaidi ya dawa. Na anakufa."—2 Selected Messages, 441.

11- MADAWA YA KULEVYA NI VITU VYA KIGENI VYENYE ASILI YA SUMU

"Wagonjwa wanaoteseka katika hali nyingi wanaweza kujifanyia wenyewe yale ambayo wengine hawawezi kuwafanyia vile vile. Wanapaswa kuanza kuipunguzia asili mzigo ambao wameiwekea juu yake. Wanapaswa kuondoa kisababisho. Wafunge saumu kwa muda mfupi, na kuacha nafasi ya kupumzika katika tumbo.

Kupunguza hali ya homa ya mfumo kwa matumizi yenye uangalifu na uelewa, ya maji. Juhudi hizi zitasaidia asili katika mapambano yake ya kuusaidia mfumo dhidi ya uchafu. Lakini kwa ujumla watu wanaougua na kuwa na maumivu huwa hawana subira. Hawako tayari kujinyima, na kuteseka kidogo kutokana na njaa. Wala hawako tayari kungoja mchakato wa polepole wa asili ili kujenga nguvu zilizozidi zenye mfumo. Lakini wameazimia kupata nafuu mara moja, na kuchukua dawa za sumu zenye nguvu, zilizopitishwa na madaktari. Asili ilikuwa ikifanya kazi yake vizuri, na ingeshinda, lakini wakati ikikamilisha kazi yake, chembe ya kigeni ya asili ya sumu ilitiwa. Ni kosa lililoje! Asili iliyodhulumiwa sasa ina maovu mawili ya kupigana nayo badala ya moja. Inaacha kazi ambayo ilikuwa ikijishughulisha nayo, na kwa uthabiti inashikilia kumfukuza mvamizi aliyeletwa hivi karibuni kwenye mfumo. Asili inahisi rasimu hii maradufu juu ya rasilimali zake, na inadhoofika. — 4 Spiritual Gifts, 133-134.

12 - MAANDALIZI YA DAWA YENYE SUMU KUTOKA KWENYE JAMII WA MBOGA AU MADINI

"Kila maandalizi yenye sumu yanayotokana na jamii ya mboga na madini, yanapoingia kwenye mwili au mfumo, yataacha athari mbaya, yataathiri ini na mapafu, na kuharibu mwili/mfumo kwa ujumla. Athari mbaya hizi haziishii hapa tu. Watoto wachanga walio na ugonjwa na dhaifu huzaliwa duniani wakishiriki taabu na huzuni hiyo, inayopitishwa kwao kutoka kwa wazazi wao."— 4 Spiritual Gifts, 140.

13- DAWA ZA FAMASIA (DRUGS) NI MCHANGANYIKO WA SUMU

"Zebaki, Camomel, na Quinine zimeleta kiasi chake cha unyonge, ambacho Siku ya Mungu pekee itafichua kikamilifu ……. Maandalizi haya ya sumu yameharibu mamilioni yao, na yameacha wanaoteseka duniani wakae na maisha duni.

Wagonjwa wenye huzuni, walio na ugonjwa wa kila aina, wana sura mbaya kwa kuteseka na vidonda vya kutisha na maumivu katika mifupa, kupoteza meno, kupoteza kumbukumbu, na matatizo ya kuona, wanaonekana karibu kila mahali. Wao ni waathirika wa maandalizi ya sumu, ambayo, mara nyingi, uruhusiwa ili kuponya upungufu fulani, ambao baada ya siku moja au mbili za kufunga ungetoweka bila dawa. Lakini michanganyiko yenye sumu inayoruhusiwa na madaktari imethibitisha uharibifu wao."— 4 Spiritual Gifts, 134, 139.

14 - DAWA ZA FAMASIA NI SUMU AMBAYO HUACHA ATHARI MBAYA

“Tiba rahisi za asili zitasaidia kupona bila kuacha matokeo mabaya ambayo mara nyingi huhisiwa na wale wanaotumia dawa zenye sumu.”— Letter 82, 1908.

15 - MADAWA YA FAMASIA (DRUGS) MARA NYINGI NI MICHANGANYIKO, YENYE NGUVU KATIKA ATHARI ZAKE, ASILI AMBAYO MARA NYINGI HAIJULIKANI, NA KUACHA/KUSABABISHA MADHARA YA KUDHURU.

"Aina nyingi za dawa sokoni zisizo na kikomo, matangazo mengi ya dawa mpya na mchanganyiko, ambazo zote, kama wanavyosema, hufanya tiba nzuri, huua mamia ambapo wanafaidika moja. Wale ambao ni wagonjwa, hawana subira (patients are not patient). Watachukua dawa mbalimbali, ambazo baadhi yake zina nguvu sana, ingawa hawajui chochote kuhusu asili ya mchanganyiko huo. Dawa zote wanazotumia huwafanya tu kukosa matumaini katika kupona kwao. Hata hivyo wanaendelea kuzitumia, na kuendelea kuwa dhaifu, mpaka kufa. Wengine watakuwa na dawa katika hali zote. Basi acha wachukue michanganyiko hii ya kuumiza na sumu mbalimbali za mauti zifanye kazi wasipofanya wajibu wao wenyewe. Watumishi wa Mungu hawapaswi kutoa dawa ambazo wanajua zitaacha madhara nyuma kwenye mwili/mfumo, hata kama zitaondoa mateso ya sasa.”— 4 Spiritual Gifts, 139-140.

16- MADAWA YA FAMASIA NI SUMU ZENYE NGUVU, ASILI AMBAYO HAIJULIKANI NA WATU WA KAWAIDA

“Wanapokuwa katika dhiki, watu huenda kwa daktari, na kumpa miili yao daktari, na kutegeema iko salama mikononi mwake, wakitarajia kwamba atawaponya. Anawapatia madawa ya famasia, ambayo hawajui chochote kuhusu asili yake; Na kwa ujasiri wao wa upofu wanameza chochote ambacho daktari anaweza kuchagua kuwapa. Kwa hivyo, sumu zenye nguvu mara nyingi hutolewa, ambazo huzuia asili katika jitihada zake zote za kusaidia kuponya dhidi ya uonevu/unyanyasaji ambao mwili/mfumo unaupitia; Na mgonjwa anawahishwa kupoteza maisha. —2 Selected Messages, 441.

17 - DAWA ZA FAMASIA (DRUGS) NI HATARI, HATA KAMA ZINAWEZA KUTOLEWA KWA MAAGIZO YA DAKTARI Rx)

"Kila dawa yenye sumu inayowekwa kwenye tumbo la mwanadamu, iwe kwa maagizo ya madaktari, au na mwanadamu mwenyewe anayefanya jeuri kwa kiumbe cha binadamu yaani mwili wake, huharibu utendaji wote mfumo au mashine ya mwil wa mwanadamu."—Manuscript 3, 1897 (Ufafanuzi wa kamusi wa "hatari" ni "madhara sana au uharibifu.")

18 - MADAWA YA FAMASIA YANAWEZA KUWA YANATOKANA KWENYE MIMEA YENYE SUMU

“Kristo hakuwahi kupanda mbegu za kifo katika mwili au mfumo. Shetani alipanda mbegu hizi……. Hakuna hata mmea mmoja mbaya uliowekwa katika bustani kuu ya Bwana, lakini baada ya Adamu na Hawa kufanya dhambi, mimea yenye sumu ilichipuka. Katika mfano wa mpanzi swali liliulizwa Je, Bwana, hukupanda mbegu njema katika konde lako? Limepata wapi basi magugu? Akawaambia, Adui ndiye aliyetenda hivi. Watumwa wakamwambia, Basi, wataka twende tukayakusanye? Mathayo 13:27-28. Magugu yote yanapandwa na yule mwovu. Kila mimea yenye sumu imepandwa na yeye, na kwa mbinu zake za werevu za kuunganisha (hybridization/amalgamation/genetic engineering) ameiharibu dunia kwa magugu. Je, madaktari wataendelea kutumia dawa zinazoacha madhara mabaya katika mwili/mfumo, na kuharibu maisha hayo ambayo Kristo alikuja kuyarejesha. Tiba za Kristo husafisha mfumo.”—2 Selected Messages, 288-289.

19 - DAWA ZENYE SUMU MARA NYINGI HUTUMIA MAJINA YA AJABU

"Hii ndiyo njia ya Mungu: mimea ambayo hukua kwa manufaa ya mwanadamu, na kwa uchache wa miti midogo-midogo ambayo imehifadhiwa kwa kulowekwa (extract) ili kutumika kwa maradhi ya ghafla, zimetumiwa mara kumi zaidi, ndiyo, mara mia moja na kuleta mambo bora zaidi, kuliko dawa zote zilizofichwa chini ya majina ya ajabu, ya siri na mafumbo, ili kutumiwa na mgonjwa.”— Letter 59, 1895.

20 - DAWA ZA FAMASIA ZINA MAJINA TATA AMBAYO HUFICHA ASILI YAO HALISI

“Majina tata yanayoandikwa kwenye dawa hutumiwa ili kuficha jambo hilo, ili mtu yeyote asijue ni dawa gani anapewa hadi/isipokura atafute msaada wa kamusi.”— Medical Ministry, 228.

21 - DAWA ZA FAMASIA (DRUGS) ZINA MAJINA MAREFU AMBAYO HUFICHA SIFA ZAO HALISI

“Kama waganga wana shughuli nyingi kiasi kwamba hawawezi kuwatibu wagonjwa nje ya taasisi, Je, haitakuwa busara kwa wote kujielimisha katika matumizi ya dawa za asili (rahisi), kuliko kujitosa kutumia dawa zenye sumu, ambazo hupewa jina refu ili kuficha sifa zao halisi. Kwa nini mtu yeyote asiwe na ufahamu wa tiba za Mungu au awe mjinga: maji ya moto, vichocheo (fomentations), na vibano/kitambaa cha baridi na moto. Ni muhimu kufahamu

faida ya lishe wakati tunaugua. Wote wanapaswa kuelewa jambo la kufanya kwa ajili yao wenyewe."— Manuscript 86, 1897.

22 - DAWA ZA FAMASIA (DRUGS) ZINA MAJINA AMBAYO HAYAWEZI KUELEWEKA BILA KUTUMIA KAMUSI

"Majina tata yanayoandikwa kwenye dawa hutumiwa ili kuficha jambo hilo, ili mtu yeyote asijue ni dawa gani hadi anapewa (isipokuwa) atafute msaada wa kamusi ili kujua maana ya majina hayo…….. Bwana ametoa mimea rahisi ya shambani…….. Na ikiwa kila familia ingeelimishwa jinsi ya kutumia mimea katika hali ya ugonjwa, mateso mengi yangeweza kuzuiwa, na hakuna daktari atakayehitajika kuitwa. Mimea hii ya kizamani, ingetumiwa kwa akili, ingeweza kuponya wagonjwa wengi, ambao wamekufa kwa kutumia dawa zenye sumu."— Letter 82, 1897.

23 - DAWA ZA FAMASIA (DRUGS(ZINA MAJINA YA KIPEKEE AMBAYO WATU WA KAWAIDA HAWAELEWI

"Tangu mwanzo hadi mwisho, uhalifu wa kutumia tumbaku, kasumba/banghi na dawa zenye sumu, asili yake ni maarifa potovu. Ni kwa sababu ya kuchuma na kula matunda yenye sumu, na kupitia ugumu wa majina ambapo watu wa kawaida hawaelewi, kwamba maelfu na makumi elfu ya maisha hupotea. Ujuzi huu mkubwa unaodhaniwa na mwanadamu kuwa wa ajabu, Mungu hakumaanisha kwamba wanadamu wanapaswa kuwa nao. Wanatumia mazao yenye sumu ambayo Shetani mwenyewe amepanda ili yawe mbadala wa Mti wa Uzima, ambao majani yake yalikuwa kwa ajili ya uponyaji wa mataifa…….Michanganyiko inayoleta kifo hutumiwa ambayo huwafanya watu kuwa wenda-wazimu, mauaji, ukatili na vurugu vinatawala kila mahali. Wakati umekaribia ambapo uvumbuzi huu wote mbaya utafikia mwisho. Mwishowe, shauku ya kupata mali kwa ulaghai itaongezeka. Wizi na unyang'anyi vitaenea zaidi. Tunda la Mti wa ujuzi litaliwa bila kizuizi."— Letter to S.N. Haskell, 1898.

24 - DAWA ZINAWEZA KUJA KWENYE CHUPA

"Sayansi ya dawa imeinuliwa, lakini ikiwa kila chupa inayotoka kwa kila taasisi kama hiyo ingeondolewa, kungekuwa na walemavu wachache ulimwenguni leo. Dawa za famasia zisingepaswa kamwe kuletwa katika taasisi zetu. Hakukuwa na haja ya kuwa hivyo, na kwa sababu hii hii Bwana angetaka tuanzishe taasisi ambapo anaweza kuingia na ambapo neema na uwezo Wake vinaweza kufunuliwa. 'Mimi Ndiye ufufuo na uzima,' asema ……"Njia ya kweli ya kuponya wagonjwa ni kuwaambia kuhusu mimea inayokua kwa manufaa ya mwanadamu ……

Elimu ya kweli itatuongoza kuwafundisha wagonjwa ambao hawahitaji kumwita daktari zaidi ya vile wangemwita mwanasheria. Wao wenyewe wanaweza kuitumia mimea hiyo rahisi ikibidi.”— Manuscript 105, 1898.

25 - DAWA ZA FAMASIA (DRUGS) ZINAPASWA KUPATIKANA KATIKA MADUKA YA DAWA

“Maelfu ambao wameteseka wanaweza kurejesha afya zao, ikiwa, badala ya kutegemea duka la dawa kwa maisha yao yote, wangetupa dawa zote, na kuishi kwa urahisi, bila kutumia chai, kahawa, pombe, au viungo, ambavyo vinakera tumbo na kuliacha likiwa dhaifu na lisiloweza kumeng'enya/kusaga hata kwa urahisi, chakula bila kusisimuliwa. Bwana yuko tayari kuruhusu nuru Yake iangaze katika miale iliyo wazi, kwa wote walio dhaifu na wasiojiweza.”— Medical Ministry, 229.

26 - DAWA ZA FAMASIA HAZIWEZI KUELEZEWA KWA MANENO RAHISI

“Hebu maagizo yatolewe kwa maneno rahisi [kama vile maji ya moto, mkaa, au mimea jamii ya Nepeta/Catnip]. Hatuna haja ya kutumia misemo mingi inayotumiwa na waganga wa kidunia leo, ambayo ni vigumu sana kuielewa kiasi kwamba lazima ifasiriwe na waganga. Majina haya marefu mara nyingi hutumiwa kuficha tabia ya dawa zinazotumiwa ili kupambana na magonjwa. Hatuhitaji hizi dawa. Tiba rahisi za asili zitasaidia kupona bila kuacha matokeo mabaya ambayo mara nyingi huhisiwa na wale wanaotumia dawa zenye sumu.”— Letter 82, 1908.

27 - DAWA ZA FAMASIA ZINA MAJINA YA KILATINI, SIO KIINGEREZA

"Kama ningekuwa mgonjwa, ningemwita mwanasheria mara moja kama ambavyo ningemwita daktari, anayeshugulikia na taaluma ya udaktari kwa ujumla (general practitioner). Nisingegusa dawa zao zisizo na uhakika wa kutibu, ambazo wanazipa majina ya Kilatini. Nimeazimia (nimekusudia) kujua, kwa Kiingereza kilichonyooka, jina la kila kitu ninachoingiza katika mwili/mfumo wangu.”— Manuscript 86, 1897.

28 - DAWA ZENYE SUMU HUTOLEWA NA SAYANSI YA BINADAMU NA HUPEWA MAJINA YA SIRI AU MAFUMBO YA AJABU

"Ingekuwa bora kama, tangu mwanzo, dawa zote zingewekwa nje ya vituo vyetu vya Sanitarium, na matumizi yangefanywa kwa tiba rahisi kama zinazopatikana katika maji safi, hewa safi, mwanga wa jua, na baadhi ya mimea rahisi inayokua shambani. Hizi zingekuwa na ufanisi sawa na dawa zinazotumiwa chini ya majina

ya ajabu, na kutengenezwa na sayansi ya binadamu. Na zisingeacha madhara yoyote katika mwili."—Manuscript 115, 1903.

29 - DAWA ZA FAMASIA HUTOLEWA KWA IDHINI YA CHAMA CHA TIBA (MEDICAL ASSOCIATION) NA HUPEWA MAJINA MAREFU YASIYOELEWEKA KWA MTU MWENYE AKILI TIMAMU, KWA WATU WA KAWAIDA, NA NI KINYUME CHA TIBA RAHISI ZA MUNGU AMBAZO HUITWA 'ZA UONGO AU KUTAPELI (QUACK MEDICINE)'.

"Vyama vya siri vya madaktari (medical fraternity), vilivyowakilishwa kwangu kama [jamii ya siri kama vile Free Masonry) vyenye majina yake marefu, yasiyoeleweka, ambayo watu wa kawaida hawawezi kuyaelewa, lingeyaita maagizo ya Bwana kwa Hezekiah 'tiba feki au quackery au waganga wa kienyeji.' Kifo kilitamkwa juu ya mfalme, lakini aliomba apate uzima, na sala yake ikasikika. Wale waliokuwa wanamhudumia waliambiwa walete vichala vya mikuyu/tini na kuviweka kwenye kidonda, na mfalme akarejeshewa uzima ……. Bwana aligeuza mawazo yao kutoka kwenye mafumbo yao ya ajabu hadi dawa rahisi ya asili. Kuna masomo kwa ajili yetu sote katika maelekezo haya. Vijana wanaotumwa kwa Ann Arbor (Michigan State University Medical school) ili kupata elimu ambayo wanafikiri itawainua kuwa wakuu katika matibabu yao ya magonjwa kwa kutumia dawa zenye sumu, watajikuta kwamba zinapelekea kupoteza maisha badala ya kurejeshwa kwa afya na nguvu. Mchanganyiko huu husababisha mzigo mara mbili juu ya mwili/asili, na kuleta madhara kwa njia ya sumu zilizomo, hivyo maelfu ya watu hupoteza maisha yao. Ni lazima tuziache dawa za famasia peke yake, kwa kuwa katika kuzitumia tunaingiza adui kwenye mwili au mfumo. Ninaandika haya kwa sababu ni lazima kukutana na tiba ya dawa hizi za famasia unapoenda kwa madaktari katika nchi hii, na hatutaki mazoezi haya kama ilivyo, yaingie Battle Creek katikati yetu kama mwizi. Tunataka mlango ufungwe dhidi ya adui kabla ya maisha ya wanadamu kuhatarishwa."—Letter 67, 1899

(Ellen White alitaka Loma Linda ianzishwe ili "kufanya matengenezo ya mazoea ya tiba ya chama cha matibabu- medical association." Lakini kabla ya wakati huo, watu wetu kadhaa walienda katika vyuo vikuu vya serikali, kama vile University of Michigan huko Ann Arbor, ili kupata shahada ya tiba ili waweze kufanya kazi ya udaktari.)

30 - DAWA ZA FAMASIA NI TIBA ILIYOWEKWA NA ULIMWENGU

"Sio lazima kwamba wamishenari wetu wa tiba wafuate nyayo zile zilizowekwa na madaktari wa ulimwengu. Hawana haja ya kutoa madawa ya famasia kwa

wagonjwa. Hawana haja ya kuendana na dawa za madawa ya kulevya ili kuwa na ushawishi katika kazi zao. Ujumbe ulitolewa kwangu kwamba kama wangejiweka wakfu kwa Bwana, kama wangetafuta kupata ujuzi kamili wa kazi yao chini ya watu waliowekwa na Mungu, Bwana angewafanya wawe na stadi. Wakiwa wameunganishwa na Mwalimu wa Kiungu, wataelewa kwamba utegemezi wao uko juu ya Mungu, na si juu ya watu wanaojiita wenye hekima wa ulimwengu."— Letter to elder J.A. Burden, April 27, 1910.

31 - DAWA ZA FAMASIA NI NJIA YA MADAKTARI AMBAYO HATUPASWI KUTUMIA

"Ni wakati wa watu wa Mungu, wale wanaovaa ishara ya ufalme Wake, na ambao mamlaka yao yanatokana na 'Imeandikwa,' kufanya kazi. Ulimwengu ni uwanja wa kazi yetu, na tunapaswa kujitahidi kutoa ujumbe wa mwisho wa rehema kwa ulimwengu. Kila hatua na tendo letu linatazamwa kwa macho ya wivu [na wale wasio wa imani yetu]. Jihadharini kama waganga. Unaweza kumtumikia Bwana katika nafasi yako kwa kufanya kazi na mbinu mpya na kutupilia mbali dawa. Kama wanamatengenezo tunapaswa kurekebisha mazoea ya tiba, kwa kutoa elimu inayoelekeza kwenye nuru."— Medical Ministry, 125.

32 - DAWA ZENYE SUMU HULEMAZA JUHUDI ZA ASILI ZENYE KUPONYA "

Kujiendekeza katika ulaji wa mara kwa mara na kiasi kikubwahuvipa mzigo viungo vya umeng'enyaji wa chakula, na huzalisha hali ya homa kwenye mwili au mfumo. Damu inakuwa chafu, na kisha magonjwa ya aina mbalimbali hutokea. Daktari anatumwa, ambaye anaagiza dawa fulani ambayo inasaidia kwa sasa, lakini ambayo haiponyi ugonjwa huo. Inaweza kubadilisha aina ya ugonjwa huo, lakini athari halisi huongezeka mara kumi. Asili ilikuwa ikifanya kila iwezavyo ili kuondoa mlundikano wa uchafu, na ingeweza kuachwa peke yake, ikisaidiwa na baraka za kawaida za mbinguni, kama vile hewa safi na maji safi, uponyaji wa haraka na ulio salama ungeweza kufanywa."— 4 Spiritual Gifts, 133.

33 – DAWA HULETA UNAFUU SASA,LAKINI KAMWE HAZIPONYI UGONJWA

"Kuendekeza kula mara kwa mara, na rundo kubwa la chakula, huuhenyesha mfumo na viungo vya usagaji chakula, na inaleta hali ya homa kwenye mfumo. Damu inakuwa najisi, na kisha magonjwa ya aina mbalimbali hutokea. Daktari anaitwa aje, naye anaagiza baadhi ya dawa ambazo zinatoa nafuu kwa sasa, lakini hazitibu ugonjwa huo. Zinaweza tu kubadilisha aina ya ugonjwa huo, lakini uovu halisi huongezeka mara kumi. Asili ilikuwa ikifanya bidii yake ili kuondoa kwenye mfumo mkusanyiko wa uchafu, na kama ingeweza kuachwa peke yake ili kufanya kazi, na kusaidiwa na baraka za kawaida za mbinguni, kama vile hewa

safi na maji safi, uponyaji wa haraka ulio salama ungeweza kutimizwa.”—4 Spiritual Gifts, 133.

34 – DAWA HUBADILISHA TU MWONEKANO WA JUMLA WA UGONJWA

“Tumia dawa za asili—maji, jua, na hewa safi. Usitumie madawa ya famasia (drugs). Dawa za kulevya haziponyi; zenyewe hubadili tu sura za ugonjwa.”—Letter 116,1903.

35 - DAWA ZA FAMASIA (DRUGS) HUBADILISHA TU MWONEKANO/SIFA ZA JUMLA ZA UGONJWA HUO

“Madawa ya famasia kwa kawaida huwa hayatibu magonjwa. Yanabadilisha tu hali na eneo. Asili pekee ndiye mrejeshaji afya anayefaa; Na angeweza kufanya kazi yake vizuri zaidi ikiwa angeachwa peke yake. Lakini watu huupa mwili fursa hii mara chache tu. Ikiwa mwili umelemewa na unavumilia mzigo mkubwa uliotwikwa kwake, na hatimaye hutimiza kwa kiasi kikubwa kazi yake maradufu na mgonjwa anapata-nafuu, na kisha anaishi- sifa hutolewa kwa daktari. Lakini ikiwa mwili/asili utashindwa katika juhudi zake za kutoa sumu kutoka mwilini au mfumo, na mgonjwa akafa, inaitwa kipindi cha ajabu cha majaliwa. Ikiwa mgonjwa angechukua hatua ya kupitia njia sahili ya kupunguza hali ya kulemewa katika muda au msimu ufaao, na kutumia maji safi na laini kwa ufahamu, mpango huu wa vifo kupitia dawa za famasia ungeweza kuepukwa kabisa. Utumiaji wa maji unaweza kutimiza kidogo tu, ikiwa mgonjwa haoni ulazima wa kuzingatia lishe yake kwa uangalifu sana.”— 4 Spiritual Gifts, 134.

36 - DAWA ZENYE SUMU ZINAWEZA BAADAYE KUSABABISHA MATESO MAKALI

"Dawa zinapoingizwa kwenye mfumo, kwa muda zinaweza kuonekana kuwa na athari yenye manufaa. Mabadiliko yanaweza kutokea, lakini ugonjwa haujaponywa. Itajidhihirisha kwa baadaye kwa namna nyingine. Katika jitihada za asili za kufukuza madawa ya kulevya kutoka kwenye mfumo, mateso makali wakati mwingine husababisha kwa mgonjwa. Na ugonjwa huo, ambao dawa hiyo ilitolewa ili kuutibu, unaweza kutoweka, lakini ukatokea tena katika hali (namna nyingine) mpya, kama vile hali ya magonjwa ya ngozi, vidonda, viungo vyenye maumivu, na nyakati nyingine katika hali mbaya zaidi, inayoleta kifo.”— 4 Spiritual Gifts, 135

37 - DAWA NI SUMU AMBAYO ITAFANYA MADHARA MAKUBWA BAADAYE

Watu wanatakiwa kufundishwa kuwa dawa hazitibu au kuponya magonjwa. Ni kweli kwamba nyakati fulani zinaleta kana kwamba ana nafuu ya muda mfupi, na

mgonjwa huonekana kupata nafuu kama matokeo ya dawa hizo; hii ni kwa sababu maumbile ya asili yana nguvu hai ya kutosha kupambana ugonjwa na kuondoa sumu na kisha kurekebisha hali zilizosababisha ugonjwa huo. Afya inarejeshwa licha ya kutokuwa na dawa. Lakini katika matatizo mengi ya kuugua, dawa hubadilisha tu sura na eneo la ugonjwa huo. Mara nyingi athari ya sumu itokanayo na madawa kwa muda huonekana kama haipo, lakini matokeo hubakia kwenye mfumo na hufanya madhara makubwa katika kipindi fulani cha baadaye. —Ministry of Healing 126. [MH 126.3]

38 - DAWA ZENYE SUMU HUACHA ATHARI MBAYA

“Majaribio ya kutumia dawa zenye sumu ni shughuli ya gharama kubwa sana. Hakupaswi kuwekwa kitu chochote katika mwili au mfumo wa kibinadamu ambacho kitaacha matokeo mabaya.”—Medical Ministry, 228.

“Tiba rahisi zaidi zinaweza kusaidia asili, na zisiache madhara yoyote baada ya matumizi yake.”—Letter 82, 1897.

39 - DAWA ZA FAMASIA HUACHA MATOKEO MABAYA KATIKA MWILI MZIMA

“Kila matayarisho ya dawa yenye sumu katika jamii za mboga-mboga au mimea na madini, yakiingizwa katika mwili au mfumo, yataacha matokeo yake mabaya, yanayoathiri ini na mapafu, na kuharibu mfumo kwa ujumla.”— 4 Spiritual Gifts, 140.

40 - MADAWA YA FAMASISA (DRUGS) NI SUMU AMBAYO HUACHA ATHARI MBAYA NA KUHARIBU UWEZO WA MGONJWA KUJISAIDIA

"Tiba rahisi za asili zitasaidia kupona bila kuacha athari mbaya ambazo mara nyingi huhisiwa na wale wanaotumia dawa zenye sumu. Dawa zinaharibu uwezo wa mgonjwa kujisaidia. Nguvu hii ambayo wagonjwa wanapaswa kufundishwa kufanya mazoezi kwa kujifunza kula vyakula rahisi na vyenye afya—kwa kukataa kuzika tumboni rundo vyakula mbalimbali kwenye mlo mmoja. Mambo haya yote yanapaswa kufundishwa wakati wa kuwaelimisha wagonjwa. Mazungumzo yanapaswa kutolewa ili kuonyesha jinsi ya kutunza afya, jinsi ya kuepuka ugonjwa, jinsi ya kupumzika wakati kupumzika kunapohitajika.”—Letter 82, 1908.

41 - DAWA ZENYE SUMU HUBADILISHA UGONJWA KWA SABABU NI SUMU YA POLEPOLE

“Wengi hubakia katika ujinga usio na udhuru kuhusiana na sheria za mwili wao. Wanashangaa kwa nini jamii yetu ya ubinadamu ni dhaifu sana, na kwa nini wengi hufa kabla ya wakati. Je, hakuna sababu? Madaktari wanaodai kuwa

wanaelewa mfumo wa binadamu, huwaagizia wagonjwa wao dawa, na hata kwa watoto wao wapendwa na marafiki zao, polepole sumu hii huingia kwenye kusambaratisha ugonjwa huo, au kuponya kwa kiasi kidogo tu tatizo. Hakika, hawawezi kutambua ubaya wa mambo haya kama yalivyowasilishwa mbele yangu, au hawakuweza kufanya hivyo. Madhara ya sumu yanaweza yasitambuliwe mara moja, lakini sumu inafanya kazi yake kwa uhakika katika mfumo, itadhoofisha viungo, na kulemaza asili katika juhudi zake. Wanatafuta kusahihisha uovu, lakini huleta ugonjwa na madhara makubwa zaidi, ambayo mara nyingi hayawezi kuponywa."— 4 Spiritual Gifts, 137.

42 - DAWA ZA FAMASIA HUINGIZA SUMU KWENYE DAMU

Katika vituo vyetu vya sanitariums, tunapendekeza matumizi ya tiba rahisi. Hatuwahamasishi watu kutumia dawa za famasia zenye sumu, kwani zinatia sumu katika mzunguko wa damu. Katika taasisi hizi mafundisho yenye busara yanapaswa kutolewa jinsi ya kula, jinsi ya kunywa, jinsi ya kuvaa, na jinsi ya kuishi ili afya ihifadhiwe. —Counsels on Diet and Foods, 303.

43 - DAWA ZA FAMASIA HUDHOOFISHA MFUMO TU

"Wengi hutenda kana kwamba afya na magonjwa ni vitu visivyotegemea kabisa mwenendo wao, na nje ya uwezo wao kabisa…… . Mashambulizi makali ya magonjwa wanayoamini kuwa ni vipindi maalum vya majaliwa, au matokeo ya uwezo fulani wa nguvu inayotawala, au nguvu inayoshindwa kuzuiwa; Na wanatumia dawa zenye sumu kama tiba ya uovu huo. Lakini dawa zinazotumiwa kutibu ugonjwa huo hudhoofisha mfumo huo."—Medical Ministry, 296-297.

44 - DAWA ZENYE SUMU HUNYANGUA MFUMO WA NEVA/FAHAMU

"Dawa zenye sumu zinazotolewa ili kusisimua [kutuliza, kustarehesha, kutia ganzi], vyovyote zitakavyokuwa, huharibu mfumo wa neva."—How to live, Number 3, page 57.

45 - DAWA ZENYE SUMU NI UVUMBUZI WA KUHARIBU AFYA

"Suala hilo liliwekwa wazi mbele yangu, na mzigo wa kusikitisha wa matokeo ya dawa za famasia uliletwa kwangu- nuru niliyopewa ni kwamba Waadventista Wasabato wanapaswa kuanzisha taasisi za afya, wakitupilia mbali uvumbuzi huu wote wa kuharibu afya, na madaktari wanapaswa kuwatibu wagonjwa kwa kanuni za afya na usafi." —Letter K-82, 1897, dated February 10, 1897.

46 - DAWA ZENYE SUMU MARA NYINGI HUSABABISHA UGONJWA UNAOENDELEA KUKAA MWILINI.

“Wale ambao wanashughulikia hivyo ugonjwa, ni wagonjwa kila mara, na wana dozi ya dawa kila mara…….. Na bado wengi wamepofushwa, hawaoni kwamba dawa zote walizotumia hazijawaponya, lakini zimewafanya kuwa na hali mbaya zaidi. Mgonjwa aliyelemaa kwa madawa anaudhika kirahisi, lakini kwa ujumla hali yake ni mbaya, na hii inamkera mgonjwa kila wakati na kusababishiwa maisha duni, na anaonekana kuishi tu kwa kuwapa wengine zoezi la kumvumilia yeye wakati wote. Dawa zenye sumu hazijawaua watu moja kwa moja, kwa maana asili haijaacha kujaribu kushikilia maisha yake. Asili haiko tayari kusitisha mapambano yake. Hata hivyo wanywaji dawa hawa hawako salama kamwe. Sikuzote wanapata kikohozi, na mafua, ambayo husababisha mateso makali, kwa sababu ya sumu katika mfumo wao wote.”— 4 Spiritual Gifts, 137-138.

47 - DAWA ZENYE SUMU HATIMAYE HUVUNJA NGUVU MUHIMU

"Dawa za famasia huwa na tabia ya kuvunja na kuharibu nguvu muhimu, na asili inakuwa kilema kikubwa katika juhudi zake, kiasi huyu kilema hukosa uwezo na hufa, sio kwa sababu alihitaji kufa, lakini kwa sababu asili ilishambuliwa. Ikiwa asili ingeachwa peke yake, ingefanya jitihada zake kuu zaidi kuokoa maisha na afya.”— Medical Ministry, 223.

48 - MADAWA YA FAMASIA NI SUMU AMBAYO HULETA UGONJWA WA MAISHA KWA WENGINE NA MIELEKEO YA URAIBU KWA WENGINE

Kwa kutumia dawa zenye sumu, wengi hujiletea wenyewe magonjwa ya kudumu maishani mwao, na watu wengi wamepoteza maisha yao, ambao wangeweza kuokolewa kwa kutumia njia za asili za uponyaji. Sumu zilizomo katika dawa nyingi ziitwazo tiba/remedies huunda tabia na hamu ya kula ambayo inamaanisha uharibifu kwa roho na mwili. Dawa hizi nyingi na maarufu za nostrum, zinazonunuliwa bila hata ya maagizo ya Daktari, zinazoitwa dawa za kaunta ambazo hazihitaji maagizo au maelekezo ya tiba toka kwa daktari unapotaka kununua (non-Prescription drugs-Rx) na hata baadhi ya dawa zinazotolewa na madaktari (za famasia zinazoitwa dawa za magharibi au za wazungu), hushiriki katika kuweka msingi wa tabia ya uraibu wa vileo, wa bangi, uraibu wa mofini, ambazo ni laana mbaya sana kwa jamii (dawa nyingi za maumivu zitumiwapo baada ya muda hujenga uraibu maana ni vileo- narcotic). — Ministry of Healing, 126-127. [MH 126.4; HU Aya ya 7]

49 - DAWA ZENYE SUMU NI MBEGU ZA KIFO ZILIZOPANDWA MWILINI

"Unapoelewa fiziolojia kwa maana yake halisi, bili zako za dawa zitakuwa ndogo sana, na mwishowe utaacha kushughulikia dawa kabisa. Daktari ambaye

anategemea dawa zenye sumu katika utendaji wake, anaonyesha ni kwa jinsi gani haelewi kuhusu utendaji nyeti wa mwili wa mwanadamu. Anaingiza katika mfumo wa utendaji mazao ya mbegu ambayo hayatawahi kupoteza sifa yake ya uharibifu katika maisha yote. Ninakuambia hivi kwa sababu sithubutu kukuficha habari hii. Kristo alilipa gharama nyingi sana kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu ili mwili wake mwanadamu usitendewe vibaya kwa jinsi ambavyo dawa zenye sumu zinavyoutendea”—2 Selected Messages, 283-284.

50 - DAWA ZENYE SUMU NI MBEGU ZILIZOWEKWA KWENYE MFUMO AMBAO UTAZAA MAVUNO MACHUNGU

"Tiba za Kristo husafisha mfumo. Lakini Shetani amemjaribu mwanadamu kuingiza katika mfumo tiba inayodhoofisha utendaji wa mfumo wa kibinadamu, kuziba na kuharibu mipango safi na mizuri ya Mungu. Dawa zinazotolewa kwa wagonjwa hazileti uzima, lakini zinaharibu. Dawa zenye sumu haziponyi. Badala yake, huleta katika mfumo mbegu ambazo huzaa mavuno machungu sana.”—2 Selected Messages, 289.

51 - DAWA ZENYE SUMU HAZIUPI UHURU MWILI

"Suala la matengenezo ya afya halijasisitizwa kama inavyopaswa kuwa na itakavyokuwa. Mlo rahisi na kutokuwepo kabisa kwa dawa zenye sumu, na kuacha mwili huru kurejesha nguvu zilizopotea za mwili, kunaweza kufanya vituo vyetu vya sanitarium kuwa na ufanisi zaidi katika kurejesha wagonjwa katika afya. —Healthful Living, 248.

52 - DAWA ZA FAMASIA HUZUIA ASILI(MWILI WA ASILI KUJIPONYA)

“Katika mazoea yao yote wanadamu wamedhihirisha kutojali kuhusu afya na maisha…….. Katika dhiki na maumivu yao wanaenda kwa daktari, na kuamini miili yao iko mikononi mwake, wakitarajia kwamba atawaponya. Daktari anawapa dawa zenye sumu, ambayo asili yake hawajui chochote kuihusu, na kwa ujasiri wao na upofu wao wanameza chochote ambacho daktari anaweza kuchagua kuwapa. Kwa hivyo sumu kali mara nyingi hutolewa, ambayo huzuia asili/mwili katika juhudi zake zote za kusaidia kupona kutokana na unyanyasaji ambao mfumo umeteseka. —How to Live, 49.

53 - DAWA ZENYE SUMU ZINAHITAJI JUHUDI ZA KISHUJAA NA MWILI

"Ingawa mgonjwa anaweza kupata nafuu, lakini juhudi kubwa ya asili/mwili itahitajika ili kushinda sumu, iliyoumiza viungo vya mwili na kufupisha maisha ya mgonjwa. Kuna wengi ambao hawafi chini ya madhara ya dawa zenye sumu,

lakini kuna wengi sana ambao wameachwa kwenye hali mbaya ya ulema, hata wasiweze kuwa na manufaa, tumaini huisha, wanakuwa ni wenye huzuni, na wenye taabu,na hakika ni mzigo kwao wenyewe na kwa jamii."—How to live, 50.

54 - DAWA ZENYE SUMU ZINAWEZA KUSHINDA MFUMO WA BINADAMU

"Mama ambaye analikuwa anaumwa kidogo tu, na ambaye angeweza kupata tu nafuu kwa njia ya kufunga kwa kuacha kula (kanuni) chakula kwa muda mfupi, na kuacha kazi, na kuwa na utulivu na kupumzika naye angekuwa sawa; ila badala ya kufanya hivyo, alijikuta amemwita daktari. Na daktari, ambaye angepaswa kuwa tayari kutoa maelekezo machache rahisi na kanuni za kuepuka kwenye ulaji, na hivyo kumweka kwenye njia sahihi, naye akakutwa hana uelewa (ni mjinga) kuhusu kufanya hivyo, au akawa na shauku kubwa ya kupata malipo yake kama daktari. Hivyo anafanya ugonjwa huo uunekane kuwa ni mbaya sana dawa zake zenye sumu ambazo, kama yeye mwenyewe angekuwa mgonjwa, hangethubutu kuzichukua, yupo huru kuwapa wengine. Mgonjwa anazidi kuwa na hali mbaya, na dawa za sumu hutolewa kwa uhuru zaidi (bila kizuizi) mpaka asili inazidiwa nguvu kutokana na jitihada za hizo dawa, na inakoma kukabiliana, na kisha mama huyo hufa. Mama huyu alipewa dawa za sumu hadi akafa. Mfumo wake unakuwa na sumu zaidi ya dawa. Mbingu ilitamani mama huyo aishi, na kifo chake kisichotarajiwa kilimvunjia Mungu heshima. Tabia mbaya za mama, na kutozingatia sheria za mwili wake, zilimfanya kuwa mgonjwa. Na dawa za daktari ambazo zipo kwenye fasheni na ambazo zililetwa kwenye mfumo, zilikikata kipindi chake cha kuishi, na akaliacha kundi lake dogo, lisilo na msaada, kwani lilikuwa, limepigwa kwa kutokuwa na mama."— How to Live, 52.

55 - DAWA ZENYE SUMU ZINAUA, IKIWA HAZITAPINGWA MARA MOJA NA MWILI

"Mwelekeo wa kutumia dawa zenye sumu, ambazo huua badala ya kutibu, unahitaji kulindwa dhidi ya……. Wengi wametibiwa na dawa zenye sumu na matokeo yake ni kifo. Madaktari wetu, kwa kutumia dawa zenye sumu, wamepoteza maisha ya wengi ambao wasingekufa endapo madaktari wasingeleta sumu zao kwenye chumba cha wagonjwa."—Medical Ministry, 227- 229.

56 - DAWA ZENYE SUMU ZIMELETA VIFO VINGI ZAIDI KATIKA ULIMWENGU HUU KULIKO UPONYAJI AU MSAADA

"Kuhusu dawa zinazotumika katika taasisi zetu, ni kinyume na nuru ambayo Bwana amependezwa kuitoa. Shughuli ya kutoa madawa kwa wagonjwa imefanya madhara zaidi kwa ulimwengu wetu na kuua zaidi kuliko kusaidia au kuponya (the drugging business). Nilipewa nuru kwanza kwamba, ni kwa nini taasisi zetu

za Sanitarium zinapaswa kuanzishwa. Sababu ya Sanitarium zetu kuanzishwa ni kufanya matengenezo kuhusiana na utendaji wa taaluma ya madaktari (reform medical practice).”—Medical Ministry, 27.

57 - DAWA ZENYE SUMU NDIO SABABU KUU YA IDADI KUBWA YA VIFO

"Nilionyeshwa kuwa vifo vingi vimesababishwa na unywaji wa dawa kuliko sababu zingine zote kwa pamoja (zikijumlishwa zote). Kama kungekuwa na daktari mmoja tu kati ya Watu maelfu, kiasi kikubwa cha vifo vya mapema kingezuiwa. Wingi wa madaktari, na wingi wa dawa zenye sumu, umelaani wakaaji wa dunia, na umebeba maelfu na makumi elfu hadi kwenye makaburi yasiyotarajiwa.”— 4 Spiritual Gifts, 133.

58 - DAWA ZENYE SUMU HUTHAMINIWA NA WALE WALIO NA HARAKA: KUCHANGANYA DAWA HUZIFANYA ZILETE KIFO KWA HARAKA ZAIDI- HUZIFANYA ZIWE NA SUMU ZAIDI ZENYE KUFISHA

“Wagonjwa wana haraka ya kupona, na marafiki wa wagonjwa hawana subira. Wangependa kupata dawa haraka, na ikiwa hawatahisi ushawishi huo wenye nguvu juu ya mifumo yao ya mwili ambayo mawazo yao potovu yanawaongoza kufikiri wanapaswa kuhisi, wanabadili Daktari haraka bila subira na kujipatia daktari mwingine. Mabadiliko mara haya nyingi huongeza uovu wa dawa. Mgonjwa anapitia njia ile ile ya kupewa dawa tena kama alivyokuwa na daktari wa kwanza, ila mara ya pili dawa zinakuwa na hatari zaidi kwa sababu tiba ya dawa za kwanza na za pili haziendani na mfumo huo wa mgonjwa, na inakuwa na sumu isiyoweza kurekebishwa.”—Healthful Living, 245.

59 - DAWA ZENYE SUMU SIO NJIA YA BUSARA

“Hebu n atuwasilishe Injili kwa wagonjwa, tukimuunganisha Yesu, Mponyaji Mkuu, na tiba rahisi zinazotumiwa; Na imani yetu hai [katika Mungu na katika tiba hizo rahisi] itajibiwa. Lakini wale wanaokuja kwa Mponyaji Mkuu lazima wawe tayari kufanya mapenzi Yake, kunyenyekeza nafsi zao, na kuungama dhambi zao…….. Kristo alitangaza kwamba alikuja kurejesha maisha ya wanadamu. Kazi hii inapaswa kufanywa na wafuasi wa Kristo, na inapaswa kufanywa kwa njia rahisi zaidi. Familia zinapaswa kufundishwa jinsi ya kuwatunza wagonjwa…….. Katika kazi ya uponyaji, hebu madaktari wafanye kazi kwa akili na hekima, na sio kwa madawa yenye sumu, lakini kwa kufuata njia za busara. Kisha ziache hizi tiba rahisi, kwa maombi ya imani zitumie nguvu za Mungu ili kuzuia ugonjwa kuendelea. Imani katika Kristo na nguvu ya maombi vitawatia moyo wale wanaoteseka na kuwapa ujasiri katika mbinu zetu rahisi za kutibu magonjwa.

Kazi kama hiyo itakuwa njia ya kuelekeza akili kwenye Ukweli, na jambo hili litakuwa na ufanisi mkubwa katika kazi ya huduma ya injili."—Medical Ministry 29.

"Bwana angetaka waganga wetu washirikiane naye katika kuwahudumia wagonjwa, wakionyesha imani zaidi, na kutumia dawa kwa uchache. Tumtegemee Mungu. Imani yetu ni dhaifu, na mioyo yetu haibadilishwi. Mungu angetaka kuwe na mabadiliko."—Medical Ministry, 40.

60 - KUTUMIA DAWA ZA FAMASIA AU ZENYE SUMU HAKUITAJI UFIKIRIE SANA UKILINGANISHA NA TIBA RAHISI (huhitaji uchekeche kichwa sana)

"Dawa zenye sumu zinapaswa kutupwa. Juu ya Kipengeke hiki dhamiri ya daktari lazima iwe nyeti/nyororo, kweli, na safi. Tunahitaji kuchukua tahadhari kwa mwelekeo wa utumiaji wa dawa zenye sumu, ambazo zinaua ikiwa hazitatibu. Mambo yamewekwa wazi mbele yangu kuhusiana na matumizi ya dawa zenye sumu (drugs). Wengi wametibiwa na dawa hizi za famasia na matokeo yake ni kifo. Madaktari wetu, kwa kutumia dawa zenye sumu, wamepoteza maisha ya wengi ambao hawakuhitaji kufa ikiwa wangeacha dawa zao nje ya chumba cha wagonjwa. Kesi za homa tu, zimefanya wagonjwa wafe kutokana na dawa walizopewa, wakati, kama madaktari wangeacha matibabu yao ya dawa, kama wangeweka akili zao kufanya kazi, na kwa busara na kwa kuendelea kutibu kwa ustahimilivu kwa kutumia tiba za Bwana mwenyewe - hewa bora na maji mengi - wagonjwa wangepona. Utumiaji mbaya wa vitu hivi ambavyo vilipaswa kutupiliwa mbali, umehitimisha maisha ya mgonjwa."—Medical Ministry, 227-228.

61 - DAWA ZENYE SUMU ZINAHITAJI UJUZI MDOGO

"Madaktari wengi sio waangalifu kwa kiasi cha kutosha, na hawatumii akili zao katika kushugulika na kesi za wagonjwa kwa uaminifu katika taaluma yao ya tiba. Wanaishia kutumia dawa zenye sumu, wakati ujuzi na maarifa makubwa waliyonayo vingewafundisha njia bora zaidi. Maisha yamepotezwa ambayo yangeweza kuokolewa ikiwa dawa hizi za famasia zisingetumiwa. Kama sheria, kadiri dawa zinavyotumiwa kwa kiwango kidogo zaidi, ndivyo mgonjwa atakavyofanikiwa."—Healthful Living, 247.

62 - KUFANYA MAJARIBIO NA DAWA ZENYE SUMU NI MAJARIBIO YA GHARAMA KUBWA

"Kufanya majaribio na dawa zenye sumu ni mradi wa gharama kubwa sana. Kupooza kwa ubongo na ulimi mara nyingi ni matokeo, na wahasiriwa hufa kifo kisicho cha kawaida, wakati, kama wangetendewa kwa uvumilivu, kwa bidii

isiyochoka, isiyo na ulegevu na maji ya moto na baridi, vitambaa vya moto vya kukandia, mito midogo ya moto na baridi ya kukandia (packs), na kufunikwa na mashuka au mablanketi katika kufukizwa kwa usalama, wangekuwa hai leo."—Medical Ministry, 228.

63 - DAWA ZINAANDIKWA KATIKA MAAGIZO NA DAKTARI (RX) BADALA YA KUMWAMBIA MGONJWA UKWELI

"Kuna wengi, wengi wanaoteseka katika ulimwengu wetu wenye sumu ya tumbaku…… Tabibu, ikiwa yeye si mgeni kwenye taaluma katika hiyo kazi, anaweza akachunguza madhara kutokana na chanzo halisi, lakini hathubutu kukataza matumizi ya sigara, kwa sababu yeye mwenyewe pia ni miongoni mwa hao wanaoendekeza uvutaji wa sigara. Wengine kwa kukosa maamuzi mazuri, wanatoa ushauri nusu-nusu wakiwashauri watumiaji wa tumbaku kuchukua kiwango kidogo cha dawa hii ya kulevya (sigara au vape); Lakini hawawaambii wagonjwa kuwa Tabia hii inakuua taratibu. Wanaagiza dawa ya kuponya ugonjwa ambao ni matokeo ya hamu ambazo sio za asili -uraibu—na madhara mawili yanatojitokeza, wakati hawajaliondoa hata dhara lile moja ambalo mngojwa alikuja nalo."—Medical Ministry, 225.

64 - DAWA ZENYE SUMU HAZIHITAJI DINI BINAFSI KWA DAKTARI

"Daima endelea kuonyesha huruma na upole wa Kristo kwa mgonjwa, na kuamsha dhamiri zao kwa imani katika uwezo Wake Bwana wa kupunguza mateso, na kuwaongoza wagonjwa kwenye imani na kumtumaini Yeye aliye Mponyaji Mkuu, nawe utakuwa umeongoa roho na mara nyingi utakuwa umeokoa maisha pia. Kwa hiyo, dini binafsi kwa madaktari wote katika chumba cha wagonjwa ni muhimu kwa mafanikio katika kutoa tiba rahisi bila madawa ya kulewesha au ya famasia. Kwa hiyo, dini binafsi ya madaktari wote katika chumba cha wagonjwa ni muhimu kwa mafanikio katika kutoa tiba rahisi bila madawa ya kulevya. Yeye ambaye ni tabibu na mlinzi na mlezi wa afya na mwili, Mungu anapaswa kufahamika kwa kila njia ili watu wajifunze masomo ya Mwalimu Mkuu—jinsi ya kufanya kazi katika Kristo na kupitia Kristo ili kuokoa roho za wagonjwa."—Medical Ministry, 234-235.

65 - DAWA SIO MAWAKALA SIO MAWAKALA WA USAFI

"Waelimishe watu katika sheria za uzima ili wajue jinsi ya kuhifadhi afya. Juhudi zinazotolewa kwa sasa haziendani na mapenzi ya Mungu. Dawa za famasia zenye sumu ni laana kwa kizazi hiki kilichoelimika (drugs). Elimisha watu mbali na madawa ya famasia. Zitumie kwa udogo sana, naam udogo sana, na tegemea

zaidi mawakala wa afya; Kisha asili itaitikia madaktari wa Mungu yaani—hewa safi, maji safi, mazoezi yanayofaa, dhamiri safi. Wengi wanaweza kupona bila hata chembe moja ya dawa, ikiwa wangeishi kulingana na sheria za afya. Tumia dawa za famasia kwa nadra sana. Zinahitajika juhudi za dhati, na subira, kwa muda mrefu ili kuanzisha kazi hiyo na kuiendeleza kwa kanuni za afya. Lakini hebu maombi ya bidii na imani viunganishwe na juhudi zako, nawe utafanikiwa. Kwa kazi hii utakuwa ukiwafundisha wagonjwa, na watu wengine pia, jinsi ya kujitunza wenyewe wakiwa wagonjwa, bila ya kutumia dawa zenye sumu."—Medical Ministry, 259-260.

66 - DAWA SIO NJIA ZA BUSARA ZA TIBA

"Bwana amenionyesha kwamba kunapaswa kuwa na vituo vya sanitarium karibu na miji mingi muhimu …….. Maeneo yanayofaa lazima yatafutwe na kupatikana, ambapo tunaweza kuwaleta wagonjwa na watu wanaoteseka mbali na miji, ambao hawajui lolote kuhusu watu wetu, na wala Ukweli wowote wa Biblia. Kila juhudi inayowezekana inapaswa kufanywa ili kuonyesha wagonjwa kwamba ugonjwa unaweza kuponywa kwa njia za busara za tiba, bila kukimbilia dawa zinazodhuru. Hebu wagonjwa watenganishwe na mazingira hatarishi na mahusiano ya namna fulani, na kuwekwa katika sehemu zetu za vituo vya afya, ambapo wanaweza kupokea tiba kutoka kwa wauguzi na waganga Wa Kikristo, na hivyo wanaweza kukutana na Neno la Mungu na kulifahamu Neno la Mungu."—Evangelism, 534-535.

67 - DAWA ZA FAMASIA SIO TIBA RAHISI NA TIBA ASILIA

"Katika njia ya Mwokozi ya uponyaji kulikuwa na masomo kwa wanafunzi Wake. Wakati mmoja Kristo aliyapaka macho ya kipofu kwa udongo na kumwambia, "Nenda ukanawe katika bwawa la Siloamu.... Basi akaenda, akanawa, akaja akiona." Yohana 9:7. Tiba hiyo ingeweza kufanywa tu kwa uweza wa Mponyaji Mkuu, lakini Kristo alitumia njia rahisi ya asili. Ingawa Yeye hakupendezwa na dawa zile tunazozijua za hospitalini, Aliidhinisha matumizi ya tiba rahisi na za asilia." - Desire of Ages, 824.

68 - DAWA ZENYE SUMU HULETA MATESO YA MWILI NA UDHAIFU

"Ameteseka sana kwa maradhi ya mwili.. . Ni mmoja wa wale ambao mfumo wake umemtiwa sumu kwa madawa (ya hospitali). Kwa kutumia hizi dawa amejiletea hali yake kuwa hivyo..." —Shuhuda kwa Kanisa 2: 184.

69. MADAWA HUDHOOFISHA MFUMO NA KUUFANYA KUPATA MAGONJWA KIRAHISI

“Badala ya kuchukua njia ya kukabiliana na ugonjwa, ninyi mnaudekesha ugonjwa na kujisalimisha katika nguvu zake. Mnapaswa kuepuka matumizi ya madawa na mzingatie kwa uangalifu sheria za afya. Kama mnayajali maisha yenu mnapaswa kula chakula rahisi (jamii ya matunda, nafaka, maharage, mboga-mboga na karanga bila viungo vingi), kilichoandaliwa kwa njia rahisi, na kufanya zaidi mazoezi ya mwili. Kila mwanafamilia anahitaji faida za matengenezo ya afya. Lakini madawa yanapaswa kuachwa milele; kwa sababu hayaponyi ugonjwa wowote, bali yanadhoofisha mfumo, na kufanya iwe rahisi kupata magonjwa." - Shuhuda kwa Kanisa 5: 311

70 - DAWA ZINAWEZA KULETA SUMU KWENYE DAMU

“Tumeagizwa kwamba katika matibabu yetu ya wagonjwa tunapaswa kutupilia mbali matumizi ya dawa zenye sumu…….Kuna mitishamba (herbs) rahisi ambayo inaweza kutumika kwa ajili ya kuponya wagonjwa, ambayo athari yake juu ya mfumo ni tofauti sana na ile ya dawa hizo ambazo hutia sumu kwenye damu na kuhatarisha maisha.”—Manuscript 73, 1908.

71 - DAWA ZA FAMASIA KAZI KWA KUTIA SUMU MKONDO WA DAMU

Katika vituo vyetu vya Sanitarium (tiba sahili), tunapendekeza matumizi ya tiba rahisi. Tunakataa matumizi ya dawa zenye sumu, kwani zinasumisha mzunguko wa damu. Katika taasisi hizi mafundisho yenye busara yanapaswa kutolewa jinsi ya kula, jinsi ya kunywa, jinsi ya kuvaa, na jinsi ya kuishi ili afya ihifadhiwe. — Counsels on Diet and Foods, 303.

72 - DAWA ZENYE SUMU HUSHUGHULIKA BILA HURUMA KWENYE MWILI- (hushughulika kwa ukatili na mwili)

“Kuna simulizi la kutisha linalopaswa kutolewa kwa Mungu na watu ambao hawajali sana maisha ya mwanadamu kiasi cha kuutendea mwili huo bila huruma katika kushughulikia dawa zao. Sisi hatuna udhuru ikiwa kwa ujinga tutaharibu jengo la Mungu kwa kuingiza ndani ya matumbo yetu dawa zenye sumu zilizopewa majina mbalimbali ambayo hatuyaelewi. Ni wajibu wetu kukataa maagizo yote hayo ya madawa. Tunataka kujenga kituo cha sanitarium [nchini Australia] mahali ambapo magonjwa yanaweza kuponywa kwa vitu vya asili, na ambapo watu wanaweza kufundishwa jinsi ya kujihudumia wakiwa wagonjwa, ambapo watajifunza kula chakula kizuri kwa kiasi, na kuelimishwa kukataa yote yasiyofaa. Madawa ya kulevya—chai, kahawa, divai zilizochacha, na vichocheo vya kila aina—na kutupilia mbali nyama ya wanyama waliokufa.” — Temperance, 88-89.

73 - DAWA ZENYE SUMU HUSABABISHA UGONJWA KUTOWEKA - NA BAADAYE KUTOKEZEA TENA MAHALI PENGINE

"Ini, moyo na ubongo huathiriwa mara kwa mara na dawa zenye sumu, na mara nyingi viungo hivi vyote hulemewa na magonjwa, na watu wenye bahati mbaya, ikiwa wataishi, wanakuwa walemavu wa maisha, kwa uchovu wa maisha duni. Je, dawa hiyo yenye sumu ilimgharimu mtu kiasi gani? Ikiwa haikugharimu maisha, iligharimu sana. Mwili wote umekuwa mlemavu katika juhudi zake zote, hali ya utendaji yote ya mashine ya mwili, iko nje ya utaratibu; na katika kipindi kijacho maishani, wakati kazi hizi nzuri ambazo zimejeruhiwa zinapaswa kutegemewa kuchukua sehemu muhimu zaidi……. Haziwezi kufanya kazi yao kwa urahisi na kwa nguvu, na mfumo mzima unahisi ukosefu. Viungo hivi ambavyo vinapaswa kuwa katika hali nzuri, vimedhoofika, damu inakuwa chafu. Mwili huendelea kuhangaika, na mgonjwa hupatwa na maradhi tofauti, mpaka kunapokuwa na kuvunjika kwa ghafula katika jitihada zake na kifo cha mtu hufuata."— 4 Spiritual Gifts, 135.

74 - DAWA ZA FAMASIA ZINAUSHINIKIZA MWILI KWA SUMU AMBAYO HAIWEZI KUTOKA

"Maisha ya wengi sana yameangamizwa na madaktari wanaotumia dawa za magonjwa yasiyojulikana……Mgonjwa lazima apewe dawa, majaribio na vipimo vilijaribu kumponya mgonjwa ….. Mwili umejaa dawa zenye sumu ambazo hauwezi kuzitoa kwenye mfumo. Mara nyingi madaktari wenyewe wamesadiki na kukiri kwamba wametumia dawa zenye nguvu kwa ajili ya ugonjwa ambao haukuwepo, na matokeo yalikuwa ni kifo."— 4 Spiritual Gifts, 135-136.

75 - ATHARI ZA DAWA HAZIWEZI KUTAMBULIWA MARA MOJA

"Athari za sumu za dawa zinaweza zisitambuliwe mara moja, lakini sumu hiyo inafanya kazi yake kwa hakika katika mfumo, ili kudhoofisha viungo, na kuulemaza mwili katika juhudi zake. Madaktari wanatafuta kurekebisha madhara, lakini wanazalisha madhara makubwa zaidi, ambayo mara nyingi hayawezi kuponya. Wale ambao wanashughulikiwa hivyo ni wagonjwa kila wakati, na wana dozi ya dawa kila wakati. Na bado, ikiwa unasikiliza mazungumzo yao, mara nyingi utawasikia wakisifu dawa hizo ambazo wamekuwa wakitumia, na kupendekeza matumizi yao kwa wengine, kwa sababu wamefaidika na matumizi yao. Inaweza kuonekana kuwa kwa wale wanaoweza kufikiri juu ya sababu hadi matokeo, wangetazama mwonekano wa ngozi uliopauka, malalamiko ya mara kwa mara kuhusiana na maradhi na udhafu katika kutembea kwa jumla kwa wale wanaodai kufaidika. Hakika hili litakuwa uthibitisho wa kutosha wa dawa

zinazoharibu afya……. Na bado wengi wamepofushwa hivi kwamba hawaoni kwamba dawa zote wanazotumia hazijawaponya, lakini zimewafanya kuwa na hali mbaya zaidi.”— 4 Spiritual Gifts, 137.

76 - DAWA ZENYE SUMU HATIMAYE HUKOMA KUSAIDIA DALILI

"Hupaswi kuweka kitu chochote kwenye mfumo ambacho kitaacha madhara mabaya. Na kwa kubeba nuru katika somo hili, jambo jema kwa mwili ni kufanya mazoezi ya afya na usafi, na ndiyo sababu ambayo nimepewa ya kuanzisha vituo vya sanitarium katika maeneo mbalimbali. Nimeumia wakati wanafunzi wengi [wetu] wamehamasishwa kwenda mahali ambapo wangepata elimu ya matumizi ya dawa zenye sumu. Nuru niliyopokea juu ya suala la dawa za famasia ni tofauti kabisa na matumizi hayo katika shule hizi au kwenye vituo vya afya. Ni lazima tuwe na nuru juu ya masomo haya……Watu wengi wanaoteseka wasio wa imani yetu watakuja katika taasisi zetu kupata matibabu. Wale ambao afya yao imeharibiwa na suala la dhambi, na ambao wametibiwa na madaktari mpaka dawa walizoelekezwa zisiwe na matokeo, watakuja kwenye sanitarium; Na watafaidika. Bwana atabariki taasisi zinazofanya kazi kwa mujibu wa mipango Yake…….. Yeye Ataingia kwenye vyumba vya wagonjwa. Na Atawapa wauguzi hekima.”—Medical Ministry, 228-229.

77 - DAWA ZA FAMASIA HAZIPASWI KAMWE KUTUMIKA KATIKA TAASISI ZETU

“Daktari anayetegemea dawa za famasia katika kazi na utendaji wake, anaonyesha kwamba haelewi utendaji nyeti wa mfumo binadamu. Anaingiza katika mfumo mbegu ya zao ambalo halitapoteza kamwe sifa yake ya uharibifu katika maisha yote…… Miaka mingi iliyopita Bwana alinifunulia kwamba taasisi zinapaswa kuanzishwa ili kutibu wagonjwa bila dawa za famasia. Mwanadamu ni mali ya Mungu, na uharibifu ambao umefanywa kwa makao haya hai, na mateso yanayosababishwa na mbegu za kifo zilizopandwa katika mfumo wa kianadamu, ni kosa kwa Mungu.”—Medical Ministry, 229.

78 - DAWA ZA FAMASIA NI MBADALA MBAYA WA MATUMIZI YA MITI-SHAMBA (simple herbs)

“Nimeonyeshwa kwamba tunapaswa kuwa na wanawake wengi zaidi wanaoweza kukabiliana na magonjwa ya wanawake, wanawake wauguzi wengi zaidi, ambao watawatibu wagonjwa kwa njia rahisi na bila kutumia dawa zenye sumu . . Kuna miti-shamba (herbs) mingi ambayo, ikiwa wauguzi wetu wangejifunza thamani yake, wangeweza kuitumia miti shamba na tiba sahili, mahali pa dawa zenye sumu, na kupata matokeo mazuri sana.”—Letter 90, 1908.

79 - MWILI HAUPENDEZWI NA DAWA AU SHERIA ZA ASILI ZA UZIMA

"Kama asili/mwili, ungeachwa peke yake, basi ungeweka juhudi zake kuu ili kuokoa maisha na afya. Mwili na asili havitaki msaada wowote kama vile wengi wanavyodai kwamba wameupatia msaada. Ondoa mizigo iliyowekwa juu ya mwili, kama desturi za mitindo ya zama hizi inavyopendekeza, nawe utaona katika hali nyingi mwili utajirekebisha wenyewe. Matumizi ya dawa sio mazuri kwa mwili, asili au sheria za uhai na afya. Kutibu kwa njia ya madawa ya famasia huupatia mwili mizigo miwili ya kubeba na kushindana nayo, badala ya mmoja. Mwili unakuwa na matatizo mawili makubwa ya kuyashinda, badala ya moja."—Medical Ministry 223.

80 - DAWA ZA FAMASIA HUINGILIA SHERIA ZA ASILI

"Maelfu wanahitaji kuelimishwa kwa subira, kwa fadhili, kwa upole, lakini kwa msisitizo, kwamba kati ya malalamiko yao kumi, malalamiko tisa yanaundwa na njia zao wenyewe na hatua wanazochukua. Kadri wanavyoingiza dawa kwenye mfumo huo wa mwili, ndivyo wanavyoingilia kati sheria za asili na kuleta matatizo yale yale ambayo wao wenyewe wanajaribu kuyaepuka."—Manuscript 22, 1889.

81 - DAWA ZENYE SUMU HAZIWAJIBIKI UPONYAJI UNAOWEZA KUFUATA

"Wagonjwa wanaotumia dawa zenye sumu wanaonekana kupata nafuu. Baadhi ya watu wana nguvu za maisha za kutosha waliyozaliwa nayo kwa asili. Hawa watasaidiwa na asili kutoa sumu kutoka kwa mfumo wao na watapona, wakiwa na kipindi cha kupumzika. Lakini hakuna sifa tunayopaswa kuipa dawa,kwa kuwa huuzuia tu mwili katika juhudi zake za uponyaji. Sifa zote zinapaswa kuhusishwa na uwezo wa kurejesha wa asili-(mwili hujirekebisha wenyewe, ndiyo Mungu alivyouumba, isipokuwa katika dharura kama ajali, presha, sukari nk)."—Healthful Living, 244.

82 - DAWA ZENYE SUMU HAZINA NGUVU ZA KUPONYA

"Wagonjwa wenyewe, ikiwa wangekuwa na subira, na washugulike lishe yao kama kufunga na kuteseka kidogo, na kutoa nafasi kwa asili/mwili kujipanga ili kurejeshwa, wangepona mapema bila kutumia dawa yoyote. Asili pekee ndiyo ina nguvu za kuponya. Dawa hazina uwezo wa kuponya, lakini kwa ujumla zitazuia asili katika juhudi zake. Asili baada ya yote, lazima ifanye kazi ya kurejesha."—How to live, 70.

83 – MADAWA YA FAMASIA HUATHIRI WATU KIMWILI, KIAKILI NA KIMAADILI

“Madaktari, kwa kuwapa watu dawa, wamefanya mengi sana kuongeza uchakavu wa jamii ya ubinadamu, kimwili, kiakili na kimaadili. Kila mahali unapoenda utaona ulemavu, ugonjwa na upumbavu kichwani, ambavyo katika hali nyingi sana unaweza kufuatiliwa moja kwa moja hadi kwenye sumu ya dawa, inayotolewa na mkono wa daktari, kama dawa ya magonjwa kadhaa ya mtu. Kinachojulikana kama tiba kimejidhihirisha kwa hofu kwa mgonjwa—kwa uzoefu mkali wa mateso—nacho kimekuwa kibaya zaidi kuliko ugonjwa wenyewe, ambao dawa hiyo ilitumiwa kwa ajili yake. Wote walio na uwezo wa kawaida wanapaswa kuelewa matakwa ya mfumo wao wenyewe. Falsafa ya afya inapaswa kutunga moja ya masomo muhimu kwa watoto wetu. Ni muhimu sana mwili wa mwanadamu ueleweke, na kisha wanaume na wanawake wenye akili wanaweza kuwa matabibu wao wenyewe. Ikiwa watu wangefikiri kutoka kwenye sababu hadi matokeo, na wangefuata nuru inayowaangazia, wangefuata njia ambayo ingewahakikisha afya yao kuwa njema, na vifo vingekuwa kidogo sana. Lakini watu wako tayari sana kubaki katika ujinga usio na udhuru, na kuiamisha miili yao kwa madaktari, badala ya kuwa na jukumu lolote la pekee katika jambo hilo wenyewe (wanapenda kuwaachia watu wengine jukumu la afya lao 100%, badala ya kufanya vile wanavyoweza).”—Disease and its Causes, 53-54.

84 - DAWA ZENYE SUMU HUDHOOFISHA MOJA KWA MOJA, NA PIA KUPITIA URITHI

"Ikiwa wale wanaotumia dawa hizi wangekuwa wagonjwa, wao peke yao tu, basi uovu haungekuwa mkubwa. Lakini wazazi sio tu kwamba wanatenda dhambi dhidi yao wenyewe kwa kumeza sumu ya dawa, lakini wanatenda dhambi dhidi ya watoto wao pia. Hali mbaya ya damu yao, sumu iliyosambazwa katika mfumo mzima, mwili uliovunjika, na magonjwa mbalimbali yanayotokana na dawa—kama matokeo ya sumu ya dawa—hupitishwa kwa watoto wao, na kuwaacha wakiwa na urithi mbaya, ambao ni sababu nyingine kubwa ya kuzorota kwa jamii ya watoto wao.”—How to live, 53.

85 - DAWA ZENYE SUMU HUHATARISHA MAISHA YOTE NA HATA BAADA YA KIFO

Wale wanaofanya mazoezi ya kutumia dawa zenye sumu hutenda dhambi dhidi ya akili zao na kuhatarisha maisha yao yote ya baadaye. Kuna mimea/herbs ambayo haina madhara, matumizi ambayo yatasaidia matatizo mengi yanayoonekana kuwa makubwa. Lakini ikiwa wote wangetaka kuwa na akili kuhusiana na mahitaji yao ya kimwili, ugonjwa ungekuwa nadra badala ya jambo

kawaida. Kinga ratili moja ya kinga ina thamani kuliko kilo moja ya tiba (Kuzuia ni bora kuliko kuponya”— 2 Selected Messages, 290-291.

SURA YA 17

JINSI MAJI YANAVYOWEZA KUSAIDIA KATIKA KUPONYA WAGONJWA

MATUMIZI YA TIBA RAHISI YA MAJI KATIKA UGONJWA NA AFYA

“Wanafunzi hawa walikuwa wawe na uweza ule ule ambao Yesu alikuwa nao wa kuponya "ugonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu." Kwa kuponya magonjwa ya mwili katika Jina Lake, wangethibitisha na kushuhudia nguvu Zake kwa ajili ya kuponya moyo. Mathayo 4:23; 9:6….Hivyo ndivyo Kristo alivyowapatia wanafunzi wWke kazi ya utume. Alitoa kwa ukamilifu mahitaji/majaliwa kwa ajili ya kutenda kazi hiyo, na alibeba Mwenyewe wajibu kwa ajili ya mafanikio ya kazi hiyo. Kwa kadri ambavyo wangetii Neno Lake, na kufanya kazi kwa kuunganika naye, wasingeshindwa. Enendeni kwa mataifa yote, aliwaambia. Enendeni sehemu za mbali zinazokaliwa na watu duniani, lakini mjue kwamba uwepo Wangu uko kule. Fanyeni kazi kwa imani na ujasiri, maana hautakuja kamwe muda ambao nitawaacha.

Agizo la Mwokozi kwa wanafunzi wale liliwajumuisha waamini wote. Linahusisha wote wanaomwamini Kristo mpaka mwisho wa wakati. —The Desire of Ages, 821-822.

“Naye Bwana Yuko tayari kuponya sasa kama wakati ule alipokuwa duniani katika mwili. Watumishi wa Kristo ndio wawakilishi Wake, mifereji ya kazi Zake. Anatamani kuonyesha uweza Wake wa kuponya kupitia sisi

“Namna Mwokozi alivyoponya magonjwa mna fundisho kwa wanafunzi Wake. Katika tukio moja alipaka macho ya mtu kipofu kwa matope, na akamwambia, "Nenda kanawe katika birika ya Siloamu,…….Basi akaenda na kunawa; akarudi anaona." Yohana 9:7. Uponyaji ule ungefanywa tu kwa uweza wa Mponyaji Yule Mkuu, lakini Kristo alitumia njia nyepesi ya asili. Wakati hakuonekana akitumia tiba ya vidoge, aliruhusu matumizi ya tiba za asili nyepesi.

“Kwa wagonjwa wengi waliopokea uponyaji, Yesu alisema, "Usitende dhambi tena, lisije likakupata jambo lililo baya zaidi." Yohana 5:14. Hivyo alifundisha kwamba ugonjwa ni matokeo ya kukiuka sheria za Mungu, zote mbili, yaani, za asili na za kiroho. Maumivu makubwa duniani yasingekuwepo ikiwa watu wangedumu kuishi kulingana na mpango wa Mwumbaji. .

“Tunapaswa tuwe watenda-kazi pamoja na Mungu kwa ajili ya kurejesha afya ya mwili na ya roho.

“Na tunapaswa tufundishe wengine namna ya kuhifadhi na kurejesha afya. Kwa wagonjwa tunapaswa kutumia tiba ambayo Mungu ametoa katika vitu vya asili, na tunapaswa tuwaelekeze watu Kwake Yeye pekee, awezaye kurejesha. Ni kazi yetu kuwapeleka wagonjwa na wenye mateso kwa Kristo katika mikono ya imani yetu. Tunapaswa tuwafundishe watu kumwamini Mponyaji Mkuu. Tunapaswa tushikilie ahadi Zake, na kuomba udhihirisho wa nguvu Zake. Kiini chenyewe cha injili ni urejeshaji, na Mwokozi anatutaka tuwafanye wagonjwa, wasio na tumaini, na wenye shida washikilie nguvu Zake.” -Desire of Ages, 821-825.

1 - UMUHIMU WA TIBA YA MAJI

Tumaini pekee la mambo yaliyo bora ni katika kuwaelimisha watu kanuni sahihi. Madaktari wawafundishe watu kwamba nguvu za urejeshwaji hazipo katika madawa, bali katika asili. Ugonjwa ni juhudi ya maumbile ya asili kuuweka mfumo huru kutoka kwenye hali iliyosababishwa na ukiukaji wa sheria za afya. Pale mtu anapopatwa na ugonjwa, sababu ya kuja kwa huo ugonjwa inapaswa kutambuliwa-kueleweka. Tabia mbaya yafaa zibadilishwe.Mazoea mabaya yarekebishwe. Kisha asili inapaswa kusaidiwa katika juhudi zake za kuondoa uchafu mwili na kuweka upya hali sahihi katika mfumo. Hewa safi, mwanga wa jua, kuwa na kiasi, pumziko, kufanya mazoezi, chakula kinachofaa, matumizi ya maji, kumtumaini Mungu na uweza Wake—hizi ndizo tiba za Kweli. Kila mtu apaswa kuwa na maarifa ya maumbile- asili yaletayo uponyaji na jinsi ya kuyatumia (azifahamu tiba nane rahisi na kuzitumia, ikiwemo usafi, roho ya shukrani, mtazamo wa maisha, na kuhudumia watu). Ni muhimu pia kuelewa kanuni zinazohusika katika tiba ya wagonjwa na kuwa na uzoefu wa vitendo

utakaomwezesha mtu kutumia ujuzi huo kwa njia ifaayo. Matumizi ya tiba za asili yanahitaji kiasi kikubwa cha uangalifu na jitihada, mambo ambayo wengi hawako tayari kuyafanyia kazi. Mchakato wa asili wa uponyaji na kuujenga mwili tena pale ulipoharibika ni wa taratibu ila una uhakika, na kwa wale wasio na subira, huona mambo yanaenda polepole sana kwao. Kusalimisha vile vitu vinavyoendekezwa au kujifurahisha navyo kunahitaji kujitoa kafara. Lakini mwishowe itagunduliwa kwamba asili, isipozuiwa, hufanya kazi yake kwa busara na kwa ubora. Wale wanaodumu katika kuzitii sheria zake watavuna thawabu katika afya zao za mwili na akili. —Ministry of Healing, 127.

"Maelfu wamekufa kwa kukosa maji safi na hewa safi, ambao wangeweza kuishi. Na maelfu ya walemavu, ambao ni mzigo kwao wenyewe na kwa wengine, wanafikiri kwamba maisha yao yanategemea kuchukua dawa kutoka kwa madaktari. Wanaendelea kujilinda dhidi ya hewa safi nje, na kuepuka matumizi ya maji. Baraka hizi wanazohitaji ili kuwa wazima wanaziepa. Ikiwa wangepata nuru, na kuacha dawa peke yake, na kujizoeza kufanya mazoezi ya nje, na hewa ndani ya nyumba zao wakati wa kiangazi na msimu wa baridi, na kutumia maji laini kwa madhumuni ya kunywa na kuoga, wangekuwa vizuri na wenye furaha, badala ya kuwa katika maisha duni (maji laini-soft water). —Counsels on Health, 55-56.

"Uchafu wa mwili, ikiwa hautatolewa, hurudishwa ndani ya damu, na kushinikizwa kwenye viungo vya ndani. Mwili, ili utoe uchafu wa hiyo sumu, hufanya jitihada za kuukomboa mfumo. Jitihada hii hupelekea kuwepo kwa homa, na kile kinachoitwa ugonjwa. Lakini hata hivyo, ikiwa wale wanaoteseka wangeusaidia mwili katika jitihada zake, kwa kutumia maji safi, na laini, mateso mengi yangezuiwa. Lakini wengi, badala ya kufanya hivyo, na kutafuta kuondoa sumu kutoka kwenye mfumo, huchukua sumu hatari zaidi kwenye mfumo, ili kuondoa sumu ambayo tayari iko.”— Counsels on Health, 61-62.

“Hewa safi, maji mazuri, mwanga wa jua, mazingira mazuri ya asili—hizi ndizo njia Zake za kuwarejeshea wagonjwa afya kupitia njia za asili.”— Counsels on Health, 166.

“Vitu vya asili ni baraka za Mungu, tunapewa ili kuleta afya kwa mwili, akili, na nafsi. Hutolewa ili zilete uzima kwenye uzima, na kwa wagonjwa ili kuwaponya. Vikitumika kwa pamoja na tiba ya maji, vinafaa zaidi katika kurejesha afya kuliko dawa zote za famasia za hapa duniani.”— Counsels on Health, 169.

“Hebu mtu yeyote asipate wazo kwamba taasisi ni mahali pake pa kuja kuponywa na kunyanyuka kwa maombi ya imani. Hapo ni mahali pa kupata nafuu

ya magonjwa kwa tiba na mtindo wa maisha mzuri, na kujifunza jinsi ya kuepukana na magonjwa. Lakini ikiwa kuna sehemu moja chini ya mbingu zaidi ya nyingine ambapo sala inayotuliza, yenye huruma inapaswa kutolewa na wanaume na wanawake waliojitoa na wenye imani ni katika taasisi kama hiyo. Wale wanaowatibu wagonjwa wanapaswa kusonga mbele katika kazi yao muhimu wakimtegemea sana Mungu kwa baraka Zake na kutumia rasilimali ambazo amezitoa kwa neema, na ambazo kwa rehema Zake amevuta usikivu wetu kama hewa safi, usafi, lishe bora, vipindi sahihi vya kazi na mapumziko, na matumizi ya maji." —Shuhuda kwa Kanisa, 1: 561.

"Kuna njia nyingi za kufanya uponyaji, lakini ipo njia moja tu ambayo mbingu inaikubali. Dawa zipatikanazo kutoka kwa Mungu ni za asili na ambazo hazitozi ushuru mwili au kudhoofisha mifumo ya mwili kwa sababu ya sifa zake kuu. Hewa safi, maji, usafi, lishe sahihi, maisha safi, usafi na imani thabiti kwa Mungu ni tiba kwa mahitaji mengi ambayo maelfu wanakufa kwa kuzikosa; lakini tiba hizi watu wamezifanya zionekane kuwa zimepitwa na wakati kwa sababu matumizi yake na uandaaji wake unahitaji ustadi maalum ambao watu hawauthamini. Hewa safi, mazoezi, maji safi, na mahali safi pa kuishi vyaweza kufikiwa na watu wote kwa gharama ndogo, lakini dawa za hospitali ulimwenguni ni ghali, gharama yake ni kubwa madukani na kwa athari inayozalishwa kwenye mifumo yetu ni kubwa pia -Shuhuda kwa Kanisa 5: 443.

"Watu wetu wanapaswa kuwa na akili mahiri katika tiba ya magonjwa bila msaada wa dawa za sumu. Wengi wanapaswa kutafuta kupata elimu ambayo itawawezesha kukabiliana na magonjwa kwa njia mbalimbali kwa njia rahisi zaidi. Maelfu wameshuka hadi kaburini kwa sababu ya matumizi ya dawa zenye sumu, ambao wangeweza kurejeshwa kwa afya kwa njia rahisi za tiba. Matibabu ya maji, yaliyotolewa kwa hekima na ustadi, yanaweza kuwa njia ya kuokoa maisha ya watu wengi."—Medical Ministry, 227.

"Ninapokiuka sheria ambazo Mungu ameweka katika nafsi yangu, nitatubu na kujirekebisha, na kujiweka katika hali nzuri zaidi chini ya madaktari ambao Mungu ametoa—hewa safi, maji safi, na uponyaji, mwanga wa jua wenye thamani (Matabibu nane)."—Medical Ministry, 230.

"Dawa za famasia, kama inavyotumika kwa ujumla, ni laana. Jielimishe kukaa mbali na madawa ya kulevya. Uzitumie kidogo na kidogo zaidi, na utegemee zaidi mawakala wa afya na usafi; Ndipo mwili utaitikia madaktari wa Mungu— hewa safi, maji safi, mazoezi yanayofaa, dhamiri safi."—2 Selected Messages, 281.

"Mwili/asili utataka kupatiwa msaada wa aina fulani ili kuleta mwili katika hali yake ifaayo, ambayo inaweza kupatikana katika tiba rahisi zaidi, haswa katika utumiaji wa dawa za asili -hewa safi, na ujuzi wa thamani wa jinsi ya kupumua; maji safi, na ujuzi wa jinsi ya kuyatumia; Mwangaza wa jua mwingi katika kila chumba ndani ya nyumba ikiwa inawezekana, na kwa ujuzi wa akili mahiri, wa faida gani zinazopatikana kwa matumizi yake. Yote haya yana nguvu katika ufanisi wao, na mgonjwa ambaye amepata ujuzi wa jinsi ya kula na kuvaa kwa afya, anaweza kuishi kwa faraja, kwa amani, kwa afya; na hataweza kuweka midomoni mwake dawa zenye sumu, ambazo badala ya kusaidia mwili, hupooza nguvu zake tu."—2 Selected Messages, 287-288.

"Bwana ametufundisha kwamba ufanisi mkubwa wa uponyaji upo katika matumizi sahihi ya maji. Tiba hizi zinapaswa kutolewa kwa ustadi. Tumeagizwa katika kutibu wagonjwa, tutupilie mbali matumizi ya dawa za famasia. Kuna mitishamba rahisi ambayo inaweza kutumika kwa ajili ya kuponya wagonjwa, ambayo athari yake juu ya mfumo ni tofauti sana na ile ya dawa hizo zinazotia sumu kwenye damu na kuhatarisha maisha."—2 Selected Messages, 288.

"Bwana ametoa dawa za magonjwa katika mitishamba sahili (herbs), na hizi zinaweza kutumiwa kwa imani, bila kukana imani; Kwani kwa kutumia baraka zinazotolewa na Mungu kwa manufaa yetu tunashirikiana Naye. Tunaweza kutumia maji na jua na mimea ambayo Bwana ameruhusu ikue, katika uponyaji wa magonjwa yanayoletwa na uzembe au ajali. Hatuonyeshi ukosefu wa imani tunapomwomba Mungu abariki tiba Zake. Imani ya kweli itamshukuru Mungu kwa ujuzi wa jinsi ya kutumia baraka hizi za thamani kwa njia ambayo itarejesha nguvu za kiakili na kimwili."—2 Selected Messages, 289.

"Ingekuwa bora kama, tangu mwanzo, dawa zote zingewekwa nje ya vituo vyetu vya sanitarium, na kisha tutumie tiba rahisi kama zinavyopatikana katika maji safi, hewa safi, mwanga wa jua, na baadhi ya mitishamba inayokua shambani. Hizi zingekuwa na ufanisi zaidi ya dawa zinazotumiwa chini ya majina ya ajabu, na kutengenezwa na sayansi ya binadamu. na zisingeacha madhara yoyote katika mfumo."— 2 Selected Messages, 291.

"Daktari anaitwa, naye anaagiza dawa fulani ambayo inasaidia kwa sasa, lakini ambayo haiponyi ugonjwa huo. Inaweza kubadilisha aina ya ugonjwa huo, lakini athari yenye uovu halisi huongezeka mara kumi. Asili ilikuwa ikifanya kila iwezavyo ili kuondoa mlundikano wa uchafu, na kama ingeweza kuachwa peke yake, ikisaidiwa na baraka za kawaida za mbinguni, kama vile hewa safi na maji safi, tiba ya haraka na salama ingeweza kufanywa."—2 Selected Messages, 450.

"Wagonjwa wanaoteseka katika hali nyingi wanaweza kujifanyia wenyewe yale ambayo wengine hawawezi kuwafanyia vile vile. Wanapaswa kuanza kupunguza asili ya mzigo ambao wameiweka juu yake. Wanapaswa kuondoa kisababisho. Wafunge saumu kwa muda mfupi, na kuacha nafasi ya kupumzisha tumbo. Kupunguza hali ya homa ya mfumo kwa matumizi yenye uangalifu na uelewa ya maji. Juhudi hizi zitasaidia asili katika mapambano yake ya kuusaidia mfumo dhidi ya uchafu. Lakini kwa ujumla watu wanaougua maumivu huwa hawana subira. Hawako tayari kujinyima au kujikana nafsi, na kuteseka kidogo kutokana na njaa. Wala hawako tayari kungoja mchakato wa polepole wa asili ili kujenga nguvu zilizozidishwa za mfumo. Lakini wameazimia kupata nafuu mara moja, na kuchukua dawa za sumu zenye nguvu, zilizoagizwa na madaktari. Asili ilikuwa ikifanya kazi yake vizuri, na ingeshinda, lakini wakati ikikamilisha kazi yake, chembe ya kigeni ya asili ya sumu iliingizwa ndani. Ni kosa lililoje! Asili iliyodhulumiwa sasa ina maovu mawili ya kupigana nayo badala ya moja. Asili inaacha kazi ambayo ilikuwa ikijishughulisha nayo, na kwa uthabiti inashikilia kazi ya kumfukuza mvamizi aliyeletwa hivi karibuni kwenye mfumo. Asili inahisi rasimu hii maradufu juu ya rasilimali zake, na inadhoofika." —2 Selected Messages, 450- 451.

Ikiwa mgonjwa angechukua njia ya kupunguza hali ya kulemewa kwa msimu, na kutumia maji safi laini kwa ufahamu, mpango huu wa vifo wa dawa zenye sumu ungeweza kuepukwa kabisa. Utumiaji wa maji unaweza kutimiza kidogo tu, ikiwa mgonjwa haoni ulazima wa kuzingatia mlo wake kwa ukali/umakini sana.

Wengi wanaishi kwa kukiuka sheria za afya, na hawajui kwamba uhusiano wa tabia zao za kula, kunywa, na kufanya kazi, hudumisha afya zao. Hawatazinduka kuhusiana na hali yao ya kweli, hadi asili ipingane dhidi ya unyanyasaji unaoitesa, kwa kukosa faraja na maumivu katika mfumo. Ikiwa, hata hivyo, ale wanaougua wangeanza tu kazi ipasavyo, na wangetumia njia rahisi ambazo wamepuuza—-Matumizi ya maji na lishe sahihi, mwili ungekuwa na msaada inaouhitaji, na ambao ulipaswa kuwa nao muda mrefu kabla. Ikiwa kanuni hii itafuatwa, mgonjwa kwa ujumla atapona bila kudhoofika au kulemaa."— 2 Selected Messages, 451.

2- BAADHI YA MATUMIZI YA MAJI KATIKA KUTIBU WAGONJWA

"Huenda watu hawa wangeishi. Mbingu hazikutaka kifo chao. Walikufa wakiwa wagonjwa kwa ujinga wao wenyewe, na ule wa marafiki zao wa kweli, na ujinga na udanganyifu wa waganga; ambao waliwapa sumu zilizokuwa katika fasheni/mtindo, na hawakuwaruhusu kunywa maji safi , na kuvuta hewa safi,

kuimarisha viungo muhimu, kusafisha damu, na kusaidia mwili katika kazi yake katika kushinda hali mbaya ya mfumo. Dawa hizi za thamani ambazo Mbingu amezitoa, bila pesa na bila gharama, zilitupiliwa mbali, na kuchukuliwa sio tu kuwa hazina thamani, lakini kama maadui wa hatari, wakati sumu, iliyowekwa na waganga, ilichukuliwa kwa ujasiri na upofu.

"Maelfu wamekufa kwa kukosa maji safi na hewa safi, ambao wangeweza kuishi. Na maelfu ya walemavu, ambao ni mzigo kwao wenyewe na kwa wengine, wanafikiri kwamba maisha yao yanategemea kuchukua dawa, kutoka kwa madaktari. Wanaendelea kujiongoza wenyewe kuwa mbali na hewa, na kujiepusha na matumizi ya maji. Baraka hizi wanazihitaji ili wapate kuwa wazima-hali nzuri kiafya. Ikiwa wangepata nuru, na kuziacha dawa, na kujizoeza kufanya mazoezi ya nje ya nyumba, na kuruhusu hewa ndani ya nyumba zao, kipindi cha joto na baridi, na kutumia maji safi kwa madhumuni ya kunywa na kuoga, wangekuwa wazima wa afya na wenye furaha, badala ya kupitia uzoefu wa maisha duni. —Counsels on Health, 55-56

Pumziko, uhuru kutoka kwenye masumbufu, utulivu, mwanga, hewa safi, maji safi, na chakula bora, ndivyo wanavyohitaji ili kuwaponya."—2 Selected Messages, 458.

"Uchafu wa mwili, ikiwa hautatolewa kwenye mwili na kuondoka, hurudishwa ndani ya damu, na kulazimishwa kuingia kwenye viungo vya ndani. Mwili/asili, ili utoe uchafu wa hiyo sumu, hufanya jitihada za kuukomboa mfumo. Jitihada hii hupelekea kuwepo kwa homa, ndiyo kile kinachoitwa ugonjwa. Lakini hata hivyo, ikiwa wale wanaoteseka wangeusaidia mwili/asili katika jitihada zake, kwa kutumia maji safi, laini, mateso mengi yangezuiwa. Lakini wengi, badala ya kufanya hivyo, na kutafuta kuondoa sumu kutoka kwenye mfumo, huchukua sumu hatari zaidi kwenye mfumo, ili kuondoa sumu ambayo tayari iko."—Counsels on Health, 61-62.

"Maji ni kioevu/kimiminika bora zaidi kinachowezekana kusafisha tishu."—Healthful Living, 90.

Katika afya njema na katika kuugua, maji safi ni mojawapo ya baraka bora na za pekee kabisa za mbingu. Matumizi yake sahihi huimarisha afya. Ni kinywaji ambacho Mungu alitupatia ili kutuliza kiu kwa wanyama na mwanadamu. Yakinywewa kwa uhuru kwa jinsi ipasavyo, husaidia kusafirisha mahitaji ya mfumo wa mwili, na kusaidia mwili kukabiliana na magonjwa (Msisitizo: lita mbili mpaka tatu kwa siku kama huna magonjwa yanayotunza maji mwilini). Matumizi ya maji kwa nje ya mwili ni mojawapo ya njia rahisi na toshelevu

katika kurekebisha mzunguko wa damu (haidrotherapia; maji huosha mwili ndani na nje). Kuoga na maji baridi yaliyotulia kunasaidia mwili uwe mchangamfu. Kuogea maji ya moto husaidia kufungua matundu ya vinyweleo vya ngozi na hivyo husaidia uondoaji wa uchafu mwilini (takamwili). Kuogea maji ya moto, na maji vuguvugu huzipoza neva na husawazisha mzunguko wa damu. [MH 237.1]

Lakini wengi hawajawahi kujifunza kupitia uzoefu binafsi kuhusu matokeo yenye manufaa ya matumizi sahihi ya maji, na huogopa jambo hili. Tiba ya maji haithaminiwi jinsi inavyopaswa, na ili kuyatumia maji kwa ustadi kuna hitaji la kufanya kazi yenye juhudi, ambayo wengi hawataki kuifanya (Msisitizo: wengi husema tiba rahisi zina mlolomgo mrefu kuziandaa). Lakini hakuna anayepaswa kuhisi kuwa na kisingizio kwa sababu tu ya ujinga wake au uzembe kuhusiana na jambo hili. Zipo njia nyingi ambazo maji yaweza kutumika kutuliza maumivu na kuzuia ugonjwa. Watu wote wapaswa kuwa na utambuzi katika maarifa ya matumizi ya tiba rahisi majumbani mwao. Hasa akina mama, wanapaswa kujua jinsi ya kutunza familia zao katika suala la afya na maradhi. [MH 237.2]

“Hakikisha watoto wanaoga kila siku, na mwili unasuguliwa hadi miili yao ing’ae (aina ya massage ya kujifunza, wengine wana brashi maalumu ya kufanya hili).”— Counsels on Health, 103.

“Watu wenye afya njema hawapaswi kabisa kupuuza kuoga. Wanapaswa kwa vyovyote kuoga mara nyingi zaidi ya mara mbili kwa wiki. Wale ambao hawana afya wana mchafuko damu, na ngozi zao hazina afya njema. Wingi wa vinyweleo, au matundu madogo, ambayo huuwezesha mwili kupumua huziba na kujaa uchafu. Ngozi inahitaji kusafishwa kwa uangalifu na kwa kina, ili vinyweleo vifanye kazi yake ya kutoa taka mwili; kwa hiyo watu dhaifu ambao ni wagonjwa kwa hakika wanahitaji faida na baraka za kuoga mara nyingi zaidi ya mara mbili kwa wiki, na ni muhimu kuoga hata mara nyingi zaidi. Ikiwa mtu ni mgonjwa au mzima, kupumua kwa urahisi zaidi ikiwa ataoga. Kwa kufanya hivyo misuli huwa huru zaidi kunyumbulika, akili na mwili hutiwa nguvu, kisha akili inafanywa kuwa angavu, na kila kiungo kinakuwa hai. Kuoga hupoozesha/hutuliza mishipa ya fahamu. Husaidia kutoa jasho mwilini, huharakisha mzunguko wa damu, huzuia kuziba katika mfumo, na husaidia figo pamoja na mfumo wa mkojo. Kuoga husaidia tumbo, na ini, kwa kuvipatia nguvu na maisha mapya. Pia husaidia mmeng’enyo wa chakula, na badala ya mfumo kuwa dhaifu huimarishwa. Badala ya kuongeza uwezekano wa kuhisi baridi, uogaji mzuri, hukinzana na baridi kwa sababu mzunguko wa damu na viungo vya mfumo wa mfuko wa uzazi hurahisishwa; kwa kuwa damu husambaa kuelekea juu ya ngozi, mtiririko rahisi

zaidi na wa kawaida wa damu kupitia mishipa yote ya damu hupatikana.” - Shuhuda kwa Kanisa, 3:70-71.

"Kesi za homa zitapotea, ikiwa madaktari wangeacha kabisa matibabu yao ya dawa, kama wangeweka akili zao kufanya kazi, na kwa busara na kwa kuendelea kutumia tiba za Bwana Mwenyewe - hewa na maji mengi - wagonjwa wangepona. "Kutumia dawa zenye sumu ni shughuli ya gharama na uzembe mkubwa sana, na inapaswa kutupiliwa mbali kwa kuazimia.

Kufanyia majaribio dawa za famasia, ni jambo la gharama sana. Kupooza kwa ubongo na ulimi mara nyingi ni matokeo, na wahasiriwa ambao hufa kifo kisicho cha kawaida, wakati, kama wangetendewa kwa uvumilivu, kwa bidii isiyochoka, isiyo na ulegevu na maji ya moto na baridi, vitambaa vya moto vya kukandia, mito midogo ya joto na baridi (packs), na shuka au blanket la kujifukiza kwa usalama, wangekuwa hai leo.”— Medical Ministry, 228.

“Nenda pamoja nami kwenye chumba cha wagonjwa. Pale amelala mume na baba, mtu ambaye ni baraka kwa jamii na kwa kazi ya Mungu. Amepigwa ghafla na ugonjwa. Moto wa homa unaonekana kumteketeza. Anatamani maji safi kulainisha midomo iliyokauka, kumaliza kiu kali, na kupoza paji la uso. Lakini, hapana; daktari amekataza maji yasinywewe. Kichocheo cha kinywaji kikali yaani kileo hutolewa na huongeza mafuta kwenye moto (joto lipande zaidi). Maji yaliyobarikiwa, yaliyotumwa toka mbinguni, yaliyotumiwa kwa ustadi, yangeweza kuzima mwali uteketezao lakini yamewekwa pembeni kwa sababu ya dawa zenye sumu." — Shuhuda kwa Kanisa 5: 195.

“Kama waganga wana shughuli nyingi kiasi kwamba hawawezi kuwatibu wagonjwa nje ya taasisi, Je, haitakuwa busara kwa wote kujielimisha katika matumizi ya dawa za asili (rahisi), kuliko kujitosa kutumia dawa zenye sumu, ambazo hupewa jina refu ili kuficha sifa zao halisi. Kwa nini mtu yeyote asiwe na ufahamu wa tiba za Mungu,—maji ya moto, vichocheo (fomentations), na vibano/kitambaa cha baridi na moto. Ni muhimu kufahamu faida ya lishe kwa kufunga ikiwa ni ugonjwa. Wote wanapaswa kuelewa jambo la kufanya kwa ajili yao wenyewe.”— 2 Selected Messages, 290.

Maji safi, ya moto ambayo mtu anakunywa kabla ya kula (nusu lita, zaidi au chini), kamwe hayataleta madhara yoyote, lakini badala yake yatakuwa ni msaada mzuri.

"Kikombe cha chai kilichotengenezwa kutoka kwa mimea ya Catnip kitatuliza mishipa ya fahamu. "Chai ya mti wa Humulus lupulus, italeta usingizi. Majimaji

au unga wa mti wa Hop huondoa maumivu kwenye tumbo. "Ikiwa macho ni dhaifu, ikiwa kuna maumivu machoni, au kuvimba, vitambaa laini vya sufu vilivyolowekwa kwenye maji ya moto na chumvi, vitaleta ahueni haraka. "Kichwa kikiwa na msongamano, ikiwa miguu na viungo vitawekwa kwenye maji yaliyo na haradali kidogo, nafuu itapatikana. "Kuna tiba nyingi rahisi zaidi ambazo zitafanya mengi kurejesha hatua za kiafya kwa mwili. Maandalizi haya yote rahisi ambayo Bwana anatarajia tutumie sisi wenyewe, lakini mwisho wa mwanadamu kupata ufumbuzi ndiyo fursa za Mungu. Ikiwa tunapuuza kufanya yale ambayo yanaweza kufikiwa na karibu kila familia, na kumwomba Bwana aondoe maumivu wakati sisi ni wavivu sana kutumia dawa hizi ndani ya uwezo wetu, hii itakuwa ni ujuvi tu."—2 Selected Messages, 297.

"Siku iliyofuata Willie alikuwa mgonjwa sana. Alikuwa akitangatanga. Hakuonekana kuniona wala kunisikia nilipozungumza naye. Moyo wake haukuwa na mapigo ya kawaida, lakini ulikuwa katika hali ya kupepesuka mara kwa mara. Tuliendelea kumtegemea Mungu juu yake, na kutumia maji juu ya kichwa chake, na kumkanda mara kwa mara kwenye mapafu yake, na mara alionekana kurejea hali yake kama zamani. Alipata maumivu makali katika upande wake wa kulia, na hakuweza kulala juu yake kwa muda. Maumivu haya tulipunguza kwa vitambaa vya za maji baridi, tofauti na joto la maji, ilikuwa kulingana na kiwango cha homa. Tulikuwa waangalifu sana kuweka mikono na miguu yake iwe na joto."—2 Selected Messages, 304.

"Mweke mgonjwa mbali na msisimko, na kila ushawishi unaohesabiwa kukandamiza au kuleta huzuni. Wauguzi wake wanapaswa kuwa wachangamfu na wenye matumaini. Anapaswa kuwa na lishe rahisi, na apewe maji mengi safi ya kunywa. Anapaswa kuwa na lishe rahisi, na aruhusiwe maji mengi safi ya kunywa. Oga mara kwa mara katika maji safi laini ikifuatiwa na kusugua kwa upole mwili (na brashi au mkono tu au mafuta kama masaji). Acha mwanga, na hewa, viingizwe kwa uhuru ndani ya chumba chake. Lazima awe na utulivu, na kupumzika bila usumbufu. (maagizo yaliyotolewa katika maono).'"— 2 Selected Messages, 446.

"Lakini wengi hawajawahi kupata matokeo ya manufaa ya maji, na wanaogopa kutumia mojawapo ya baraka kuu za mbinguni. Maji yamekataliwa watu wanaougua homa kali, kwa hofu kwamba ingewaumiza. Ikiwa, katika hali yao ya joto, wangepewa maji ili kunywa kwa uhuru, na maombi pia yangefanywa nje, mchana mrefu na usiku wa mateso vingeokolewa, na maisha mengi ya thamani yangeokolewa. Lakini maelfu wamekufa kwa homa kali iliyowateketeza, hadi

mafuta yaliyolisha homa yaliteketezwa, viungo muhimu vinaungua, na kufa katika uchungu mkubwa, bila kuruhusiwa kuwa na maji ya kutuliza kiu yao inayowaka. Maji, ambayo yanatumiwa kwenye jengo lisilo na maana kuzima vipengele vinavyowaka, hayatumiwi kwa wanadamu kuzima moto unaoteketeza viungo muhimu."—2 Selected Messages, 453.

SURA YA 18

JINSI MITISHAMBA INAVYOWEZA KUSAIDIA KATIKA KUPONYA WAGONJWA

"Kuhusiana na suala la kuwaombea wagonjwa, mawazo mengi yenye kutatanisha yameendelezwa. Mmoja anasema, Yule ambaye ameombewa lazima atoke kwa imani, akimpa Mungu utukufu, na kutotumia tiba. Ikiwa yuko katika taasisi ya afya, anapaswa kuiacha mara moja. Ninajua kwamba mawazo haya si sahihi, na kwamba yakikubaliwa, yangesababisha maovu mengi. Kwa upande mwingine, sitaki kusema chochote ambacho kinaweza kufasiriwa kumaanisha ukosefu wa imani katika ufanisi wa maombi. Njia ya imani iko karibu na njia ya dhana/ujuvi……. Haimaanishi kuikana imani tunapotumia tiba sahihi kwa busara. Maji, hewa, na jua—hawa ni mawakala wa uponyaji ya Mungu…….Matumizi ya mitishamba fulani ambayo Bwana ameifanya kukua kwa manufaa ya mwanadamu, yanapatana na matumizi ya imani."—Manuscript 31, 1911 (written June 3, 1888).

"Sasa kuhusu yale ambayo tunaweza kujifanyia wenyewe: kuna jambo ambalo linahitaji kuzingatiwa kwa uangalifu na kwa uangalifu. Lazima nijifahamu mwenyewe. Ni lazima niwe mwanafunzi siku zote jinsi ya kutunza jengo hili, mwili ambao Mungu amenipa, ili nipate kuuhifadhi katika hali bora kabisa ya afya.

Lazima nile vitu hivyo ambavyo vitanifaa sana kimwili na lazima nichukue tahadhari maalum ili kuwa na mavazi yangu ambayo yataruhusu mzunguko mzuri wa damu. Sipaswi kujinyima mazoezi na hewa. Lazima nipate mwanga wote wa jua ambao inawezekana kwangu kuupata…….. Lazima niwe na hekima ili kuwa mlinzi mwaminifu wa mwili wangu. Nitakuwa nimefanya jambo lisilo la busara sana kuingia kwenye chumba cha baridi wakati wa jasho; Nitakuwa nimejionyesha kuwa msimamizi asiye na hekima ili kujiruhusu kuketi kwenye unyevunyevu, na hivyo kujiweka wazi ili nipate baridi. Ninapaswa kuwa na busara kuketi na miguu baridi na viungo na hivyo kurudisha damu kutoka mwisho hadi kwa ubongo au viungo vya ndani. Ninapaswa kulinda miguu yangu kila wakati katika hali ya hewa yenye unyevunyevu. Ninapaswa kula mara kwa mara chakula chenye afya zaidi ambacho kitafanya ubora wa damu, na sipaswi kufanya kazi bila kiasi ikiwa ni katika uwezo wangu kuepuka kufanya hivyo. Na ninapokiuka sheria ambazo Mungu ameweka katika mwili wangu, nitatubu na kujirekebisha, na kujiweka katika hali nzuri zaidi chini ya madaktari ambao Mungu ametoa—hewa safi, maji safi, na mwanga wa jua mzuri unaoponya. Maji safi, ya moto ambayo mtu anakunywa kabla ya kula (nusu lita, zaidi au chini), kamwe hayataleta madhara yoyote, lakini badala yake yatakuwa ni msaada mzuri.

"Kikombe cha chai kilichotengenezwa kutoka kwa mimea ya Catpin kitatuliza mishipa ya neva. "Chai ya mti wa Humulus lupulus, italeta usingizi. Majimaji au unga wa mti wa Hop huondoa maumivu kwenye tumbo. "Ikiwa macho ni dhaifu, ikiwa kuna maumivu machoni, au kuvimba, vitambaa laini vya sufu vilivyolowekwa kwenye maji ya moto na chumvi, vitaleta ahueni haraka. "Kichwa kikiwa na msongamano, ikiwa miguu na viungo vitawekwa kwenye maji yaliyo na haradali kidogo, nafuu itapatikana. "Kuna tiba nyingi rahisi zaidi ambazo zitafanya mengi kurejesha hatua za kiafya kwa mwili. Maandalizi haya yote rahisi ambayo Bwana anatarajia tutumie sisi wenyewe, lakini mwisho wa mwanadamu ni fursa za Mungu. Bwana anatutarajia tufanye kazi ili tupate chakula. Hapendekezi kwamba tutakusanya mavuno bila kuuchimba udongo, kuilima ardhi, na kupanda mazao. Kisha Mungu hutuma mvua na jua na mawingu ili kuifanya mimea istawi. Mungu hufanya kazi, na mwanadamu hushirikiana na Mungu. Kisha kuna wakati wa kupanda na wakati wa mavuno……..Mungu amewezesha ukuaji wa mimea ya ardhi, kwa matumizi ya mwanadamu, na ikiwa tunaelewa asili ya mizizi na mimea hii - na kuitumia ipasavyo - hakutakuwa na ulazima wa kukimbilia kwa daktari mara kwa mara, na watu wangekuwa na afya bora zaidi kuliko ilivyo leo.

“Ninaamini katika kumwita daktari Mkuu pale tutakapokuwa tumekwishatumia dawa nilizotaja. Kuhusiana na namna ya kazi, kwa hakika tunahitaji kuwa na hekima kama nyoka na wasio na madhara kama njiwa. Tunaweza kuwa na bidii sana, lakini inaweza kuwa bidii isiyo ya busara, na itakayotumika kuzuia njia yetu. Kisha kuna hatari ya kung'ang'ania sana katika kazi yetu kiasi cha kufanya mema machache sana.”— Letter 35, Februari 6, 1890.

"Tiba rahisi huwa hazina madhara sawa na yale ya dawa za sumu za famasia (kuliko sumu ya dawa) kulingana na urahisi wake, lakini katika hali nyingi sana hutumiwa wakati ambao sio lazima kabisa. . Hizi ni mimea na mizizi rahisi ambayo kila familia inaweza kutumia yenyewe, na haifai kumwita daktari mapema zaidi kuliko vile wangemwita wakili.

"Sidhani kama ninaweza kukupa safu yoyote ya dawa zilizokusanywa na kutengenezwa na madaktari ambazo hazina madhara kabisa. Na bado isingekuwa busara kushiriki katika mabishano juu ya somo hili.

Wataalamu wana bidii sana katika kutumia michanganyiko yao hatarishi; Na ninapinga kabisa kugeukia mambo kama haya. Hawaponyi kamwe; Wanaweza kubadilisha kilicho kigumu na kutengeneza kilicho kibaya zaidi. Wengi wa wale wanaotumia maagizo ya dawa zenye sumu, wasingetakiwa kutumia, au kuwapa watoto wao. Ikiwa wana ujuzi wa akili wa mwili wa mwanadamu. Ni lazima wajue kwamba tumeumbwa kwa njia ya kutisha na ya ajabu, na kwamba hakuna hata chembe ya dawa hizi kali zinazopaswa kuletwa ndani ya kiumbe hiki hai cha binadamu. Jambo hilo lilipowekwa wazi mbele yangu, na mzigo wa kusikitisha wa matokeo ya dawa zenye sumu, nuru niliyopewa kwamba Waadventista Wasabato wanapaswa kuanzisha taasisi za afya, wakitupilia mbali uvumbuzi huu wote unaoharibu afya, na madaktari wanapaswa kuwatibu wagonjwa kwa kanuni za usafi.”—Letter 17a, October. 2, 1893.

“Majina tata yaliyoandikwa kwenye dawa hizo hutumika kuficha jambo hilo, ili asiwepo atakayejua alishaolewa atumie kama tiba isipokuwa hadi atafute kamusi ili kujua maana ya majina hayo. Bwana ametoa baadhi ya mimea rahisi ya shamba ambayo wakati fulani ni ya manufaa; Na ikiwa kila familia ingeelimishwa jinsi ya kutumia mimea hii kwa ajili ya ugonjwa, mateso mengi yanaweza kuzuiwa, na hakuna daktari anayehitaji kuitwa. Mimea hii ya kizamani, rahisi, ingetumiwa kwa akili ingeweza kuponya wagonjwa wengi, ambao wamekufa kwa kutumia dawa zenye sumu.”—Letter 82, Feb 10, 1897.

"Kama ningekuwa mgonjwa, ningejiondoa mara moja kwa wakili na daktari kwa ujumla. Nisingegusa dawa zao zisizo na uhakika wa kutibu, ambazo wanazipa

majina ya Kilatini. Nimeazimia (nimekusudia) kujua, kwa Kiingereza kilichonyooka, jina la kila kitu ninachoingiza katika mwili/mfumo wangu."—Manuscript 86, 1897.

"Dawa zenye sumu zinapaswa kutupwa. Juu ya hatua hii dhamiri ya daktari lazima iwekwe nyororo, na kweli, na safi. Mwelekeo wa kutumia dawa zenye sumu, ambazo zinaua ikiwa hazitatibu, unahitaji kulindwa dhidi yake. Mambo yamewekwa wazi mbele yangu kuhusiana na matumizi ya dawa zenye sumu. Wengi wametibiwa na dawa zenye sumu na matokeo yake ni kifo. Madaktari wetu, kwa kutumia dawa zenye sumu, wamepoteza maisha ya wengi ambao hawakuhitaji kufa ikiwa wangeacha dawa zao nje ya chumba cha wagonjwa. Kesi za homa zingepotea, wakati, kama madaktari wangeacha matibabu yao ya dawa, kama wangeweka akili zao kufanya kazi, na kwa busara na kwa kuendelea kutumia tiba za Bwana mwenyewe - hewa na maji mengi - wagonjwa wangepona. Utumiaji mbaya wa vitu hivi ambavyo ulipaswa kutupiliwa mbali imesababisha hali ya ugonjwa."—Medical Ministry, 227-228

"Kujaribu dawa zenye sumu ni shughuli ya gharama kubwa sana. Kupooza kwa ubongo na ulimi mara nyingi ni matokeo, na wahasiriwa hufa kifo kisicho cha kawaida, wakati, kama wangetendewa kwa uvumilivu, kwa bidii isiyochoka, isiyo na ulegevu na maji ya moto na baridi, vitambaa vya moto, pakiti, na karatasi ya kudondosha, wangekuwa hai leo."—Medical Ministry, 228.

"Hakupaswi kuwekwa kitu chochote kwenye mfumo ambacho kitaacha madhara mabaya. Na kwa kutekeleza mwanga juu ya somo hili, kufanya mazoezi ya usafi, ndiyo sababu ambayo nimepewa ya kuanzisha vituo vya afya katika maeneo mbalimbali. Nimeumia wakati wanafunzi wengi [wetu] wamehimizwa kwenda ambapo wangepata elimu ya matumizi ya dawa zenye sumu. Nuru niliyoipata juu ya suala la dawa zenye sumu ni tofauti kabisa na matumizi yao katika shule hizi au kwenye vituo vya afya. Ni lazima tuwe na nuru juu ya masomo haya. .Watu wengi wanaoteseka wasio wa imani yetu watakuja katika taasisi zetu kupata matibabu. Wale ambao afya yao imeharibiwa na suala la dhambi, na ambao wametibiwa na madaktari mpaka dawa walizoelekezwa zisiwe na matokeo, watakuja; Na watafaidika. Bwana atabariki taasisi zinazofanywa kwa mujibu wa mipango Yake. . Ataingia kwenye vyumba vya wagonjwa. Atawapa wauguzi hekima."—Medical Ministry, 228-229.

"Majina tata yanayoandikwa kwenye dawa hutumiwa ili kuficha jambo hilo, ili mtu yeyote asijue ni dawa gani hadi (isipokuwa) atafute msaada wa kamusi ili kujua maana ya majina hayo..

“Kuhusu dawa zinazotumika katika taasisi zetu, ni kinyume na nuru ambayo Bwana amependezwa kuitoa. Shughuli ya madawa ya kulevya imefanya madhara zaidi kwa ulimwengu wetu na kuua zaidi kuliko kusaidia au kuponya. Nuru niliyopewa kwanza kwa nini taasisi [zetu za afya] zinapaswa kuanzishwa, yaani, vituo vyetu vya afya vilipaswa kurekebisha mazoea ya matibabu ya madaktari.”—Medical Ministry, 27.

"Hii ndiyo njia ya Mungu: mimea ambayo hukua kwa manufaa ya mwanadamu, na kwa uchache wa miti midogo midogo ambayo imehifadhiwa kwa gharama ili kutumika kwa maradhi ya ghafla, imetumika mara kumi, ndiyo, mara mia moja bora zaidi, kuliko dawa zote zilizofichwa chini ya majina ya ajabu ili kutumiwa na mgonjwa.”—Letter 59, 1895.

Ni udanganyifu na mchezo wa kuigiza, na Bwana amenifunulia kwamba jambo hili haliwezi kutunza afya, bali linaleta mwilini vitu ambavyo havipaswi kuwapo kamwe, kwa kuwa vitasababisha madhara katika mwili wa mwanadamu.” — Letter 59, August 29, 1898.

"Sayansi ya dawa imeinuliwa, lakini ikiwa kila chupa inayotoka kwa kila taasisi kama hiyo ingeondolewa, kungekuwa na walemavu wachache ulimwenguni leo. Dawa zenye sumu/sumu hazipaswi kamwe kuletwa katika taasisi zetu. Hakukuwa na haja ya kuwa hivyo, na kwa sababu hii hii Bwana angetaka tuanzishe taasisi ambapo anaweza kuingia na ambapo neema na uwezo Wake vinaweza kufunuliwa. ‘Mimi ndiye ufufuo na uzima,’ asema . .“Njia ya kweli ya kuponya wagonjwa ni kuwaambia kuhusu mimea inayokua kwa manufaa ya mwanadamu……. Elimu ya kweli itatuongoza kuwafundisha wagonjwa ambao hawahitaji kumwita daktari zaidi ya vile wangemwita wakili. Wao wenyewe wanaweza kuitumia mimea hiyo rahisi ikibidi.”—Manuscript 105, 1898.

Kuelimisha familia ya kibinadamu kwamba daktari peke yake anajua magonjwa yote ya watoto wachanga na watu wa kila rika ni fundisho ya uwongo, na kadiri tunavyosimama juu ya kanuni za matengenezo ya afya, ndivyo baraka kubwa zaidi itawajia wale ambao watafanya kazi ya kweli ya tiba. Kuna kazi ya kufanywa katika kutibu wagonjwa kwa maji na kuwafundisha kutumia vyema mwanga wa jua na mazoezi ya viungo. Hivyo kwa lugha rahisi, tunaweza kuwafundisha watu jinsi ya kutunza afya, jinsi ya kuepuka magonjwa. Hii ndiyo kazi ambayo vituo vyetu vya afya vinaitwa kufanya. Hii ni sayansi ya kweli.”—Manuscript 105, August 26, 1898.

"Je, madaktari waendelea kutumia dawa, ambayo huacha madhara mabaya katika mfumo, kwa kuharibu uhai ambao Kristo alikuja kuurejesha? "Tiba za

Kristo husafisha mfumo. Lakini Shetani amemjaribu mwanadamu kuingiza katika mfumo tiba inayodhoofisha utendaji wa mfumo wa kibinadamu, kuziba na kuharibu mipango safi na mizuri ya Mungu. Dawa zinazotolewa kwa wagonjwa hazileti uzima, lakini zinaharibu. Dawa zenye sumu haziponyi. Badala yake, huleta katika mfumo mbegu ambazo huzaa mavuno machungu sana."—2 Selected Messages, 289.

Mwokozi wetu Ndiye mrejeshaji wa sura ya maadili ya Mungu ndani ya mwanadamu. Ametoa katika ulimwengu wa asili dawa za magonjwa ya mwanadamu, ili wafuasi Wake wapate uzima, naam uzima tele. Kwa ajili ya usalama tunaweza kuachana na dawa ambazo mwanadamu alizitumia hapo awali. Bwana ametoa dawa za magonjwa katika mimea rahisi, na hizi zinaweza kutumiwa kwa imani, bila kukana imani; Kwani kwa kutumia baraka zinazotolewa na Mungu kwa manufaa yetu tunashirikiana naye. Tunaweza kutumia maji na mwanga wa jua na mimea ambayo ameiotesha ili kuleta uponyaji kwa magonjwa yanayosababishwa na uzembe au ajali."—Manuscript 65, Aprili 25, 1899.

"'Ingekuwa bora kama, tangu mwanzo, dawa zote za famasia zingewekwa nje ya vituo vyetu vya afya, na badala yake tiba rahisi zitumiwe kadri zinavyopatikana katika maji safi, hewa safi, mwanga wa jua, na baadhi ya mimea rahisi inayokua shambani. Hizi zingekuwa na ufanisi sawa na dawa zinazotumiwa chini ya majina ya ajabu, na kutengenezwa na sayansi ya binadamu. Na zisingeacha madhara yoyote katika mwili."—Manuscript 115, 1903.

"Maelfu ambao wameteseka wanaweza kurejesha afya zao, ikiwa, badala ya kutegemea duka la dawa kwa maisha yao yote, wangetupilia mbali dawa zote, na kuishi kwa usahili, bila kutumia chai, kahawa, pombe, au viungo vivyonakera tumbo na kuliacha likiwa dhaifu na lisiloweza kumeng'enya/kusaga hata kwa urahisi chakula bila kusisimuliwa. Bwana Yuko tayari kuruhusu nuru Yake iangaze katika miale iliyo wazi, kwa wote walio dhaifu na wasiojiweza."—Manuscript 115, September 4, 1902.

"Tumeagizwa kwamba katika matibabu yetu ya wagonjwa tunapaswa kutupilia mbali matumizi ya dawa zenye sumu…….Kuna mitishamba rahisi ambayo inaweza kutumika kwa ajili ya kuponya wagonjwa, ambayo athari yake juu ya mfumo ni tofauti sana na ile ya dawa hizo ambazo hutia sumu kwenye damu na kuhatarisha maisha."—Manuscript 73, 1908.

"Nimeonyeshwa kwamba tunapaswa kuwa na wanawake wengi zaidi wanaoweza kukabiliana na kujihusisha katika tiba na magonjwa ya wanawake, wanawake

wengi zaidi wauguzi ambao watawatibu wagonjwa kwa njia rahisi na bila kutumia dawa zenye sumu……. Kuna miti shamba mingi ambayo, ikiwa wauguzi wetu wangejifunza thamani yake, wangeweza kutumia mahali pa dawa zenye sumu,na kupata matokeo mazuri sana."—Letter 90, 1908.

Yeye ameunda nyenzo ambazo zitarejeshea wagonjwa afya, kupitia mawakala wake wa kufanya kazi. Ikiwa wanadamu wangetumia ipasavyo hekima ambayo Mungu amewapa, ulimwengu huu ungekuwa mahali panapofanana na mbinguni."—Manuscript 63, 1899.

"Tunapaswa kufanya jitihada zilizoamuliwa kutii maagizo ambayo Bwana ametoa kuhusiana na utunzaji wa wagonjwa. Wanapaswa kupewa kila msaada unaowezekana. Mawakala wote wa urejeshaji ambao Bwana ametoa wanapaswa kutumiwa katika kazi yetu ya vituo vya afya."— Manuscript 19, 1911.

"Bwana alipomwambia Hezekia kwamba angeokoa maisha yake kwa muda wa miaka kumi na tano, na kama ishara kwamba angetimiza ahadi yake, alilifanya jua kurudi nyuma madaraja kumi, kwa nini hakuweka nguvu zake za moja kwa moja, za kurejesha juu ya mfalme? Alimwambia atumie vichala vya tini kwenye kidonda chake, na dawa hiyo ya asili, iliyobarikiwa na Mungu, ilimponya. Mungu wa asili huelekeza wakala wa kibinadamu kutumia dawa za asili sasa."—Letter 182

"Maelekezo maalum yanapaswa kutolewa katika jinsi ya kutibu wagonjwa, bila kutumia dawa zenye sumu, kwa kulingana na nuru ambayo Mungu ametoa. Wanafunzi wanapaswa kumaliza shuleni bila ya kuziacha kanuni za matengenezo ya afya."— Letter 90, 1908.

"Wale wanaotamani kuwa wamishenari wanapaswa kusikia maelekezo kutoka kwa madaktari wenye uwezo, ambao watawafundisha jinsi ya kuwahudumia wagonjwa, bila kutumia dawa. Masomo hayo yatakuwa ya thamani ya juu zaidi kwa wale wanaokwenda kufanya kazi katika nchi za kigeni. Na dawa sahili zitakazotumiwa zitaokoa maisha ya watu wengi."— Manuscript 83, 1908.

"Bwana atakuwa msaidizi wa kila tabibu ambaye atafanya kazi pamoja Naye katika jitihada za kurejesha ubinadamu unaoteseka kwenye afya, pasipo kutumia dawa zenye sumu, bali na dawa za asili. Kristo Ndiye tabibu Mkuu, Mponyaji wa ajabu. Yeye huwapa mafanikio wale wanaofanya kazi kwa kushirikiana Naye."— Letter 142, 1902.

Wakati tabibu anatumia dawa za asili kwa ajili ya magonjwa ya kimwili, anapaswa pia kuwaelekeza wagonjwa wake Kwake Yule ambaye anaweza kuondoa maradhi ya roho na mwili. — Ministry of Healing, 111.

Pale mtu anapopatwa na ugonjwa, sababu ya kuja kwa huo ugonjwa inapaswa kutambuliwa-kueleweka. Tabia mbaya yafaa zibadilishwe. Mazoea mabaya yarekebishwe. Kisha asili inapaswa kusaidiwa katika juhudi zake za kuondoa uchafu mwili na kuweka upya hali sahihi katika mfumo. —Ministry of Healing, 127.

Hewa safi, mwanga wa jua, kuwa na kiasi, pumziko, kufanya mazoezi, chakula kinachofaa, matumizi ya maji, kumtumaini Mungu na uweza Wake—hizi ndizo tiba za kweli. —Ministry of Healing, 127.

“Kuna njia nyingi za kufanya uponyaji, lakini ipo njia moja tu ambayo mbingu inaikubali. Dawa zipatikanazo kutoka kwa Mungu ni za asili na ambazo hautatoa ushuru au kudhoofisha mifumo ya mwili kwa sababu ya sifa zake kuu. Hewa safi, maji, usafi, lishe sahihi, maisha safi, usafi na imani thabiti kwa Mungu ni tiba kwa mahitaji mengi ambayo maelfu wanakufa kwa kuzikosa; …… Hewa safi, mazoezi, maji safi, na mahali safi pa kuishi yanaweza kufikiwa na watu wote……Daktari anahitaji zaidi ya hekima na uwezo wa kibinadamu ili aweze kujua jinsi ya kuhudumia magonjwa mengi na yenye kushangaza yahusuyo akili na moyo aliyoitwa kuyashughulikia. Ikiwa hana ufahamu juu ya Neema ya Mungu basi hatoweza kuwasaidia wenye magonjwa, bali atazidisha ugumu wao; lakini ikiwa amemshikilia sana Mungu, ataweza kuwasaidia wanadamu wenye kuteseka na wagonjwa wa akili wenye mawazo yaliyotawanyika.” —Shuhuda kwa Kanisa 5: 443-444.

"Katika majira ya kupukutisha majani cha 1864, Willie wangu alizidiwa ghafla na kwa nguvu na homa ya mapafu. Tulikuwa tumemaliza tu kumemzika mtoto wetu wa kiume mkubwa kwa sababu ya ugonjwa huu, na tulikuwa na wasiwasi sana kuhusiana na Willie, tukihofia kwamba yeye pia anaweza kufa. Tuliamua kwamba tusimwite daktari, lakini tufanye yote tuwezayo juu yake kwa kutumia maji, na kumsihi Bwana kwa ajili ya mtoto. Tuliwaita wachache, ambao walikuwa na imani ya kuunganisha maombi yao na yetu. Tulikuwa na uhakikisho wa msaada wa uwepo wa Mungu na baraka. .“Siku iliyofuata Willie alikuwa mgonjwa sana. Alikuwa akitangatanga. Hakuweza kuniona wala kunisikia nilipozungumza naye. Moyo wake haukuwa na mpigo ya kawaida, lakini ulikuwa katika hali ya kupepesuka mara kwa mara. Tuliendelea kumwomba Mungu kwa niaba yake, na kutumia maji juu ya kichwa chake, na kukanda kila mara mapafu yake, na mara alionekana kuwa mwenye afya kama siku zote. Alipata maumivu makali katika

upande wake wa kulia, na hakuweza kulala juu yake kwa muda. Maumivu haya tuliyapunguza kwa kutumia maji baridi, na kubadilisha joto la maji kulingana na kiwango cha homa. Tulikuwa waangalifu sana kuweka mikono na miguu yake ipate joto.

"Tulitarajia tatizo lingekuja siku ya saba. Tulipumzika kidogo tu wakati alipokuwa katika ugonjwa wake, na tulilazimika kumtoa chini ya uangalizi wa mwingine usiku wa nne na wa tano. Mume wangu na mimi mwenyewe, siku ya tano, tulipatwa na wasiwasi sana. Mtoto alitoa mdomoni damu safi nyekundu na kukohoa sana. “Mume wangu alitumia muda mwingi katika maombi. Tulimwacha mtoto wetu katika mikono makini usiku huo. Kabla ya kupumzika kwa usiku, mume wangu aliomba kwa muda mrefu na kwa bidii.

Ghafla alikoma kuomba, na ilionekana kana kwamba sauti ilizungumza naye, na kusema, Nenda kalale, nitamtunza mtoto..

"Nilikuwa mgonjwa, na sikuweza kulala kutokana na wasiwasi kwa saa kadhaa. Nilihisi pumzi kubana. Ingawa nililala kwenye chumba kikubwa, niliinuka na kufungua mlango ndani ya jumba kubwa, na mara moja nikafarijika, na mara nikalala. Niliota kwamba daktari mwenye uzoefu alikuwa amesimama karibu na mtoto wangu, akitazama kila pumzi, mkono mmoja akiwa ameweka juu ya moyo wake, na mwingine akisikiliza mapigo yake. Alitugeukia na kusema, ‘tatizo limeisha. Amepitia usiku mbaya zaidi. Sasa atainuka haraka, kwa kuwa hana madhara mabaya yanayotokana na dawa zenye sumu na atapona. Mwili umefanya kazi yake kwa ustadi ili kuondoa mfumo wa uchafu.’

“Nilimsimulia hali yangu ya uchovu, shinikizo la kupumua, na nafuu iliyopatikana baada ya kufungua mlango. “Alisema, ‘Kile kilichokupa ahueni pia kitamsaidia mtoto wako. Anahitaji hewa. Umemuweka kwenye joto sana. Hewa yenye joto inayotoka kwenye jiko inadhuru, na kama si hewa inayoingia kwenye nyufa za madirisha, ingekuwa sumu na kuharibu maisha. Joto la jiko huharibu uhai wa hewa, na kudhoofisha mapafu. Mapafu ya mtoto yamedhoofishwa, kutokana na chumba kuwa na joto sana. Wagonjwa hudhoofishwa na magonjwa, na wanahitaji hewa yote yenye kuleta nguvu ya uzima ambayo inaweza kuimarisha viungo muhimu vya kupinga magonjwa. Na bado katika hali nyingi, hewa na mwanga havipewi nafasi ya kuwepo kwenye chumba cha wagonjwa wakati ambao vihitajika sana, havipewi nafasi kana kwamba ni adui hatari.’

"Ndoto hii na uzoefu wa mume wangu vilikuwa faraja kwetu sote. Tuligundua asubuhi kwamba mtoto wetu alikuwa amepitia usiku usio na utulivu. Alionekana kuwa na homa kali hadi saa sita mchana. Kisha homa ikamwacha, na alionekana vizuri kabisa, japo dhaifu. Alikuwa amekula japo mkate mmoja mdogo kwa muda wa siku tano za ugonjwa wake. Alikuja haraka, hali akiwa na afya bora kuliko aliyokuwa nayo kwa miaka kadhaa kabla. Uzoefu huu ni wa thamani kwetu."— Facts of Faith, 151- 153.

"Ndugu alipatwa na ugonjwa wa kuvimba tumbo na kuhara damu. Mtu huyo hakuwa na matengenezo makini katika afya, bali alijiingiza katika ulafi wake. Tulikuwa tukijiandaa kuondoka Texas, ambako tulikuwa tukifanya kazi kwa miezi kadhaa, na tulikuwa na magari yaliyotayarishwa kumchukua ndugu huyu na familia yake, na wengine kadhaa waliokuwa wakiugua homa ya malaria.

"Mume wangu pamoja na mimi tuliwaza kuibeba gharama hii kuliko kuwaacha wenye familia hizi wakifa na kuwaacha wake zao na watoto wao bila mahitaji. Wawili au watatu walichukuliwa kwenye gari kubwa lenye magodoro yaliyonesa.

Lakini yule mtu aliyekuwa akisumbuliwa na tumbo, alinisihi niende kwake. Mume wangu pamoja mimi tuliamua kwamba haingekuwa vyema kumhamisha. Hofu ilitanda kwakuwa hali ya huzuni ilikuwa imeanza.

“Kisha wazo likanijia kama mawasiliano kutoka kwa Bwana, chukua mkaa uliopondwa, weka maji juu yake, na umpe maji hayo mgonjwa anywe, uweke bandeji za mkaa juu ya tumbo (uji wa mkaa kwenye kitambaa, poultice). Tulikuwa karibu maili moja kutoka jiji la Dennison, lakini kijana wake wa kiume wa huyo mgonjwa alienda kwenye duka la mhunzi, akaweka mkaa, na kuuponda, kisha akautumia kulingana na maagizo yaliyotolewa. Matokeo yake ni kwamba ndani ya nusu saa kulikuwa na mabadiliko yaliyo bora.

"Ilitubidi tuendelee na safari yetu na kuiacha familia, lakini tulishangaa sana siku iliyofuata kuona gari lao likitupita. Mgonjwa alikuwa amelala kwenye kitanda kwenye gari. Baraka ya Mungu ilikuwa imefanya kazi kwa njia rahisi iliyotumiwa."— Letter 182, 1899.

"Mojawapo ya tiba ya manufaa zaidi ni mkaa uliopondwa kwenye mfuko na kuutumia kwa njia ya kupaka. Hii ni dawa yenye mafanikio zaidi. Ikiwa utalowekwa katika mimea jamii ya smartweed (Persicaria), na kuchemsha, bado utakuwa ni bora. Nimeamuru hili katika hali ambapo wagonjwa walikuwa wakipata maumivu makali, na wakati nimepewa siri na daktari kwamba alifikiri ilikuwa ndiyo mwisho kabla ya ule mwisho wa kuishi. Kisha nikapendekeza mkaa,

wakati mgonjwa akiwa amelala, baada tu ya kufanya hivyo kisha aliamka kwa afueni, kisha afya yake ilirejea.

"Kwa wanafunzi, wakati wanapopata majeraha ya mikono, na kuteseka na uvimbe, nimeagiza dawa hii rahisi ili kuleta mafanikio kamili. Sumu ya uvimbe inakoma (inashindwa), na maumivu huondolewa, na uponyaji unaendelea haraka. Uvimbe mkali zaidi wa macho utaondolewa na dawa ya mkaa, weka kwenye mfuko na kuchovya kwenye maji ya moto au baridi kwa namna itakavyofaa zaidi. Hii inafanya kazi, kama hirizi. Natarajia utacheka kwa hili; Lakini kama ningeweza kuipatia jina lisilo la kawaida dawa hii, ambalo hakuna mtu anayelijua ila mimi mwenyewe, lingekuwa na ushawishi mkubwa zaidi."— Letter 82, 1897.

"Nitakuambia kidogo juu ya uzoefu wangu na mkaa kama dawa. Kwa aina fulani za matatizo ya tumbo yanayotokana na ulaji wa haraka (mfano kiungulia, kichechefu n.k), dawa ya mkaa ina ufanisi zaidi kuliko madawa ya kulevya. Kiasi kidogo cha mafuta ya mzeituni kinapochanganywa na dawa hii ya mkaa uliopondwa (poda au unga), huleta matokeo ya kusafisha na kuponya. naona ni bora.

Daima soma na fundisha matumizi ya tiba rahisi zaidi, na baraka za pekee za Bwana zitafuatana na matumizi ya njia hizi ambazo zinaweza kufikiwa na watu wa kawaida."—Letter 100, 1903.

"Nuru ilitolewa kwamba kuna afya katika harufu ya mtidhari (pine), mierezi, na mberoshi. na kuna aina nyingine kadhaa za miti ambayo ina sifa za dawa ambayo inakuza afya."—Letter 95, June 26, 1902.

"Wakati mmoja daktari alinijia akiwa katika dhiki kubwa. Alikuwa ameitwa kumhudumia mwanamke ambaye alikuwa mgonjwa na hatarini. Alikuwa amepatwa na homa akiwa kwenye uwanja wa kambi na alipelekwa kwenye jengo letu la shule, karibu na Melbourne, Australia. Lakini alizidi kuwa na hali mbaya zaidi kiasi kwamba alihofiwa kwamba hangeweza kuishi. "Daktari, Dk. Merritt Kellogg, alinijia na kusema, 'Dada White, Je unaweza kunipa uelewa/nuru kuhusu jambo hili? Kwa maana ikiwa dada yetu huyu hatapewa msaada, anaweza kuishi kwa masaa machache tu.' Nilijibu, 'Nenda kwenye duka la mhunzi ili upate mkaa uliopondwa; utengeneze ujiuji (poda), na uweke juu ya tumbo na ubavu wake.' Daktari akaharakisha kufuata maagizo yangu. Muda si mrefu alirudi, akisema, 'Utulivu na ahueni ilikuja kabla ya nusu saa baada ya kupaka dawa hizo. Sasa ana usingizi wa kwanza wa asili ambao amekuwa nao kwa siku nyingi. .

"Nimeagiza kufanya tiba kwa namna hiyo kwa wengine ambao walikuwa wakipata maumivu makali, na imeleta ahueni, na imekuwa njia ya kuokoa maisha. Mama yangu alikuwa ameniambia kwamba kuumwa na nyoka, au wanyama watambaao na wadudu wenye sumu mara nyingi tunaweza kuondoa madhara/sumu yake kwa kutumia dawa za mkaa (poda ya mkaa). Walipokuwa wakifanya kazi kwenye ardhi huko Avondale, Australia, wafanyakazi hao mara nyingi walichubuka mikono na viungo vyao, na hilo mara nyingi lilitokeza uvimbe wenye maumivu sana kiasi kwamba mfanyakazi huyo angelazimika kuacha kazi yake kwa muda fulani.

“Mmoja alinijia siku moja akiwa katika hali hii, huku mkono wake ukiwa umefungwa. Alikuwa na wasiwasi sana juu ya hali; kwa maana msaada wake ulitegemea katika kusafisha ardhi. Nikamwambia, ‘Nenda mahali ambapo umekuwa ukichoma mbao, na uniletee mkaa kutoka kwenye mti wa mikaratusi, uukate, nami nitaupaka mkononi wako.’ Baada ya kufanya hivyo, asubuhi iliyofuata aliripoti kwamba maumivu yalikuwa yamekoma. Hivi karibuni alikuwa tayari kurudi kazini kwake. .

“Ninaandika mambo haya ambayo unaweza kujua kwamba Bwana hajatuacha bila kutumia dawa sahili ambazo zikitumiwa, hazitasababisha hali mbaya kwenye mwili kama ambavyo matumizi ya dawa mara nyingi husababisha.

Tunahitaji wauguzi waliofunzwa vyema ambao wanaweza kuelewa jinsi ya kutumia tiba rahisi ambazo asili hutoa kwa ajili ya kurejesha afya, na ambao wanaweza kuwafundisha wale ambao hawajui sheria za afya jinsi ya kutumia tiba hizi rahisi lakini huponya hakika.”—Letter 90, 1908.

“Upana wa kazi ya umishenari ya injili haueleweki. Kazi ya umishenari wa tiba inayotakiwa sasa ni ile iliyoainishwa katika utume ambao Kristo aliwapa wanafunzi Wake kabla ya kupaa Kwake. Mathayo 28:18-20 "Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Maneno haya yanaonyesha eneo letu na kazi yetu. Eneo letu ni ulimwengu; Kazi yetu ni kutangaza Ukweli ambazo Kristo alikuja katika ulimwengu wetu kutangaza.” —Counsels on Health, 509

SEHEMU YA 6

KANUNI ZA AFYA

SURA YA 19

JE, TUNAPASWA KUHATARISHA KANUNI ZETU ZA AFYA ILI KUWASAIDIA WALE WALIO KARIBU NASI?

Tunapokuwa na watu wengine—ama Waadventista au wasio Waadventista—ambao hawaelewi au hawakubaliani na kanuni zetu za afya, ni wakati gani tunapaswa kusimama na kanuni zetu binafsi za kidini na kiafya? Je, ni sawa

kuafikiana nao kwa muda ili kuwafikia watu walipo? Je, tunapaswa kwenda umbali gani ili kuwapatanisha wale wanaotuzunguka?

1- NI LAZIMA TUKUTANE NA WATU PALE WALIPO NA KUANZA HUDUMA YETU ILI KUFIKIA MAHITAJI YAO KWA KIWANGO CHAO CHA UFAHAMU

Kuwafikia watu po pote pale walipo, bila ya kujali nafasi au hali yao, na kuwasaidia kwa kila njia kwa kadiri inavyowezekana— hii ndiyo huduma ya kweli. Kwa juhudi kama hizo unaweza kuileta mioyo yao kwa Bwana na kufungua mlango wa kuzifikia hizo roho zinazoangamia. —Ministry of Healing, 156.

Katika kufundisha,Masihi alishuka chini hata kuwa sawa na wao kwa hadhi. Yeye, Mkuu na enzi ya mbinguni, alijibu maswali yao na kurahisisha masomo Yake muhimu ili kukidhi ufahamu wao wa kitoto.—Ministry of Healing, 42.

Kuna haja ya kuwa karibu na watu kwa juhudi binafsi. Ikiwa wakati mdogo tu, ndio ungetolewa katika kuhubiri,na wakati mwingi ungetumika katika huduma binafsi,matokeo makubwa yangeonekana. Masikini wanapaswa kupumzishwa, wagonjwa wahudumiwe, wenye huzuni na wafiwa wafarijiwe, wajinga wafundishwe, wasio na uzoefu washauriwe. Tunapaswa kulia na wale wanaolia, na kufurahi pamoja na wale wanaofurahi. Ikifuatana na nguvu ya ushawishi, nguvu ya maombi, nguvu ya upendo wa Mungu, kazi hii haitakosa matunda. — Counsels on Diet and Foods, 458.

Kuwakubali watu mahali walipo na kuwasaidia kwa njia yoyote inawezekana ni huduma ya kweli Welfare Ministry, 121.

Tukio ambapo mchuzi wa kuku ulitolewa chini ya maelekezo ya dada White ni kwa sababu ya watu walikuwa maskini na hakuna kitu kingine chochote kilichopatikana. -Counsels on Diet and Foods, 462.

Usifanye harakati za haraka haraka kuhamasisha maoni juu ya watu, lakini acha matengenezo ya afya yawasilishwe kwa uangalifu na elimu inayoungwa mkono na mfano. -Counsels on Diet and Food, 462. Usitetee hatua za juu katika matengenezo ya afya bila kuwafundisha watu jinsi ya kuandaa chakula chenye afya; Counsels on Diet and Food, 462, 460, mbinu kwa wale ambao mlo wao unakosa vipengele sahihi vya lishe (Counsels on Diet and Food, 462, 474).

Ni lazima tuwatendee waongofu wapya kwa upole, wale ambao wamebanwa na umaskini na ambao wameishi kwa kiasi kikubwa wakitegemea juu ya chakula cha nyama (Counsels on Diet and Foods, 463).

“Huduma ya Yesu ilikuwa tofauti kabisa na mtazamo wa wazee wa Kiyahudi. Heshima yao kwa desturi za mazoea ilikuwa imeharibu uhuru halisi wote wa mawazo na matendo. Waliishi katika uchafu wa kutisha na kudumu. Wakikwepa kukutana na watu "walio najisi," walidumu kujitenga, si tu na Mataifa, bali hata na wengi miongoni mwa watu wa taifa lao, wakitaka kwamba watu hao wasinufaike nao kwa lolote wala wasipate urafiki kutoka kwao. Kwa kuzama katika mambo haya wakati wote, walikuwa wamepotosha mawazo yao na kufanya upeo wa maisha yao kuwa finyu. Kielelezo chao kilifundisha kujipenda na kukosa uvumilivu miongoni mwa matabaka yote ya watu. Yesu aliianza kazi Yake ya matengenezo kwa kuja katika huruma ya karibu na wanadamu. Wakati alionyesha heshima kubwa kwa sheria ya Mungu, alikemea uchaji-Mungu wa kujionyesha wa Mafarisayo, na alijaribu kuwafanya watu wawe huru pasipo kufungwa na taratibu zisizo maana ambazo zilikuwa zimewafunga. Alikuwa anajitahidi kuvunja vizuizi vilivyotenganisha matabaka tofauti- tofauti ya jamii, ili kwamba awalete watu pamoja kama watoto wa familia moja” -The Desire of Ages, 150.

Yesu alijumuika kijamii katika asili na kutembelea nyumba za tabaka zote za jamii. -The Desire of Ages, 150-151).

Ni lazima tukutane na watu pale walipo na kuunganisha maslahi yetu na ubinadamu. -The Desire of Ages, 152).

Yesu alijifunza jinsi ya kuwafikia matajiri pia kwa kuchukuliana na maslahi yao. -Ministry of Healing, 24-25

Yesu aliaminika mbele ya watoza ushuru alipokuwa akila pamoja nao. -The Desire of Ages, 26.

Kristo alitumia kwa uangalifu talanta ya usemi kwa jinsi alivyojishiriki na tabaka zote za jamii na mara kwa mara alizungumza Neno kwa wakati unaofaa na kwa kila tukio. -Welfare Ministry, 286-288.

Uangalifu katika kuwasilisha matengenezo ya afya katika hali yake ya juu zaidi unahitajika pale ambapo mazingira yanakataza kuasiliwa kwake (Counsels on Diet and Food, 463)

Tunahitaji pia kuwa waangalifu ili tusitoe kauli za kufagilia (kuondoa), lakini tuzingatia mazingira (hali) (Counsels on Diet and Food, 462-463).

Usifanye mawazo ya pekee kuwa mtihani na kuwakosoa wengine, lakini jizoeze kuwa na kiasi wewe mwenyewe (Counsels on Diet and Foods, 464).

"Hatupaswi kwenda kwa kasi zaidi kuliko tunavyoweza kwenda pamoja na wale ambao dhamiri na akili zao zinaamini zile Kweli tunazozitetea. Lazima tukutane na watu mahali walipo. Baadhi yetu wamechukua miaka mingi kufika katika nafasi yetu ya sasa katika matengenezo ya afya. Kufanya matengenezo katika lishe, ni kazi ya taratibu. Tunatakiwa kukabiliana na uchu wenye nguvu; kwakuwa ulimwengu umejitoa katika ulafi. Ikiwa tutawapa watu wakati mwingi kama ule tuliouhitaji kufikia katika hali ya juu ya sasa katika matengenezo, tungekuwa wavumilivu sana kwao,na kuwaruhusu wasonge mbele hatua kwa hatua, kama tulivyofanya, mpaka miguu yao isimamishwe imara juu ya jukwaa la matengenezo ya afya. Lakini tunapaswa kuwa waangalifu sana kutosonga mbele haraka sana, tusije tukalazimika kurudisha nyuma hatua zetu. Katika matengenezo, ni bora tungeku wa nyuma ya mstari hatua moja kuliko kwenda mbele ya mstari hatua moja. Na ikiwa kuna kosa kwa namna yoyote, hebu liwe upande wa pili wa watu. CD 468.1

Zaidi ya yote, hatupaswi kwa kalamu zetu kutetea misimamo ambayo hatuiweki katika vitendo katika familia zetu, juu ya meza zetu wenyewe. Huu ni udanganyifu, aina ya unafiki. Huko Michigan tunaweza kuishi vizuri bila chumvi, sukari, na maziwa, kuliko watu wengi walioko Magharibi ya Mbali au Mashariki ya Mbali, ambako kuna uhaba wa matunda....Tunajua kuwa matumizi holela ya vitu hivi ni mabaya kwa afya, na katika hali nyingi tunafikiria kwamba ikiwa havitatumiwa kabisa, hali bora zaidi ya afya ingefurahiwa. CD 468.2

Lakini kwa sasa mzigo wetu hauko juu ya vitu hivi. Watu wako nyuma sana kiasi kwamba tunaona kuwa kutufanya tuweke mstari juu ya uendekezaji wao mbaya na dawa za kusisimua ndiyo kile tuwanachoweza kuvumilia. Tunatoa ushuhuda mzuri dhidi ya tumbaku, pombe kali, ugoro, chai, kahawa, chakula cha nyama, siagi, viungo, keki zenye sukari nyingi, mikate yakukatakata, chumvi nyingi, na vitu vyote vya kusisimua vinavyotumika kama aina za chakula- CD 468.3

Tunapokuja kwa watu ambao hawajaangaziwa kuhusu matengenezo ya afya, na kutoa msimamo wetu wenye nguvu zaidi mwanzoni,kuna hatari ya kukatishwa tamaa wanapoona ni mengi kiasi gani wanapaswa kuachana nayo, kiasi kwamba hawatafanya juhudi yoyote katika kufanya matengenezo. Lazima tuwaongoze watu kwa uvumilivu na hatua kwa hatua, tukikumbuka tundu la shimo ambamo tulichimbwa.” -Counsels on Diet and Foods, 468-469.

2- KISHA, HATUA KWA HATUA/TARATIBU, TUNAPASWA KUWAONGOZA WATU KWENYE VIWANGO VYA JUU ZAIDI NA UTII KAMILI ZAIDI WA SHERIA ZA MUNGU

“Lipo hitaji kubwa la kufundisha watu kuhusu matengenezo ya lishe, na utayarishaji wa chakula bora. Mazoea mabovu ya ulaji na matumizi ya vyakula visivyokuwa na afya ndivyo huhusika kwa kiwango kikubwa katika hali ya kukosa kiasi na uhalifu na unyonge ambavyo ni laana kwa ulimwengu.” -Ministry of Healing, 146. [MH 146.3]

"Katika kufundisha kanuni za afya, weka akilini lengo kuu la matengenezo, - kwamba kusudi Lake ni kupata maendeleo ya juu zaidi ya mwili na akili na roho. Onyesha kwamba sheria za asili, zikiwa sheria za Mungu, zimeundwa kwa faida yetu; kwamba utii kwazo hukuza furaha katika maisha haya, na husaidia katika maandalizi kwa ajili ya maisha yajayo. Counsels on Diet and Food 457.4

Ongoza watu kujifunza udhihirisho wa upendo wa Mungu na hekima katika kazi za uumbaji (asili). Waongoze kujifunza juu ya kiumbe hicho cha ajabu, mfumo wa mwanadamu, na sheria zinazoutawala. Wale ambao wanaona Ushahidi wa upendo wa Mungu, ambao wanaelewa kitu fulani kuhusu hekima na faida ya sheria Zake, na matokeo ya utii, watayatazama majukumu na wajibu wao kwa mtazamo tofauti kabisa. Badala ya kuangalia utunzaji wa sheria za afya kama suala la kujitoa kafara au kujikana nafsi, watauchukulia, kama ulivyo kwa hakika, kama baraka isiyo na kifani. Counsels on Diet and Food 457.5

Kila mtendakazi wa injili anapaswa kuhisi kwamba utoaji wa mafundisho katika kanuni za kuishi kiafya, ni sehemu ya kazi aliyopewa. Kuhusu kazi hii kuna uhitaji mkubwa, na ulimwengu uko wazi kwa ajili yake. –Ministry of Healing, 146,147, 1905. CD 458 .1

Watu wanapaswa kufundishwa kuweka kando mazoea yasiyofaa (Counsels on Diet and Foods, 447).

Watu wavutiwe na umuhimu ya kuishi kulingana na matengenezo ya afya (Counsels on Health, 441).

Wasilisha kanuni ya matengenezo ya afya kwa makini na kwa kina kwa wote (Counsels on Diet and Foods, 449).

Usijaribu kufanya matengenezo kwa kushambulia tabia mbaya za wengine, lakini wawasilishie kitu bora kuliko walicho nacho (Counsels on Diet and Foods, 459).

Usihimize mabadiliko ya ghafla katike lishe, lakini shikilia kanuni za matengenezo ya afya na umruhusu Bwana awaongoze walio waaminifu moyoni (Counsels on Diet and Foods, 465).

Ni lazima tuwafundishe watu kwa subira; kila kitu hakiwezi kueleweka kwa mara moja (Counsels on Diet and Foods, 465).

3- KATIKA KUKUTANA NA WATU MAHALI WALIPO, HATUPASWI KAMWE KUKIUKA SHERIA ZA MUNGU

Warumi 6:1-2: Hatupaswi kuendelea katika mwenendo wa dhambi.

Yakobo 4:17: Ni dhambi ikiwa tunajua kutenda mema na tusiyafanye.

Warumi 6:6-23: Utu wa zamani wa dhambi umesulubishwa pamoja na Kristo; Jitoe kwa Mungu.

Yohana 9:41: Nuru inapokuja, dhambi huhesabiwa kwa kuwa nuru haifuatwi.

Yohana 12:35 Basi Yesu akawaambia, Nuru ingaliko pamoja nanyi muda kidogo. Enendeni maadamu mnayo nuru hiyo, giza lisije likawaweza; maana aendaye gizani hajui aendako.

Mathayo 10:32-33: Kama tutaendelea katika Neno la Mungu, sisi ni wanafunzi; Ukweli hutuweka kuwa huru.

Mhubiri 10:17: Tunapaswa kula ili tupate nishati na si kwa ajili ya ulevi.

1 Wakorintho 10:31: Fanya yote kwa utukufu wa Mungu.

1 Wakorintho 6:19-20: Tunapaswa kumtukuza Mungu katika miili yetu kwa sababu ni hekalu Lake.

1 Wakorintho 3:16-17 Mungu atawaangamiza wale wanaolitia unajisi Hekalu la Mwili.

Warumi 12:1: Miili yetu inapaswa kutolewa kama dhabihu iliyo hai.

Kumbukumbu la Torati 14:2-3: Watu waliochaguliwa na Mungu hawapaswi kula kitu chochote chenye machukizo.

Kutoka 15:26: Ikiwa tunatii amri Zake, Mungu atatuepusha na magonjwa ambayo ulimwengu unateseka.

Mhubiri 12:13-14: Mche Mungu na kushika amri; Hili ndilo jukumu zima la mwanadamu.

Ufunuo 14:12: Watakatifu hushika amri za Mungu na imani ya Yesu.

Ufunuo 22:14: Wale washikao amri Zake wanaingia Yerusalemu mpya.

“Tunapokaribia mwisho wa wakati lazima tuinuke juu zaidi na zaidi juu ya suala la matengenezo ya afya na kiasi cha Kikristo, tukiliwasilisha kwa njia chanya na iliyoamuliwa zaidi. Ni lazima tujitahidi daima kuwaelimisha watu, si kwa maneno yetu tu, bali kwa matendo yetu. Maagizo ya nadharia na matendo halisi kwa pamoja yana ushawishi wa kusema." — Shuhuda kwa Kanisa 6: 112.

"Hatuna haki ya kukiuka hata kanuni moja ya sheria za afya. Wakristo hawapaswi kufuata desturi na tamaduni za ulimwengu. “Historia ya Danieli imewekwa kwenye kumbukumbu kwa manufaa yetu. Nabii huyu alichagua kufuata njia ambayo ingemfanya awe mtu wa kipekee kabisa katika Ikulu ya mfalme. Hakuendana na mazoea ya watumishi katika kula na kunywa, bali aliazimia moyoni mwake kwamba hatakula chakula cha mfalme wala kunywa divai zake. Hili halikuwa kusudi lililoundwa moyoni kwa haraka, na linaloyumba-yumba, bali lile ambalo liliundwa kwa akili na kutekelezwa kwa uthabiti- siku kwa siku.

“Wale wanaomtumikia Mungu kwa unyofu na Ukweli watakuwa watu wa pekee, tofauti na ulimwengu, waliojitenga na ulimwengu. Chakula chao kitatayarishwa, sio kwa kusudi la kuchochea ulafi au kuridhisha ladha potovu, bali kwa kujipatia tu nguvu kubwa zaidi za kimwili, na hivyo basi hali bora za kiakili. .

“Imani yetu inatuhitaji kuinua kiwango cha matengenezo, na kuchukua hatua za juu. Sharti ya kukubalika kwetu na Mungu ni kujitenga kwa vitendo dhidi ya ulimwengu. Bwana anatuita sisi kama watu,2 Wakorintho 6:7, 17 Kwa hiyo, Tokeni kati yao, Mkatengwe nao, asema Bwana, Msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha. Ulimwengu unaweza kukudharau kwa sababu hufikii kiwango chao, hujihusishi na burudani zao za muda kitambo, na hufuati njia zao mbaya; Lakini Mungu wa Mbinguni anaahidi kukupokea, na kuwa Baba kwako. 2 Wakorintho 6:18 Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike. —Counsels on Health, 50-51.

“Akili ni lazima ifundishwe kwa njia ya mitihani ya kila siku ili kuunda tabia zenye uadilifu, na kuwa na hisia za madai ya haki na majukumu yaliyo juu ya mambo ya anasa na ya kujifurahisha nafsi. Akili iliyofundishwa hivyo huwa haiyumbi kati ya mema na mabaya, kama matete yanavyotetemeka na kuyumba wakati wa upepo; lakini mara tu jambo linapotokea mbele ya akili, hutambuliwa mara moja kwamba kuna kanuni inayohitajika, na mara moja huchagua jema bila kuchukua muda mrefu wa kujadiliana kuhusiana na hilo jambo. Watu wa namna hiyo ni watu waungwana/waadilifu kwa sababu wamejifunza wao wenyewe katika masafa ya tabia za uaminifu na Ukweli tu. - Shuhuda kwa Kanisa 3: 22.

Katika uhusiano wenu na wasio amini, msiruhusu kuondolewa katika kanuni sahihi. Kama ukiketi mezani pao, kula kwa kiasi, na chakula kile tu ambacho hakitavuruga akili. Weka wazi hali ya kutokuwa na kiasi. Hauwezi kumudu kudhofisha nguvu zako za akili na mwili, kwani itakufanya kushindwa kupambanua mambo ya kiroho. Iweke akili yako katika hali ambayo Mungu anaweza kuivuta kwa zile Kweli za thamani za Neno Lake. Usitazame wengine ili kusonda au kuonyesha makosa yao au kasoro zao. Fundisha kwa mfano. Hebu kujikana nafsi kwako na ushindi wako juu ya uchu wa chakula uwe kielelezo cha utii kwa kanuni sahihi. Hebu maisha yenu yatoe ushuhuda kwa mvuto wa Ukweli unaotakasa, na kukuza tabia. —Counsels on Diet and Foods, 464-465.

"Kwa wale wote walioamua kuwa wanamatengenezo wa usafi ningesema, ishi haya matengenezo kwa uthabiti, kwa imani ya akili yako mwenyewe, yenye utambuzi, iliyoelimishwa. Usiongozwe katika anasa na makundi ya marafiki. Matengenezo nyumbani; Na unapoenda nje ya nchi, yabebe pamoja nawe. Yaishi, na kwa nyakati zinazofaa, mahali pazuri, na kwa njia ifaayo, zungumza kanuni zake. Daima shikilia njia yako, na kwa njia zote fanya kazi ili kuwavutia wale walio karibu nawe umuhimu wa somo. —Counsels on Health, 447.

Katika kufikia uamuzi huu, vijana wa Kiebrania hawakutenda kwa kiburi bali katika tegemeo thabiti kwa Mungu. Hakukuchagua kutengana, lakini ingekuwa vyema hata watengane kuliko kutokumtii Mungu. Iwapo wangekubaliana na makosa katika jambo hili kwa kukubaliana na msukumo wa hali iliyopo kuondoka kwao kutoka kwenye kanuni kungeweza kudhoofisha hali zao za haki na kuchukia kwao uovu. Hatua ya kwanza mbaya ingewapeleka kwenye hatua zingine, mpaka uhusiano wao na mbingu utakapokatika, wangekuwa wamechukuliwa na majaribu —Prophets and Kings, 483.

Soma Prophets and Kings, 481-483 (Manabii na Wafalme), kuhusu Danieli na wale vijana watatu wa Kiebrania.

“Udugu wa kweli hauwezi kamwe kudumishwa kwa kuafikiana……Upinzani wa kizazi kisicho na utii unaamshwa na Ukristo ambao ni wa kiroho. Katika zahama hizi ni wakati wa kuamua ni akina nani ambao ni watumishi waaminifu wa Mungu, ambao watakuwa waaminifu kwenye kanuni, ambao watakumbuka kwamba Ukweli unanunuliwa tu kwa kanuni yake ndogo zaidi ya kusalimu amri. Amani hiyo na maelewano ambayo yanalindwa kwa makubaliano ya pande zote ili kuepuka tofauti zote za maoni hayastahili Jina. Kuhusu masuala ya hisia kati ya mwanadamu na mwanadamu, makubaliano yanapaswa kufanywa wakati

mwingine; Lakini hata chembe moja ya kanuni haipaswi kutolewa dhabihu ili kuleta maelewano.” —Review and Herald, January 16, 1900.

“Kamwe Yesu mwenyewe hakutafuta amani kwa maafikiano ya kulegeza msimamo. Moyo wake ulifurikishwa na pendo kwa wanadamu wote, lakini kamwe hakuendekeza dhambi zao.

Hakuna mtu yeyote anayeweza kuwa katika kanuni ya Ukweli halafu asiamshe hali ya upinzani. Ukristo ulio wa kiroho utapingwa na watoto wasio watiifu.” - The Desire of Ages, 356.

Tunapaswa kuupa ulimwengu uwakilishi safi wa Kristo (Counsels on Diet and Foods, 459). Iwasilishe kwa uangalifu nuru juu ya matengenezo ya afya na uweke mfano sahihi (Counsels on Diet and Foods, 462). Dada White daima aliliweka mezani somo la matengenezo ya afya (Counsels on Diet and Foods, 472-473). Mazoea ya tamaa ya kula huleta magonjwa yaliyoachwa na mababu zetu (Counsels on Health, 49).

Ulimwengu sio kipimo chetu; Utulivu thabiti katika mambo yote unahitajika. (Counsels on Health, 51).

Kila mtu anapaswa kufikiri na kutenda kwa ajili yake mwenyewe, na kumwomba Mungu kwa ajili ya hekima. (Counsels on Health, 48).

Njia yoyote ambayo inapunguza afya yetu ya kimwili ni dhambi dhidi ya Mungu. (Counsels on Health, 43).

Mtu lazima awe mwaminifu; kukosa uaminifu katika ile Kweli ni mbaya (Counsels on Health, 34-35).

Hatuna wakati au nguvu ya kutumia katika kujifurahisha (Counsels on Health, 128).

Tutapata maumivu makali ikiwa tutapunguza au kulemaza kazi yoyote ya mwili. (Counsels on health, 107). Kuupenda ulimwengu, ulafi, na mawazo binafsi ndiyo majaribu matatu makuu (Counsels on Health, 287-288).

Ikiwa kanuni za kidini zinatawala, hatari ya kufanya makosa makubwa ni ndogo (Counsels on Health, 288).

Mvuto wetu ni kuwaongoza wengine kuelekea juu au kuwashusha chini. (Counsels on Health, 421).

Hatutambui ushawishi tunaotoa kwa wengine siku baada ya siku. (Counsels on Health, 413).

Mwinjilisti wa vitabu, anapokaa majumbani, anaweza kuweka mfano mzuri wa matengenezo ya afya kwa kutokula nyama au vitu vingine vyenye madhara. (Counsels on Health, 463).

Kurudi nyuma mara kwa mara katika matengenezo ya afya ni sababu ya hali ya chini ya kiroho na imeweka vikwazo. (Counsels on Health, 578-579).

Ikiwa Waadventista Wasabato wangetekeleza matengenezo ya afya, kwa hakika ingekuwa tamasha kwa ulimwengu, na tungeonyesha bidii kubwa zaidi kwa ajili ya wokovu wa roho zilizopotea (Counsels on Health, 575).

Wale ambao hawashindi uchu wa kula watashindwa kukamilisha tabia ya Kikristo (Counsels on Health, 574).

Iwapo kuna ulazima wa mlo rahisi, ni sasa (Counsels on Health, 622).

Ulimwengu huu ni shule ya mafunzo ya shule ya juu inayofuatia (Counsels on Health, 581).

Mfano wetu katika matengenezo ya afya una nguvu zaidi kuliko kuuhubiri kwetu (Counsels on diets and Foods, 141).

4- WAJIBU WA WATUMISHI KUHUSIANA NA MATENGENEZO YA AFYA

Sehemu moja ya muhimu ya kazi ya huduma ni kuwasilisha kwa uaminifu kwa watu matengenezo ya afya, kama yasimamavyo yakiwa yameunganishwa na ujumbe wa Malaika yule watatu, kama sehemu hasa ya kazi ile. Hawapaswi kushindwa kuyafuata wao wenyewe, na wangehimiza juu ya wote ambao hudai kuamini ukweli. —Counsels on Diet and Foods, 74.

“Wahudumu wetu wanapaswa kuwa na akili juu ya suala hili. Hawapaswi kupuuza, wala kugeuzwa na wale wanaowaita watu wenye msimamo mkali. Hebu na wajue ni nini kinachojumuisha matengenezo ya kweli ya afya, na kufundisha kanuni zake, kwa kanuni na kwa tulivu, na mfano thabiti. ." - Temperance, 499.

Watendakazi wana kazi ya kufanya hapa.Wanapochukua msimamo sahihi juu ya somo hili, mengi yatapatikana. Katika maisha yao na nyumba zao wanapaswa kutii sheria za uzima, wakitenda kanuni sahihi na kuishi kiafya. Hapo wataweza kuzungumza kwa usahihi juu ya mada hii, wakiwaongoza watu juu zaidi na zaidi katika kazi ya matengenezo. (Counsels on Diet and Foods, 452).

Wenyeviti wa koferensi zetu wanahitaji kujua kuwa ni wakati muafaka wa kujiweka wao wenyewe upande sahihi wa suala hili. (Counsels on Diet and Foods, 452-453).

Kama watendakazi wangeshikilia kazi hii katika idara zake mbalimbali kulingana na nuru ambayo Mungu ametoa, kungekuwa na matengenezo yaliyo wazi zaidi katika ulaji, unywaji, na uvaaji. (Counsels on Diet and Foods, 453).

Hakuna mtu anayepaswa kutengwa kama mwalimu wa watu wakati mafundisho yake mwenyewe au mfano wake unapingana na ushuhuda ambao Mungu amewapa watumishi wake kutoa kuhusu lishe, kwani hili litaleta mkanganyiko. Kupuuza kwake matengenezo ya afya humfanya asifae kusimama kama mjumbe wa Bwana. (Counsels on Diet and Foods, 453-454).

Wale ambao wanasimama mbali na kazi kubwa ya kuwafundisha watu juu ya suala hili, hawafuati ambako Tabibu Mkuu anaongoza njia (Counsels on Diet and Foods, 454).

Wahudumu lazima wawe na kiasi kabisa katika kula, kunywa, au kuongeza juhudi katika ujumbe wanaouhubiri (Counsels on Health, 575)

Watu wanaohubiri ujumbe huu wanapaswa kuwa mifano kwa watu katika kula, kunywa, mazungumzo, na mwenendo (Counsels on Health, 572-573).

Kadiri msimamo unavyowajibika zaidi, ndivyo ushawishi mkubwa wa mema au mabaya (Counsels on Health, 614).

HITIMISHO

Katika suala la kuwaongoza watu kwenye kiwango cha Yesu, tunapaswa kuwa waangalifu na kuwaleta kwenye kweli mpya polepole mara tu wanapojitayarisha kuzipokea. Ikiwa kutakuwa na ulazima mara zote wa kuwa na makosa basi iwe ni kwa upande wa watu. Daima ni bora kuzuia ishara au alama kwenye hatua ndogo kuliko kwenda hatua moja zaidi yake. Mpango wa Mungu wa kufundisha matengenezo ya afya kwa wengine ambao hawajui unaonekana kuwa (1) mfano thabiti kwetu wenyewe na, (2) uchunguzi unapofanywa kuhusu sababu yetu ya msimamo tunaochukua, tuna nafasi ya kuitanguliza kanuni mbele.

Ni wazi kwamba kulingana na uaminifu binafsi juu ya kiwango cha ufuasi wetu, hakuna kitu kinachopaswa kuturuhusu tupotoke—si wakati wala mahali, desturi, marafiki, jamaa, au maadui. Kuunganishwa kwetu kiroho na mbingu na ushuhuda wetu wenye nguvu zaidi—mfano wetu—vitadhihirishwa na uaminifu huo.

KIELELEZO BINAFSI CHA ELLEN G. WHITE

Sijarudi hata hatua moja nyuma, tangu nuru kutoka mbinguni juu ya mada hii ilipoangaza katika njia yangu. Niliachana na kila kitu mara moja,-kutoka katika utumiaji wanyama na siagi, na kutoka katika kula milo mitatu,- Japokuwa wakati huo nilikuwa nikifanya kazi ya kuchosha ya ubongo, kuandika kutoka asubuhi mapema hadi jioni. Nilirudi mezani kwenye lishe yangu ya milo miwili kwa siku bila kubadilisha kazi yangu. (Counsels on Diet and Foods, 483).

Kisha nikaona kwamba lazima nibadilishe mwenendo wangu wa maisha, na kwa kupumzika siku chache nilitoka nikiwa vizuri tena. Niliacha vitu hivi kutokana na kanuni. Nilichukua msimamo wangu juu ya matengenezo ya afya kutokana na kanuni. Na tangu wakati huo, ndugu, hamkunisikia nikitanguliza maoni ya kishupavu juu ya matengenezo ya afya ambayo imenilazimu kuchukua. Sijasonga mbele ila kile ninachosimama leo. Ninapendekeza kwako lishe yenye afya, yenye lishe (Counsels on Diet and Foods, 484).

Kadri unavyoikubali tabia hii kwa kuiendekeza, Shetani atashikilia mapenzi yako, na kuyafanya yamtii yeye mwenyewe. Lakini ikiwa utaamua kushinda, Bwana atakuponya, na atakupa nguvu ya kupinga kila jaribu. Daima kumbuka kuwa Kristo Ndiye Mwokozi na Mtunzaji wako (Counsels on Diet and Foods, 485).

Ninakula chakula cha kutosha kukidhi mahitaji ya asili (mwili); lakini ninapoinuka kutoka mezani, hamu yangu ya chakula ni nzuri, sawa tu na wakati nilipoketi mezani. Na mlo unaofuata unapokuja, niko tayari kuchukua sehemu yangu ya mlo, na wala sio zaidi ya hapo. Je! Ninapaswa kula maradufu zaidi mara kwa mara kwa sababu tu chakula kilichotayarishwa kina ladha nzuri? Je, ningewezaje basi kupiga magoti na kumwomba Mungu anisaidie katika kazi yangu ya uandishi, wakati nimekuwa sina hata fikra kuhusiana na ulafi wangu? Je, ningeweza kumwomba Mungu kushughulikia rundo la mzigo huo wa chakula usio na sababu ndani ya tumbo langu? Hakika huku kungekuwa ni kumwaibisha Yeye. Huku kungekuwa ni kumwomba kuridhisha tamaa yangu tu. Sasa ninakula kile tu ambacho ninafikiri kuwa ni sahihi, na kisha ninaweza kumwomba Bwana anipe nguvu ya kufanya kazi ambayo amenipa niifanye. Na nimejua kuwa Mbingu zimesikia na kujibu maombi yangu, wakati nilipotoa maombi haya (Counsels on Diet and Foods, 485-486).

Daima Bwana alitoa chakula rahisi, cha afya cha kutosha kwa wote waliokuja (Counsels on Health, 486).

Hakuweka kikwazo kwa wengine. Meza yake ilitayarishwa kwa chakula mara mbili kwa siku; lakini, kama wengine walitaka kula mlo wa tatu jioni, hawakukatazwa (Counsels on Diet and Food, 491).

Alifanya mpango wa milo miwili kwa miaka thelathini na tano, kama alivyoandika mnamo 1903 (Counsels on Diet and Food, 490).

Hakuna siagi, nyama, jibini, au mchanganyiko wa grisi wa chakula ulikuwa kwenye meza yake (Grease ni mafuta mazito ya wanyama au mimea, enzi zile yalikuwa mafuta ya nguruwe mara nyingi-lard) (Counsels on Diet and Food, 491).

Anaripoti, kwamba hakuwa ameishi kulingana na kanuni za matengenezo ya afya, hazikuwa za kweli (Counsels on Diet and Food, 491-492).

Alikataa kuweka tumboni mwake michanganyiko yoyote inayozalisha uvundaji/uchachushaji wa chakula. (Counsels on Diet and Food, 493).

Nuru aliyopewa ilitoka kwa Bwana; Hakuwahi kumvamia mtu yeyote kuhusiana na meza au vitu vya kuweka mezani (Counsels on Diet and Food, 493).

Alijaribu kujifunza kile kilichokuwa bora kwake, na akashiriki kimya kimya (Counsels on Diet and Food, 493-494).

Alijilinda kwa uangalifu dhidi ya tabia yoyote ambayo ilipunguza nguvu za akili (Counsels on Diet and Food, 492)

5- PALE UNAPOWABURUDISHA/KUWAFURAHISHA WAGENI AU KUTEMBELEANA MAJUMBANI MWETU NA WATU WENGINE

Hatupaswi kukiuka viwango vyetu tunapokuwa na wengine. Kutembeleana kama mtindo mara nyingi ni tukio la ulafi tu. (Counsels on Diet and Food, 88).

Wakristo hawapaswi kuwa watumwa wa mitindo kwa uchu wa kula (Counsels on Diet and Food, 232).

Kusudi la kutembeleana na wengine ni kuwa baraka, na sio kujifurahisha nafsi. (Counsels on Diet and Food, 88).

Watu wengine wana lishe duni katika familia zao wenyewe, ili waweze kuwa na chakula cha ziada kwa ajili ya wageni (Counsels on Diet and Food, 180).

Kuna haja ya kuwa na usahili zaidi katika kutumbuiza wageni (entertaining guests); Mahitaji ya familia yanapaswa kuzingatiwa kwanza (Counsels on Diet and Food, 89).

Sikukuu za kina kwa wageni ni mzigo kwa mke na jeraha kwa tumbo (Counsels on Diets and Food, 132).

Madhara mabaya ya burudani ya kina kama hii kwa watoto wa mtu mwenyewe (Counsels on Diet and Food, 202).

Chakula bora, chenye lishe, na rahisi kinaweza kutayarishwa kwa wageni (Counsels on Diets and Food, 88-89).

Muda pekee ambapo Dada White alikula chakula kisicho na afya pamoja na wengine ilikuwa wakati ambapo kila kitu kilichokuwa kwenye meza hakikuwa na afya, na ilimbidi kula kitu kidogo ili tu aendelee kuishi.(Counsels on Diet and Foods, 257).

Kukuza kujidhibiti; Zuia uchu wa kula (Counsels on Diet and Food, 176).

Wachache wana uwezo wa kimaadili wa kupinga majaribu; Wanawazia wana njaa wakati mapenzi/nia ya akili haijaimarishwa kwa kanuni thabiti (4 Testimonies, 574).

Tunaweza kufanya kazi ya umishenari wa tiba kwa kula na kunywa kwa utukufu wa Mungu (Manuscript 93, 1901).

Tunaweza kufanya kazi ya umishenari wa tiba kwa kula na kunywa kwa utukufu wa Mungu (Manuscript 93, 1901).

SURA YA 20

MAONI JUU YA MAFUA

KIELELEZO CHA JINSI YA KUKABILIANA NA UGONJWA

Nitakuwa nimefanya jambo lisilo la busara sana kuingia kwenye chumba cha baridi wakati wa jasho; Nitakuwa nimejionyesha kuwa msimamizi asiye na hekima ili kujiruhusu kuketi kwenye unyevunyevu, na hivyo kujiweka wazi ili nipate baridi. Ninapaswa kuwa na busara kuketi na miguu baridi na viungo na hivyo kurudisha damu kutoka mwisho hadi kwa ubongo au viungo vya ndani. Ninapaswa kulinda miguu yangu kila wakati katika hali ya hewa yenye unyevunyevu. . —Counsels on Diet and Foods, 302.

"Ikiwa mtoto amepata mafua, kwa ujumla ni kutokana na usimamizi mbaya wa mama. Ikiwa anafunika kichwa chake, pamoja na mwili wake, wakati wa kulala, kwa muda mfupi atakuwa katika jasho, linalosababishwa na kupumua kwa taabu, kwa sababu ya ukosefu wa hewa safi muhimu. Anapoivuta karibu na nguo, mara zote atapata mafua.”—2 Selected Messages, 469.

"Mikono ikiwa wazi, humsababishia mtoto mchanga kuwa na mafua ya mara kwa mara, na msongamano wa mapafu au ubongo. Hali hizi za mtoto kuwa wazi hutayarisha njia kwa mtoto mchanga kuwa mgonjwa na pia kukosa ukuaji mzuri.” —2 Selected Messages, 469.

"Tunapozichosha nguvu zetu, tunaishiwa nguvu, tunakuwa kwenye hatari ya kupata mafua, na katika nyakati kama hizo kunakuwepo hatari ya kupata magonjwa ya hatari.” —Shuhuda kwa Kanisa 3: 13.

“Watu wengi wangepata faida kutokana na kuoga maji ya baridi au ya vuguvugu kila siku asubuhi au jioni. Badala ya kuongeza riski ya kupata mafua na kikohozi, kuoga, kukifanywa kwa jinsi inavyofaa, huimarisha mwili dhidi ya magonjwa ya baridi kama vile mafua, kikohozi, pnemonia au fundo-fundo (tonsils), kwa sababu huboresha mzunguko wa damu." -Ministry of Healing, 276.

"Nguo hiyo inapaswa kustiri vizuri, na isizuie mzunguko wa damu wala upumuaji.

Miguu inapaswa kulindwa ipasavyo kutokana na baridi na unyevunyevu. Tukiwa tumevaa kwa njia hii, tunaweza kufanya mazoezi katika hewa ya wazi, hata katika umande wa asubuhi na jioni, au baada ya kunyesha kwa mvua au theluji, bila kuhofia kupata mafua.”—Child Guidance, 425.

"Hakuna mtu anayeweza kuwa na nguvu nzuri ya mmeng'enyo na ubongo safi ambaye atakula sana keki zenye sukari na keki zenye malai (cream) na kila aina ya pai,na kula vyakula vya aina nyingi katika mlo mmoja. Tunapofanya hili,na kisha tunapata mafua, mfumo wote unazibwa kabisa na unadhoofishwa kiasi kwamba unakosa nguvu ya kupinga,unakosa nguvu ya kupambana na magonjwa." -Counsels on Diet and Food, 334.

"Wale ambao wamezuia hewa isipite kwenye vyumba vyao vya kulala, wanapaswa kuanza kubadilisha mazoea yao mara moja. Wanapaswa kuruhusu hewa kwa viwango, na kuongeza mzunguko wake hadi waweze kuitumia wakati wa baridi na kiangazi, bila hatari ya kupata mafua. "—Counsels on Health 57- 58.

"Chumba cha wagonjwa, ikiwezekana, kinapaswa kuwa na sehemu inayochuja hewa inayopita, mchana na usiku. Sehemu ya kupitisha hewa haipaswi kugusana na mgonjwa. Wakati homa zinapovuma, kutakuwa na hatari kidogo ya kupata mafua. Lakini umakini zaidi unahitajika wakati tatizo linapokuja, na homa inapokoma."— Counsels on Health, 56.

"Nishati ya umeme wa ubongo, inayozalishwa na shughuli za kiakili, huchangamsha mfumo mzima, na hivyo ni msaada muhimu sana katika kustahimili magonjwa."—Education, 197.

"Mawazo yanafanya kazi; Wanatazamia kupata mafua, na watapata."— Counsels on Health, 97.

"Zalisha nguvu ya fikra, ambayo itastahimili mafua, na itatoa nguvu kwa mfumo wa neva."— Counsels on Health, 54.

"Mazoezi ya asubuhi, kutembea katika anga ya mbinguni iliyotolewa bure, yenye kutia moyo…….. ni kinga ya uhakika dhidi ya mafua, kikohozi, msongamano wa ubongo na mapafu. . na magonjwa mengine mia moja." —Healthful Living, 210.

"Wanywaji wa dawa zenye sumu hawako salama kamwe. Sikuzote wanapata mafua, ambayo husababisha mateso makali, kwa sababu ya sumu katika mifumo yao yote."—Healthful Living, 209.

Watendakazi wamishenari wa tiba wanafanya kazi ambayo ilipuuzwa kwa muda mrefu ambayo Mungu alilipatia kanisa…….. Wanatoa wito wa mwisho wa karamu ambayo Mungu ameiandaa. Shuhuda kwa Kanisa 8:71

SEHEMU YA 7

MUUNDO WA BIBLIA

SURA YA 21

UJUMBE WA AFYA KAMA UNAVYOPATIKANA KATIKA BIBLIA

1- NIA YA MUNGU KUHUSU AFYA YETU

Zaburi 139:13-17 “Maana Wewe Ndiwe uliyeniumba mtima wangu, Uliniunga tumboni mwa mama yangu. Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa Kwa jinsi ya ajabu ya kutisha. Matendo Yako ni ya ajabu, Na nafsi yangu yajua sana, Mifupa yangu haikusitirika kwako, Nilipoumbwa kwa siri, Nilipoungwa kwa ustadi pande za chini za nchi; Macho yako yaliniona kabla sijakamilika; Chuoni Mwako ziliandikwa zote pia, Siku zilizoamriwa kabla hazijawa bado. Mungu, fikira Zako zina thamani nyingi kwangu; Jinsi ilivyo kubwa jumla yake!”

Mathayo 9:35-36 “Naye Yesu alikuwa akizunguka katika miji yote na vijiji, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri habari njema ya ufalme, na kuponya magonjwa yote na udhaifu wa kila aina. Na alipowaona makutano, aliwahurumia, kwa sababu walikuwa wamechoka na kutawanyika kama kondoo wasio na mchungaji.”

3 Yohana 1:2, Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo.

Mathayo 10:8, Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure.

2- SEHEMU YA MWILI KATIKA UTAKASO

Warumi 12:1-2 “Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa

kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu."

1 Wakorintho 6:19-20 "Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu."

2 Wakorintho 7:1 "Basi, wapenzi wangu, kwa kuwa tuna ahadi hizo, na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu."

3- HEKALU LA ROHO LINAPASWA KUWA SAFI

1 Wakorintho 3:16-17 "Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi."

1 Wakorintho 9:25-27 "Na kila ashindanaye katika michezo hujizuia katika yote; basi hao hufanya hivyo kusudi wapokee taji iharibikayo; bali sisi tupokee taji isiyoharibika. Hata mimi napiga mbio vivyo hivyo, si kama asitaye; napigana ngumi vivyo hivyo, si kama apigaye hewa; bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa."

1 Petro 2:11 "Wapenzi, nawasihi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tamaa za mwili zipiganazo na roho."

4- MVINYO ULIOCHACHUSHWA

Mithali 20:1 "Mvinyo hudhihaki, kileo huleta ugomvi; Na akosaye kwa vitu hivyo hana hekima."

Mithali 23:29-32 "Ni nani apigaye, yowe? Ni nani aliaye, Ole? Ni nani mwenye ugomvi? Ni nani mwenye mguno? Ni nani aliye na jeraha zisizo na sababu? Ni nani aliye na macho mekundu? Ni wale wakaao sana kwenye mvinyo; Waendao kutafuta divai iliyochanganyika. Usiitazame mvinyo iwapo ni nyekundu; Iitiapo bilauri rangi yake, ishukapo taratibu; Mwisho wake huuma kama nyoka; Huchoma kama fira."

Isaya 5:11-12 "Ole wao waamkao asubuhi na mapema, wapate kufuata kileo; wakishinda sana hata usiku wa manane mpaka mvinyo imewaka kama moto ndani

yao! Na kinubi, na zeze, na matari, na filimbi, na mvinyo, zote ziko katika karamu zao; lakini hawaiangalii kazi ya Bwana wala kuyafikiri matendo ya mikono yake. (Tazama pia Habakuki 2:5, 15; Waefeso 5:18)

1Wakorintho 6:9-10: Walevi hawataurithi ufalme wa Mungu. Mambo ya Walawi 10:8-11: Haruni asinywe divai.

Ezekieli 44:21: Makuhani hawakupaswa kunywa mvinyo.

Luka 1:15: Maelekezo kwa mama ya Yohana Mbatizaji yalikuwa kwamba asinywe mvinyo.

Mithali 31:4: Wafalme na wakuu hawakupaswa kunywa divai wala mvinyo bali juisi ya mizabibu tu.

Divai Isiyochachushwa: Mwanzo 40:11; Zaburi 104:14-15; Marko 2:22.

5- TUMBAKU, DAWA ZENYE SUMU, NA BIDHAA ZA KAFEINI

Wengine hufasiri Kumbukumbu la Torati 29:18-21 kuwa inarejelea mimea na mizizi inayosababisha “kiu” na “kufanya fikra kuwa na mawazo ya kufikirika-imaginations” (sawa na ile inayotengenezwa na dawa zenye kileo (narcotic), tumbaku, na bidhaa za kafeini).

6 - ULAJI WA MAZAO YA MIMEA AU MBOGAMBOGA

Mwanzo 1:29 Mungu akasema, Tazama, nimewapa kila mche utoao mbegu, ulio juu ya uso wa nchi yote pia, na kila mti, ambao matunda yake yana mbegu; vitakuwa ndivyo chakula chenu”

Mwanzo 3:18 “Michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni”

Mwanzo 9:3 “Kila kiendacho kilicho hai kitakuwa chakula chenu, kama nilivyowapa mboga za majani, kadhalika nawapeni hivi vyote.”

Kutoka 16:35 “Na wana wa Israeli walikula Mana muda wa miaka arobaini, hata walipofikilia nchi iliyo na watu, wakala ile Mana, hata walipofikilia mipakani mwa nchi ya Kanaani.”

Yoshua 5:11-12 “Nao wakala katika mazao ya nchi siku ya pili ya kuiandama hiyo sikukuu ya pasaka, mikate isiyotiwa chachu, na bisi, siku iyo hiyo. Ndipo ile mana ikakoma siku ya pili yake, baada ya wao kuyala hayo mazao ya nchi; na hao wana wa Israeli hawakuwa na mana tena; lakini wakala katika viliwa vya nchi ya Kanaani mwaka huo.”

Danieli 1:8-21: “Mfano wa Danieli na wenzake na jinsi walivyobarikiwa kwa kuwa waaminifu kwa kanuni za kiasi na matengenezo ya afya.”

Mathayo 3:4: Nzige na asali ya mwituni ilikuwa ni chakula cha Yohana Mbatizaji. Inakubaliwa kwa ujumla kwamba "nzige" yalikuwa matunda ya mti wa carob.

7 – ULAJI WA NYAMA

Mwanzo 9:3-5 “Kila kiendacho kilicho hai kitakuwa chakula chenu, kama nilivyowapa mboga za majani, kadhalika nawapeni hivi vyote. Bali nyama pamoja na uhai, yaani, damu yake, msile. Hakika damu yenu ya uhai wenu nitaitaka; na kwa mkono wa kila mnyama nitaitaka; na kwa mkono wa mwanadamu, kwa mkono wa ndugu ya mtu nitataka uhai wa mwanadamu.”

Mwanzo 7:2 “Katika wanyama wote walio safi (wasio najisi) ujitwalie saba saba, mume na mke; na katika wanyama wasio safi wawili wawili, mume na mke.”

Mambo ya Walawi 11 na Kumbukumbu la Torati 14: Orodha ya wanyama, ndege na samaki safi na najisi.

8 - DAMU NA MAFUTA

Mwanzo 9:4 “Bali nyama pamoja na uhai, yaani, damu yake, msile.”

Mambo ya Walawi 3:17 “Neno hili litakuwa amri ya daima, katika vizazi vyenu vyote, ndani ya nyumba zenu zote, ya kwamba hamtakula mafuta wala damu kabisa.”

Mambo ya Walawi 7:23-25 “Nena na wana wa Israeli, uwaambie, Msile mafuta yoyote, ya ng'ombe, wala ya kondoo, wala ya mbuzi. Tena mafuta ya mnyama afaye mwenyewe (kibudu), na mafuta ya mnyama aliyeraruliwa na wanyama, mna ruhusa kuyatumia kwa ajili ya matumizi mengine; lakini msiyale kabisa. Kwani huyo mtu atakayekula mafuta ya mnyama, ambaye ni katika wanyama ambao watu husongeza sadaka kwa Bwana kwa moto, mtu huyo atakayekula mafuta hayo atakatiliwa mbali na watu wake.”

Tazama pia Mambo ya Walawi 17:10-12; Kumbukumbu la Torati 12:23-25; Mambo ya Walawi 10:17-18.

Matendo ya Mitume 15:28-29 “Kwa maana ilimpendeza Roho Mtakatifu na sisi, tusiwatwike mzigo ila hayo yaliyo lazima, yaani, mjiepushe na vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu, na damu, na nyama zilizosongolewa, na uasherati. Mkijizuia na hayo, mtafanya vema. Wasalamu.”

9 - NYAMA YA NGURUWE

Mambo ya Walawi 11:11 Watakuwa machukizo kwenu; msiile nyama yao, na mizoga yao itakuwa machukizo kwenu.

Mambo ya Walawi 11:8 Msiile nyama yao, wala msiiguse mizoga yao; hao ni najisi kwenu.

2 Petro 2:22 “Lakini imetukia kwao sawasawa na ile mithali ya kweli, Mbwa ameyarudia matapiko yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudi kugaa-gaa matopeni.”

Mathayo 7:6 “Msiwape mbwa kilicho kitakatifu, wala msitupe lulu zenu mbele ya nguruwe, wasije wakazikanyaga chini ya miguu yao, wakageuka na kuwararua.”

Isaya 65:3-5 “Watu wanikasirishao mbele za uso Wangu daima, wakitoa dhabihu katika bustani zao, na kufukiza uvumba juu ya matofali; waketio kati ya makaburi, na kulala katika mahali pao pa siri; walao nyama ya nguruwe, na mchuzi wa vitu vinichukizavyo u katika vyombo vyao; watu wasemao, Simama peke yako, usinikaribie Mimi, kwa maana Mimi ni mtakatifu kuliko wewe; watu hao ni moshi puani Mwangu, moto uwakao mchana kutwa.”

Isaya 66:15-17: Uharibifu wa walaji wa nyama ya nguruwe.

10 - MATOKEO YA KULA CHAKULA CHA NYAMA

Mithali 23:20-21 “Usiwe miongoni mwao wanywao mvinyo; Miongoni mwao walao nyama kwa pupa. Kwa maana mlevi na mlafi huingia umaskini, Na utepetevu humvika mtu nguo mbovu.”

1 Samweli 2:12-17, 22: Wana wa Eli, ambao walikula nyama mbichi, walikuwa na uasherati (Tazama Testimonies, Vol. 2; 62, 352, 362).

KABLA YA KULA NYAMA

Adamu ……..930

Sethi …….....912

Enoshi …….. …..905

Kenani ……910

Mahalaleli …….. 895

Yaredi ……..962

Henoko ……365

Methusela ……..969

Lameki ……..777

Nuhu ……950

BAADA YA KULA NYAMA

Shemu ……..600

Arfaksadi ……..438

Sela ……..433

Eberi ……..464

Pelegi ……..239

Reu ……..239

Serugi ……..230

Nahori ……..148

Tera ……..205

Ibrahimu ……..175

Nuhu, kizazi cha kumi, aliishi miaka 20 zaidi ya Adamu; Kizazi cha Nane kiliishi miaka 39 zaidi ya Adamu: Shemu alilelewa kwa lishe ya mboga na aliishi hadi kufikia umri mzuri; Lakini kizazi cha pili baada ya mafuriko kilishuka umri hadi miaka 438; na kizazi cha nane, badala ya kuwa kirefu zaidi kama kabla ya gharika, kilikuwa kifupi zaidi—miaka 148 pekee.

11 - UWIANO, URAHISI, UCHANGAMFU NA KUJIDHIBITI KATIKA KULA

Mithali 15:17 “Chakula cha mboga penye mapendano; Ni bora kuliko ng'ombe aliyenona pamoja na kuchukiana.”

Mithali 17:1 “Afadhali mego kavu pamoja na utulivu, Kuliko nyumba yenye karamu nyingi pamoja na magomvi.”

Mithali 16:32 “Asiye mwepesi wa hasira ni mwema kuliko shujaa; Na mtu aitawalaye roho yake kuliko mtu atekaye mji.”

Mithali 23:1-3 “Utakapoketi kwa chakula pamoja na mtawala, Mwangalie sana yeye aliye mbele yako. Tena ujitie kisu kooni, Kama ukiwa mlafi. Usivitamani vyakula vyake vya anasa; Kwa maana ni vyakula vya hila.”

Mhubiri 10:17 Heri kwako, nchi, mfalme wako akiwa mtoto wa watu, Na wakuu wako hula wakati ufaao, Ili makusudi wapate nguvu, wala si kwa ajili ya ulevi.

Yohana 21:12-13 “Yesu akawaambia, Njoni mfungue kinywa. Wala hakuna mtu katika wale wanafunzi aliyethubutu kumwuliza, U nani wewe? Wakijua ya kuwa ni Bwana. Yesu akaenda akautwaa mkate, akawapa, na samaki vivyo hivyo.”

Mwanzo 25:29-34: “Mfano wa Esau ambaye aliuza haki yake ya mzaliwa wa kwanza kwa sehemu ya chakula.”

Waebrania 12:16-17 “Asiwepo mwasherati wala asiyemcha Mungu, kama Esau, aliyeuuza urithi wake wa mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya chakula kimoja. Maana mwajua ya kuwa hata alipotaka baadaye kuirithi baraka, alikataliwa (maana hakuona nafasi ya kutubu), ijapokuwa aliitafuta sana kwa machozi.”

Warumi 16:18 “Kwa sababu walio hivyo hawamtumikii Bwana wetu Kristo, bali matumbo yao wenyewe; na kwa maneno laini na ya kujipendekeza waidanganya mioyo ya watu wanyofu.”

Asali, Mfano:

Mithali 24:13: Kula kwa sababu ni nzuri.

Mithali 25:16 Je! Umeona asali? Kula kadiri ya kukutosha; Usije ukashiba na kuitapika.

Mithali 25:27-28: Si vizuri kula asali nyingi.

12 – TAMAA YA CHAKULA NA PAMBANO KUU

—KIPIMO CHA MAADILI

Mwanzo 3:1-11: Anguko la Adamu na Hawa lilikuwa katika kipengele cha tamaa ya kula.

Hesabu 11:4-5, 31-33 Tamaa ya Israeli ya nyama na matokeo yake: “Kisha mkutano wa wafuasi waliokuwa waliochanganyika, wakashikwa na tamaa; wana wa Israeli nao wakalia tena, wakasema, Ni nani atakayetupa nyama tule? Twakumbuka samaki tuliokula huko Misri bure; na yale matango, na matikiti, na mboga, na vitunguu vya liki, na vitunguu saumu; Kisha upepo ukavuma kutoka kwa Bwana, nao ukaleta kware kutoka pande za baharini, nao ukawaacha wakaanguka karibu na kambi, kama kiasi cha mwendo wa siku moja upande huu, na kama kiasi cha mwendo wa siku moja upande huu, kuizunguka, nao wakafikia kiasi cha dhiraa mbili juu ya uso wa nchi. Watu wakaondoka mchana huo wote, na usiku huo wote, na siku ya pili yote, kuwakusanya hao kware; yeye aliyepata pungufu kuliko wenziwe alipata kiasi cha homeri kumi; nao wakawaanika wote kando-kando ya kambi kuizunguka pande zote. Kisha hapo hiyo nyama ilipokuwa ikali kati ya meno yao, hawajaitafuna bado, hasira za Bwana ziliwaka juu ya watu, Bwana akawapiga watu kwa pigo kuu mno.

Zaburi 106:14-15: Hali ya kukondeana iliruhusiwa kwenye miili yao kwa sababu ya kula nyama.

Isaya 7:14-15 “Kwa hiyo Bwana Mwenyewe atawapa ishara. Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita Jina Lake Imanueli. Siagi na asali atakula, wakati ajuapo kuyakataa mabaya na kuyachagua mema.

Mathayo 4:1-4- Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi.

Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa.

Mjaribu akamjia akamwambia, Ukiwa Ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate. Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.

Warumi 5:12-19; 1 Wakorintho 15:45-47: Adamu wa pili (Kristo) alishinda pale Adamu wa kwanza alipoanguka.

1 Petro 2:21 Kwa sababu ndio mlioitiwa; maana Kristo Naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuate nyayo Zake.

Mathayo 24:38 Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya Gharika watu walivyokuwa wakila, na kunywa, wakioa na kuolewa, hata siku ile aliyoingia Nuhu katika safina,

Luka 17:26-30: Kula na kunywa hadi kumsahau Mungu kulienea katika siku za Nuhu na Lutu, na itakuwa katika siku za mwisho kabla ya Yesu kuja.

Ezekieli 16:49 -Tazama, uovu wa umbu lako, Sodoma, ulikuwa huu; kiburi, na kushiba chakula, na kufanikiwa, hayo yalikuwa ndani yake na binti zake; tena hakuutia nguvu mkono wa maskini na mhitaji.

Wafilipi 3:18-19 “Maana wengi huenenda, ambao nimewaambieni mara nyingi habari zao, na sasa nawaambia hata kwa machozi, kuwa ni adui za msalaba wa Kristo; mwisho wao ni uharibifu, mungu wao ni tumbo, utukufu wao u katika fedheha yao, waniao mambo ya duniani.”

SURA YA 22

KAZI YA UMISHENARI WA TIBA KAMA INAVYOPATIKANA KATIKA BIBLIA

1- KIELELEZO CHA YESU

Mathayo 4:23-25 “Naye alikuwa akizunguka katika Galilaya yote, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri Habari Njema ya ufalme, na kuponya ugonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu. Na habari Zake zikaenea katika Syria/Shamu yote; wakamletea wote waliokuwa hawawezi, walioshikwa na maradhi mbalimbali na mateso, wenye pepo, na wenye kifafa, na wenye kupooza; akawaponya. Na makutano mengi wakamfuata, kutoka Galilaya, na Dekapoli, na Yerusalemu, na Uyahudi, na ng'ambo ya Yordani.”

Mathayo 8:16-17 “Hata kulipokuwa jioni, wakamletea wengi wenye pepo; akawatoa pepo kwa Neno Lake, akawaponya wote waliokuwa hawawezi, ili litimie lile Neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema, Mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu, Na kuyachukua magonjwa yetu.

Mathayo 9:35-36 “Naye Yesu alikuwa akizunguka katika miji yote na vijiji, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri habari njema ya ufalme, na kuponya magonjwa yote na udhaifu wa kila aina. Na alipowaona makutano, aliwahurumia, kwa sababu walikuwa wamechoka na kutawanyika kama kondoo wasio na mchungaji.”

Mathayo 14:13-14 “Naye Yesu aliposikia; hayo, aliondoka huko katika chombo, akaenda mahali pasipo watu, faraghani. Na makutano waliposikia, walimfuata kwa miguu kutoka mijini mwao. Yesu akatoka, akaona mkutano mkuu, akawahurumia, akawaponya wagonjwa wao.”

Mathayo 15:30-31 “Wakamwendea makutano mengi wakimletea viwete, vipofu, mabubu, vilema, na wengine wengi, wakawaweka miguuni pake; akawaponya; hata ule mkutano wakastaajabu, walipowaona mabubu wanasema, vilema wanakuwa wazima, viwete wanakwenda, na vipofu wanaona; wakamtukuza Mungu wa Israeli.”

Luka 4:17-21 “Akapewa chuo cha nabii Isaya, akakifungua chuo, akatafuta mahali palipoandikwa, Roho wa Bwana yu juu Yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa

kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa, Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa. Akakifunga chuo, akamrudishia mtumishi, akaketi; na watu wote waliokuwamo katika sinagogi wakamkazia macho. Akaanza kuwaambia, Leo Maandiko haya yametimia masikioni mwenu."

Mathayo 11:2-6 "Naye Yohana aliposikia huko gerezani matendo yake Kristo, alituma wanafunzi Wake, kumwuliza, Wewe ndiwe yule ajaye, au tumtazamie mwingine? Yesu akajibu akawaambia, Nendeni mkamweleze Yohana mnayoyasikia na kuyaona; vipofu wanapata kuona, viwete wanakwenda, wenye ukoma wanatakaswa, viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa, na maskini wanahubiriwa habari njema. Naye heri awaye yote asiyechukizwa Nami."

2- AGIZO LA UTUME WA YESU

Mathayo 28:18-20 "Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."

Marko 16:15-20 "Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya. Basi Bwana Yesu, baada ya kusema nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu. Nao wale wakatoka, wakahubiri kotekote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulithibitisha lile Neno kwa ishara zilizofuatana nalo.]"

Mathayo 10:1, 7-8 "Akawaita wanafunzi Wake kumi na wawili, akawapa amri juu ya pepo wachafu, wawatoe, na kupoza magonjwa yote na udhaifu wa kila aina. Na katika kuenenda kwenu, hubirini, mkisema, Ufalme wa mbinguni umekaribia. Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure."

3 – MUNGU PEKEE NDIYE ANAYEWEZA KUPONYA WAGONJWA

Zaburi 103:2, 4-5 "Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana, Wala usizisahau fadhili Zake zote. Aukomboa uhai wako na kaburi, Akutia taji ya fadhili na rehema, Aushibisha mema uzee wako, Ujana wako ukarejezwa kama tai;"

Yeremia 17:14 “Uniponye, Ee Bwana, nami nitaponyeka; uniokoe, nami nitaokoka; kwa maana Wewe Ndiwe uliye sifa zangu.”

Kumbukumbu la Torati 7:15 “Na Bwana atakuondolea ugonjwa wote; wala hatatia juu yako maradhi yoyote mabaya uyajuayo ya Misri, lakini atayaweka juu ya wote wakuchukiao.”

4 - AMINI KATIKA UPENDO WAKE, UTAYARI WAKE NA NGUVU ZAKE

Yohana 10:10 “Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.”

Luka 8:48, 50 “Akamwambia Binti, imani yako imekuponya; enenda zako na amani. Lakini Yesu aliposikia hayo, alimjibu, Usiwe na hofu, amini tu, naye ataponywa.”

Marko 9:23-24 “Yesu akamwambia, Ukiweza! Yote yawezekana kwake aaminiye. Mara babaye yule kijana akapaza sauti, akasema, Naamini, nisaidie kutokuamini kwangu.”

Matendo ya Mitume 3:16 “Na kwa imani katika Jina Lake, Jina Lake limemtia nguvu mtu huyu mnayemwona na kumjua; na imani ile iliyo Kwake Yeye imempatia huyu uzima huu mkamilifu mbele yenu ninyi nyote.”

5 - MTUMAINI MUNGU NA UJISALIMISHE KWA MAPENZI YAKE

Warumi 8:26 Kadhalika Roho Naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho Mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa.

Luka 22:41-43 “Akaenda mbali kidogo nao, kama umbali anaoweza mtu kutupa jiwe, akapiga magoti, akaomba akisema, “Baba, kama ni mapenzi Yako, niondolee kikombe hiki cha mateso. Lakini si kwa mapenzi Yangu, bali mapenzi Yako yafanyike.” Malaika kutoka mbinguni akamtokea, akamtia nguvu.”

Zaburi 37:5-7 “Umkabidhi Bwana njia yako, Pia umtumaini, naye atafanya.

Ataitokeza haki yako kama nuru, Na hukumu yako kama adhuhuri. Ukae kimya mbele za Bwana, Nawe umngojee kwa saburi; Usimkasirikie yeye afanikiwaye katika njia yake, Wala mtu afanyaye hila.”

6- KUUNGAMA DHAMBI

Zaburi 66:18-Kama ningaliwaza maovu moyoni mwangu, Bwana asingesikia.

Zaburi 103:3 Akusamehe maovu yako yote, Akuponye magonjwa yako yote,

Yakobo 5:16 Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii.

Yakobo 5:16-Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii.

1 Yohana 2:1 Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo Mwenye haki,

1 Yohana 1:9 Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.

7 - UTII KWA SHERIA ZA MUNGU 1 WAKORINTHO 6:19-20

Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu.

Kumbukumbu la Torati 28:1-8; Mambo ya Walawi 26: Baraka na laana, magonjwa na afya, huamuliwa na utii wetu.

1 Wakorintho 3:16-17 “Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi.”

Mithali 4:20-22 “Mwanangu, sikiliza Maneno Yangu; Tega sikio lako, uzisikie kauli Zangu. Zisiondoke machoni pako; Uzihifadhi ndani ya moyo wako. Maana ni uhai kwa wale wazipatao, Na afya ya mwili wao wote.”

Kutoka 15:26 akawaambia, Kwamba utaisikiza kwa bidii sauti ya Bwana, Mungu wako, na kuyafanya yaliyoelekea mbele Zake, na kutega masikio usikie maagizo Yake, na kuzishika amri Zake, Mimi sitatia juu yako maradhi yoyote niliyowatia Wamisri; kwa kuwa Mimi Ndimi Bwana nikuponyaye.

Kutoka 23:25 Nanyi mtamtumikia Bwana, Mungu wenu, Naye atakibarikia chakula chako, na maji yako; Nami nitakuondolea ugonjwa kati yako.

8 - TUNAPASWA KUTII SHERIA YAKE

Isaya 1:16, 18 “Jiosheni, jitakaseni; ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho Yangu; acheni kutenda mabaya; Haya, njoni, tusemezane, asema

Bwana. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu.

Yohana 5:14 “Baada ya hayo Yesu akamkuta ndani ya hekalu, akamwambia, Angalia, umekuwa mzima; usitende dhambi tena, lisije likakupata jambo lililo baya zaidi.”

Luka 9:23 “Akawaambia wote, Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate.”

1 Wakorintho 10:31 “Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu.”

Wafilipi 4:13 “Nayaweza mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu.”

Wafilipi 3:13-14 “Ndugu, sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu.”

Waebrania 12:1-4 “Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, tukimtazama Yesu, Mwenye kuanzisha na Mwenye kutimiza imani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu. Maana mtafakarini sana Yeye aliyeyastahimili mapingamizi makuu namna hii ya watendao dhambi juu ya nafsi zao, msije mkachoka, mkizimia mioyoni mwenu. Hamjafanya vita hata kumwagika damu, mkishindana na dhambi”

9 - AHADI KWA WAGONJWA

Isaya 26:3 Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea Katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini.

Isaya 30:15 Kwa maana Bwana MUNGU, Mtakatifu wa Israeli, asema hivi, Kwa kurudi na kustarehe mtaokolewa; nguvu zenu zitakuwa katika kutulia na kutumaini; lakini hamkukubali.

Zaburi 27:14 Umngoje Bwana, uwe hodari, Upige moyo konde, naam, umngoje Bwana.

Kumbukumbu la Torati 33:25 Makomeo yako yatakuwa ya chuma na shaba; Na kadiri ya siku zako ndivyo zitakavyokuwa nguvu zako.

Kumbukumbu la Torati 33:27 Mungu wa milele Ndiye makazi yako, Na mikono ya milele i chini yako. Na mbele yako amemsukumia mbali adui; Akasema, Angamiza.

Yoshua 1:9 Je! Si Mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa Bwana, Mungu wako, Yu pamoja nawe kila uendako.

Zaburi 4:8 Katika amani nitajilaza na kupata usingizi mara, Maana Wewe, Bwana, peke yako, Ndiwe unijaliaye kukaa salama.

Zaburi 17:15 Bali Mimi nikutazame uso wako katika haki, Niamkapo nishibishwe kwa sura yako.

Zaburi 23:4 Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, Sitaogopa mabaya; Kwa maana Wewe upo pamoja nami, Gongo lako na fimbo yako vyanifariji.

Zaburi 27:1 Bwana ni nuru yangu na wokovu wangu, Nimwogope nani? Bwana ni ngome ya uzima wangu, Nimhofu nani?

Zaburi 27:5 Mradi atanisitiri bandani Mwake siku ya mabaya, Atanisitiri katika sitara ya hema Yake, Na kuniinua juu ya mwamba. Zaburi 28:6-7

Na ahimidiwe Bwana. Maana ameisikia sauti ya dua yangu; Bwana ni nguvu zangu na ngao yangu. Moyo wangu umemtumaini, Nami nimesaidiwa; Basi, moyo wangu unashangilia, Na kwa wimbo wangu nitamshukuru.

Zaburi 42:8 Mchana Bwana ataagiza fadhili Zake, na usiku wimbo Wake utakuwa nami, Naam, maombi kwa Mungu aliye uhai wangu.

Zaburi 37:5 Umkabidhi Bwana njia yako, Pia umtumaini, Naye atafanya.

Zaburi 57:1-2-Unirehemu, Ee Mungu, unirehemu mimi, Maana nafsi yangu imekukimbilia Wewe. Nitaukimbilia uvuli wa mbawa zako, Hata misiba hii itakapopita. Nitamwita MUNGU Aliye juu, Mungu anitimiziaye mambo yangu.

Zaburi 61:2-4-Toka mwisho wa nchi nitakulilia nikizimia moyo, Uniongoze juu ya mwamba nisioweza kuupanda. Kwa maana ulikuwa kimbilio langu, Ngome yenye nguvu adui asinipate. Nitakaa katika hema Yako milele, Nitaikimbilia sitara ya mbawa Zako

Zaburi 62:1-2-Nafsi yangu yamngoja Mungu peke yake kwa kimya, Wokovu wangu hutoka Kwake. Yeye tu Ndiye mwamba wangu na wokovu wangu, Ngome yangu, sitatikisika sana.

Zaburi 63:3 Maana fadhili zako ni njema kuliko uhai; Midomo yangu itakusifu.

Zaburi 91: Sura maalum kwa watu wa Mungu wakati wa dhiki. Zaburi 103:13-14

Kama vile baba awahurumiavyo watoto Wake, Ndivyo Bwana anavyowahurumia wamchao. Kwa maana Yeye anatujua umbo letu, Na kukumbuka ya kuwa sisi tu mavumbi.

10 - JE, MUNGU HUWAPONYA WAKRISTO WOTE?

Mathayo 8:14-15: Alimponya mama mkwe wa Petro.

2 Wakorintho 12:7-9: Hakuondoa mwiba wa Paulo katika mwili.

1 Timotheo 5:23: Timotheo alikuwa na shida ya tumbo ya mara kwa mara.

11 – TAHADHARI KUHUSU MIUJIZA

Yohana 10:41: Yohana Mbatizaji hakufanya miujiza.

Mathayo 24:24 Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule.

Ufunuo wa Yohana 16:14 Hizo ndizo roho za mashetani, zifanyazo ishara, zitokazo na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi.

Ufunuo wa Yohana 13:13-14

Naye afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu. Naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya mbele ya huyo mnyama, akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi.

Isaya 8:20 Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na Neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi.

Mathayo 7:21-23 “Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba Yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa

Jina Lako, na kwa Jina Lako kutoa pepo, na kwa Jina Lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu."

12 - MAGONJWA YOTE MARA NYINGI NI MATOKEO YA UVUNJAJI WA SHERIA ZA MUNGU

[1] – MIFANO

1 Samweli 25:38: Nabali alikufa kwa kuogopa matokeo ya dhambi zake dhidi ya wengine.

2 Samweli 12:15 Mtoto wa Daudi akafa kwa sababu ya dhambi ya babaye.

2 Wafalme 5:27: Gehazi akawa mtu mwenye ukoma kwa sababu ya dhambi yake dhidi ya Naamani na Elisha.

2 Mambo ya Nyakati 13:20: Yereboamu alikufa kwa sababu ya maisha yake ya dhambi ya uasi.

2 Mambo ya Nyakati 21:12-19: Yehoramu alikufa kwa sababu ya uongozi wake mwovu.

2 Mambo ya Nyakati 26:21: Uzia akawa mwenye ukoma kwa sababu ya kitendo chake cha kiburi cha uasi dhidi ya Mungu.

Ugonjwa uliwapiga kama hukumu ya kutotii sheria za Mungu (Mambo ya Walawi 26:15-16; Kumbukumbu la Torati 28:15, 21,

22, 27-28, 32-35, 58-63, 65-67; 29:22-23).

[2] - AINA ZA MAGONJWA

Magonjwa ya homa, Malaria/ague au (pengine homa, Mambo ya Walawi 26:16); Majipu yenye kufura na kutumbuka (Kutoka 9:9-10); majipu mabaya (Ayubu 2:7) ; magonjwa ya ngozi (Mambo ya Walawi 21:18-21); upofu (Kumbukumbu la Torati 28:28); Majipu, (Kumbukumbu la Torati 28:27-35); Mikono iliyovunjika, nyayo zilizopinda ndani, kiguu (ugonjwa ambao kisigino, kifundo cha mguu, au vidole kuponda), michubuko, majeraha ya ajali, donda-ndugu, saratani (2 Timotheo 2:17); Kifua kikuu (Mambo ya Walawi 26:16; Kumbukumbu la Torati 28:22); Nundu-nundu/Kibyongo (Mambo ya Walawi 21:20); kuhara damu (Matendo 28:8); pua iliyobonyea (Mambo ya Walawi 21:18); Magonjwa ya tumbo/kuhara (2 Mambo ya Nyakati 21:15, 19); shida ya moyo (halt)

(kiwete) (Luka 14:21; Yohana 5:3); kilema; kutokuwa, kutojiweza, au kutokuwa na nguvu za uzazi. (Yohana 5:3).

Udhaifu: [1] Uchafu wa mwili au unajisi (Mambo ya Walawi 12:2); [3] Ulemavu (Yohana 5:5); [4] Udhaifu wa kiakili na kiroho (Warumi 8:26); Kuvimba (Mambo ya Walawi 13:28: Kumbukumbu la Torati 28:22).

Kisonono au Uzazi-uchafu kutoka kwenye uzazi: [1] Sadaka (Mwanzo 48:6); 2 Kutokwa na damu, (Mambo ya Walawi 15:2; Mathayo 9:20) 3. Aina zingine za kutokwa na usaha au shahawa (Mambo ya Walawi 15:2) Kujikuna (Kumbukumbu la Torati 28:27); Ulemavu (Mambo ya Walawi 21:18; Matendo 3:2): ukoma (Kumbukumbu la Torati 28:35; Kutoka 4:6; 14:34; Mathayo 8:3, 11:15; Luka 7:22: 17:14); Wazimu).

Kumbukumbula Torati 28:28; 1 Samweli 21:15; Mithali 26:18); Ulemavu (Luka 14:21); ajali kubwa; magonjwa ya wanyama (Kutoka 9:1-6); tauni, uwezekano wa homa ya wengu; Kupooza (Mathayo 4:24; Marko 2:1-12); tauni (Yeremia 21:6; Ezekieli 6:11); Kikoko (Mambo ya Walawi 13:2, 6, 7: 14:56; Isaya 3:17; Mambo ya Walawi 21:20; 22:22); Kipwepwe (Mambo ya Walawi 13:30, 35; 14:54).

Milipuko: kiseyeye, pengine kuwasha badala ya kiseyeye (Kumbukumbu la Torati 28:27); Vidonda (Isaya 1:6; Luka 16:20; Ufunuo 16:11); Vidonda, Magonjwa yasababishwayo na mionzi mikali ya jua (2 Wafalme 4:18-32); kunyauka (Maombolezo 4:8; Mathayo 12:10; 1Wafalme 13:4-6); Misuli kulegea na mifupa kupinda; majeraha (Luka 10:34, Zaburi 68:21); minyoo, usaha, na funza (Matendo 12:23; Ayubu 21-25)

Hii ni orodha kamili ya magonjwa yaliyotajwa katika Biblia. Hata hivyo, rejea zilizoorodheshwa si kamili wala si za kina (sio zote).

13 – BIBLIA INASEMA NINI KUHUSU WAGANGA/MADAKTARI

2 Mambo ya Nyakati 16:12 Akashikwa Asa na ugonjwa wa miguu katika mwaka wa thelathini na kenda wa kumiliki kwake; ugonjwa wake ukazidi sana; lakini hakumtafuta Bwana katika ugonjwa wake, bali waganga.

Mathayo 9:12 -Naye aliposikia, aliwaambia, Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi.(Pia Marko 2:17; Luka 5:31).

Marko 5:25-27-Na mwanamke mmoja mwenye kutoka damu muda wa miaka kumi na miwili, na kuteswa mengi kwa mikono ya matabibu wengi, amegharimiwa vitu vyote alivyo navyo, kusimfae hata kidogo, bali hali yake ilizidi kuwa mbaya aliposikia habari za Yesu, alipita katika mkutano kwa nyuma, akaligusa vazi Lake; (pia Luka 8: 43).

Luka 4:23-24-Akawaambia, Hapana shaka mtaniambia mithali hii, Tabibu, jiponye nafsi yako; mambo yote tuliyosikia kwamba yametendeka Kapernaumu, yatende na hapa pia katika nchi Yako Mwenyewe. Akasema, Amin, nawaambia ya kwamba, Hakuna nabii mwenye kukubaliwa katika nchi yake mwenyewe.

Wakolosai 4:14 Luka, yule tabibu mpendwa, na Dema, wanawasalimu.

Ayubu 13:4 Lakini ninyi hubuni maneno ya uongo, Ninyi nyote ni matabibu wasiofaa.

Yeremia 8:22 Je! Hapana zeri katika Gileadi? Huko hakuna tabibu? Mbona, basi, haijarejea afya ya binti ya watu wangu?

14 – MTENGENEZAJI MANUKATO AU FUNDI WA KUTENGENEZA NA KUCHANGANYA DAWA (APOTHECARY)

Katika Biblia, mtengeneza manukato ni sawa na mtu anayeuza madawa ya famasia (druggist).

Kutoka 30:25, 35: Mafuta ya kutiwa matakati na manukato ya uvumba.

"Nawe utayafanya haya yawe mafuta matakatifu ya upako, yenye harufu nzuri, kazi ya fundi wa kutengeneza marhamu; yatakuwa mafuta matakatifu ya upako". Aya hii inaelezea jinsi ya kuchanganya viungo vilivyotajwa awali (manemane, mdalasini, kassia na mwanzi mtamu) na mafuta ya mzeituni ili kupata mafuta matakatifu ya kupaka.

Nawe utatengeneza uvumba wa vitu hivyo, mchanganyo wa viungo, kazi ya fundi wa kutengeneza marhamu, uliotiwa chumvi, safi, na mtakatifu". Hii inaelezea Mungu akimwelekeza Musa kutumia viungo maalum (manemane, mdalasini, kalmu, na uvumba) kutengeneza uvumba maalum wa kuteketezwa katika madhabahu ya uvumba.

Kutoka 37:29 Kisha akayafanya hayo mafuta matakatifu ya kutiwa, na ule uvumba safi wa viungo vya manukato vizuri, kwa kuandama kazi ya mtengezaji manukato.

2 Mambo ya Nyakati 16:14: Kifo cha Asa—alizikwa kwa manukato, manukato yaliyotoka kwa mafundi wa dawa.

Mhubiri 10:1 Mainzi mafu huvundisha marhamu ya mwuza marashi; Kadhalika upumbavu haba ni mzito kuliko hekima na heshima.

15 - MAWAKALA WA TIBA

[1] - DAWA MBALIMBALI

Mithali 17:22 Moyo uliochangamka ni dawa nzuri; Bali roho iliyopondeka huikausha mifupa.

Mithali 20:30 Machubuko ya fimbo husafisha uovu, Na mapigo hufikilia ndani ya mtima (dawa ya kusafisha uovu ndani).

Yeremia 30:13 Hapana mtu wa kukutetea; kwa jeraha yako huna dawa ziponyazo.

Yeremia 46:11 Panda uende Gileadi, ukatwae zeri, Ee binti, bikira wa Misri; unatumia dawa nyingi bure tu; hupati kupona kamwe.

[2] - KIBANDIKO CHA UJIUJI WA DAWA KWENYE NGOZI-MFANO WA KIBANDIKO NI MKAA, UDONGO MFINYAZI, VIAZI NK (POULTICE)

2 Wafalme 20:7 Naye Isaya akasema, Twaeni mkate wa tini. Wakautwaa, wakauweka juu ya jipu, naye akapona.

Isaya 38:21 Maana Isaya amesema, Na watwae mkate wa tini, wakauweke juu ya jipu, naye atapona.

[3] - DAWA ZA KUPAKA JUU YA NGOZI, ZINGINE ZINA MAFUTA (OINTMENTS)

Yeremia 8:22- Je! Hapana zeri katika Gileadi? Huko hakuna tabibu? Mbona, basi, haijarejea afya ya binti ya watu wangu?

Isaya 1:5-6-Mbona mnataka kupigwa hata sasa, hata mkazidi kuasi? Kichwa chote ni kigonjwa, moyo wote umezimia. Tangu wayo wa mguu hata kichwani hamna uzima ndani yake; bali jeraha na machubuko na vidonda vitokavyo usaha; havikufungwa, havikuzongwa-zongwa, wala havikulainishwa kwa mafuta.

Luka 10:33-34-Lakini, Msamaria mmoja katika kusafiri kwake alifika hapo alipo; na alipomwona alimhurumia, akakaribia, akamfunga jeraha zake, akizitia mafuta na divai; akampandisha juu ya mnyama wake, akampeleka mpaka nyumba ya wageni, akamtunza.

Yeremia 51:8- Babeli umeanguka na kuangamia ghafula; mpigieni yowe; twaeni zeri kwa maumivu yake; ili labda apate kuponywa.

[4] - MATIBABU KATIKA KUVUNJIKA MIFUPA

Ezekieli 30:21 Mwanadamu, nimeuvunja mkono wa Farao, mfalme wa Misri, na tazama, haukufungwa ili kuutia dawa, haukuzongwa kwa kitambaa, upate kuwa na nguvu za kushika upanga.

16 - MATUMIZI YA MAJI

[1] - OSHA (KABAKA, KUOSHA)

Zaburi 51:2 Unioshe kabisa na uovu wangu, Unitakase dhambi zangu.

Zaburi 51:7 Unisafishe kwa hisopo nami nitakuwa safi, Unioshe, nami nitakuwa mweupe kuliko theluji

Yeremia 2:22 Maana ujapojiosha kwa magadi, na kujipatia sabuni nyingi, lakini uovu wako umeandikwa mbele zangu, asema Bwana MUNGU.

[2] - OSHA (RACHMATS/REHEMA, KUOSHA)

2 Wafalme 5:10 Naye Elisha akampelekea mjumbe, akisema, Enenda ukaoge katika Yordani mara saba, na nyama ya mwili wako itakurudia, nawe utakuwa safi.

2 Wafalme 5:14 Ndipo akashuka, akajichovya mara saba katika Yordani, sawasawa na neno lake yule mtu wa Mungu; nayo nyama ya mwili wake ikarudi ikawa kama nyama ya mwili wa mtoto mchanga, akawa safi.

Isaya 1:16-17-Jiosheni, jitakaseni; ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho yangu; acheni kutenda mabaya; jifunzeni kutenda mema; takeni hukumu na haki; wasaidieni walioonewa; mpatieni yatima haki yake; mteteeni mjane.

Isaya 4:4 hapo Bwana atakapokuwa ameuosha uchafu wa hao binti za Sayuni na kuisafisha damu ya Yerusalemu kati yake, kwa roho ya hukumu na kwa roho ya kuteketeza.

Mithali 30:12 Kuna kizazi cha watu walio safi machoni pao wenyewe; Ambao hawakuoshwa uchafu wao.

[3] - MAJI KATIKA AGANO LA KALE

Kutoka 23:25 Nanyi mtamtumikia Bwana, Mungu wenu, Naye atakibarikia chakula chako, na maji yako; nami nitakuondolea ugonjwa kati yako.

Ezekieli 36:25 Nami nitawanyunyizia maji safi, nanyi mtakuwa safi; nitawatakaseni na uchafu wenu wote, na vinyago vyenu vyote.

Ezekieli 47:8-9 Maji yanayoponya

[4] - MAJI KATIKA AGANO JIPYA

Matendo ya Mitume 22:16 Basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukiliitia Jina Lake.

1 Wakorintho 6:11 Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu.

Yohana 9:6,7- Alipokwisha kusema hayo, alitema mate chini, akafanya tope kwa yale mate. Akampaka kipofu tope za macho,Kisha akamwambia, “Nenda kanawe uso katika kijito cha Siloamu.” Neno ‘Siloamu’ maana yake ni ‘aliyetumwa.’ Yule kipofu akaenda akanawa na akarudi akiwa anaona!

Ufunuo wa Yohana 7:14 Nikamwambia, Bwana wangu, wajua wewe. Akaniambia, Hao ndio wanatoka katika dhiki ile iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo.

Waefeso 5:26 ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika Neno;

Tito 3:5 si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema Yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu;

Marko 9:41 Kwa kuwa yeyote atakayewanywesha ninyi kikombe cha maji, kwa kuwa ninyi ni watu wa Kristo, amin, nawaambia, hatakosa thawabu yake.

1 Petro 3:20 watu wasiotii hapo zamani, uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja, siku za Nuhu, safina ilipokuwa ikitengenezwa; ambamo ndani yake wachache, yaani, watu wanane, waliokoka kwa maji.

17 - MBOGA ZA KONDENI (HERBS)

Mwanzo 1:29: Mwanadamu alipewa kila mche wa mbegu kwa ajili ya chakula wakati wa uumbaji.

Mwanzo 3:18: Miche ya shambani iliongezwa baada ya dhambi kuingia.

Zaburi 104:14 Mungu huwezesha nyasi kukua na miche kwa ajili ya kumhudumia mwanadamu.

Mithali 27:25 Manyasi huchukuliwa, na majani mabichi huonekana, Na maboga ya milimani hukusanyika.

Luka 11:42 Mafarisayo walitoa zaka juu ya mnanaa, na kila aina ya miche; Hata hivyo waliuacha upendo wa Mungu.

Mathayo 23:23: Waandishi na Mafarisayo walitoa zaka ya mnanaa na bizari na jira; na waliacha mambo muhimu ya sheria.

Warumi 14:2: Mwingine aliye dhaifu hula mboga za kondeni.

Mathayo 15:13: Kila mmea ambao Mungu hajaupanda utang'olewa

Ezekieli 47:12: Matunda kwa ajili ya chakula na majani kwa ajili ya dawa-uponyaji.

Ufunuo 22:2: Majani ya mti kwa ajili ya kuponya mataifa.

Kumbukumbu la Torati 29:18: Isije kuwa na mzizi unaozaa nyongo (mimea yenye sumu).

Ayubu 30:3-4: Ng'oa mboga ya chumvi na mizizi ya mretemu kwa chakula.

Mathayo 7:16 Mtawatambua kwa matunda yao.

18 - MIPANGO YA UTAKASO

Zaburi 51:1-13: Utakaso wa kiroho unaofananishwa na hisopo, kuosha kwa maji. Isaya 1:16: Osha na ufanye usafi.

Mathayo 10:7-8: Waponye wagonjwa, watakase wenye ukoma. 2 Wakorintho 7:1: Tujitakase na uchafu wote wa mwili.

1 Wakorintho 3:16-17: Usitie unajisi Hekalu la Mwili.

Mathayo 17:19-21: Hali zingine huondoka tu kwa maombi na kufunga.

Mathayo 4:1-2: Mfungo wa Kristo kwa siku arobaini mchana na usiku.

Zaburi 107:17-21: Tunateswa kwa sababu ya makosa na maovu: Mungu hutuokoa na shida zetu.

1 Samweli 30:11-12: Wakati wa kufunga, anza kula na mlo mdogo wa matunda.

2 Samweli 16:1-2: Juisi ya zabibu kwa wagonjwa.

Mithali 30:8 Unilishe chakula kilicho kadiri yangu. (chakula kinachofaa kwa wakati ufaao).

Mathayo 12:43-45: Kuhusu mtu aliyekwishatokwa na pepo chafu; Baada ya kupuuza kufanya sehemu yake, pepo saba wabaya zaidi walimwingia.

2 Petro 2:17-22: Wengi hurudi kwenye dhambi zao zinazochafua baada ya kutakaswa.

Mhubiri 3:1, 3: Kuna wakati wa kuponya, wakati wa kuvunjika, na wakati wa kujenga.

19 –NJIA ZA KIBIBLIA ZA KUSAFISHA (KUTAKASA MWILI)

[1] – MAJI

Zaburi 51:7 Unisafishe kwa hisopo nami nitakuwa safi, Unioshe, nami nitakuwa mweupe kuliko theluji

2 Wafalme 5:14 Naamani alijiosha mara saba katika Yordani.

[2] – MIMEA/MICHE(MITISHAMBA)-MBOGA ZA KONDENI-HERBS

Zaburi 51:7: Hisopo sasa inajulikana kuwa mojawapo ya dawa bora za kusafisha damu za.

[3] - MATUNDA

2 Samweli 16: 2 na divai ni kwamba wanywe hao wazimiao nyikani.

Luka 10:34: Mafuta na divai vilimwagika juu ya majeraha. Isaya 38:21; 2 Wafalme 20:7: Dawa ya Mtini uji-uji wake unakandikwa kwenye kidonda (poultice).

20 – MADAKTARI WA BIBLIA (WAJENZI)

[1] – MIMEA NA MAJANI YA KIJANI

Zaburi 104:14; Ezekieli 47:12; Warumi 14:2

[2] – MAFUTA NA MKATE

Luka 10:34; Zaburi 104:14-15

21 -SUMU

Kutoka 20:13: "Usiue."

1 Wakorintho 3:16-17: Tukiliharibu hekalu la miili yetu, Mungu atatuangamiza.

Kumbukumbu la Torati 27:24-25;

Mithali 6:16- 17: Alaaniwe anayempiga jirani yake.

Mwanzo 9:5: Mungu atahitaji damu ya uhai wako mikononi mwa kila mnyama.

Hesabu 35:16-18: Muuaji hakika atauawa.

Habakuki 2:12 Ole wake yeye ajengaye mji kwa damu, awekaye imara mji mkubwa kwa uovu!

Ezekieli 22:8-9: Watu huzungumzia hekaya nyingi zinazosababisha kumwaga damu.

22 - MKAA

Isaya 61:3: Mafuta mwilini ukiwa na afya njema na furaha.

Esta 4:1-3; Ayubu 2:8; 30:19; 42:6; Isaya 58:5; 61:3; Danieli 9:3;

Yona 3:6; Yeremia 6:26; Maombolezo 3:16, 28: Majivu juu ya mwili wakati wa ugonjwa au wa kukosa furaha.

Zaburi 102:9; Isaya 44:20: Kula majivu ukiwa huna furaha.

Waebrania 9:13; Hesabu 19:17, 19. Tazama pia Mambo ya Walawi 1:16; 4:12; 6:10, 11; 1 Wafalme 13:3, 5. Majivu yanayotumika kwa utakaso

SURA YA 23

VISA VYA UMISHENARI WA AFYA NA TIBA KATIKA BIBLIA

1- Mwanzo 1-2: chakulaLishe/ inayotolewa na Mungu ni chakula/Lishe wa asili.

2- Mwanzo 2: Kazi ya awali.

3- Mwanzo 3: Kipengele ambacho mwanadamu aliangukia.

4- Mwanzo 6:9; Mathayo 24:38; Luka 17:26-30: Kwa nini gharika ilikuja.

5- Mwanzo 18-19; Ezekieli 16:49; Luka 17:26-30: Dhambi ya Sodoma ni dhambi ya zama zetu.

6- Mwanzo 27; Waebrania 12:16-17: Udhaifu wa Esau, mtu aliyethamini chakula kuliko Mungu.

7- Kutoka 16; Yoshua 5:11-12; Zaburi 78:25; Nehemia 9:15: Chakula sahili ambacho Mungu alitoa ili kumtayarisha mwanadamu kwa ajili ya Kanaani— chakula ambacho malaika hutoa.

8- Kutoka 25:8; 1 Wakorintho 3:16-17; 6:19-20: “Na wanifanyie mahali Patakatifu ili nipate kukaa kati yao.”

9- Kutoka 32: Kuabudu ndama wa dhahabu huongoza kwenye kifo.

10- Mambo ya Walawi 1-9: Matoleo ya Patakatifu.

11- Mambo ya Walawi 11; 7:23-27; Kumbukumbu la Torati 14: Sheria za Chakula Safi zilizotolewa na Mungu. Mungu anataka watu Wake waishi safi-bila taka, au mawaa.

12- Mambo ya Walawi 12-20: Usiguse kilicho najisi. Sheria za usafi.

13 - Hesabu 11:4-33; Zaburi 106:14-15: Somo la kware, kuasi mpango wa Mungu.

14 - Hesabu 21; Yohana 3:14-15; Kumbukumbu la Torati 30:19-20: Nyoka wa shaba.

15- Kumbukumbu la Torati 28; Mambo ya Walawi 26: Baraka na Laana. Utii pekee huleta afya. 16 - 1 Samweli 2:12-17, 22: wana wa Eli, wana wa Beliali.

17- Waamuzi 13-16: Udhaifu wa Samsoni ulikuwa ni ukosefu wa kujidhibiti-nafsi.

18- 1 Wafalme 11: **Anguko la Sulemani**. Katika Jarida la Afya la Pasifiki, "Ukengeufu wa Solomon," Agosti 1889, E.G. White anaeleza jinsi anguko la Sulemani lilivyokuja katika hatua tatu:

1. kula mlo wa tatu; 2. Vinywaji vyenye kileo; 3. mitala-wake wengi. "Ilikuwa desturi kwa Waebrania kula lakini mara mbili kwa siku, mlo wao walioupenda zaidi haukuzidi masaa ya katikati ya mchana."

19- 1 Wafalme 17-21: Mlo wa unyakuo-Mlo kabla ya kutwaliwa kwenda mbinguni. (mfano wa Eliya).

20- 2 Wafalme 2:19-22: Kusafisha chemchemi na uponyaji kupitia mawakala rahisi ya asili.

21- 2 Wafalme 5:5-15: Kutakaswa kwa Naamani ni somo katika njia ya Mungu ya uponyaji.

22- Esta: Kula na kufunga wakati wa Esta na Ahasuero.

23- Isaya 58: Ujumbe wa Mungu kwa Kanisa Lake la Masalia.

24- Isaya 65:3-5; Isaya 66:15-17; Isaya 33:14-17: Matengenezo ya Afya Wakati wa Ujio wa Pili.

25 - Ufunuo 22:1-3; Isaya 33:24; 35:5,6,10: Matengenezo ya afya yanafanywa mbinguni.

26- Ezekieli 47: Maji ya Uponyaji.

27- Danieli 1: Tuthibitishie sasa. Kuthubutu kuwa na ujasiri wa Daniel na lishe ya Danieli.

28- Mathayo 4:1-4; Luka 4:1-4; 1 Wakorintho 15:45-47; Warumi 5:12-19: Majaribu ya Yesu.

29- Luka 4:17-21: Utume wa Yesu; Kazi ambayo Mungu alimpa Mwanawe.

30- Mathayo 4:23-25; 8:16-17; 9:35-36; 14:13-14; 15; Warumi 5:12-19: Mfano wa Yesu.

31- Luka 11; Isaya 61: Kwa nini Yesu alitumwa.

32- Mathayo 11:2-6; Huduma ya Uponyaji 34-37: Sifa za Yesu-Jesus Credentials.

33- Mathayo 10: Utume la Kwanza.

34- Mathayo 28:18-20; Marko 16:15-20: Agizo Kuu kwa wafuasi wote wa Yesu.

35- Luka 10: Msamaria Mwema.

36- Yohana 6:13; Mathayo 26; Luka 22; Marko 14; 1 Wakorintho 11: Wewe ni kile unachokula, kimwili na kiroho.

37- Matendo 3: Kukaa katika hatua za Mwalimu.

38- 1 Wakorintho 5: Usafi kati ya watu wa Mungu.

39- Yakobo: Barua kwa Masalia.

SURA YA 24

MAANDISHI YA UMISHENARI WA AFYA NA TIBA

YALIYOPANGWA KULINGANA NA KITABU

MWANZO

Mwanzo 1:29: Mlo wa asili.

Mwanzo 3:1-3, 6, 11: Anguko lilikuwa kwa sababu ya tamaa ya kula na kuchagua mlo wa mtu mwenyewe.

Mwanzo 3:18: Mlo baada ya dhambi.

Mwanzo 7:2: Wanyama safi na najisi waliingia ndani ya safina. Mwanzo Mwanzo 9:3-6: Mlo baada ya gharika.

Mwanzo 25:29-34: Esau anauza haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Mwanzo 48:15: Ibrahimu na chakula kilichotolewa na Mungu.

KUTOKA

Kutoka 16:4, 25: Mlo wa jangwani.

Kutoka 22:31: Kutokula wanyama waliokufa au waliooza.

Kutoka 23:25: Watumishi watiifu wa Mungu wangebarikiwa, chakula chao na magonjwa yangeondolewa.

MAMBO YA WALAWI

Kutoka 3:17: Hakuna mafuta wala damu iliyopaswa kuliwa.

Kutoka 7:23-27: Kutokula mafuta au damu (marejeleo bora juu ya hili).

Kutoka 10:8-11: Haruni na makuhani kutokunywa vinywaji vikali.

Kutoka 11:2-47 (hasa 7-8): wanyama safi na wasio safi.

Kutoka 15:2-13: “Mfano wa maji kama wakala wa utakaso katika kuondoa magonjwa.

Kutoka 17:10, 12, 15: haramu kula damu.

Kutoka 26:3-6, 9-10, 14:16, 20-21, 25-26, 36-39, 46: Afya ya kiakili,

kimwili, na kimaadili inatokana na utii wa sheria za Mungu.

HESABU

Hesabu 11:4-5, 31, 33: Kipindi cha kware kiliwarudisha kwenye chakula cha nyama na kuwaletea magonjwa na kifo.

Hesabu 12:13-15: Uponyaji wa Bwana wakati mwingine huahirishwa hadi somo liweze kueleweka-watu wapate elimu.

Hesabu 19:9, 17-18: Maji ya mkaa yalitolewa kama wakala wa utakaso.

KUMBUKUMBU LA TORATI

Kumbukumbu 7:15 Bwana ataondoa magonjwa yote kutoka kwa watu Wake watiifu na kuyaweka juu ya adui zao.

Kumbukumbu 8:1-3: Mlo wa pekee wa Mungu wa nyikani kwa watu Wake ulikuwa mtihani wa kutakasa.

Kumbukumbu 12:23-25: Watu wake hawakupaswa kula damu.

Kumbukumbu 14:3-20: Wanyama safi na najisi.

Kumbukumbu 8:1-67: Afya ya kiakili, kimwili, kiadili inatokana na utii wa sheria zote za Mungu.

Kumbukumbu 29:18-22: Laana juu ya wale wanaoongeza ulevi kwenye kiu.

Kumbukumbu 33:25-27: Ahadi:

“Kumbukumbu la Torati 33:25 Ahadi, Na kadiri ya siku zako ndivyo zitakavyokuwa nguvu zako.

JOSHUA

Yoshua 1:9 Ahadi "Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa Bwana, Mungu wako, Yu pamoja nawe kila uendako."

Yoshua 4:11-12; 5:11-12: Mana iliisha walipoingia Kanaani; Mwaka huo walikula matunda ya nchi.

I SAMWELI

1 Samweli 2:12-17, 22: Matokeo ya mlo wa nyama mbichi. 30:11-12: Mlo rahisi wakati baada ya mfungo.

2 SAMWELI

2 Samweli 16:1-2: Juisi ya zabibu wakati wa ugonjwa.

1 WAFALME

1 Wafalme 17:4, 6, 12; 19:4-8: Mlo endelevu wa Eliya.

2 WAFALME

2:19-22: Chumvi kama wakala wa utakaso.

5:10-11, 14: Uponyaji wa Naamani ulikuwa kupitia imani na matumizi ya maji.

20:1-11 (hasa 7): Uponyaji wa Hezekia ulikuwa kwa njia ya maombi na dawa ya kibandiko cha mtini -tunda la mkuyu.

2 MAMBO YA NYAKATI

1 Mambo ya Nyakati 16:12-13: Asa aliwatafuta waganga kuliko Bwana.

ZABURI

Zaburi 4:8: Ahadi ya amani na usingizi.

Zaburi 17:15: Ahadi ya kuridhika inapoamshwa.

Zaburi 21:4: Ahadi ya zawadi ya uzima.

Zaburi 23:4: Ahadi ya ulinzi hata katika bonde la uvuli wa mauti.

Zaburi 27:1-5: Ahadi ya nguvu kwa kumngoja Bwana.

Zaburi 28:6-7: Ahadi "Na ahimidiwe Bwana. Maana ameisikia sauti ya dua yangu; Bwana ni nguvu zangu na ngao yangu.

Zaburi 37:5, 7: Ahadi ya mwongozo na kufundishwa ikiwa njia zetu zimewekwa kwa Bwana.

Zaburi 42:8: Ahadi ya upendo wa Mungu mchana na wimbo usiku.

Zaburi 51:2-7 (1-13): Mimea ya mbogamboga za makondeni na maji kama mawakala wa utakaso.

Zaburi 61:2-3: Ahadi "Toka mwisho wa nchi nitakulilia nikizimia moyo, Uniongoze juu ya mwamba nisioweza kuupanda. Kwa maana ulikuwa kimbilio langu, Ngome yenye nguvu adui asinipate."

Zaburi 62:1-2: Nafsi yangu inamngoja Mungu, Yeye ndiye mwamba wangu, wokovu, na ulinzi.

Zaburi 63:3: “Kwa sababu fadhili zako ni bora kuliko uzima.”

Zaburi 66:18 Kama ningaliwaza maovu moyoni mwangu, Bwana asingesikia.

Zaburi 90:12 Basi, utujulishe kuzihesabu siku zetu, Tujipatie moyo wa hekima.

Zaburi 91:1, 11-16 Aketiye mahali pa siri pake Aliye juu Atakaa katika uvuli wake Mwenyezi. Kwa siku nyingi nitamshibisha, Nami nitamwonyesha wokovu wangu.

Zaburi 103:2-3 Akusamehe maovu yako yote, Akuponya magonjwa yako yote,

Zaburi 103:13-14 Kama vile baba awahurumiavyo watoto wake, Ndivyo Bwana anavyowahurumia wamchao. Kwa maana Yeye anatujua umbo letu, Na kukumbuka ya kuwa sisi tu mavumbi.

Zaburi 104:14 Huyameesha majani kwa makundi, Na maboga kwa matumizi ya mwanadamu; Ili atoe chakula katika nchi,

Zaburi 104:15 Na divai imfurahishe mtu moyo wake. Aung'aze uso wake kwa mafuta, Na mkate umburudishe mtu moyo wake.

Zaburi 106:14 Bali walitamani sana jangwani, Wakamjaribu Mungu nyikani.

107:17-21: Ugonjwa unatokana na kutotii; Bwana atasaidia ikiwa ataitwa.

Zaburi 111:5 Amewapa wamchao chakula; Atalikumbuka agano Lake milele.

Zaburi 116:3-8: Kukombolewa na huzuni za mauti kama tokeo la kumwita Bwana.

Zaburi 136:25 Kila chenye mwili akipa chakula chake; Kwa maana fadhili Zake ni za milele.

Zaburi 139:14 Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa Kwa jinsi ya ajabu ya kutisha. Matendo Yako ni ya ajabu, Na nafsi yangu yajua sana,

Zaburi 145:15 Macho ya watu wote yakuelekea Wewe, Nawe huwapa chakula chao wakati wake.

Zaburi 147:9 Humpa mnyama chakula chake, Wana-kunguru waliao.

Zaburi 4:20 Mwanangu, sikiliza Maneno yangu; Tega sikio lako, uzisikie kauli Zangu.

MITHALI

Mithali 15:17 Chakula cha mboga penye mapendano; Ni bora kuliko ng'ombe aliyenona pamoja na kuchukiana.

Mithali 16:32 Asiye mwepesi wa hasira ni mwema kuliko shujaa; Na mtu aitawalaye roho yake kuliko mtu atekaye mji.

Mithali 17:1 “Afadhali mego kavu pamoja na utulivu, Kuliko nyumba yenye karamu nyingi pamoja na magomvi.

Mithali 17:22 Moyo uliochangamka ni dawa nzuri; Bali roho iliyopondeka huikausha mifupa.

Mithali 20:1 Mvinyo hudhihaki, kileo huleta ugomvi; Na akosaye kwa vitu hivyo hana hekima.

Mithali 20:30 Machubuko ya fimbo husafisha uovu, Na mapigo hufikilia ndani ya mtima.

Mithali 23:3 Usivitamani vyakula vyake vya anasa; Kwa maana ni vyakula vya hila.

Mithali 23:20-21 Usiwe miongoni mwao wanywao mvinyo; Miongoni mwao walao nyama kwa pupa.

Kwa maana mlevi na mlafi huingia umaskini, Na utepetevu humvika mtu nguo mbovu.

Mithali 23:29-32 Ni wale wakaao sana kwenye mvinyo; Waendao kutafuta divai iliyochanganyika.

Mithali 24:13 Mwanangu, ule asali, kwa maana ni njema, Na sega la asali lililo tamu ulionjapo.

Mithali 25:16, 27 Haifai kula asali nyingi mno; Vile vile mtu kutafuta utukufu wake mwenyewe si utukufu.

Mithali 25:28 Asiyetawala roho yake Ni mfano wa mji uliobomolewa, usio na kuta.

Mithali 27:25 Mboga za kondeni, na nyasi (herbs) hukusanywa, na majani mabichi huonekana, Na maboga ya milimani hukusanyika.

Mithali 27:27 Tena yatakuwapo maziwa ya mbuzi, Ya kukutosha kwa chakula chako, Na chakula cha watu wa nyumbani mwako, Na posho la vijakazi vyako.

Mithali 30:8 Uniondolee ubatili na uongo; Usinipe umaskini wala utajiri; Unilishe chakula kilicho kadiri yangu.

Mithali 30:12 Kuna kizazi cha watu walio safi machoni pao wenyewe; Ambao hawakuoshwa uchafu wao.

MHUBIRI

Mhubiri-3:1-3 Kwa kila jambo kuna majira yake, Na wakati kwa kila kusudi chini ya mbingu. Wakati wa kuzaliwa, na wakati wa kufa; Wakati wa kupanda, na wakati wa kung'oa yaliyopandwa; Wakati wa kuua, na wakati wa kupoza; Wakati wa kubomoa, na wakati wa kujenga;

Mhubiri-10:1 Mainzi mafu huvundisha marhamu ya mwuza marashi; Kadhalika upumbavu haba ni mzito kuliko hekima na heshima.

Mhubiri-10:17 Heri kwako, nchi, mfalme wako akiwa mtoto wa watu, Na wakuu wako hula wakati ufaao, Ili makusudi wapate nguvu, wala si kwa ajili ya ulevi.

ISAYA

Isaya-1:5-6 Mbona mnataka kupigwa hata sasa, hata mkazidi kuasi? Kichwa chote ni kigonjwa, moyo wote umezimia. Tangu wayo wa mguu hata kichwani hamna uzima ndani yake; bali jeraha na machubuko na vidonda vitokavyo usaha; havikufungwa, havikuzongwa-zongwa, wala havikulainishwa kwa mafuta.

Isaya- 1:16-17 Jiosheni, jitakaseni; ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho yangu; acheni kutenda mabaya; jifunzeni kutenda mema; takeni hukumu na haki; wasaidieni walioonewa; mpatieni yatima haki yake; mteteeni mjane.

Isaya- 5:11 Ole wao waamkao asubuhi na mapema, wapate kufuata kileo; wakishinda sana hata usiku wa manane mpaka mvinyo imewaka kama moto ndani yao!

Isaya- 7:14-15: Imanueli kula siagi na asali.

Isaya- 26:3 Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea Katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini.

Isaya- 30:15 Kwa maana Bwana MUNGU, Mtakatifu wa Israeli, asema hivi, Kwa kurudi na kustarehe mtaokolewa; nguvu zenu zitakuwa katika kutulia na kutumaini; lakini hamkukubali.

Isaya-33:14-17: Wakati wa taabu, mkate na maji yetu yatakuwa hakika.

Isaya- 35:8 Na hapo patakuwa na njia kuu, na njia, nayo itaitwa, Njia ya utakatifu; wasio safi hawatapita juu yake; bali itakuwa kwa ajili ya watu hao; wasafirio, wajapokuwa wajinga, hawatapotea katika njia hiyo.

Isaya- 38:1-8, 21:

Isaya 38:21 Maana Isaya amesema, Na watwae mkate wa tini, wakauweke juu ya jipu, naye atapona.

Isaya- 52:11 Nendeni zenu, nendeni zenu, tokeni huko, msiguse kitu kichafu; tokeni kati yake; iweni safi ninyi mnaochukua vyombo vya Bwana.

Isaya-55:2 Kwani kutoa fedha kwa ajili ya kitu ambacho si chakula? Na mapato yenu kwa kitu kisichoshibisha? Nisikilizeni kwa bidii, mle kilicho chema, Na kujifurahisha nafsi zenu kwa unono.

Isaya- 61:1: "Roho wa Bwana juu yangu," utume wa Kristo, kazi ya ustawi.

Isaya- 61:3: Uzuri kwa majivu, mafuta ya furaha kwa maombolezo.

Isaya- 65:3-5: Kula nyama ya nguruwe na mchuzi wa vitu vya kuchukiza (siku za mwisho).

Isaya- 65:21-25: Maelezo ya mbinguni.

Isaya-66:15-17: Wale wanaokula nyama ya nguruwe na panya watauawa.

Isaya-66:20-22: Waleteni ndugu zako wote mbele za Bwana kwa ajili ya sadaka.

YEREMIA

Yeremia-2:22 Maana ujapojiosha kwa magadi, na kujipatia sabuni nyingi, lakini uovu wako umeandikwa mbele Zangu, asema Bwana MUNGU.

Yeremia-8:22 Je! Hapana zeri katika Gileadi? Huko hakuna tabibu? Mbona, basi, haijarejea afya ya binti ya watu Wangu?

Yeremia- 17:14 Uniponye, Ee Bwana, nami nitaponyeka; uniokoe, nami nitaokoka; kwa maana Wewe Ndiwe uliye sifa zangu.

Yeremia- 30:13 Hapana mtu wa kukutetea; kwa jeraha yako huna dawa ziponyazo.

Yeremia- 46:11 "Panda uende Gileadi, ukatwae zeri, Ee binti, bikira wa Misri; unatumia dawa nyingi bure tu; hupati kupona kamwe.

51:8 Babeli umeanguka na kuangamia ghafula; mpigieni yowe; twaeni zeri kwa maumivu yake; ili labda apate kuponywa.

EZEKIELI

Ezekieli-4:16-17 Tena akaniambia, Mwanadamu, tazama, nitalivunja tegemeo la chakula katika Yerusalemu; nao watakula mkate kwa kuupima, na kwa kuutunza sana; nao watakunywa maji kwa kuyapima, na kwa kushangaa; wapate kupungukiwa na mkate na maji, na kustaajabiana, na kukonda kwa sababu ya uovu wao.

Ezekieli- 5:16 hapo nitakapopeleka mishale mibaya ya njaa juu yao, iletayo uharibifu, nitakayoipeleka ili kuwaharibu ninyi; Nami nitaiongeza njaa juu yenu, na tegemeo lenu la mkate nitalivunja.

Ezekieli- 14:13 Mwanadamu, nchi itakapofanya dhambi na kuniasi, kwa kukosa, nikaunyosha mkono wangu juu yake, na kulivunja tegemeo la chakula chake, na kuipelekea njaa, na kukatilia mbali mwanadamu na mnyama;

Ezekieli- 16:4 Na katika habari za kuzaliwa kwako, siku ile uliyozaliwa, kitovu chako hakikukatwa, wala hukuoshwa kwa maji usafishwe; hukutiwa chumvi hata kidogo, wala hukutiwa katika nguo kabisa.

Ezekieli- 16:49 Tazama, uovu wa umbu lako, Sodoma, ulikuwa huu; kiburi, na kushiba chakula, na kufanikiwa, hayo yalikuwa ndani yake na binti zake; tena hakuutia nguvu mkono wa maskini na mhitaji.

Ezekieli- 30:21 Mwanadamu, nimeuvunja mkono wa Farao, mfalme wa Misri, na tazama, haukufungwa ili kuutia dawa, haukuzongwa kwa kitambaa, upate kuwa na nguvu za kushika upanga.

Ezekieli-36:25 Nami nitawanyunyizia maji safi, nanyi mtakuwa safi; nitawatakaseni na uchafu wenu wote, na vinyago vyenu vyote.

Ezekieli- 44:21 Wala kuhani awaye yote hatakunywa mvinyo, aingiapo katika ua wa ndani.

Ezekieli- 47:8-12: Maji ya kuponya kutoka Patakatifu ili kuponya bahari na samaki.

Ezekieli 47:12 Na karibu na mto, juu ya ukingo wake, upande huu na upande huu, utamea kila mti wa chakula, ambao majani yake hayatanyauka, wala matunda yake hayatatindika kamwe; utatoa matunda mapya kila mwezi, kwa sababu maji

yake yanatoka mahali patakatifu; na matunda yake yatakuwa ni chakula; na majani yake yatakuwa ni dawa.

DANIELI

Danieli- 1:3-2:1: Utii wa chakula wa Danieli na matokeo yake.

HOSEA

Hosea-4:6 Watu Wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa; kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa;

MIKA

Mika 6:12 Kwa maana matajiri wake wamejaa jeuri, na wenyeji wake wamesema uongo, na ulimi wao una udanganyifu kichwani mwao.

HABAKUKI

Habakuki 2:5, 15: “Naam, nao, kwa sababu yeye hukosa kwa divai.”

MALAKI

Malaki-4:5-6 Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya Bwana, iliyo kuu na kuogofya. Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga dunia kwa laana.

MATHAYO

Mathayo-3:4: Mlo wa Yohana: Nzige na Asali.

Mathayo-3:10 basi kila mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa motoni.

Mathayo-4:1-4 Kisha Yesu akaongozwa kwenda nyikani, ambapo alifunga siku 40.

Mathayo- 4:23-25: Yesu akaenda Galilaya, akifundisha na kuponya.

Mathayo-6:11 Utupe leo riziki yetu.

Mathayo- 7:16 Mtawatambua kwa matunda yao.

Mathayo- 8:2,3Na tazama, akaja mtu mwenye ukoma akamsujudia, akisema, Bwana, ukitaka, waweza kunitakasa.

Mathayo- 8:7, 13: Uponyaji wa mtumishi wa akida.

Mathayo-8:14-15: Mama mkwe wa Petro aliponywa.

Mathayo-8:16-17: Usiku ulipofika, Yesu aliponya na kutoa pepo.

Mathayo- 9:12 Naye aliposikia, aliwaambia, Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi.

Mathayo-9:35-36: Yesu akaenda akifundisha, akihubiri na kuponya.

Mathayo- 10:1, 5, 7-8: alipowaita wanafunzi 12 (utume wa kwanza).

Mathayo- 11:3 Je, Wewe Ndiwe Yule ajaye, au tumtazamie mwingine? 12:43-45: Wakati pepo mchafu anapomtoka mtu.

14:13-14 Yesu akaondoka, watu wakamfuata; Yesu alipona mgonjwa.

15:13 Akajibu, akasema, Kila pando asilolipanda Baba yangu wa mbinguni litang'olewa.

15:30-31: Viwete, vipofu, bubu, vilema, na wengine waliponywa.

24:24 Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule.

24:37-38: “Kama siku za Nuhu zilivyokuwa, ndivyo pia ujio wa Mwana wa Adamu utakavyokuwa.”

26:26-29: Yesu akatwaa mkate na kikombe.

26:42 Akaenda tena mara ya pili, akaomba, akisema, Baba Yangu, ikiwa haiwezekani kikombe hiki kiniepuke nisipokunywa, mapenzi Yako yatimizwe.

28:18-20 Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.

MARKO

Marko-5:22-23: Binti Yairo.

Marko-5:27-29: Yesu aliponya suala la damu.

Marko-6:13 Wanafunzi walitoa pepo wengi, wakawapaka wagonjwa mafuta.

Marko-9:23 Yesu akamwambia, Ukiweza! Yote yawezekana kwake aaminiye.

Marko- 9:50 Chumvi ni njema; lakini chumvi ikiwa si chumvi tena, mtaitia nini ikolee? Mwe na chumvi ndani yenu, mkakae kwa amani ninyi kwa ninyi.

Marko- 16:17 Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;

LUKA

Luke-1:15 Kwa sababu atakuwa mkuu mbele za Bwana; hatakunywa divai wala kileo; naye atajazwa Roho Mtakatifu hata tangu tumboni mwa mamaye.

Luke- 4:23 Tabibu, jiponye nafsi yako;

Luke-8:43-44: Suala la kutokwa damu miaka 12; kuponywa na Yesu.

Luke-8:48 Akamwambia Binti, imani yako imekuponya; enenda zako na amani.

Luke-9:23 Akawaambia wote, Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate.

Luke-10:33-34: Msamaria fulani alimwona, akaenda, akafunga majeraha yake.

Luke-11:34-36: “Nuru ya mwili ni jicho.”

Luke- 11:42 Lakini, ole wenu, Mafarisayo, kwa kuwa mwatoa zaka za mnanaa na mchicha na kila mboga, na huku mwaacha mambo ya adili, na upendo wa Mungu; iliwapasa kuyafanya hayo ya kwanza, bila kuyaacha hayo ya pili.

Luke-17:12-19: Mkoma mmoja alirudi kumshukuru Yesu.

Luke- 17:26 Na kama ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika siku zake Mwana wa Adamu.

Luke 22:42 akisema, Ee Baba, ikiwa ni mapenzi Yako, uniondolee kikombe hiki; walakini si mapenzi yangu, bali Yako yatendeke.

YOHANA

Yohana-5:14 Baada ya hayo Yesu akamkuta ndani ya hekalu, akamwambia, Angalia, umekuwa mzima; usitende dhambi tena, lisije likakupata jambo lililo baya zaidi.

Yohana -6:5 Basi Yesu alipoinua macho yake akaona mkutano mkuu wanakuja kwake, alimwambia Filipo, Tununue wapi mikate, ili hawa wapate kula?

Yohana -6:23-40: Mkate wa uzima—mkate ulio hai.

Yohana -8:11 Akamwambia, Hakuna, Bwana. Yesu akamwambia, Wala mimi sikuhukumu. Enenda zako; wala usitende dhambi tena.]

Yohana -9:6-7, 11: Udongo wa mfinyanzi juu ya macho ya kipofu; Alioshwa kwenye Dimbwi la Siloamu.

Yohana -10:10 Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.

Yohana -21:12-13: Yesu anawapa mkate na samaki.

MATENDO YA MITUME

Mdo-3:16 Imani kwa Jina Lake ilimfanya awe na nguvu.

Mdo-15:28-29: “Wajiepushe na nyama zinazotolewa kwa sanamu na damu.”

WARUMI

Warumi-5:12-19: “Kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni . . ”

Warumi-8:26 Kadhalika Roho Naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho Mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa.

Warumi-Warumi-12:1-2 Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma Zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.

Warumi-14:2 Mtu mmoja anayo imani, anakula vyote; lakini yeye aliye dhaifu hula mboga.

Warumi-14:14 Najua, tena nimehakikishwa sana katika Bwana Yesu, ya kuwa hakuna kitu kilicho najisi kwa asili yake, lakini kwake yeye akionaye kitu kuwa najisi, kwake huyo kitu kile ni najisi.

1 WAKORINTHO

1 Wakorintho-3:16 Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?

1 Wakorintho-6:11 Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika Jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu.

1 Wakorintho-6:9 Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu? Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti,

1 Wakorintho-6:19-20: “Mwili wako ni hekalu la Roho Mtakatifu.”

1 Wakorintho-9:25-27: Uwe mwenye kiasi katika mambo yote—ili kupata taji.

1 Wakorintho-10:23 Vitu vyote ni halali; bali si vitu vyote vifaavyo. Vitu vyote ni halali; bali si vitu vyote vijengavyo.

1 Wakorintho- 10:16, 17: Kikombe cha baraka.

10:31 Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu.

1 Wakorintho- 11:23-29: Meza ya Bwana.

1 Wakorintho-15:45-47: Adamu wa kwanza na Adamu wa pili.

2 WAKORINTHO

2 Wakorintho-7:1 Basi, wapenzi wangu, kwa kuwa tuna ahadi hizo, na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu.

2 Wakorintho-6:15-17: Hekalu la Mungu ni miili yetu; Usiguse kitu kichafu.

2 Wakorintho-9:9 kama ilivyoandikwa, Ametapanya, amewapa maskini, Haki yake yakaa milele.

2 Wakorintho-12:7 Na makusudi nisipate kujivuna kupita kiasi, kwa wingi wa mafunuo hayo nalipewa mwiba katika mwili, mjumbe wa Shetani ili anipige, nisije nikajivuna kupita kiasi.

WAEFESO

Waefeso-5:5 Maana Neno hili mnalijua hakika, ya kwamba hakuna mwasherati wala mchafu wala mwenye tamaa, ndiye mwabudu sanamu, aliye na urithi katika ufalme wa Kristo na Mungu.

Waefeso-5:18 Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho;

WAFILIPI

Wafilipi-3:13 Ndugu, sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele;

Wafilipi-3:19 mwisho wao ni uharibifu, mungu wao ni tumbo, utukufu wao u katika fedheha yao, waniao mambo ya duniani.

Wafilipi-4:13 Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.

WAKOLOSAI

Wakolosai-4:14 Luka, yule tabibu mpendwa, na Dema, wanawasalimu.

1 TIMOTHEO

1Timotheo-3:8 Vivyo hivyo mashemasi na wawe wastahivu; si wenye kauli mbili, si watu wa kutumia mvinyo sana,si watu wanaotamani fedha ya aibu.

1Timotheo- 4:3 wakiwazuia watu wasioe, na kuwaamuru wajiepushe na vyakula, ambavyo Mungu aliviumba vipokewe kwa shukrani na walio na imani wenye kuijua hiyo kweli.

WAEBRANIA

Waebrania-9:19: Damu ya ndama na mbuzi, maji, pamba nyekundu, na hisopo.

Waebrania-10:22 na tukaribie wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya, tumeoshwa miili kwa maji safi.

Waebrania- 12:3 Maana mtafakarini sana yeye aliyeyastahimili mapingamizi makuu namna hii ya watendao dhambi juu ya nafsi zao, msije mkachoka, mkizimia mioyoni mwenu.

Waebrania-12:15 mkiangalia sana mtu asiipungukie neema ya Mungu; shina la uchungu lisije likachipuka na kuwasumbua, na watu wengi wakatiwa unajisi kwa hilo.

YAKOBO

Yakobo-2:20 Lakini wataka kujua, wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba imani pasipo matendo haizai?

Yakobo-5:14 Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana.

1 PETRO

1 Petro-2:11 Wapenzi, nawasihi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tamaa za mwili zipiganazo na roho.

2 PETRO

2 Petro-2:18 Maana wakinena maneno makuu mno ya kiburi, kwa tamaa za mwili na kwa ufisadi huwahadaa watu walioanza kuwakimbia wale wanaoenenda katika udanganyifu;

1 YOHANA

1 Yohana-1:9 Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.

1Yohana-2:1 Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki,

3 YOHANA

1Yohana-3:2 Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo.

UFUNUO

Ufunuo-13:12 Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake. Naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza, ambaye jeraha lake la mauti lilipona.

Ufunuo-Ufunuo-16:14 Hizo ndizo roho za mashetani, zifanyazo ishara, zitokazo na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi.

Ufunuo-18:2 Akalia kwa sauti kuu, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu; umekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza;

Ufunuo-22:2 katikati ya njia kuu yake. Na upande huu na upande huu wa ule mto, ulikuwapo mti wa uzima, uzaao matunda, aina kumi na mbili, wenye kutoa matunda yake kila mwezi; na majani ya mti huo ni ya kuwaponya mataifa.

SURA YA 25

UPONYAJI WA KIMUNGU KAMA UNAVYOPATIKANA KATIKA BIBLIA

Dhambi na magonjwa vinatokana na uvunjaji wa sheria za Mungu. Ili kupata afya ya kimwili ni lazima tutii sheria nane za afya za Mungu. Ili kupata afya ya kiroho ni lazima tutii sheria kumi za maadili za Mungu.

Mungu hatawarudishia afya wale wanaotamani tu ili waendelee kutenda dhambi na kumvunjia heshima Muumba wao. Kupenda utii ni kupenda afya na maisha. Kupenda dhambi ni kupenda maanguko, kuelekea chini kimaadili na kifo.

Sisi, kwa nguvu zetu wenyewe, hatuwezi kubadili tabia zetu za dhambi, za kujiangamiza, lakini—Ukweli wa ajabu,—Yesu wa ajabu anaweza kufanya hivyo kwa ajili yetu! Tunapotazama dhabihu Yake kuu kwa ajili yetu msalabani, kwa kukiri dhambi zetu, na kujisalimisha kwa nguvu za upendo Wake, Yeye atakuja katika maisha yetu na, kwa Roho Yake, kufanya hivyo kwa ajili yetu ambayo hatuwezi kufanya kwa ajili yetu wenyewe: na kutupatia akili mpya, moyo mpya, mitazamo mipya, njia mpya ya maisha na—ikiwa ni mapenzi Yake, uponyaji—uponyaji wa kimwili wa miili yetu iliyo na magonjwa na dhaifu.

Je, ni hatua zipi ambazo kwazo tunakuwa viumbe vipya katika Kristo na kupokea uponyaji wa mwili na akili na roho? Biblia inatuambia mambo kumi:

1- Nenda kwa Tabibu Mkuu; Mungu pekee Ndiye anayeweza kuponya.

Zaburi 103:2-4- Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana, Wala usizisahau fadhili Zake zote.

Akusamehe maovu yako yote, Akuponya magonjwa yako yote, Aukomboa uhai wako na kaburi, Akutia taji ya fadhili na rehema,

Kumbukumbu la Torati- 7:15 Na Bwana atakuondolea ugonjwa wote; wala hatatia juu yako maradhi yoyote mabaya uyajuayo ya Misri, lakini atayaweka juu ya wote wakuchukiao.

Kutoka 23:25- Nanyi mtamtumikia Bwana, Mungu wenu, naye atakibarikia chakula chako, na maji yako; nami nitakuondolea ugonjwa kati yako.

2- Kubali na uamini katika nguvu Zake za uponyaji; na kumwomba akuponye ikiwa ni mapenzi Yake.

Yohana 10:10 Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.

Matendo ya Mitume 3:16 Na kwa imani katika Jina Lake, Jina Lake limemtia nguvu mtu huyu mnayemwona na kumjua; na imani ile iliyo Kwake Yeye imempatia huyu uzima huu mkamilifu mbele yenu ninyi nyote.

3- Mtumainie, kuwa mtiifu kwa mapenzi Yake, na amini kwamba atakuponya ikiwa ni mapenzi Yake.

Warumi 8:26 Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho Mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa.

Luka 22:42 akisema, Ee Baba, ikiwa ni mapenzi Yako, uniondolee kikombe hiki; walakini si mapenzi Yangu, bali Yako yatendeke.

Zaburi 37:5, 7 Umkabidhi Bwana njia yako, Pia umtumaini, Naye atafanya.

Ukae kimya mbele za Bwana, Nawe umngojee kwa saburi; Usimkasirikie yeye afanikiwaye katika njia yake, Wala mtu afanyaye hila.

4- Ungama dhambi zako kwa Mungu, waombe msamaha wale uliowadhulumu, na uwasamehe.

Zaburi 66:18 Kama ningaliwaza maovu moyoni mwangu, Bwana asingesikia.

Yakobo 5:16 Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii.

1 Yohana 2:1 Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo Mwenye haki,

1 Yohana 1:9 Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.

5- Badilisha mazoea mabaya na utii sheria Zake zote, kupitia nguvu ambazo Yesu anakupa.

Kutoka 15:26 -akawaambia, Kwamba utaisikiza kwa bidii sauti ya Bwana, Mungu wako, na kuyafanya yaliyoelekea mbele Zake, na kutega masikio usikie maagizo Yake, na kuzishika amri Zake, Mimi sitatia juu yako maradhi yoyote niliyowatia Wamisri; kwa kuwa Mimi Ndimi Bwana nikuponyaye.

Yohana-5:8,14 Yesu akamwambia, Simama, jitwike godoro lako, uende. Baada ya hayo Yesu akamkuta ndani ya hekalu, akamwambia, Angalia, umekuwa mzima; usitende dhambi tena, lisije likakupata jambo lililo baya zaidi.

Yohana 8:11 Akamwambia, Hakuna, Bwana. Yesu akamwambia, Wala mimi sikuhukumu. Enenda zako; wala usitende dhambi tena.]

Warumi 12:1 Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana.

1 Wakorintho 3:16-17 Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi.

1 Wakorintho 10:31 Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu.

Wafilipi 4:13 Nayaweza mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu.

Luka 9:23 Akawaambia wote, Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate.

6- Saidia asili/mwili katika kusafisha mfumo na kutoa uchafu.

Zaburi 51:7 Unisafishe kwa hisopo nami nitakuwa safi, Unioshe, nami nitakuwa mweupe kuliko theluji

Isaya 1:16-17 Jiosheni, jitakaseni; ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho yangu; acheni kutenda mabaya; jifunzeni kutenda mema; takeni hukumu na haki; wasaidieni walioonewa; mpatieni yatima haki yake; mteteeni mjane.

Mathayo 10:7-8 Na katika kuenenda kwenu, hubirini, mkisema,

Ufalme wa mbinguni umekaribia. Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure.

2 Wakorintho 6:16-17 Tena pana mapatano gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu? Kwa maana sisi tu hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema, ya kwamba, Nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, Nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu Wangu.

Kwa hiyo, Tokeni kati yao, Mkatengwe nao, asema Bwana, Msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha.

7- Tumia Tiba rahisi ya maji.

Zaburi 51:1-2 Ee Mungu, unirehemu, Sawasawa na fadhili Zako. Kiasi cha wingi wa rehema zako, Uyafute makosa yangu. Unioshe kabisa na uovu wangu, Unitakase dhambi zangu.

2 Wafalme 5:10, 14 “Naye Elisha akampelekea mjumbe, akisema, Enenda ukaoge katika Yordani mara saba, na nyama ya mwili wako itakurudia, nawe utakuwa safi. Ndipo akashuka, akajichovya mara saba katika Yordani, sawasawa na neno lake yule mtu wa Mungu; nayo nyama ya mwili wake ikarudi ikawa kama nyama ya mwili wa mtoto mchanga, akawa safi.”

Yoshua 9:6-7 Nao wakamwendea Yoshua hata maragoni huko Gilgali, nao wakamwambia yeye na watu wa Israeli, Sisi tumetoka nchi ya mbali sana; basi kwa hiyo fanyeni agano pamoja nasi. Basi watu wa Israeli wakawaambia hao Wahivi, Labda mwakaa kati yetu; nasi tutawezaje kufanya agano nanyi?

2 Wakorintho 7:1 Basi, wapenzi wangu, kwa kuwa tuna ahadi hizo, na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu.

8- Tumia mimea rahisi ya shamba.

Mwanzo 1:29 Mungu akasema, Tazama, nimewapa kila mche utoao mbegu, ulio juu ya uso wa nchi yote pia, na kila mti, ambao matunda yake yana mbegu; vitakuwa ndivyo chakula chenu

Mwanzo 3:18-michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni; kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi.

Mithali 27:25 Manyasi huchukuliwa, na majani mabichi huonekana, Na maboga ya milimani hukusanyika.

Warumi 14:2 Mtu mmoja anayo imani, anakula vyote; lakini yeye aliye dhaifu hula mboga.

Zaburi 104:14 Huyameesha majani kwa makundi ya wanyama, Na maboga kwa matumizi ya mwanadamu; Ili atoe chakula katika nchi

Ezekieli 47:12 Na karibu na mto, juu ya ukingo wake, upande huu na upande huu, utamea kila mti wa chakula, ambao majani yake hayatanyauka, wala matunda yake hayatatindika kamwe; utatoa matunda mapya kila mwezi, kwa sababu maji yake yanatoka mahali patakatifu; na matunda yake yatakuwa ni chakula; na majani yake yatakuwa ni dawa.

Ufunuo wa Yohana 22:2 katikati ya njia kuu yake. Na upande huu na upande huu wa ule mto, ulikuwapo mti wa uzima, uzaao matunda, aina kumi na mbili, wenye kutoa matunda yake kila mwezi; na majani ya mti huo ni ya kuwaponya mataifa.

9- Mshukuru Mungu kwa rehema na neema Yake, vyovyote itakavyokuwa matokeo, na uyatoe maisha yako mikononi Mwake.

Isaya 26:3 Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea Katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini.

Isaya 30:15 Kwa maana Bwana MUNGU, Mtakatifu wa Israeli, asema hivi, Kwa kurudi na kustarehe mtaokolewa; nguvu zenu zitakuwa katika kutulia na kutumaini; lakini hamkukubali.

Zaburi 27:14-Amini ya kuwa nitauona wema wa Bwana Katika nchi ya walio hai.

Umngoje Bwana, uwe hodari, Upige moyo konde, naam, umngoje Bwana.

Kumbukumbu la Torati 33:25 Makomeo yako yatakuwa ya chuma na shaba; Na kadiri ya siku zako ndivyo zitakavyokuwa nguvu zako.

Kumbukumbu la Torati 33:27 Mungu wa milele Ndiye makazi yako, Na mikono ya milele i chini yako. Na mbele yako amemsukumia mbali adui; Akasema, Angamiza.

Yoshua 1:9 Je! Si Mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa Bwana, Mungu wako, Yu pamoja nawe kila uendako.

Zaburi 4:8 Katika amani nitajilaza na kupata usingizi mara, Maana Wewe, Bwana, peke yako, Ndiwe unijaliaye kukaa salama.

Zaburi 27:1 Bwana ni nuru yangu na wokovu wangu, Nimwogope nani? Bwana ni ngome ya uzima wangu, Nimhofu nani?

Zaburi 42:8 Mchana Bwana ataagiza fadhili Zake, na usiku wimbo Wake utakuwa nami, Naam, maombi kwa Mungu aliye uhai wangu.

Zaburi 37:5 Umkabidhi Bwana njia yako, Pia umtumaini, Naye atafanya.

10 - Fanya yote uwezayo kuwaongoza wengine kwenye msalaba wa Yesu na kwa nguvu Zake za uponyaji. Afya tele imeahidiwa kwa wale wanaofanya hivi.

Isaya 58:7-8 “Je! Siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? Umwonapo mtu aliye uchi, umvike nguo; wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe? Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara; na haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakufuata nyuma ukulinde.”

Kumbuka: Ikiwa unatoa somo moja la Biblia juu ya somo lililo hapo juu, soma msitari mmoja (au mafungu mawili kwa nadra) kutoka kwa kila sehemu kati ya sehemu kumi zilizoorodheshwa hapo juu.

NUKUU MUHIMU

Nukuu/kauli zifuatazo zinatokana na mkusanyiko wa afya tulioweka nyuma ya toleo letu la bei ya chini sana la Desire of Ages. Nukuu/kauli zifuatazo zinaonyesha kwamba utii kwa sheria ya Mungu—unajumuisha sheria za kimwili na kiafya:

“Uvunjaji wa sheria ya kimwili ni uvunjaji wa sheria ya Mungu. Muumba wetu ni Yesu Kristo. Yeye Ndiye Mwandishi wa nafsi/utu wetu. Yeye Ameunda muundo wa mwanadamu-amemwumba mwanadamu. Yeye Ndiye mwandishi wa sheria za kimwili, kwa kuwa Yeye Ndiye Mwandishi wa sheria za maadili. Na mwanadamu ambaye ni mzembe na asiyejali mazoea na mambo yanayohusu maisha na afya yake ya kimwili, hutenda dhambi dhidi ya Mungu.”—Letter, May 19, 1897.

"Sheria ya Mungu imeandikwa kwa kidole Chake Mwenyewe juu ya kila neva, kila misuli, kila uwezo ambao umekabidhiwa kwa mwanadamu."—Letter, August 30, 1896.

“Afya, nguvu, na furaha hutegemea sheria zisizobadilika; Lakini sheria hizi haziwezi kutiiwa pale ambapo hakuna tashwishwi ya kuzifahamu.” —Health Reformer.

“Bwana ameifanya kuwa sehemu ya mpango Wake kwamba uvunaji wa mwanadamu utakuwa sawasawa na upandakizaji wake.”— Letter, May 19, 1897.

“Hebu mtu yeyote asipate wazo kwamba taasisi ni mahali pao pa kuja kuponywa kwa maombi ya imani. Hapo ni mahali pa kupata nafuu ya magonjwa kwa matibabu na mtindo wa maisha mzuri wa kuishi, na kujifunza jinsi ya kuepukana na magonjwa. Lakini ikiwa kuna sehemu moja chini ya mbingu zaidi ya nyingine ambapo sala inayotuliza, yenye huruma inapaswa kutolewa na wanaume na wanawake waliojitoa na wenye imani ni katika taasisi kama hiyo. Wale wanaowatibu wagonjwa wanapaswa kusonga mbele katika kazi yao muhimu wakimtegemea sana Mungu kwa baraka Zake na kutumia rasilimali ambazo amezitoa kwa neema, na ambazo kwa rehema Zake amevuta usikivu wetu kama hewa safi, usafi, lishe bora,vipindi sahihi vya kazi na mapumziko, na matumizi ya maji.” —Shuhuda kwa Kanisa, 1: 561.

“Kuna njia nyingi za kufanya uponyaji, lakini ipo njia moja tu ambayo mbingu inaikubali. Dawa zipatikanazo kutoka kwa Mungu ni za asili na ambazo hautatoa ushuru au kudhoofisha mifumo ya mwili kwa sababu ya sifa zake kuu. Hewa safi, maji, usafi, lishe sahihi, maisha safi, usafi na imani thabiti kwa Mungu ni tiba kwa mahitaji mengi ambayo maelfu wanakufa kwa kuzikosa; lakini dawa hizi zimepitwa na wakati kwa wengi sababu matumizi yake na uandaaji wake unahitaji muda na ustadi maalum ambao watu hawauthamini. Hewa safi, mazoezi, maji safi, na mahali safi pa kuishi yanaweza kufikiwa na watu wote kwa gharama ndogo, lakini dawa za hospitali ulimwenguni ni ghali, gharama yake ni kubwa madukani na kwa athari inayozalishwa kwenye mifumo yetu ni kubwa pia -Shuhuda kwa Kanisa 5: 443.

“Ni wajibu wa kila mwanadamu, kwa ajili yake mwenyewe na kwa ajili ya binadamu, kuwa na ufahamu binafsi kuhusiana na sheria za viungo vya mwili , na kuzitii kwa uangalifu…….. Ni wajibu wa kila mtu kuwa na akili kuhusiana na magonjwa na sababu zake.”—Letter, December 4, 1896.

“Mungu ametunga sheria za kutawala kila sehemu ya viungo vyetu, na sheria hizi alizoziweka katika utu wetu ni za Kiungu, na kwa kila uvunjaji wa sheria kuna adhabu isiyobadilika, ambayo hivi karibuni au baadaye lazima itimie.”—Health Reformer.

Wajibu wetu wa kwanza, ambao tunadaiwa na Mungu, kwetu wenyewe, na kwa wenzetu, ni kutii sheria za Mungu, ambazo ni pamoja na sheria za afya. Tukiwa wagonjwa tunawalemea rafiki zetu, na kujiweka kwenye mazingira ya kutofaa kutimiza majukumu yetu kwa familia na majirani zetu. —Shuhuda kwa Kanisa 3:164

“Sheria zinazotawala mwili ni sawa na zile za Kiungu katika asili na tabia kama ilivyo kwa sheria ya Amri Kumi. Mwanadamu ameumbwa kwa njia ya kutisha na ya ajabu; Kwa maana Yehova ameandika sheria Yake kwa mkono Wake Mwenyewe wenye nguvu juu ya kila sehemu ya mwili wa mwanadamu.”—Letter, August 5, 1896.

“Je, sina haki ya kufanya nipendavyo juu ya mwili wangu mwenyewe?’—Hapana, huna haki ya kiadili, kwa sababu unakiuka sheria za uzima na afya ambazo Mungu amekupa. Wewe ni mali ya Bwana, - ni mali yake kwa njia ya uumbaji na kwa njia ya ukombozi. Kila mwanadamu yuko chini ya wajibu wa kutunza nguvu ya uzima ambayo imetengenezwa kwa njia ya kutisha na ya ajabu sana.”—Letter, May 19, 1897.

“Miili yetu yenyewe si yetu wenyewe, kuitumia jinsi tupendavyo, kuidhoofisha kwa njia ya mazoea ambayo husababisha uozo, kutaifanya isiwezekane kumtumikia Mungu kwa ukamilifu. Maisha yetu na uwezo wetu wote hutokana na Yeye. Anatujali kila wakati; anaruhusu nguvu ya uzima iendelee kutenda kazi. Ikiwa tungeachwa tuiendeshe kwa dakika moja, tungekufa. Tunamtegemea Mungu kabisa.”—Letter, October 12, 1896.

"Afya inapaswa kulindwa kwa utakatifu kama ilivyo kwa tabia."— Christian Temperance, 82.

“Kwa kadiri sheria za asili zinavyovunjwa, ndivyo akili na roho zinavyodhoofika…….. Mateso ya kimwili ya kila aina yanaonekana.

Mateso lazima yafuate hatua hii. Nguvu muhimu ya utendaji ya mwili (mfumo) haiwezi kubeba mzigo unaowekwa juu yake, na hatimaye inavunjika.—Letter, August 30, 1896.

Ugonjwa husababishwa na kukiuka sheria za afya; ni matokeo ya kukiuka sheria ya asili. Shuhuda kwa Kanisa 3:164

"Afya ni hazina kubwa. Ni kitu chenye thamani kubwa zaidi ambacho mwanadamu anaweza kuwa nacho. Utajiri, heshima, au elimu hununuliwa kwa gharama sana, endapo kuna upotevu wa nguvu ya afya. Hakuna mafanikio yoyote kati ya hayo yanayoweza kuleta furaha ikiwa afya inakosekana.”—Christian Education, 16.

“Muda huo hutumika vizuri pale unapoelekezwa katika uimarishaji na utunzaji wa afya nzuri ya kimwili na kiakili…….. Ni rahisi kupoteza afya, lakini ni vigumu kuipata tena.”—Review, No. 39, 1884.

Afya kamili inategemea mzunguko mzuri wa damu. Shuhuda kwa Kanisa 2:531

“Wengi wameniuliza, ‘Ipi ni namna iliyo bora zaidi ninayoweza kutunza afya yangu vizuri zaidi?’ Jibu langu ni, acha kukiuka sheria za kuishi; Acha uchu wa chakula, kula chakula rahisi, Uvae kiafya, yaani wa kiasi, fanya kazi kwa afya, nawe hutakuwa mgonjwa.” —Health Reformer.

"Maisha yasiyo na malengo ni kifo hai. Akili inapaswa itafakari juu ya mada zinazohusiana na masilahi yetu ya umilele. Hii itasaidia afya ya mwili na akili.”— Review, No. 31, 1884.

“Mungu ameahidi Mwenyewe kuiweka karakana hii hai katika utendaji mzuri, ikiwa wakala wa kibinadamu atatii sheria Zake na kushirikiana na Mungu.”— Letter, January 11, 1897.

"Hebu iwekwe daima akilini kwamba lengo kuu la matengenezo ya usafi ni kwa ajili kupata maendeleo ya juu zaidi ya akili na roho na mwili." ”— Christian Temperance, 120.

“Asili itarejesha nguvu na nguvu zao katika saa zao za kulala, ikiwa sheria zake hazitakiukwa.”—Solemn Appeal, 16.

"Kufungiwa ndani ya nyumba kunawafanya wanawake kuwa wa rangi ya kijivu (Kabaka)na kuwa dhaifu, na kusababisha kifo cha mapema." —Health Reformer.

"Mazoea ya tamaa katika ulaji wa mara kwa mara, na kwa kiasi kikubwa, huvilemea viungo vya umeng'enyaji wa chakula, na kusababisha joto la mwili (mfumo) kuongezeka/kupanda. Damu kuwa chafu, na kisha magonjwa ya aina mbalimbali hutokea.”— Spiritual Gifts, Vol. 4, 133.

Madhara yanayotokana na kuishi katika vyumba vilivyofungwa, visivyo na hewa safi ni haya: Mfumo unakuwa dhaifu na usiofaa kiafya, mzunguko unakuwa duni, damu hutembea taratibu katika mfumo kwa sababu haijasafishwa na kuimarishwa na hewa safi, yenye nguvu ya mbinguni. Akili inakuwa na huzuni na majonzi, wakati mfumo mzima ukidhoofika; homa na magonjwa mengine ya papo hapo yanazalishwa. Kujitenga kwako na hewa ya nje na hofu ya kuingiza hewa ndani kumekufanya uvute hewa mbaya, chafu ambayo hutolewa kutoka kwenye mapafu ya wale wanaokaa katika vyumba hivi, na ambayo ni sumu, isiyofaa kwa msaada wa maisha. Mwili unasinyaa, ngozi inakauka, mmeng'enyo unapungua, na mfumo unaathiriwa sana na mafua. Uingizaji wa hewa kidogo tu huleta magonjwa makubwa. — Shuhuda kwa Kanisa 1: 702.

Je! Kula kupita kiasi kuna athari gani kwa tumbo? Tumbo linakuwa dhaifu, viungo vya mmeng'enyo vinadhoofika, na magonjwa, pamoja na mtiririko wa uovu huletwa kama matokeo.—Shuhuda kwa Kanisa 2: 364.

"Matumizi ya holela ya sukari kwa namna yoyote hupelekea kuziba kwa mfumo, na sio sababu ya mara kwa mara ya ugonjwa." —Counsels to parents and Teachers, 57.

Dhima ya kupata ugonjwa huongezeka mara kumi kwa kula nyama. —Shuhuda kwa Kanisa 2: 64.

"Michanganyiko mingi na yenye kutatiza ya chakula inaharibu afya. Nyama zilizokolea sana na keki nyingi huchakaza/huchosha viungo vya umeng'enyaji wa chakula."— Letter, November 5, 1896.

Lakini madawa yanapaswa kuachwa milele; kwa sababu hayaponyi ugonjwa wowote, bali yanadhoofisha mfumo, na kufanya iwe rahisi kupata magonjwa."— Shuhuda kwa Kanisa 5: 311.

“Kupuuza usafi kutasababisha magonjwa.”— How to Live, Chapter 4, 61.

“Vyumba ambavyo havijaangaziwa na mwanga na hewa huwa na unyevunyevu…….. Magonjwa mbalimbali yamesababishwa (letwa) kwa kulala katika vyumba hivyo.”— How to Live, 243.

"Makazi, ikiwezekana, yanapaswa kujengwa kwenye mwinuko na palipo pakavu. Ikiwa nyumba itajengwa mahali ambapo maji yanatuama, yanapobakia kwa muda na kisha kukauka, hewa yenye sumu hutokea, na homa ya baridi, donda koo, magonjwa ya mapafu, na hivyo kupelekea homa mbalimbali. ”— How to Live, 246.

“Ikiwa nguo zinazovaliwa hazioshwi mara kwa mara, zinakuwa chafu na uchafu ambao hutolewa nje ya mwili kwa njia ya jasho au isiyo ya jasho…….. Matundu ya ngozi hufyonzwa tena, na kuurudisha uchafu uliokuwa umetolewa.” —How to Live, 242.

“Tunapofanya yote tuwezayo kwa upande wetu kuwa na afya, basi na tutegemee kwamba matokeo yenye baraka yatafuata, na tunaweza kumwomba Mungu kwa imani abariki jitihada zetu kwa ajili ya kutunza afya.” How to Live, 246.

Kauli zifuatazo ni baadhi ya zile bora kutoka katika kitabu ulicho nacho sasa mkononi. Kwa sababu hiki ni kitabu cha bei ya chini, unaweza kupata nukuu zifuatazo kutoka kwa nakala ya kitabu— na kuzibandika kwenye kuta ili watu wote wasome!

“Huruma ya kweli kati ya mwanadamu na wanadamu wenzake inapaswa kuwa ni ishara ya kuwatofautisha wale wanaompenda na kumcha Mungu na wale ambao hawajali sheria Yake. Ni huruma iliyoje ambayo Kristo alionyesha katika kuja katika ulimwengu huu kutoa maisha Yake dhabihu kwa ajili ya ulimwengu unaokufa! Dini Yake iliongoza kwenye kazi ya Kweli ya umishenari wa tiba.” — Medical Ministry, 251

Mivuto inayohusishwa na matengenezo ya afya itapendekezwa kwenye maamuzi ya wote wanaotaka nuru, na watasonga mbele hatua kwa hatua ili kupokea Kweli maalum kwa wakati huu. — Shuhuda kwa Kanisa 6: 379

Tangu sasa kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kuendelezwa kwa bidii ambayo haikuwahi kuendelezwa kabla. Kazi hii ni mlango ambao Ukweli hupata kuingia katika miji mikubwa. —Shuhuda kwa Kanisa 9: 167

"Tutaona kazi ya umishenari wa tiba ikipanuka na kuongezeka katika kila hatua ya maendeleo yake, kwa sababu ya kuingia kwa mamia na maelfu ya vijito, hadi dunia yote ifunikwe kama maji yanavyofunika bahari." —Medical Ministry, 317

"Kote karibu nasi ni milango iliyo wazi kwa ajili ya huduma. Tunapaswa kufahamiana na majirani zetu, na kutafuta kuwavuta kwa Kristo. Tunapofanya hivi,Yeye atakubali na kushirikiana nasi.” —Counsels on Health 396

“Upana wa kazi ya umishenari ya injili haueleweki. Kazi ya umishenari wa tiba inayotakiwa sasa imeainishwa katika utume ambao Kristo aliwapa wanafunzi Wake kabla tu ya kupaa Kwake. ‘Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani,’ akasema. Mathayo 28:19-20

Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari. Maneno haya yanaonyesha uwanja wetu na kazi yetu. Shamba letu ni ulimwengu; Kazi yetu ni kutangaza Kweli ambazo Kristo alikuja katika ulimwengu wetu kuzitangaza.” —Counsels on Health, 509

“Kazi ya umishenari wa tiba ndiyo kazi inayotangulia injili, upenyo ambao Ukweli kwa wakati huu unazifikia nyumba nyingi. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa wamishenari wa Kweli wa tiba, kwa kuwa wanapaswa kujifunza kuhudumia mahitaji ya roho na mwili. Kutokuwa na ubinafsi wa aina zote kunapaswa kuonyeshwa na watendakazi wetu kwani, kwa ujuzi na uzoefu unaopatikana kwa kazi ya vitendo, wanatoka kwenda kutoa matibabu kwa wagonjwa. Wanapoenda

nyumba kwa nyumba, na watapata ufikiaji wa mioyo ya watu wengi. —Welfare Ministry, 125

"Kuna njia nyingi za kufanya sanaa ya uponyaji, lakini kuna njia moja tu ambayo Mbingu anaikubali. Tiba za Mungu ni mawakala rahisi wa asili, ambao hawataudhuru au kudhoofisha mfumo kupitia sifa zake zenye nguvu. —Counsels on Health, 323

“Hatuna muda wa kupoteza. Mwisho uko karibu. Njia kutoka mahali hadi mahali ili kueneza Ukweli hivi karibuni itazungukwa na hatari kwenye mkono wa kulia na wa kushoto. Kila kitu kitawekwa ili kuzuia njia ya Mitume wa Bwana, ili wasiweze kufanya yale ambayo inawezekana kwao kufanya sasa. Ni lazima tuangalie kazi yetu ipasavyo kuhusu wakati ujao, na tusonge mbele haraka iwezekanavyo katika vita vikali.” —Evangelism, 30-31

“Mbele ya Mwanamatengenezo wa kweli, kazi ya umishenari wa tiba itafungua milango mingi. Hakuna mtu anayehitaji kusubiri hadi aitwe kwenye uwanja fulani wa mbali kabla ya kuanza kuwasaidia wengine. Popote ulipo, unaweza kuanza mara moja. Fursa ziko ndani ya kila mtu. Chukua kazi ambayo unawajibika kwayo—kazi inayopaswa kufanywa nyumbani kwako na katika ujirani wako. Usisubiri wengine wakusihi uchukue hatua. Katika kumcha Mungu songa mbele bila kukawia, ukizingatia wajibu wako binafsi kwa Yeye aliyetoa maisha Yake kwa ajili yako. Tenda kana kwamba umemsikia Kristo akikuita wewe binafsi kufanya uwezavyo katika utumishi Wake. Angalia usione ni nani mwingine yuko tayari. Ikiwa umewekwa wakfu kikweli, Mungu, kwa njia ya chombo chako, atawaleta katika Kweli wengine ambao anaweza kuwatumia kama njia za kuwaletea wengi nuru wanaopapasa gizani.” —Counsels on Health, 425-426

"Hatupaswi kufunika rehema kwa ubinafsi na kisha kuiita kazi ya umishenari wa tiba." —Medical Ministry, 131

"Kamwe mwonekano haupaswi kutegemewa kama njia ya mafanikio. Huu ni udanganyifu……. Ni kama ugonjwa unaoendelea kula uhai. —Counsels on Health, 277

"Sehemu nyingi za vituo vya afya zinapaswa kuanzishwa. Hazipaswi kuwa kubwa, lakini zilizokamilika na za kutosha kufanya kazi nzuri na yenye mafanikio.” — Counsels on Health, 225

"Kuwa makini na matumizi madogo madogo. Jiepushe na kila uvujaji. Ni hasara ndogo ambazo huzungumza sana mwishoni. Kusanya vipande; Usiruhusu chochote kipotee. Usipoteze dakika katika kuzungumza; dakika zilizopotea

huharibu masaa. Bidii inayodumu, kufanya kazi kwa imani, daima itavikwa taji la mafanikio.” —Counsels on Health, 304-305

“Onyo langu ni: Tokeni mijini. Msijenge kituo cha afya katika miji. Elimisheni watu wetu kutoka nje ya miji na kuingia shambani (nchini), ambapo wanaweza kupata kipande kidogo cha ardhi, na kujitengenezea makazi yao na watoto wao. —Country Living, 10

“Lazima tufanye zaidi ya tulivyofanya ili kuwafikia watu wa miji yetu. Hatupaswi kujenga majengo makubwa mijini, lakini tena na tena nuru imetolewa kwamba tunapaswa kuanzisha katika miji yetu yote taasisi ndogo-ndogo ambazo zitakuwa vituo vya mvuto. — Counsels on Health, 481

"Kunapaswa kuwa na saa zisizobadilika, na zilizotengwa za kufanya kazi, na saa za zisizobadilika-badilika, zilizotengwa kwa kula." —Medical Ministry, 79

“Tiba rahisi zaidi hazina madhara [kuliko sumu za dawa za famasia] kulingana na usahili wao, lakini katika hali nyingi sana hizi hutumiwa wakati si lazima….. Kuna mimea na mizizi rahisi ambayo kila familia inaweza kutumia yenyewe, na haifai kumwita daktari mapema kama vile ambavyo wangemwita wakili. —2 Selected Messages, 279

Kwa nini watu wawili au watatu hawakutani pamoja na kumsihi Mungu kwa ajili ya wokovu wa mtu mmoja maalum, na kisha mwingine? Katika makanisa yetu hebu makundi yaundwe kwa ajili ya huduma. Hebu watu tofauti waungane katika kazi kama wavuvi wa watu. Hebu watafute kukusanya roho kutoka katika uharibifu wa ulimwengu kwenda kwenye usafi wa kuokoa wa upendo wa Kristo. Uundaji wa makundi madogo madogo kama msingi wa juhudi za Kikristo umewasilishwa kwangu na Yule ambaye hawezi kukosea kamwe. Ikiwa kuna idadi kubwa ya watu kanisani, hebu washiriki wapangwe katika makundi madogo madogo, kufanya kazi sio tu kwa ajili ya washiriki wa kanisa, bali kwa ajili ya watu wasioamini. Ikiwa katika sehemu moja wapo watu wawili tu au watatu ambao wanaujua Ukweli, hebu wajiunge katika kikundi cha wafanyakazi. Hebu waweke dhamana yao ya muungano kutokuvunjika, wakisihi pamoja kwa upendo na umoja, wakitiana moyo kusonga mbele, kila mmoja akipata ujasiri na nguvu kutoka kwa msaada wa wengine. —Shuhuda kwa Kanisa 7: 21-22

“Ukweli kwa wakati huu, ujumbe wa malaika wa tatu, unapaswa kutangazwa kwa sauti kuu, tunapokaribia Jaribio Kuu la Mwisho. Jaribio hili lazima lije kwa makanisa kuhusiana na kazi ya ile Kweli ya umishenari wa tiba, kazi ambayo ina

Daktari Mkuu wa kutoa maagizo na kusimamia katika yote yaliyo ndani yake.” —Loma Linda Messages, 62

Wafanyakazi wa umishenari wa tiba wanafanya kazi ambayo imepuuzwa kwa muda mrefu ambayo Mungu alitoa kwa kanisa huko Battle Creek - wanatoa wito wa mwisho kwa ajili ya karamu ambayo [Bwana] ameiandaa. —Shuhuda kwa Kanisa 8: 71

Hewa safi, mwanga wa jua, kuwa na kiasi, pumziko, kufanya mazoezi, chakula kinachofaa, matumizi ya maji, kumtumaini Mungu na uweza Wake—hizi ndizo tiba za kweli. Kila mtu apaswa kuwa na maarifa ya maumbile ya asili (nature) yaletayo uponyaji na jinsi ya kuyatumia (azifahamu tiba nane rahisi na kuzitumia, ikiwemo usafi, roho ya shukrani, mtazamo wa maisha, na kuhudumia watu). Ni muhimu pia kuelewa kanuni zinazohusika katika tiba ya wagonjwa na kuwa na uzoefu wa vitendo, utakaomwezesha mtu kutumia ujuzi huo kwa njia ifaayo. [MH127.2]

Matumizi ya tiba za asili yanahitaji kiasi kikubwa cha uangalifu na jitihada, mambo ambayo wengi hawako tayari kuyafanyia kazi. Mchakato wa asili wa uponyaji na kuujenga mwili tena pale ulipoharibika ni wa taratibu ila una uhakika, na kwa wale wasio na subira, huona mambo yanaenda polepole sana kwao. Kusalimisha vile vitu vinavyoendekezwa au kujifurahisha navyo kunahitaji kujitoa kafara. Lakini mwishowe itagunduliwa kwamba asili, isipozuiwa, hufanya kazi yake kwa busara na kwa ubora. Wale wanaodumu katika kuzitii sheria zake watavuna thawabu katika afya zao za mwili na akili. —Ministry of Healing, 127

Maelekezo maalum yanapaswa kutolewa katika sanaa ya kutibu wagonjwa bila kutumia dawa za famasia zenye sumu na kupatana na nuru ambayo Mungu ameitoa. Katika matibabu ya wagonjwa, dawa zenye sumu hazihitajiki kutumiwa. —Shuhuda kwa Kanisa 9: 175

"Tiba rahisi za asili zitasaidia kupona bila kuacha athari mbaya ambazo mara nyingi huhisiwa na wale wanaotumia dawa zenye sumu." —2 Selected Messages, 281

“Ikiwa watachukua msimamo kwamba katika kuomba kwa ajili ya uponyaji hakupaswi kutumia tiba rahisi zinazotolewa na Mungu ili kupunguza maumivu na kusaidia asili katika kazi yake, wasije wakawa wanaikana imani, wanachukua (wao) msimamo usio wa hekima. Huku sio kuikana imani; hili linapatana kabisa na mipango ya Mungu. . Katika kila kitu tunahitajika kusonga mbele kwenye mstari wa majaliwa (ulinzi) ya Mungu. Wakala wa kibinadamu anapaswa kuwa na

imani na anapaswa kushirikiana na nguvu ya Mwenyezi Mungu, kwa kutumia kila nyenzo, akifurahia kila kitu ambacho, kulingana na akili yake, ni cha manufaa, kufanya kazi kwa kupatana na sheria za asili; Na kwa kufanya hivyo haikani wala haifichi imani." —Counsels on Health, 381-382

Tujapoomba uponyaji kwa mgonjwa, haijalishi hatima ya hali ya mgonjwa itakuwaje, tusipoteze imani kwa Mungu. Ikiwa tunaitwa kukutana na msiba, tupokee kikombe hiki kichungu, tukikumbuka kwamba mkono wa Baba yetu ndiyo hukishikilia midomoni mwetu. Lakini tujapopona, isisahaulike kwamba mpokeaji wa rehema ya uponyaji anawekwa chini ya wajibu uliofanywa upya kwa Muumba. —Ministry of Healing, 233

Tumaini pekee la mambo yaliyo bora ni katika kuwaelimisha watu kanuni sahihi. Waganga wawafundishe watu kwamba nguvu za urejeshwaji hazipo katika madawa, bali katika asili. —Ministry of Healing, 127

Ugonjwa ni juhudi ya maumbile ya asili, kuuweka mfumo huru kutoka kwenye hali iliyosababishwa na ukiukaji wa sheria za afya. Pale mtu anapopatwa na ugonjwa, sababu ya kuja kwa huo ugonjwa inapaswa kutambuliwa-kueleweka. Tabia mbaya yafaa zibadilishwe. Mazoea mabaya yarekebishwe. Kisha asili inapaswa kusaidiwa katika juhudi zake za kuondoa uchafu mwilini na kuweka upya hali sahihi katika mfumo. Matumizi ya tiba za asili yanahitaji kiasi kikubwa cha uangalifu, muda na jitihada, mambo ambayo wengi hawako tayari kuifanyia kazi. Mchakato wa asili wa uponyaji na kuujenga mwili tena pale ulipoharibika ni wa taratibu ila una uhakika, na kwa wale wasio na subira, huona mambo yanaenda polepole sana kwao. Kusalimisha vile vitu vinavyoendekezwa au kujifurahisha navyo kunahitaji kujitoa kafara. Lakini mwishowe itagunduliwa kwamba asili, isipozuiwa, hufanya kazi yake kwa busara na kwa ubora. Wale wanaodumu katika kuzitii sheria zake watavuna thawabu katika afya zao za mwili na akili. —Ministry of Healing, 127

"Maelfu wamekufa kwa kukosa maji safi na hewa safi, ambao wangeweza kuishi. Na maelfu ya walemavu, ambao ni mzigo kwao wenyewe na kwa wengine, wanafikiri kwamba maisha yao yanategemea kuchukua dawa kutoka kwa madaktari. Wanaendelea kujiongoza wenyewe kuwa mbali na hewa bora nje, na kujiepusha na matumizi ya maji. Baraka hizi wanazihitaji ili wapate kuwa wazima. Ikiwa wangepata nuru, na kuziacha dawa, na kujizoeza kufanya mazoezi ya nje, na kuruhusu hewa ndani ya nyumba zao, kipindi cha joto na baridi, na kutumia maji safi kwa madhumuni ya kunywa na kuoga, wangekuwa wazima na

wenye furaha, badala ya kupitia uzoefu wa maisha duni. — Counsels on Health, 55-56

Lakini wengi hawajawahi kujifunza kupitia uzoefu binafsi kuhusu matokeo yenye manufaa ya matumizi sahihi ya maji, na huogopa jambo hili. Tiba ya maji haithaminiwi jinsi inavyopaswa, na ili kuyatumia maji kwa ustadi kuna hitaji la kufanya kazi yenye juhudi, ambayo wengi hawataki kuhusika. Lakini hakuna anayepaswa kuhisi kuwa na kisingizio kwa sababu tu ya ujinga wake au uzembe kuhusiana na jambo hili. Zipo njia nyingi ambazo maji yaweza kutumika kutuliza maumivu na kuzuia ugonjwa.—Ministry of Healing, 237

“Njia ya kweli ya kuponya wagonjwa ni kuwaambia kuhusu mimea kama miti shamba (herbs) inayokua kwa manufaa ya mwanadamu. Wanasayansi wameambatanisha majina makubwa kwa maandalizi haya rahisi zaidi mimea pale wanapotengeneza dawa, lakini elimu ya kweli itatuongoza kuwafundisha wagonjwa ambao hawahitaji kumwita daktari zaidi ya vile wangemwita wakili. Wao wenyewe wanaweza kusimamia mimea rahisi ikiwa itahitajika. Kuielimisha jamii ya mwanadamu kwamba ni daktari peke yake ndiye anajua magonjwa yote ya watoto wachanga na watu wa kila umri ni fundisho la uongo, na kwa kadiri sisi kama watu tunaposimama juu ya kanuni za matengenezo ya afya, ndivyo baraka tele itakavyowajia wale ambao wangefanya kazi ya kweli ya tiba…… Kwa lugha rahisi, tunaweza kuwafundisha watu jinsi ya kutunza afya, jinsi ya kuepuka magonjwa. Hii ndiyo kazi ambayo vituo vyetu vya afya vya sanitarium vinaitwa kufanya. Hii ni sayansi ya kweli.” —Spalding-Megan Collection, 137

“Imani yetu inatuhitaji kuinua kiwango cha matengenezo, na kuchukua hatua za juu. Sharti la kukubalika kwetu na Mungu ni kwa njia ya kujitenga kwa vitendo na ulimwengu. Bwana anatuita kama watu, ‘Tokeni kati yao, mkatengwe nao. — Counsels on Health, 50-51

BONASI YA JUMBE KUTOKA LOMA LINDA

MIPANGO YA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA

Vijana walio na ujuzi wa kivitendo wa jinsi ya kuwatibu wagonjwa, sasa watatumwa kufanya kazi ya umishenari wa tiba ya injili, kuhusiana na wahudumu wenye uzoefu zaidi wa injili. Ikiwa vijana hawa watajitolea kujifunza Neno, watakuwa wainjilisti wenye mafanikio. Wahudumu hawa vijana ambao wanafanya kazi pamoja nao wanapaswa kuwapa nafasi ileile ya kujifunza ambayo Eliya alimpa Elisha. Wanapaswa kuwaonyesha jinsi ya kuwafundisha wengine Kweli. Inapowezekana vijana hawa wanapaswa kutembelea hospitali, na katika kesi zingine wanaweza kuungana nao kwa muda, wakifanya kazi bila kujali. Mfano safi kabisa wa kutokuwa na ubinafsi sasa unapaswa kuonyeshwa na wahudumu wetu wa umishenari wa tiba. Kwa ujuzi na uzoefu unaopatikana kwa kazi ya vitendo, wanapaswa kwenda kuwatibu wagonjwa. Wanapoenda nyumba

kwa nyumba, watapata ufikiaji wa mioyo mingi. Wengi watafikiwa ambao vinginevyo hawangesikia ujumbe wa injili. LLM 69.3

Mengi mazuri yanaweza kufanywa na wale ambao hawana masomo ya udaktari, na walioidhinishwa kikamilifu. Wengine wanapaswa kuwa tayari kufanya kazi kama madaktari wenye uwezo. Wengi, wakifanya kazi chini ya maelekezo ya watu kama hao, wanaweza kufanya kazi zinazokubalika bila kutumia muda mrefu sana katika kujifunza kama ilivyofikiriwa kuwa ni lazima kutumia hapo awali. LLM 69.4

Wengi wataenda kufanya kazi kama Mwalimu ambaye hajaweza bado kuchukua kozi ya kawaida ya masomo shuleni (untrained teacher). Mungu atawasaidia watendakazi hawa. Watapata maarifa kutoka kwa shule ya upili, nao watafaa kuchukua nafasi zao katika safu na mistari ya watendakazi kama wauguzi. Mmishenari Mkuu wa tiba anaona kila juhudi inayofanywa kupata ufikiaji wa roho kwa kuwasilisha kanuni za matengenezo ya afya. LLM 69.5

Mabadiliko yaliyoamuliwa yanafanyika katika ulimwengu wetu. Bwana ametangaza kwamba atageuza na kupindua mambo. Wanaume wanyenyekevu, ambao hadi sasa wamekuwa katika giza, lazima sasa wapewe nafasi ya kuwa watendakazi. LLM 70.1

Kwa wale wanaotoka kufanya kazi ya umishenari wa tiba, ningesema, Mtumikie Bwana Yesu kwa ufahamu uliotakaswa, kuhusiana na wahudumu wa injili na Mwalimu mkuu. Yeye ambaye amekupa utume wako atakupa ujuzi na ufahamu unapojiweka wakfu kwa utumishi Wake, ukijishughulisha kwa bidii katika kazi na masomo, ukifanya yote uwezayo kuleta kitulizo kwa wagonjwa na wanadamu wanaoteseka. LLM 70.2

Kwa wale ambao wamechoshwa na maisha ya dhambi, lakini ambao hawajui wapi pa kugeukia ili kupata kitulizo/afueni, mwasilishe kwao Mwokozi Mwenye huruma, aliyejaa upendo na huruma kwao, akitamani kuwapokea wale wanaomjia kwa mioyo iliyovunjika na roho iliyotubu. Wachukue kwa mkono, wainue, sema nao maneno ya matumaini na ujasiri. Wasaidie kuushika mkono Wake Yeye aliyesema, “Na azishike nguvu Zangu, apate kufanya amani Nami, naam afanye amani nami.” LLM 70.3

“Tazama,” Kristo atangaza, “Naja upesi; na ujira Wangu u pamoja Nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo." Mungu anatuita sisi kutamka Maneno, “Amina! Njoo Bwana Yesu.” Mungu atafanya mengi zaidi kwa watu Wake ikiwa watakuwa na imani Kwake. Ukafiri unanyemelea nje ya nchi kupitia ardhini.

Shetani ameweka mipango yake ya kudhoofisha imani yetu katika historia na kusudi la kazi ya Mungu. Niko makini sana ninapoandika haya. Shetani anafanya kazi na watu walio katika vyeo maarufu ili kufagilia mbali misingi ya imani yetu. Je, turuhusu hili lifanyike, ndugu? LLM 70.4

Nafsi yangu imesisimka ndani yangu. Nitamtumaini Mungu kwa moyo na roho. Nitatangaza ujumbe ambao amenipa niutangaze. Ninashuhudia katika Bwana kwamba vijana wetu wasihamasishwe kwenda Battle Creek kufanywa kuwa makafiri. Mungu atatusaidia tuone ni nini kifanyike ili kuzuia hili. Sasa tunapaswa kufanya kazi kwa bidii na akili, katika kuwaokoa vijana wetu dhidi ya kuchukuliwa mateka na adui. LLM 70.5

Ndipo wataweza kuona kwa macho ya upako wa Roho mtakatifu, jinsi kazi ya umishenari wa tiba inavyounganishwa kwa ukaribu na utangazaji wa ujumbe wa wakati huu. LLM 70.6

Bwana amewasilisha mbele yangu hatari zinazowatishia watu Wake walio na kazi takatifu ya kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu kwa uwazi na udhahiri. Watu wa Mungu wanapaswa kujihadhari wasije wakanaswa na mapendekezo yasiyotakaswa. Vijana wetu hawapaswi kuwekwa mahali ambapo watapotoshwa na hisia zisizo sahihi. Ukweli sio wa kufumbiwa macho. Ujumbe wa siku hizi za mwisho haupaswi kutolewa kwa maneno yasiyo wazi. LLM 70.7

Kazi ya Umishenari wa tiba ingali changa. Maana ya kazi halisi ya umishenari wa tiba inajulikana na watu wachache. Kwa nini?—Kwa sababu pesa za Mungu zimetumiwa vibaya. Kazi za vitendo vya uinjilisti inafanywa. Wanaume na wanawake ambao wanapaswa kuwa shambani kama wamishenari wa tiba ili kusaidia wale wanaoshughulika na huduma ya injili, wanakusanywa hapo Battle Creek, wakisimamia mpango ule ule ambao umetekelezwa hapo awali, wakifunga majeshi, na kuwafunga. katika sehemu moja. Mungu amesema dhidi ya hili kwa kutuma hukumu Zake kwenye taasisi katika Battle Creek. Lakini kila harakati kwa upande wa wale wanaotii maonyo, ili wabadili mpangilio wa mambo, imefanywa kuwa ngumu sana na maoni potofu ya wengine kuhusu njia ambayo kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kuendelezwa. LLM 71.2

Mungu hajatupa kazi ya kujenga nyumba kubwa za sanitarium ili zitumike kama vituo vya afya kwa wote wanaokuja. Wala si kusudi Lake kwamba wamishenari wa tiba watumie muda mrefu chuoni kabla hawajaingia shambani. Wacha vijana wa kiume na wa kike wanaoijua Kweli waende kazini, si mahali ambapo Kweli imetangazwa tayari, bali mahali ambapo hawajasikia ujumbe, na watu hawa wafanye kazi kama wahubiri na wainjilisti. Waalimu wa vijana hawa wawaondoe

mahali ambapo Mungu ameonyesha kwa hukumu Zake kwamba hawapaswi kuwa... LLM 71.3

Wanaume na wanawake wengi watakuja kwenye Sanitarium mpya mjini Battle Creek, ambao si wagonjwa kabisa. Wafanyakazi watahitajika kuwahudumia. Lakini hii sio kazi ambayo Mungu amewapa wamishenari Wake wa tiba. Jukumu letu limetolewa kwetu na Mmshenari mkuu wa tiba ambaye ulimwengu huu umepata kumwona. Akiwa amesimama hatua chache tu kutoka kwenye kiti cha enzi cha Baba Yake, Kristo aliwaambia wanafunzi Wake, LLM 71.4

“Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu.” Hakuwaambia waanzishe seminari huko Yerusalemu, na wakusanye pamoja wanafunzi ili kufundishwa katika darasa la juu zaidi. “Enendeni ulimwenguni mwote,” Alisema, “mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe,” “na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” LLM 71.5

Msiwakusanye pamoja wale ambao Mungu amewapa utume huu, na kuwafanya waamini kwamba imewapasa kukaa miaka mingi chuoni ili kupata mafunzo kwa ajili ya kazi ya Bwana. Uwepo wa Kristo kuna thamani zaidi kuliko miaka ya mafunzo. Hebu vijana wetu wawe chini ya nira ya Kristo, na kwa imani waende mbele kama wamishenari wa tiba wa injili, wakichukua pamoja nao ahadi, “Tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” Hebu Waende wawili wawili, wakimtegemea Mungu, si mwanadamu, kwa hekima yao na mafanikio yao. Acha wayachunguze Maandiko, na kisha watoe zile Kweli za Neno la Mungu kwa wengine. Waongozwe na kanuni ambazo Mungu ameweka. LLM 72.1

Hebu wahudumu wetu ambao wamepata uzoefu katika kuhubiri Neno wajifunze jinsi ya kutoa tiba sahili, na kisha waende kama wainjilisti wamishenari wa tiba. LLM 72.2

Wafanyakazi,—wamishenari wa tiba wa injili—wanahitajika sasa. Hatuwezi kumudu kutumia miaka mingi katika maandalizi. Hivi karibuni milango iliyofunguliwa kwa Ukweli itafungwa milele. Beba ujumbe sasa. Usisubiri, kuruhusu adui kuchukua milki ya mashamba yaliyo sasa wazi mbele yako. Acha vikundi vidogo viende kufanya kazi ambayo Kristo aliwateua wanafunzi Wake. Acheni wafanye kazi kwa bidii kama waeneza-injili, wakitawanya machapisho yetu, kuzungumza juu ya Kweli na wale wanaokutana nao, wakiwaombea wagonjwa, na ikihitajika, wawatibu, si kwa dawa za kulevya au za famasia, bali

kwa tiba za asili. Watenda kazi wakumbuke daima kwamba wanamtegemea Mungu. Wasiwategemee wanadamu ili wapate hekima, bali wamtumaini Yeye asemaye, “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.” Hivyo tulifanya kazi katika historia ya mapema ya ujumbe.” LLM 72.3

Kutokana na nuru ambayo nimepewa, kazi ya umishenari wa tiba na huduma ya injili havipaswi kutenganishwa kamwe. Zinapaswa kuunganishwa pamoja kama kazi moja. Kristo Ndiye Kichwa cha mwili—Kanisa, na tunapaswa kufanya kazi kwa umoja pamoja Naye. Akirejelea uhusiano wetu Naye, mtume anasema, “Sisi tu watendakazi kazi pamoja na Mungu.” LLM 72.4

Katika siku za Kristo hapakuwa na nyumba za sanitarium katika Nchi takatifu ya Israeli. Lakini popote alipokwenda, Yeye Mwenyewe alikuwa sanitarium (au hospitali!). Tabibu Mkuu alibeba pamoja Naye uwezo wa uponyaji ambao ulikuwa ni tiba ya kila ugonjwa, wa kiroho na kimwili. Aliwapa afueni wale waliokuwa chini ya nguvu za adui, akawaponya magonjwa na udhaifu wao.... LLM 72A.1

Katika kufanya kazi ya umishenari wa tiba tutakutana na upinzani uleule ambao Kristo alikutana nao. Yeye Anatangaza hivi: “Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya Jina Langu; Watakapowaudhi katika mji huu, kimbilieni mwingine; kwa maana, amin, nawaambia, Hamtaimaliza miji ya Israeli, hata ajapo Mwana wa Adamu. LLM 72A.2

Tunapaswa kuwafundisha wengine jinsi ya kupata uzima wa milele. Na tunapaswa kukumbuka daima kwamba ufanisi wa kazi ya umishenari wa tiba ni katika kuwaelekeza wanaume na wanawake wagonjwa kwa Yesu. Tunapaswa kuwaita “wamtazame Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu.” LLM 72A.3

Maisha ya Kristo na huduma Yake kwa watu wanaoteseka yanaunganishwa bila kutenganishwa. Na leo Yeye ni Tabibu Yule Yule Mwenye huruma. Tunapaswa kuwaruhusu wote wanaoteseka waelewe kwamba ndani Yake mna zeri ya uponyaji kwa kila ugonjwa, kurejesha nguvu kwa kila udhaifu. LLM 72A.4

Ulimwengu umejitenga mbali na kanuni za Kweli za urejesho na afya. Tamaa iliyopotoka na shauku za kuelekea chini zimechukua udhibiti wa akili za wengi. Mara nyingi mwelekeo wa kukasirika huimarishwa na kupaliliwa. Hasira mbaya, kuthaminiwa, na huharibu mitazamo nyeti, safi, mitakatifu ya roho. Shetani anatamani kutufanya tuhangaike na kunyanyaswa kwa mambo madogo tu, ili tusahau mambo mazito yanayohusu ustawi wetu wa milele. LLM 72A.5

Bwana anatamani kila mtu afanye sehemu yake kwa ubora. Unaweza kufikiri kwamba unaweza kufanya kidogo sana; lakini kumbuka kwamba katika mfano wa talanta, Kristo hakuwawakilisha watumishi wote wakipokea kiasi kile kile. Mtumishi mmoja alipewa talanta tano; kwa mwingine, wawili, na kwa mwingine, mmoja. Ikiwa una talanta moja tu, itumie kwa busara, ukiongeza kwa kuipeleka kwa wabadilishanaji. Fanya uwezavyo kurudisha nyuma wimbi la magonjwa na mateso ambalo linaenea katika ulimwengu wetu. Njooni kwa msaada wa Bwana, kwa msaada wa Bwana dhidi ya nguvu kuu za giza- Waamuzi 5:23. LLM 72A.6

Kazi hii ya zahanati ya tiba ambayo Ndugu Sadler ametueleza, ni sawa na kazi tuliyofanya huko Australia. Tulipokuwa Cooranbong, hapakuwa na tabibu kwa umbali wa maili nyingi kutoka kwetu; na muuguzi wangu, mwanamke mwenye uzoefu katika kutibu wagonjwa, alitenda kazi ya nafasi ya daktari katika jumuiya yetu. Aliitikia miito mingi, akisafiri kutoka mahali hadi mahali na kufanya kazi ambayo Mungu anataka wengine wengi wafanye. Katika kazi hii, wengine hawawezi kufanya mengi kama wengine, lakini kila mmoja anapaswa kufanya awezavyo ili kuondoa mateso. Mungu anataka kila mmoja wa watoto Wake awe na akili na maarifa, ili kwa nguvu, utukufu Wake udhihirishwe katika ulimwengu wetu kwa wazi kabisa. LLM 72B.1

Katika kazi ya umishenari wa tiba lazima kuwe na matamanio zaidi ya roho za watu. Shauku hii ndiyo iliyojaza mioyo ya wale walioanzisha taasisi yetu ya kwanza ya tiba. Kristo anapaswa kuwepo katika chumba cha wagonjwa, akiujaza moyo wa daktari harufu ya upendo Wake. Wakati maisha yake yanapokuwa hivi, Kristo anaweza kwenda pamoja naye kando ya kitanda cha wagonjwa, na utawajia usadikisho kwamba Yeye, Mwokozi Mwenye huruma, Yuko, na kisha usadikisho huo utafanya mengi katika kuwarudishia afya zao. LLM 72B.2

Kwa maneno na vitendo matabibu na wauguzi katika taasisi zetu za tiba wanapaswa kusema, kwa uwazi sana, kiasi kwamba haiwezi kueleweka vibaya, "Mungu Yuko mahali hapa," kuokoa, sio kuharibu. Kristo anawaalika waganga wetu kumfahamu. Wanapoitikia mwaliko Wake, watajua kwamba wanapokea mambo wanayoomba. Akili zao zitaangazwa na hekima itokayo juu. Wakimtazama Mwokozi mara kwa mara, watafanana kama Yeye zaidi na zaidi, hadi mwishowe inaweza kusemwa juu yao katika nyua za mbinguni, “Ninyi mmetimilika katika Yeye.” Kristo amejitolea kuwapa wanafunzi Wake kile wanachoomba kwa Jina Lake. Wanapofanya kazi kwa kupatana Naye, wanaweza kumwomba Yeye kuwasaidia katika kila wakati wa hitaji. LLM 72B.3

Soma sura ya nane ya Mathayo, na ujifunze kutoka kwayo jinsi Kristo alivyounganisha huduma ya Neno na kazi ya umishenari wa tiba. Jifunze mbinu za Mponyaji mkuu, na fanya kazi kama Yeye alivyofanya kazi. LLM 73.1

Wale wanaodai kuwa wamishenari wa tiba wanapaswa kuwekwa wakfu, wakifanya kazi kwa ajili ya maslahi ya ulimwengu, lakini hawajanaswa na hila za ulimwengu. Bwana anataka uwe chombo cha heshima... LLM 73.2

Maneno yafuatayo yanaeleza kwa muhtasari kazi ya Kweli ya umishenari wa injili,—kazi ambayo wote watashiriki, naam wale ambao wameongoka kikweli: (Ona MS. kwa Maandiko mengi.) LLM 73.3

Wafanyakazi wa kimishenari wa tiba wanahitajika katika uwanja wa Kusini mwa nchi, ambao wanaweza kushiriki katika kazi ya Sanitarium. Sanitarium zinahitajika, ambazo mafanikio ya kazi ya tiba na upasuaji inaweza kufanyika. Taasisi hizi, zinazoendeshwa kwa mujibu wa mapenzi ya Mungu, zingeondoa ubaguzi, na kufanya kazi yetu ionekane vizuri. Lengo kuu la watendakazi katika taasisi hizi ni kuwa na afya ya kiroho ya wagonjwa. Kazi ya uinjilisti yenye mafanikio inaweza kufanywa kuhusiana na kazi ya umishenari wa tiba. Ni jinsi mistari hii ya kazi inavyounganishwa ndipo tunaweza kutarajia kukusanya tunda la thamani zaidi kwa Bwana. LLM 73.4

Kutokana na maagizo ambayo Bwana amenipa mara kwa mara, ninajua kwamba kunapaswa kuwa na watendakazi wanaofanya safari za uinjilisti wa tiba kati ya miji na vijiji. Wale wanaofanya kazi hii watakusanya mavuno mengi ya roho, kutoka kwenye tabaka za juu na za chini. Njia ya kazi hii imeandaliwa vyema zaidi na juhudi za mwinjilisti wa vitabu. LLM 73.5

Wengi wataitwa shambani kufanya kazi ya nyumba kwa nyumba, kusoma Biblia, na kusali pamoja na wale wanaopendezwa. LLM 73.6

Ni muhimu sana kuwepo na maelewano katika taasisi zetu. Afadhali kazi ilemae kuliko watendakazi ambao hawajajitolea kikamilifu kuajiriwa. Ni wale ambao hawajawekwa wakfu, ambao hawajaokoka ambao wamekuwa wakiharibu kazi ya Mungu. Bwana hana matumizi yoyote na watu ambao hawajajiweka wakfu kabisa kwa utumishi Wake. LLM 73.7

Mioyo na maslahi ya watenda kazi wa Mungu vinapaswa kuwa kitu kimoja. Watenda kazi wanapaswa kufungwa pamoja na Kristo, na kuheshimiana wao kwa wao ni jambo la juu kwa ajili ya kazi yao… LLM 73.8

Kazi iliyoamuliwa zaidi inahitaji kufanywa katika makanisa yetu huko Michigan. Kumekuwa na ukosefu wa ushirikiano na vitendo vyenye upatanifu, lakini ikiwa nyote mtafuata kwa uthabiti mistari ya Biblia, badiliko litafanyika katika makanisa..... LLM 74.1

Ninatumaini kwamba sasa, kuliko wakati mwingine wowote, ninyi nyote,—wahudumu na washiriki wa kanisa—mtakuja kwa msaada wa Bwana, kwa msaada wa Bwana dhidi ya nguvu kuu za giza (Waamuzi 5:26). Lakini nimeandika mambo mengi sana, hivi kwamba sihitaji kuwaandikia kwa sehemu kubwa. Nitauliza kwa nini baadhi ya ndugu zetu wachungaji wako nyuma sana katika kutangaza mada iliyotukuka ya kiasi? (temperance) Kwa nini, nia kubwa zaidi haionyeshwi katika matengenezo ya afya? Kuna wengi wanaolisha na kuiweka hai chuki ya mara kwa mara dhidi ya Dk. Kellogg. Daktari huyu anafanya kazi kubwa. Kwa nini watu hawa wasijaze nafasi zao katika huduma pia, kwa bidii kama vile yeye anavyojaza nafasi yake? Kwa nini wahudumu wa makanisa yetu hawafanyi kazi ile ile ambayo ilipaswa kufanywa miaka mingi iliyopita? Ninafurahi kwamba mtu fulani ameichukua kazi ambayo imepuuzwa sana. LLM 74.2

Malalamiko yanakuja kwa viongozi kwamba Dk. Kellogg amekusanya vijana wote anaoweza kupata, na kwa hiyo sisi hatuna watendakazi. Lakini hili ndilo jambo bora zaidi ambalo lingeweza kufanywa kwa vijana na kazi. (Haya yaliandikwa takribani 1898) Hebu tuchunguze tarehe kama hizo kwa uangalifu, ili tusichanganywe na Shetani. Muda mfupi baada ya habari hizo hapo juu kuandikwa, Dada White aliona ni muhimu kutoa shauri dhidi ya kuwapeleka vijana Battle Creek kwa sababu kazi ilikuwa kubwa sana na Dakt. Kellogg alifundisha makosa mengi yaliyochanganyika na mwanga mwingi uliokuwa tofauti na Maandiko (pantheismu nk).— Copyist, ERP) LLM 74.3

Kwako, (maneno hayapo kwenye ukurasa) kama Mwenyekiti wa General Konferensi, na kwa Ndugu Evans, Mwenyekiti wa union Konferensi Kuu, na kwa Ndugu Durland, kama Mwenyekiti wa Konferensi ya Michigan, ningesema, Endelea kufanya kazi kwa busara na kwa hekima. Pata baadhi ya hawa vijana wa kiume na wa kike kufanya kazi makanisani. Unganisha kazi ya umishenari wa tiba na tangazo la ujumbe wa malaika wa tatu. Fanya juhudi za mara kwa mara, zilizopangwa ili kuyainua makanisa kutoka katika kiwango kilichokufa ambacho yamekuwa humo kwa miaka mingi. Tuma wahudumu wa makanisa ambao wataweka kanuni za matengenezo ya afya mbele kwa kila kanisa huko Michigan. Utaona jinsi pumzi ya uhai itakavyoingia katika makanisa haya. LLM 74.4

Kipengele kipya kinahitaji kuletwa kwenye kazi. Watu wa Mungu lazima wapokee maonyo, na kufanyia kazi roho pale walipo; kwa maana watu hawatambui hitaji lao kuu na hatari. Kristo aliwatafuta watu mahali walipo, na kuweka mbele yao zile Kweli kuu kuhusu ufalme Wake. Alipoenda kutoka mahali hadi mahali, Aliwabariki na kuwafariji walioteseka, na kuwaponya wagonjwa. Hii ni kazi yetu. Mungu angetaka tuwasaidie wasio na mahitaji. Sababu ya kwamba Bwana haonyeshi uwezo Wake kwa kudhamiria zaidi ni kwa sababu kuna hali ya kiroho ndogo sana miongoni mwa wale wanaodai kuuamini Ukweli. LLM 74.5

Katika ulimwengu wetu kuna wafanyakazi wengi Wakristo ambao bado hawajasikia zile Kweli kuu na za ajabu ambazo zimetujia. Hawa wanafanya kazi nzuri, kwa mujibu wa nuru waliyo nayo, na wengi wao wameendelea zaidi katika elimu, na kazi ya vitendo kuliko wale ambao wamekuwa na nuru kubwa na fursa kubwa. LLM 75.1

Kutojali miongoni mwa wahudumu wetu kuhusiana na matengenezo ya afya na kazi ya umishenari wa tiba , kunashangaza. Hata wale ambao ambao hawadai kuwa Wakristo wanalitendea somo hilo kwa heshima kubwa kuliko baadhi ya watu wetu wenyewe, na wanatangulia mbele yetu. Neno nililopewa kwa ajili yako ni, “Nenda mbele.” “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari....” LLM 75.2

Ndugu. Irwin, shikilia kazi ya mageuzi ya afya. Ikiwa yeyote kati ya wahudumu ana wazo kwamba kazi ya umishenari wa tiba inazidi kuwa ngumu, acha wachukue wanaume ambao wamekuwa wakifanya kazi katika safu hizi pamoja nao kwenye nyanja zao za kazi, wawili hapa na wawili pale. Hebu wahudumu wawapokee wamishenari hawa wa tiba kama ambavyo wangempokea Kristo, na kuona ni kazi gani wanaweza kufanya. Sidhani kama watawaona vijana katika uzoefu wa kidini kama waliokuwa nao. Angalia kama kwa njia hii, huwezi kuleta baadhi ya mkondo muhimu wa mbinguni kwenye makanisa. Angalia kama hakuna tabaka ambalo litashika elimu wanayohitaji sana, na uone kama hawatatoa ushuhuda, “Lakini Mungu, ambaye ni mwingi wa rehema, kwa upendo Wake mkuu aliotupenda sisi, hata tulipokuwa wafu katika dhambi, alituhuisha pamoja na Kristo, (si mbali na Kristo), (mmeokolewa kwa neema) akatufufua pamoja Naye, akatuketisha pamoja (si katika atomi za kujitegemea) katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu. ” LLM 75.3

Katika kazi yetu ya Washington, madaktari wenye busara, wenye uwezo, wasimamizi bora, na wauguzi walio na sifa bora zaidi watahitajika. Vijana wenye bidii, waliojitolea pia watahitajika, kuingia kazini kama wauguzi. Vijana hawa wa kiume na wa kike wataongezeka katika uwezo wanapotumia kwa uangalifu ujuzi wanaopata, na watakuwa bora na wenye kustahili kuwa mkono wa msaada wa Bwana. Wanaweza kuwa wamishenari waliofaulu, wakielekeza roho kwa Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu, na ambaye ufanisi Wake wa uponyaji unaweza kuokoa roho na mwili. LLM 75.4

Bwana anataka wanaume na wanawake wenye hekima, wanaotenda kazi kama wauguzi, kuwafariji na kuwasaidia wagonjwa na watu wanaoteseka. Kupitia huduma za wauguzi hawa, wale ambao hapo awali hawajapendezwa na mambo ya kidini/kiroho wataongozwa kuuliza, “Nifanye nini ili nipate kuokolewa?” Wagonjwa wataongozwa kwa Kristo kwa usikivu na subira za wauguzi wanaohudumia mahitaji yao, na ambao huinama kwa sala na kumwomba Mmishenari mkuu wa tiba umtazame mgonjwa kwa huruma, na kuruhusu mvuto wa neema Yake usikike na kurejesha nguvu kutekelezwa. Laiti wote walio wagonjwa na wanaoteseka wangeweza kuhudumiwa na matabibu na wauguzi wanaofanana na Kristo, ambao wangewasaidia kuiweka miili yao iliyochoka, na yenye maumivu makali chini ya uangalizi wa Mponyaji mkuu, kwa imani wakimtazamia kwa urejeshwaji. LLM 75.5

Woga wa neva za wagonjwa utashindwa wanapofahamishwa na shauku kubwa ambayo Mwokozi anayo kwa wanadamu wote wanaoteseka. Ee, Ni kina cha upendo mkubwa kiasi gani, alicho nacho Kristo! Ili kutukomboa kutoka kwa kifo, alipokufa msalabani Kalvari. LLM 76.1

Hebu waganga wetu na wauguzi daima wakumbuke Maneno, “Sisi ni watenda kazi pamoja na Mungu.” Hebu kila daktari na kila muuguzi ajifunze jinsi ya kufanya kazi kwa ajili ya kupunguza mateso ya kiakili na kimwili. Kwa wakati huu, wakati dhambi imeenea sana na kufunuliwa kwa ukali sana, ni muhimu jinsi gani kwamba huduma zetu za sanitarium zifanywe kwa njia ambayo zitatimiza kiasi kikubwa cha wema. Ni muhimu sana kwamba watendakazi wote katika taasisi hizi wajue jinsi ya kunena neno kwa wakati kwa wale waliochoka na wagonjwa. LLM 76.2

Madaktari na wauguzi wanapaswa kuwa wenye fadhili na furaha, wakiondoa huzuni na sikitiko zote. Hebu imani ishike mkono wa Kristo kwa mguso Wake wa uponyaji... LLM 76.3

Wauguzi wetu wanapowahudumia wagonjwa wa mwili na roho kwa subira, wamuombe Mungu awafanyie kazi wanaoteseka, wapate kuongozwa kumjua Kristo, na waamini kwamba maombi yao yatajibiwa. Katika yote yanayofanyika, upendo wa Kristo na udhihirishwe. LLM 76.4

Kila Mkristo mwaminifu huinama kwa Yesu kama daktari wa kweli wa roho. Bwana Atakaposimama kando ya kitanda cha walioteseka, kutakuwa na wengi, sio tu walioongoka, bali ambao wameponywa, Yeye aliyetangaza, "Mimi Ndimi Njia, na Kweli, na Uzima," atakuwa pamoja na matabibu na wauguzi wake waaminifu wakiwa wanajitahidi kushirikiana Naye. Ikiwa kwa njia ya huduma ya busara mgonjwa anaongozwa kutoa roho yake kwa Kristo, na kuleta mawazo yake katika utii wa mapenzi ya Mungu, ushindi mkubwa hupatikana. LLM 76.5

B 29 '05 (Imenakiliwa Januari 1, '05)

Lo! jinsi ninavyotamani kuona kazi ikienda kwa nguvu katika miji ya New Bedford na Fairhaven, na katika maeneo mengine mengi tu yaliyo na uhitaji mkubwa wa Ukweli kama vile maeneo haya. Tunatumai kwamba wakati fulani kituo cha sanitarium kinaweza kuanzishwa New Bedford. Wafanyakazi Wamishenari wa tiba wanahitajika katika miji kama hiyo. Lakini, dada mpendwa, inahitajika talanta isiyo na uwezo wa kawaida kusimamia huduma za sanitarium. Wanaume wenye uzoefu, waliojaribiwa na kutahiniwa lazima washikilie kazi hiyo. Kwamba sehemu ya watendakazi wanaojitolea kuanzisha taasisi hiyo wana uzoefu na sifa, haitoshi. Kwa ajili yao wenyewe, kwa ajili ya taasisi, na kwa ajili ya kusudi kwa ujumla, ni muhimu kwamba idadi kamili ya wanaume na wanawake waliohitimu vizuri ipatikane kuingia kwenye kazi. Jicho la Bwana liko juu ya shamba zima, na wakati umefika wa taasisi kuanzishwa katika uwanja fulani, Yeye anaweza kugeukia mahali hapo ambapo akili za wanaume na wanawake zilizoandaliwa vyema ziingie kwenye taasisi hiyo. LLM 76.6

Kuna mistari mingi ya kazi inayopaswa kuendelezwa. Kuna fursa kwa wauguzi walioelimishwa na kuzoezwa vizuri kwenda miongoni mwa familia na kuamsha shauku ya kupendezwa katika familia. Kuna hitaji la dharura la wainjilisti wengi na watendakazi wanaoendeleza darasa la Biblia katika miji kama vile Boston na New Bedford. Wafanyakazi hao wangepata fursa nyingi za kupanda mbegu nzuri. Kuna kazi kwa kila mtendakazi mwenye juhudi makini na mwenye bidii. Mafundisho ya Kristo ya Kweli rahisi zinazofundishwa na mifano Yake, yanahitajika sana leo kama ilivyokuwa wakati alipokuwa ulimwenguni ana kwa ana. LLM 77.1

*****

O, -55 '05 (Imenakiliwa Januari 30, '05)

Bwana alinipa mwanga mkubwa juu ya matengenezo ya afya. Kuhusiana na mume wangu nilipaswa kuwa mfanyakazi wa kimishenari wa tiba. Nilipaswa kuweka mfano kwa kanisa kwa kuwapeleka wagonjwa nyumbani kwangu na kuwatunza. Hii nimefanya, mimi mwenyewe kwa kuwapa wanawake na watoto tiba zenye nguvu zaidi. Pia nilipaswa kuzungumza juu ya somo la kiasi cha Kikristo, kama mjumbe aliyeteuliwa na Bwana. Nilijishughulisha kwa moyo wote katika kazi hii, na nilizungumza na mkutano mkubwa juu ya kiasi kwa maana yake pana na ya kweli... LLM 77.2

Tulipokuwa Australia tulifanya kazi kama wamishenari wa tiba katika kila maana ya neno hili. Nyakati fulani nilijenga nyumba yangu huko Cooranbong, kama makao ya wagonjwa, na walioteseka. Katibu muhtasi wangu, ambaye alikuwa amepata mafunzo huko Battle Creek Sanitarium, alisimama kando yangu, na kufanya kazi ya mmishenari muuguzi. Hakuna malipo yoyote yaliyotolewa kwa ajili ya huduma yake, nasi tulipata ujasiri wa watu kwani walipendezwa na tulisaidia wagonjwa na wanaoteseka. Baada ya muda Retreat ya Afya huko Cooranbong ilijengwa, na kisha tukaondolewa mzigo huu. LLM 77.3

B. 59 '05 (Imenakiliwa Feb. 4 '05) LB 38, p. 173.

Wauguzi wanaohusishwa na taasisi hizi wanapaswa kuwa tayari kutoa ushawishi wa kuokoa roho. Wale wasio na mizizi na msingi katika Ukweli hawapaswi kuajiriwa. Waache kwanza wathibitishwe katika Kweli. Basi na wajifunze kuwa macho siku zote, wakitafuta daima kutoa maoni yanayofaa katika akili za wagonjwa... LLM 77.4

Wauguzi wanapaswa kuonyesha kupendezwa na kuwa wachangamfu kila wakati, na wanapaswa kuonyesha kufikiria wenzao. Wanapaswa daima kujitahidi kufanya kazi yao kwa hekima na kwa uzuri, wakitambua kwamba wanamtumikia Bwana, na kwamba katika kutekeleza wajibu wao wanapaswa kuishi mbele ya wasioamini imani yao katika Ukweli kwa wakati huu. LLM 78.1

Uangalifu mkubwa unapaswa kuonyeshwa katika kuchagua vijana wa kuungana na sanitariums zetu. Wale ambao hawana upendo na Ukweli katika nafsi hawapaswi kuchaguliwa. Wagonjwa wanahitaji kuambiwa maneno ya busara. Mvuto wa kila mfanyakazi unapaswa kuibua akilini kupenda dini ya Kristo. Nuru imetolewa kwangu kwamba vijana waliochaguliwa kuungana na nyumba zetu za usafi wanapaswa kuwa wale ambao wana ushahidi kwamba wamekuwa wanafunzi wanaofaa katika shule ya Kristo... LLM 78.2

Wauguzi wanapaswa kuwa na mafundisho ya Biblia ya kawaida, ili waweze kuzungumza na wagonjwa maneno ambayo yatawaelimisha na kuwasaidia. Malaika wa Mungu wako katika vyumba ambamo watu wanaoteseka wanapaswa kutibiwa, na hali inayozunguka roho ya yule anayetoa matibabu inapaswa kuwa safi na yenye harufu nzuri. Katika maisha ya waganga na wauguzi wema wa Kristo unapaswa kuonekana. Kanuni Zake ni za watu kuishi. Kisha, kwa kile wanachofanya na kusema, wagonjwa watavutwa kwa Mwokozi… LLM 78.3

Ni kuokoa roho, na pia kuponya miili ya wanaume na wanawake, kwamba huduma zetu za sanitarium zimeanzishwa kwa gharama kubwa. Mungu anakusudia kwamba kupitia kwao, matajiri na maskini, walio juu na chini, watapata mkate kutoka mbinguni na maji ya uzima… LLM 78.4

Muuguzi Mkristo mwenye uzoefu katika chumba cha wagonjwa atatumia tiba bora zaidi anazojua ili kumrudishia mgonjwa afya yake. Naye atamvuta kwa furaha na kwa mafanikio yule ambaye anamfanyia kazi kwa Kristo, Mponyaji wa roho na mwili pia. Masomo yaliyotolewa, mstari juu ya mstari, hapa kidogo na pale kidogo, yatakuwa na ushawishi wake Wauguzi wakubwa, wawe wanaume au wanawake, wasipoteze nafasi yoyote ya kuita usikivu wa wagonjwa kwa Kristo. Wale wanaowatunza wagonjwa wanapaswa kuwa tayari kuchanganya uponyaji wa kiroho na uponyaji wa kimwili. Wauguzi katika vyumba vyetu vya sanitarium waonyeshe kwamba katika kazi nzito ya kutunza wagonjwa, hawategemei dawa za kulevya (drugs with patents or copyrighted), bali nguvu za Kristo, na matumizi ya tiba rahisi ambazo ametoa, - matumizi ya maji moto na baridi na chakula sahili, chenye lishe, bila kileo cha aina yoyote, pamoja na mazoezi ya busara, na kuachana na mazoea yote mabaya. Katika matibabu kama haya kuna afya kwa wagonjwa. LLM 78.5

UFUNDISHAJI NA UPONYAJI

Haja ya ulimwengu ya kufundisha na uponyaji haijawahi kuwa kubwa kuliko ilivyo leo. Ulimwengu umejaa wale ambao wanahitaji kuhudumiwa, - wanyonge, dhaifu, wasio na ufahamu, wagonjwa. Ukiukaji wa sheria za afya wa mwanadamu mara kwa mara kwa karibu miaka elfu sita umeleta magonjwa, maumivu, na kifo kama matunda yake. Umati wa watu unaangamia kwa kukosa maarifa. Wakati wahudumu wa Mungu wanapoona matokeo mabaya ya dhambi iliyoendelea kwa

muda mrefu, mioyo yao imeguswa na ole ya ulimwengu, na wanajitahidi kufanya kazi kama Mtendakazi Mkuu na wanafunzi Wake walivyofanya kazi. Kuunganishwa na Mponyaji wa Mbinguni, kutasaidia kwenda kwa nguvu za uweza Wake kufundisha na kuponya. Wanatambua kwamba injili ndiyo dawa pekee ya dhambi, na kwamba kama mashahidi wa Kristo wanapaswa kutoa ushuhuda juu ya nguvu Zake.

Wanapowaelekeza wale waliotaabika kwa Mwana-Kondoo wa Mungu, ambaye huondoa dhambi ya ulimwengu, neema Yake inayobadilisha na nguvu ya kufanya miujiza inasababisha wengi kukubali ujumbe wa Ukweli unaobebwa. Nguvu Yake ya uponyaji, iliyounganishwa na ujumbe wa injili, inaleta mafanikio katika dharura. Roho Mtakatifu anafanya kazi juu ya mioyo, na wokovu wa Mungu unafunuliwa.

Wahubiri, waganga, na wauguzi wanapaswa kuunganisha kazi zao. Lakini hitaji la ulimwengu leo haliwezi kutimizwa kikamilifu na huduma ya watumishi wa mungu ambao wameitwa kuhubiri injili ya milele kwa kila kiumbe. Ingawa ni vizuri, kwa kadiri inavyowezekana, kwa wafanyikazi wa kiinjili kujifunza jinsi ya kuhudumia mahitaji ya mwili na roho, kwa hivyo kufuata mfano wa kristo, lakini hawawezi kutumia wakati wao wote na nguvu katika kuwasaidia wakihitaji msaada. Bwana ameamuru kwamba pamoja na wale wanaohubiri neno watahusishwa pia watendakazi wake wa kimishenari wa tiba, madaktari na wauguzi wa kikristo, ambao wamepata mafunzo maalum katika uponyaji wa magonjwa na katika kuzileta roho kwa kristo.

Wamishenari wa tiba na watendakazi katika huduma ya injili wanapaswa kufungwa pamoja na mahusiano yasiyofutwa. Kazi yao inapaswa kufanywa kwa upya na nguvu. Kwa juhudi zao za pamoja, ulimwengu unapaswa kuwa tayari kwa ujio wa pili wa kristo. Kupitia kazi yao ya pamoja, jua la haki litachomoza, likiwa na uponyaji katika mabawa yake, na kupeperusha kwenye maeneo yasiyo na nuru ya dunia, ambapo watu wameishi kwa muda mrefu katika giza kuu. Wengi ambao sasa wanaishi katika uvuli wa dhambi na mauti, wanapoona kwa watumishi waaminifu wa mungu mwangaza wa nuru ya ulimwengu, watatambua kuwa wana tumaini la wokovu, na watafungua mioyo yao kupokea mihimili ya uponyaji, na sisi tutakuwa wachukuaji wa nuru kwa wengine ambao bado wamo katika giza.

Sanitariamu (Nyumba za kusaidia wagonjwa kwa tiba rahisi za asili)-Japo Kristo hayupo tena hapa ulimwenguni kimwili, lakini Yeye ametuamuru kuendeleza kazi ya umishenari wa tiba aliyoanza; na katika kazi hii tunapaswa kufanya bidii yetu

yote. Kwa maendeleo ya kazi hii taasisi za utunzaji wa wagonjwa zinapaswa kuanzishwa, ambapo wanaume na wanawake wanaougua magonjwa wanaweza kuwekwa chini ya uangalizi wa matabibu na wauguzi wanaomcha Mungu. ' Bwana ameamuru kwamba vituo vya sanitariamu vianzishwe mahali pengi kusimama kama kumbukizi ya kazi Yesu aliyoifanya akiwa duniani.

Hii ni mojawapo ya njia Zake teule za kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu, yaani injili ya milele ya kutayarisha watu kusimama katika hukumu wakiwa bila mawaa au hatia. Kwa njia hii Ukweli utawafikia wengi ambao wangekuwa wazito kusikia Habari njema ya Msalaba. Lakini kwa mashirika mengine yaliyo na injili kavu peke yake, kamwe hawataangazwa na mwangaza wa ujumbe wa injili ila tu kwa njia ya kujali afya yao kwa njia rahisi. Katika uwasilishaji wa Ukweli, wengine watavutiwa na awamu moja ya ujumbe wa injili na wengine na njia nyingine. Tumeagizwa na Bwana kufanya kazi kwa njia ambayo madaraja yote yatafikiwa. Ujumbe lazima uende kwa ulimwengu wote, hata ule wa Kiswahili

Kazi yetu ya Sanitarium, usafi na afya ni kusaidia kuongeza idadi ya watu wa Mungu. Kupitia safu hii ya juhudi za kimishenari makafiri watageuzwa na kuwa wacha Mungu. Kwa urejeshwaji mzuri unaofanyika katika nyumba zetu za Sanitarium wengi wataongozwa kumtazama Kristo kama mponyaji wa roho na mwili.

Watendakazi wa kujitolea, ambao wana imani kamili kwa Mungu, wanapaswa kuchaguliwa kuchukua jukumu la taasisi hizi. Wanaume na wanawake wenye busara, wanaofanya kazi kama wauguzi, wanapaswa kuwafariji na kuwasaidia wagonjwa na wanaoteseka. Usafi wetu unapaswa kuwa kama taa inayoangaza mahali penye giza, kwa sababu waganga, wauguzi, na wasaidizi wanaonyesha mwangaza wa jua wa haki ya Kristo.

Nyumba za afya na usafi, yaani sanitarium zinapaswa kuanzishwa na kuendeshwa hivi kwamba zitakuwa zenye kuelimisha kwa tabia. Zinapaswa kuuonyesha ulimwengu wema wa mbinguni. Ingawa uwepo wa Kristo hauonekani kwa macho leo, lakini watendakazi wanaweza kudai ahadi hii, "Tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata mwisho wa ulimwengu." Amewahakikishia wafuasi Wake kwamba kwa wale wanaompenda na kumcha Yeye atawapa nguvu ya kuendelea na kazi aliyoianza. Alizunguka-zunguka akitenda mema, akiwafundisha wasiojua au wajinga, na kuponya wagonjwa. Kazi Yake haikuacha maonyesho ya nguvu Zake juu ya magonjwa (miujiza). Alifanya kila kazi ya uponyaji, tukio la kuingiza ndani ya moyo kanuni za Mungu za upendo na ukarimu. Kwa hivyo wafuasi Wake wanapaswa kufanya kazi. . . ……

Mungu amewahitimisha watu Wake kuangaza ulimwengu. Amewapa wanaume vitivo vinavyowabadilisha ili kupanua bidii zao na kukamilisha kazi ambayo italinda ulimwengu.

Kumbuka:

- Mashauri juu ya Afya, ukurasa wa 497-499.
- Mashauri kwa Wazazi na Walimu, uk. 467-469.
- The Review and Herald, Mei 2, 1912.

MAENDELEO YA UMISHENARI WA TIBA/KITABIBU

Kristo hayupo tena hapa ulimwenguni kwa binafsi, lakini ametuamuru kuendeleza kazi ya umishonari ya matibabu aliyoanza; na katika kazi hii tunapaswa kufanya bidii yetu yote. Kwa maendeleo ya kazi hii ya kutunza wagonjwa ili wanadamu wanaougua magonjwa wanaweza kuwekwa chini ya uangalizi wa matabibu na wauguzi wanaomcha Mungu. '

Ni vyema kwetu kwamba tuna vituo vya tiba rahisi yaani Sanitarium na migahawa ya chakula cha afya (Hygeine restaurant). Hii ni moja wapo ya njia za Mungu teule za kutangaza ujumbe wa malaika watatu. Kwa njia hii Ukweli utawafikia wengi ambao, wasingepata ujumbe wa injili, na hivyo makundi yote yaweze kufikiwa. Kupitia tiba rahisi makafiri watageuzwa nao wataongozwa kumtazama Kristo kama mponyaji wa roho na mwili. Wauguzi wa nyumbani au kwenye taasisi, wanapaswa kuwafariji na kuwasaidia wagonjwa na watu wanaoteseka.

Huduma yetu ya tiba inapaswa kuwa kama taa inayoangaza mahali penye giza, kwa sababu madaktari, wauguzi, na wasaidizi wanaonyesha mwangaza wa jua wa haki ya Kristo na wema wa mbinguni. Ingawa uwepo wa Kristo hauonekani, lakini watendakazi wanaweza kudai ahadi hii, "Tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata mwisho wa ulimwengu." Bwana amewahakikishia wafuasi Wake kwamba kwa wale wanaompenda na kumcha Yeye, atawapa nguvu ya kuendelea na kazi aliyoanza. Alizunguka-zunguka akitenda mema, akiwafundisha wasiojua/wajinga, na kuponya wagonjwa. Kazi Yake haikukoma na maonyesho ya nguvu Zake juu ya magonjwa. Mungu amewastahilisha watu Wake kuangaza ulimwenguni. Amewapa watu vitivo vinavyowabadilisha ili kupanua bidii zao na kukamilisha kazi ambayo italinda ulimwengu.'

*Wale wote wanaompenda Mungu ni vyema wajue kwamba kuna njia nyingi za Tiba ambazo haziendani na imani yetu, na kuna mstari mwembamba wa

kuzitofautisha wakati mwingine. Hapa amezungumza njia ya tiba ya maji waliyotumia ambayo ilikuwa na mambo ya giza. Hivyo anashauri kufungua vituo vya tiba rahisi kwa kutumia vitu kama maji hayo hayo, ila wajielekeze kwenye mambo ya Mungu wa mbinguni maana Ndiye Mponyaji, na Tabibu Mkuu (tiba zingine ambazo Wakristo hawapaswi kutumia ni kama hyponotism, reiki, yoga, ramli, ayuverdic, uaguzi, wabashiri, kusoma mikono, uaguzi nk).

Hapa ndiyo walianza vituo vyao vya tiba rahisi –(Sanitarium-Hygienic Institute), pia kulikuwa na migahawa ya afya (Hygeneic restaurants). Ukisoma zaidi hata Dr Kellog tabibu alikuja na nadharia ya Patheismu ambayo inapingana na Maandiko, kwamba Mungu si Nafsi hai, ila ni uwepo tu kwenye miti, mimea na kila kitu. Japo alikuwa muumini, alikataa kushauriwa, mchungaji wa mke wake alimwambukiza nadharia hii. Hakuna binadamu aliye na elimu yote, ushauri na maonyo ni muhimu na kuomba Mungu atusaidie maamuzi wakati wa dhiki ya ugonjwa au muafaka ili tusiingie gizani kirahisi.Mara nyingi mtu akiumwa, anaweza kughafilika katika maamuzi na kuelekea kwenye tiba ambazo ziko kinyume ya imani.

Njia mbali mbali za giza ambazo tusizifuate kwetu Afrika ni kama kwenda kwa wachawi au waganga wa kienyeji, kusoma mikono, kubashiri, kupiga ramli, wanajimu, kuzungumza na mizimu ili kupata suluhu za mambo, frenology, mesmerism, New Age, yoga, Ayuverdic n.k. Watu wengi wa Mashariki yaani bara la Asia wameingia kwetu Afrika, nao wamekuja na tamaduni zingine nzuri za tiba za miti/mimea au maji, ila wana zingine ambazo haziendani na imani yetu. Muumini anapaswa kuchunguza na kupata habari zaidi kutoka kwa Biblia au viongozi wake, Madaktari waumini, au walei ambao wana elimu ya jambo hili.

Soma zaidi Kumbukumbu la Torati 18:9-12. Neno la MUNGU linasema mtu akifa hana kumbukumbu tena, ni kama yupo katika usingizi mzito, hivyo umizimu au kutumia nguvu za giza ili kujaribu kuungana na wale waliokufa ni kinyume kabisa na Neno la MUNGU. Makaburi yatafunguliwa ili wafu watolewe kumlaki, Yesu!

Dondoo la msaada katika kuchagua tiba rahisi: Kuna njia nyingi za kufanya sanaa ya uponyaji; lakini kuna njia moja tu ambayo Mbingu zinaithibithisha na kuikubali. Uponyaji/ tiba ya Mungu ni namna rahisi ya asili, ambayo haitakugharimu wala kudhoofisha mwili kupitia nguvu Mungu alizoziweka. Hewa safi na maji, usafi, lishe bora/sahihi, maisha safi, na imani thabiti kwa Mungu, ni tiba wengi wanaokufa wanaihitaji, na bahati mbaya tiba hizi zinaonekana kupitwa na wakati kwa sababu matumizi yake yanahitaji ustadi na kazi ambayo watu wengi hawaithamini kuifanya. Hewa safi, mazoezi, maji safi na salama,

mazingira safi ya kuishi wengi wanaweza kuvimudu, kwa gharama kidogo pengine; lakini dawa za hospitali zina gharama za aina zote, katika utengenezaji na kuzinunua, na kwa athari zinazozalishwa kwenye mfumo kwa kuzitumia. — Ushuhuda wa Kanisa 5: 443, 1885 CD 301.2

Hapa ni vyema kujua kwamba wakati wa dharura mtu aende hospitalini haraka, kama vile kuvunjika mguu, presha au sukari iliyopanda au kushuka. Ila hali itakapokuwa na afueni atafute watalaamu wa kujifunza kutibu hivi vitu kwa njia rahisi, za mtindo wa maisha, ambazo huondoa ugonjwa kabisa mara nyingi, ili apunguze mzigo wa kutumia dawa maishani mwote, japo kutibu huku kunakofuata mtindo wa maisha, kunahitaji nidhamu kubwa! Tafadhali, yote haya uyafanye kwa kushauriana na Daktari wako, mwenye leseni ya kutibu.

Madaktari na wahudumu wanapaswa kuungana katika jitihada ya kuwaongoza wanaume na wanawake kutii amri za Mungu."— The Review and Herald, Aprili 21, 1906.

"Kazi mliyokuwa mkiifanya mijini inapata kibali cha mbingu... Mlichofanya kinadhihirisha kwamba ikiwa matabibu wetu na wahudumu wetu wanaweza kushirikiana katika uwasilishaji wa Ukweli kwa wananchi, mengi zaidi yanaweza kufikiwa kuliko kushawishiwa. Na mchungaji anayefanya kazi peke yake."— Medical Ministry, p. 263.

"Mungu anawaita vijana wa kiume na wa kike ambao tayari wamepata ujuzi wa vitendo wa jinsi ya kuwatendea wagonjwa, kufanya kazi kama wamishenari wa tiba wa injili, kuhusiana na wahudumu wa injili wenye uzoefu."— Counsels to Parents and Teachers, p. 469.

"Hakuna matabibu wacha Mungu walio wengi wanaoweza kuhudumu katika taaluma yao. Kuna kazi nyingi ya kufanywa na wachungaji na madaktari, na hawa wanapaswa kufanya kazi kwa umoja kamili. ....

"Wahudumu na matabibu wanapaswa kufanya kazi kwa upatanifu na kwa bidii ili kuokoa roho."—Testimonies, gombo la 1. 6, uk. 233.

"Madaktari wetu wanapaswa kuungana na kazi ya wahudumu wa injili. . . .

"Kazi ya umishenari wa tiba haiwezi kufanywa bila huduma ya injili. Bwana amebainisha kwamba mawili hayo yatakuwa na uhusiano wa karibu kama mkono ulivyo na mwili. Bila muungano huu hakuna sehemu ya kazi itakuwa imekamilika. Mmishenai wa tiba ni mtenda kazi wa injili katika kielelezo, na katika matendo."—Ibid., uk. 240, 241.

"Kwa waganga wetu na wahudumu ninatuma ujumbe: Shikilia kazi ya Bwana kana kwamba unaamini ile Kweli ya wakati huu. Wahudumu wamishenari wa tiba na wafanyakazi katika huduma ya injili wanapaswa kufungwa pamoja kwa mahusiano yasiyoweza kuvunjika." - Ibid., juzuu ya 8, uk. 46.

“Kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kuunganishwa kwa ukaribu na kazi ya kuhubiri.”—Ibid., ukurasa wa 521, 522.

"Wamishenari wa tiba wanaofanya kazi katika safu za uinjilisti wanafanya kazi ya daraja la juu kama wafanya kazi wenzao walio katika huduma ya kichungaji. Aina hii ya kazi ya tiba au matibabu, pamoja na kazi ya huduma, haipaswi kuzuiwa kwa tabaka maskini zaidi tu...

"Daktari mwaminifu na mhudumu wanahusika katika kazi moja. Wao Wanapaswa kufanya kazi kwa upatanifu kamili. Wanapaswa kushauriana pamoja." - Ibid., p. 546.

"Ningependa kuzungumza juu ya uhusiano uliopo kati ya kazi ya umishenari wa tiba na huduma ya injili. Imewasilishwa kwangu kwamba kila idara ya kazi inapaswa kuunganishwa katika umoja mkubwa…..... ili kusimama imara katika ile siku kuu ya mwisho, ni lazima kazi yetu isiwe ile iliyogawanyika.

"Pasiwe na mgawanyiko kati ya huduma na kazi ya tiba. Tabibu anapaswa kufanya kazi kwa usawa na mchungaji, na kwa bidii na uangalifu mwingi kwa wokovu wa roho, na pia kwa urekebishaji na matengenezo ya mwili.

"Inapounganishwa na njia zingine za juhudi za injili, kazi ya umishenari ya tiba ni chombo chenye ufanisi zaidi ambacho udongo hutayarishwa kwa ajili ya kupanda mbegu za Ukweli, na chombo ambacho kwa hicho mazao huvunwa. Kazi ya umishenari wa tiba ni mkono wa kusaidia,huduma ya injili..…... Bwana ameagiza kwamba madaktari wa Kikristo na wauguzi wafanye kazi katika uhusiano na wale wanaohubiri Neno.

“Wahudumu wa injili wanapaswa kuungana na kazi ya umishenari wa tiba, ambayo imewahi kuwasilishwa kwangu kama kazi ambayo huvunja chuki iliyopo miongoni mwa watu au kushukiana. . . .

“Matabibu wanapoungana na wahudumu katika kutangaza injili katika miji mikubwa ya nchi, kazi yao iliyounganishwa itasababisha kushawishi akili nyingi kupenda Ukweli kwa wakati huu. . . .

“Watumishi waliowekwa wakfu peke yao hawatoshi katika kuifanya kazi ya Bwana. Mungu hawaiti wahudumu peke yao tu, bali pia matabibu, wauguzi,

waombezi, wafanyakazi wa Biblia, na walei wengine waliojiweka wakfu, wenye vipaji mbalimbali ila ambao wana ujuzi wa Ukweli wa sasa, wafikirie mahitaji ya miji ambayo haijaonywa.

"Hakuna mstari ambao unapaswa kuwekwa kwenye kazi ya umishenari wa kweli kati ya tiba na huduma ya injili. Hivi viwili lazima vichanganywe pamoja. Havipaswi kusimama kando kama safu tofauti za kazi. Zinapaswa kuunganishwa katika muungano usioweza kutenganishwa, kama vile ambavyo mkono na mwili haviwezi kutenganishwa……

"Hakuna hata neno moja lililosemwa sana katika kuhalalisha na kusifu kazi halisi ya umishenari wa tiba.... Ikiwa kazi ya umishenari wa tiba itatenda kama mkono wa usaidizi wa huduma ya injili, wagonjwa wangerudishwa kwenye afya, na roho nyingi zingeongozwa, kwenye nuru ....

"Injili ya Kristo inapaswa kuunganishwa na kazi ya umishenari wa tiba, na kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kuunganishwa na huduma ya injili. Ulimwengu unahitaji juhudi za wamishenari wa tiba ambao wamefungamanishwa na ujumbe wa injili. . . . [wahudumu wa injili] wanapaswa kuiona kazi hii kama mkono wa kusaidia wa injili, wakiichukulia na kuithamini kwa hali ya juu na kutayarisha mioyo kwa ajili ya kupanda mbegu ya ile Kweli, na kuwaleta wengi kwa Kristo."—Yoh. Medical Ministry, ukurasa wa 237

253.

"Bwana ameagiza kwamba wamishenari wa tiba washirikiswe pamoja na wale wanaohubiri Neno,—madaktari na wauguzi Wakristo, ambao wamepata mafunzo maalum katika uponyaji wa magonjwa na katika kuzileta roho kwa Kristo.

"Wamishenari wa tiba na watenda kazi katika huduma ya injili wanapaswa kuunganishwa pamoja na mahusiano yasiyoweza kuvunjika. Kazi yao inapaswa kufanywa kwa upya na kwa nguvu. Kwa juhudi zao za pamoja, ulimwengu unapaswa kutayarishwa kwa ajili ya ujio wa pili wa Kristo. Kupitia kazi zao za umoja. Jua la Haki litachomoza, likiwa na uponyaji katika mbawa Zake."—Counsels to Teachers, p. 468.

"Kazi ya uinjilisti yenye mafanikio inaweza kufanywa kuhusiana na kazi ya umishenari wa tiba. Ni pale ambapo safu hizi za kazi zinavyounganishwa pamoja, ndipo tunaweza kutazamia kukusanya tunda la thamani zaidi kwa ajili ya Bwana." - Medical Ministry, uk. 26, 27.

"Ikiwa wakati wowote Bwana amesema kupitia mimi, Yeye hunena ninaposema kwamba watenda kazi wanaojishughulisha na masuala ya elimu, katika safu za huduma na katika safu za umishenari wa lazima lazima wasimame kama kitengo kimoja, wote wakifanya kazi chini ya usimamizi wa Mungu, mmoja akimsaidia mwingine. kila mmoja akimbariki mwingine."—Testimonies, vol. 9, ukurasa wa 169, 170.

"Ndugu zangu, Bwana anaita umoja, kusimama pamoja. Twapaswa kuwa kitu kimoja katika imani. Nataka kuwaambia kwamba wahudumu wa injili na wahudumu wa umishenari wa tiba wanapokosa umoja, uovu mbaya zaidi unawekwa kwenye makanisa yetu, jambo ambalo lisingelikuwapo."—Medical Ministry, p. 241.

"Kristo, Mmishenari mkuu wa tiba, Ndiye kielelezo chetu. ... Yeye Aliponya wagonjwa na kuhubiri injili. Katika huduma Yake, uponyaji na mafundisho yaliunganishwa kwa ukaribu. Leo idara hizi hazipaswi kutenganishwa." - Testimonies, vol. 9, ukurasa wa 170, 171.

"Maisha ya Kristo na huduma Yake kwa wanaoteseka yameunganishwa kwa njia isiyoweza kutenganishwa. Kutoka kwa nuru ambayo nimepewa, najua kwamba uhusiano wa karibu unapaswa kuwepo kati ya kazi ya umishenari wa tiba na huduma ya injili. Hivi vimefungwa pamoja katika muungano mtakatifu kama kazi moja, na kamwe havipaswi kuachanishwa. Kanuni za mbinguni zinapaswa kuchukuliwa na kutekelezwa na wale wanaodai kutembea katika nyayo za Mwokozi. Kwa mfano Wake Yeye ambaye ametuonyesha kwamba kazi ya umishenari wa tiba haipaswi kuchukua nafasi ya mahubiri ya injili, lakini inapaswa kuunganishwa nayo."—Counsels on Health, p. 528.

"Mungu hufikia mioyo kupitia kutulizwa kwa mateso ya kimwili ... Mungu anafanya kazi leo kufikia mioyo kwa njia ile ile aliyofanya wakati Kristo alipokuwa katika dunia hii. Katika kusoma Neno la Mungu, tunaona kwamba Kristo alileta kazi ya umishenari wa tiba katika kufanya huduma Yake. Je, macho yetu hayawezi kufunguliwa ili kutambua mbinu za Kristo? Je, hatuwezi kuelewa agizo alilolitoa kwa wanafunzi Wake na kwetu sisi?"—Medical Ministry, p. 246.

"Kama kazi ya umishenari wa tiba inafanywa kama sehemu ya injili, walimwengu wataona wema unaofanywa; nao watasadikishwa hatiani na ile Kweli Yake, nao wataiunga mkono." - Testimonies, vol. 6, uk. 292.

"Mwokozi alifanya kila kazi ya kuponya watu kuwa nafasi ya kupandikiza kanuni za Kiungu/mbinguni katika akili na nafsi Yake. Hili ndilo lilikuwa kusudi la kazi

Yake. Alitoa baraka za kidunia, ili Aweze kuelekeza mioyo ya wanadamu kuipokea injili ya neema Yake." - Huduma ya Uponyaji, uk. 20.

“Kuna baraka za thamani na uzoefu mzuri wa kupata ikiwa wahudumu watachanganya uwasilishaji wa suala la afya na kazi zao zote makanisani.”—Counsels on Health, p. 431.

“Katika kazi ya Mungu, mafundisho na uponyaji haviwezi kutenganishwa kamwe.”—Testimonies, vol. 8, uk. 165.

"Huduma ya injili inahitajika ili kutoa udumishaji na uthabiti kwa kazi ya umishenari wa tiba; na huduma inahitaji kazi ya umishenari ya tiba ili kuonyesha kazi katika vitendo kwenye injili. Hakuna sehemu yoyote ya kazi iliyokamilika bila nyingine. ....

"Katika Neno Lake Mungu ameunganisha mistari hii miwili ya kazi, na hakuna mtu anayepaswa kuiacha." - Counsels on Health, uk. 514, 515.

KUMBUKUMBU ZA NYUMBANI 1955 OKTOBA "TABIBU NA WACHUNGAJI TUUNGANE"

Madaktari na wahudumu wanapaswa kuungana katika jitihada ya kuwaongoza wanaume na wanawake kutii amri za Mungu.”— The Review and Herald, Aprili 21, 1906.

“Kazi mliyokuwa mkiifanya mijini inapata kibali cha mbingu... Mlichofanya kinadhihirisha kwamba ikiwa madaktari wetu na wachungaji wetu wanaweza kushirikiana katika uwasilishaji wa Ukweli kwa wananchi, basi mengi zaidi yanaweza kutimizwa kuliko ushawishi wa mchungaji anayefanya kazi peke yake.”—Medical Ministry, p. 263.

“Mungu anawaita vijana wa kiume na wa kike ambao tayari wamepata ujuzi wa vitendo wa jinsi ya kuwasaidia kwa vitendo wagonjwa, kufanya kazi kama wamishenari wa tiba wa injili kwa kuhusiana na wahudumu wa injili wenye uzoefu.”— Counsels to Parents and Teachers, p. 469.

"Hatuna matabibu wacha Mungu wengi ambao wamebobea katika taaluma yao. Kuna kazi nyingi ya kufanywa, ambayo wachungaji na madaktari wanapaswa kufanya kazi hii, kwa umoja kamili. ....

“Wahudumu/wachungaji na matabibu wanapaswa kufanya kazi kwa upatanifu na kwa bidii ili kuokoa roho.”—Testimonies, gombo la 1. 6, uk. 233.

“Madaktari wetu wanapaswa kuungana na kazi ya wahudumu wa injili. . . .

"Kazi ya umishenari wa tiba haiwezi kuachwa mbali kutoka kwenye huduma ya injili. Bwana amebainisha kwamba hivi viwili vitakuwa na uhusiano wa karibu kama mkono ulivyo na mwili. Bila muungano huu hakuna sehemu ya kazi itakuwa imekamilika. Kazi ya mmishenari wa tiba ni ya kazi ya injili katika kielelezo yaani injili kwa vitendo."—Ibid., uk. 240, 241.

"Ninatuma agizo la huduma kwa madaktari na wahudumu wetu: Shikilia kazi ya Bwana kana kwamba unaamini Ukweli wa wakati huu. Wahudumu wamishenari wa tiba na wafanyakazi katika huduma ya injili wanapaswa kufungwa pamoja na mahusiano yasiyoweza kuvunjika." - Ibid., juzuu ya 8, uk. 46.

"Kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kuunganishwa kwa ukaribu na kazi ya kuhubiri."—Ibid., ukurasa wa 521, 522.

"Wamishenari wa tiba wanaofanya kazi katika safu za uinjilisti wanafanya kazi ya daraja la juu kama ile kazi ya wenzao kwenye idara ya huduma ya kichungaji. Aina hii ya kazi ya tiba, pamoja na kazi ya huduma, haipaswi kufanywa kwa tabaka maskini zaidi tu bali kwa matajiri na watu wa kati, yaani watu wote.....

"Daktari mwaminifu na mchungaji wanahusika katika kazi moja. Wao Wanapaswa kufanya kazi kwa upatanifu kamili. Wanapaswa kushauriana pamoja." - Ibid., p. 546.

"Ningependa kuzungumza juu ya uhusiano uliopo kati ya kazi ya umishenari wa tiba na huduma ya injili. Imewasilishwa kwangu kwamba kila idara ya kazi inapaswa kuunganishwa katika umoja mkubwa ..... ili watu waweze kusimama imara katika siku kuu ya mwisho ya hukumu, yabidi kusiwe na kazi iliyogawanyika.

"Pasiwe na mgawanyiko kati ya huduma na kazi ya tiba. Tabibu anapaswa kufanya kazi kwa usawa, pamoja na mhudumu, na kwa bidii na uangalifu mwingi kwa wokovu wa roho, na pia katika urekebishaji na matengenezo ya mwili.

"Inapounganishwa na njia zingine za juhudi za injili, kazi ya umishenari wa tiba ni chombo chenye ufanisi zaidi ambacho udongo hutayarishwa kwa ajili ya kupanda mbegu za Ukweli, na chombo ambacho kwa hicho mavuno huvunwa. Kazi ya umishenari wa tiba ni ya kusaidia, kwani ni mkono wa kulia wa huduma ya injili.... Bwana ameagiza kwamba waganga wa Kikristo na wauguzi wafanye kazi katika uhusiano na wale wanaolihubiri Neno.

“Wahudumu wa injili wanapaswa kuungana na kazi ya umishenari wa tiba, ambayo imewahi kuwasilishwa kwangu kama kazi ambayo inasaidia kuvunja chuki iliyopo miongoni mwa watu wasio waumini ….

“Matabibu wanapoungana na wahudumu katika kutangaza injili katika miji mikubwa ya nchi, kazi yao iliyounganishwa na wamishenari wa tiba, itasababisha kushawishiwa kwa akili nyingi kuupenda Ukweli wa wakati huu...

“Watumishi waliowekwa wakfu peke yao hawatakuwa sawa katika kuifanya kazi ya injili peke yao. Mungu anawaita si wachungaji au wahudumu wa injili tu, bali pia matabibu, wauguzi, watu wa maombezi, wafanyakazi wa Biblia, na walei wengine waliojiweka wakfu, wenye vipaji mbalimbali ambao wana ujuzi wa Ukweli wa sasa, wachekecheke vichwa vyao na kuona mahitaji ya miji ambayo haijaonywa.

"Hakuna mstari utakaowekwa kati ya kazi ya umishenari ya Kweli ya tiba na huduma ya injili. Hizi shuguli mbili lazima zichanganywe pamoja. Hazipaswi kusimama kando ya nyingine kama safu tofauti za kazi. Zinapaswa kuunganishwa katika muungano usioweza kutenganishwa, kama vile mkono usivyoweza kutenganishwa na mwili

"Hakuna hata neno moja lililosemwa sana katika kuhalalisha na kusifu kazi halisi ya umishenari wa tiba..…… Kwa kuwa kazi ya umishenari wa tiba ikitenda kama mkono wa msaada, katika kusaidia huduma ya injili, wagonjwa watarudishwa kwenye afya, na roho nyingi zingeongozwa kwenye nuru ya Mwenyezi Mungu ....

"Injili ya Kristo inapaswa kuunganishwa na kazi ya umishenari wa tiba, na kazi ya umishenari ya matibabu inapaswa kuunganishwa na huduma ya injili. Ulimwengu unahitaji juhudi za wamishenari wa tiba ambao wamefungamanishwa na ujumbe wa injili. . . . [wahudumu wa injili] wanapaswa kuiona kazi ya umishenari wa tiba kama mkono wa kusaidia injili, mkono wa kufungua mlango, wakiichukulia kwa kuithamini kwa ukubwa kama ndiyo fursa ya kutayarisha mioyo kwa ajili ya kupanda mbegu ya Kweli, na kuwaleta wengi kwa Kristo.”— Yoh. Medical Ministry, ukurasa wa 237

“Bwana ameagiza kwamba pamoja na wale wanaohubiri Neno, washirikishwe wahudumu Wake wa kimishenari wa tiba,—madaktari na wauguzi Wakristo, ambao wamepata mafunzo maalum katika uponyaji wa magonjwa na katika kuleta roho kwa Bwana.

"Wamishenari wa tiba na watenda kazi katika huduma ya injili wanapaswa kuunganishwa pamoja na mahusiano yasiyoweza kuvunjika. Kazi yao inapaswa

kufanywa kwa upya na kwa nguvu. Kwa juhudi zao za pamoja ulimwengu unapaswa kutayarishwa kwa ajili ya ujio wa pili wa Kristo. Kupitia kazi zao za mshikamano wenye umoja. Jua la Haki litachomoza, likiwa na uponyaji katika mbawa Zake."—Counsels to Teachers, p. 468.

"Kazi ya uinjilisti yenye mafanikio inaweza kufanywa kwa kuhusianishwa na kazi ya umishenari wa tiba. Niwa pale tu, safu hizi za kazi zinavyounganishwa ndipo twaweza kutazamia kukusanya matunda ya thamani zaidi kwa ajili ya Bwana-yaani roho za watu waliojitoa kwa Mwenyezi Mungu." - Medical Ministry, uk. 26, 27.

"Ikiwa wakati wowote Bwana amesema kupitia mimi, Yeye hunena ninaposema kwamba watenda kazi wanaojishughulisha na masuala ya elimu, katika safu za huduma na katika safu za umishenari wa tiba lazima wasimame kama kitengo, wote wakifanya kazi chini ya usimamizi wa Mungu, mmoja akimsaidia mwingine. kila mmoja akibariki kila mmoja."—Testimonies, vol. 9, ukurasa wa 169, 170.

"Ndugu zangu, Bwana anaita umoja, mfanye kazi kwa pamoja. Twapaswa kuwa kitu kimoja katika imani. Nataka kuwaambia kwamba wahudumu wa injili na wahudumu wamishenari wa tiba wanapokosa umoja, kunawekwa kwenye makanisa yetu uovu mbaya zaidi hapo."—Medical Ministry, p. 241.

"Kristo, Mmishenari mkuu wa tiba, Ndiye kielelezo chetu…….. Yeye Aliponya wagonjwa na kuhubiri injili. Katika huduma Yake, uponyaji na mafundisho yaliunganishwa kwa karibu. Leo hawapaswi kutenganishwa." - Testimonies, vol. 9, ukurasa wa 170, 171.

"Maisha ya Kristo na huduma Yake kwa wanaoteseka yameunganishwa kwa njia isiyoweza kutenganishwa. Kutoka kwa nuru ambayo nimepewa, najua kwamba uhusiano wa karibu unapaswa kuwepo kati ya kazi ya umishenari wa tiba na huduma ya injili. Hivi vimefungwa pamoja katika muungano mtakatifu. kama kazi moja, na kamwe havipaswi kuachana. Kanuni za mbinguni zinapaswa kuchukuliwa na kutekelezwa na wale wanaodai kutembea katika nyayo za Mwokozi. Kwa mfano Wake ametuonyesha kwamba kazi ya umishenari wa tiba haipaswi kuchukua nafasi ya mahubiri ya injili, lakini inapaswa kuunganishwa nayo."—Counsels on Health, p. 528.

"Mungu hufikia mioyo kupitia kitulizo cha mateso ya kimwili ... Mungu anafanya kazi leo kufikia mioyo kwa njia ile ile aliyofanya wakati Kristo alipokuwa juu ya dunia hii. Katika kusoma Neno la Mungu, tunaona kwamba Kristo alileta kazi ya umishenari wa tiba katika kufanya kazi ya huduma Yake. Je, macho yetu

hayawezi kufunguliwa ili kutambua mbinu za Kristo? Je, hatuwezi kuelewa agizo alilotoa kwa wanafunzi Wake na kwetu sisi?”—Medical Ministry, p. 246.

"Ikiwa kazi ya umishenari wa tiba inafanywa kama sehemu ya injili, walimwengu wataona wema unaofanywa; nao dhamira zao zitasadikishwa na ile Kweli ya Mungu na kisha wataiunga mkono." - Testimonies, vol. 6, uk. 292.

"Mwokozi alifanya kila kazi ya kuponya kuwa nafasi ya kupandikiza kanuni Zake katika akili na nafsi za watu. Hili ndilo lilikuwa kusudi la kazi Yake. Yeye Alitoa baraka za kidunia, ili Aweze kuielekeza mioyo ya wanadamu kupokea injili ya neema Yake." - Huduma ya Uponyaji, uk. 20.

“Kuna baraka za thamani na uzoefu mzuri utakaopatikana kama wahudumu watachanganya uwasilishaji wa ujumbe wa afya na kazi zao zote makanisani.”—Counsels on Health, p. 431.

“Katika kazi ya Mungu, mafundisho na uponyaji haviwezi kutenganishwa kamwe.”—Testimonies, vol. 8, uk. 165.

"Huduma ya injili inahitajika ili kutoa uendelevu na uthabiti kwa kazi ya umishenari ya tiba; na huduma inahitaji kazi ya umishenari wa tiba ili kuonyesha utendaji au vitendo vya injili. Hakuna sehemu yoyote ya kazi iliyokamilika bila nyingine. ....

"Katika Neno Lake Mungu ameunganisha mistari hii miwili ya kazi, na hakuna mtu anayepaswa kuviachanisha." - Counsels on Health, uk. 514, 515.

451. Kuna njia nyingi za kushughulika na stadi ya uponyaji/tiba; lakini kuna njia moja tu ambayo Mbingu huidhinisha. Dawa za Mungu ni wakala rahisi wa asili, ambao hautatoza ushuru mwili au kudhoofisha mfumo kupitia silika yake yenye nguvu. Hewa safi na maji, usafi, mlo ufaao, usafi wa maisha, na imani thabiti katika Mungu, ni tiba inayohitajika kwa maelfu ambao wanakufa; na bado tiba hizi hazitumiwi na hivyo kusahauliwa kwa sababu utumiaji wake unahitaji weledi/stadi na kazi nyingi ambayo watu hawathamini kuifanya. Hewa safi, mazoezi, maji safi, na mapumziko, lishe bora, kiasi, hewa bora, yanaweza kufikiwa na wote, kwa gharama ndogo tu; lakini madawa ya kulevya ni ghali, katika matumizi ya fedha, na matokeo yanayoletwa kwenye mfumo wa mwili wa mwanadamu.— Testimonies for the Church 5:443, 1885

452. Hewa safi, mwanga wa jua, kiasi, pumziko, mazoezi, mlo ufaao, matumizi ya maji, kumtumaini Mungu —haya ndiyo tiba ya kweli. Kila mtu anapaswa kuwa na ujuzi na jinsi ya kutumiamawakala wa asili wanaouhisika na kurekebisha. Ni

muhimu pia kuelewa kanuni zinazohusika katika tiba ya wagonjwa na kuwa na mazoezi ya kivitendo ambayo yatamwezesha mtu kutumia ujuzi huo kwa njia ifaayo.

Matumizi ya tiba asili yanahitaji kiasi cha huduma na jitihada ambazo wengi hawako tayari kutoa. Mchakato wa asili wa uponyaji na kujenga ni wa polepole, na kwa wale wasio na subira inaonekana ni polepole sana. Kujisalimisha kwa msamaha wa dhambi kunahitaji dhabihu. Lakini mwishowe itapatikana kwamba asili, bila ya kupunguzwa, hufanya kazi yake kwa busara na vizuri. Wale wanaodumu katika kutii sheria zake watapata thawabu katika afya ya mwili na akili.— The Ministry of Healing, 127, 1905

453. Madaktari mara nyingi hushauri wagonjwa kutembelea nchi za kigeni na meli (cruise), kwenda kwenye chemchemi ya madini, au kuvuka bahari, ili kupata afya tena; wakati, katika visa tisa kati ya kumi, ikiwa wangekula kwa kiasi, na kufanya mazoezi yenye afya wakiwa na roho ya uchangamfu, wangepata afya tena na kuokoa wakati na pesa. Mazoezi, na matumizi mengi kwa ukarimu ya hewa nje ya majumba yetu na mwanga wa jua—baraka ambazo mbingu imewapa wote—katika hali nyingi zingewapa uzima na nguvu wale waliodhoofika.—Christian Temperance and Bible Hygiene, 160, 1890

BAADHI YA MAMBO TUNAYOWEZA KUJIFANYIA WENYEWE

454. Kuhusiana na yale tunayoweza kujifanyia sisi wenyewe, kuna jambo ambalo linahitaji mazingatio makini na akili zenye akili.

Ni lazima nijitambue, lazima niwe mtu wa kujifunza siku zote jinsi ya kutunza jengo hili, yaani mwili ambao Mungu amenipa, ili niuhifadhi katika hali bora kabisa ya afya. Ni lazima nile vile vitu ambavyo vitanisaidia vyema kimwili, na lazima nichukue uangalifu wa pekee kuwa na mavazi yangu kwa ubora, na kwa jinsi ambavyo yatachangia mzunguko wa damu wenye afya. Sipaswi kujinyima mazoezi na hewa. Lazima nipate mwanga wote wa jua ambao inawezekana kwangu kuupata. Lazima niwe na hekima ya kuwa mlinzi mwaminifu wa mwili wangu.

Kuingia katika chumba chenye baridi nikiwa katika jasho ni jambo lisilo na hekima; Ninapaswa kuonyesha kwamba ninasimia kwa busara hili, ili kujiruhusu kukaa kwenye mkutano, na hivyo kutojiweka wazi kupata magonjwa ya baridi/cold kama vile kikohozi, mafua, na mafundofundo kooni. Sio busara kukaa mkao wa kuacha miguu baridi na viungo vilivyo mbali na moyo kama mikono, miguu na kichwa, na hivyo kufanya kurudishwa damu kutoka kwenye ncha za

mwili yaani miguu na mikono hadi kwenye ubongo au viungo vya ndani kuwa vigumu. Ninapaswa kuilinda miguu yangu kila wakati wakati wa hali ya hewa yenye unyevunyevu. Ninapaswa kula kwa kawaida, kwa kiasi, chakula chenye afya zaidi ambacho kitafanya damu iwe bora zaidi, na sipaswi kufanya kazi kwa kupitiliza kiasi ikiwa iko katika uwezo wangu kuepuka kufanya hivyo. Na ninapokiuka sheria ambazo Mungu aliweka katika nafsi yangu, ninapaswa kutubu na kurekebisha hali hiyo, na kujiweka katika hali nzuri zaidi chini ya madaktari sahili ambao Mungu ametupa kwa uponyaji, matabibu hao ni —hewa safi, lishe bora, maji safi, mazoezi, kumtumaini Mungu, kupumzika, kuwa na kiasi au kutawala na nafsi, uponyaji, mwanga wa jua wenye thamani.

NUKUU ZA RYU AFYA

Mchanganyiko wa nukuu za afya: IMETOLEWA NA DKT CALVIN DENCE NA GRACE MOMADI-MASAKA 1992, Andrews University Lectures.

1. Ikiwa tunashinda hamu ya kula tunaweza kushinda juu ya yote. CD145

2. Soma waandishi bora juu ya sheria za maisha, uzima na afya. Kisha utii kwa kutumia busara yako. GW 242

3. Edeni ilipotea kwa hamu ya kula, na itarejeshwa kwa kushinda hamu ya kula. 161

4. Wale wanaotenda dhambi dhidi ya maarifa ya afya, na kutegemea dawa watapoteza maisha. MM 224

5. Dawa za famasia (drugs) zimefanya madhara zaidi na kuua zaidi kuliko zilivyosaidia. MM 27

6. Dawa za famasia nyingi zinapaswa kutupwa. MS 162

7. Ushawishi wa Roho Mtakatifu ni dawa bora kabisa kwa wagonjwa. MM 12

8. Vitu vya asili ni bora kwa afya kuliko dawa zote ulimwenguni. CH 169

9. Dawa ni dutu ya kigeni na yenye asili ya sumu. 134

10. Ugonjwa ni adhabu ya kukiuka sheria za asili. CH 347

11. Zuia magonjwa kwa usafi na kutii sheria za afya. 4 SG 140

12. Magonjwa ni juhudi ya mwili na maumbile kuondoa uchafu wa mwili. CH 61

13. Kufanya vizuri ni dawa bora ya magonjwa. HH 447

14. Ugonjwa hauji kamwe bila sababu.2SM 469.

15. Kusoma Biblia na kufanya kazi ni tiba bora kwa miili na akili za wagonjwa. 2T 325

16. Kufunga siku moja au mbili ni bora kuliko dawa za Famasia. CH 477

17. Kuacha kula kwa muda mfupi, au kuacha kabisa pombe na sigara ndiyo njia ya kuelekea kwenye afya. CDF 310

18. Pika kidogo na kula matunda mengi katika hali ya asili. 7T 134

19. Imani katika Kristo na utii ni sayansi ya kweli ya uponyaji. CH 346

20. Tutakapochukua mpango wa asili wa bustani ya Edeni mapema, afya yetu itarejeshwa mapema. CH 174

21. Kwa kutii sheria za maisha TUNAHAKIKISHA AFYA YETU kuwa bora. CH 49

22. Maisha ya nje ya myumba, hurejesha afya. MM 231

23. Imani ya mtu mgonjwa imekufa isipokuwa ikiwa yuko tayari kubadilisha tabia zake. MM 262

24, Ikiwa una afya mbaya, wasaidie wengine na utajikuta unaanza kupona. 442

25. Panda juu katika Matengenezo ya Afya tunapokaribia mwisho. CH 467

26. Chochote kinachopunguza nguvu ya mwili, hufanya akili iwe dhaifu. KOL 346

27. Bila Matengenezo ya Afya matumaini yote ya mbinguni ni bure. CH 574-9

28. Tutakutana mbinguni na wale ambao tumewafanyia kazi katika Matengenezo ya afya. KOL 373

29. Hakuna usalama katika bidhaa za wanyama au samaki-kuzitumia kama chakula hakuna usalama. CD1 411

30. Hakuna chakula hata iwe punje ya karanga, kinachopaswa kupita kati ya midomo yako kati ya mlo mmoja mpaka mwingine CH 408

31. Kula chakula kwa kupindukia na ulafi, husababisha ganzi ubongoni na kuleta njaa ya uwongo (false hunger). 2T 212-3

32. Sukari huziba mifumo na inazuia mitambo ya mashine ya mwili. CH 149

33. Ikiwa wagonjwa wangeelimishwa kutumia mimea (herbs(, wasingekufa kama vile watumiapo dawa za kulevya na dawa za famasia zenye sumu-drugs and narcotic. HL 308

34. Kuelewa utumiaji sahihi wa mimea na mizizi inamaanisha hakuna haja ya daktari. HL 306

35. Matumizi ya mimea huafikiana na zoezi la imani.HL 305

36. Njia ya kweli ya kuponya wagonjwa ni kutumia mimea (herbs mboga za makondeni). HL 310

38. Chakula cha nyama na samaki, huunda magonjwa. KK 1: 1112

38. Wale walioongoka nusu-nusu kwenye ulaji wa nyama wataliacha kanisa. Ch 575

39. Dhima ya magonjwa ni mara 10 zaidi kwa wale wanaokula nyama, HL 62

40, kula nyama ni sababu ya moja kwa moja ya magonjwa. 2 SM 418-9

41. Wafanyakazi wa kimishenari wa tiba wanatoa wito wa mwisho. UT 71

42. Ufahamu wa kutenda haki ni dawa bora kwa mgonjwa. 502

43. Vitu vya asili/uumbaji ni matabibu wa MUNGU; walio bora kwa afya kuliko dawa za mfamasia (drugs). CH 169-170

44. Kutii sheria za asili ni njia ya moja kwa moja kwenda mbinguni CH

45. Kuna silika ya uponyaji katika zeri za mpaini, mierezi na miti ya miberoshi. 7T 77

46. Waganga wanashughulikia dawa na mgonjwa anauawa. SM 441

47. Daktari mwenye busara ataweza kugundua ugonjwa kwa kuchunguza mzizi ugonjwa au sababu yake. HL269

48. Mishipa ya fahamu bora, inaweza kupatikana tu kwa njia ya kujikana nafsi, na kuwa na kiasi. KK 3: 1165

49. Tiba ya maji huleta matokeo mazuri ya asili (hydrotherapia). KK 7:938

50. Lazima tuwe na afya kamilifu au hatuwezi kumpendeza MUNGU. KK 1:1102

51. Huzuni hupunguza nguvu muhimu katika mishipa ya fahamu. KK 3: 1146

52. Mazoezi ya asubuhi katika hewa safi ni kinga dhidi ya magonjwa yote. MLT

53. Masaa yasiyo ya kawaida ya kula na kunywa hupunguza nguvu za ubongo. YT 5/3/9

54. Wengi hufa kutokana na magonjwa ambayo ni ya kufikirika kabisa. HH 171

55. MUNGU aliiondoa nyama na akawapa mwanadamu mana ili kuamsha nguvu za akili. KK 1:1113

56. Kuhusu matengenezo ya afya, watu wenye utindio wa ubongo hawawajibiki. MM 289

57. Wokovu hauwezekani bila Matengenezo ya Afya. 7T 137

58. Madaktari wa Kikristo hawawezi kutoza bei kubwa kama vile waganga wa kidunia. MM 125

59. Dawa za BWANA Mwenyewe ni hewa safi, maji na jua. 228

60. Amani ya ndani, na upendo kwa MUNGU vitaimarisha akili. 2T 327

K

MWONGOZO WA UMISHENARI WA KITABIBU KUTOKA KATIKA ROHO YA UNABII

- *Kwa nini kazi tulipewa Kazi ya Umishenari wa Tiba.*
- *Kwa nini kazi ya Umishenari wa tiba ni muhimu.*
- *Ni nani anapaswa kuifanya kazi ya Umishenari wa Tiba.*
- *Je kazi ya Umishenari wa Tiba inapaswa ifanywaje*
- *Je, kazi ya Umishenari wa Tiba inapaswa ifanywe wapi*
- *Je, kazi ya Umishenari wa Tiba inapaswa kufanywa wakati gani*
- *Wakati wa taabu na dhiki*
- *Kazi binafsi na kazi kwa vikundi*
- *Kanuni za kufanya kazi*
- *Jinsi, ambavyo Yesu alivyofanya kazi ya Umishenari wa Tiba.*
- *Hatua kumi za Uponyaji.*
- *Utumiaji wa Tiba Sahili/Rahisi*
- *Utumiaji wa Maji*
- *Dawa za Magharibi au Dawa za vidonge za Hospitalini.*
- *Yote yaliyoandikwa katika Biblia kuhusu Umishenari wa Tiba*